

**KUCHUNGUZA MAENDELEO YA UBUNIFU KATIKA TAMTHILIA YA  
KISWAHILI: UTAFTI LINGANISHI WA TAMTHILIA ZA AWAMU YA  
AZIMIO LA ARUSHA NA SOKO HURIA**

**FURAHA JUMAPILI MASATU**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KAMA SHARTI PEKEE LA  
KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMIVU KATIKA KISWAHILI IDARA  
YA TAALUMA ZA ISIMU NA FASIHI CHUO KIKUU HURIA CHA  
TANZANIA**

**2023**

## UTHIBITISHO

Waliotia saina hapa chini wanathibitisha kwamba wameisoma tasnifu hii inayojipambanua kwa mada, **Kuchunguza Maendeleo ya Ubunifu katika Tamthilia ya Kiswahili: Utafiti Linganishi wa Tamthilia za Awamu ya Azimio la Arusha na Soko Huria** na kupendekeza kwamba inafaa kukubaliwa na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kama sharti pekee la kutunukiwa Shahada ya Uzamivu katika Kiswahili (PhD. Kisw.).

.....

Prof. Emmanuel Mbogo

(Msimamizi)

.....

Tarehe

.....

Dkt. Hadija Jilala

(Msimamizi)

.....

Tarehe

## **HAKIMILIKI**

Hairuhusiwi kuzalisha, kuhifadhi katika mfumo wowote wa kunakili, au kusambaza sehemu yoyote ya tasnifu hii kwa namna yoyote ile bila kibali cha maandishi kutoka kwa mwandishi wa tasnifu hii au Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa niaba ya mwandishi.

**TAMKO**

Mimi, **Furaha Jumapili Masatu** ninatamka kwamba, tasnifu hii ni halisi. Haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu wala taasisi yoyote. Vyanzo vyote vya taarifa vilivyorejelewa, vimetambuliwa kwa usahihi. Ni katika msingi huu, ninatamka kwamba kazi hii ni yangu dhahiri. Na kwamba, inawasilishwa kama sharti pekee la kutunukiwa Shahada ya Uzamivu katika Kiswahili (PhD. Kisw.).

.....  
Saini

.....  
Tarehe

## **TABARUKU**

Ninaitabaruku kazi hii kwa wazazi wangu marehemu baba yangu Jumapili P. Masatu na mama yangu Annah J. Kidata. Pia, kwa mlezi na mjomba wangu Alphayo J. Kidata.

## **SHUKRANI**

Kuhitimu masomo ya shahada ya uzamivu siyo muujiza bali ni sayansi ya neema na rehema kutoka kwa Mungu. Siyo kwa uwezo wangu, akili yangu na nguvu zangu hata nimeweza kukamilisha tasnifu hii. Yote yamewezekana kwa mkono wake ulio hodari, Jehovah Elohim - El-Gibhor, Jehovah Jireh, Jehovah-Shammah, Jehovah-M'kaddesh, Jehovah-Tsidkenu, Jehovah-Rafa, Jehovah - El Roi, Jehovah-Nissi, Yahwe, BWANA wa mabwana, MFALME wa wafalme. Sifa na utukufu nakurudishia Ewe Mungu katika utatu wako mtakatifu ndani ya kao lako la amani na ushindi wa umilele. Asante sana Ee Baba kwa kunipigania upeo – kiroho na kimwili. Amin.

Shukrani za kipekee ni kwa wasimamizi wangu, Prof. Emmanuel Mbogo na Dkt. Hadija Jilala. Umakini na ushauri wenu wa kiufundi umeifanya tasnifu hii kustahiki kuwa miongoni mwa nyaraka rasmi zenye kuleta athari chanya kwangu binafsi, familia, jamii na jumuiya ya wanataaluma za Fasihi ya Kiswahili aghalabu Tamthilia ya Kiswahili – ndani na nje ya Tanzania. Mungu awalipe mema daima.

Vilevile, ninawashukuru Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa kutengeneza mazingira rafiki kwa sisi wanafunzi wa nje ya Dar es salam kutimiza ndoto zetu za kitaaluma pasipo kupoteza ajira wala fedha nyingi. Asante sana Prof. Elifas T. Bisanda, Makamu Mkuu wa Chuo; Prof. Magreth S. Bushesha, Mkurugenzi Taaluma za Shahada za Juu; Dkt. Dunlop O. Ochieng, Mtiva Kitivo cha Sanaa na Sayansi za Jamii; Dkt. Zelda Elisifa, Mudir Idara ya Taaluma za Isimu na Fasihi; na Dkt. Omary Maguo, Mratibu Taaluma za Shahada za Juu za Kiswahili. Ninawashukuru kwa

uongozi na uratibu mzuri. Mungu azidi kuwapa kibali cha huduma njema kwa wanafunzi wanaochagua kutimiza ndoto zao za kitaaluma chini ya taasisi hii adhimu.

Siwezi kusahau kumshukuru mwajiri wangu Chuo Kikuu cha Kikatoliki Mwenge. Chini ya uongozi mahiri wa Fr. Prof. Philbert Vumilia na wasaidizi wake, masomo yangu hayakuwa gunia la misumari. Ninawashukuru kwa kuridhia ombi langu la kujisomesha ngazi ya uzamivu. Mliruhusu nitumie muda na raslimali nyingine za taasisi pasipo kinyongo. Asanteni sana tena sana. Mungu azidi kuwabariki Chuo Kikuu cha Kikatoliki Mwenge na uongozi wake wote.

Nitakuwa mchoyo wa fadhila kama nisipowashukuru wanakitengo wenzangu; ndugu Rick Ngowi, ndugu Deogratius F. Mkawe, ndugu Sultani Musa, Br. Eric Ndumbaro na Sr. Rehema N. Mbwambo. Daima hamkunichoka bali mlikuwa nami kwa maombi, vitendea kazi, motisha na ushauri. Ndugu Deogratius F. Mkawe na Br. Eric Ndumbaro ninawashukuru mno kwa namna mlivyojitolea kubeba vipindi vyangu kwa moyo mweupe. Aidha, ninakushukuru ndugu Deogratius F. Mkawe kwa kuungana nami katika safari ya elimu kwa njia ya masafa. Hatua hii ilijenga uelewa mpana zaidi juu ya hali na mapito yanayomkuta mwanafunzi wa mfumo huu wa elimu. Sote tubarikiwe.

Aidha, ninawashukuru ndugu zangu wote. Kila mmoja kwa nafasi yake alinishika mkono kiroho na kimwili. Kipekee, ninawashukuru sana tena sana mama yangu mzazi, Annah J. Kidata, mjomba wangu Alphayo J. Kidata, kaka yangu Tumaini, dada zangu Sarah, Asante na Neema. Kupitia ninyi na familia zenu, maisha yangu ya kitaaluma, kikazi na kiuchumi yalisawazika kwa kiasi cha kunifanya nione haya

kusitisha masomo. Asanteni sana. Mungu azidi kuturehemu na kutulipa mema sisi sote.

Kwako mke wangu, Naomi J. Migire na watoto wetu Elyon na Elyana, sina cha kuwalipeni. Mmekuwa nami katika mapito yote. Asanteni kwa uvumilivu, dua, faraja na hamasa. Michango yenu ya hali na mali hailipiki. Nanyi dada Naomi Joshua, dada Agness J. Migire, Sr. Annah Etlawe Safari na Shangazi Hannah Migire ninawashukuru kwa maombi, ushauri na hamasa. Mungu atutetee na kutubariki upeo.

Kamwe siwezi kuwasahau wapendwa wote waliokoka moto mwema chotoni mwa masomo yangu ya uzamivu. Kila mmoja kwa nafasi na wakati wake alifanyika baraka na msaada kwangu. Orodha ni ndefu lakini niwatambue wachache kati yao. Hawa ni Kurasini SDA Choir kupitia nyimbo zao, Dkt. Christopher A. Senyamanza, Dkt. Walesi Mlaga, ndugu Ndimyake Mwakanjuki, ndugu Neema Onesmo na ndugu Wakuru Thomu. Zaidi yao wapo Sr. Rehema Bayo, Sr. Anitha E. Mgimba, Sr. Venancia F. Hyera, Sr. Osmunda R. Ndunguru na Sr. Mary F. Mwiru. Wengine ni ndugu Adam Janga, ndugu Alvin B. Lema, ndugu Rahel M. Mdimilaje na ndugu Alpha Ng'ondya.

Pamoja nao ni ndugu Frida Mgalla, ndugu Deus M. Nyamasheki, ndugu Minael Doriye, ndugu Elen H. Kidenya, ndugu Magdalena Swai, ndugu Alfred Malugu, ndugu Editha Malewo, ndugu Joyce F. Lulu, ndugu Monica L. Luciani, ndugu Mercy S. Masawe na ndugu Paul Kalanga. Pia, wanafunzi wangu wote na wafanyakazi wenzangu wote wa Chuo Kikuu cha Kikatoliki Mwenge. Faukwa ya hao, ninatambua na kuheshimu mno msaada mkubwa niliopata kwa yeyote ambaye hayumo katika kurasa hizi za shukrani. Mungu awe kila kitu kwetu sote, daima na milele.



## IKISIRI

Utafiti huu ulijikita katika kuchunguza maendeleo ya ubunifu katika Tamthilia ya Kiswahili kwa kulinganisha tamthilia za awamu ya Azimio la Arusha na soko huria nchini Tanzania. Lengo lilikuwa ni kulinganisha kazi za awamu mbili tofauti ili kubaini kufanana na kutofautiana katika ubunifu wa ujenzi wa dhamira na matumizi ya lugha ili kubaini kama kuna maendeleo endelevu ama la. Utafiti ulimakinikia dhamira, matumizi ya ucheshi, matumizi ya misimu, matumizi ya uchanganyaji ndimi na uwepesi na ugumu wa lugha. Kiunzi cha utafiti kilikuwa ni nadharia ya Fasihi Linganishi. Utafiti ulikuwa ni wa maktabani. Tamthilia sita za Kiswahili (*Mashetani, Kijiji Chetu, Harakati za Ukombozi, Safari ya Chinga, Changamoto na Nje – Ndani*) ziliteuliwa kwa kutumia mbinu ya usampulishaji nasibu tabakishi. Data zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji makini. Uchambuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti uliongozwa na mkabala wa kiufafanuzi. Matokeo ya utafiti yanadhihirisha kuwa, waandishi wa tamthilia teule wanafanana na kutofautiana katika uteuzi na ujenzi wa dhamira na lugha ya tamthilia zao. Ubunifu katika kila tamthilia teule umethibitika kwenda na wakati, hali, lengo la utunzi na mazingira ya utunzi. Kila mwandishi ameonesha upya wa kipekee katika kazi yake. Hivyo, utafiti huu umebaini kuwa siyo kweli kwamba tamthilia za Kiswahili za nchini Tanzania ambazo watunzi wake ni zao la awamu ya soko huria hazina ubunifu endelevu. Kwa hiyo basi, tafiti zaidi zinahitajika kuhusu tamthilia za Kiswahili ambazo watunzi wake ni zao la awamu ya soko huria ili kuondoa ombwe la taarifa za msingi katika kutathmini historia na maendeleo ya Tamthilia ya Kiswahili nchini Tanzania. Maneno muhimu ni dhamira, maendeleo, misimu, ubunifu, uchanganyaji ndimi, ucheshi, uwepesi na ugumu wa lugha.

## YALIYOMO

Uthibitisho.....	i
Hakimiliki .....	ii
Tamko .....	iii
Tabaruku .....	iv
Shukrani .....	v
Ikisiri .....	viii
Yaliyomo.....	ix
Orodha ya Majedwali.....	xiv
Ufunguo wa Vifupisho.....	xv
<b>SURA YA KWANZA .....</b>	<b>1</b>
<b>UTANGULIZI.....</b>	<b>1</b>
1.1 Utangulizi wa Sura .....	1
1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti .....	1
1.3 Tamko la Tatizo la Utafiti .....	12
1.4 Malengo ya Utafiti.....	13
1.4.1 Lengo Kuu.....	13
1.4.2 Malengo Mahususi .....	13
1.5 Maswali ya Utafiti .....	14
1.6 Umuhimu wa Utafiti.....	14
1.7 Mipaka ya Utafiti.....	16
<b>SURA YA PILI.....</b>	<b>20</b>
<b>MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA .....</b>	<b>20</b>
2.1 Utangulizi .....	20

2.2	Ufafanuzi wa Dhana Mbalimbali .....	20
2.2.1	Dhana ya Tamthilia .....	20
2.2.2	Maudhui na Dhamira .....	27
2.2.3	Matumizi ya Lugha.....	31
2.2.3.1	Lugha ya Ucheshi .....	34
2.2.3.2	Misimu.....	38
2.2.3.3	Uchanganyaji Ndimi.....	41
2.2.3.4	Uwepesi na Ugumu wa Lugha katika Kazi Bunilizi .....	44
2.2.4	Ubunifu.....	47
2.3	Maendeleo ya Tamthilia ya Kiswahili Nchini Tanzania .....	55
2.3.1	Maendeleo ya Tamthilia ya Kiswahili katika Awamu ya Azimio la Arusha.....	56
2.3.2	Maendeleo ya Tamthilia ya Kiswahili katika Awamu ya Soko Huria .....	67
2.4	Tafiti Tangulizi kuhusu Tamthilia Teule.....	78
2.4.1	Tafiti kuhusu Tamthilia Teule za Awamu ya Azimio la Arusha.....	79
2.4.2	Tafiti kuhusu Tamthilia Teule za Awamu ya Soko Huria.....	84
2.5	Pengo la Maarifa.....	85
2.6	Kiunzi cha Nadharia .....	86
2.7	Hitimisho .....	93
	<b>SURA YA TATU.....</b>	<b>94</b>
	<b>MBINU ZA UTAFITI.....</b>	<b>94</b>
3.1	Utangulizi.....	94
3.2	Usanifu wa Utafiti.....	94
3.3	Wango wa Utafiti .....	95

3.4	Sampuli na Usampulishaji .....	96
3.5	Mbinu za Kukusanyia Data.....	98
3.6	Mbinu za Uwasilishaji na Uchambuzi wa Data .....	100
3.7	Uzingativu wa Masuala ya Kiitikeli (Kimaadili).....	102
3.8	Hitimisho.....	103
	<b>SURA YA NNE .....</b>	<b>104</b>
	<b>UBUNIFU KATIKA DHAMIRA ZA TAMTHILIA TEULE .....</b>	<b>104</b>
4.1	Utangulizi .....	104
4.2	Muhtasari wa Tamthilia Teule.....	105
4.3	Kulinganisha Ubunifu katika Dhamira za Tamthilia Teule .....	110
4.3.1	Kufanana kwa Ubunifu wa Dhamira katika Tamthilia Teule .....	111
4.3.2	Kutofautiana kwa Ubunifu katika Ujenzi wa Dhamira katika Tamthilia Teule .....	188
4.4	Hitimisho .....	219
	<b>SURA YA TANO .....</b>	<b>220</b>
	<b>UBUNIFU KATIKA MATUMIZI YA LUGHA YA TAMTHILIA TEULE... 220</b>	
5.1	Utangulizi.....	220
5.2	Kufanana na Kutofautiana katika Ubunifu wa Matumizi ya Lugha katika Tamthilia Teule .....	221
5.2.1	Matumizi ya Ucheshi .....	221
5.2.2	Matumizi ya Misimu .....	282
5.2.3	Matumizi ya Uchanganyaji Ndimi.....	305
5.2.4	Uwepesi na Ugumu wa Lugha .....	327
5.3	Hitimisho.....	352

<b>SURA YA SITA.....</b>	<b>354</b>
<b>ATHARI YA UBUNIFU WA DHAMIRA NA MATUMIZI YA LUGHA KATIKA KUCHOCHEA MAENDELEO ENDELEVU YA TAMTHILIA YA KISWAHILI .....</b>	<b>354</b>
6.1 Utangulizi .....	354
6.2 Athari ya Ubunifu Endelevu katika Tamthilia ya Kiswahili .....	354
6.2.1 Athari ya Ubunifu wa Dhamira katika Tamthilia ya Kiswahili .....	355
6.2.2 Athari ya Ubunifu wa Matumizi ya Lugha katika Tamthilia ya Kiswahili ...	376
6.3 Hitimisho .....	387
<b>SURA YA SABA .....</b>	<b>388</b>
<b>MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO .....</b>	<b>388</b>
7.1 Utangulizi .....	388
7.2 Muhtasari .....	388
7.2.1 Muhtasari wa Jumla.....	388
7.2.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti.....	392
7.3 Ufaafu wa Utafiti Huu .....	393
7.4 Mahitimisho.....	393
7.5 Mapendekezo.....	394
7.5.1 Mapendekezo kwa Watunzi .....	395
7.5.2 Mapendekezo kwa Wahakiki na Watafiti.....	395
7.5.3 Mapendekezo kwa Walimu na Wanafunzi .....	396
<b>MAREJELEO .....</b>	<b>397</b>
<b>VIAMBATISHO .....</b>	<b>417</b>

Kiambatisho A: Jedwali 5.16 Uchanganyaji Ndimi katika Tamthilia ya Mashetani .....	417
Kiambatisho B: Jedwali 6.1 Mdafao wa Dhamira Zilizotawala Tamthilia Teule ...	420
Kiambatisho C: Maswali ya Kuongoza Uchunguzi wa Matini Teule kwa Ajili ya Data za Msingi.....	423
Kiambatisho D: Orodha ya Tamthilia ya Kiswahili Zilizotumika katika Hatua za Usampulishaji .....	427

## ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 5.1	Mdafao wa Utokeaji wa Lugha ya Ucheshi katika <i>Mashetani</i> .....	224
Jedwali 5.2	Mdafao wa Utokeaji wa Lugha ya Ucheshi katika <i>Kijiji Chetu</i> .....	234
Jedwali 5.3	Mdafao wa Utokeaji wa Lugha ya Ucheshi katika <i>Harakati za Ukombozi</i> .....	239
Jedwali 5.4	Mdafao wa Utokeaji wa Lugha ya Ucheshi katika <i>Safari ya Chinga</i> .....	246
Jedwali 5.5	Mdafao wa Utokeaji wa Lugha ya Ucheshi katika <i>Changamoto</i> ...	264
Jedwali 5.6	Mdafao wa Utokeaji wa Lugha ya Ucheshi katika <i>Nje-Ndani</i> .....	273
Jedwali 5.7	Misimu Neno katika <i>Mashetani</i> .....	285
Jedwali 5.8	Misimu Neno katika <i>Kijiji Chetu</i> .....	288
Jedwali 5.9	Misimu Neno katika <i>Harakati za Ukombozi</i> .....	291
Jedwali 5.10	Misimu Neno katika <i>Safari ya Chinga</i> .....	293
Jedwali 5.11	Misimu Kikundi katika <i>Safari ya Chinga</i> .....	296
Jedwali 5.12	Misimu Neno katika <i>Changamoto</i> .....	298
Jedwali 5.13	Misimu Kikundi katika <i>Changamoto</i> .....	299
Jedwali 5.14	Misimu Neno katika <i>Nje – Ndani</i> .....	301
Jedwali 5.15	Misimu Kikundi katika <i>Nje – Ndani</i> .....	303
Jedwali 5.16	Matumizi ya Uchanganyaji Ndimi katika <i>Safari ya Chinga</i> .....	318
Jedwali 6.1	Mdafao wa Ubunifu wa Matumizi ya Lugha katika <i>Tamthilia Teule</i> .....	377

**UFUNGUO WA VIFUPISHO**

ASP	Afro Shiraz Party
BAKITA	Baraza la Kiswahili la Taifa
Br.	Brother (Mtawa wa Kiume)
CCM	Chama Cha Mapinduzi
Dkt.	Dakta (Daktari wa Falsafa)
DUP	Dar es Salaam University Press
Fr.	Father (Padre)
h.m	hakuna mwaka
N/M	Namba Mfuatano
Nk. (nk.)	Na kadhalika
NUTA	National Union of Tanganyika Workers
PhD	Doctor of Philosophy
PhD. Kisw	Doctor of Philosophy in Kiswahili
Prof.	Profesa
Rej. (rej.)	Rejea (rejea)
Rev.	Reverend
Sr.	Sister (Mtawa wa Kike)
TANU	Tanganyika Africans National Union
TATAKI	Taasisi ya Taaluma za Kiswahili
TEHAMA	Teknolojia ya Habari na Mawasiliano
TPH	Tanzania Publishing House
TUKI	Taasisi ya Ukuzaji Kiswahili
TYL	TANU Youth League
Uk. ( uk.)	Ukurasa (ukurasa)
UKIMWI	Upungufu wa Kinga Mwilini
UWT	Umoja wa Wanawake Tanzania
VVU	Virusi Vya Ukimwi



## **SURA YA KWANZA**

### **UTANGULIZI**

#### **1.1 Utangulizi wa Sura**

Sura hii ni sura tangulizi ambayo ndiyo msingi wa utafiti wetu. Sura imegawanywa katika sehemu saba (7) ambazo ni: utangulizi wa sura, usuli wa tatizo la utafiti, tamko la tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti na mipaka ya utafiti. Kwa ujumla sehemu hizi zimewasilisha na kujadili kwa kina sababu za msingi zilizosababisha kufanyika kwa utafiti huu. Kwa hiyo, sura hii ni ufunguo wa sura zinazofuata kimantiki na kimtiririko.

#### **1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti**

Maendeleo ni dhana mtambuka, yaani telezi. Hivyo, hatuna budi kutambua kwamba hakuna namna moja na rahisi ya kufasili na kuelezea dhana “maendeleo” pasipo kuibua mvutano hasa kijamii (Barnett, 1988a). Kwa mujibu wa Barnett (1988a), wapo wanataaluma wanaotazama maendeleo kama hali au kitu kisichokuwa na uendelevu baada ya kukipata. Lakini wengine wanatazama maendeleo kama mchakato endelevu wa kupata, kuongeza, kusaka na kuboresha zaidi ya hapo ulipofikia. Mathalani, Seers (1972) anapendekeza maendeleo yapimwe kwa kuangalia idadi, hali, ubunifu, mchakato wa maamuzi, urahisi wa upatikanaji wa mahitaji, ushirikiano na ushirikishanaji wa fursa, teknolojia na raslimali. Vigezo hivi vya kupima maendeleo ni sharti vithibitishwe kama kuna mabadiliko chanya ama hasi au hakuna chanya wala hasi. Mabadiliko chanya ndiyo yanayotambulika kama ishara ya kuwapo maendeleo ilhali mabadiliko hasi au yasiyo chanya wala hasi

yanatambulika kama ishara ya kutokuwapo kwa maendeleo bali kuna udumavu katika nyanja husika ya maisha.

Nyerere (1973) anayatazama maendeleo kwa jicho la athari yake kwa watu husika. Mathalani, kwa Nyerere (1973), kuongezeka kwa idadi ya barabara, majumba, mazao, madarasa, na vitu vingine siyo maendeleo kwani hivi vyote ni vyombo vya maendeleo. Kinachofanya maendeleo yawe maendeleo ni pale tu vyombo hivi vinapomsaidia mtu kutatua matatizo yake kwa ufanisi. Yaani, tunasema kuna maendeleo endapo; na endapo tu mtu amepata au ameongeza ujuzi na elimu ili kutokomeza adui ujinga. Pia, tunaweza kusema kwamba kuna maendeleo kama mtu huyo amepata au kuongeza afya bora ili kutokomeza adui maradhi. Vilevile, tutasema kuna maendeleo kama mtu anaweza kujiongezea kipato kwa njia halali ili kupigana na kutokomeza adui umaskini.

Nayo tume ya Independent Commission of the South on Development Issues (1992) inasisitiza kwamba, maendeleo ni sharti yawe ni hatua ya kutoka katika uduni kwenda katika hali bora. Tena, maendeleo yalenge uvumbuzi na ugunduzi wa teknolojia, kuongeza vitu na nguvu ya maamuzi yenye tija ili kukidhi uhitaji wa watu. Maendeleo yajikite katika kuendelea kupiga kelele dhidi ya dhuluma, chuki, matabaka na unyonyaji ili kuleta usawa na haki kwa wote. Na kwamba, maendeleo sharti yawe ni mchakato endelevu ili kukimbizana na mahitaji ya wakati yanayosababisha mabadiliko yanayotokea kila siku duniani. Tume hii (imetajwa awali) inasisitiza kuwa, jamii isiyokubali mabadiliko haina budi kutambua nguvu yao ya kupinga mabadiliko ni nguvu ya muda tu. Kwani wakati kwa nguvu yake ya asili utawabadilisha.

Pearson (2000) pia anakubaliana na mawazo ya wataalamu waliotangulia kwa kuisitiza kuwa maendeleo ni sharti yapimwe kwa kulenga watu badala ya vitu. Pearson (2000) anaweka mkazo katika umuhimu wa kupima maendeleo kwa kutazama hali, idadi na namna mambo hayo yanavyoruhusu maboresho, ugunduzi na uvumbuzi wenye kuleta tija endelevu kwa jamii. Kamwe maendeleo yasiwe kitu dumavu ambacho kikifikiwa tu, akili inakoma kuwaza upya.

Kwa jumla tunaweza kusema, maendeleo dhahiri huanzishwa na watu wa jamii husika na kuendelezwa na watu wa jamii husika. Kitendo cha jamii kutambua fursa au changamoto kisha kuzikabili kwa lengo la kuvuna tija ni mfano wa maendeleo. Hii ndiyo kusema, maendeleo ni maboresho endelevu yenye kulenga ustawi, uimarifu au kuenzi kilicho na tija kwa faida ya mtu mmoja mmoja na jamii ya sasa na zijazo pasipo kuwapo ukomo wa juhudi za maboresho endelevu. Na kwamba, maendeleo yanaweza kupimwa kwa namna mtambuka zikiwemo kulinganisha: idadi, hali ya ubora, ubunifu, mchakato wa maamuzi, urahisi wa upatikanaji wa huduma, ushirikiano na ushirikishanaji wa fursa, uvumbuzi wa teknolojia na matumizi endelevu ya rasilmali. Maendeleo ya kweli hujidhihirisha kupitia maboresho yenye kuleta mabadiliko chanya katika nyanja zote za maisha kisiasa, kijamii, kiuchumi na kiutamaduni. Kinyume cha mabadiliko chanya ni udumavu wa maendeleo katika kila uga wa maisha. Kwa sababu, athari moja katika maendeleo ya binadamu, husambaa hata kuathiri nyanja nyingine, pia.

Ufafanuzi huu kuhusu dhana ya maendeleo, unatusaidia nasi kupata mwelekeo juu ya maendeleo ya tamthilia. Kwamba, kama kunatokea mabadiliko katika nyanja za siasa, jamii, uchumi, utamaduni, sayansi na teknolojia, basi hatuna budi kuamini

kwamba hata Tamthilia ya Kiswahili nayo imeathirika katika maendeleo yake. Kwa hiyo, pana uhitaji wa kufahamu kama kuna maendeleo katika Tamthilia ya Kiswahili ama la. Senkoro (1987) anasisitiza ya kuwa, fasihi ni zao la jamii ambayo inaishi katika sayari iliyo katika mwendo. Hivyo, hata mwanadamu naye yumo katika mwendo wa mabadiliko. Kwa hiyo, hata fasihi inabadilika kulingana na mabadiliko ya mifumo ya maisha ya kila siku ya mwanadamu. Hoja ya Senkoro (1987) inatupatia picha ya kutambua kuwa hata tamthilia kama sanaa ya fasihi andishi inaweza kubadilika kulingana na mabadiliko ya wakati na mifumo ya maisha ya watu. Kwa hiyo hatuna budi kuzingatia nyakati kuchunguza maendeleo ya utanzu huu.

Wapo wanataaluma na watafiti waliowahi kujishughulisha na maendeleo ya Fasihi ya Kiswahili na Tamthilia ya Kiswahili. Baadhi yao ni Wafula (1999), Njogu na Chimerah (1999), Semzaba (2003), S. M. A. Massoud<sup>1</sup> (2013), Murungi (2013), Samwel (2013), Gromov (2014), Olali (2015) na Mulokozi (2017). Wanataaluma hawa wanaonesha ya kwamba, Tamthilia ya Kiswahili katika ujumla wake imepiga hatua kubwa kimaendeleo katika vipindi tofauti tofauti vya historia na makuzi yake. Hata hivyo, kipindi kinachoonekana kuzungumziwa zaidi tena kwa utajiri mwingi wa mifano ni kile cha awamu ya Azimio la Arusha kuliko kipindi cha kabla na baada ya awamu tajwa.

---

<sup>1</sup> Uandishi huu umezingatia mwongozo wa chuo wa uandishi wa tasnifu (rej. OUT, 2022/2023). Mwongozo unatutaka kutumia vifupisho vya majina ya awali pamoja na jina kamili la ubini pindi tunaporejelea maandishi wawili au zaidi wenye jina moja la ubini. Yaani, tahajia za jina la ubini zinafanana. Kwa tasnifu yetu tunao S. M. A. Massoud (2013) na S. S. Massoud (2018).

S. M. A. Massoud (2013) na Mulokozi (2017) wanaeleza kuwa tamthilia chache katika awamu ya Azimio la Arusha zilitungwa ili kutetea sera, sheria, matamko ya majukwaani na mifumo iliyowekwa na viongozi wa kisiasa pasipo kuchuja mambo hayo. Mfano wa tamthilia hizo ni *Dunia Iliyofarakana* (1967) ya Crispin Hauli, *Bwana Mkubwa* (1974) ya John P. Mbonde, na *Heko Kuanzisha Chama* (1977) ya Kung'ala L. Kangula. Mulokozi (2017) anabainisha kuwa, tamthilia hizi hazikuonesha ukomavu kisanaa katika kuchunguza kwa kina maisha ya watu na utekelezaji wa sera, mipango na matamko yenye kufungamana na Azimio la Arusha.

Mulokozi (2017) anaendelea kutanabaisha zaidi kwamba, tamthilia nyingi za awamu ya Azimio la Arusha zilitungwa zikilenga kuyajadili na kuyatathmini maisha ya binadamu hasa mtu mnyonge. Huku zikihoji utekelezwaji wa sera, sheria, matamko ya kisiasa majukwaani, mifumo ya utawala na athari za ukoloni na ukoloni mamboleo katika nyanja zote za maisha. Miongoni mwa tamthilia zilizotilia maanani changamoto za maisha ya tabaka la chini ni *Wakati Ukuta* (1973) ya Ebrahim N. Hussein, *Wala Mbivu* (1974) ya Angelina Chogo, *Kijiji Chetu* (1975) ya Ngalimecha Ngahyoma, *Pambo* (1975) ya Penina Mhando, *Giza Limeingia* (1980) ya Emmanuel Mbogo, *Harakati za Ukombozi* (1982) ya Amandina Lihamba, Ndyanao Balisidya na Penina Mhando. Tamthilia nyingine ni *Lina Ubani* (1984) ya Penina Mhando, *Duka la Kaya* (1985) ya Tegamwage Ndimara, *Kwenye Ukingo wa Thim* (1988) ya Ebrahim N. Hussein, na *Ngoswe Penzi Kitovu Cha Uzembe* (1988) ya Edwin Semzaba.

Kwa upande wa fani, hususani matumizi ya lugha katika tamthilia za awamu ya Azimio la Arusha, Semzaba (2003) na Mulokozi (2017) wanatujaza zaidi kuwa,

kipindi hiki kiliwabeba vema watunzi kadhaa. Watunzi hao ni pamoja na Ebrahim N. Hussein na Penina Mhando ambao walianza kuitambulisha Tamthilia ya Kiswahili kwa misingi ya fani ya sanaa jadia ya Mwafrika kupitia kazi zao. Miongoni mwa kazi hizo ni *Lina Ubani, Pambo, Jogoo Kijijini, Ngao ya Jadi na Mashetani*. S. M. A. Massoud (2013) na Samwel (2013) wanaishibisha kauli ya Semzaba (2003) kwa kufafanua kuwa ni katika kipindi hiki ndipo majaribio ya msingi katika Tamthilia ya Kiswahili yaliposhika kasi kwa kuisitiza na kuenzi utamaduni wa Mwafrika.

S. M. A. Massoud (2013) na Samwel (2013) wanaongeza kuwa, matumizi ya lugha sanifu ya Kiswahili na semi za Kiafrika yalizingatiwa sana katika utunzi na uandishi wa tamthilia ili kuifungamanisha jamii ya Waswahili na sanaa yao ya Tamthilia ya Kiswahili. Wanataaluma hawa S. M. A. Massoud (2013) na Samwel (2013) wanaitaja chachu nyingine kuwa ni matumizi ya lugha ya mficho yaliyozitajirisha sana tamthilia zilizojaribu kuzungumza mambo mazito yaliyoonekana mwiba mchungu moyoni mwa wakubwa. Naye Gromov (2014) anaelezea mafanikio ya awamu ya Azimio la Arusha nchini Tanzania yalichagizwa na ubunifu uliotokana na watunzi kuakisi hali halisi ya maisha ya watu, utashi wa kisiasa na sera ya elimu na sera ya utamaduni ya taifa (rej. Wizara ya Elimu na Utamaduni, h. m). Gromov (2014) anaeleza kuwa tamthilia nyingi za kipindi hiki zilijaa lugha na maudhui yaliyoathiriwa zaidi na Umaksi, Unegritudi, Uhistoria Mpya, Uhalisia, na Ufeministi kwa kiasi.

Mlama (2003), S. M. A. Massoud (2013) na Mulokozi (2017) wanasema, majaribio katika uandishi wa tamthilia za Kiswahili za awamu ya Azimio la Arusha yalizidisha mvuto kwa sanaa hii kuonekana mpya miongoni mwa wasomaji. Wanataaluma hawa

wanauelezea upya huo kuwa ni ule wa kutoka katika uandishi wa Kimagharibi na kuingia katika uandishi wa Kiafrika zaidi. Uandishi wa Kimagharibi ulikita zaidi katika utunzi wa Kiaristotle, kushusha hadhi ya Mwafrika na kutukuza hadhi ya mzungu kwa maslahi mapana ya kutawala, kumiliki, kunyonya na kuendeleza ajenda za ukoloni. Wanataaluma hawa wanaendelea kufafanua kwamba, upya katika Tamthilia ya Kiswahili uliingiza Falsafa ya Mwafrika, Sanaa Jadia ya Mwafrika na kujadili maslahi ya Mwafrika. Pia, upya huu ulibeba utambulisho wa Mwafrika, kuenzi na kutetea utamaduni chanya wa Mwafrika na kukuza Lugha ya Mswahili (Mlama, 2003; S. M. A. Massoud, 2013; Mulokozi, 2017).

Bila shaka hali hii ilikuwa ni kichocheo kikubwa kwa wasomaji nchini Tanzania kupenda kusoma tamthilia za Kiswahili. Historia hii kutoka kwa wanataaluma na watafiti tuliowataja hapo awali, inaonesha kuwapo kwa maendeleo endelevu katika Tamthilia ya Kiswahili. Hata hivyo, Gromov (2014) na Olali (2015) wanakiri kushuka kwa kasi ya maendeleo ya Fasihi ya Kiswahili ikiwemo tamthilia nchini Tanzania. Watafiti hawa wawili (2), wanaonesha kuwapo kwa ongezeko la utunzi na ari ya usomaji wa Fasihi ya Kiswahili tamthilia ikiwemo, nchini Kenya tofauti na hali ilivyo nchini Tanzania. Miongoni mwa sababu wanazotoa ni mabadiliko ya kisera nchini Kenya yaliyochochea matumizi makubwa ya Kiswahili, uimarifu wa soko la kazi za Kiswahili, ubunifu miongoni mwa watunzi na wachapishaji, pamoja na ari ya wasomaji wa kazi za Kiswahili nchini Kenya. Pia, hali ya kukinaiwa miongoni mwa wasomaji wa Tanzania na kushuka kwa ubunifu miongoni mwa watunzi wengi na wachapishaji baadhi wa Tanzania.

Hoja hii ya Gromov (2014) na Olali (2015) ndiyo ilichochea hamu na msukumo wa kufanyika kwa utafiti huu ili kujua iwapo madai haya yana ukweli ama la. Vilevile, tuliona kuna haja ya kufanya utafiti linganishi wa awamu mbili ambazo ni awamu ya Azimio la Arusha na awamu ya soko huria. Lengo ni kutaka kulinganisha ubunifu wa ujenzi wa dhamira na matumizi ya lugha katika vipindi hivyo viwili. Kwani, Jilala (2016) anaeleza kuwa ulinganishaji wa kazi za fasihi haulengi kazi ya mtu na mtu bali unaweza kuwa wa vipindi ama awamu mbili za kihistoria. Kwa hiyo, kwa kuzingatia hilo tuliona kuna haja ya kufanya utafiti wa kina zaidi kuhusu maendeleo ya Tamthilia ya Kiswahili.

Pia, hoja ya Gromov (2014) na Olali (2015) juu ya ubunifu kupungua nchini Tanzania kwa mfano, yanaonekana kupingana na taarifa zilizomo katika maandiko ya wanataaluma na watafiti wengine mfano Semzaba (2003), Mutembe (2009), Samwel (2013) na Mulokozi (2017). Wanataaluma hawa (Semzaba, 2003; Mutembe, 2009; Samwel, 2013; Mulokozi, 2017) wanasisitiza kuwapo kwa ubunifu katika utunzi wa tamthilia za zamani na za sasa. Aidha, wanatambua kuwapo kwa uhuru zaidi miongoni mwa watunzi katika kuteua, kusana na kuwasilisha mawazo yao kwa mapana na marefu tofauti na ilivyokuwa wakati wa awamu ya Azimio la Arusha.

Tofauti hii ya taarifa ndiyo iliyochochea wazo la kulinganisha tamthilia za awamu ya Azimio la Arusha na awamu ya soko huria nchini Tanzania. Kwa sababu, zipo tamthilia za Kiswahili zinazotajwa na wasomaji na wanataaluma kadhaa kwamba zimesukwa kiubunifu kujadili mambo ya kisiasa, kijamii, kiuchumi na kitamaduni yanayogusa maisha ya watu wa zama hizi. Tamthilia hizo ni pamoja na *Mkutano wa*



*Pili wa Ndege* (1992) ya Amandina Lihamba, *Morani* (1993) ya Emmanuel Mbogo, *Mzizi Je?* (1994) ya Idara ya Sanaa na Muziki na Sanaa za Maonyesho – Chuo Kikuu cha Dar es salaam, *Shinikizo* (1994) ya Idara ya Sanaa na Muziki na Sanaa za Maonyesho – Chuo Kikuu cha Dar es salaam, *Amezidi* (1995) ya Said Ahmed Mohamed.

Tamthilia nyingine zinazojadili mambo ya msingi kwa maendeleo ya Mswahili ni *Kilio Chetu* (1995) ya Medical Aid Foundation, *Kila Siyesikia* (1997) ya Mathias Eugen Mnyampala, *Kaptula la Marx* (1998) ya Euphrase Kezilahabi, na *Kitumbua Kimeingia Mchanga* (2000) ya Said Ahmed Mohamed. Nyingine ni *Adila* (2002) ya Fikeni E. M. K. Senkoro, *Giza* (2004) ya Hadija Jilala, *Mpaka Lini?* (2004) ya Mariam S. Mwiru, *Mazonge* (2004) ya Ali Mwalim Rashid, *Kilio cha Jesca* (2004) ya Ambrose F. Mghanga, *Orodha* (2004) ya Steve Reynolds (Mfasiri: Saif D. Kiango), *Safari ya Chinga* (2009) ya Shani Omari, *Changamoto* (2010) ya Elizabeth Mahenge, *Sadaka ya John Okello* (2015) ya Emmanuel Mbogo, *Nje – Ndani* (2016) ya A. A. Majid Mswahili na M. S. Njonjolo na *Utangamano Wetu Ushindi Wetu* (2017/2023) ya Anitha E. Mgimba.

Tukichunguza orodha hii ya watunzi katika awamu ya Azimio la Arusha na awamu ya soko huria, tunabaini kuwapo kwa watunzi chipukizi (wapya) mfano Shani Omari, Hadija Jilala na Mariam S. Mwiru. Mbali na hao, tunawaona watunzi wakongwe wakiendelea kujitokeza katika kipindi cha awamu ya soko huria. Watunzi hao ni pamoja na Emmanuel Mbogo, Idara ya Sanaa na Muziki na Sanaa za Maonyesho – Chuo Kikuu cha Dar es salaam na Said Ahmed Mohamed. Mchanganyiko huu unatujengea tafakuri pana zaidi. Kwamba, siyo rahisi wakongwe kama Emmanuel

Mbogo, Idara ya Sanaa na Muziki na Sanaa za Maonyesho – Chuo Kikuu cha Dar es salaam na Said Ahmed Mohamed wakapoteza uwezo wa kubuni, kuteua na kusana maudhui na fani inayowagusa hadhira.

Vivyo hivyo, kwa watunzi chipukizi; tunadhani siyo rahisi wao kutunga kazi bila kuwasoma waandishi waliowatangulia ama kuomba msaada wao ili wahariri matini husika. Hapa tunajiuliza, Je, inawezekanaje watunzi chipukizi wakashindwa kunufaika kimbinu (mbinu za kisanaa) na kiufundi (ushauri wa kitaalamu, uhariri na ubwakuzi) kutoka kwa watunzi wakongwe kama vile Amandina Lihamba, Ebrahim N. Hussein, Edwin Semzaba (kipindi kabla hajatangulia mbele ya haki), Emmanuel Mbogo, na Penina Mhando? Kwa sababu, watunzi nguli hawa walikuwa ni watunzi chipukizi katika awamu ya Azimio la Arusha. Lakini, kwa sasa ni watunzi wakongwe na kazi zao zinaendelea kutambulika kwa heshima kubwa miongoni mwa wasomaji wa zama zao na wasomaji wa zama hizi kama wanavyotambulishwa na S. M. A. Massoud (2013), Samwel (2013) na Mulokozi (2017).

Kwa hiyo, tunapovuta picha juu ya hoja ya Gromov (2014) na Olali (2015), tunapata dukuduku moyoni na akilini juu ya usahihi wa taarifa zao kuhusiana na maendeleo ya Tamthilia ya Kiswahili katika awamu ya soko huria nchini Tanzania. Bila shaka hoja yao inaangukia kwenye hoja iliyowahi kusemwa na baadhi ya wanataaluma juu ya anguko la Azimio la Arusha. Kwamba, baada ya anguko la Azimio la Arusha, nyanja kuu za kiuchumi, kijamii, kiutamaduni na siasa zilijiendea shagharabagala bila kuwapo kwa mifumo madhubuti ya kusimamia na kudhibiti nyanja hizo za maisha (Ally na wenzake, 2013; Chachage, 2014).

Bila shaka, kuna uwezekano wa kutokuwapo kwa taarifa rasmi za kutosha za maendeleo ya Tamthilia ya Kiswahili katika awamu ya soko huria tofauti na ilivyo kwa awamu ya Azimio la Arusha nchini Tanzania. Na, bila shaka katika usoko huria pamepenyezwa kazi zisizobora kisanaa ambazo Gromov (2014) na Olali (2015) wamebahatika kukutana nazo. Kwa sababu serikali ilijiondoa katika kudhibiti na kuhodhi njia kuu za uzalishaji mali pasipo kuweka mikakati madhubuti ya kuliratibu soko (Chachage, 2014). Kwa hiyo kuanzia hapo, mambo mengi kama siyo baadhi hayajulikani namna yanavyoingia na kutoka sokoni pasipo kusahau ubora na usahihi wa taarifa. Kwani kuna nyakati ambapo hata mamlaka husika huonekana kutokujua kinachoendelea huko sokoni (Chachage, 2014).

Kama madai ya Gromov (2014) na Olali (2015) juu ya ubunifu kupungua nchini Tanzania ni sahihi, basi pana hatari ya kushusha hadhi ya Tamthilia ya Kiswahili na ari ya watunzi chipukizi. Kwani, wasomaji wengi hawataziamini tena tamthilia zilizotungwa na watunzi wa zama hizi. Matokeo yake, sanaa hii itadharaulika kiasi cha wanajamii kuacha kuipatia kipaumbele sokoni na kiuandishi. Hali hii itaathiri kwa namna hasi hata historia na maendeleo, utunzi, ufadhili, uchapishaji, usambazaji na utafiti wa Tamthilia ya Kiswahili, hususani tamthilia za watunzi wanaochipua kila kukicha.

Kwa muktadha huu, ukweli dhahiri kuhusu maendeleo ya ubunifu wa Tamthilia ya Kiswahili nchini Tanzania ni sharti ujulikane ili kuondoa utata wa taarifa na athari hasi tulizozitambulisha hivi punde. Kwa kujua ukweli, jamii ya wanataaluma na watunzi wa Fasihi ya Kiswahili, watashirikiana kutatua changamoto zinazodunisha ubunifu endelevu katika Tamthilia ya Kiswahili nchini Tanzania. Hivyo, utafiti huu

ulimakinikia vipindi vikuu viwili (2) vya historia ya makuzi na ustawi wa taifa la Tanzania - kisiasa, kijamii, kiuchumi, kiutamaduni, kisayansi na kiteknolojia. Vipindi hivyo ni awamu ya Azimio la Arusha na awamu ya soko huria.

### **1.3 Tamko la Tatizo la Utafiti**

Mukubwa (1985), S. M. A. Massoud (2013), Murungi (2013), Samwel (2013), Gromov (2014) na Olali (2015) ni miongoni mwa watafiti wanataaluma wanaobainisha kupitia maandiko yao kwamba, kumekuwapo na maendeleo katika Fasihi ya Kiswahili hususani tamthilia. Hata hivyo, Gromov (2014) na Olali (2015) wanabainisha kwamba, kumekuwa na hali ya kushuka kwa kiwango cha ubunifu katika tamthilia za Kiswahili za nchini Tanzania huku zile za nchini Kenya zikionekana kuimarika kiubunifu.

Kama madai haya ni ya kweli, maana yake uchapwa katika ubunifu unatishia uhai na ustawi wa maendeleo ya Tamthilia ya Kiswahili nchini Tanzania. Hata kama hisia hii ni sahihi, bado tafiti za wataalamu hawa haziwezi kuwa hitimisho la hali ya maendeleo ya Tamthilia ya Kiswahili kwa sasa. Kwa sababu tafiti zao zina miaka kadhaa sasa tangu zilipofanyika na kutoa mapendekezo ya nini kifanyike. Bila shaka, kuna juhudi kubwa zimefanyika ili kunusuru hali ya ukuaji na ustawi wa Tamthilia ya Kiswahili kiubunifu nchini Tanzania; lakini juhudi hizo hazijatambulika rasmi hadharani. Aidha, tafiti hizi (Gromov, 2014; Olali, 2015) zinaonekana kujikita zaidi katika tamthilia za awamu ya Azimio la Arusha kuliko tamthilia za awamu ya soko huria. Bila shaka mahitimisho yao yaliathiriwa na uchache wa data zilizopatikana kwa upande wa tamthilia za Kiswahili za awamu ya soko huria za nchini Tanzania.

Mtafiti alijitahidi kusaka taarifa za kisayansi juu ya maendeleo ya Tamthilia ya Kiswahili katika awamu ya soko huria. Lakini hakufanikiwa kukutana na ripoti yenye matokeo ya utafiti uliochunguza maendeleo ya Tamthilia ya Kiswahili kwa kulinganisha ubunifu katika uteuzi na ujenzi wa dhamira na matumizi ya lugha katika tamthilia za Kiswahili za awamu ya Azimio la Arusha na awamu ya soko huria. Hali hii ndiyo ilimpa msukumo mtafiti kufikia uamuzi wa kufanya utafiti linganishi wa awamu mbili tofauti ili kuchunguza maendeleo ya ubunifu katika matumizi ya lugha na uibuaji wa dhamira za Tamthilia za Kiswahili. Lengo lilikuwa ni kuchunguza ili kubaini kama kuna ubunifu endelevu katika Tamthilia za Kiswahili nchini Tanzania.

#### **1.4 Malengo ya Utafiti**

Kazi hii ina malengo mawili, lengo kuu na malengo mahususi matatu (3), kama ifuatavyo: -

##### **1.4.1 Lengo Kuu**

Utafiti ulilenga kulinganisha kazi za awamu ya Azimio la Arusha na zile za soko huria ili kubaini kufanana na kutofautiana katika ubunifu wa ujenzi wa dhamira na matumizi ya lugha ili kuona kama kuna maendeleo endelevu ama la.

##### **1.4.2 Malengo Mahususi**

Utafiti huu una malengo mahususi matatu (3). Nayo ni: -

- i. Kulinganisha ubunifu katika dhamira zinazojitokeza katika tamthilia teule za Kiswahili za awamu ya Azimio la Arusha na zile za soko huria ili kubaini kama kuna ubunifu endelevu.

- ii. Kulinganisha ubunifu katika matumizi ya lugha yanayojitokeza katika tamthilia teule za Kiswahili za awamu ya Azimio la Arusha na zile za soko huria ili kubaini kama kuna ubunifu endelevu.
- iii. Kutathmini athari ya ubunifu katika dhamira na matumizi ya lugha yanayojitokeza katika tamthilia teule za Kiswahili za awamu ya Azimio la Arusha na zile za soko huria ili kubaini namna zinavyochochea maendeleo endelevu ya Tamthilia ya Kiswahili kisanaa.

### **1.5 Maswali ya Utafiti**

Utafiti huu umeongozwa na maswali mahususi matatu (3). Nayo ni: -

- i. Je, ubunifu katika dhamira zinazojitokeza katika tamthilia teule za Kiswahili za awamu ya Azimio la Arusha unafanana na kutofautiana vipi na ule wa tamthilia teule za Kiswahili za awamu ya soko huria?
- ii. Je, ubunifu katika matumizi ya lugha yanayojitokeza katika tamthilia teule za awamu ya Azimio la Arusha unafanana na kutofautiana vipi na ule wa tamthilia teule za Kiswahili za awamu ya soko huria?
- iii. Kwa vipi athari ya ubunifu katika dhamira na matumizi ya lugha yanayojitokeza katika tamthilia teule za Kiswahili za awamu ya Azimio la Arusha na zile za soko huria yanaweza kuchochea maendeleo endelevu ya Tamthilia ya Kiswahili kisanaa?

### **1.6 Umuhimu wa Utafiti**

Utafiti huu ulikusudia kutafuta taarifa sahihi juu ya hali ya maendeleo ya ubunifu katika Tamthilia ya Kiswahili kwa kulinganisha utunzi bunilizi kati ya awamu ya Azimio la Arusha na awamu ya soko huria. Hivyo, matokeo ya utafiti huu yana

umuhimu mkubwa katika taaluma ya fasihi kinadharia na kivitendo. Kwa umahususi zaidi matokeo ya utafiti yatakuwa na mchango mkubwa wa maarifa katika taaluma ya fasihi linganishi na Tamthilia ya Kiswahili. Kulingana na malengo ya utafiti huu, matokeo ya utafiti wetu ambayo yamejikita katika misingi na mwongozo wa kisayansi; yatasaidia kuwawezesha wahakiki wa tamthilia za Kiswahili kumakinikia namna ubunifu ulivyojengwa katika tamthilia wanazozihakiki. Vilevile, wahakiki watapata maarifa ya namna sahihi ya kuhakiki tamthilia kwa kuongozwa na nadharia ya Fasihi Linganishi ambayo inaonekana kuwa faafu zaidi kwa uhakiki wa zama hizi. Pia, taarifa hizo zitasaidia kujua ukweli juu ya kufanana na kutofautiana kwa maendeleo ya ubunifu katika dhamira na matumizi ya lugha katika awamu mbili tofauti.

Pili, ripoti ya utafiti huu itakuwa rejeo muhimu kwa walimu na wanafunzi kuongeza wigo wa maarifa ya namna ya kutathmini au kuchunguza maendeleo ya Tamthilia ya Kiswahili. Kwa wao kulinganisha tamthilia tofauti tofauti zilizomo katika mazingira yao ambazo zimetokana na vipindi tofauti tofauti vya kihistoria - mbali na vyanzo vya maarifa wanavyotumia. Pia, tasnifu hii utakuwa kichocheo kwao katika kujenga utamaduni wa kutafuta maarifa mapya kupitia vyanzo tofauti tofauti badala ya kutegemea chanzo kimoja cha maarifa katika kuandaa matini ya kujifunzia na kufundishia maendeleo ya Tamthilia ya Kiswahili. Kwa sababu, imebainika wazi kwamba Watanzania wengi hawana utamaduni wa kusaka taarifa sahihi kupitia kujisomea badala yake wanangojea kuletewa tu (Senkoro, 1995).

Tatu, utafiti huu utakuwa wa manufaa kwa walimu na wanafunzi wa kozi ya uandishi bunilizi pamoja na watunzi chipukizi kufanya ulinganifu wa vipengele vya kifani na

kidhamira vya tamthilia za Kiswahili zilizotungwa katika vipindi tofauti tofauti. Lengo ni kuwawezesha kubaini hali na maendeleo ya Tamthilia ya Kiswahili kiubunifu. Kisha kutoa tathmini na maboresho ya kiutunzi kupitia kazi zao. Kupitia tasnifu hii, walimu na wanafunzi watapata kujua maeneo ya kisanaa ambayo hayatiliwi mkazo sana katika mchakato wa utunzi, uhariri na uchapishaji wa tamthilia za Kiswahili. Hivyo, kwa wao kuyatambua maeneo husika, kutawawezesha kutunga tamthilia za Kiswahili zinazobeba ubunifu endelevu wenye kuhusisha vipengele vya kisanaa visivyotiliwa mkazo miongoni mwa watunzi walio wengi.

Nne, utafiti huu hatimaye utawapa mwongozo watafiti wanaohitaji kujikita katika utafiti wa maendeleo ya Tamthilia ya Kiswahili. Kwa wao kuanza au kuendelea kutumia mbinu ya utafiti linganishi ambayo imeonekana kuwa na tija zaidi katika kuchunguza historia na maendeleo ya Tamthilia ya Kiswahili hususani eneo la ubunifu endelevu. Pia, utafiti huu utawasaidia watafiti wapya kuchunguza hali na sababu zinazochangia kutokupatikana kwa taarifa sahihi na za kutosha juu ya maendeleo ya ubunifu endelevu ya Tamthilia ya Kiswahili nchini Tanzania.

### **1.7 Mipaka ya Utafiti**

Katika utafiti huu neno “maudhui” linafasiliwa kulingana na fasili iliyotolewa na Wamitila (2008) na Samwel (2013) kuwa limemaanisha mambo yanayojadiliwa na mwandishi katika kazi za kisanaa. Na kwamba, maudhui huundwa na vipengele kadhaa vikiwemo dhamira, ujumbe, falsafa, itikadi, propaganda, msimamo na mtazamo. Kwa mantiki hii, vipengele vya maudhui ni vingi. Hivyo, utafiti hauwezi kuvitalii kwa kina vipengele hivi vyote vya maudhui pasipo kuacha ombwe la maarifa kwa sababu ya upana wake kimawanda. Aidha, dhamira ndicho kipengele



cha maudhui kinachobeba utajiri mkubwa wa kile anachokijadili mwandishi ndani ya matini yake (Wamitila, 2008; Samwel, 2013).

Hivyo, kwa muktadha huu, mtafiti amejifungia katika kipengele cha dhamira pekee ili kubainisha na kulinganisha ubunifu wa maudhui yanayopatikana katika tamthilia sita (6) teule. Sababu ya kujifungia katika kipengele kimoja cha maudhui ilikuwa ni kuruhusu udurusi wa kina katika kuchimba na kuibua dhamira nyingi kwa kadri ya uwezo wa mtafiti kutoka katika kila tamthilia teule. Kisha kufanya uchunguzi wa kina kwa lengo la kukidhi matakwa ya utafiti wa kisayansi wa tasnifu ya kitaaluma ya shahada ya uzamivu. Kwa hiyo, ili kuondoa utata wa kimaarifa miongoni mwa wasomaji wa andiko hili, mahali popote ndani ya andiko hili patakapobeba sauti ya mtafiti kupitia neno “maudhui” (endapo itatokea), basi itambulike kuwa tunamaanisha “dhamira.”

Kwa upande wa matumizi ya lugha, utafiti huu umemakinikia vipengele vya lugha ya ucheshi, misimu, uchanganyaji ndimi pamoja na wepesi na ugumu wa lugha iliyotumika katika kuwasilisha maudhui katika tamthilia sita (6) teule. Uteuzi wa vipengele hivi ulizingatia ushahidi wa kisayansi unaothibitisha kwamba wahakiki wengi hasa wale wenye tahakiki zinazotumika mashuleni hawaonekani kutilia mkazo vipengele hivi pindi wanapohakiki matumizi ya lugha katika kazi za kifasihi. Baadhi ya wahakiki hao ni Masebo na Nyangwine (2008), pia Mhilu na wenzake (2008). Hivyo, tuliona kupitia utafiti huu ni vema kutilia mkazo vipengele hivi vya lugha ili kuwaamsha wahakiki na watafiti kuvipatia nafasi ya kutosha pindi wafanyapo uhakiki na utafiti wa tamthilia na kazi nyinginezo za kisanaa.

Kuhusu vipindi teule, mtafiti anaporejlea awamu ya Azimio la Arusha anamaanisha kipindi kati ya mwaka 1967 kulipozaliwa Azimio la Arusha na mwaka 1991 kulipozaliwa kwa kile kilichoitwa Azimio la Zanzibar. Hapa tunapata jumla ya miaka 25. Kwa hiyo, ili kupata uwiano sawia katika kulinganisha vipindi, mtafiti ameteua miaka 25 mingine kuanzia 1992 hadi 2016 ili kuwakilisha kipindi cha awamu ya soko huria. Ieleweke kwamba, miaka hii hailengi kumaanisha kwamba kila badiliko la kijamii, kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni, kisayansi na kiteknolojia lililojitokeza ndani ya kipindi teule chanzo chake ni kipindi husika.

Hii ni kwa sababu, kimakuzi; Barnett (1988a & 1988b) anafafanua vema kuwa, maendeleo huchochewa na mambo mengi – ya kabla, wakati na baada ya kipindi husika. Barnett (1988a & 1988b) anaongeza kwamba, kawaida, maendeleo hutokana na mifumo inayowekwa ili kuruhusu au kudhibiti matokeo yanayotarajiwa au yasiyotarajiwa. Kwa hiyo, vipindi hivi teule vimewakilisha matokeo (mambo) ya kimaendeleo yanayotambulika kihistoria kutokea katika miaka tunayoihusisha na utafiti wetu – si vinginevyo. Naye Ntarangwi (2004) anaongeza kuwa, “kila kipindi cha kihistoria kina mifano mbalimbali ya kazi za tamthilia. Hivyo basi, hatuwezi kusema kuwa ni aina moja tu ya tamthilia (kimaudhui na kifani<sup>2</sup>) inayopatikana katika kipindi maalumu (kimoja<sup>3</sup>) cha historia” (uk. 42).

Faukwa ya hayo, tamthilia zilizochunguzwa ni sita (6); tatu (3) kutoka kila kipindi. Tamthilia tatu (3) kutoka awamu ya Azimio la Arusha ni *Mashetani* (1971) ya Ebrahim N. Hussein, *Kijiji Chetu* (1975) ya Ngalimecha Ngahyoma na *Harakati za Ukombozi* (1982) ya Amandina Lihamba, Ndyanao Balisidya na Penina Mhando.

<sup>2</sup> Maneno haya yameongezwa na mtafiti. Siyo kauli iliyomo katika kauli nukuliwa ya Ntarangwi (2004).

<sup>3</sup> Maneno haya yameongezwa na mtafiti. Siyo kauli iliyomo katika kauli nukuliwa ya Ntarangwi (2004).

Nazo tamthilia tatu (3) za awamu ya soko huria ni *Safari ya Chinga* (2009) ya Shani Omari, *Changamoto* (2010) ya E. Mahenge na *Nje – Ndani* (2016) ya A. A. Majid Mswahili na M. S. Njonjolo. Upatikanaji wa tamthilia hizi ni matokeo ya mbinu ya usampulishaji nasibu tabakishi. Mbinu hii ilitusaidia kupata sampuli kwa njia isiyo ya upendeleo lakini yenye kuwakilisha miaka tofauti tofauti ndani ya awamu husika. Uteuzi huu ni wa tija katika kutoa picha kamili ya hali ya maendeleo ya ubunifu katika uteuzi na ujenzi wa maudhui na matumizi ya lugha katika Tamthilia ya Kiswahili nchini Tanzania.

Uteuzi wa tamthilia tatu (3) kwa kila awamu ulikuwa sahihi kwa sababu siyo rahisi kutumia sampuli kubwa kushinda uwezo wa mtafiti katika kutafiti mambo kisayansi. Utafiti wetu ulichunguza jumla ya vipengele vitano (5) katika kila tamthilia ambavyo ni dhamira, ucheshi, uchanganyaji ndimi, misimu, uwepesi na ugumu wa lugha. Dhamira peke yake ni kipengele kinachobeba mambo mengi kutoka kila tamthilia. Hivyo, haikuwa busara kuongeza idadi ya tamthilia teule. Aidha, tafiti nyingi zilizochunguza maendeleo ya maudhui na matumizi ya lugha zilitumia tamthilia mbili pekee. Pamoja na matumizi ya tamthilia mbili (2), bado matokeo ya tafiti husika yalionekana kukidhi matakwa ya tafiti husika. Miongoni mwa tafiti hizo ni ule wa Massoud (2013) na Massoud (2018).

## **SURA YA PILI**

### **MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA**

#### **2.1 Utangulizi**

Sura hii inahusu mapitio tangulizi yanayohusiana na mada ya utafiti wetu na kiunzi cha nadharia. Sura imegawanyika katika sehemu kuu mbili. Sehemu ya kwanza inahusu maandiko tangulizi na sehemu ya pili inahusu kiunzi cha nadharia. Katika sehemu ya kwanza mjadala umejikita katika ufafanuzi wa dhana muhimu zinazohusiana na utafiti huu, mapitio kuhusu historia na maendeleo ya Tamthilia ya Kiswahili katika awamu mbili (2) teule, mapitio ya tahakiki na tafiti tangulizi kuhusu tamthilia sita (6) teule na pengo la kimaarifa. Sehemu ya pili imejadili kiunzi cha nadharia iliyoongoza utafiti huu.

#### **2.2 Ufafanuzi wa Dhana Mbalimbali**

Sehemu hii inahusu ufafanuzi wa dhana ya tamthilia, maudhui na dhamira, matumizi ya lugha ya ucheshi, misimu, uchanganyaji ndimi, uwepesi na ugumu wa lugha na ubunifu. Ufafanuzi wa dhana hizi ulikuwa muhimu kwa sababu umesaidia kujenga uelewa mpana kuhusu dhana zilizotumika katika utafiti huu.

##### **2.2.1 Dhana ya Tamthilia**

Kumekuwapo na namna mbili za uandishi wa istilahi “tamthilia.” Kamusi ya Kiswahili Sanifu toleo la pili (TUKI, 2004: 394) inatumia “tamthiliya” pasipo kutambua istilahi “tamthilia.” Wanataaluma wengine waliotumia istilahi “tamthiliya” ni pamoja na Mukobwa (1985), Mohamed (1995), Wafula (1999), Mlama (2003), Samwel (2013), Semzaba (2003) na S. S. Massoud (2018). Hata hivyo, Kamusi ya Kiswahili Sanifu toleo la tatu (TUKI, 2014: 548) inazitambua istilahi zote mbili

yaani “tamthilia” na “tamthiliya” huku maana ikiwa ni ile ile. Naye Mulokozi (2017: 287 - 293) ametumia istilahi “tamthilia” sawa na S. M. A. Massoud (2013).

Kwa hiyo, mtu anayetumia istilahi “tamthilia” na yule anayetumia istilahi “tamthiliya” wote wawili wako sahihi kwa mujibu wa Kamusi ya Kiswahili Sanifu toleo la tatu (TUKI, 2014). Kwa muktadha wa utafiti huu (pale panapotokea sauti ya mtafiti) tumetumia istilahi “tamthilia.” Lakini tuliponukuu kauli, tumetumia istilahi iliyotoka katika matini chanzi. Yaani, ama “tamthilia” au “tamthiliya.”

Mazigwa (1991) anaifasili tamthilia kama “sanaa inayoonyeshwa kwa vitendo. Ni sanaa ambayo mtu hana budi kuviona vitendo vikifanyika ili kupata uzuri na dhana iliyomo katika sanaa inayoonyeshwa” (uk. 2). Mtazamo huu umejikita zaidi katika matumizi ya vitendo vinavyotendeka na kuonwa dhahiri. Maelezo ya Mazigwa yanaelekea kumrejelea Mlama (2003 – toleo la kwanza lilikuwa mwaka 1983) ambaye anaiona tamthilia kuwa ni aina mojawapo ya sanaa za maonesho ambayo usanii wa utendaji wake hutegemea zaidi vitendo na uongejaji. Tofauti na aina nyingine kama ngoma ambazo hutegemea zaidi uchezaji ngoma na upigaji muziki. Na kwamba sanaa hii inaweza kuwa imeandikwa au haijaandikwa.

Ufafanuzi wa wataalamu hawa hautoi mpaka kati ya tamthilia na sanaa za maonesho na sanaa za uigizaji katika fasihi simulizi. Tunasema hivi kwa sababu, wataalamu wengi wa fasihi wakiwemo Wamitila (2003; 2008), Senkoro (2011) na Mulokozi (2017), huitambulisha tamthilia kuwa ni sanaa andishi katika tawi la fasihi andishi. Ili kuitofautisha tamthilia na sanaa nyinginezo, hususani tanzu za fasihi andishi, Mohamed (1995) anadokeza kuwa tamthilia huandikwa kwa ajili ya kutendwa jukwaani au kupitia redio au televisheni wakati riwaya na hadithi fupi hakuna

utendaji, kuna usimulizi. Msisitizo unaojitokeza zaidi katika fasili ya Mohamed ni utendaji halisi na uwili wa kiutendaji kwa njia ya maandishi. Hata hivyo, kuna utata katika kuweka mipaka ya tamthilia pindi inapopelekwa jukwaani, redioni au kwenye televisheni. Kwani kuitazama tamthilia mbali ya maandishi ni kuisukumia kwenye sanaa za maonesho jambo ambalo si sahihi kwa tamthilia (Hussein, 2003).

Katika hili, Wafula (1999) anatoa tahadhari kwamba “dhana ya tamthiliya hukanganya kwa sababu imeingiliana sana na dhana nyingine kama drama, uigizaji na sanaa za utendaji” (uk. 1). Kwa maelezo haya, ina maana drama na tamthilia ni vitu viwili tofauti ijapokuwa dhana hizi zinaweza kuwa ni kitu kimoja kama wanavyozitumia baadhi ya wanataaluma, jambo ambalo siyo sahihi. Hata hivyo, Wafula anapendekeza drama iwe ni “taaluma inayofafanua mitazamo mbalimbali ya kuhakiki tamthiliya [...] taaluma inayoshughulikia tamthiliya, uhakiki na utathmini wake [...]” ilhali tamthilia iwe ni “ule mtungo hasa ulioandikwa kwa ajili ya kuigizwa au utungo wa fasihi unaowasilisha hadithi na migongano kwa kutumia maongezi na matendo ya wahusika” (uk. 2). Na kwamba, pindi tu tamthilia inapowekwa jukwaani na kuigizwa, basi ihesabiwe kuwa imekuwa ni kitendo cha sanaa ya utendaji, wakati sanaa ya uigizaji ichukuliwe kuwa ni “istilahi ya jumla inayoshirikisha uigizaji uwe wa ushairi, tamthiliya au riwaya [...]” (uk. 2).

Kwa upande mwingine, Hussein (2003) anaona kwamba tamthilia inaweza kutazamwa kuwa ni drama. Ambapo, drama iliyoandikwa “huishia kwenye fasihi” na ile inayokwenda jukwaani moja kwa moja bila kuandikwa au kupita kwenye kitabu huishia kwenye “ulimwengu wa jukwaa” (uk. 198). Maelezo ya namna hii juu ya tofauti kati ya tamthilia na drama yametolewa pia na Mulokozi (2017). Kwa hiyo

basi, tunaweza kusema kwamba Wafula, Hussein na Mulokozi wametusaikia kuhitimisha mjadala wa mpaka kati ya tamthilia na drama kwa kuweka bayana kuwa tamthilia itazamwe kama sanaa ya vitendo viliyoandikwa ilhali drama iwe ni ile sanaa ya vitendo inayotendwa jukwaani moja kwa moja bila kuandikwa au imetoka kwenye kitabu na kupelekwa kwenye ulimwengu wa jukwaa. Kwa mantiki hii, tunaweza kusema kuwa, endapo drama itaandikwa, basi hiyo ni tamthilia. Lakini tamthilia ikipelekwa jukwaani inageuka kuwa drama. Jambo la msingi ni kuwa, tamthilia iliyoandikwa haiwezi kuvua umbo la utendaji wala haiwezi kufanana na riwaya ama hadithi au ushairi kiuandishi.

Ndiyo maana, hata ukimkurupua mtu kutoka usingizini, ukampa maandiko matatu - hata kama siyo kazi za fasihi, lakini uandishi wake ukawa umebeba umbo la tamthilia, umbo la ushairi na umbo la riwaya. Halafu ukamtaka mtu huyo akuoneshe ipi ni tamthilia, ipi ni ushairi na ipi ni riwaya. Mtu huyo atatazama mpangilio wa maandishi husika. Kama mtu huyo anatambua kanuni za uandishi na mpangilio wa maandishi ya kazi hizo, hatapata ukakasi kukuonesha mara moja. Kwa hiyo, kiutunzi, umbo la drama huendelea kujitokeza ndani ya tamthilia. Hii ndiyo sababu kazi kama vile *Jogoo Kijijini* na *Ngao ya Jadi* (1976) za Ebrahim N. Hussein, baadhi ya wanataaluma wa Fasihi ya Kiswahili huziona kuwa ni sanaa popo. Sababu kuu ni mwonekano wake kiumbo. Baadhi huzitambulisha kazi hizi mbili kama tamthilia za kitendi na kingano. Huku wengine wakizitazama kama hadithi andishi za kitendi na kingano. Ilhali, wengine wakiziweka kwenye kapu la ushairi andishi wa kitendi na kingano (rej. Mulokozi, 2017).

Naye Ntarangwi (2004) anatujuza zaidi kuwa, tamthilia ni utanzu wa fasihi andishi ambao twaweza kusema ni zao la mabadiliko ya fasihi kama kipengele cha utamaduni wa jamii. Na kwamba, sanaa hii ni maigizo ya matukio au visa fulani kwa uhalisi wake kwa ajili ya kuyasawiri maudhui au maelezo fulani. Ntarangwi anaendelea kusema kuwa, dhana ya tamthilia imekuwapo tangu asili na jadi hata katika jamii zetu za Kiafrika kabla ya athari za kimagharibi kupitia ukoloni. Kwa vile palikuwapo sanaa mbalimbali za maonyesho ambazo humithilishwa na tamthilia. Ntarangwi anafafanua zaidi kuwa, ugeni au tofauti ya tamthilia ya fasihi andishi na sanaa za maonesho za hapo awali upo katika “kugawanya mchezo katika vijishehemu matendo na maonyesho na kumpa kila mhusika sehemu maalum ya kushiriki” (uk. 38).

Kwa jumla, mjadala uliojitokeza kuhusu dhana ya tamthilia unadhihirisha utata uliopo katika kuisawiri sanaa hii pindi uhai wake unapohama kutoka kuandikwa na kusomwa hadi kutendwa jukwaani na kinyume chake. Mjadala wa hoja ya tamthilia unaonesha kuwapo kwa istilahi ambazo mara nyingi zimekuwa zikitumika kama visawe vya neno “tamthilia.” Hivyo, kuhatarisha tathmini ya maendeleo ya tamthilia kwani pana hatari ya mtathmini kuitazama kwa jicho la maendeleo ya filamu na michezo ya jukwaani kama ilivyo kwa sanaa maarufu katika luninga. Mfano *Isidingo the Need, Usalo* na nyingine za Kichina, Kifilipino, Kihindi na Kikorea. Sanaa hizi kwa sasa zimekuwa maarufu sana miongoni mwa watazamaji wa michezo ya jukwaani na filamu nchini Tanzania. Nazo zinatambulishwa na wasomaji kama tamthilia.



Kwa vyovyote vile, watu wasione ajabu hata kwa siku za usoni kuja kushuhudia aina mpya ya sanaa inayopatikana katika runinga na mitandaoni, itakayozalisha aina mpya ya Tamthilia ya Kiswahili. Kihistoria (Ntarangwi, 2004; Samwel, 2013; Mulokozi, 2017), tamthilia imepitia hatua nyingi tangu miviga mpaka kwenye maandishi na kwenye vyombo vya upashanaji habari. Kwani ilikuwapo tangu kale ila siyo katika mfumo tulionao hivi sasa wa upashanaji habari. Pia, wasione ajabu pindi wanapokutana na mbinu mpya za kiutunzi katika Tamthilia ya Kiswahili. Hali hii inatokana na ukaribu wa utanzu huu kwa sanaa za fasihi simulizi na sanaa za maonesho kama alivyowahi kusema Madumulla (2009), Samwel (2013) na Mulokozi (2017). Ukaribu wa utanzu huu na changamoto inayojitokeza katika kuchora mstari wa kutenganisha sanaa za jukwaani na sanaa ya utendaji katika maandishi yaani tamthilia, siyo wa bahati mbaya hata kidogo.

Kihistoria, asili ya tamthilia ni sanaa za maonesho kuanzia mbinu mpaka waasisi wa tamthilia kama sanaa andishi. Kwa hiyo, kwa vyovyote vile, tamthilia kama sanaa andishi imebeba kwa asilimia kubwa sana sura na umbo la sanaa za jukwaani yaani sanaa za maonesho. Kihistoria, “tamthilia” nyingi za kabla na wakati wa awamu ya Azimio la Arusha zilitambwa jukwaani kabla ya kuzalishwa kuwa vitabu (Mulokozi, 2017). Miongoni mwa “tamthilia” hizo ni *Imekwisha* (1951) ya C. Frank, *Afadhali Mchawi* (1957) ya Graham Hyslop, *Nakupenda, Lakini...* (1957) ya Henry Kuria, *Alikiona* (1967) na *Wakati Ukuta* (1967) zote za Ebrahim N. Hussein.

Nyingine ni *Bwana Mkubwa* (1974) ya John Pantaleon Mbonde, *Mwanzo wa Tufani* (1975 / 1976) ya Kulikoyela K. Kahigi na A. A. Ngerema, *Pambo* (1975) ya Penina Mhando, *Heko Kuanzisha Chama* (1977) ya Kung’ala L. Kangula, *Harakati za*

*Ukombozi* (1982) ya Amandina Lihamba, Ndyanao Balisidya na Penina Mhando, na *Ngoswe Penzi Kitovu cha Uzembe* (1988) ya Edwin Semzaba. Hata kwa watunzi nguli wengi wa tamthilia za Kiswahili tunaowafahamu hivi leo, kwa mfano, Amandina Lihamba, Ebrahim N. Hussein, Edwin Semzaba, Emmanuel Mbogo, Ndyanao Balisidya, Ngalimecha Ngahyoma, na Penina Mhando, nao ni zao la taaluma ya sanaa za maonesho.

Pamoja na athari ya sanaa za maonesho katika maendeleo ya “tamthilia” kihistoria, tunaweza kusema kuwa, tamthilia inapaswa kubaki katika vazi la fasihi andishi ili uhai wa sanaa za maonesho ujidhihirishe katika upekee wa mawanda yake kama tulivyoifafanua drama hapo awali. Kuitazama tamthilia kuwa ni fani ya sanaa za maonesho au drama kunaipunguzia hadhi na kuzidi kuiondoa sanaa hii kutoka kuwa utanzu wa fasihi andishi. Hata hivyo, “uhai” wa tamthilia kama sanaa andishi hauwezi kuwa bora na imara, wenye ustawi mpana kisanaa, kama watunzi wa tamthilia watajitenga na sanaa za maonesho. Kwa sababu sanaa za maonesho ni tanuru la kuwasana watunzi wa tamthilia kama ilivyowaibua watunzi nguli wakiwemo Amandina Lihamba, Ebrahim N. Hussein, Edwin Semzaba, Emmanuel Mbogo, Ndyanao Balisidya, Ngalimecha Ngahyoma, Penina Mhando, kutaja kwa uchache.

Pamoja na ukweli huu, hata hivyo, tunalazimika kukubaliana na ukweli kwamba, kifani na kitaaluma pana ugumu katika kuchora mstari halisi ili kutenganisha dhana ya tamthilia na drama; pia tamthilia na sanaa za maonesho. Kwani, kazi zote huumbwa akilini na kuwasilishwa machoni mwa kaumu ya watu kwa njia ya ama maandishi au mdomo. Kwa zama hizi ambazo watunzi wengi ni wasomi na

teknolojia imekuwa kiganjani mwa wengi, siyo rahisi kutunga mchezo na kuachwa kichwani pasipo kuuandika ili watendaji waweze kukariri mswada husika na kuufanyia mazoezi kabla ya kutendwa jukwaani au kurekodiwa katika maandishi ama picha tembezi au sauti. Kwa lengo la kuzalishwa kama kitabu ama filamu au sauti redioni na mtandaoni kupitia wahusika watu au katuni za kutengenezwa kidijitali.

Kwa hiyo hatuna budi kuungana na Eagleton (2008) kukubali kuwa, katika kufasili na kuifafanua dhana, mapokeo na filimbi za utamaduni – jamii ndizo huamua kipi kitambulike vipi, na siyo vinginevyo. Hivyo, kwa mujibu wa utafiti huu, tamthilia imetambulika kama kazi andishi ya kifasihi yenye wahusika watendaji wanaomathilisha maisha ya wanajamii kwa njia ya matendo na mazungumzo. Mazungumzo hayo yanaweza kuwa ya monolojia (mtu binafsi – ya ndani / kujisemesha kama kichaa), ama dailojia (baina ya watu wawili / pande mbili), au poligia / poligi (baina ya watu zaidi ya wawili / pande zaidi ya mbili). Monolojia na poligia / poligi ni mbinu za kisanaa zisizotumika sana katika tamthilia nyingi tunazozishuhudia sokoni. Baadhi ya tamthilia zimetumia mbinu mojawapo au zote mbili japo kwa uchache sana. Katika hizo chache, nyingi zimetumia monolojia kwa uchache kwa mfano tamthilia ya *Pambo* (1975) ya Penina Mhando, *Kivuli Kinaishi* (1990) ya Said Ahmed Mohamed, *Sadaka ya John Okello* (2015) ya Emmanuel Mbogo, na *Utangamano Wetu Ushindi Wetu* (2017/2023) ya Anitha E. Mgimba.

### **2.2.2 Maudhui na Dhamira**

Sengo na Kiango (1973) wanaeleza kuwa maudhui ni sawa na chai katika kikombe ama nyama ya chungwa ndani ya ganda lake. Naye Senkoro (1982) anatumkumbusha

ya kwamba kimsingi, kile kinachoitwa maudhui na mgawanyo wake ni dhana ambazo zipo kwa ajili ya uhakiki pekee lakini kiutunzi maudhui ni umbo moja zima lenye ukamilifu ambalo huwa halimsumbui mwandishi kiubunaji; tofauti na kipengele cha fani. Senkoro (1982) anaongezea kuwa, fani na maudhui ni vitu visivyotenganishika kiutunzi. Wanaovitenganisha ni wahakiki kwa malengo ya uhakiki. Kwa hiyo, siyo busara kuvitenganisha hivi viwili kwa namna nyepesinyepesi tu. Senkoro (1982) anaendelea kusesitiza kuwa, hata kimgawanyo; hakuna mgawanyo sawia uliowahikufanywa na wanataaluma juu ya aina na idadi ya vijenzi vya maudhui.

Ushahidi wa hoja ya Senkoro (1982) tunauona katika maandiko mengi ya wanataaluma wa fasihi. Kwa mfano, Njogu na Chimera (1999) wanasema, maudhui ni mawazo ya mtunzi kwa mkabala na muktadha fulani. Na kwamba, masuala makuu ya utungo yenye kuzaa maudhui ni dhamira, lengo na shabaha vinavyozaliwa baada ya kuunganishwa na mtazamo wa mtunzi na kuhusishwa na muktadha wa utungo. Naye Wamitila (2008) anaongeza mtazamo mwingine kuhusu maudhui. Kwamba, maudhui yanaweza kutazamwa kama “kiwango cha kimaana cha matini au kazi ya fasihi” (uk. 521). Wamitila (2008) anagawa maudhui katika vipengele vya dhamira, itikadi, msimamo, maadili, mafunzo na falsafa.

Tofauti na Wamitila (2008), Madumulla (2009) anagawanya maudhui katika dhamira, ujumbe, falsafa, mtazamo na msimamo. Aidha, kwa mujibu wa Madumulla (2009), dhamira ni “wazo kuu katika kazi ya fasihi. [...] ni sehemu tu ya maudhui. Na, aghalabu, dhamira kuu ndiyo hujenga kiini cha kazi ya fasihi. Dhamira kuu husindikizwa na dhamira ndogondogo. Wazo kuu hubeba funzo kuu” (uk. 123).

Wakati Njogu na Chimerah (1999) wanasema maudhui ni mawazo ya mtunzi, Madumulla anaelezea mawazo aghalabu wazo kuu ni dhamira. Na, Madumulla anakiri kuwapo kwa mawazo madogo ambayo ni sehemu ya dhamira ambayo ameita dhamira ndogondogo. Huu ni ushahidi wa kuwapo utata katika kutenganisha dhana ya dhamira kutoka katika maudhui.

Changamoto ya fasili kati ya maudhui na dhamira inaonekana kujitokeza hata kwa Samwel (2013). Samwel (2013) anataja vipengele vya maudhui kuwa ni migogoro, masuluhisho, fundisho, dhamira, ujumbe, falsafa na msimamo. Samwel (2013) anaelimisha kuwa “maudhui ni umbo la ndani la kazi ya fasihi. Maudhui ni mawazo yanayojitokeza katika kazi ya fasihi. Ni jumla ya mambo yote yanayobebwa na kazi husika ya kifasihi. Maudhui hujumuisha dhamira, ujumbe, migogoro, masuluhisho, falsafa, fundisho na msimamo” (uk. 126). Kwa upande wa dhamira, Samwel (2013) ana haya ya kusema:-

Dhamira ni mada, lengo, kusudi, wazo kuu linalozungumzwa na [...] kazi ya sanaa. [...] huweza kuwa na dhamira za kisiasa, kiuchumi, kijamii na hata kiutamaduni. Mifano ya baadhi ya dhamira zinazoonekana [...] ni pamoja na uongozi bora, mapenzi, dini, ndoa, elimu, kazi na ukombozi. Dhamira hizi huweza kuelezwa kwamba mwandishi anakusudia kuielimisha jamii juu ya dhana na sifa za kiongozi bora, kuionya jamii juu ya madhara ya mapenzi shuleni, kuielekeza jamii juu ya umuhimu wa dini katika jamii, kuiasa jamii kuwa na uaminifu katika ndoa na kadhalika. (uk. 126).

Nukuu hii inaonesha kuwapo kwa mkanganyiko katika kuchora mstari baina ya maudhui na dhamira. Kwa mfano, Samwel anarejelea “wazo” kama utambuzi wa dhana ya dhamira ilhali katika kufasili maudhui amerejea istilahi “wazo (mawazo)”

kufafanua dhana ya maudhui. Nao Njogu na Chimerah (1999) wanatambulisha dhamira, lengo na shabaha kama masuala makuu ya utungo yenye kuzaa maudhui. Hii inamaanisha kuwa, dhamira, lengo na shabaha ni vijenzi tofauti vya kisanaa wakati lengo na shabaha kwa Samwel ndiyo dhamira yenyewe hasa.

Naye Mulokozi (2017) amegawa maudhui kwa kigezo cha nyanja kuu za maisha ambazo ni maudhui ya kisiasa, maudhui ya kiuchumi, maudhui ya kijamii, na maudhui ya kiutamaduni. Mgawanyo huu uligusiwa hata na Samwel (2013) anayesema dhamira zinaweza kuwa “[...] za kisiasa, kiuchumi, kijamii na hata kiutamaduni” (uk. 126). Mgawanyo huu unatupatia picha kwamba, hakuna namna moja ya kuweza kuyachambua maudhui kwa misingi ya kuyavunjavunja pasipo kuibua swali la kimantiki. Pamoja na ukweli kwamba wanataaluma hawa wameonesha kuwa maudhui na dhamira ni dhana tofauti, lakini kimatumizi, baadhi ya wanafasihi wakiwemo wanataaluma hawa huzitazama dhana hizi mbili kama vitu vinavyofungamana kimantiki na kimatumizi. Yaani, maudhui hutazamwa kuwa ni dhana inayotumika kurejelea wazo kuu au mawazo madogo yanayojitokeza katika kazi ya kifasihi; sawa na ufafanuzi uliozoeleka miongoni mwa wanataaluma wengi pindi wanapofasili dhana ya dhamira. Hii ndiyo sababu waandishi na watafiti wengi wanapotaja mifano ya maudhui bila kutamka mipaka ya istilahi hii kimatumizi, huishia kurejelea dhamira bila kugusa vipengele vingine vya maudhui. Ni kana kwamba, istilahi maudhui na dhamira ni visawe sawa vya neno moja.

Hata hivyo, tunafahamu ya kwamba, maudhui ni sawa na jengo lenye vyumba kadhaa vilivyopewa utambuzi na majukumu mahususi. Chumba kimojawapo kimepewa utambuzi kwa kuitwa dhamira. Kwa hiyo hapa tunasema, maudhui na

dhamira ni vitu viwili tofauti vyenye kukamilishana. Kwa minajili ya andiko hili, dhamira tuliichukulia kuwa ni wazo ama mawazo au mambo yanayobebwa katika kazi bunilizi ikiwemo Tamthilia ya Kiswahili ili kuwasilisha ujumbe, falsafa, itikadi, propaganda, msimamo na mtazamo wa mwandishi na, au jamii iliyoizaa kazi husika.

Ili mhakiki aweze kuchambua maudhui hususani dhamira katika matini ya kifasihi hana budi kuongozwa na maswali yafuatayo kama anavyotanabaisha Senkoro (1982): - (i) Je, msanii anatueleza nini? (ii) Je, msanii ameandika kazi yake akilenga mtu wa tabaka gani? (iii) Je, kuna utukuzaji? Kama ndiyo, anamtukuza nani na kwani nini? (iv) Je, kuna ubezaji? Anambeza nani na kwa nini? (iv) Je, kuna matatizo yanayojitokeza? Je, msanii anapendekeza njia ya kuyasuluhisha matatizo hayo? Na, (vi) Je, ni migogoro ipi inayojitokeza? Ya kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni, ya kibinafsi (kimawazo, kifalsafa, kihali)? Ingawa pendekezo la Senkoro limetumia dhana maudhui yenye kuhusisha vipengele vingi vya maudhui kikiwemo dhamira, bado mtafiti aliona fomula hii ni msaada mkubwa katika kuongoza uchunguzi wetu katika tamthilia teule. Kwa sababu kwa upande mwingine, maswali haya yanafungamana vema na mawanda ya nadharia ya Fasihi Linganishi iliyoongoza utafiti.

### **2.2.3 Matumizi ya Lugha**

Mnyampala (1990) anaamini kwamba matumizi ya lugha katika kazi ya kubuni yapo ili kuleta athari kwa msomaji na mtazamaji au msikilizaji wa kazi ya kubuni. Hii ni kutokana na ukweli kwamba, hakuna kazi inayoshushwa kutoka mbinguni. Bali hubuniwa kutokana na matukio yaliyotokea au yanayoendelea kutokea katika jamii. Kwa hiyo, mbunifu huyavika lugha ya kisanaa matukio hayo ili yaoneshe upya;

tofauti na yalivyotokea katika uhalisi wake. Kwa hiyo, kinachofanya matukio machoni na hisiani mwa msomaji, mtazamaji na msikilizaji kuwa na mvuto ni weledi wa mtunzi katika kuteua na kujenga kwa weledi bunifu lugha ya kisanaa katika kazi husika.

Naye Senyamanza (h. m.) anatumia ya kwamba, matumizi ya lugha ni mojawapo ya mambo yanayoitofautisha kazi ya kubuni na ile isiyo ya kubuni. Senyamanza (h. m.) anasema, katika uga wa fasihi, mtunzi huwa na lugha yake ndani ya ubunifu wake. Kwa maana hiyo, jinsi mtunzi wa kazi ya fasihi anavyotumia lugha yake na kiwango cha ubunifu anachofikia, ndiyo alama muhimu inayomtofautisha na wabunifu wengine. Senyamanza (h. m.) anaendelea kufafanua kuwa, ubunifu hujitokeza katika uteuzi na matumizi ya tamathali za semi, misemo, nahau, methali, lugha za wahusika - hasa lahaja zao, uchaguzi wa msamiati na miundo ya sentensi. Pia, ubunifu wa lugha hujitokeza katika ufundi wa kuteua na kuumba wahusika, miktadha, mandhari na matukio. Na, utamu wa lugha yenyewe itumiwayo hujidhihirisha kupitia maumbo yaliyoubwa kwa kunatishwa vizuri. Aidha, Senyamanza (h. m.) anasisitiza kuwa, weledi wa mtunzi katika kuumba lugha kuna maana pana sana kisanaa. Kwa sababu mwandishi katika uga wa fasihi anategemea matumizi maalumu ya lugha katika kuliumba na kuliwasilisha jambo alilolikusudia kuliwasilisha kwa jamii. Ubunifu wa mtunzi katika kuifumbata lugha, huifanya lugha husika ama iwe na mvuto ama ichushe hadhira.

Maelezo ya Mnyampala (1990) na Senyamanza (h. m.) yalitusaidia kuweza kuitazama thamani na nafasi ya matumizi ya lugha katika kuwasilisha dhamira za kazi ya kifasihi. Uchaguzi mzuri na sahihi wa matumizi ya lugha unaifanya kazi ya



kifasihi kuwa na ushawishi wenye muwashawasha pindi msomaji au msikilizaji anapoisoma au kuisikiliza. Uchaguzi mzuri unatokana na ubunifu na uhodari katika kutumia na kuitawala lugha tumizi. Kinyume chake, kazi ya kifasihi itakuwa chapwa tena yenye kuchusha na isiyo na mvuto fikrani, machoni na masikioni mwa msomaji, mtazamaji na msikilizaji. Ufafanuzi wenye mrengo kama wa wanataaluma hawa wawili unaonekana kujitokeza hata kwa wanataaluma wengine, mathalani Grenville (2001), Hussein (2003), Mlama (2003) na Madumulla (2009). Wote hawa wanakubali kuwa, lugha ni nguzo muhimu yenye kubeba utambulisho wa ubunifu au uchapwa wa mwandishi kiutunzi.

Katika kuhakiki tamthilia, Samwel (2013) anatusisitiza kuchunguza na kubaini kama lugha iliyotumika ni ya Kiswahili ama la. Kama ni Kiswahili, ni kwa asilimia 100 ama mwandishi amechanganya ndimi. Na, kama lugha hiyo ni fasaha, sanifu au ni ya vijiwani. Vilevile, Samwel (2013) anaongeza kwamba, mhakiki hana budi kuyatazama kwa makini matumizi ya lugha ya picha, ishara, ucheshi, mtambaji, ngano na taswira. Kwa maelezo haya ya Samwel (2013), ni dhahiri kwamba matumizi ya lugha ya kisanaa ni uwanja mpana wenye utajiri mkubwa wa vionjo vyenye kumfanya mtu anayejihusisha nayo kuwa mweledi wa kiwango cha juu mbali na kuwa mwenyeji wa lugha anayoitumikia.

Kwa hiyo, kwa mustakabali wa utafiti huu, mtafiti hakuwa budi kuvitalii vipengele vinne (4) pekee vya matumizi ya lugha vilivyoshughulikiwa katika tamthilia sita (6) teule. Vipengele hivyo ni lugha ya ucheshi, misimu, matumizi ya uchanganyaji ndimi na uwepesi na ugumu wa lugha iliyotumika katika tamthilia teule (rej. kipengele cha

1.7 Mipaka ya Utafiti - kwa ufafanuzi zaidi). Vipengele hivi vinne (4) vya lugha vimefafanuliwa katika sehemu zinazofuata:

### **2.2.3.1 Lugha ya Ucheshi**

Gurdjieff (1963) kama alivyonukuliwa katika Wamitila (2008) anasema kuwa, siyo rahisi kueleza vizuri dhana ya uchezi na asili yake pasipo kubakiza swali. Hata hivyo, Gurdjieff (1963) anafafanua kuwa, ucheshi kwa Wanabaolojia ni tokeo la mwili wa binadamu kuitikia vichocheo vya msisimko wa furaha na raha vinavyozalishwa na homoni mahususi kwa kazi hiyo tu ndani ya mwili. Hivyo, mtu anaweza kuafiki kuwa, ucheshi ni tokeo la msisimko, mkataano wa fikra, bubujiko la furaha na raha, ukubalifu na kujiamini kunakomtokea mwanadamu kwa kujua au kutokujua.

Katika kuidadavua lugha ya ucheshi ili iweze kueleweka kinadharia, Provine (1996) amebainisha nadharia tatu (3) za ucheshi. Nadharia hizo ni nadharia ya burudiko (*relief theory*), nadharia ya mkwezo (*superiority theory*) na nadharia ya msigano (*incongruity theory*). Provine anafafanua kuwa, nadharia ya burudiko inautazama ucheshi katika umbo la kicheko kinachotokea kama njia ya kupumua sumu na msongamano wa mawazo uliojaa akilini mwa binadamu. Nayo nadharia ya mkwezo inadai kicheko cha ucheshi hutokea pale mtu anapojihisi kujawa na raha hata kama anasongwasongwa na changamoto kadha wa kadha. Ucheshi huu hujiumba ndani ya mtu kiasi cha kumfanya ajione kuwa ni mwenye hadhi ya juu, aliyejitosheleza ama kuridhika kwa nafsi. Ijapokuwa, mara baada ya furaha kuisha hujikuta akiyarudia matatizo yake aliyojitenga nayo kwa muda. Pia, nadharia ya msigano, inasisitiza kwamba, kicheko hutokea mara tu mawazo yetu yanapokataa kuafiki neno, kitu, hali

au jambo lililotendwa baada ya kubaini kuwa liko kinyume au tofauti na lilivyopaswa kuwa.

Ucheshi unaweza kugawanyika katika aina kadhaa kutegemeana na vigezo wazi na funge vya mwainishaji. Mathalani, Wamitila (2008) amebainisha aina tano (5) za ucheshi ambazo ni: ucheshi wa kimazungumzo, ucheshi wa kitanzia, ucheshi wa ujibeuzi, ucheshi wa kimwingilianomatini na ucheshi wa kibwege. Naye Senyamanza (h. m.) anazo aina tano (5) za ucheshi ambazo ni: ucheshi wa kibeuzi, ucheshi wa kitanzia, ucheshi wa kimazungumzo, ucheshi wa kimwingiliano na ucheshi zimbwe.

Baadhi ya aina za ucheshi zilizobainishwa na Wamitila (2008) na Senyamanza (h. m.), zinaonekana kuwa tofauti. Hata hivyo, ukisoma ufafanuzi wa kila mmoja, unagundua istilahi walizotumia ndiyo tofauti lakini ufafanuzi juu ya dhana husika zinakupatia picha kwamba ni kitu kilekile. Istilahi hizo ni “ujibeuzi” (kutoka kwa Wamitila) na “kibeuzi” (kutoka kwa Senyamanza) ni sawa. Vivyo hivyo kwa “kibwege” (kutoka Wamitila) na “zimbwe” (kutoka kwa Senyamanza) nayo ufafanuzi wake hautofautiani. Huku ndiko kusema, waandishi hawa wametofautiana kiistilahi lakini ufafanuzi wao unarejelea dhana zilezile. Ufuatao ni muhtasari wa aina hizo za ucheshi kama zilivyofafanuliwa na Wamitila (2008) na Senyamanza (h. m.): -

- i. Ucheshi wa kibeuzi. Huu unatokana na ubinafsi wa mhusika mwenyewe kujikinai, kujidhihaki, kujitweza au kujiumiza kutokana na tendo, kauli, neno, tamko au mchoro wake ambao humchokonoa yeye mwenyewe hadi akajikuta akicheka pasipo kutarajia. Kicheko hiki hutokea baada ya mhusika kutambua

ya kwamba kauli au tendo alilolifanya ni la kijinga au kizembe. Kwani, kiuhalisi asingeweza kulitamka au kulitenda kwa namna ile endapo angekuwa ametuliza akili na kutafakari kama mtu mwenye akili na utambuzi timamu kabla ya kuchukua uamuzi alioufanya.

- ii. Ucheshi wa kitanzia: Huu hutokea pale ambapo tukio la kuhuzunisha hujengewa taswira ya mhusika kutenda jambo au kutamka neno kama mtu asiyejitambua wala kuchuja. Lakini, mwenyewe akiamini kwamba anachokifanya au kukisema ni sahihi na chenye kukubalika kiasi cha kumjengea heshima. Mhusika huyo huyatenda au kuyanena mambo bila kutambua wale wanaomtazama wanamshangaa na kumsikitikia. Ijapokuwa, matendo yake huwachochea watazamaji kumdharau na kuishia kumcheka au kumsifu kwa ghiribu.
- iii. Ucheshi wa kimazungumzo: Huu huzaliwa pale tu wahusika wa kifasihi wanapotumia dailojia yenye kauli zinazoamsha hisia za furaha, raha na vicheko katika muktadha mahususi.
- iv. Ucheshi wa kimwingiliano: Huu unatokana na kazi ya kifasihi kuchopeka ndani yake usemi, mchoro, simulizi, vionjo, sanaa, wazo, tukio au fikira fulani ambayo msomaji ama msikilizaji au mtazamaji anafahamu na kutambua chanzo cha matini yaliyochopekwa. Kitendo hiki cha kuyang'amua matini chanzi humfanya msomaji ama msikilizaji au mtazamaji ajione kuwa ni mtu makini, mwerevu na mjanja kumshinda ama kuwa na hadhi sawa au zaidi ya mtunzi aliyeyatumia matini husika. Hivyo, mhusika kuishia kucheka na kujihisi mwenye raha sana.

- v. Ucheshi zimbwe (au kibwege): Huu ni ucheshi unaowakutanisha wahusika wenye viwango tofauti vya uelewa, ustaarabu na stadi zinazotokana na ujuzi na maarifa ya kitaaluma. Hivyo, mhusika mmoja aghalabu mwenye mamlaka hutenda na kunena kwa usahihi na ustaarabu kutokana na weledi wa kitaaluma. Wakati huo, mhusika wa pili hutenda na kunena kwa wasiwasi, hofu, mashaka, mkanganyiko, makosa na kuonekana kuwa mgeni wa mambo mengi. Hii ni kutokana na kutokuwa na tajiriba, ujuzi, stadi na maarifa yanayoumbwa kupitia taaluma husika. Lengo la ucheshi wa namna hii ni kuchochea fikra, mawazo, uwazaji na tathmini ambayo ni ya kitaaluma (Wamitila, 2008).

Faukwa ya hayo, ucheshi una mchango mkubwa katika kumshawishi msomaji kupenda kufuatilia simulizi husika (Gurdjieff, 1963 katika Wamitila, 2008). Kwa hiyo matumizi ya ucheshi kwa kiwango cha kutosha kunaweza kuwasogeza jirani zaidi wasomaji kwa kiwango cha kuifanya Tamthilia ya Kiswahili iweze kukua na kustawi zaidi. Ili kurahisisha uchunguzi, utafiti huu uliongozwa na muhtasari wa aina za ucheshi zilizobainishwa na Wamitila (2008) na Senyamanza (h. m.). Nazo ni: ucheshi wa kibeuzi, ucheshi wa kitanzia, ucheshi wa kimazungumzo, ucheshi wa kimwingiliano na ucheshi zimbwe. Kwa mujibu wa Senkoro (2011), ucheshi ni mbinu ambayo wasanii huitumia katika kazi zao za kifasihi kuzichekesha hadhira zao, au walau kuzifanya hadhira hizo zitabasamu. Na kwamba, dhima ya ucheshi huo ni kuwafurahisha wasomaji, wasikilizaji au watazamaji. Pia, dhima nyingine ya ucheshi ni kuiondolea uchovu hadhira na kujenga kejeli.

Hivyo basi, katika utafiti huu utambuizi na mjadala wa aina za ucheshi ulimsaidia mtafiti kuweza kuzichunguza tamthilia teule ili kubaini kama kuna ucheshi ama la. Kama upo, basi ni wa aina gani? Kwa kiwango gani? unajitokeza vipi? na kwa sababu gani umejitokeza hivyo? Maswali haya yalitusaidia katika kupata maarifa ya kubaini kama mtunzi amezingatia ubunifu katika uteuzi na uumbaji wa dhamira ama la. Kwa maana kuwa, kisanaa hii ni njia mojawapo yenye kumfanya msomaji aendelee kuzitafuta kwa shauku tamthilia za Kiswahili.

### **2.2.3.2 Misimu**

Misimu hujulikana pia kama simo (Masebo na Nyangwine, 2016; Mulokozi, 2017). Semi hizi hujipambanua kama semi za muda na mahali maalumu zinazozuka na kutoweka kulingana na mazingira mahususi. Misimu husika ikitumiwa mara nyingi na kwa muda mrefu huzoeleka na hatimaye husanifiwa hata kugeuka msamiati, methali au vitendawili rasmi (Samwel, 2013). Misimu inaweza kuwa ni neno jipya au kauli mpya iliyoundwa na mtu au kundi fulani la watu linalojulikana au lisilojulikana. Pia, misimu inaweza kuwa ni neno au kauli iliyopo katika jamii lakini ikatanuliwa maana. Maana hiyo mpya huvuma na kuonekana kupata msisitizo na msisimko wa kipekee kiutumizi katika kipindi husika (John na Mduda, 2014). Kuzuka kwa misimu huendana na wakati, mazingira na tukio. Hivyo, semi hizi hutusaidia kutambua historia za jamii katika vipindi tofauti tofauti vya uhai wa maisha ya jamii husika (Mulokozi, 2017).

Misimu imegawanyika katika aina kadhaa kutegemeana na uainishaji uliofanywa na mtaalamu husika (Masebo na Nyangwine, 2016). Mathalani, Masebo na Nyangwine wanabainisha vigezo na aina za misimu kwa kila kigezo. Masebo na Nyangwine

(2016) wanaeleza kwamba, (i) kwa kigezo cha mada tunapata misimu inayohusiana na pesa, majina ya vyakula, ulevini, nguo, usafiri, na misimu inayohusiana na wanawake. Pia, (ii) kwa kuzingatia kigezo cha makundi ya watu wanaotumia lugha; tunapata misimu ya wanafunzi, misimu ya wafanyabiashara, misimu ya majangili, misimu ya majambazi, misimu ya wanamichezo, misimu ya walanguzi, na kadhalika.

Masebo na Nyangwine (2016) wanaongeza kusema, (iii) kwa kigezo cha jumla au kawaida; tunapata: (a) misimu ya pekee ambayo huwa na eneo dogo kiutumizi kwa kulenga kundi dogo sana. Tena maneno yake huwa ni siri miongoni mwa watumiaji. (b) Misimu ya kitarafa ambayo huwa na eneo pana kiasi kimatumizi kwa kuhusisha tamaduni changamani, jografia na historia pana kiasi kuliko misimu ya pekee. Na, (c) misimu zagao ambayo hutambulika pia kama misimu ya kitaifa / kikanda / kimataifa. Misimu hii huvuka mipaka ya nchi, hutumika hata katika maandiko na kusanifishwa kuwa lugha rasmi.

Misimu hujitokeza sana katika lugha za mitaani kwa sababu kundi kubwa kwa uzalishaji na utumiaji misimu ni vijana huko mtaani kuliko ofisini (Reuster-Jahn na Kiebling, 2006). Misimu hii huwa na lengo la kurahisisha mawasiliano baina ya wazungumzaji. Lakini huweza kufanya kazi kama misemo, mafumbo na ishara miongoni mwa wahusika wake kama njia ya kutunza siri (Malima, 2018). Matumizi na maana ya neno ambalo ni msimu haitegemei uwezo au kiwango cha elimu ya darasani bali mazingira na mahusiano ya watumia lugha ya misimu husika. Ndiyo maana ni kawaida kuwakuta watu wa rika zote, hadhi fulani, viwango tofauti vya elimu, imani na mapokeo wakitumia na kuzalisha misimu. Hali hii hujitokeza kwa sababu ya kuwapo kwa shughuli maalumu na mahususi zinazowaunganisha kitabia

na kimawasiliano (Reuster-Jahn na Kiebling, 2006; Malima, 2018). Mifano ya misimu ni: mkukuta, kilimo kwanza, chai ma'rage, safari ya matumaini, ukawa, ukitaka kuliwa sharti nawe uliwe, pupuchi, kutumbua na chukua chako mapema.

Inasadikiwa ya kwamba, idadi kubwa ya misimu huzalishwa na vijana wahuni hasa wasio na kazi maalumu na watumiaji wa dawa za kulevya (Malima, 2018). Kwa zama hizi, mitandao ya kijamii ndiyo inayoonekana kuwa kitovu cha kuzalisha misimu (Timothy, 2016; Malima, 2018). Tafiti zilizofanywa na Mohamed (2013), Kipacha (2014) na Malima (2018) zinaonesha kuwapo kwa matumizi makubwa ya misimu miongoni mwa watumiaji wa lugha ya Kiswahili. Idadi kubwa ya misimu hiyo huishia katika ngazi ya makundi mahususi ya watumiaji lugha. Ndiyo maana hakuna utajiri mkubwa wa misimu inayofahamika miongoni mwa watumiaji lugha ya Kiswahili - kama kundi maslahi moja kubwa la kijamii. Kwa sababu misimu mingi huishia katika vikundi maslahi badala ya kundi maslahi moja kubwa la kitaifa au kijamii.

Hali hii inatokana na ukweli kuwa, aina hii ya maneno huzuka ghafla katika kipindi na tukio mahususi linalohusiana na kikundi kidogo cha watumia lugha wenye maslahi maalumu. Kisha, maneno hayo kwa kiasi kikubwa hupotea ghafla pasipo kujulikana miongoni mwa jamii kubwa zaidi (King'ei, 2010; Malima, 2018). Hivyo, kwa mtu asiyejua historia na mahusiano ya jamii na lugha yake, pia etimolojia ya maneno, kamwe hawezi kubaini neno lipi ni msimu na lipi siyo msimu na humaanisha nini.

Mtafiti anayechunguza misimu hana budi kuichunguza jamii na lugha yake, kihistoria. Kinyume na hapo atajikuta akipata shida kubaini misimu iliyoibuka nje ya



wigo wa utambuzi wake yeye kama mtafiti. Kwa kuzingatia jambo hili mtafiti alisoma maandiko na kufuatilia vyanzo mbalimbali vya upashanaji habari mfano mazungumzo ya kihistoria na wasifu wa watu, pia kusikiliza mazungumzo ya watu katika redio, TV, mitandao ya kijamii na ana kwa ana ili kubaini misimu ya awamu ya Azimio la Arusha na ile ya awamu ya soko huria. Kwa njia hii, mtafiti hakupata ugumu sana kubaini misimu ya kila awamu iliyotumika katika tamthilia zote sita (6) teule.

### **2.2.3.3 Uchanganyaji Ndimi**

Hii ni mbinu mojawapo katika matumizi ya lugha ambapo mtunzi hutumia lugha zaidi ya moja katika kutambulisha mhusika, wazo, muktadha na ulumbi katika kazi yake. Uchanganyaji ndimi unaweza kuwa ni matamshi yenye athari ya lugha mama, matumizi ya Kiswahili na lahaja, matumizi yasiyo sanifu ya miundo au kauli katika lugha ya Kiswahili. Pia, uchanganyaji ndimi unaweza kutokana na matumizi ya ubadilishaji au uchanganyaji misimbo katika lugha ya Kiswahili na kadhalika (Muysken, 2000). Muysken (2000) anaongeza kwa kusema, uchanganyaji ndimi unaweza kujitokeza kuanzia ngazi ya neno mpaka ngazi ya kauli na idadi yake siyo sahili. Kwa mfano, “*nitaku-call*” badala ya “*nitakupigia (simu)*” - kwa ngazi ya neno. Katika ngazi ya vikundi vya maneno, mfano wake ni “*you* na Juma...” Kwa ngazi ya kishazi, mfano ni “*when I come*, nitakueleza kila kitu.” Kwa ngazi ya sentensi, mfano ni “*don't worry, I will be there before 2 o'clock. Kwa hiyo, usijali tafadhali.*”

Romaine (1995) na Muysken (2000) wanabainisha sababu nne (4) zinazowafanya watu kuchanganya ndimi. Sababu ya kwanza ni hali ya athari ya ulevi unaoifanya akili ichangamke kwa kiasi cha mzungumzaji kujisikia raha kuzungumza maneno ya

luga zaidi ya moja. Sababu ya pili ni athari ya ukoloni na elimu rasmi kwa jamii zetu. Sababu ya tatu ni uchanganyaji ndimi huwavutia sana watu wanaopenda kuchanganya ndimi, iwe wanajua au hawajui kile kinachotoka kinywani. Na, sababu ya nne, uchanganyaji ndimi ni zao la wazungumzaji au mzungumzaji kushindwa kumudu lugha husika kwa kiwango cha kuweza kuongea au kuzungumza bila shida yoyote ile ya kimilisi.

Nao Wibowo na wenzake (2017) wanasema, uchanganyaji ndimi hufanyika siyo kwa bahati mbaya, bali kwa sababu mahususi. Zikiwemo: - (i) wazungumzaji kuonesha umilisi wao katika kumudu lugha zaidi ya moja, (ii) kutaka kuficha jambo ambalo wazungumzaji katika kikundi hawapendi mtu asiyekuwa sehemu ya mazungumzo kutambua kinachosemwa. Pia, (iii) kuonesha athari ya lugha mama katika lugha ya pili au zaidi, na (iv) kujivunia utamaduni wao wa asili kupitia lugha.

Kwa mujibu wa Wanaisimu, Wanasosholojia na Wanasaikolojia, hali ya watu kutumia lugha zaidi ya moja katika mazungumzo inazidi kupata nguvu na kasi katika jamii zenye mwingiliano mkubwa wa jamii lugha zaidi ya moja (Reuster-Jahn na Kiebling, 2006). Reuster-Jahn na Kiebling (2006) wanaonesha kuwa; kisaikolojia na kisosholojia, watumiaji wa misimbo isiyorasmi hujisikia huru zaidi kuwasiliana kuliko kutumia lugha rasmi wanayohisi inawanyima uhuru. Aidha, kuna wachanganyaji ndimi wengine au wasikilizaji wanaamini hali hii ni sehemu ya maendeleo, utoshelevu wa msamiati na mbinu ya kimawasiliano katika lugha za kigeni kuliko katika lugha mama zao.

Mfano mzuri ni nchini Kenya ambako kuna “lahaja” iliyozaliwa kutokana na uchanganyaji ndimi uliokubuhu. “Lahaja” hiyo inajulikana kama Sheng ambapo

inatajwa kuathiri kwa kasi ustawi wa lugha rasmi ikiwemo lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Tafiti zinaonesha watumiaji wa Sheng huchomeka maneno mengi yenye kubeba muunganiko wa maneno au sentensi kutoka lugha tofauti tofauti ikiwemo lugha ya Kiswahili na Kiingereza (Momanyi, 2009; Kioko, 2017). Momanyi (2009) na Kioko (2017) wanakiri kwamba, athari ya Sheng miongoni mwa watumiaji wa lugha ya Kiswahili au Kiingereza ni kubwa mno kimawasiliano na kitaaluma kwa zama hizi.

Katika Tanzania, kutokana na changamoto ya kutumia lugha ya Kiingereza, mbali na sababu nyinginezo, inatajwa kuwa muda mwingi wa wanafunzi na walimu wa shule za sekondari na vyuo, hutumia Kiswahili badala ya Kiingereza. Wanapotakiwa kutumia Kiingereza, wengi wao hujikuta wakichanganya ndimi (Roy-Campbell na Qorro, 1997). Hali inayotajwa kusababisha kuibuka kwa kile kinachoitwa *Kiswanglishi* ndani na nje ya darasa. Kama tulivyoona awali, uchanganyaji ndimi unatokana na sababu tofauti tofauti. Nao unapendwa na watu tofauti tofauti kwa minajili tofauti tofauti miongoni mwa watumiaji wa lugha. Kwa hiyo, kisanaa, mwandishi naye hulazimika kubuni lugha inayogusa mahitaji ya watumiaji wa lugha kwa viwango na sababu mahususi.

Kwa mantiki hii, kisanaa; uchanganyaji ndimi ni mbinu mojawapo katika kazi bunilizi ikiwemo tamthilia. Mbinu hii ina athari kubwa kwa wasomaji wa matini bunilizi husika. Maarifa kuhusu mbinu ya uchanganyaji ndimi ulitusaidia kutanua mawanda yetu ya ufahamu. Maarifa yaliyopatikana yalimsaidia mtafiti katika kuchunguza aina, kiwango na nafasi ya uchanganyaji ndimi katika tamthilia sita (6) teule ili kung'amua ubunifu na athari yake kiutunzi miongoni mwa wasomaji.

#### **2.2.3.4 Uwepesi na Ugumu wa Lugha katika Kazi Bunilizi**

Shklovsky (1966) anaeleza ya kwamba lugha ya kifasihi ni sharti ionekane kuwa mpya daima machoni na masikioni mwa wasomaji na wasikilizaji. Kwa sababu, lugha ya kifasihi ikizoeleka sana miongoni mwa wasomaji basi hugeuka chapwa. Halafu kazi husika hupoteza mvuto mbele ya wasomaji. Kwa hiyo basi, ili kazi ya kifasihi izidi kukubalika na kutamanika machoni pa wasomaji haina budi kuwa na ubunifu wa hali ya juu. Shklovsky anaendelea kusema, mbinu inayoifanya kazi ya kifasihi kuwa mpya daima ni matumizi ya lugha ngumu hasa ya mficho na matumizi ya mbinu ya ukengeushi usiokuwa wa kawaida (uchomozi / uajinabishaji).

Kwa Wanauumbuji wa Kirusi, mathalani Roman Jacobson, kazi ya kifasihi ni sharti imfikirishe na kumkomaza msomaji kifikra, kimaono, kimtazamo na kimakuzi (Mushengyezi, 2003). Lugha hiyo kwa sehemu kubwa itahitaji zaidi ujenzi bora wa taswira. Fasihi inapotumia taswira kwa sehemu kubwa, hujikuta ikihukumiwa kama sanaa ngumu. Ugumu wa lugha unaweza kumkuta mtu yeyote yule ambaye siyo mmaizi wa lugha husika. Hii ina maana kuwa, hata kama wewe ni Mswahili, lakini u masikini wa msamiati wa Kiswahili, masikini wa semi za Kiswahili na masikini wa utamaduni wa Mswahili, unaweza kukutana na kazi ya Kiswahili iliyotumia lugha ya Kiswahili ambayo msamiati, semi na utamaduni uliomo hujauzoea hadi ukabaki kuduwa kama siyo kushindwa kupata maana ya kile kilichosemwa.

Zipo sababu tofauti tofauti za kwa nini watunzi hutumia lugha ngumu. Jilala (2012) anatueleza kuwa baadhi ya waandishi hulazimika kutumia lugha ngumu si kwa lengo la kuichosha ama kuitenga jamii ya wasomaji au kuonesha ukomavu wao kiubunifu. Bali hufanya hivi ili kukwepa mkono wa chuma wa tabaka tawala ambalo hupenda

kusikia mazuri pekee. Kwa hiyo anachokieleza Jilala, ni kwamba mwandishi akitumia lugha nyepesi katika kulikosoa tabaka lisilopenda kukosolewa, basi hana budi kutambua kwamba, anahatarisha kesho yake – kiuandishi na kiuhai. Kwa hali hii, mwandishi atalazimika kukimbiza mbawa zake kwa kutumia lugha ngumu kama kinga ya pumzi yake kiuandishi na kiuhai.

Faukwa na hilo, ugumu wa lugha unaweza kutokana na matumizi makubwa ya lugha ya picha au maneno ambayo hayajazoeleka masikioni na machoni mwa msomaji husika – kwa makusudi au kwa bahati mbaya. Lakini kwa anayeyajua maneno husika au ni mmaizi katika kupasua sitiara, kazi hiyo haitaonekana kuwa na matumizi ya lugha ngumu bali lugha rahisi (Senkoro, 2007). Aidha, lugha ya kifasihi ni lazima iwe ngumu na kamwe isizoeleke kwa wasomaji maana endapo ikizoeleka basi upya wa kazi ya kifasihi hufa hivyo kukosa ushawishi kwa walaji. Wanauumbuji wa Kirusi, mathalani Roman Jacobson huiona kazi inayotumia lugha nyepesi kuwa ni kazi isiyokuwa ya kifasihi. Na endapo kazi hiyo italazimishwa kuingizwa katika kundi la kazi za kifasihi basi kazi hiyo haina budi kuhesabika kuwa ni fasihi ya watoto na wanawake kwani haiwakomazi wasomaji kifikra na kintazamo (Mushengyezi, 2003).

Kwa mantiki hiyo, wepesi na ugumu wa lugha ni suala la kiujumi zaidi ambalo haliwezi kujadilika kwa urahisi. Kwa sababu, kile unachokiona kuwa ni chepesi, bila shaka mwingine atasema kwake ni kigumu! Changamoto hii katika kubaini mipaka ya wepesi na ugumu wa jambo ni suala la kihisia tu sawa na kutafuta mpaka dhahiri kati ya uzuri na ubaya (Eagleton, 2008). Hivyo basi, wepesi na ugumu katika kulitazama jambo huamriwa na tajiriba na mapokeo yanayoimiliki jamii husika na si

vinginevyo. Hata hivyo, hatuwezi kuhitimisha mjadala huu kwa hoja kwamba, hakuna uwezekano wa kuweka vigezo vya kutambua wepesi na ugumu wa lugha iliyotumika katika kazi ya kifasihi.

Kwa mujibu wa utafiti huu, wepesi wa lugha ya kifasihi ulihitimishwa kwa kuwapo katika tamthilia sita (6) teule pale tu tamthilia hizo zilithibitika kuwa hazijatumia ama zimetumia kwa uchache lugha ya uficho. Mathalani, sitiari, tashihisi, tafsida, mafumbo, uchanganyaji ndimi (kwa wasioijua lugha ya pili) na misimu isiyokuwa ya kitaifa. Pili, pale ambapo tamthilia teule ilibainika kutumia aina tajwa ya semi (hata kama ni kwa kiwango cha juu) lakini kauli zilizotumika kuwakilisha semi hizi zilionekana siyo ngeni masikioni mwa wasomaji wa tamthilia za Kiswahili, basi; tamthilia husika zilihesabika kuwa na matumizi ya lugha yaliyo mepesi. Kinyume chake, endapo tamthilia teule zilithibitika kuwa na utajiri mkubwa wa lugha ya uficho, tena kauli wakilishi za semi ni ngeni masikioni mwa wasomaji, basi tamthilia husika ilihesabika kutumia lugha ngumu.

Upimaji wa ubunifu kwa kigezo cha uwepesi na ugumu wa lugha haukuweza kukamilika pasipo kuzingatia mambo mengine kiutunzi. Mambo hayo ni maudhui, vijenzi vya kisanaa vya kazi husika, walengwa wa mwandishi, lengo la mwandishi, wakati na hali ya mazingira yaliyotawala kipindi cha utunzi husika. Kwa sababu, kama alivyoeleza Jilala (2012), matumizi ya lugha ya uficho ambayo ni ngumu kueleweka hutokana na unyeti wa jambo linalojadiliwa, mazingira ya utunzi na aina ya maslahi ya mlaji na mtunzi husika. Kwa hiyo, hatuwezi kusema, kazi zilizotumia lugha ngumu zimebeba ubunifu halafu zilizotumia lugha nyepesi hazijabeba ubunifu.

Kiubunifu, wazo linaloteuliwa na mwandishi, huamua mbinu za kisanaa na mawanda ya sanaa husika (Senyamanza, h. m.).

#### **2.2.4 Ubunifu**

Siyo rahisi sana kuijadili dhana ya ubunifu kwa lugha inayojitosheleza kwa asilimia 100 pasipo kuibua swali (Senkoro, 1995). Hata hivyo, zipo fasili na mijadala inayotambulika miongoni mwa wanataaluma wa fasihi juu ya dhana ya ubunifu. Baadhi ya wanataaluma hao ni Abdulla (1974), Matteru (1974), Msokile (1992), Mohamed (1990), Senkoro (1995), Mbise (1996), na Senyamanza (h. m.). Ubunifu unahusishwa na dhana “buni,” “ubunilizi,” “ubunaji” na kwa lugha ya Kiingereza ni “create” au “creativity.” Ijapokuwa, bado ufafanuzi unaotolewa unaonekana kuwa na mkanganyiko kiasi cha kutokutoa picha iliyoangavu kuhusu ubunifu.

Mathalani, Abdulla (1974) katika Senyamanza (h. m.) anasema, “kubuni ni kuzua na kuandika uwongo uliofanana na ukweli. [...]; ni kuumba kiumbe kwa fikra na mawazo kikawa kinashikika, [...] ingawa kuumba ni kwa mawazo tu, kiumbe cha kubuni kina sifa zote za kiumbe cha kweli” (uk. 4). Ufafanuzi wa Abdulla unatuaminisha kwamba, ubunifu ni mchakato wa udanganyifu unaosababisha jambo likaribiane na ukweli. Wakati huohuo anatambua ya kwamba sifa za zao la udanganyifu huwa sawa na sifa za zao halisi. Kwa hiyo tunaweza kusema, ubunifu ni hila au mazingaombwe yanayoumbwa ndani ya fikra ili yazae matokeo yanayobeba sifa halisi za viumbe au mambo ya dhati. Maelezo haya kwa pamoja tunaweza kuyaweka katika usemi wa kuwa, ubunifu unatokana na kitendo cha kuumba wazo au jambo la uongo ili lionekane kuwa la kweli. Mtazamo huu unaonekana kufanana kwa kiasi na ule wa Matteru (1974) na Msokile (1992).

Matteru (1974) anaona kuwa, kubuni (kifasihi) ni pale mtunzi anapotunga kufuatana na uwezo wake kwa “kuibusha mambo kutokana na mazingira yake.” Na kwamba, kuna uwezekano wa mazingira na vituko vilivyobebwa kutokuwa vya kweli lakini vikawa vinawakilisha mambo mahususi, watu mahususi, na kadhalika katika nyakati na mahali tofauti tofauti. Matteru anaonesha kuwapo kwa mazingira ya jambo au kitu kutokuwa halisi lakini zao hilo la kufikirika likaishia kuwa fotokopi ya kitu au jambo halisi. Pia, Matteru anatuongoza kutambua ya kwamba, hakuna ubunifu jumuishi. Kwa maana kwamba, ubunifu hutegemeana na uwezo wa mbunaji kutegemea tajiriba na mazingira anayoyatawala mwanadamu. Kwa hiyo, hata tukishindwa kusema ubunifu ni nini, basi tuseme hakuna ubunifu unaofanana kwa asilimia 100; ukifanana huo siyo ubunifu bali uigaji. Yaani aliyebuni ni wa kwanza, wa pili ameiga badala ya kubuni.

Kwa upande mwingine, Mohamed (1990) katika Senkoro (1995) anaibua wazo la upya na mazingira kuamua ufafanuzi wa dhana ya ubunifu ambao yeye anautambua kwa istilahi “ubunaji.” Mohamed (1990) anasema, “ubunaji ni hali inayompa msanii kuja na muundo au umbo fulani kutokana na hisi au mawazo fulani, umbo ambalo kwa namna fulani lina upya wa kimawazo na kimuundo au wa utumizi wa maneno au upya wa zana yoyote ile inayotumika kuundia au kubunia sanaa fulani” (katika Senkoro, 1995; uk. 85). Na kwamba, upya huo hautoki hewani tu. Bali hutokana na hali halisi ya mambo ambayo mtunzi ameyasoma mahali fulani, ameyasikia, ameyaishi, ameyahisi, ameyanusa, ameyaona na, au ameyaonja. Kutoka katika uzoefu huo, ndipo mtunzi kwa uweza aliokirimiwa na Mungu huanza “kuyafinyanga upya mambo hayo ili kuunda umbo la kisanaa” (katika Senkoro, 1995; uk. 85).



Mohamed (1990) anakwepa kuingiza uongo, uigaji na ushabihishaji wa umbo au jambo linaloishi katika mazingira halisi na dhahania ya msanii. Aidha, Mohamed (1990) anatambua kinachompa msanii uwezo wa kuumba upya ni kipawa cha kuiga umbo dhahiri kwa kulipa upya wenye kulitofautisha na umbo mama. Mohamed (1990) ni kama haamini kuwa mtu anaweza kujifunza kufinyanga umbo jipya pasipo kuwa na kipawa cha kisanaa. Kwa mantiki hii, tunapochunguza ubunifu katika tamthilia teule ni sharti tuchunguze jambo au kitu kipya kilichomo ndani ya matini husika. Hata msisitizo hauna budi kuwekwa katika historia ya wakati na namna jambo husika lilivyofinyangwa.

Naye Msokile (1992) anafafanua kuwa mwandishi huandika mambo yaliyotokea kweli, lakini huyafanya kuwa ni ya kubuni, na pengine huandika maneno: hii ni hadithi ya kubuni, haimhusu mtu yeyote aliyehai au marehemu. Na kwamba, mwandishi huweza kuandika mambo aliyoyasikia na kuyafanya ya kubuni. Maelezo ya Msokile (1992) yanaonesha kuwa mwandishi habuni bali huuhadaa umma kupitia simulizi yake huku akijua fika anachokieleza ni zao la jambo la kweli aliloliona, kulisikia au kulifanya. Hii ina maana kuwa, mtunzi anabadilisha majina ya wahusika halisi na mazingira / mahali halisi kwa kuweka majina bandia kisha anaanza kusimulia kana kwamba ni kitu kipya - kwa msaada wa lugha uliyoichota kutoka jamii husika au unayoandikia. Hivyo, kujenga imani kwamba kuna kipya au upya kutoka katika ombwe au utoupya.

Kwa upande wa Senkoro (1995), yeye anaonekana kusitasita katika kutoa fasili yenye mwanga angavu - usio na kiza hata chembe. Kwa tahadhari kubwa, Senkoro (1995) anapendekeza ubunifu utazamwe kama “uwezo wa kuunda dunia mpya

kutokana na dunia tuliyomo, [...] uwezo wa kuanzisha kitu ambacho hakipo kabisa kutokana na kitu ambacho tayari kipo” (uk. 87). Senkoro (1995) anaonekana kukubaliana kwa namna fulani na Mohamed (1990) – japo kwa tahadhari! Tunasema hivi kwa sababu, naye Senkoro (1995) anaamini kuwa ubunifu hutokana na uhalisi ambapo bila kuwapo kwa mazingira halisi yaliyomtotoa na kumkuza msanii basi hakuna ubunifu kabisa. Senkoro anakubaliana na Mohamed (1990) kuhusu umuhimu wa mazingira kutawala falsafa ya ubunifu ili kuzalisha kitu kipya kutoka katika kitu kilichozaa fikra husika.

Hoja ya upya kutoka katika kuwapo kwa kitu haikubaliki kwa Mbise (1996) bali yeye anakubaliana na kutokuwapo kwa kitu. Kwa mantiki kwamba, ubunifu huzaa hali au jambo ambalo halijawahi kuwapo. Mbise (1996) katika Senyamanza (h. m) anaeleza kuwa: “To create is to produce. In a sense that, it is to cause something to exist. Something created therefore is something new or original.” Kwa Kiswahili, Mbise anasema, “ubunifu ni kuzalisha (au kuumba / tengeneza / kuunda). Yaani, ni kufanya kisichokuwapo, kutokea. Kwa hiyo, kilichobuniwa ni kitu kipya au cha asili (cha awali / cha kwanza kutokea)<sup>4</sup>” (uk. 5). Mbise (1996) hakuishia hapa katika kuelezea dhana ya ubunifu. Bali amerejelea pia uumbaji wa Mungu unaopatikana katika Biblia, kitabu cha Mwanzo 1 na 2 kinachoeleza kwamba vitu vyote viliumbwa na Mungu kwa kuamrisha viwe, navyo vinakuwa. Maelezo na ufafanuzi wa Mbise unatusukuma kuamini katika udhanifu na kutulazimisha tuamini kwamba, Mungu ndiye aliyekuwa mbunifu wa kwanza baada ya hapo wengine wote ni waigaji.

---

<sup>4</sup> Tafsiri hii siyorasmi. Imetoka kwa mtafiti.

Hata hivyo, hatupaswi kuamini kwa asilimia 100 kwamba Mbise anatutaka tuamini kwamba kuna mbunifu wa awali. Halafu, wanaofuatia kuumba kitu chenye umbo la awali hawana ubunifu wowote. Ama kwamba, kinachoitwa ubunifu ni uigaji wa maumbo na maono tunayoyaona, kuyasikia na kuyatenda maishani. Upya au asili anayoirejelea Mbise tunaweza kuifananisha na utengenezaji wa vitu. Kwamba, nikichukua mbao na kuzikatakata kwa mpangilio maalumu, halafu nikaviunganisha vipande hivyo, daima nitapata umbo. Umbo hilo kama kitu halisi, halikuwapo machoni kwangu (hata kama nimeona / nalijua awali) lakini lilikuwapo fikrani mwangu. Hivyo, umbo lililozaliwa kwa kuunganisha vipande vya mbao ni kitu kipya cha asili.

Kitu hicho kinaweza kikawa ni kipya kwa vile nimekitengeneza. Lakini, umbo lake likawa linafahamika au lilishawahi kutengenezwa na mtu mwingine. Ndiyo maana tunasema, yawezekana tukawa tunajadili mambo mawili tofauti bila kujua. Yaani, kujadili asili ya kitu na mtu wa awali na kujadili zao la uigaji na muigaji. Mtu wa kwanza akizalisha kutoka umbo la fikrani bila shaka huyo ndiye mbunifu aliyeuwasilisha ubunifu mbele yetu. Lakini watakapokuja wengine kutengeneza kitu cha umbo hilo hatuna budi kuwaita waigaji. Hata hivyo, kuna imani kwamba, hakuna mtu mwenye uwezo wa kuiga kitu au jambo nalo likafanana vivyo hivyo kwa asilimia 100. Imani ni kuwa muigaji huyo, lazima atabadilisha muonekano wa picha ya awali kwa namna fulani – iwe kwa kujua au kutokujua; kwa ubora zaidi au udunisho.

Kwa hiyo, mtu wa kwanza anaweza kuumba kitu au jambo kutoka kitu au jambo lisiloonekana. Wakitokea watu wengine wakaendeleza utengenezaji wa umbo husika

kwa namna moja au nyingine; halafu machoni mwa mtazamaji umbo hili likaonekana kuwa sawa na la kazi ya awali, bila kutambua utofauti katika vipimo, aina na kiwango cha nakshi, mtazamaji husika atasema huyu wa pili ameiga. Lakini ikitokea mtengenezaji wa pili akalibadilisha umbo mama, bila shaka tutasema huyu amekosea. Si ajabu tukasema hivyo pasipo kutambua nafasi ya ubunifu wake katika kile kilichofanyiwa maboresho.

Katika muktadha wa kifasihi, tuseme mtu wa kwanza kuandika riwaya ama ushairi au tamthilia ama hadithi, basi ndiye mbunifu kwani alitumia ubunifu kuumba kisichokuwapo. Au, mtu wa kwanza aliyeandika juu ya jambo fulani kisanaa, ndiye mbunifu. Halafu walipoibuka watu wengine kuendeleza uandishi wa riwaya, ushairi, tamthilia, hadithi au jambo lilelile, basi wahesabike kuwa ni waigaji tu! Kisanaa hatuwezi kukiri hivi kwani hakuna mbunifu mwigaji kwa asilimia 100. Hili ni suala la kiuajumi zaidi. Huu ni ushahidi mwingine juu ya ugumu uliopo katika kutalii dhana ya ubunifu kimawanda. Kiukweli, ubunifu haupaswi kumtazama mwasisi pekee.

Hata mwendelezaji au mwigaji wa kile cha awali huwa ana kionjo chake cha pekee. Kwa sababu, hata mwendelezaji atakuwa na namna ya tofauti katika kulibeba umbo aliloliona, alilolisikia, analolihisi na analoliishi. Wote hawa hawawezi kuiga umbo la awali kwa asilimia 100, iwe kwa kujua au kutokujua. Senyamanza (h. m.) anatuongezea ufafanuzi kwa kusema: -

Tunachopaswa kujua ni kuwa ubunifu ni namna maalumu ya kuuelewa na kuusawiri ulimwengu kulingana na hali ya maendeleo ya jamii inayohusika. Mbunifu siku zote hujitahidi kudhihirisha aina fulani ya urazini na utambuzi wa hali ya maisha alionao mtunzi pamoja na wale anaowawakilisha. Hata hivyo, ubunifu hutumia

lugha, maumbo, mbinu, ufundi na mitindo inayopatikana na inayowezezana katika jamii inayoizua. Kwa hali hiyo, ubunifu hujiegemeza katika maisha halisi na ndiyo msingi na mzazi wa kazi ya kibunifu. Kwa sababu mbunifu hujitahidi kutafuta mbinu mbalimbali ili kuunda kazi bora, wakati mwingine huweza kuvuka kidogo kiwango cha jamii ya mbunifu kwa kuwa mbele ya wakati, lakini mbegu ya uvukaji huo huwa tayari imepandwa katika urazini na uzoefu wa jamii inayohusika (uk. 10).

Ufafanuzi wa Senyamanza umejenga taswira pana kuhusu ubunifu na unatuongoza katika kuutazama ubunifu kama mchakato maalumu wa kuutambua na kuutambulisha ulimwengu ijapokuwa hapo kwenye umaalumu ndipo penye shida. Aidha, Senyamanza kama walivyo wanataaluma wengine mathalani Abdulla (1974), Matteru (1974), Senkoro (1987; 1995), Msokile (1992), Culpeper na wenzake (1998), anakubaliana na suala la kufungamanishwa kwa uhalisi na mazoea ya jamii kama sehemu ya kuubeba ubunifu. Hili linatokana na ukweli kuwa ubunifu hutumia lugha, maumbo, mbinu, ufundi na mitindo inayopatikana katika jamii inayoizaa. Hata hivyo, kauli hii inapaswa ibebwe kwa tahadhari kwani si kila kitu kinachopatikana au kutokupatikana, au kuwezekana au kutokuwezekana katika jamii ni zao la hiyo jamii ama ndio ubunifu wenyewe.

Wanauumbuji wa Kirusi wakongwe, mathalani Roman Jacobson husisitiza sanaa lazima iwe ni kazi yenye kubeba upya kila iitwapo leo kwa sababu kazi ikibeba kinachojulikana na kuzoeleka huchusha na kutupwa, hivyo kukosa sifa za kuwa sanaa (Mushengyezi, 2003). Kumbe basi, kazi inaweza kuwa na ubunifu lakini kwa sababu ya kuzoeleka au nyakati kuendelea sana, kazi hiyo ikaishia kuonekana kukosa ubunifu. Hapa jamii haitakuwa imeitendea haki kazi husika kwa vile sanaa andishi

siyo sawa na sanaa simulizi. Sanaa andishi haiwezi kupokea mabadiliko ya papo kwa papo kutokana na ukweli kuwa ikishaandikwa na kusambazwa kwa walaji kamwe haiwezi kujiumba upya papo kwa papo labda liandaliwe toleo jipya (Mulokozi, 2017).

Pamoja na Senyamanza kutokufafanua umaalumu wa ubunifu, bado tunadhani umaalumu huo ndio unaosisitizwa na Roman Jacobson, kuwa ubunifu siyo mazoea bali kugeuza mazoea kuwa na mwonekano mpya. Ndiyo maana, siyo ajabu kukuta kazi fulani ikisifiwa kwa ubunifu na nyingine kubezwa. Vivyohivyo, si ajabu kukuta kazi iliyosifiwa kwa ubunifu hapo awali, leo inabezwa na kuondolewa katika kundi la kazi bunilizi (Eagleton, 2008). Hili ni jambo la kiujumi zaidi. Hivyo ni vigumu sana kuchora mstari sahili ili kutenganisha kati ya ubunifu na mazoea au utobunifu.

Pamoja na ugumu uliopo katika kudadavua dhana ya ubunifu, bado tunaweza kusema kwamba, ubunifu ni dhana ya kidhahania na kiujumi ambayo huwezi kuishika bali unaweza kuihisi na kuitambulisha kupitia vionjo vya ndani ya mwili pale unapohisi kutambua upya katika wazo au mbinu uliyoizoea, usiyojua ama unayojua lakini hujazoea. Ubunifu ni ujanja wa kulipanga wazo katika mfumo maalumu wa kisanaa unaolichukua jambo lililopo au lisilokuwapo na kuitambulisha kwa namna inayoibua utamu na, au uchungu kwa lengo la mtu kupata burudani, utiisho na mafunzo.

Ujanja huo hutambulishwa na msanii kupitia umbo halisi linaloonekana kupitia uteuzi na ujenzi wa wazo na wahusika. Pia, kupitia motifu, lugha, mazingira, mandhari, muktadha, muundo, falsafa, propaganda, na kadhalika. Ujanja huo ndiyo huleta upya katika kazi za kisanaa hata kuwasukuma watu kusema kuna maendeleo

kiutunzi. Kwa minajili ya andiko hili, ubunifu umepimwa kwa kutazama namna mwandishi alivyoweza kubaini, kuongeza tija na kuwasilisha jambo lenye maslahi kwa jamii kupitia dhamira na lugha teule kwa namna iletayo nyongeza ya pekee ya upya na mguso maalumu kwa wasomaji, wasikilizaji na watazamaji.

### **2.3 Maendeleo ya Tamthilia ya Kiswahili Nchini Tanzania**

Sehemu hii inatalii historia ya maendeleo ya Tamthilia ya Kiswahili nchini Tanzania katika awamu ya Azimio la Arusha na awamu ya soko huria. Uwasilishaji umegawanyika katika sehemu mbili, ambapo awamu ya Azimio la Arusha imeanza kisha kufuatiwa na awamu ya soko huria. Katika kila awamu, mwandishi amehusisha maendeleo ya tamthilia na baadhi ya matukio muhimu ya kijamii, kiuchumi na kisiasa yaliyojili katika kipindi husika. Tunalazimika kujadili maendeleo ya Tamthilia ya Kiswahili kwa kufungamanisha na matukio ya kihistoria yaliyotawala mfumo wa nchi kwa sababu, Wanafasihi Linganishi wanaamini kuna uhusiano mkubwa sana kati ya maisha ya sanaa husika na maisha ya jamii katika kipindi fulani cha kihistoria (Zepetnek, 1998; Villanueva, 2011).

Hivyo basi, hatuwezi kuitalii historia ya makuzi na ustawi wa Tamthilia ya Kiswahili kwa kujitenga na matukio makuu ya nchi kwani athari ya kisiasa, kiuchumi, kijamii na kitamaduni huathiri hata utunzi na ustawi wa sanaa moja kwa moja (Nazareth, 1978; Culpeper na wenzake, 1998; Ntarangwi, 2004; Ruhumbika, 2006). Kwa hiyo mabadiliko yoyote yanayotokea katika jamii lazima yatajibainisha kupitia fani na, au maudhui ya sanaa husika - tamthilia ikiwemo.

### **2.3.1 Maendeleo ya Tamthilia ya Kiswahili katika Awamu ya Azimio la Arusha**

Azimio la Arusha lilipitishwa katika kikao cha TANU kilichoketi mjini Arusha mnamo tarehe 26 hadi 29 Januari 1967. Kisha likatangazwa rasmi jijini Dar es salaam na Mwalimu Julius K. Nyerere, Mwenyekiti wa TANU na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mnamo tarehe 5 Februari 1967. Kipindi hiki kiliambatana na matukio mengine kama vile kuundwa na kuanzishwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1967, mapitio ya sera ya lugha, sera ya utamaduni, sera ya elimu (hasa mpango wa watu wote kujua kusoma, kuandika na kuhesabu - maarufu kwa jina la K.K.K) na sera ya uchumi nchini Tanzania. Pia, kuanzishwa kwa Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) mwaka 1967.

Mabadiliko haya ya kisera na kisheria yaliyogusa mfumo wa siasa, uchumi, jamii, utamaduni, sayansi na teknolojia yanatajwa kugusa hata maendeleo ya Tamthilia ya Kiswahili moja kwa moja. Kwa mfano, Mlama (2003) anaeleza kuwa, kabla ya mwaka 1967 Tanzania haikuwa na tamthilia zilizotungwa na kuchapishwa bali zilizotungwa ziliishia kuigizwa jukwaani. Tena nyingi ya tamthilia zilikuwa kwa Kiingereza. Semzaba (2003) anaungana na Mlama (2003) kwa kusema, tungo hizi zilijikita zaidi katika kunadi utu, utamaduni na ustaarabu wa kigeni badala ya kumuinua mwenyeji katika nyanja zote za kiutu na kimaisha.

Mlama (2003) na Semzaba (2003) wanasisitiza kuwa, hata tamthilia zilizotungwa au kutafsiriwa zikisawiri madhira ya mtu mnyonge, bado hazikuonesha ukomavu katika fani na taswira ya Mwafrika na Mtanzania akiwamo. Badala yake, tamthilia hizo zilibeba maudhui mepesi kwani zilikuwa zimejaa stadi za kiutunzi za drama za Kimagharibi na dhima ya kukuza ustaarabu wa Kimagharibi kwa njia fiche. Hali hii



inatajwa kulelewa na wamiliki na wafadhili wa kampuni za uchapishaji ambao wengi wao walikuwa zao la ukoloni. Hivyo, haikuwa rahisi kuchapishwa kwa kazi isiyokidhi matakwa ya wamiliki na wafadhili wa uchapishaji vitabu.

Kwa hiyo, baada ya mabadiliko yenye utashi wa kisiasa wenye kumlenga mzawa mnyonge, ndipo Tamthilia ya Kiswahili yenye kubeba mambo mazito na chanya kwa maslahi ya Mswahili zikaanza kuingia sokoni kwa wingi. Pia, pamoja na mambo mengine, kwa namna moja au nyingine mabadiliko ya kisera na utashi wa kisiasa yalisaidia kuzalisha wasomi wenye chembechembe za utaifa na Uafrika (Semzaba, 2003). Aidha, hamasa za kisiasa katika kukuza hisia za kujikomboa na kuwakomboa wengine kwa faida ya taifa zima, kuhimiza na kuenzi utu wa mtu mweusi, upendo, uzalendo, na umoja wa kitaifa kulisaidia pamoja na mambo mengine kujenga na kukuza stadi na maarifa ya kuitambua na kuitetea falsafa na sanaa ya Mwafrika. Matokeo yake waigizaji na watunzi wazawa (wasomi) wakaanza kutotolewa na kuusaka ukweli dhidi ya mafundisho ya kikoloni waliyolishwa (Mulokozi, 2017).

Miongoni mwa wasomi hao ni pamoja na Amandina Lihamba, Crispin Hauli, Ebrahim N. Hussein, Felician Nkwera, Ndyanao Balisidya na Penina Mhando. Wasomi hawa walianza kuandika tamthilia zenye kuwa na tija kwa Mwafrika, hususani Mtanzania katika nyanja za kijamii, kiutamaduni na kiasi fulani kisiasa na kiuchumi. Kazi walizotunga zenye kubeba dhamira za kijamii na kiutamaduni ni pamoja na *Wakati Ukuta* na *Alikiona* (1967) za Ebrahim N. Hussein na *Dunia Iliyofarakana* (1967) ya Crispin Hauli ambazo zote tatu (3) zilichapishwa kwa mara ya kwanza katika jarida / gazeti la *DarLite*. Kazi nyingine ni *Johari Ndogo* (1968) ya

Felician Nkwera, na *Kinjekitile* (1969) ya Ebrahim N. Hussein ambazo zilizajili mambo ya kijamii, kisiasa, kiuchumi na kitamaduni yenye tija kwa Mtanzania.

Mulokozi (2017) anazitambua pia tamthilia za Kiswahili zilizotokana na kutafsiriwa kwa tamthilia za kigeni. Wafasiri wake walikuwa ni Watanzania wakilenga kutumia sanaa ili kukidhi matakwa ya kisiasa yaliyohitaji kubadili mifumo iliyokuwapo ya kiutamaduni, kiuchumi na kijamii. Baadhi ya tamthilia hizo ni *Makbethi* (1968) na *Tufani* (1969) za Samwel S. Mushi, *Juliasi Kaizari* (1969) na *Mabepari wa Venisi* (1969) za Julius K. Nyerere. Pamoja na kuwapo kwa tamthilia chache za watunzi wazawa, Tamthilia ya Kiswahili (kama sanaa andishi) bado haikuwa na nguvu sana kwani Watanzania wengi walikuwa hawajui kusoma, kuandika na kuhesabu. Msekwa (2013) anatujuza kuwa, hata miundombinu ya kijamii, kiuchumi na kielimu ilikuwa bado ni duni ikilinganishwa na kipindi cha miaka ya 2000s. Kwa hiyo katika kusaidia kuleta mabadiliko ya haraka, mbali ya juhudi nyingine, serikali ililazimika kutoa elimu bure kwa njia mbalimbali zikiwemo elimu vijijini na kwa njia ya masafa ili watu wengi zaidi wafikiwe na elimu angalau ya kujua kusoma, kuandika na kuhesabu kwa Kiswahili. Hatua hii ilisaidia kuongeza wigo wa watu wanaojua kusoma na kuajirika ili kukuza kipato cha kaya na taifa (Msekwa, 2013). Hivyo, sanaa andishi ikiwemo Tamthilia ya Kiswahili nayo ikapaa kwa kupata watunzi na walaji wazawa wengi zaidi.

Hata hivyo kisanaa, baadhi ya watunzi hawakuonesha ukomavu kwani walijikita katika kunakili matamko ya kisiasa kwa lugha nyepesi ili hadhira na wasomaji waelewe mwelekeo wa serikali na chama kwa urahisi pasipo kufikiri kwa kina. S. M. A. Massoud (2013) anaeleza kwamba, baadhi ya tamthilia za miaka hii zilibeba

ajenda ya Azimio la Arusha lililotajwa kuwa ni uamuzi wa busara wa Watanzania kuondoa unyonge, kujitegemea kama taifa. Ajenda nyingine zilikuwa ni chama kushika hatamu, na serikali kutaifisha mali za watu binafsi kwa manufaa ya “wote,” kukomesha unyonyaji wa mtu na mtu, serikali kumiliki njia kuu za uchumi kwa faida ya watu “wote,” na kuwa na utawala wa kidemokrasia. Mambo haya yaliwakosha baadhi ya watunzi kiasi cha kugeuka vipaza sauti vya matamko ya kisiasa ya watawala pasipo kuchuja matamko hayo. Tamthilia zikasifia ujamaa wa majukwaani katika kuupiga vita ubepari.

Kwa jumla, tunaweza kusema kwamba, kipindi kati ya 1967 na 1970 pamoja na uchanga wa taifa huru pia msuko wa fani na maudhui, kuwapo kwa idadi ndogo ya wasomi na watunzi wa Tamthilia za Kiswahili, kuwapo kwa idadi kubwa ya watu wasiojua kusoma, kuandika na kuhesabu katika kipindi hiki, bado Watanzania walipata nafasi ya kutunga na kuchapisha na wengine kuzisoma / kusomewa Tamthilia ya Kiswahili. Hivyo, kujitambua kwa namna na viwango tofauti tofauti katika kuyakabili maisha na changamoto zinazowazunguka. Kwa sababu, elimu na vitendea kazi vyake vilitolewa bure kwa kila mtu katika ngazi zote za elimu. Pia, serikali ilitoa ruzuku kwa kampuni za uchapishaji za ndani.

Msekwa (2013) anatujuza pia, kipindi cha kati ya mwaka 1970 na 1989 kilitawaliwa na mabadiliko ya uendelezwaji na uanzishwaji wa mikakati mingi ya kisera na kimipango katika nyanja za kisiasa, kitamaduni, kiutawala, kijamii na kiuchumi iliyokuwapo kabla na baada ya mwaka ya 1970. Ni katika kipindi hiki, ndipo pamoja na mambo mengine Tanzania iliposhuhudia ongezeko la wasomi na watunzi wa Kitanzania, ongezeko la idadi ya watu wanaojua kusoma, kuhesabu na kuandika /

kutunga kutokana na juhudi za makusudi za serikali kuhakikisha wananchi wake wanapata elimu ya kujua kusoma, kuandika na kuhesabu kupitia mpango maalumu wa elimu kwa wote. Pia, kulianzishwa na, au kuimarishwa kwa taasisi mbalimbali. Aidha, kuliongezeka au kuboreshwa kwa kampuni za uchapishaji kama vile DUP, TUKI, TPH na Benedictine Publishers ya Ndanda na Peramiho. Huku Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima ikaanza kutoa elimu kwa njia ya masafa kupitia Shirika la Posta mnamo mwaka 1970.

Vilevile, kulikuwa na kutekelezwa kwa uanzishwaji wa vijiji vya ujamaa, na kuvunjwa rasmi kwa TANU na ASP kisha kuundwa kwa chama kimoja – Chama cha Mapinduzi (CCM, tarehe 5 Februari 1977). Kadhalika, kipindi hiki kilishuhudia kuuawa kwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar – Hayati Abeid Karume (1972), kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki (1977), kuzuka kwa vita vya Kagera (1978 - 1979), kudorora kwa uchumi wa Tanzania na kuibuka kwa uhujumu uchumi (mwishoni mwa 1979 na kuendelea). Kulishuhudiwa pia mapambano ya kuukabili uhujumu uchumi (1983 - 1984). Kulishuhudiwa pia kung'atuka kwa Rais wa kwanza wa Tanzania Mwalimu Julius K. Nyerere na Alhaji Ali Hassan Mwinyi kuwa Rais wa pili wa Tanzania (1985). Vilevile, kulishuhudiwa “kufa” kwa Azimio la Arusha na kuzaliwa kwa Azimio la Zanzibar (Chachage, 2014).

Msekwa (2013) anaeleza ya kwamba, kipindi hiki kilishuhudia baadhi ya wasomi, wafanyakazi, na viongozi weusi wakiwasaliti Watanzania wa tabaka la chini kwa kushiriki unyonyaji, udhalimu, unyanyasaji, ubaguzi na uifisadi kwa kujilimbikizia mali. Msekwa anaendelea kueleza kwamba, wengine walikwenda mbali zaidi hadi kujigeuza miungu watu kwa kuwadhulumu wananchi haki na mali zao kwa

kisingizio cha kutekeleza maagizo ya chama na serikali. Matendo haya, pamoja na mengine, yalichochea uhasama, hasira na chuki miongoni mwa wananchi. Haya yote yalikuwa kinyume kabisa na malengo ya msingi ya kuzaliwa kwa Azimio la Arusha na sera ya siasa ya ujamaa na kujitegemea. Kwani azimio na sera yake vilikuja ili kusisitiza heshima, utu, ushiriki sawa na haki kwa watu wote pasipo kujali rangi, dini wala ukanda atokao mtu (rej. TANU, 1967).

Kwa mujibu wa S. M. A. Massoud (2013), matendo haya yakachochea athari chanya katika uteuzi na ujenzi wa Tamthilia ya Kiswahili. Kwa hiyo, tamthilia nyingi za Kiswahili nazo zikaanza kujifungamanisha zaidi na jamii ya wanyonge - kifani na kidhamira kwa kujikita katika kuyasawiri machungu ya Mtanzania mnyonge katika nyanja zote za maisha. Wakati utamaduni na imani ya wananchi kuwaamini na kuwathamini baadhi ya viongozi wao ikiongezeka zaidi, hali ilikuwa kinyume kwa viongozi walio wengi. Viongozi wengi walizidi kuwasaliti na kuwanyonya wananchi. Jambo hili lilizidisha msukumo kwa watunzi kuanza kuonesha na kujadili unafiki na usaliti wa viongozi. Pasipo kusahau kuyajadili mambo mengine yanayohusu maisha ya wanyonge kabla, wakati na baada ya ukoloni (Mulokozi, 2017).

Miongoni mwa tamthilia zilizoonesha uchungu wa mnyonge na kadhia ya tabaka tawala ni pamoja na: *Mashetani* (1971) ya Ebrahim N. Hussein, *Mfalme Juha* (1971) ya Farouk Topan, *Hatia* (1972) ya Penina Mhando, *Ndoto ya Mwendawazimu* (1972) ya E. Ganzel, *Tambueni Haki Zetu* (1973) ya Penina Mhando na *Heshima Yangu* (1974) ya Penina Mhando. Nyingine ni *Wala Mbivu* (1974) ya Angelina Chogo, *Pambo* (1975) ya Penina Mhando na *Kijiji Chetu* (1975) ya Ngalimecha Ngahyoma.

Nyingine ni *Jogoo Kijijini* na *Ngao ya Jadi* (1976) za Ebrahim N. Hussein, *Thamani Yangu* (1976) ya Johnson Mwangudza na *Mbio za Sakafuni* (1976) ya Abel Ndumbu. Pia, *Machazi ya Mwanamke* (1977) ya Ibrahim Ngozi, *Taraka Si Mke Wangu* (1977) ya Penina Mhando, *Mtumwa* (1978) ya Tigiti S. Y. Sengo na *Mukwava wa Uhehe* (1979) ya Mugyabuso M. Mulokozi.

Mulokozi (2017) anabainisha kuwa maudhui (ikiwemo dhamira) na fani ya Tamthilia ya Kiswahili iliimarika zaidi katikati ya miaka ya 1970s na kupata kuungwa mkono na waandishi wengi katika miaka ya 1980s na kuendelea. Tamthilia za miaka ya 1980s zinazotajwa kubeba maudhui hasa dhamira na fani iliyokomaa ni pamoja na: *Giza Limeingia* (1980), *Tone la Mwisho* na *Watoto Wetu* (1981) za Emmanuel Mbogo, *Njia Panda* (1981) ya Henry Muhanika, *Harakati za Ukombozi* (1982) ya Amandina Lihamba, Ndyanao Balisidya na Penina Mhando na *Nguzo Mama* (1982) ya Penina Mhando. Nyingine ni *Buriani* (1983) ya David Mulwa na A. S. Yahya, *Uchafu* (1983) ya V. A. Malima na *Lina Ubani* (1984) ya Penina Mhando. Vilevile, tamthilia za *Ukame* (1984) ya David Mulwa na A. S. Yahya, *Sofia wa Gongolamboto* (1984) ya Edwin Semzaba, na *Ayubu* (1984) ya Paukwa Theater Group.

S. M. A. Massoud (2013), Olali (2015) na Mulokozi (2017) wanazitaja tamthilia nyingine zilizoonesha uimarifu wa maudhui na fani katika awamu hii. Nazo ni *Maisha Subira* (1985) ya Said Abdallah Omar, *Zabibu Chungu* (1985) ya Amana Boukheit, *Duka la Kaya* (1985) ya Tegamwage Ndimara na *Zinduko* (1986) ya S. Ryanga. Nyingine ni *Mama Ee* (1987) ya Ari Katini Mwachofi, *Kwenye Ukingo wa Thim* (1988) ya Ebrahim N. Hussein, *Pungwa* (1988) ya Said Ahmed Mohamed, *Mkimbizi* (1988) ya A. S. Yahya na David Mulwa na *Ngoswe Penzi Kitovu Cha*

*Uzembe* (1988) ya Edwin Semzaba. Nyingine ni *Kivuli Kinaishi* (1990) ya Said Ahmed Mohamed, *Ushuhuda wa Mifupa* (1990) ya Ibrahim Ngozi, *Msomu* (1990) ya V. Rukambelya na *Zimwi la Mrima* (1991) ya F. Fawah, kutaja kwa uchache.

Kwa upande wa tafsiri, uteuzi wa tamthilia za kigeni kisha kuzitafsiri katika lugha ya Kiswahili haukuishia katika miaka ya 1960s pekee. Bali uliendelea huku ukizingatia maudhui hasa dhamira zinazolenga kumtetea mnyonge na uimarifu wa fani (S. M. A. Massoud, 2013). Baadhi ya kazi hizo ni *Mfalme Edipode* (1971) iliyotafsiriwa na Samwel S. Mushi, *Masaibu ya Ndugu Jero* (1974) iliyotafsiriwa na A. S. Yahya, *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* (1979) iliyotafsiriwa na Christon Mwakasaka na *Usaliti Mjini* (1990) iliyotafsiriwa na Kisia Adaka na Josephat.

Kwa jumla, kipindi kati ya 1970s na mwishoni mwa miaka ya 1980s, kwa mujibu wa wanataaluma tuliowatalii, kinaonekana kiubunifu kiliwabeba vema watunzi na waandishi wa Tamthilia ya Kiswahili. Watunzi wanaotajwa zaidi kuchangia kuikuza Tamthilia ya Kiswahili ni Ebrahim N. Hussein na Penina Mhando. Hawa wanatajwa kuitambulisha Tamthilia ya Kiswahili kwa misingi ya Falsafa ya Kiafrika na fani ya sanaa za maonesho za kijadi kupitia kazi zao - tofauti na utunzi wa awali wa Kiaristotle. Samwel (2013) anasema kuwa, uzalendo wao uliweza kuonekana zaidi katika fani jadia mara walipoanza kutumia vipengele vya fani za sanaa za maonesho zenye asili ya Tanzania na Afrika katika kuandika tamthilia zao.

Samwel (2013) anaongeza kuwa, ni katika ubunifu wao Ebrahim N. Hussein na Penina Mhando ndipo ikawa ni mwanzo wa majaribio katika utunzi wa Tamthilia ya Kiswahili hatimaye kuzalisha Tamthilia ya Kiswahili ya Kimajaribio. Majaribio haya pamoja na mengine ni kama vile kutumia ngoma, nyimbo, utambaji, hadithi na

majigambo katika tamthilia. Ubunifu huu ulikua na kukomaa kiasi cha kukubalika na kuanza kutumika katika tamthilia mbalimbali za Kiswahili. Baadhi ya tamthilia hizo ni: *Arusi, Ayubu, Harakati za Ukombozi, Jogoo Kijijini na Ngao ya Jadi, Lina Ubani, Lina Ubani, Mashetani, Mkokoteni, Nuru Mpya, na Pambo*. Samwel (2013) kama ilivyo kwa Mlama (2003) anatumia kwamba, fani na maudhui hasa dhamira za Tamthilia ya Kiswahili zilizidi kubadilika kiumbo kwa kuukumbatia Uafrika na utu wa Mwafrika. Kwa mfano, Mlama (2003) anatumia kuwa tamthilia za Kiswahili hususani zile za kuchekeka nazo zilianza kutungwa. Tamthilia hizi zililenga kukejeli ukoloni na wakoloni badala ya kuwaenzi. Semi za kuwathamini Waafrika na kuwashusha thamani wazungu (kwa mfano, *wazungu wawili wanachungulia dirishaji - jibu lake ni kamasi*) nazo zikaanza kuonekana ndani ya Tamthilia ya Kiswahili.

Kwa mujibu wa Samwel (2013), Tamthilia ya Kiswahili ya majaribio ni tamthilia ya Kiswahili ambayo inafumbata ufasahi simulizi na sanaa jadia za Mwafrika ndani yake. Kwa mfano, kuwapo kwa vionjo vya ngoma, nyimbo zisizokuwa na mipaka kiutendwaji, shughuli za kiibada mfano matambiko, kupunga pepo, uganga na usihiri. Pia, masimulizi jadia na wahusika wa masimulizi jadia mfano mazimwi, mashetani, wanga, walozi, washirikina na wachawi. Vilevile, matumizi ya wahusika haishwa wa kitashihisi (mfano majabari, majengo makubwa au marefu) na wahusika huishwa wa kitashihisi (kwa mfano, ardhi, mimea, ndege, wadudu, maji, na wanyama) hupewa uzito. Pia, maudhui yake huenda na wakati katika kujadili mambo ambayo awali hayakuweza kujadiliwa kwa sababu ya kutokuwapo katika jamii ama



kutokupewa uzito au kuonekana kuwa ni miiko ya kijamii kuweza kujadiliwa kwa kina na upana.

Mabadiliko ya kiutunzi yanayoelezwa na Samwel (2013), yanarejea maelezo ya Mlama (2003) na Hussein (2003) waliowahi kubainisha ya kwamba hata utunzi wa tamthilia za Kiaristotle haujawahi kuwa wa fomula moja kifani kutokana na mabadiliko ya wakati. Lakini utunzi wa tamthilia za Kiaristotle haukuruhusu Uafrika ujitawale kupitia sanaa hii. Naye S. M. A. Massoud (2013) anabainisha kwamba, fani ya utunzi wa tamthilia za Kiswahili nyingi ulishabihiana na zile za Waingereza isipokuwa katika vipengele vya maudhui, lugha na mandhari. Watanzania baada ya kusoma na kuelewa asili ya Mwafrika na sanaa za maonesho ya Kiafrika, wakaanza kutafakari na kuona uwezekano wa kuingiza vipengele vya fasihi simulizi ya Mwafrika katika Tamthilia ya Kiswahili ili ichukue umbo la Kiafrika zaidi.

S. M. A. Massoud (2013) anaongeza kuwa, mitazamo ya kifalsafa ya Mwafrika ilihusika sana katika kuiumba upya tamthilia itakayobeba maisha halisi ya Mwafrika - Mtanzania akiwemo, pamoja na utamaduni wake. Matokeo yake, watunzi wakazidi kuingiza na kujaribu kutumia vipengele fulani vya fani za sanaa za maonesho zenye asili ya Tanzania katika kuandika tamthilia zao. Samwel (2013) anafafanua zaidi kuwa, katika kila kipindi cha historia na maendeleo ya tamthilia huwa na upya wake kutokana na mabadiliko ya kila siku yanayotokea katika jamii. Kwa hiyo, majaribio ni jambo endelevu ambalo ni zao la mabadiliko hayo ya kijamii. Ndiyo maana ni rahisi kwa watunzi kuingiza majaribio katika fani na maudhui ya kazi bunilizi za zama hizi tofauti na huko nyuma.

Kwa kuakisi fursa za usambazaji na upatikanaji wa vitabu katika shule za ngazi zote nchini Tanzania, pia madarasa ya wanafunzi wa elimu ya watu wazima na mwitiko wa kujifunza na kusoma kwa wale waliokosa fursa za kwenda shule katika kipindi hiki, ni wazi kwamba athari ya fani na maudhui hasa dhamira za Tamthilia ya Kiswahili yaliifikia na kuigusa jamii moja kwa moja. Mulokozi (2017) anaeleza kwamba maendeleo haya ya tamthilia ya Kiswahili yalifikia kilele chake katika miaka ya mwishoni mwa 1980s. Hata kufanya Penina Mhando kwa upande wa Tanzania na Ngugi wa Thiong'o kwa upande wa Kenya kuanzisha drama iliyokuwa maarufu kwa jina la Thieta ya Umma. Drama hizi zilimakinikia changamoto zinazogusa umma wa wanyonge kwa kutumia fani na lugha inayoeleweka vema miongoni mwao.

Kwa Wanamabadiliko kama vile John Darwin, kila jambo hutokea kwa sababu maalumu na kwa wakati wake maalumu. Hivyo hakuna mabadiliko yanayojitokeza kwa bahati nasibu (Richards, 1992). Mtazamo huu unafanana na ule wa Senkoro (1987) anayeamini kwamba, kama ilivyo dunia na majira yake kutokuwa tuli, ndivyo alivyo mwanadamu na sanaa yake. Kwa hiyo, mwanadamu anabadilika kwa sababu anaishi katika sayari iliyo katika mwendo unaomfanya naye asiwe kiumbe tuli. Hapa tunabaini kuwa, mabadiliko ya kijamii, kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni na kimazingira katika wakati mahususi huchochea uwezo bunifu wa mwandishi kukua au kudumaa kisanaa. Ndiyo maana tumeona awamu hii ilikuwa na makuzi makubwa na endelevu kwa uhai na ustawi wa ubunifu na tamthilia yenyewe ya Kiswahili nchini Tanzania.

### **2.3.2 Maendeleo ya Tamthilia ya Kiswahili katika Awamu ya Soko Huria**

Ally na wenzake (2013) pia Chachage (2014) wanaitambua awamu hii kama kipindi kilichoibuka baada ya kuzaliwa kwa kile kinachoitwa Azimio la Zanzibar la mwaka 1991. Kwa hiyo kinadharia, tunaweza kusema kuwa awamu ya soko huria inaanzia mwaka 1992. Azimio la Zanzibar lilipitishwa na Kamati Kuu ya Taifa ya CCM iliyoketi huko Zanzibar mnamo tarehe 14 Februari 1991 ikiwa ni siku 181 tangu Mwalimu Julius K. Nyerere ang'atuke rasmi kutoka kiti cha uenyekiti wa CCM, Taifa (Shivji, 2013, katika Ally na wenzake, 2013). Mwalimu Julius K. Nyerere aling'atuka rasmi kutoka kiti cha uenyekiti wa CCM, Taifa mnamo Oktoba, 1990. Azimio la Zanzibar pamoja na mambo mengine liliruhusu mtu mmoja mmoja pia serikali kukopa katika taasisi za kifedha zikiwemo Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa.

Vilevile, watu binafsi wakiwemo viongozi wa chama na serikali waliruhusiwa kumiliki mali pasipo kuwekewa utaratibu madhubuti wa kuepuka mgongano ya kimaslahi. Aidha, Azimio la Zanzibar lilifungua milango kwa wawekezaji na biashara huru kutekelezwa nchini Tanzania (Ally na wenzake, 2013). Kwa hiyo, azimio hili lilibariki sera ya maboresho ya mfumo na utendaji serikalini almaarufu kwa jina la "Structural Adjustment Policies" iliyoratibiwa na Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa. Kwa mujibu wa Chachage (2014) na Shivji (katika Ally na wenzake, 2013), kuzaliwa kwa Azimio la Zanzibar ndiko kulikokuwa mwisho wa uhai wa Azimio la Arusha.

Hata hivyo, Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (kupitia hotuba yake ya tarehe 25 Februari 1991 katika Ukumbi wa

Diamond Jubilee, Dar es Salaam) anasisitiza kwamba maamuzi ya Zanzibar yalipitishwa ili kupanua tafsiri ya azimio na sio kulizika (Ally na wenzake, 2013). Katika hotuba hii, Mheshimiwa Rais (mstaafu) anasisitiza umuhimu wa kutafsiri Azimio la Arusha kwa kulihuisha kulingana na wakati ili kuepuka kuachwa na wakati wa ulimwengu halisi wa kipindi mahususi. Kwa hiyo, kwa maneno yake, kufanyika kwa mapitio ya tafsiri za Azimio la Arusha kwa kuzingatia wakati uliopo ilikuwa ni kuliimarisha azimio na siyo kuliua kama wanavyotanabaisha baadhi ya watu.

Utetezi wa Mheshimiwa Rais mstaafu, masikioni na machoni mwa Chachage (2002, 2014) na Mwalimu Julius K. Nyerere kupitia Hotuba ya Mei Mosi, 1995 Jijini Mbeya (rej. Mtoi, 2012) na ile ya 14 Juni 1995 katika Hoteli ya Kilimanjaro, Dar es salaam, ni kama mtu kujivua nguo hadharani. Hii ilitokana na sababu kwamba kufa kwa siasa ya ujamaa na kujitegemea, kwa kuzikwa na kuzaliwa Azimio la Zanzibar pasipo kuwekwa mikakati madhubuti ya kulinda maslahi ya nchi na taifa, kulibadilisha mfumo wa siasa na uchumi kwa kiasi kikubwa bila kuwapo kwa tahadhari ya kulinda raslimali za ndani.

Hiki ni kipindi ambacho kinatajwa kuwa Tanzania ilianza kutekeleza rasmi sera za Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa. Sera ya serikali kutoa huduma za kijamii bure kwa wananchi wake ilisitishwa rasmi. Kiwango cha umaskini na ujinga kikapanda huku pengo kati ya maskini na tajiri likazidi kukua na kupaa. Vyama vya siasa vikarudishwa rasmi mwaka 1992 na uchaguzi mkuu chini ya vyama vingi ukafanyika kwa mara ya kwanza mwaka 1995 na kuendelea mpaka sasa kwa kila baada ya miaka mitano (5). Pia, serikali ikajikita katika kutekeleza sera za

utandawazi pasipo tahadhari ikiwemo utekelezaji wa sera ya ubinafsishaji pasipo tathmini ya kina. Haya yote yanapatikana katika Arkadie (1995), Chachage (2014) na Msekwa (2013).

Kipindi hiki ndicho kimeshuhudia mabadiliko makubwa ya kisera katika nyanja zote za maisha ya kisiasa, kiuchumi, kiuongozi na kiutawala, na kadhalika. Mathalani, Arkadie (1995) anatumia kwamba, kipindi hiki kinahusisha mabadiliko ya kutoka mfumo wa siasa ya chama kimoja kwenda mfumo wa vyama vingi. Pia, kutoka mfumo wa sera ya ujamaa na kujitegemea hadi mfumo wa soko huria. Msekwa (2013) anasema, kipindi hiki kilishuhudia mabadiliko ya kutoka mfumo wa huduma za jamii kutolewa bure kwa wananchi hadi mfumo wa wananchi kushiriki katika ujenzi wa miundombinu na kuchangia gharama za upatikanaji wa huduma mbalimbali.

Arkadie (1995) anaendelea kusema, mabadiliko mengine yalikuwa kutoka mfumo wa serikali “kujitegemea” kwa fedha na bidhaa za ndani hadi kutegemea mikopo na misaada ya fedha pia bidhaa nyingi zaidi kutoka nje badala ya kusafirisha nje bidhaa kwa wingi. Kutoka mfumo wa serikali kuhodhi nyanja kuu za uzalishaji mali hadi kubinafsisha kiholela shughuli, huduma na miundombinu ya taifa. Kutoka mfumo wa serikali kuwa mwajiri mkuu hadi serikali kupunguza wafanyakazi. Arkadie (1995) anaendelea kueleza zaidi kwamba, pato la taifa lilishuka huku kampuni na vyanzo vya mapato vikidorora na vingine kufa kabisa. Viwanda na mashirika ya umma yakawa hoi bin taabani. Bajeti na upatikanaji wa fedha kwa ajili ya mishahara kwa wafanyakazi, mitaji na fedha za kuendesha shughuli za kila siku za serikali na chama tawala ikashuka. Kushuka kwa bajeti kuliathiri kwa kiwango kikubwa utoaji wa

elimu bure, huduma za maji na afya bure, ujenzi na uboreshaji wa miundo mbinu, kutajwa kwa uchache. Hivyo, serikali na chama tawala vilijiondoa katika kuwa mhimili mkuu wa kusimamia na kutoa huduma kwa jamii ya Watanzania wa viwango tofauti tofauti vya kipato na elimu.

Naye Chachage (2014), anaongeza kuwa hiki kilikuwa ni kipindi cha kutoka mfumo wa waajiriwa wengi kuwa watumishi wazalendo kwa umma hadi kuwa watumishi wa kujilimbikizia mali kuliko ilivyoshuhudiwa kabla na wakati wa awamu ya Azimio la Arusha. Mambo haya na mengine mengi yalichangia kuongezeka kwa kasi kwa kiwango cha ujinga, maradhi na umasikini miongoni mwa wananchi wengi. Pia, taifa lilishuhudia kufa ama kudhoofika kwa kampuni za umma zikiwemo za uchapishaji vitabu na machapisho mengine. Zaidi sana, kukawa na ongezeko la gharama za uzalishaji na usambazaji wa huduma na uzalishaji (Msekwa, 2013).

Athari za matukio na utekelezaji katika miaka ya nyuma yakazifanya taasisi nyingi kushindwa kujiendesha na kufanya wafanyakazi na wakulima kukosa ajira na kipato cha uhakika. Hata huduma ya vitabu vya bure mashuleni na elimu ya bure kwa kila mtoto ikawa haitekelezeki tena. Makovu ya vita vya Kagera na sera za nje zikaigharimu zaidi Tanzania kwa kiwango kikubwa hata nchi ikashindwa kukopesheka huku sekta binafsi ikikua kwa msaada dharimu wa watumishi wa umma wasiowaadilifu. Kutokana na hali hii, serikali na chama wakalazimika kusalimu amri kwa kutii na kutekeleza sera na masharti ya Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa bila kujiandaa wala kuzingatia uhusiano wa sera na masharti hayo kwa mazingira ya Tanzania huru (Ally na wenzake, 2013; Chachage, 2014).

Pamba (2012) anautazama utekelezaji huu kama mkurupuko sawa na kipofu anayetembea kwenye njia ngeni kwa kutegemea ulinzi, usalama na imani ya yule aliyemwelekeza apite njia hiyo. Hivyo, badala ya Tanzania kama nchi kuinuka, ikajikuta ikididimia zaidi. Semzaba (2003) anaeleza kwamba, kuathiriana kwa jamii mbili au zaidi zinazokutana kwa mara ya kwanza ni jambo lisiloepukika. Na daima, jamii yenye nguvu hupenyeza amali zake za kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni, na kijamii. Kiasi kwamba, jamii nyonge hulazimika kukana na kuacha mifumo yake ya maisha na kufuata mifumo ya maisha ya jamii yenye nguvu. Kwa mantiki hii, Tanzania kama nchi nyonge mbele ya mabepari, haikuwa na namna ya kujihami ila kutii matakwa ya mataifa yenye nguvu.

Jambo jingine lililobadilisha mfumo wa maisha ya Mtanzania na sanaa yake ni mabadiliko ya viongozi wakuu wa kisiasa katika muhimili wa chama na serikali kila baada ya miaka ama mitano (5) au kumi (10). Tofauti na awamu ya Azimio la Arusha, awamu ya soko huria ilishuhudia utawala wa marais wanne (4). Viongozi wakuu kwa kila awamu ni Mheshimiwa Rais mstaafu Alhaji Ali Hassan Mwinyi (awamu ya pili ya uongozi, 1985 hadi 1995), Mheshimiwa Rais mstaafu (Hayati) Benjamin William Mkapa (1995 hadi 2005), Mheshimiwa Rais mstaafu Jakaya Mrisho Kikwete (2005 hadi 2015) na Mheshimiwa Rais (Hayati) John Pombe Joseph Magufuli (2015 - Machi 17, 2021). Utafiti huu umejishughulisha kwa uchache sana na kipindi cha Mheshimiwa Rais (Hayati) John Pombe Joseph Magufuli (2015 - Machi 17, 2021) kwani utafiti wetu uliishia mwaka 2016.

Awamu ya Mheshimiwa Alhaji Ali Hassan Mwinyi inatambulika kama kipindi kikuu cha kuruhusiwa rasmi kwa soko huria nchini Tanzania. Awamu ya Mheshimiwa

Benjamin William Mkapa inatambulika zaidi kama kipindi cha ubinafsishaji holela wa raslimali za taifa. Pia, awamu hii inatajwa kurudisha heshima ya kazi rasmi, kudhibiti mfumuko wa bei, kukuza pato la taifa na kusamehewa kwa madeni makubwa kutoka kwa nchi wahisani (Mkapa, 2019). Awamu ya Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete inatambulika zaidi kama kipindi cha ukuaji wa demokrasia na diplomasia ya kimataifa, kukua kwa pato la taifa, mfumuko wa bei kupaa na biashara kustawi. Pia, deni la taifa kuongezeka, na miundombinu ya kijamii na kiuchumi kujengwa kwa wingi na kuimarishwa, kuongezeka kwa taasisi za kutolea huduma za kijamii na kifedha hasa sekta binafsi, kuongezeka maradufu kwa wasomi pamoja na kukua na kustawi kwa teknolojia.

Awamu ya Mheshimiwa John Pombe Joseph Magufuli (kati ya Novemba, 2015 hadi Disemba, 2016) kulishuhudiwa kuwapo kwa juhudi za makusudi za kukuza uchumi, kupungua kwa gharama za malipo katika uchangiaji wa huduma za jamii, kuboresha miundombinu, kudhibiti upotevu wa raslimali na mapato ya taifa. Vilevile, kuongezeka kwa makusanyo ya kodi, heshima ya kazi kurejea, diplomasia ya kimataifa kuimarika zaidi huku biashara holela ikidhoofika. Mengine ni wafanyakazi kupunguzwa katika mfumo wa ajira rasmi, mzunguko wa fedha kudhibitiwa na vyanzo holela (visivyo rasmi) vya mapato kupungua miongoni mwa wananchi na vita dhidi ya ufasidi, madawa ya kulevya na rushwa kupamba moto.

Mabadiliko ya uongozi na, au mifumo ya kisiasa katika taifa inaelezwa na Siegler na Schlosser (1990) kuwa na athari kubwa sana katika maendeleo ya mtu mmoja mmoja na taifa na nchi. Kwa hiyo, mabadiliko yoyote ya kisiasa yanaweza kuwa msaada chanya au hasi kwa uchumi na ustawi wa watu na maisha yao. Matukio haya yote



tumeyatambulisha kwa kuwa kihistoria, udumavu au ukuaji wa sanaa (kwa muktadha wetu ni Tamthilia ya Kiswahili) unaendana na hali halisi ya udumavu au ukuaji wa maendeleo ya watu - kijamii, kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni (Sanchez, 1973). Mfumo wa maisha ya jamii na kisiasa katika kipindi mahususi cha historia ya jamii husika una nafasi kubwa katika kuathiri uwezo na ubunifu wa msanii na sanaa ya wakati husika (Sanchez, 1973; Siegler na Schlosser, 1990).

Katika mapitio ya historia na maendeleo ya Tamthilia ya Kiswahili, tumebaini kuwa kipindi cha awamu ya soko huria hakijaandikiwa sana. Hata waandishi waliogusa historia na maendeleo ya Tamthilia ya Kiswahili katika awamu hii, wameonekana kutokuwa na data za kutosha kama walivyoitalii awamu ya Azimio la Arusha. Baadhi ya wanataaluma hao ni Wafula (1999), Zúbková na wenzake (2009), S. M. A. Massoud (2013), Samwel (2013), Gromov (2014), Olali (2015) na Mulokozi (2017). Katika kukidhi mahitaji ya kipengele hiki, mtafiti alilazimika kupitia ripoti nyingi zaidi za utafiti, vitabu na tovuti za kampuni za uchapishaji vitabu. Huko nako hakukuwa na taarifa za kutosha zinazopatikana katika chanzo kimoja au viwili kama tunavyoona kwa upande wa kipindi cha Azimio la Arusha.

Hata hivyo, kupitia utalii wetu, tulifanikiwa kukusanya na kuunganisha taarifa zilizosaidia kuzalisha hasa dhamira zinazoakisi awamu ya soko huria. Pamoja na uchache wa mapitio ya kifasihi yanayohusu awamu ya soko huria kiutunzi, vyanzo tulivyovitambulisha katika aya ya awali kabla ya hii vinaonesha kuwa, Tamthilia ya Kiswahili ya kipindi hiki kwa kiwango kikubwa imejikita katika kusawiri mapito ya mtu mnyonge kuliko kusifia tabaka tawala. Kazi nyingi zinaonekana kujadili athari za ukoloni mamboleo, hali ngumu ya maisha na changamoto zake, pamoja na

mchango na thamani ya mwanawake katika ulimwengu wa sasa. Lengo likiwa ni kuendelea kupigania ujenzi wa jamii yenye maendeleo endelevu, haki na usawa kwa kila mtu.

Miongoni mwa tamthilia zinazoangukia katika awamu ya soko huria kwa kuchapishwa ni *Mkutano wa Pili wa Ndege* (1992) ya Amandina Lihamba, *Kinyamkera* (1992) ya Edwin Semzaba, *Adui wa Umma* (1992) (tafsiri kutoka *An Enemy of the People* ya Henrik Ibsen) mfasiri E. K. Maarugu (1993) na *Morani* (1993) ya Emmanuel Mbogo. Nyingine ni *Jinyama Madevu* (1993) ya Edwin Semzaba, *Pipani* (1993) ya Parapanda Arts, *Mchawi Wetu* (1993) ya Idara ya Sanaa na Muziki na Sanaa za Maonyesho – Chuo Kikuu cha Dar es salaam, *Mzizi Je?* (1994) na *Shinikizo* (1994) zote za Idara ya Sanaa na Muziki na Sanaa za Maonyesho – Chuo Kikuu cha Dar es salaam.

Tamthilia nyingine zenye kujadili machungu ya mtu mnyonge ni pamoja na *Amezidi* (1995) ya Said A. Mohamed, *Kilio Chetu* (1995) ya Medical Aid Foundation, *Chuano* (1995) ya Paukwa Theater Group, *Sundiata* (1995) ya Emmanuel Mbogo, *Kila Siyesikia* (1997) ya Mathias E. Mnyampala, *Kaptula la Marx* (1998) ya Euphrase Kezilahabi, *Kitumbua Kimeingia Mchanga* (2000) ya Said A. Mohamed, *Adila* (2002) ya Fikirini E. M. K. Senkoro, *Giza* (2004) ya Hadija Jilala, *Mpaka lini?* (2004) ya Mariam S. Mwiru, *Mazonge* (2004) ya Ali M. Rashid, *Kilio cha Jesca* (2004) ya Ambrose F. Mghanga, *Orodha* (2004) ya Steve Reynolds (Mfasiri: Saif D. Kiango) na *Kija: Chungu cha Mwana Mwari wa Giningi* (2005) ya Shani Kitogo.

Tamthilia nyingine za kipindi hiki ni *Mabepari wa Bongo: Kumbukizi* (2007) ya Frowin P. Nyoni, *Utando* (2007) ya Tatu M. Ngelangelela, *Mwalimu Rose* (2007) ya

Ambrose F. Mghanga, *Ngoma ya Ng'wanamalundi* (2008) ya Emmanuel Mbogo, *Posa ya Bikisiwa* (2008) ya Said A. Mohamed na Kitula King'ei, na *Safari ya Chinga* (2009) ya Shani Omari. Zipo pia, *Amri ya Wakati* (2009) ya Said A. Mohamed, *Fumo Liongo* (2009) ya Emmanuel Mbogo, *Ningekuwa na Uwezo* (2009) ya Katama Mkangi, *Changamoto* (2010) ya Elizabeth Mahenge na *Janga la Werevu* (2011) ya Said A. Mohamed. Nyingine ni *Joseph na Josephine* (2014) ya Edwin Semzaba, *Mkokoteni* (2014) ya Edwin Semzaba, *Damu ya Kibena Mzimuni* (2015) ya Subira S. Kabelwa na *Nyerere na Safari ya Kanaani* (2015) ya Emmanuel Mbogo. Nyingine ni *Profesaa* (2015) ya Deogratius F. Mkawe, *Sadaka ya John Okello* (2015) ya Emmanuel Mbogo, *Wangari Maathai* (2015) ya Emmanuel Mbogo, *Mashetani Wamerudi* (2016) ya Said A. Mohamed pamoja na *Nje – Ndani* (2016) ya A. A. Majid Mswahili na M. S. Njonjolo.

Tamthilia zote hizi zinaonekana kuchapishwa katika awamu ya soko huria. Nyingi zinaonekana kupatikana katika tovuti za makampuni ya uchapishaji husika huku chache sana zinapatikana kwenye maduka ya vitabu na maktaba za vyuo. Chache zaidi zinajitokeza katika maandiko yanayohusu historia na maendeleo ya Tamthilia ya Kiswahili zikiwemo tafiti za kitaaluma. Hata hivyo, chache zaidi ndizo zinaonekana kuchunguzwa na kuandikiwa tafiti. Pamoja na uchache huo, sehemu kubwa ya hizo chache ni za watunzi ambao siyo zao la soko huria (kiutunzi) bali awamu ya Azimio la Arusha. Yaani, watunzi walioanza kuandika katika awamu ya Azimio la Arusha na wanaendelea kuandika katika awamu ya soko huria. Baadhi ya tamthilia hizo ni *Morani* (1993) ya Emmanuel Mbogo, *Amezidi* (1995) ya Said A. Mohamed, *Kaptula la Marx* (1998) ya Euphrase Kezilahabi. Nyingine ni *Kitumbua*

*Kimeingia Mchanga* (2000), *Amri ya Wakati* (2009) na *Mashetani Wamerudi* (2016) zote za Said A. Mohamed. Picha hii inaweza kuwaaminisha watu kuwa madai ya kwamba watunzi wa zama hizi za soko huria wamechangia kuua maendeleo ya ubunifu katika Tamthilia ya Kiswahili. Kauli ambayo inaweza kuwa siyo sahihi au ikawa ni sahihi.

Kwa mfano, Zúbková na wenzake (2009) walifanya utafiti kisha kuchapisha kitabu. Kitabu hiki ni uboreshwaji wa kitabu cha awali cha Elena Bertoncini Zúbková kinachoitwa *Outline of Swahili literature* (1989). Utafiti wao ulilenga kuwasilisha picha halisi kuhusu maendeleo ya Fasihi ya Kiswahili kwa tanzu mbili walizosiita kuwa tanzu ngeni katika fasihi ya Kiswahili. Tanzu hizo ni nathari bunilizi na tamthilia ambazo kwa maelezo yao zilipandikizwa katika tamaduni za wenyeji. Lengo la utafiti huo lilikuwa ni kuchunguza mafanikio ya upandikizwaji huo kiutunzi na kiusomwaji wa sanaa hizi miongoni mwa wenyeji wa Afrika Mashariki.

Kazi walizotathmini ni zile zilizochapishwa kuanzia mwishoni mwa miaka ya 1950 hadi mwaka 2008. Matokeo ya utafiti wao yameonesha kwamba kupandikizwa kwa nathari bunilizi na tamthilia katika tamaduni za wenyeji kifani na kimaudhui kulikuwa kugeni mwanzoni. Lakini kwa sasa, “ugeni” ule umegeuka “uwenyeji” katika Fasihi ya Kiswahili nchini Kenya, Tanzania Bara na Zanzibar. Chanzo hiki kina mahusiano ya karibu na utafiti wetu kwani kimegusa maendeleo ya Tamthilia ya Kiswahili nchini Tanzania kwa kiasi. Maana kimetazama fani na maudhui ya Fasihi ya Kiswahili katika vipindi tofauti tofauti vya historia ya Afrika Mashariki, Tanzania ikiwemo.

Naye Olali (2015) aliandika makala yanayotokana na utafiti wake kuhusu historia na maendeleo ya Tamthilia ya Kiswahili kuanzia mwaka 1957 hadi mwaka 2014. Makala haya yana mifano mingi ya tamthilia za Tanzania ambazo waandishi wake ni zao la Azimio la Arusha – kiutunzi. Pia, nyingi ya tamthilia hizo zimeandikwa katika kipindi cha Azimio la Arusha na chache wakati wa awamu ya soko huria. Alipotalii tamthilia ambazo zinaangukia katika miaka tunayoiita ya awamu ya soko huria, Olali anatumia mifano mingi kutoka watunzi na tamthilia za Kenya. Kisha anahitimisha makala yake kwa kusema, kuanzia katikati ya miaka ya 1980s, waandishi wa Kenya wamechangia kwa kiwango kikubwa uzalishaji wa tamthilia za Kiswahili. Lakini kwa upande wa Tanzania, kumekuwapo anguko la kisanaa katika uzalishaji wa kazi bunilizi za Kiswahili.

Pamoja na matokeo haya, tunadhani kitendo cha Olali (2015) kurejelea mifano mingi ya tamthilia za Kiswahili za upande mmoja, na kuacha mifano ya tamthilia za upande mwingine katika kipindi husika cha historia na maendeleo ya utanzu husika, kunaibua pengo la maarifa linalotusukuma kuchunguza ukweli wa hitimisho lake. Ndiyo maana, nasi tulilazimika kuchunguza tamthilia za vipindi viwili vya kihistoria nchini Tanzania ili kubaini kama kuna kushuka kwa ubunifu ama la. Kuchunguza maendeleo ya tanzu za Fasihi ya Kiswahili kwa jumla au pasipo urari wa data kunafinya uchunguzi kimawanda. Kwani hufanya utafiti usiweze kuzama zaidi katika kila utanzu ama kila eneo au kila kipindi katika umahususi wake. Kwa kuwa, kila utanzu, eneo na kipindi husika huwa na upekee wake katika msuko na uwasilishwaji - kifani na kimaudhui mbele ya wasomaji na makuzi ya sanaa husika (Ntarangwi, 2004).

Upekee huo ndio unaobeba umbo na kiwango cha ubunifu kilichonaksisha kazi husika. Kwa hiyo, bado pana umuhimu wa kuchunguza namna ubunifu katika dhamira na matumizi ya lugha yalivyoteuliwa na kusanwa katika Tamthilia ya Kiswahili ya awamu ya Azimio la Arusha na awamu ya soko huria ili kubaini kama kuna maendeleo endelevu kiutunzi ama la. Tunahitimisha udurusi wa maendeleo ya Tamthilia ya Kiswahili katika awamu ya Azimio la Arusha na awamu ya soko huria kwa nukuu kutoka kwa Ntarangwi (2004) anayesema:-

[...] tamthilia kama tuijavyo leo imepitia mikondo mbalimbali. Hili ni jambo la kawaida katika fasihi yoyote kwani kila fasihi na tanzu zake, hubadilika, kwa hivyo twapata mabadiliko ya tamthilia kutoka hali ya awali hadi ilivyo kwa hivi sasa. [...]. Katika Fasihi ya Kiswahili vichekesho na kutumbuiza viligeuka na kuwa maigizo ya kuwacheka Waafrika walioazimia kuwa wazungu. Hatimaye maudhui mazito ya kihalisia yakachukua nafasi ya vichekesho na watunzi wakaanza kutunga tungo zenye maudhui mazito zaidi. Hata hivyo, kila kipindi cha kihistoria kina mifano mbalimbali ya kazi za tamthilia. Hivyo basi, hatuwezi kusema kuwa ni aina moja tu ya tamthilia inayopatikana katika kipindi maalumu cha historia” (uk. 41 - 42).

#### **2.4 Tafiti Tangulizi kuhusu Tamthilia Teule**

Utafiti huu ulipitia tafiti mbalimbali tangulizi zinazohusiana na tamthilia sita (6) teule za utafiti wetu. Mpangilio wa uwasilishaji umegawa sehemu hii katika awamu mbili teule za utafiti huu. Sehemu ya kwanza ni ya tamthilia teule za awamu ya Azimio la Arusha na sehemu ya pili ni ya tamthilia teule za awamu ya soko huria. Katika kila awamu, uwasilishaji umezingatia historia ya ukongwe wa tamthilia husika. Yaani, kihistoria, tamthilia ipi ilianza kuchapishwa.

#### **2.4.1 Tafiti kuhusu Tamthilia Teule za Awamu ya Azimio la Arusha**

Sehemu hii inatalii tafiti tangulizi kuhusu tamthilia teule za utafiti huu. Katika sehemu hii tumejadili angalau tafiti tatu zilizofanyika kuhusu mwandishi wa tamthilia teule. Katika uwasilishaji, tumeanza na mapitio ya tamthilia za Ebrahim N. Hussein. Kisha zimefuata za Amandina Lihamba, Penina Mhando, na Ndyanao Balisidya (kama kundi) na kuhitimisha utalii wetu kwa zile za Ngalimecha Ngahyoma.

Mukobwa (1985) alichunguza maendeleo ya kimaudhui katika tamthilia tano zilizoandikwa na Ebrahim N. Hussein kati ya mwaka 1967 na mwaka 1981. Tamthilia hizo ni *Kinjeketile*, *Wakati Ukuta*, *Alikiona*, *Mashetani* na *Arusi*. Katika *Kinjeketile*, mtafiti alibaini kwamba tamthilia hii inasawiri historia ya vita vya Maji Maji dhidi ya ukoloni na ubeberu wa Mjerumani. Vilevile aligundua kuwa tamthilia ya *Wakati Ukuta* na ile ya *Alikiona* zote kwa pamoja zinaakisi matokeo ya athari za mfumo wa kiuchumi na kibepari katika kipindi cha ukoloni mamboleo. Ilhali, katika *Mashetani* na *Arusi* alibaini kwamba zote mbili zina mjadala mpana juu ya masuala mazito yanayogusa uchumi, siasa, itikadi na utamaduni. Mukobwa amehitimisha kwa kusema ya kwamba, utunzi wa Ebrahim N. Hussein ulifungamana na mifumo halisi ya maisha ya watu katika kipindi husika cha kihistoria lakini maudhui yaani dhamira na mvuto wa kazi husika vinaishi hadi kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

Kwa hiyo, umuhimu wa tamthilia hizi kidhamira bado ni mkubwa kwa zama hizi kwani unafungamana na maisha ya leo ya wanadamu. Tamthilia hizi zitaendelea kuishi na umuhimu wa kuzisoma utabakia palepale ijapokuwa zilitungwa zamani. Pamoja na Mukobwa kujikita katika kuchunguza maudhui hasa dhamira, ni dhahiri

kwamba maudhui hubebwa na lugha. Kwa hiyo kutokuguswa kwa matumizi ya lugha katika utafiti wake kama kipengele mahususi cha kutafitiwa kulitufanya tubaki na kiu ya kujua ubunifu wa Ebrahim N. Hussein katika kuiteua na kuisana lugha. Aidha, utafiti huu unahusiana na utafiti wetu kwa sababu umehusisha tamthilia ya *Mashetani* ambayo ni miongoni mwa kazi teule za utafiti wetu. Hivyo, utafiti huu ni daraja muhimu katika kuonesha namna tamthilia za awamu ya Azimio la Arusha zilivyoubwa kwa kulinganishwa na zile za awamu ya soko huria.

Naye S. M. A. Massoud (2013) alifanya utafiti linganishi kuhusu maudhui na fani katika tamthilia za Kiswahili za *Mashetani* ya Ebrahim N. Hussein na *Kivuli Kinaishi* ya Said Ahmed Mohamed. Lengo la utafiti huu lilikuwa kuchunguza jinsi gani wasanii huweza kufanana ama kutofautiana katika kuteua na kutumia vipengele vya mtindo ili kuyaumba maudhui na fani ya kazi zao. Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kwamba, watunzi hao wametoka katika mazingira tofauti ya kijografia na kiwakati. Hata hivyo, kwa upande mmoja, wamethibitika kufanana katika uteuzi na aina ya maudhui. Maudhui hayo yanagusa historia, itikadi, hali ya kiuchumi, kijamii, kisiasa na kiutamaduni. Kwa upande mwingine, watunzi hawa wanaonekana kutofautiana na kufanana katika mbinu za kimtindo zilizojenga kazi zao. S. M. A. Massoud (2013) anathibitisha kuwapo kwa ubunifu katika uteuzi na ujenzi wa kazi zote mbili. Na kwamba, kazi hizi zote zimetajirishwa kwa wingi wa majaribio ya kifani huku matumizi ya lugha yakisheheni taswira. Kwa mwono wa S. M. A. Massoud (2013), utunzi wa Mohamed ni kana kwamba una sura ya kuwa Mohamed alijaribu kutembea katika usemezano wa kifani wa Hussein.



Pamoja na utafiti huu kuchunguza kufanana na kutofautiana kwa tamthilia teule katika eneo la maudhui na mtindo, bado tuliona kuna haja ya kuchunguza maendeleo ya ubunifu wa ujenzi wa dhamira na matumizi ya lugha katika Tamthilia ya Kiswahili katika awamu ya Azimio la Arusha na awamu ya soko huria kwa kutumia utafiti linganishi. Lengo likiwa ni kubainisha kama kuna kufanana au kutofautiana kiubunifu. Tunatambua kuwa kazi zote zimebainika kuwa na wingi wa majaribio na taswira, lakini viwango vya ubunifu huo havijaoneshwa. Kazi zote mbili na waandishi wake ni sehemu ya awamu ya Azimio la Arusha, zenye kuelezea usaliti na unafiki wa viongozi kwa wananchi wanyonge kwa kutumia lugha ya picha.

Kwa hiyo, utafiti huu unatofautiana na ule wa S. M. A. Massoud (2013) kwa sababu katika utafiti wake hakushughulikia awamu ya soko huria kwa vile haikuwa sehemu ya malengo na mipaka ya utafiti wake. Kwa muktadha wa utafiti wetu, mbali na awamu ya Azimio la Arusha tunakwenda kuzingatia tamthilia zilizochapishwa awamu ya soko huria. Huku waandishi wake wakiwa ni kizazi cha awamu ya soko huria kisanaa. Aidha, utafiti wetu haukujihusisha na tamthilia ya *Kivuli Kinaishi* kwa sababu siyo sehemu ya kazi teule za utafiti huu. Ijapokuwa, nayo inaangukia katika kipindi cha awamu ya Azimio la Arusha. Hivyo, utafiti huu ulikuwa na umuhimu kwa sababu awamu ya soko huria kupitia watunzi wake haijapewa nafasi kubwa miongoni mwa watafiti tangulizi. Hivyo, tuliona kuna haja kubwa ya kuchunguza maendeleo ya tamthilia za Kiswahili za awamu ya soko huria kwa kuzilinganisha na zile za awamu ya Azimio la Arusha.

Utafiti mwingine uliofanyika kuhusu tamthilia ya *Mashetani* ni ule wa S. S. Massoud (2018). S. S. Massoud (2018) alitathmini kwa kulinganisha matumizi ya mtindo na

dhamira katika tamthilia za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi*. Lengo la utafiti wake lilikuwa ni kubainisha, kulinganisha na kulinganua matumizi ya mtindo na dhamira zinazojitokeza katika tamthilia teule. Matokeo ya utafiti wake yanaonesha kwamba, tamthilia hizi zina dhamira na mtindo ukiwemo ule wa lugha unaofanana. Lakini kuna tofauti ndogo katika mtindo ambapo *Mashetani* imetumia mbinu ya mchezo ndani ya mchezo. Mbinu hii haimo katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*. Na kwamba, tamthilia zote mbili zimezingatia ubunifu katika mtindo na dhamira zinazokwenda na wakati.

Utafiti huu ni wa mwaka 2018 lakini kazi zote mbili zilizotafitiwa ni zao la watunzi wa awamu ya Azimio la Arusha - kimakuzi. *Mashetani Wamerudi* ni tamthilia iliyotungwa na Said A. Mohamed na kuchapishwa mwaka 2016. Kiumri, tamthilia hii ni ya awamu ya soko huria lakini mtunzi wake siyo zao la soko huria bali awamu ya Azimio la Arusha. Hali inayotusukuma kubaini kuwapo kwa haja ya kuchunguza maendeleo ya ubunifu wa Tamthilia ya Kiswahili kwa kulinganisha matumizi ya lugha na dhamira za tamthilia zinazotokana na watunzi chipukizi katika kila awamu. Kwa sababu, mbali na malengo na mipaka ya utafiti wa S. S. Massoud, bado naye amejifungia katika watunzi wa awamu ya Azimio la Arusha ambao ni sehemu moja tu ya awamu tunazoshughulika nazo.

Kwa upande wa tamthilia ya *Kijiji Chetu*, Mochiwa (1978) alichunguza na kubaini dhamira zinazopatikana katika tamthilia ya *Kijiji Chetu*. Kupitia makala yake, Mochiwa anabainisha na kuwasilisha dhamira tatu (3) ambazo ni uongozi, uvivu, pia ujamaa na ndoa. Dhamira hizi zinaonekana kujitokeza pia kwa Kiango (1988). Hata hivyo, tunadhani ndani ya tamthilia hii ya *Kijiji Chetu*, mna dhamira zaidi ya hizi

tatu (3) zilizobainishwa na Mochiwa, au zaidi ya zile zilizobainishwa na Kiango. Hata hivyo, Mochiwa hakutalii matumizi ya lugha, kipengele ambacho utafiti huu uliona kuna umuhimu mkubwa wa kukishughulikia. Hivyo, Haya mawili – idadi ya dhamira na kutokuwapo kwa kipengele cha matumizi ya lugha, yanatusukuma kupata shauku ya kujua zaidi kuhusu uteuzi na ujenzi wa dhamira na matumizi ya lugha bunilizi katika tamthilia hii ya *Kijiji Chetu*.

Naye, Kiango (1988) alifanya uchambuzi wa tamthilia ya *Kijiji Chetu*. Uchambuzi wake ulitalii dhamira, wahusika, mandhari na jina la tamthilia. Uchambuzi wake haukutalii matumizi ya lugha. Kiango alibainisha dhamira tano (5) ambazo ni ujenzi wa jamii mpya, uongozi, uvivu, ujamaa na ndoa, na nafasi ya mwanamke ambayo aliita picha ya mwanamke. Hata hivyo, utafiti wake haukuzingatia matumizi ya lugha na jinsi yanavyoibua dhamira hizo. Hivyo, kwa kutokuchunguza matumizi ya lugha kunaibua uhitaji wa kujua namna mwandishi alivyoteua na kuisana tamthilia husika. Kwa sababu, lugha ndicho chombo kinachoitambulisha kazi husika kwa jamii (Senyamanza, h. m.). Vilevile, kwa mujibu wa Senkoro (1982), fani na maudhui ni vitu visivyotenganishika kiutunzi. Kwa hiyo, utafiti huu uliona kuna haja ya kuchunguza kipengele cha lugha ili kubaini aina na namna dhamira na matumizi ya lugha yalivyosanwa katika tamthilia hii.

Tofauti na ilivyo kwa tamthilia ya *Mashetani* kuwa na tafiti nyingi zinazoihusu, mtafiti hakufanikiwa kupata tafiti zaidi zilizochunguza ubunifu wa dhamira na matumizi ya lugha katika tamthilia ya *Kijiji Chetu*. Changamoto ya upatikanaji wa tafiti tangulizi zinazohusiana na tamthilia teule za awamu ya Azimio la Arusha imejitokeza pia kwa tamthilia ya *Harakati za Ukombozi*. Mtafiti hakufanikiwa kupata

utafiti hata mmoja unaohusiana na tamthilia hii. Hali hii inatoa picha kuwa, yawezekana ripoti hizo zipo lakini mtafiti hakufanikiwa kuzifikia au hazipo kabisa. Hivyo, tuliona kuna haja kubwa ya kuzitafiti tamthilia hizi. Katika mjadala huu tumezitalii tafiti tangulizi zinazohusu tamthilia teule za awamu ya Azimio la Arusha. Kwa hiyo, kipengele kinachofuata kimetalii na kuwasilisha yaliyojili kuhusu tafiti tangulizi za awamu ya soko huria.

#### **2.4.2 Tafiti kuhusu Tamthilia Teule za Awamu ya Soko Huria**

Sehemu hii ilikusudiwa kubeba ripoti ya tathmini ya tafiti tangulizi juu ya tamthilia tatu (3) teule za awamu ya soko huria. Tamthilia hizo ni *Safari ya Chinga*, *Changamoto* na *Nje – Ndani*. Mbali ya mtafiti kutembelea maktaba na, au makavazi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Dodoma, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania na Maktaba Kuu ya Taifa – Dar es Salaam ili kupata tafiti zaidi, bado aligonga mwamba. Hivyo, juhudi za mtafiti zikahamia kusaka tafiti zilizowekwa mkondoni zenye kufungamana na tamthilia sita (6) teule, bado huko nako alifanikiwa kupata tafiti nyingi zinazohusiana na tamthilia ya *Mashetani* huku tamthilia zilizobakia zikisalia kutokuwa na tafiti tangulizi – isipokuwa kwa tamthilia ya *Kijiji Chetu* iliyofanikiwa kuwa na ripoti mbili (2).

Hali hii inaibua mitazamo miwili. Mtazamo wa kwanza ni kwamba, upo uwezekano wa kuwapo kwa tafiti zilizojishughulisha na tamthilia teule tunazozishughulikia lakini mtafiti ameshindwa kuzifikia. Mtazamo wa pili ni kuwa, kuna uwezekano tamthilia hizi teule hazijafanyiwa utafiti kabisa. Kama ni kweli, kwamba tamthilia hizi tatu hazijachunguzwa kabisa, basi kuna umuhimu wa kuzichunguza ili kubaini ubunifu wa watunzi wa awamu ya soko huria katika vipengele teule vya dhamira na

matumizi ya lugha. Kisha kulinganisha vipengele teule vya dhamira na matumizi ya lugha ya tamthilia hizi teule dhidi ya tamthilia teule za Kiswahili za awamu ya Azimio la Arusha. Lengo likiwa ni kubaini kama kuna kufanana na kutofautiana kwa ubunifu ili kutambua ukweli wa madai tuliyoyatambulisha katika usuli na tamko la utafiti juu ya ukuaji na ustawi wa Tamthilia ya Kiswahili nchini Tanzania.

## **2.5 Pengo la Maarifa**

Tafiti tangulizi tulizozitalii zinaonesha kuwapo kwa tafiti kadha wa kadha zenye kuhusiana na tamthilia ya *Mashetani* na mbili kuhusiana na tamthilia ya *Kijiji Chetu*. Utafiti haukufanikiwa kupata tafiti zaidi juu ya tamthilia ya *Kijiji Chetu*. Pia, hatukufanikiwa kupata kabisa tafiti zinazohusiana na tamthilia ya *Harakati za Ukombozi* ambayo ni sehemu ya utunzi wa tamthilia za Kiswahili za awamu ya Azimio la Arusha. Aidha, hatukufanikiwa kabisa kuzifikia tafiti tangulizi zinazohusiana na tamthilia teule ambazo watunzi wake ni zao la awamu ya soko huria - kiutunzi. Yawezekana ripoti hizo zipo au hazipo.

Kama zipo, basi tatizo limekuwa ni upatikanaji wake. Kwa sababu, kiuhalisi siyo rahisi kwa mtu kusafiri kila mahali na kila wakati ili kukusanya kila kitu kinachohusiana na ripoti za utafiti juu ya jambo fulani (rej. Kezilahabi, 1995; Simala, 2002). Baada ya kuzitalii tafiti tangulizi tulizoziwasilisha hivi punde tulibaini kuwa hakuna utafiti linganishi ambao umefanyika kwa lengo la kuchunguza na kulinganisha maendeleo ya ubunifu ya tamthilia za awamu ya Azimio la Arusha na soko huria kwa kumakinikia tamthilia sita (6) teule tulizozichunguza. Hivyo, utafiti huu uliona kuna haja ya kufanya utafiti wa kina ili kuziba pengo hili. Katika kuziba pengo hili, utafiti huu ulichunguza maendeleo ya ubunifu wa dhamira na matumizi

ya lugha katika Tamthilia ya Kiswahili katika awamu ya Azimio la Arusha na awamu ya soko huria kwa kutumia utafiti linganishi. Lengo lilikuwa ni kubaini kama kuna ubunifu endelevu ama la.

## **2.6 Kiunzi cha Nadharia**

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Fasihi Linganishi ili kuchunguza ubunifu wa dhamira na matumizi ya lugha katika Tamthilia ya Kiswahili katika awamu ya Azimio la Arusha na awamu ya soko huria ili kubaini kama kuna ubunifu endelevu ama la. Sperger (1921, katika Cao, 2013), Tieghern (1931, katika Cao, 2013) na Guyard (1951, katika Cao, 2013) na Carrer (1987, katika Cao, 2013) wanaitazama Fasihi Linganishi kama mchakato wa ujarabati na udhahiri wa mambo kwa kuzingatia historia ya mahusiano ya kijamii na kifasihi katika ngazi ya kitaifa na kimataifa. Tieghern (katika Cao, 2013) anaiona Fasihi Linganishi kama mkabala wa sayansi ya kihistoria unaobainisha kwa mapana uwezekano wa kuwapo ukweli wenye sura tofauti tofauti katika matini. Mhakiki anayeutumia nadharia hii kuongoza uchambuzi, hana budi kuanza na ufafanuzi wa kila msingi wa ukweli. Kisha, kutumia msingi wa maarifa hayo kugundua sababu za athari kuu ya mwonekano wa matini husika.

Naye Guyard (katika Cao, 2013) anaongeza ya kwamba, Fasihi Linganishi siyo ulinganishaji wa fasihi bali ni kuzingatia historia ya mahusiano ya fasihi kitaifa na kimataifa. Aidha, Carrer (katika Cao, 2013) anaitazama Fasihi Linganishi kama tawi la fasihi historia linalochunguza kwa kina mahusiano ya kimataifa, yenye mawasiliano ya dhati yanayohusisha pande mbili au zaidi za sanaa. Mawasiliano hayo ni kati ya kazi na kazi, pia misukumo na maisha ya waandishi wa fasihi kadhaa

ndani na nje ya mipaka ya fasihi hizo. Cao (2013) anatambulisha Fasihi Linganishi kama nadharia ya kifasihi na uhakiki ambayo asili na chimbuko lake ni nchini Ufaransa kabla ya kuboreshwa na wanataaluma kutoka Marekani.

Kwa utangulizi huu, tunapata kujua kuwapo kwa makundi mawili makuu ya Wanafasihi Linganishi - kundi la wanataaluma wa Kifaransa na kundi la wanataaluma wa Kimarekani. Waasisi wa nadharia hii ni Balden Sperger na Paul Van Tieghern. Baadhi ya waumini wa nadharia hii ni Marius-Francois Guyard na Jean-Marie Carrer. Kwa mujibu wa Cao (2013), kundi la wanataaluma wa Kifaransa lilisisitiza uzingatiaji wa mambo yanayoonekana na kujulikana vema miongoni mwa wanadamu. Na kwamba, mhakiki anapochunguza historia ya mahusiano ya fasihi hana budi kuzingatia mambo matatu. Nayo ni: (i) kuchunguza safari na athari ya vitu vya kifasihi kwenye fasihi za kigeni. (ii) Kuchunguza safari na athari ya waamuzi na vyombo vya kupashana habari mfano wakalimani na wafasiri, wahakiki, wanataaluma, wasafiri au nyaraka kama vitabu na majarida. Na (iii) kuwatambua waandishi kama wapokeaji na wachunguzi wa vyanzo vya athari wanazokumbana nazo.

Kwa upande mwingine, Cao (2013) anafafanua kwamba, wanataaluma wa Kimarekani hutofautiana kidogo na wale wanataaluma wa Kifaransa. Wanataaluma wa Kifaransa wanaamini katika falsafa ya mahusiano ya kihistoria na yenye ukweli lakini wenzao wa Kimarekani wanaamini katika ufafanuzi wa kisanaa na tathmini. Wanataaluma wa Kimarekani wanaiona Fasihi Linganishi kuwa ni zaidi ya mipaka iliyowekwa kinchi. Pia, wanaamini katika uchunguzi wa mahusiano baina ya fasihi kwa upande mmoja na eneo jingine la maarifa na imani. Maeneo hayo ni pamoja na:

sanaa, falsafa, historia, sayansi za jamii, sayansi, dini, na kadhalika. Faukwa ya hayo, wanataaluma wa Kimarekani wanaitazama Fasihi Linganishi kuwa aina ya ulinganifu mtambuka unaovuka mipaka ya nchi na taaluma.

Kundi hili la wanataaluma wa Kimarekani linapigia chapuo uchunguzi unaolinganisha vitu vyenye haiba ya namna moja (*analogy*). Msisitizo wao umekita zaidi katika uchunguzi wa ndani wa umbo la kifasihi ili kubainisha kama kazi husika ina uhalali wa kuhesabika kuwa ni kazi ya kifasihi (*literariness*) au la. Kwa hiyo, wanatilia mkazo katika kuchunguza uainishaji na namna waandishi wa mataifa na nyakati tofauti wanavyotazama jambo lile lile moja, mfano motifu, hali na ishara. Ili kufanikisha uhakiki kwa mujibu wa wanataaluma wa Kimarekani, uchunguzi husika ni lazima uzingatie mambo kadhaa. Mathalani: (i) kulinganisha kazi za kisanaa za mataifa, watunzi na nyakati tofauti tofauti, (ii) kulinganisha kati ya kazi za kifasihi na zisizokuwa za kifasihi, (iii) kubainisha viwango vya ujumi vinavyofanana, na (iv) kutambua kanuni jumuishi katika fasihi na maendeleo ya kifasihi (Cao, 2013).

Ufafanuzi wa wataalamu hawa wote unaelezwa vema na Jilala (2016). Kimuhtasari, Jilala anaeleza kuwa Fasihi Linganishi haijishughulishi na kuuliza “nini.” Badala yake hutafuta kujibu maswali: Kwa vipi? Ya nini? Kwa nini? Lini? na wapi? Jilala anaendelea kutanabaisha kuwa, lengo la Fasihi Linganishi kama mbinu ya kisanaa, ni “kuibua vipengele vinavyofananisha, kutofautisha na kuhusianisha kazi za fasihi za ulimwengu na Fasihi Linganishi za jamii mahususi” (uk. 140). Tunapobeba jukumu la kulinganisha kazi za fasihi, hatuna budi kutii “kanuni, sheria, mbinu na matokeo ya utafiti wa kisayansi (uk. 140)” ili kutoa hitimisho la kufanana au kutofautiana kazi za sanaa kisayansi.



Kwa mujibu wa Jilala, mhakiki au mtafiti hana budi kusoma matini moja baada ya nyingine kwa utulivu na umakini wa hali ya juu. Kisha, kuzirudia mara kadhaa huku akimakinikia zaidi na zaidi. Umakiniko huo ni sharti uwe na dira. Kama amekusudia kuchunguza maudhui na fani iliyotumika kusana kazi teule, basi mhakiki au mtafiti aanze na eneo moja kabla ya jingine. Mathalani, aanze kuangalia vipengele vyote teule vya maudhui atakavyovimakinikia katika kila kazi teule. Jilala anaendelea kueleza kuwa, mhakiki au mtafiti akishamaliza kusoma maudhui, sasa anaweza kugeukia vipengele vya fani atakavyovimakinikia katika kazi teule. Majibu ya uchunguzi huo ni sharti yariptiwe kwa kuambatisha ushahidi wa nukuu, ukurasa, majibu ya usaili na tafiti nyingine zilizogusa ukweli wa ulinganishaji teule. Mchunguzi anafanya hivi ili kushadadiza hoja ya kuwapo kwa athari, uigaji, upokezi na upya wa kile anachokimakinikia.

Katika utafiti huu tulichagua kutumia nadharia ya Fasihi Linganishi kuongoza utafiti wetu kwa sababu mawanda yake yanajumuisha mawanda ya nadharia nyingine nyingi. Kwa mantiki kwamba, kutafti kwa kutumia nadharia ya Fasihi Linganishi kunaruhusu kulinganisha na kuchambua matini ya kifasihi ya mwandishi mmoja dhidi ya matini yake nyingine au dhidi ya matini ya mwandishi mwingine ndani na, au nje ya nchi moja. Nadharia hii humsukuma mwandishi kutathmini vyanzo na athari ya kile kilichoelekezwa na mwandishi kwa jamii ya watu au watunzi wengine. Kwani, uchunguzi na tathmini hiyo haina budi kulinganisha kwa kuzingatia vigezo anuai kama vile kigezo cha kijiografia, kiwakati, kihistoria, upokevu na athari yake kwa jamii ya fasihi iliyoathiriwa (Zepetnek, 1998).

Zepetnek (1998) anaendelea kusema, nadharia ya Fasihi Linganishi haichagui upande wa kimkabala pindi inapoongoza uhakiki na utunzi wa matini. Bali yenyewe huchunguza vipengele vyote vya kidhima, kifani na kimaudhui tofauti na nadharia nyingi zenye mkito mahususi katika eneo moja tu la uhakiki. Mfano wa nadharia za mkito mahususi ni Uhistoriampya, Mwitiko wa Msomaji, Umaksi, Ufeministi, Unegritudi, Uhakikimpya, kutaja kwa uchache. Naye Villanueva (2011) anaongeza kuwa, Fasihi Linganishi inampa mchunguzi msukumo wa pekee kusaka maarifa ambayo hata yeye mwenyewe hakuwa anayajua hapo awali. Na kwamba, kwa kufanya hivyo mchunguzi huipa mawanda mapana kazi yake hata ikaweza kuwa bora kwa faida ya wasomaji na taaluma anayoishughulika.

Pamoja na uzuri wa kipekee wa matumizi ya nadharia ya Fasihi Linganishi, Zepetnek (1998) anaeleza kwamba, matumizi ya nadharia hii huwa na changamoto kwani watu wawili au zaidi wanaweza kutathmini jambo moja na kuhitimisha hoja kwa kauli zinazokinzana. Hali hii hutokana na ukweli kwamba ni vigumu kudhibiti kwa asilimia 100 mtazamo na utashi binafsi wa mchunguzi katika kuamua mwelekeo wa matokeo ya kile kilicholinganishwa. Naye Villanueva (2011) anaongeza kwamba, kama mchunguzi hana utamaduni wa kufuatilia mambo kwa karibu na kina sana – yawe ni andishi, picha au simulizi hataweza kukidhi mawanda ya uchunguzi wa kisayansi kupitia nadharia ya Fasihi Linganishi. Hii ni kwa sababu, mchunguzi hataweza kujibu maswali ya msingi ya kihistoria, kijografia na kisayansi yenye kufungamana na matini anayoshughulikia. Kwa mantiki hii, mtafiti anayeamua kutumia nadharia ya Fasihi Linganishi ni sharti ajitoe mhanga kusoma, kusikiliza, kutazama na kuuliza kila chanzo cha kihistoria cha kila kipindi katika jamii husika.

Kwa upande wake Cao (2013) anaona kwamba uhakiki kwa kutumia Fasihi Linganishi hauwezi kuwa mkamilifu endapo utajiegemeza kwenye mlengo wa Wafaransa na ule wa Wamarekani pasipo kutambua nafasi ya nadharia ya Mwachano (*theory of variation*). Kwa sababu, nadharia ya Mwachano inasisitiza uchunguzi na uainishaji wa viwango vya kubadilika kwa fasihi kutokana na hali mpya ya mageuzi katika jamii zinazolingiliana na kuathiriana. Cao anaongeza kwamba, hali hii inatokana na ukweli kuwa katika zama hizi Fasihi Linganishi imebadilika kutoka jukwaa la kutafuta ufanano hadi kuwa jukwaa la kutafuta utofauti au vyote viwili. Cao anahitimisha hoja yake kwa kusema, uchunguzi kwa kutumia nadharia ya Fasihi Linganishi ni sharti uhusishe hali ya mabadiliko ya kijamii na sababu za utokeaji huo hata kuathiri watunzi na fasihi husika kama inavyosisitiza nadharia ya Mwachano.

Pamoja na udhaifu huu wa nadharia ya Fasihi Linganishi, haukuwa kikwazo kwetu kutumia nadharia ya Fasihi Linganishi kama kiunzi teule cha utafiti wetu. Kwa sababu, kwa mujibu wa Mushengyezi (2003) na Eagleton (2008), hakuna nadharia hata moja yenye ukamilifu kamili kimatumizi. Kwa kuwa, kila nadharia ina ukomo wake kimawanda. Na, kutumia nadharia zaidi ya moja hakumaanishi kwamba ukamilifu utakuwa wa asilimia 100 kwa sababu kila nadharia ina mkito katika jambo mahususi. Kwa hiyo, kwa kuzingatia faida za nadharia ya Fasihi Linganishi kimawanda na kimatumizi, tuligundua kuwa ina ufaafu wa kiwango cha juu kwetu. Kwa vile nadharia hii inagusa vipengele vingi vya uhakiki kifani na kimaudhui kwa kufungamanisha na mazingira halisi ya makuzi na ustawi wa jamii na fasihi yake. Vilevile, nadharia ya Fasihi Linganishi ina nafasi kubwa ya kuonesha kwa uangavu namna, kiwango, athari na hali ya ubunifu inavyofungamana na matukio ya kijamii

katika vipindi tofauti tofauti vya kijamii, kiuchumi, kisiasa, kijografia na kiutamaduni kama anavyobainisha Jilala (2016).

Tunasema nadharia hii ilikuwa na nafasi kubwa kwa utafiti huu kwa sababu, kwa Mwanafasihi Linganishi; hakuna mahusiano ya kiajali katika kufanana na kutofautiana kwa matini ya kisanaa - ndani na nje ya wakati husika, mazingira husika na mifumo husika ya maisha ya watu nyanjani (Zepetnek, 1998). Zepetnek (1998) anafafanua kuwa, mahusiano yote ya kisanaa na kijamii ni matokeo ya michakato ya maisha inayoaksi kukua, kustawi au kudumaa kwa mwanadamu na mfumo wake wa kuishi. Na kwamba, michakato hiyo ni zao la ama nguvu za maumbile asili au utashi wa mwanadamu husika. Kwa kutambua haya, ni dhahiri kwamba nadharia ya Fasihi Linganishi ilituongoza katika kulinganisha kazi za awamu mbili tofauti ili kupata majibu ya kina juu ya hoja kuwa Tamthilia ya Kiswahili nchini Tanzania imedumaa kiubunifu katika awamu ya soko huria tofauti na hali ilivyokuwa wakati wa awamu ya Azimio la Arusha.

Hata hivyo, hatuwezi kupuuza mapungufu ya nadharia ya Fasihi Linganishi hata kidogo. Kwa hiyo, katika kudhibiti mapungufu ya nadharia hii, mtafiti alihakikisha kanuni za utafiti wa kisayansi zinazingatiwa. Lengo lilikuwa kuondoa uwezekano wa mwandishi kupotosha taarifa au kuegemea upande fulani kwa maslahi yake kinyume na kaida za utafiti wa kisayansi. Udhibiti huu ulifanyika mbali na mambo mengine, kwa kusoma, kutazama na kusikiliza kwa makini sana vyanzo rasmi vya taarifa vingi kadri alivyoweza ili kupata maarifa, stadi na utamaduni halisi wa jamii ya Watanzania na nje ya Tanzania. Pia, miiko ya utafiti wa kisayansi ilizingatiwa wakati wa uchambuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti. Kwa hiyo, malengo

yote matatu yalitafitiwa chini ya kiunzi kimoja cha utafiti ambacho ni nadharia ya Fasihi Linganishi kama ilivyofafanuliwa na wanataaluma tuliowarejelea.

## **2.7 Hitimisho**

Sura hii imeonesha uhusiano kati ya tatizo la utafiti lililoelezwa katika sura ya kwanza na namna maandiko mbalimbali yalivyosaidia kujenga msingi na haja ya kufanyika kwa utafiti huu. Kupitia maandiko tuliyoyatalii ni dhahiri kuwa, mada yetu tuliyoitafiti haijafanyiwa tafiti za kutosha. Mapitio ya maandiko na kiunzi cha nadharia ni egemeo na mwongozo kwa ajili ya sura ya kwanza na sura zinazofuatia. Sura inayofuata inajishughulisha na mbinu za utafiti ili kuonesha jinsi utafiti huu ulivyofanyika.

## **SURA YA TATU**

### **MBINU ZA UTAFITI**

#### **3.1 Utangulizi**

Sura hii imejikita katika kuelezea namna utafiti ulivyofanyika. Sura imemakinia maeneo yafuatayo ya kiutafiti: usanifu wa utafiti, wango wa utafiti, sampuli na usampulishaji, mbinu za kukusanyia data, mbinu za uwasilishaji na uchambuzi wa data, uzingativu wa masuala ya kiitikeli na hitimisho la sura. Ufafanuzi wa vipengele hivi ulisaidia sana kujenga na kuonesha dira ya namna mtafiti alivyopaswa kulifikia lengo kuu la utafiti lengwa.

#### **3.2 Usanifu wa Utafiti**

Utafiti huu ulikuwa ni wa maktabani. Utafiti wa maktabani siyo kitendo cha kuketi katika jengo linaloitwa maktaba, bali ni muundo wa utafiti ambao mtafiti huutumia kukusanya data kutokana na usomaji wa nyaraka na, au utazamaji na usikilizaji wa taarifa zilizohifadhiwa kwa njia ya maandishi, picha na sauti zilizorekodiwa badala ya kwenda uwandani kuwauliza watu (Kothari na Gaurav, 2019). Mtafiti alichagua mfumo huu kutokana na mahitaji ya msingi ya asili ya utafiti wenyewe. Kwa mantiki kwamba, utafiti wetu ulilenga kufanya mambo makuu matatu (3). Lengo la kwanza lilikuwa ni kulinganisha ubunifu katika dhamira zinazojitokeza katika tamthilia teule za Kiswahili za awamu ya Azimio la Arusha na zile za soko huria ili kubaini kama kuna ubunifu endelevu. Lengo la pili lilikuwa ni kulinganisha ubunifu katika matumizi ya lugha yanayojitokeza katika tamthilia teule za Kiswahili za awamu ya Azimio la Arusha na zile za soko huria ili kubaini kama kuna ubunifu endelevu. Na, lengo la tatu lilikuwa kutathmini athari ya ubunifu katika dhamira na matumizi ya

lugha yanayojitokeza katika tamthilia teule za Kiswahili za awamu ya Azimio la Arusha na zile za soko huria ili kubaini namna zinavyochochea maendeleo endelevu ya Tamthilia ya Kiswahili kisanaa.

Hivyo, ukichunguza malengo yote ya utafiti huu utaona kuwa hakuna lengo ambalo lilihitaji data za uwandani. Badala yake, kila lengo lilitutaka kuketi na kusoma nyaraka kwa njia ya usomaji makini ili kubaini kama kuna uendelevu wa dhamira na matumizi ya lugha, kiubunifu. Kwa msingi huu basi, mtafiti aliona hana budi kuufungamanisha utafiti wake na maktaba kwa asilimia 100. Kwa maana hiyo sababu ya kuchagua utafiti huu kuwa wa maktabani ni asili ya utafiti wenyewe ambao unahitaji usomaji makini zaidi ili kupata data. Kama utafiti huu ungepelekwa uwandani ukiwa na malengo mahususi haya, basi mtafiti angepaswa kujiridhisha ili kuona kama watafitiwa wana maarifa muhimu kuhusiana na kila tamthilia teule. Hali ambayo ingempa changamoto mtafiti. Kwa sababu, kwa mujibu wa Senkoro (1995), Watanzania wengi hawana utamaduni wa kuthamini ama kununua na, au kujisomea maandiko; fasihi ikiwemo.

### **3.3 Wango wa Utafiti**

Kwa mujibu wa Kothari na Gaurav (2019), wango wa utafiti ni mahali ama pa kijiografia au kimatini ambapo mtafiti atapateua ili kupatumia kukusanya data. Wango wetu ulioteuliwa ni tamthilia za Kiswahili za Tanzania zilizochapishwa kati ya mwaka 1967 na 2016. Miaka hii imeteuliwa ili kuleta uwiano sahili wa vipindi teule vya kihistoria nchini Tanzania. Vipindi hivyo ni awamu ya Azimio la Arusha (1967 - 1991) na awamu ya soko huria (1992 - 2016). Kila awamu ina jumla ya miaka 25. Eneo hili lilitoteuliwa ili kuwezesha upatikanaji wa data zilizokusudiwa

kujibu madai yasiyorasmi. Madai hayo ni kuwa, watunzi chipukizi wa tamthilia za Kiswahili nchini Tanzania katika zama hizi (aghalabu awamu ya soko huria) wamekosa ubunifu. Hivyo, pana hatari kwa Tamthilia ya Kiswahili nchini Tanzania kufa au kudumaa. Kwa hiyo, uteuzi huu ulikusudiwa kutupatia picha kamili ya hali halisi ya utunzi kati ya kizazi cha awamu ya Azimio la Arusha na kizazi cha awamu ya soko huria.

### **3.4 Sampuli na Usampulishaji**

Sampuli ni sehemu ya wango lengwa ya utafiti ambayo imechujwa mahususi kuiwakilisha wango husika (Kothari na Gaurav, 2019). Kothari na Gaurav (2019) wanafafanua usampulishaji kuwa ni mchakato maalumu wa kimbinu katika kupata wawakilishi watakaowasilisha taarifa na uzoefu wao kwa niaba ya kila mwanajamii wa kundi lengwa. Na kwamba, mchakato huo una namna nyingi za kupata sampuli. Kwa mfano, mbinu ya usampulishaji lengwa, mbinu ya usampulishaji nasibu rahisi, mbinu ya usampulishaji elekezi au tajwa, mbinu ya usampulishaji nasibu tabakishi, na kadhalika.

Katika utafiti huu, tulitumia mbinu ya usampulishaji nasibu tabakishi. Kothari na Gaurav (2019) wanaielezea mbinu ya usampulishaji nasibu tabakishi kuwa ni mbinu ambayo humlazimisha mtafiti kuzitenga sampuli zake katika matabaka kulingana na sifa mahususi za kila kundi. Sifa hizo ni pamoja na mamlaka, utendaji, fursa, umri, matini, kimo, jinsia, elimu, umbo, rangi, na kadhalika. Kothari na Gaurav (2019) wanaendelea kufafanua kuwa, baada ya kutenga sampuli hizo kitabaka, mtafiti hutumia usampulishaji nasibu rahisi kufanya uteuzi wa wawakilishi watakaohusika moja kwa moja katika utafiti husika. Kwa muktadha wa utafiti wetu, mbinu hii



ilihusika kukusanya na kuorodhesha tamthilia za Kiswahili zinazoangukia katika vipindi viwili yaani; kipindi cha awamu ya Azimio la Arusha na awamu ya soko huria, nchini Tanzania. Jumla ya tamthilia za awamu ya Azimio la Arusha zipatazo 52 na za awamu ya soko huria zipatazo 34 zilitambuliwa na kuingizwa katika orodha (rej. Kiambatisho D).

Tamthilia hizi zilipangwa katika makundi makuu mawili (2) kwa kuzingatia miaka ya kuchapishwa na watunzi wake. Kwa kila kundi (linalowakilisha awamu husika), tamthilia zote ziliorodheshwa kwa kupewa namba mfuatano kwa kutumia kompyuta kisha mtafiti alichapisha na kuzikata karatasi zenye orodha husika katika vipande ili kila tamthilia katika kila kundi isomeke kwenye kipande chake cha karatasi. Baada ya kupata vipande vya karatasi vyenye kubeba namba na jina la tamthilia mojawoja, mtafiti akakunja kila kipande cha karatasi kimoja baada ya kingine kwa kuzingatia kundi teule. Vipande vya karatasi vilivyokunjwa vikiwakilisha tamthilia za awamu ya Azimio la Arusha viliwekwa katika bakuli tofauti na zile za awamu ya soko huru. Kisha mtafiti akamuomba mtoto wa miaka minne (4) kuchukua vipande vitatu (3) vya karatasi vilivyokunjwa kutoka katika kila bakuli ili kupata jumla ya tamthilia sita (6) teule.

Kwa kutumia mbinu hii, mtafiti aliweza kupata vipande sita (6) vya karatasi zilizowakilisha tamthilia za Kiswahili sita (6) teule. Mchakato mzima wa usampulishaji ulifanyika mahususi ili kuleta uwiano usio na shaka kisayansi katika uteuzi wa tamthilia ambazo ziliwakalisha tamthilia nyingine zilizochapishwa katika vipindi tofauti tofauti vya kihistoria. Tamthilia teule tatu (3) za awamu ya Azimio la Arusha zilizopatikana ni *Mashetani* (1971) ya Ebrahim N. Hussein, *Kijiji Chetu*

(1975) ya Ngalimecha Ngahyoma na *Harakati za Ukombozi* (1982) ya Amandina Lihamba, Ndyanao Balisidya na Penina Mhando. Tamthilia za Kiswahili za awamu ya soko huria kwa utafiti huu zilikuwa ni *Safari ya Chinga* (2009) ya Shani Omari, *Changamoto* (2010) ya E. Mahenge na *Nje – Ndani* (2016) ya A. A. Majid Mswahili na M. S. Njonjolo. Kwa jumla, mbinu ya usampulishaji nasibu tabakishi ilitusaidia kupata sampuli kwa njia isiyo ya upendeleo lakini yenye kuwakilisha miaka tofauti tofauti ndani ya awamu husika.

### **3.5 Mbinu za Kukusanyia Data**

Oso na Onen (2009) wanasema, mbinu za kukusanyia data ni mchakato mpana unaotawala hatua na mahitaji ya namna ya kufanikisha upatikanaji wa data. Miongoni mwa michakato hiyo ni usomaji makini, ushuhudiaji kwa macho au masikio, ujazaji wa dodoso la utafiti, ushiriki katika majadiliano ya vikundi na usaili. Kwa utafiti huu, mtafiti alitumia mbinu ya usomaji makini iliyoongozwa na maswali kadhaa yenye kuhusiana na malengo mahususi ya utafiti huu. Oso na Onen (2009) wanaifafanua mbinu ya usomaji makini kama mbinu maalumu na yenye kufaa kukusanya data zinazopatikana katika picha na maandishi mfano nyaraka na vitabu vya kifasihi.

Oso na Onen (2009) wanaendelea kueleza kuwa, hii ni mbinu maarufu katika tafiti za kifasihi na kihistoria. Mbinu hii humuongoza mtafiti kusoma matini na kutambua sifa mahususi kwa njia ya mkabala wa kiufafanuzi, kidhamira, kitakwimu na kadhalika. Na kwamba, mtafiti hulazimika kuwa na kalamu na shajara ya kurekodia data na mwongozo utakaokuwa fensi ili kuzibaini sifa mahususi anazozihitaji katika matini lengwa pasipo kutangatanga. Ambapo, mwongozo huo unaweza kuwa ni

maswali, viashiria au kauli maalumu zinazozitambulisha sifa mahususi zitakazokuwa zinachunguzwa katika matini husika. Katika utafiti huu, mtafiti alitumia maswali mahususi (rej. Kiambatisho C) ili kuongoza ukusanyaji wa data kutoka tamthilia sita (6) teule za Kiswahili ambazo tumezitaja hapo awali. Lengo lilikuwa ni kupata data zenye kufungamana na malengo mahususi ya utafiti huu.

Kwa msingi huu, utafiti ulilazimika kufuata kanuni za usomaji makini ili kufikia lengo la utafiti. Ambapo, hatua ya kwanza ilikuwa kuzitambua tamthilia teule. Hatua ya pili ilikuwa ni kunakili jina la kila tamthilia teule na mtunzi wake. Halafu, kunakili mwaka wa kuchapishwa kwa kila tamthilia na kutambua idadi ya kurasa zinazoumba tamthilia husika na kunakili mahali na jina la mchapishaji. Hatua iliyofuata ilikuwa ni kusoma kwa makini utangulizi na, au dibaji ya kila tamthilia. Katika usomaji huo, mtafiti alizingatia utambuzi wa kunakili kurasa, wazo na semi mahususi zilizokusudiwa katika utafiti huu.

Katika kuchunguza matini za tamthilia sita (6) teule, mtafiti alisoma kwa makini na kubaini dhamira zinazojitokeza na namna zilivyosukwa kiubunifu katika kila tamthilia teule. Uchunguzi mwingine uliofanyika ulikuwa wa kubaini aina, kiwango na namna lugha ya ucheshi, misimu, matumizi ya uchanganyaji ndimi na wepesi au ugumu wa lugha ulivyosanwa katika kila tamthilia. Kila dhamira iliyobainishwa ilinakiliwa katika kompyuta au katika shajara ili kumwezesha mtafiti kufanya uchambuzi na urejeleo wa wazo lililotarajiwa kuwasilishwa wakati wa uchakataji wa data na hatimaye kama sehemu muhimu ya matokeo ya utafiti na mjadala.

### **3.6 Mbinu za Uwasilishaji na Uchambuzi wa Data**

Kothari na Gaurav (2019) wanasema, mbinu za uwasilishaji na uchambuzi wa data ni hatua muhimu katika utafiti ambapo mtafiti hana budi kupangilia data, kurekodi data, kuchakata data, pamoja na kuchuja data pasipo kuathiri matokeo na maudhui ya msingi ya utafiti. Kisha kuziumba kwa namna itakayomwezesha msomaji wa ripoti ya utafiti husika kuelewa kwa urahisi na haraka. Utafiti wetu uliongozwa na mkabala wa kiufafanuzi katika uchambuzi, ulinganishaji na uwasilishaji wa data na matokeo yaliyopatikana kupitia nadharia ya Fasihi Linganishi. Mbinu ya uwasilishaji na uchambuzi wa data kwa kutumia mkabala wa kiufafanuzi, kwa mujibu wa Kothari na Gaurav (2019) ni mbinu ya kimaelezo inayotegemea uelewa wa mshiriki kuhusu hali, dhana, mikazo ya kimifumo, kategoria na taratibu fulani ilhali mbinu za uwasilishaji na uchambuzi wa data kwa mkabala wa kitakwimu hujikita zaidi katika takwimu ili kufasili dhana au hali.

Uwasilishaji na uchambuzi wa data za utafiti zinazohusiana na dhamira na matumizi ya lugha umewasilishwa kwa njia ya maelezo, tarakimu na nukuu kutoka tamthilia sita (6) teule. Vilevile, majedwali yametumika katika kuwezesha uwasilishaji wa data zilizohusiana na mchanganuo wa dhamira zinazopatikana katika kila tamthilia pamoja na matumizi ya lugha yaani matumizi ya ucheshi, matumizi ya misimu na matumizi ya uchanganyaji ndimi. Uwasilishaji huo unajitokeza katika sura zinazofuata kwa kuzingatia mpangilio wa malengo mahususi kama yalivyotambulishwa katika kipengele cha 1.4.2. Ufafanuzi wa data umeambatana na ushahidi kutoka tamthilia sita (6) teule kwa kuweka nukuu na ukurasa mahususi ili kuthibitisha kwamba data teule si maoni binafsi au mawazo binafsi ya mtafiti.

Mtafiti alipitia kila kipengele na mbinu zilizotumika katika utafiti ili kutathmini iwapo hatua na vigezo mbalimbali vya ukusanyaji wa data vilizingatiwa vema. Baada ya tathmini hiyo, mtafiti alianza kuhakiki data moja baada ya nyingine kwa utulivu kisha kuzinakili, kuzipanga na kuzitathmini kwa kuzingatia malengo mahususi ya utafiti huu. Aidha, mtafiti aliepuka kuchambua data na kuwasilisha matokeo ya utafiti kwa kusukumwa na utashi, imani, mtazamo na hisia binafsi ili kuepuka kughushi matokeo au kuathiri masuala ya ufaafu wa utafiti.

Mchakato huu ulihusisha upangaji wa nukuu na utambuzi wa dhamira kupitia data nukuliwa ili kuwakilisha nyanja mahususi za maisha ya mwanadamu. Nyanja hizo ni uchumi, jamii, utamaduni na siasa. Baada ya hatua hiyo, mtafiti alitengeneza jedwali mbili. Jedwali la kwanza lilijazwa dhamira zinazogusa nyanja na nukuu zinazotoka katika kila tamthilia teule ya awamu ya Azimio la Arusha. Jedwali la pili lilijazwa dhamira zinazogusa nyanja na nukuu zinazotoka katika kila tamthilia teule ya awamu ya soko huria. Baada ya kujaza dhamira katika majedwali, mtafiti alifanya ulinganishaji wa dhamira zilizobeba mjadala mpana katika kila tamthilia ili kuweza kuteua dhamira zinazopaswa kuingizwa katika ripoti ya utafiti.

Dhamira zilizobainika kuwa na nukuu nyingi yaani zinazorudia wazo lile lile kwa mapana ndizo zilizoingizwa katika ripoti hii. Dhamira ambazo hazikuwa na nukuu nyingi zilihesabika kuwa na uzito mdogo kimjadala. Hivyo hazikuingizwa kabisa kuwa sehemu ya ripoti ya utafiti huu. Hata hivyo, katika uwasilishaji wa dhamira, mtafiti ametumia nukuu chache kutoka kila tamthilia teule ili kuwakilisha ushahidi mpana wa dhamira zilizobainika kuwapo ndani ya kila tamthilia teule. Vilevile, majedwali hayakutumika kuwasilisha dhamira na nukuu teule. Badala yake, dhamira

zimewasilishwa kwa njia ya maelezo, nukuu na tarakimu zenye kuonesha ukurasa wa kila nukuu teule. Mtafiti alifanya hivi kwa sababu, njia hii ilionekana kubeba ujazo wa kufaa kuruhusu nukuu za kutosha tofauti na njia ya majedwali. Jedwali pekee la dhamira limewekwa mwishoni kama Kiambatisho B.

Kwa upande wa matumizi ya lugha, mtafiti alirekodi kauli na ukurasa uliobeba semi husika. Halafu, akazipanga data katika majedwali kwa kuzingatia aina teule ya matumizi ya lugha yanayolengwa katika utafiti wetu. Baada ya hapo, mtafiti akaanza kuchakata data kwa kulinganisha na kulinganua matumizi hayo ili kubaini kama upo ubunifu au ni ukasuku miongoni mwa watunzi wanaowakilisha kila awamu. Uwasilishaji wa matumizi ya lugha umezingatia majedwali, maelezo na nukuu kulingana na mahitaji yaliyomsukuma mtafiti kufanya hivyo.

### **3.7 Uzingativu wa Masuala ya Kiitikeli (Kimaadili)**

Mtafiti hakuwa budi kuheshimu na kutii kanuni za kufanya kazi za tafiti za kisayansi. Mtafiti aliomba barua ya utambulisho kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Tafiti, Machapisho, na Taaluma za Shahada za Juu katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Kwa kila taasisi aliyoifikia mtafiti kwa minajili ya kupitia maandiko hitajika kwa utafiti huu, alilazimika kuonana na mkuu wa taasisi husika ili kujitambulisha kwa kumkabidhi barua ya utambulisho, kutoa ufafanuzi wa ziada (pindi ulipohitaji) na, au vitambulisho vingine vya utambulisho kwa kadri ya matakwa ya mkuu huyo. Baada ya utambulisho, mtafiti aliomba idhini ya kuingia kwenye eneo la kimamlaka la mkuu husika kwa lengo la kutumia raslimali za taasisi husika kwa kuzingatia sheria, taratibu, kanuni na utamaduni wa taasisi husika. Maeneo aliyoyatembelea mtafiti kwa kibali hiki ni Makavazi ya TATAKI - Chuo Kikuu cha Dar es salaam, Maktaba

Kuu ya Chuo Kikuu cha Dar es salaam, Maktaba Kuu ya Taifa Dar es salaam na Maktaba ya Chuo Kikuu cha Dodoma.

Aidha, mbinu na vifaa teule vya kukusanyia data mathalani fomu yenye maswali mahususi ili kuongoza ukusanyaji na uchakataji wa data vilitathminiwa ubora wake kwa kutumia wahadhiri wanaofundisha kozi ya Tamthilia ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Kikatoliki Mwenge – Moshi, Kilimanjaro - Tanzania. Aidha, mtafiti alihakikisha kila nukuu halisi na vyanzo vyote vya taarifa vinatambulishwa kwa usahihi huku akiepuka kuchukua maandishi pasipo kutambua chanzo na usahihi wake, au mwaka wa chapisho na ukurasa husika. Uchambuzi wa data ulikwepa kwa kiwango cha juu maoni hasi na hisia binafsi za mtafiti kama njia ya kuepuka ubaguzi, ushawishi usiofaa machoni pa wanataaluma na mamlaka za nchi na taasisi nyingine katika jamii.

### **3.8 Hitimisho**

Mbinu za utafiti ni eneo muhimu sana katika utafiti. Eneo hili lilitoa mwongozo bora katika mchakato mzima wa ukusanyaji, uchambuzi, uchakataji na uwasilishaji wa data ili kukidhi mahitaji ya utafiti huu. Ufafanuzi wa kina wa kila kipengele katika sura hii ulikuwa na utakuwa ni wenye tija kwa mtafiti na watafiti wajao pamoja na wanafunzi wanaosoma kozi ya mbinu za utafiti. Sura hii ni ufunguo kwa sura zinazofuatia ambazo zinahusu uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa matokeo ya utafiti huu.

## SURA YA NNE

### UBUNIFU KATIKA DHAMIRA ZA TAMTHILIA TEULE

#### 4.1 Utangulizi

Sura hii inahusu muhtasari wa tamthilia sita (6) teule pamoja na lengo la kwanza la utafiti huu. Lengo hilo ni kulinganisha ubunifu katika dhamira zinazojitokeza katika tamthilia teule za Kiswahili za awamu ya Azimio la Arusha na zile za soko huria ili kubaini kama kuna ubunifu endelevu. Ili kufikia lengo hili, utafiti huu uliongozwa na swali hili; “Je, ubunifu katika dhamira zinazojitokeza katika tamthilia teule za Kiswahili za awamu ya Azimio la Arusha unafanana na kutofautiana vipi na ule wa tamthilia teule za Kiswahili za awamu ya soko huria?” Msingi wa swali hili ulikuwa ni kuzizamia tamthilia zote sita (6) teule ili kubaini kama kufanana na, au kutofautiana kwa uteuzi na ujenzi wa dhamira kunaonesha ubunifu endelevu katika kukua na kustawi kiutunzi kwa Tamthilia ya Kiswahili nchini Tanzania ama la.

Hivyo, kwa kutumia mbinu ya usomaji makini tuliweza kusoma tamthilia zote sita (6) ili kukusanya data zinazokidhi lengo hili. Aidha, utafiti wetu uliongozwa na nadharia ya Fasihi Linganishi. Uwasilishaji wa matokeo umeongozwa na mkabala wa kiufafanuzi kwa kuhusisha maelezo, nukuu na ufafanuzi mwingine kutoka vyanzo mbalimbali vya kihistoria. Vyanzo vyote rejelewa vimekuwa ni mwongozo bora kwetu katika kujibu maswali ya Wanafasihi Linganishi ambayo ni kwa vipi? Ya nini? Kwa nini? Lini? na wapi? (Jilala, 2016).

Faukwa ya hayo, majina ya wahusika katika nukuu zote yameandikwa kwa namna ilivyo ndani ya tamthilia husika. Mathalani, majina yote ya wahusika katika tamthilia ya *Mashetani* yameandikwa kwa herufi kubwa zote pasipo kukolezwa wino. Wakati



tamthilia za *Kijiji Chetu* na *Harakati za Ukombozi*, majina yote ya wahusika yameandikwa kwa herufi kubwa zote na kukolezwa wino. Nayo majina ya wahusika katika tamthilia za *Safari ya Chinga*, *Changamoto* na *Nje – Ndani* yameandikwa kwa herufi ndogo (isipokuwa herufi ya kwanza kwa kila jina) na kukolezwa wino.

Kwa hiyo, msomaji anapokutana na aina hii ya uandishi katika tasnifu yetu kupitia nukuu au utambulisho wa mhusika, hana budi kutambua uandishi huo siyo utashi wa mtafiti bali unukuzi wa matini chanzi. Tumefanya hivi kwa sababu, kanuni za uandishi rasmi aghalabu uandishi wa kitaaluma huzuia kubadilisha umbo mama – hata kama limekosewa, pindi mwandishi afanyapo unukuzi halisi wa matini chanzi (Oso na Onen, 2009; Stephano, 2015).

#### **4.2 Muhtasari wa Tamthilia Teule**

Tamthilia ya *Mashetani* (1971) ya Ebrahim N. Hussein ni tamthilia yenye jumla ya kurasa 57 za utendaji jukwaani zinazobeba mjadala na tathmini ya hali halisi ya maisha ya kabla na baada ya mapinduzi ya kisiasa nchini Zanzibar. Mapinduzi hayo almaarufu kwa jina la mapinduzi matukufu ya Zanzibar, yalitokea Aprili 1964. Azimio la Arusha lilizaliwa mwaka 1967, ikiwa ni miaka mitatu (3) na miezi kadhaa baada ya mapinduzi hayo ya Zanzibar. Sababu za kuzaliwa Azimio la Arusha na Mapinduzi ya Zanzibar hazitofautiani. Tamthilia hii ilichapishwa mnamo mwaka 1971, ikiwa ni miaka minne (4) na miezi kadhaa tangu kuanzishwa kwa Azimio la Arusha, na miaka saba (7) na miezi kadhaa tangu kutokea kwa mapinduzi ya kisiasa nchi Zanzibar.

Mnenuka (2010) anaitazama tamthilia hii kama kazi inayowakilisha vipindi viwili vya kihistoria. Kipindi cha kwanza ni baada ya Waafrika kupata uhuru ambapo

viongozi wazawa walirithi tabia na sera za mkoloni (rej. mhusika Shetani) kwa kuendelea kutweza utu wa mwananchi mzawa mnyonge (rej. mhusika Binadamu). Kipindi cha pili ni kile cha Azimio la Arusha ambapo mfumo kandamizi uliendelezwa na viongozi wazawa kwa maneno matamu ilhali matendo yao ni ya kikoloni (rej. mhusika Shetani). Mtafiti amechunguza na kubaini kuwapo kwa dhamira mbalimbali hususani imani za kijadi, athari na nafasi ya mapinduzi na ukoloni mamboleo kwa jamii, umuhimu wa elimu rasmi na isiyo rasmi, matumizi mabaya ya madaraka na mamlaka, pia matabaka na ubaguzi. Lugha iliyotumika ni ya picha zaidi. Hivyo kuleta ugumu kueleweka kwa wasomaji wasiokuwa wamaizi katika upasuaji wa sitiara.

*Kijiji Chetu* (1975) ya Ngalimecha Ngahyoma ni tamthilia ya Kiswahili yenye jumla ya kurasa 56 za utendaji jukwaani. Tamthilia hii inajadili na kutathmini utekelezwaji wa Azimio la Arusha ili kutambua namna azimio hili lilivyowezesha kupatikana au kusambaratika kwa dhamira na dira ya ukombozi na ujenzi wa jamii mpya na endelevu. Tamthilia hii imechapishwa mnamo mwaka 1975, ikiwa ni miaka minane (8) na miezi kadhaa toka kuzaliwa kwa Azimio la Arusha mwaka 1967. Kwa mfumo wa elimu rasmi nchini Tanzania, tunaweza kusema umri huu ni wa mtoto anayesoma darasa la pili (rej. Taasisi ya Elimu Tanzania, 2005 / 2013). Mtafiti ameichambua tamthilia hii na kubaini kuwapo kwa dhamira tofauti tofauti zikiwemo: - mapokeo ya kiimani, nafasi ya mwanamke, Azimio la Arusha, nafasi ya wazee, nafasi ya ndoa na mapenzi, umuhimu wa elimu, utamaduni wa kujisomea na unyonyaji. Dhamira nyingine ni dhuluma, fitina, usaliti na uzalendo, wizi na rushwa, matumizi mabaya

ya mamlaka, matabaka, ubaguzi, na ukuaji wa demokrasia. Tamthilia imetumia lugha inayoeleweka kwa urahisi na haraka - kwa yeyote anayejua Kiswahili.

*Harakati za Ukombozi* (1982) ni kazi bunilizi ya kitamthilia ya Kiswahili inayojadili na kutathmini namna Azimio la Arusha lilivyotekelezwa. Tamthilia hii ilitungwa mwanzoni mwa mwaka 1978 ikiwa ni ombi maalumu kutoka Ofisi ya Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Dar es salaam, kwa Mwalimu Penina Mhando. Tamthilia hii iliwasilishwa kimkoa mbele ya kaumu ya watu mnamo tarehe 1 Februari 1978 ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya kumbukizi ya mwaka mmoja tangu kuzaliwa kwa CCM - mnamo tarehe 5 Februari 1977. Utunzi wa tamthilia hii uliwahusisha watunzi wengine wawili ambao ni Amandina Lihamba na Ndyanao Balisidya. Tamthilia hii ilichapishwa mnamo mwaka 1982 hivyo kufanya kuwapo kwa tofauti ya miaka mitano (5) tangu kuzaliwa kwa CCM, na miaka kumi na mitano tangu kuzaliwa kwa Azimio la Arusha lililotangazwa rasmi na Mwalimu Julius K. Nyerere mnamo tarehe 5 Februari 1967.

Bila shaka, baada ya kutambwa jukwaani, kulifanyika maboresho ya kiufundi katika drama iliyotambwa jukwaani kabla ya kwenda kuchapwa ili iwe tamthilia. Tamthilia hii iliingia sokoni baada ya miaka 15 tangu kuzaliwa kwa azimio la Arusha. Aidha, waandishi wake ni kizazi cha wakati wa ukoloni, baada ya ukoloni, wakati na baada ya Azimio la Arusha. Tamthilia hii imejadili na kutathmini kwa kina mambo kadhaa yakiwemo: - imani mpya, nafasi ya vijana, nafasi ya wazee, mikataba ya kazi na bima, utumwa, ukoloni na ukoloni mamboleo. Mengine ni umuhimu wa elimu na utamaduni wa kujisomea, unafiki, unyonyaji, dhuluma, fitina, usaliti na uzalendo. Vilevile, wizi na rushwa, matumizi mabaya ya mamlaka, matabaka na ubaguzi,

kukata tamaa, mapinduzi na uzalendo. Mambo haya yote yamejengwa katika mchezo uliochapishwa kwenye jumla ya kurasa 25 za utendaji jukwaani. Uandishi wake ni tofauti sana na tamthilia nyingi tulizozioea kwani umekaa kimajaribio zaidi. Lugha yake ni nyepesi kueleweka haraka na kwa urahisi kwa mtu yeyote anayetumia Kiswahili kuwasiliana - kimaandishi.

Tamthilia ya *Safari ya Chinga* (2009) ya Shani Omari ni tamthilia ya kimapinduzi inayobainisha na kujadili vyanzo na changamoto za uhamaji holela wa watu kutoka vijijini kwenda mijini. Miongoni mwa mambo yanayobainishwa kuchangia uhamaji huo holela ni hali ngumu ya maisha huko vijijini kutokana na changamoto nyingi. Mifano yake ni uduni wa miundombinu ya kusaidia kuzalisha na kuuza bidhaa kwa tija, kufuata mkumbo, upotofu wa taarifa na ukosefu wa elimu. Changamoto nyingine ni kutokuzingatiwa kwa sheria, miundombinu isiyorafiki kwa wafanyabiashara wa sekta isiyorasmi, imani za kijadi, athari za mfumodume, ndoa na mimba za utotoni. Pia, unyonyaji, dhuluma na usaliti, wizi na rushwa, ukosefu wa ajira kwa vijana, mila na desturi. Nyingine ni matumizi mabaya ya fedha, utapeli, kukata tamaa, na athari ya UKIMWI / VVU katika jamii. Mambo haya yote yamejengwa ndani ya matini yenye jumla ya kurasa 56 za utendaji jukwaani. Lugha yake ni rahisi kueleweka kwa haraka miongoni mwa wasomaji wanaojua Kiswahili.

Tamthilia ya *Changamoto* (2010) ni kazi bunilizi ya kiutendaji iliyotungwa na kuandikwa na Elizabeth Godwin Mahenge. Tamthilia hii inayajadili matatizo na changamoto wanazopitia watu wenye ulemavu katika nyanja zote za maisha. Mwandishi anaonesha ukubwa wa madhira wanayoyapata watu wenye ulemavu kutokana na unyanyapaa uliokita mizizi toka enzi za mababu hadi leo hii, karne ya

21. Kasumba, dharau na kutokukomboka kifikra kwa jamii kumesababisha watu wenye ulemavu wanyimwe haki na fursa mbalimbali za maisha bora. Mathalani, wamenyimwa kugombea nafasi za uongozi, kupata ajira, elimu, kulindwa, kuheshimika na kutetewa, pia kupewa matumizi sawa ya barabara kwa usalama. Changamoto nyingine ni miundombinu isiyorafiki katika majengo marefu, amani na usalama, kujiamini na kuaminiwa, na kupata msaada wa kisheria.

Kutokana na changamoto hizi, tumebaini kuwapo kwa dhamira kadhaa zikiwemo ukombozi wa kifikra, umoja na ushirikiano katika jamii, imani potofu na ushirikina, ukatili, tamaa na wizi. Pia, kuna dhamira za elimu ya uraia, unyanyapaa kwa watu wenye ulemavu, nafasi ya mwanamke katika jamii na nafasi ya wanajamii katika kumtetea mlemavu. Dhamira nyingine ni nafasi ya vyombo vya ulinzi, usalama, haki na sheria, rushwa na uonevu, umasikini, elimu na wasomi katika jamii. Mambo haya yote yamejengwa katika kurasa 39 za utendaji jukwaani. Matumizi ya lugha yamebainika kuwa mepesi kwa yeyote anayejua kusoma kwa ufasaha lugha ya Kiswahili.

Tamthilia nyingine ni *Nje-Ndani* (2016). Tamthilia hii imeandikwa na watunzi wawili ambao ni A. A. Majid Mswahili na M. S. Njonjolo. Tamthilia hii imejitana vema katika mawanda ya kisaikolojia, kifalsafa na kiuhalisiamazingaombwe. Matumizi ya taswira zinazowaumba wahusika kupitia viungo na hisi za maumbile yanayopatikana katika maungo ya mwili aghalabu mwili wa binadamu, kunaifanya kazi hii kuwa ya kipekee yenye kubeba tafakuri zilizojengwa kupitia lugha ya picha na ucheshi kwa kiasi. Tamthilia hii inajadili kwa njia ya tafakuri ya “kimafumbo”

mambo mbalimbali yanayoendelea kutokea katika jamii ya watu, wakiwemo Watanzania.

Baadhi ya mambo yaliyobainika katika tamthilia hii ni suala la matumizi ya busara, hekima, subira na maarifa katika uongozi, athari za ukoloni na ukoloni mamboleo. Mengine ni unafiki na usaliti wa viongozi, hali ngumu ya maisha, tamaa na usaliti katika ndoa na mapenzi. Masuala mengine ni ulinzi na usalama kwa watu wa makundi maalumu, nafasi ya elimu na wasomi katika ukombozi, uhujumu uchumi, unyonyaji na rushwa. Mengine ni athari ya kukosekana umoja na ushirikiano, umuhimu wa elimu na utamaduni wa kujisomea, matabaka na ubaguzi na umuhimu wa ukombozi wa kifikra. Mambo haya yote yamejengwa ndani ya matini yenye jumla ya kurasa 95 za utendaji jukwaani.

#### **4.3 Kulinganisha Ubunifu katika Dhamira za Tamthilia Teule**

Kwa ufupi, tunaweza kusema ubunifu ni ujanja wa kulipanga wazo katika mfumo maalumu wa kisanaa unaolichukua jambo lililopo au lisilokuwapo na kulitambulisha kwa namna inayoibua utamu na, au uchungu kwa lengo la mtu kupata burudani, utiisho na mafunzo (rej. 2. 2. 4 kwa ufafanuzi wa kina). Kwa minajili ya andiko hili, ubunifu ulipimwa kwa kutazama namna mwandishi alivyoweza kubaini, kuongeza tija na kuwasilisha jambo lenye maslahi kwa jamii kupitia ujenzi wa dhamira kwa namna iletayo nyongeza ya pekee ya upya na mguso maalumu kwa wasomaji, wasikilizaji na watazamaji.

Kwa jumla, utafiti huu ulibaini kuwa, tamthilia zote sita (6) teule zinafanana na kutofautiana kiubunifu katika uwasilishaji wa uhalisia wa mambo yanayogusa jamii. Kila tamthilia imeibua dhamira kwa ubunifu na mtindo wa kipekee. Aidha, utafiti

ulibaini kuwa kuna kufanana na kutofautiana kwa dhamira zilizoibuliwa katika tamthilia hizo. Matokeo ya kina ya utafiti yanawasilishwa na kujadiliwa katika sehemu zifuatazo.

#### **4.3.1 Kufanana kwa Ubunifu wa Dhamira katika Tamthilia Teule**

Uchunguzi umebaini ya kwamba tamthilia zote sita (6) teule zimejadili maisha ya watu kwa kuzamia changamoto endelevu zinazowakabili wananchi hasa wa tabaka la chini. Na kwamba, matamko na mabadiliko ya sera, sheria na mfumo bado hayajamsaidia mwananchi mnyonge kwa kiwango cha kuridhisha. Badala yake, mabadiliko haya yamekuwa manukato kwa watu wachache wa tabaka la juu kwa kuendelea kujinufaisha. Dhamira zinazojadiliwa katika tamthilia hizi sita (6) yanagusa nyanja za kiuchumi, kisiasa, kijamii, na kiutamaduni. Kwa hiyo, uwasilishaji wa matokeo ya uchambuzi wa data kwa kuzingatia kufanana kwa dhamira zinazojitokeza katika tamthilia teule za awamu ya Azimio la Arusha na zile za awamu ya soko huria umeainishwa kwa kurejelea nyanja za maisha ya mwanadamu aghalabu uchumi, siasa, jamii na utamaduni.

#### **Dhamira za Kiuchumi**

Utafiti umebaini kuwapo kwa mfanano wa dhamira zinazohusiana na mambo ya kiuchumi katika tamthilia zote sita (6) teule. Mambo yanayogusa uchumi katika tamthilia hizi ni pamoja na wizi, ufisadi, unyonyaji, tamaa, kujilimbikizia mali, kudhibiti wengine kiuchumi, dhuluma, na matabaka ya kiuchumi kwa maslahi binafsi au ya wachache. Athari ya mambo haya inaonekana miongoni mwa wananchi walio wengi kushindwa kupata huduma bora na sahihi kutokana na hali ngumu ya kiuchumi ilhali wachache wakiishi maisha ya anasa. Uchu, ubinafsi na ukatili wa

wachache kwa maslahi yao kunawafanya wahujumu uchumi wa taifa kusababisha uchumi wa taifa kudorora na kutokuwa wa uhakika. Yote haya tunayapata kupitia ushahidi ndani ya kila tamthilia teule.

Katika tamthilia ya *Mashetani*, mwandishi anatumia ubunifu kumchora kiongozi mbadhirifu anayelisababishia taifa hasara kubwa kutokana na kampuni ya umma aliyokuwa akiisimamia kufilisika. Jambo ambalo linachangia kuua uchumi wa nchi na wa mwananchi mmoja mmoja aliyetegemea kampuni husika kuzalisha kipato kupitia biashara ya huduma, ajira ya moja kwa moja ama isiyokuwa ya moja kwa moja kutoka katika kampuni husika. Uthibitisho wa uhujumu uchumi huu unapatikana katika data za nukuu ifuatayo: -

MTU 1: [...] (*Mlio wa gari inapita.*) Doo doo! Salaale! Umeona mdudu ule?

MTU 2: Nini? Ile gari? Nimeiona. Aah, ataiuza kesho ile. We ngoja tu.

MTU 1: Kwani we unamjua yule?

MTU 2: Kwani we humjui?

MTU 1: Hata.

MTU 2: Jana hatukuwa wote pamoja, alipokuwa akitusimulia Bwana Mathew juu ya kufungwa kwa ile kampuni.

MTU 1: Aah! Aah! Ndiyo, ndiyo, ndiyo. Aha! Kwani ndiye huyu bwana mwenyewe?

MTU 2: Eh. Pesa chungu nzima bwana zimepotea. Lakini ndiyo haijulikani kuwa zimeibiwa au zimepotea katika mahisabu.

MTU 1: Alaa. Kumbe ndiye huyu? Shetani kweli kweli... (uk. 42 - 43)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Mashetani*, 1971)



Nukuu hii inaonesha kuwapo kwa tatizo la uaminifu miongoni mwa watendaji wanaopewa dhamana ya kusimamia na kuzistawisha taasisi za umma. Data hii inadhihirisha kwamba, uchumi wa taifa unahodhiwa na wachache kwa faida yao pasipo kujali kesho ya taifa na wananchi walio wengi wanaonuka umasikini wa kutupwa. Kauli ya MTU 2 isemayo “[...] alipokuwa akitusimulia Bwana Mathew juu ya kufungwa kwa ile kampuni” na “[...] Pesa chungu nzima bwana zimepotea. Lakini ndiyo haijulikani kuwa zimeibiwa au zimepotea katika mahisabu” zinathibitisha umchwa wa wachache wenye kuhodhi madaraka kwa faida yao.

Kwa data hii, ni dhahiri kuwa mchwa wa namna hii hawawazi kesho ya vizazi vyao na athari ya mahusiano ya kijamii na kiuchumi miongoni mwa watu wanaoishi katika jamii moja yenye kushuhudia ubadhilifu, tamaa, unyonyaji, wizi, ufiisadi na kujilimbikizia mali. Ubinafsi na ufiisadi huu siyo wa kufikirika. Jambo hili alilolisema Ebrahim N. Hussein linajitokeza katika mijadala ya Ally na wenzake (2013), Mwiru (2013), Sitta (2013), Chachage (2000, 2014) na Masabo (2014). Hali inayothibitisha kwamba, mwandishi amejadili jambo halisi kwa njia ya ubunifu wa kisanaa kwa kuwaambia wahusika wake lugha na matendo yanayoakisi uhujumu uchumi wa taifa na jamii kwa faida binafsi.

Utafiti umebaini, uchu, ubinafsi na ukatili wa kiuchumi wa wachache katika jamii unaosahau athari hasi za matendo haya, umejitokeza pia katika tamthilia ya *Kijiji Chetu*. Katika tamthilia ya *Kijiji Chetu*, mwandishi anaonesha kundi dogo linavyonufaika kiuchumi kwa kula na kunywa jasho la walio wengi bila huruma wala makubaliano ya pamoja kama jamii moja yenye upendo, umoja na mshikamano. Mwandishi anamuonesha Mwenyekiti wa Kijiji akishirikiana na watu wa mjini na

viongozi wengine wachache kujimilikisha na kujilimbikizia mali huku wakiwadhiti wananchi wengine wasiweze kumiliki mali, kwa kisingizio cha kutekeleza maazimio ya Azimio la Arusha - kinyume na makubaliano ya kijiji. Hujuma ya kundi hili dogo kupoka haki na usawa wa uzalishaji na ugawanywaji wa raslimali za kiuchumi, unasababisha kuanguka kwa lengo kuu la Azimio la Arusha la jamii yenye usawa kumiliki na kuboresha maisha yao kiuchumi. Haya yanathibitika kupitia mazungumzo yafuatayo:-

**MWANAMKE I:** [...] zaidi kuna jambo ambalo limenikera siku nyingi sana ambalo Kamati yetu inaelekea kuridhika na kuna watu wanaokaa nje ya kijiji hiki – wengine mjini kabisa. Wengi wako Dar es Salaam. Sikuwa nafahamu kuwa watu hawa wanaitwa wanakijiji wa hapa mpaka wiki iliyopita wakati tunagawana faida ya mwaka. Wao walifika kuchukua faida yao na kuondoka. Wengine walipelekewa. Wengi tulistushwa na jambo hili. Itawezekanaje watu wasioishi kijijini wawe wanakijiji... Tulipouliza tukaelezwa kuwa eti wanaleta fedha. Ah! Fedha. Kwa hiyo unaweza kununua uanakijiji! (uk. 14)

**KIZITO:** Ngoja basi nimalize. Usijifanye mjinga. Kila mtu, hata mjamaa, anataka kuchuma. Mtazame mwenyekiti wa Kijiji. Uta sema kweli ni mjamaa? Ana duka, kuku, vyote vyamletea utajiri juu ya utajiri! Lakini yuko wapi? Tunaye hapa kwenye kijiji. Bali yeye haonekani ila mimi, kwa sababu? Siji kwenye shamba la ushirika. (uk. 30)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Kijiji Chetu*, 1975)

Ukiangalia nukuu hii kwa makini, utabaini kuwapo kwa matendo ya uhujumu uchumi wa taifa na wananchi walio wengi unaofanywa na watu wachache, wakiwemo viongozi wasiokuwa waaminifu. Aidha, kundi hili dogo ndilo linaonekana kuwa na nguvu kiasi cha kuwafanya wananchi wasio na upeo wa kung'amua ukweli wa mambo kujikuta wakiimba ujamaa bila kutambua athari na kiwango cha unyonyaji, dhuluma, ujilimbikiziaji mali, wizi na ufasadi unaotendwa na kundi hili dogo dhidi ya kesho ya jamii nzima. Matendo ya Mwenyekiti wa Kijiji cha Ujamaa yanathibitisha kiwango cha juu cha ubinafsi, ubaguzi, unyonyaji, udhalimu na kiburi cha mali alizojilimbikizia ikiwa ni sehemu ya uhujumu uchumi wa kijiji. Sehemu ya data tuliyomnukuu Mwanamke 1 inaonesha usiri na ukengeushi wa viongozi kwa maslahi ya wachache. Mwanamke 1 anasema, “Wengi wako Dar es Salaam. Sikuwa nafahamu kuwa watu hawa wanaitwa wanakijiji wa hapa mpaka wiki iliyopita wakati tunagawana faida ya mwaka. Wao walifika kuchukua faida yao na kuondoka. Wengine walipelekewa. [...] Tulipouliza tukaelezwa kuwa eti wanaleta fedha. Ah! Fedha. Kwa hiyo unaweza kununua uanakijiji!” Tunasema ni usiri kwa sababu maamuzi haya yangekuwa ni azimio la wanakijiji wote basi mwanamke huyu asingeshangaa wala kuuliza.

Naye Kizito anaonesha masikitiko yake dhidi ya hujuma za viongozi kwa kusema “Mtazame mwenyekiti wa Kijiji. Utasema kweli ni mjamaa? Ana duka, kuku, vyote vyamletea utajiri juu ya utajiri! Lakini yuko wapi? Tunaye hapa kwenye kijiji. Bali yeye haonekani ila mimi, kwa sababu? Siji kwenye shamba la ushirika.” Nukuu hizi ni ushahidi halisi kwamba baadhi ya viongozi walitumia kofia zao kulihujumu taifa kwa manufaa ya wachache. Data hizi zinaonesha kuwa matendo haya ya uhujumu

uchumi yamechangia pakubwa sana katika kuua ustawi na maendeleo ya kijiji husika (uk. 55 - 56). Hili la viongozi kwenda kinyume na sera ya ujamaa na kujitegemea linatajwa na Hyden (1980), Ally na wenzake (2013), Mwiru (2013) na Sitta (2013) kuchangia kwa sehemu kubwa umasikini tulionao sasa. Hivyo kuthibitisha kuwa, msukumo wa utunzi wa tamthilia hii kiubunifu haukutoka hewani bali katika jamii halisi ya Watanzania. Kwa data hizi, tunagundua ya kwamba, mwandishi ametumia maneo mahususi yanayobeba ubunifu katika kuelezea madhira yanayotokana na uhujumu uchumi katika jamii halisi.

Tatizo la kundi dogo katika jamii linalobebwa na viongozi wasiowaaminifu kuhujumu uchumi wa taifa na wananchi walio wengi pia linajitokeza katika tamthilia ya *Harakati za Ukombozi*. Waandishi wanawachora viongozi wa umma wasiowaaminifu wakishirikiana kuhujumu uchumi wa taifa na wa mwananchi mmoja mmoja. Kwa kutumia madaraka waliyokabidhiwa, viongozi hawa wanadiriki kutumia mgongo wa chama kuwadhiti watendaji wa serikali wanaonekana kuwa wazalendo na waadilifu katika maeneo yao ya kazi kwa faida ya taasisi husika na taifa. Aidha, viongozi hawa wanaonekana kutumia vyeo vyao kuliua Azimio la Arusha kupitia wizi, rushwa, ubadhilifu wa mali za umma na matumizi mabaya ya madaraka. Hili linathibitika katika majadiliano yafuatayo ya viongozi wasiowaaminifu kwa taifa na umma: -

**KIONGOZI 2:** (*Anakaa*). Ah! Nilikuwa kwenye shughuli za Chama, halafu nikapitia kwenye miradi yangu kuangalia isianguke. (*Wote wanacheka*).

**MENEJA:** Unajua bwana kiwanda changu kimechukuliwa?

**MKURUGENZI:** Ala! Tayari?

- MENEJA:** Hasa. Lakini mwenzenu Azimio hili linaniumiza kichwa. (*Wanacheka*).
- KIONGOZI 2:** [...] Kwani Bwana Meneja una nyumba ngapi?
- MENEJA:** Nina nyumba nne.
- KIONGOZI 1:** Nne tu?
- MENEJA:** Nne.
- KIONGOZI 2:** Aa! Mimi nilidhani una nyumba nyingi sana kumbe nne tu. Mbona mimi ninazo kumi (*anacheka*) na sina tatizo.
- MKURUGENZI:** Kwani ndugu Meneja huna watoto wowote?
- MENEJA:** Nina watoto wanne. Huyu wa nne kazaliwa juzi tu, hata siku kumi hajafikisha.
- MKURUGENZI:** Sasa kumbe una shida gani. Wagawie hao watoto hizo nyumba.
- KIONGOZI 1:** Eee! Kila mtoto mpe nyumba moja.
- MENEJA:** Eti kweli. Kwa nini sikufikiria jambo hili.  
(*Viongozi wanaendelea kunywa na wanaonyesha kulewa zaidi*)
- KIONGOZI 2:** Hivi Bwana Meneja, kwenye kiwanda chako bado mnasafirisha vitu nje?
- MENEJA:** Siyo kiwanda changu, chetu.
- KIONGOZI 2:** Ee ndiyo! Chetu.
- MENEJA:** Ndiyo, bado tunapeleka bidhaa Marekani, Uchina, Ujerumani na pia Uingereza. Vipi?
- KIONGOZI 2:** Nilitaka unisafirishie mzigo wangu kwenda Marekani. Je, si inawezekana?
- MENEJA:** Tunaweza, lakini juzi tu serikali ilimleta kijana mmoja kufagiafagia pale ofisini kwangu. Bali

ninavyomwona kijana huyo, sidhani kama mfagiaji.

**KIONGOZI 2:** Wewe unafikiri ni nani.

**MENEJA:** Mimi naona ni kati ya wale... (*Anapiga mkono kama vile anaua mbu anayemuuma*).

**KIONGOZI 2:** Aa! Usiwajali hao, wote wako chini ya Chama wale.

**MENEJA:** Kama ni hivyo, basi hamna taabu, maana yake nyie ndio viongozi wa Chama na serikali, mtume mtoto kesho aje achukue fomu za kujaza. (uk. 18 – 21)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Harakati za Ukombozi*, 1982)

Katika nukuu hii tunabaini kuwapo kwa dhamira ya rushwa ya kujuana, matumizi mabaya ya madaraka ili kupindisha sheria na taratibu, udanganyifu na ukwepaji wa wazi wa kodi katika usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi. Hivyo, tunaweza kusema kwamba haya yote yanatokea kwa sababu ya kutokuwapo kwa uwajibikaji, huku chama kikitumika kudhibiti vijana wazalendo. Matokeo yake viongozi hawa wanashiriki na kutekeleza mikakati ya kuhujumu uchumi, na ustawi wa viwanda, elimu, nidhamu ya kazi na uwajibikaji huru na wa pamoja. Kwa mfano, tunaona Kiongozi 2 aliyetoka jukwaani kujinadi na kupiga vita ubepari na ukupe katika jamii (rej. uk. 17), anaposhuka anawashawishi Meneja na Mkurugenzi kwenda kinyume na maadili ya Azimio la Arusha kwa faida binafsi. Haya tuliyabaini kupitia data nukuliwa kutoka kinywa cha Kiongozi 2, kwa mfano, “Aa! Mimi nilidhani una nyumba nyingi sana kumbe nne tu. Mbona mimi ninazo kumi (*anacheka*) na sina tatizo.” Data nyingine nukuliwa inayomwonesha kiongozi kuhujumu uchumi wa

taifa na jamii ni “Nilitaka unisafirishie mzigo wangu kwenda Marekani. Je, si inawezekana?” Na “Aa! Usiwajali hao, wote wako chini ya Chama wale.”

Matendo ya viongozi na watendaji hawa ni kinyume cha sheria, kanuni na miiko ya uongozi chini ya Azimio la Arusha kama inavyoelezwa na wanazuoni wengine (rej. Fouéré 2014; TANU, 1967). Ally na wenzake (2013) na Sitta (2013) wamelitambulisha tatizo hili kama tatizo kubwa miongoni mwa watendaji na viongozi wengi wa umma wa wakati huo na wa zama hizi. Vilevile, utafiti umebaini kuwa, waandishi wameonesha aina nyingine ya uhujumu uchumi unaotokana na uhalalishwaji wa mfumo mpya wa kusimamia uchumi kupitia sheria kandamizi zinazotumika kuuha uchumi wa taifa. Kitendo cha chama na serikali kutaifisha mali za watu kwa maslahi ya taifa ni dosari kubwa katika utekelezaji wa Azimio la Arusha. Kwani walionyang’anywa mali hizi mathalani viwanda, walianza kushirikiana na viongozi wasiowaaminifu kuhujumu viwanda husika kama tulivyoona katika mazungumzo baina ya Meneja na Mkurugenzi (uk. 19 - 20).

Data za utafiti kutoka nukuu ya Meneja isemayo “Unajua bwana kiwanda changu kimechukuliwa?” na ile isemayo “Kama ni hivyo, basi hamna taabu, maana yake nyie ndio viongozi wa Chama na serikali, mtume mtoto kesho aje achukue fomu za kujaza” zinathibitisha uozo wa viongozi baadhi katika kusimamia uchumi wa taifa. Huu ni ushahidi unaodhihirisha jinsi kundi dogo linaloongozwa na viongozi wasiowaaminifu wala wazalendo linavyokosa utu na utashi wa dhati wa kuwasaidia wananchi na taifa kujikomboa kiuchumi. Kwa mujibu wa Chachage (2000), ukosefu wa utu, utashi wa dhati na umakini miongoni mwa viongozi, huchangia sana kuua dira na kesho ya taifa – kiuchumi na kijamii. Suala hili limejengwa kiubunifu kupitia

uteuzi wa maneno mahususi yanayotambulisha kuwapo kwa dhuluma na uhujumu uchumi kwa faida ya kundi dogo katika jamii.

Suala la uhujumu uchumi halijaishia kujadiliwa na waandishi wa awamu ya Azimio la Arusha pekee, bali hata waandishi wa awamu ya soko huria. Jambo hili linaonesha kuwapo kwa dondasugu lililojigeuza kansa maungoni mwa wazawa wachache waliojaa hila, tamaa, ubinafsi na ukatili usiopimika. Wachache hawa wanaonekana kutumia vibaya fursa za uongozi na mamlaka kuendeleza mfumo wa kibepari unaowajali wachache na kuwaangamiza walio wengi wanaoendelea kuishi katika mzunguko wa umasikini. Viongozi wengi wanaonekana kutokuwa sehemu ya mapambano dhidi ya unyonyaji, dhuluma, ulanguzi, ufisadi na kujilimbikizia mali. Wala hawaonekani kutengeneza na kusimamia mfumo wezeshi kwa kila mwananchi kuhodhi na kushirikiana kwa usawa, juhudi na maarifa katika kukuza na kuendeleza uchumi shirikishi. Kitendo cha viongozi kuwa sehemu ya tabaka tawala lililodhalimu, kunasababisha mwananchi wa tabaka la chini kuonewa na kudhulumiwa kila wakati. Haya yamebainishwa pia katika tamthilia ya *Safari ya Chinga*. Tazama nukuu ifuatayo: -

**Che Mundu:** Ulipata magunia mangapi?

**Mata:** Magunia matano. Kila moja nimeuza shingi elfu tano tano.

**Che Mundu:** Wanunuzi wa huko njini wanatunyonya kweli. Wenzetu wanauza gunia moja shingi elfu selasini. Sisi tunaokata miti na kula moshi na vumbi tunapata pesa kiduchu?

**Bi. Somoe:** Ehe mara nyingi nkulima huwa hafaidiki sana. Si unaona korosho tunapata nazo tabu sana. Tunahangaika kufyekea na kupulizia dawa. Lakini ukija kuuza kilo



shingi mia mbili. Eti korosho zetu hazina ubora. Mara soko la dunia limeshuka. Lakini wenzetu huko njini, kwenye kifuko kidogo tu korosho zinauzwa shingi elfu tano.

**Che Mundu:** Natamani siku moja ningepata nafasi ya kwenda huko soko la dunia! Nikawaeleze tabu tunazopata. Ndo mana watu wengine wanaamua kutokupalilia kabisa mikorosho yao. Bei duni na bado tunauza kwa nkopo na kulipwa kwa awamu. Pembejeo na madawa bei kubwa. Wakulima tutaendelea kweli? (uk. 12)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Safari ya Chinga*, 2009)

Data kutoka mjadala kati ya Che Mundu, Mata na Bi. Somoe tuliounukuu unaonesha namna wanyonge wanavyoshindwa kunufaika na jasho lao. Kauli kama vile “Wanunuzi wa huko njini wanatunyonya kweli. Wenzetu wanauza dunia moja shingi elfu selasini. Sisi tunaokata miti na kula moshi na vumbi tunapata pesa kiduchu?” “Tunahangaika kufyekea na kupulizia dawa. Lakini ukija kuuza kilo shingi mia mbili. Eti korosho zetu hazina ubora. Mara soko la dunia limeshuka. Lakini wenzetu huko njini, kwenye kifuko kidogo tu korosho zinauzwa shingi elfu tano” na “Bei duni na bado tunauza kwa nkopo na kulipwa kwa awamu. Pembejeo na madawa bei kubwa. Wakulima tutaendelea kweli?” zinatoa picha angavu. Picha tunayoipata hapa ni kwamba, mnyonge ananyonywa na mkoloni mweusi na mkoloni mweupe kwa wakati mmoja. Masikini ananyonywa, kudhulumiwa na kusalitiwa kwa njia mbalimbali zikiwemo kupangiwa bei ya raslimali zinazotumika katika shughuli za uzalishaji mali, malipo duni tena yasiyo ya mkupuo mmoja, pia kupangiwa bei ya bidhaa wanazozuza kwa wanunuzi. Masikini hawa hawana uwezo wala mamlaka ya

kupanga bei ya bidhaa wanazonunua au kuzalisha. Tena, hawana uwezo wa kuchagua pa kwenda kuuza bidhaa zao. Kundi hili halionekani kuwa na nafasi ya kupata malipo ya uhakika na kwa mkupuo mmoja. Huu nao ni uhujumu uchumi wa kundi kubwa katika jamii na taifa.

Stewart (1951) anasema, uchumi wa aina hii siyo shirikishi wala endelevu kwa taifa linalopigania kujikomboa kiuchumi, kisiasa na kijamii. Daima, uchumi wa namna hii huzalisha chuki na visasi. Mfumo huu huzalisha matabaka yanayoishi kwa kuwindana. Mathalani, tabaka la kati la mabepari uchwara wanaopatikana ndani ya tabaka tawaliwa ambao hudhulumu na kuiba jasho la mtu wa chini. Na, punde wapatapo nafasi hulihujumu hata tabaka tawala bila hofu wala uoga. Athari hasi za mfumo huu wa kinyonyaji na kidhalimu ni jamii kukosa maadili, haki, upendo, ulinzi na usalama, na usawa kwa wote. Badala yake, kila mtu hujigeuza “mzalendo” mwenye kutumia kila aina ya fursa kujitajirisha kwa njia na gharama yoyote ile – iwe ya halali au isiyohalali. Hali inayosababisha kuibuka kwa kundi la kati dhalimu linalotokana na tabaka tawaliwa.

Shivji (1976; 1985) anaongeza kuwa, kundi la tabaka la kati hujiona kama sehemu ya tabaka tawala kwa kuanza kuishi maisha ya ujanjaujanja yanayowafanya kubuni mbinu zitakazowasaidia kusaka mali kwa njia halali na haramu mfano wizi na utapeli. Huku wakipambana kujinasibisha na tabaka tawala kwa lengo la kukubalika na kulindwa. Kwani pindi wanapojilinganisha na tabaka tawala lililojaa uovu, hujiona yale watendayo ni si lolote wala chochote bila kutambua ya kwamba mbuyu nao ulianza kama mchicha. Ni katika juhudi hizi, tabaka tawala huwaona watu wa kundi la kati kuwa watu sahihi wa kutumika kuvuna kwa niaba yao, kulinda na

kuficha siri za uovu wa tabaka la juu. Matokeo yake, mnyonge anajikuta yuko katikati ya matabaka dhalimu mawili (2) yanayomnyonya na kumdunisha katika kila hali na kila nyanja ya maisha. Hii ndiyo hali halisi iliyojengwa kiubunifu kupitia uteuzi wa maneno mahususi yanayotambulisha kuwapo kwa dhuluma na uhujumu uchumi kwa faida ya kundi dogo katika jamii.

Hali hii ya tabaka la kati kutamani na kuhalalisha matendo maovu yenye kusababisha dhuluma, wizi, unyonyaji na hasara kwa kundi jingine linaloshikilia uchumi ndiyo inayojitokeza kwa mara nyingine katika tamthilia ya *Safari ya Chinga*. Mwandishi anaonesha namna uchumi usivyokuwa shirikishi kwa wananchi wote, na athari yake kwa ustawi na maendeleo ya jamii nzima. Badala ya watu kushirikiana kukuza uchumi, wao huunda makundi yenye umoja na mshikamano kwa lengo la kushirikiana kuhujumu, kuiba na kufisadi mali za wengine. Mbaya zaidi, kila kundi linaonekana kuamini kile linachokifanya ni sahihi na halali. Tazama nukuu ifuatayo:

-

**Ntumusha:** Sunche, leo nimekuja na ndugu yangu. Naye anataka kutembeza nguo kama mimi. Amefikia juzi tu toka Ntwara. Bado yu n'geni.

**Sunche:** Ni dugu yako kweli au iko danganya mimi. Hapana letea mutu tapeli. Juzi iko kijana moja letea mimi tapeli hapa. 'Paka leo iko natafuta yeye imekimbia kabisa. Mimi hapana pokea tena mutu ngeni. (uk. 24)

**Beka:** *(Anaongea na akina Ntumusha kwa sauti ya chini).* Kama kawaida nimeongeza nguo mbili mbili katika kila fungu.

**Ntumusha:** *(Kwa sauti ya chini).* Poa haina noma.

**Beka:** Mwambie rafiki yako asiye akanigeuka baadaye.

**Ntumusha:** Huyu wangu hana noma. Ntamweleza mipango yote.  
(uk. 27)

**Ntumusha:** Ndo hivyo njini tunavyoishi. Maisha ni ujanja na kusaidiana. Ni kama zile nguo alizotupa Beka. Unauza na nnagawana pesa kidogo. Hivi ni baadhi ya vitu ambavyo vinatupatia faida.

**Mata:** Ikitokea siku tukagundulika na tajiri?

**Ntumusha:** Sio rahisi. Usiwe mwoga. Wenzako wanaiba mabilioni we unaogopa hivi vijisenti tu? Bila hivyo hapa njini hatuwezi kuishi. Ukikamatwa unalipa.

**Mata:** Baba alisema nisiibe. Wahenga pia hawatafurahi nikiwa na tabia hiyo. Inaweza kuniletea matatizo.

**Ntumusha:** Sisi hatuibi ila tunakula kazini. Na unakula kwa urefu wa kamba yako. Mwizi ni yule anayetumia nguvu. (uk. 31-32)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Safari ya Chinga*, 2009)

Ukichunguza nukuu hii, utagundua kuwa hujuma ya kiuchumi haifanywi na matajiri pamoja na viongozi pekee. Hata watu wa hali ya chini nao wanashiriki bila hofu kuhujumu uchumi wa waajiri na taifa kwa jumla. Data tuliyonukuu inaonesha tamaa ya vijana kutumia njia haramu kujiongezea kipato kinyume cha utaratibu kama anavyosema Beka kwa Ntumusha “[...] Kama kawaida nimeongeza nguo mbili mbili katika kila fungu. Mwambie rafiki yako asije akanigeuka baadaye.” Naye Ntumusha anamfundisha Mata wizi kwa kusema, “Maisha ni ujanja na kusaidiana. Ni kama zile nguo alizotupa Beka. Unauza na nnagawana pesa kidogo. Hivi ni baadhi ya vitu ambavyo vinatupatia faida.” Data hizi kutoka kauli ya Beka na Ntumusha zinaonesha namna vijana wasio na mitaji wanavyotamani kujiajiri na kusimamia biashara zao ili

siku moja wawe wamiliki wa biashara kubwa kama alivyo tajiri mwajiri wao - Sunche. Kwa kukosa mitaji, data nukuliwa inawaonesha vijana Beka, Mata na Ntumusha anaishia kujiingiza katika kumhujumu Sunche.

Laiti uchumi wa Sunche ungekuwa ni sehemu ya uchumi jumuishi katika biashara na ajira, vijana hawa wasingeweza kumuibia Sunche. Kitendo cha Sunche kunyonya jasho la vijana Beka na Ntumusha ndicho kinachowasukuma vijana hawa kumhujumu. Huku wakihalalisha wizi wao mdogo kuwa siyo wizi kwa kujilinganisha na wale wanaofyonza raslimali nyingi za taifa na jamii kwa manufaa binafsi, kama asemavyo Ntumusha, “Usiwe mwoga. Wenzako wanaiba mabilioni we unaogopa hivi vijisenti tu? Bila hivyo hapa njini hatuwezi kuishi. Ukikamatwa unalipa. [...] Sisi hatuibi ila tunakula kazini. Na unakula kwa urefu wa kamba yako. Mwizi ni yule anayetumia nguvu.”

Data za utafiti huu inaonesha kuwa mwandishi anadhihirisha kwamba hujuma za kiuchumi zinazalisha matabaka yasiyokuwa na utu wala huruma kwani kila mmoja anapambana kujinasua kutoka katika hali ya umasikini. Matokeo yake, baadhi ya watu katika jamii wanageuka wezi, wanyonyaji, wadhulumati, wakatili, vibaka na waporaji wa mali za watu wengine kama ilivyotokea kwa kijana aliyepotea na mali za Sunche (uk. 24) na kumuacha Sunche akilalama, “[...]. Hapana letea mutu tapeli. Juzi iko kijana moja letea mimi tapeli hapa. ‘Paka leo iko natafuta yeye imekimbia kabisa. Mimi hapana pokea tena mutu ngeni.’” Au wale vijana waliopora mali za wafanyabiashara wadogo wadogo siku ya kile kilichoitwa usafishaji jiji (uk. 46) na kuwaacha akina Mata na Ntumusha wakilalama; kama asemavyo Mata, “[...] kitu ambacho kimeniuma ni vibaka kutuibia mali zetu. Yaani waliiba kama nyuki. Hata

sijui walitoka wapi. Walinyang'anya hata kama nguo ulishika nkononi. Ama kweli kufa kufaana. Huwezi kuamini hakuna kitu tulichosevu" (uk. 51).

Hapa tunaona badala ya watu kushirikiana kukuza uchumi, wao wanajitahidi kwa gharama yoyote ile kuhujumu uchumi. Kwa mujibu wa Nyerere (1970, 1973) kuwapo kwa matabaka yasiyo sawia kiuchumi ni kielelezo cha jamii kutokujali utu, umoja, amani, ulinzi wala ujenzi wa uchumi wenye fursa sawa na shirikishi kwa wote. Kwa sababu jamii isiyotenda haki wala usawa, huishia kuviziana na kuhujumiana huku wengine wakitumia mabavu kujihami na kuhodhi uchumi wote. Hivyo, kuna umuhimu wa kupigania haki na usawa endelevu katika jamii. Hali hii imejengwa kiubunifu kupitia uteuzi wa maneno mahususi yanayotambulisha kuwapo kwa dhuluma na uhujumu uchumi kwa faida ya kundi dogo katika jamii.

Tatizo la uchumi duni na usiokuwa shirikishi miongoni mwa wanajamii hasa jamii ya watu wa tabaka la chini la wanyonge wasiolindwa wala kuthaminiwa limejitokeza pia katika tamthilia ya *Changamoto*. Katika tamthilia hii, mwandishi anaonesha namna uduni wa kipato unavyozalisha tabaka la masikini jeuri, katili, wadhalimu, wanyonyaji, na mabepari uchwara wanaowageuza wanyonge kuwa vyanzo vyao vya mapato na utajiri. Mwandishi anamchora Kimweri kama mwanadamu katili na mnyonyaji asiye na haya wala utu kutokana na tabia yake ya uporaji wa jasho la watu wengine katika jamii. Hili tunalionga katika mvutano unaojidhihirisha katika nukuu ifuatayo: -

- Kimweri:** Nyie vilema mnangoja nini hapa?
- Peti:** Koma! Kilema ni wewe. Sisi sio vilema, sisi ni walemavu.
- Kimweri:** Sasa unakataa nini? Tena wewe una dhambi sana ndiyo maana macho yako yamefumbika! Lione kwanza.
- Peti:** (*Akicheka kwa kejeli*). Hee! Ungejua sikununua upofu? Hongera zako uliyewekeana mkataba na Mungu!
- Kimweri:** Tena wewe ndio unajidai sana (*Akampiga mweleka Peti*).
- Peti:** Mama wee! Nafaa...
- Kimweri:** Tena lete hii. (*Akiupokonya mkoba na kuanza kukimbia, akiufungua*). Siye tuna shida nyie mna pesa zote hizi umezipata wapi wewe kilema?
- Peti:** Wewe laana yako! Na hutaendelea kamwe!
- Kimweri:** Na wewe unasemaje? (*Akielekea alipoketi Megno*) Hamjakoma tu?
- Megno:** Sasa unataka nini? Sema!
- Kimweri:** Wewe kiwete utanifanya nini? (*Akambinua kutoka kwenye baiskeli yake*)
- Megno:** Jamani! Nauawaa! (*Anagaragara chini; Kimweri anachukua baiskeli, anaikunja kunja na anajitwika kichwani na kukimbia nayo*). (uk. 23 – 24)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Changamoto*, 2010)

Data nukuliwa inathibitisha kuwapo kwa matendo ya hujuma hata miongoni mwa watu wa tabaka la chini. Kitendo cha Kimweri kuwapiga watu wenye ulemavu halafu kuchukua mali zao zinazowasaidia katika kujikimu kimaisha kunaonesha kiwango cha juu kabisa cha unyama, dhuluma, ukatili, ubinafsi, unyanyapaa, na unyang'anyi wenye kulenga kuwadunisha daima watu wanyonge. Haya yamethibitishwa na

mwandishi pale anaposema “Tena lete hii. (*Akiupokonya mkoba na kuanza kukimbia, akiufungua*). Siye tuna shida nyie mna pesa zote hizi umezipata wapi wewe kilema?” Dhuluma hii inathibitisha ya kwamba, hata katika tabaka la chini wapo wenye nguvu dhidi ya wengine waliodhaifu.

Kitendo cha Kimweri kwa watu wenye ulemavu kinamaana kubwa. Kwamba, uhujumu uchumi haufanywi na matajiri au viongozi pekee kwa watu wa tabaka la chini. Bali hata walio tabaka la chini wanazidiana nguvu kisha aliye mnyonge anaishia kupokwa haki yake. Badala ya kuwasaidia wanyonge kuinuka kiuchumi, wao wanawanyang’anya wanyonge hata kile kidogo wanachokitumia kujikimu au kujitengenezea fursa za maisha yao, kiuchumi. Huku ndiko kusema ya kwamba, tangu zama za awamu ya Azimio la Arusha hadi awamu hii ya soko huria, uchumi bado unahodhiwa na kundi dogo lenye kuamua hatima ya walio wengi katika jamii. Jambo hili limethibitishwa na Luoga na wenzake (2000). Watatu hawa wanakili kuwapo kwa unyonyaji miongoni mwa wanyonge kunakofanywa na watu wa tabaka la juu wakishirikiana na wale wa tabaka la kati. Jambo hili limejengwa kiubunifu kupitia uteuzi wa maneno mahususi yanayotambulisha kuwapo kwa dhuluma na uhujumu uchumi kwa faida ya kundi dogo katika jamii.

Mjadala huu kuhusu hali ya kiuchumi ya walio wachache dhidi ya walio wengi, unaonekana kujitokeza pia katika tamthilia ya *Nje – Ndani*. Waandishi wanaonesha viongozi wengi wamegeuka miungu watu kwa wanyonge hususani wajasiriamali wanaosaka misaada ya kukuza mitaji yao kwa njia ya misaada na mikopo nafuu. Ushahidi wa madai haya unatambulishwa na data ifuatayo inayorejelea mazungumzo kati ya Utashi-Nafsi, Akili, Moyo na Macho: -



**Utashi-Nafsi:** Ama kweli mpe mpika mkate akupikie mkate wako hata akila nusu yake.

**Njozi:** Alaah! Mbona sielewi? [*Anakaa vizuri zaidi sasa pale mkekani*]. Mpika mkate, apike na ale nusu! [*Anashangazwa na maneno yale*]

**Utashi-Nafsi:** Nusu itakayobaki itakuwa ni ya mkate. Ona tulowapa, walivyoharibu mchele wetu, hakuna nusu yetu wala yao haina baraka. [*Anaimba*] Maadui zetu ni marafiki...

Wote watatu twawafikii... (uk. 55)

**Akili:** Utumwa unakujaje sasa? Mbona ulishaisha?

**Moyo:** Chukua moja rudisha mbili, yaani mara mbili!!

**Macho:** Tena ulete mbili kabla hiyo moja haujaipata vizuri.

**Moyo:** Duuuh! Ni ukatili, unyama na ufedhuli mkuuu. (uk. 69 – 70)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Nje – Ndani*, 2016)

Data kutoka katika nukuu hii inaonesha namna wachache wanavyofaidi raslimali za taifa ilhali hali ni tofauti kwa wanyonge hususani wajasiriamali walio wengi. Data inaonesha kuwa wanyonge wengi wanataabika japo kupata fursa ya kujiendeleza kiuchumi na kijamii kupitia mitaji kwa njia ya mikopo na misaada. Haya yanathibitika kupitia kauli kama vile, “Nusu itakayobaki itakuwa ni ya mkate. Ona tulowapa, walivyoharibu mchele wetu, hakuna nusu yetu wala yao haina baraka. [...] Maadui zetu ni marafiki... Wote watatu twawafikii...,” “Chukua moja rudisha mbili, yaani mara mbili!!” “Tena ulete mbili kabla hiyo moja haujaipata vizuri.” Na, “Duuuh! Ni ukatili, unyama na ufedhuli mkuuu.”

Data katika nukuu hizi zinaonesha ya kwamba, ili mtu aweze kupata kitu ni sharti atoe kitu. Pia, misaada na, au mikopo hiyo ni ya kinyonyaji na kiutumwa zaidi kwani

inakutaka urudishe mara mbili ya kile ulichokabidhiwa hata kabla haijazaa matunda tarajiwa. Kwa maneno mengine, unaporudisha ni lazima urudishe mtaji na faida inayolingana au kuzidi mtaji uliotoa mbali ya ile rushwa uliyotoa ili uweze kupata msaada / mkopo huo. Hii ni njia mojawapo ya kuhujumu uchumi wa jamii na taifa. Kwani mikopo na misaada ya namna hii haiwezi kumuinua mnyonge, kamwe. Hali hii inaonesha dhamira za mwandishi zimejengwa kiubunifu kupitia uteuzi wa maneno mahususi yanayotambulisha kuwapo kwa dhuluma na uhujumu uchumi kwa faida ya kundi dogo katika jamii.

Kwa mujibu wa Langa (2013), mazingira ya mikopo mingi inayotolewa kwa wajasiriamali siyo rafiki na haina tija. Mikopo mingi imejaa masharti magumu kwa wakopaji wa kipato cha chini kuweza kuipata. Maeneo mengine hadi rushwa huombwa ili kuwezesha upatikanaji wa mkopo husika ilhali mwombaji mkopo hana kipato cha kuhonga. Nazo riba ziko juu na muda wa marejesho ni mfupi huku hesabu za marejesho na kiwango cha deni kikiongezeka pasipo kuwapo kwa fomula wazi. Haya yote yanatokana na sekta ya fedha kutokuwa na sera rafiki zaidi kwa mnyonge. Hata sera na sheria zilizopo zinaonekana kutokusimamiwa kikamilifu. Kwa maelezo ya Langa (2013), taasisi za kifedha zilizo nyingi, zimegeuka kitanzi cha mauaji ya biashara na mitaji ya wajasiriamali walio wengi. Kwa hiyo, siyo rahisi kwa mnyonge kuinuka kupitia mfumo wa mikopo uliotawala soko la sasa.

Kwa jumla, tunaweza kusema ya kwamba, waandishi wote katika tamthilia zote sita (6) teule tulizozitalii wamethibitisha kwa njia ya ubunifu katika ujenzi wa dhamira kuwapo kwa dondasugu katika uchumi wa taifa na kwa wananchi walio wengi. Kwamba, tangu zama za awamu ya Azimio la Arusha mpaka zama hizi za awamu ya

soko huria, uchumi bado umo mikononi mwa kundi dogo la wanyonyaji, wadhalimu, wafisidi, wadhulumati, wajaa tamaa na roho za kujilimbikizia mali bila hofu. Shivji (1976) anasema, makundi ya namna hii kwa kawaida hupata nguvu kutokana na kubebwa na mfumo wa kibepari unaolindwa na dola. Vongozi wengi wasiowazalendo huyakumbatia makundi haya kwa maslahi ya wachache na kuwaacha walio wengi nje ya mfumo halali wa umiliki na usimamizi wa mali. Tamthilia zote sita (6) zimeonesha ya kwamba aina hii ya uchumi siyo wezeshi wala shirikishi na kamwe hauwezi kuleta afya yenye tija, usawa, uhuru, umoja, haki, ustawi na maendeleo endelevu katika jamii.

Utafiti huu umebaini kuwa, athari hasi za uchumi usiokuwa rafiki kwa jamii yote ni kujengeka kwa ubaguzi na matabaka ya kiuchumi na kijamii, dhuluma na ukatili, mabepari na vibepari uchwara, wizi na ukibaka. Mengine ni uhamaji holela wa watu kwenda mijini, rushwa na ufigadi, ubinafsi na uungu, husuda na visasi. Huku kila mwenye nguvu huzidisha vita ya kuhodhi mali na fursa. Kila mwizi huhalalisha wizi wake kuwa mfumo halali wa uzalishaji na umiliki wa mali. Matokeo yake, amani na uhakika wa ulinzi na usalama huwa mashakani kila wakati kwani kila mtu anayejiamini hujitahidi kujitutumua kuinuka. Tatizo hili ni kubwa na wanaoonekana kuathirika zaidi ni makundi ya wanyonge hasa vijana waadilifu, wanawake na watu wenye ulemavu (Masabo, 2014; United Nations, 2014).

Kwa hiyo, waandishi hawa wanazidi kupaza sauti juu ya umuhimu wa kuwapa kwa ukombozi wa kweli na endelevu wa kifikra na kiuchumi kwa faida ya jamii nzima. Lengo ni kila mtu aweze kufurahia na kushiriki kikamilifu katika uzalishaji na utumiaji wa fursa na huduma bora na sahihi za kiuchumi na zile wezeshi. Mathalani,

huduma rafiki za kisheria, afya, maji, nishati, elimu, biashara, kilimo, ufugaji, uvuvi, ulinzi na usalama. Vilevile, huduma za miundombinu kama vile barabara na majengo rafiki kwa kila mwanajamii. Kwa sababu jamii ambayo haiwezi kulinda maslahi yake ya kiuchumi, kamwe haiwezi kufanikiwa hata katika nyanja nyingine za maisha (Settles, 1996).

### **Dhamira za Kijamii**

Utafiti huu ulibaini kuwa, tamthilia zote sita (6) teule zimejadili hali ya mambo ilivyo katika masuala ya kijamii. Data zinadhihirisha kuwa waandishi wanaonekana kutambua na kuthibitisha hali duni ya maisha ya wananchi walio wengi. Waandishi wanaonesha kiwango kikubwa cha ufukara miongoni mwa watu wa tabaka la chini. Hali ambayo inaathiri upatikanaji bora wa fursa na utatuzi wa changamoto za kijamii zinazowakabili. Aidha, waandishi wanaonesha mpaka sasa ujinga, umasikini na maradhi bado ni maadui wakuu wa taifa.

Aidha, uduni huu unatokana na kutokuwapo au upatikanaji duni wa huduma bora za kijamii kama vile huduma za afya, maji, nishati, elimu, huduma za kisheria, barabara, masoko na pembejeo. Pia, ugumu wa upatikanaji wa mahitaji mengine ya nyumbani mathalani malazi, chakula na makazi. Hali ni mbaya zaidi pale pengo la hali za maisha linapozidi kuwa kubwa baina ya wale wenye kipato na wale wasio na kipato kama inavyobainishwa katika kila tamthilia teule. Katika tamthilia ya *Mashetani*, mwandishi analithibitisha jambo hili kupitia malumbano baina ya Juma na Kitaru. Data ifuatayo inathibitisha kuwapo kwa changamoto hizi. Tunanukuu: -

JUMA: Hatuwezi kusahau. Kila siku tunafunguliwa vifua na kujazwa sumu ya mambo ya jana.

(*Kitaru anaitikia. Kimya.*)

JUMA: Kwa heri.

KITARU: Hatuonani tena?

JUMA: Hatuonani tena.

KITARU: Kwa nini?

JUMA: Sababu nyingi.

KITARU: Mojawapo?

JUMA: Mpanda ngazi na mshuka ngazi hawewezi kushikana mikono.

KITARU: Pili?

JUMA: Wewe unaishi leo mimi naishi jana. Tutakuwaje marafiki? Na kila leo yako ni kidato cha kesho yako. Mimi, kila leo yangu ni kidato cha jana zangu. Na kila nikienda huko, nikirudi ninarudi na hadithi... hadithi za mashetani. (uk. 56)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Mashetani*, 1971)

Data tuliyoinukuu inaonesha kuwapo kwa pengo la hali ya maisha baina ya makundi yanayowakilishwa na pande hizi mbili, yaani upande wa Juma na ule wa Kitaru. Kitaru anawakilisha kundi la watu wachache wenye uhakika wa maisha bora. Naye Juma anawakilisha kundi la wananchi ambao kadri siku zinavyokwenda, ndivyo hali zao za kimaisha zinavyozidi kuwa mbaya. Picha tunayoipata hapa ni kwamba, hata wakati wa Azimio la Arusha hali ya maisha ya watu wengi ilikuwa ni duni. Na, matumaini ya kujinasua kutoka katika lindi hilo hayakuwapo. Kwa sababu, kila kukicha hali za wanyonge huzidi kuwa mbaya kuliko hapo awali kwa kujazwa ubaguzi, chuki na visasi. Tunayapata haya kupitia Juma anayesema, “Hatuwezi

kusahau. Kila siku tunafunguliwa vifua na kujazwa sumu ya mambo ya jana.” Pia, kauli yake nyingine isemayo, “Wewe unaishi leo mimi naishi jana. Tutakuwaje marafiki? Na kila leo yako ni kidato cha kesho yako. Mimi, kila leo yangu ni kidato cha jana zangu. Na kila nikienda huko, nikirudi ninarudi na hadithi... hadithi za mashetani.”

Data hii tuliyoinkuu inatupatia tafsiri kuwa, uduni huu wa kimaisha hauwezi kuwakomboa wanyonge kutoka katika lindi la umasikini wa kipato na upatikanaji wa huduma bora za kijamii kwa sababu wachache wamehodhi fursa za maisha bora pasipo huruma wala utashi rafiki kwa watu duni. Matokeo haya ya utafiti wetu hayatofautiani na kile kinachoelezwa katika ripoti ya Economic and Social Research Foundation (2018). Ripoti ya Economic and Social Research Foundation (2018) inaonesha kuwa, hali ya huduma za kijamii katika nchi nyingi zilizochini kiuchumi siyo nzuri kabisa. Na, hali hiyo itakuwa mbaya kadri siku zinavyozidi kusonga mbele kutokana na majanga ya asili, vita, umaskini, migogoro ya kisiasa, utoroshaji wa raslimali na ubinafsi wa waliohodhi uchumi wa taifa na jamii. Kwa ufafanuzi huu, ni dhahiri kwamba Ebrahim N. Hussein alitumia ubunifu katika kuteua na kujenga kiweledi dhamira zake.

Tatizo la wananchi wengi kukabiliwa na hali duni katika upatikanaji wa huduma na maisha bora ya kijamii, yanajadiliwa pia katika tamthilia ya *Kijiji Chetu*. Tunayaona haya kupitia data tulizozikusanya wakati wa utafiti wetu. Miongoni mwa data hizo ni hii ifuatayo: -

**BI KIZITO:** [...] Nikufanyie kazi zote, kwa nini? Mimi si mtumwa wako umesikia? Uliponioa hatukukubaliana kuwa nitakuwa mtumwa. Mimi ni binadamu kama wewe. Nimechoka, kila siku niwe wa mwisho kutoka shambani kwa sababu ya kukulimia wewe... Hushangai kwa nini nyumba yetu hupata chakula kidogo kuliko zingine....

**KIZITO:** Wanakuibia. Kama tunagawana sawa kwa nini ulalamike kuwa unapunjwa? Sasa usawa huo uko wapi!

**BI KIZITO:** Tazama, unashindwa kuelewa hata kitu kimoja katika siasa ya ujamaa na vijiji vya ujamaa. Nani analalamika kuwa anapunjwa? Ninachokuambia ni kuwa katika hisa yetu ya ushirika ninapata mimi tu ambapo nyumba zingine wanapata zaidi kwa sababu ya uzito wa kazi yao katika shamba la ushirika. Wenzangu hupalilia sehemu kubwa kuliko mimi kwa sababu bibi na bwana huwa kitu kimoja. Lakini sio wewe na mimi, hata. Leo utakwenda shambani. (uk. 3)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Kijiji Chetu*, 1975)

Data tuliyoinkuu ya mvutano baina ya Bi Kizito na Kizito inaonesha uduni wa maisha ya familia hii kutokana na kukosekana kwa ukombozi wa kifikra unaomwandama Bi Kizito. Bi Kizito anaonekana hakufanikiwa kupata elimu sahihi. Hata elimu ya siasa ya ujamaa na kujitegemea hakuielewa vizuri. Kama aliipata, basi haikufanikiwa kumkomboa. Bali ilikuwa ya kuhitimu kiwango fulani cha elimu; tofauti na Kizito (rej. uk. 24 – 27). Kauli zake za kwamba “Nimechoka, kila siku niwe wa mwisho kutoka shambani kwa sababu ya kukulimia wewe... Hushangai kwa nini nyumba yetu hupata chakula kidogo kuliko zingine....” ni dhahiri kwamba Bi Kizito angali katika ujinga kwa kukosa elimu sahihi. Pia, kauli yake ya “Nani

analalamika kuwa anapunjwa? Ninachokuambia ni kuwa katika hisa yetu ya ushirika ninapata mimi tu ambapo nyumba zingine wanapata zaidi kwa sababu ya uzito wa kazi yao katika shamba la ushirika. Wenzangu hupalilia sehemu kubwa kuliko mimi kwa sababu bibi na bwana huwa kitu kimoja. Lakini sio wewe na mimi, hata” nayo inayothibitisha kwamba changamoto ya elimu ya utambuzi sahihi wa mambo miongoni mwa wanajamii wengi ni kubwa. Tafsiri tunayoipata katika data hii ni kuwa, elimu sahihi bado ni changamoto kwa wananchi walio wengi. Kwani, elimu inatakiwa imkomboe mtu kwa kumsaidia kutambua na kuzitathmini changamoto zilizomo katika mazingira yake na kuzitatua kisayansi au kufanya maboresho kwa faida yake na kizazi chake na vijavyo (Independent Commission of the South on Development Issues, 1992).

Kitendo cha Bi Kizito kutokuweza kung’amua changamoto zinazomkabili katika mgawanyo wa mali zitokanazo na jasho lake katika shamba la kijiji, kunaonesha kutokuwa na elimu sahihi na bora yenye kumsaidia mtu kujikomboa kifikra na kijamii. Hii ni ishara ya kwamba, mifumo na huduma za kijamii katika kijiji cha ujamaa ni duni na isiyokuwa na msaada wa kiukombozi kwa watu wa hali ya chini. Jamii yenye watu kama Bi Kizito haiwezi kupata maendeleo ya kijamii kamwe. Badala yake wajanja wachache watawatumia kama manamba kwa manufaa ya hao wajanja na kundi lao.

Changamoto za maisha duni ya kijamii zenye kuathiri maisha ya watu kwa namna hasi, zinajitokeza na kujadiliwa pia katika tamthilia ya *Harakati za Ukombozi*. Katika tamthilia ya *Harakati za Ukombozi*, waandishi wanaonesha sababu mojawapo ya wananchi wengi kuwa duni ni kutokana na usaliti wa “wazalendo” wazawa



waliopewa dhamana ya kuleta mabadiliko chanya kwa jamii kushindwa kufanya hivyo. Badala yake wanageuka wazungu kwa kwenda kuishi maeneo yaliyokuwa yameendelezwa na wakoloni huku wakijisahaulisha magumu ya wananchi wenzao waliowaacha katika maeneo yenye miundombinu na huduma duni ya kijamii (Mwiru, 2013). Hoja hii inathibitishwa na Mzee kupitia data ifuatayo: -

**MZEE:** Uhuru tuliupata, ndiyo. Lakini haukuleta mapinduzi yoyote. Kwani hao ndugu zetu, ambao walishika madaraka baada ya kuondoka wakoloni, walirithi pia zile tabia za kikoloni. Walijifanya Wazungu weusi. Walihama kule Buguruni na kwenda kuishi Uzunguni. Basi mambo yao yakawa ya uzungu – uzungu na kuanza kutunyonya na kutunyanyasa sisi ndugu zao. Hivyo, uhuru wetu ulikuwa wa bendera tu na sio wa kuleta mapinduzi... (uk. 11 – 12)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Harakati za Ukombozi*, 1982)

Data hii tuliyoinkuu kutoka kinywani mwa Mzee inaonesha namna viongozi wasaliti walivyoshindwa kuleta maendeleo na ustawi endelevu wa jamii nzima. Badala ya kuwasaidia wanyonge kupiga hatua chanya kimaendeleo, viongozi hawa wasiowaaminifu kwa makabwela wanageuka wanyonyaji wa jasho la wananchi wanyonge. Mwandishi analiumba jambo hili kwa ufasaha pale anaposema, “Uhuru tuliupata, ndiyo. Lakini haukuleta mapinduzi yoyote. [...] hao ndugu zetu, ambao walishika madaraka baada ya kuondoka wakoloni, walirithi pia zile tabia za kikoloni.” Mzee anaongeza kusema, “Walijifanya Wazungu weusi. [...] kuanza kutunyonya na kutunyanyasa sisi ndugu zao. Hivyo, uhuru wetu ulikuwa wa bendera tu na sio wa kuleta mapinduzi...”

Nukuu hii inathibitisha athari ya ukolonimamboleo kupitia vibaraka wa ukoloni walioshika hatamu ya uongozi wa nchi. Huu ni ushahidi mwingine unaoonesha kwamba, kipindi cha awamu ya Azimio la Arusha jamii kubwa iliendelea kuwa nyuma kimaendeleo. Dhamira hii imeungwa mkono na waandishi wengine wakiwemo Msekwa (2013) na Mwiru (2013). Kwa maelezo ya Msekwa (2013) na Mwiru (2013), baadhi ya viongozi wazawa waliwasaliti wananchi mchana kweupe bila hofu wala tashwishwi hivyo wakashindwa kuwapigania na kuwasaidia wananchi kujikomboa kifikra, kiuchumi, kisiasa na kijamii. Kwa data hizi, tunaona kuwa mwandishi ametumia ubunifu kulijenga kisanaa tatizo hili la kijamii.

Ubunifu katika kulisuka wazo la usaliti wa viongozi walio wengi kwa wananchi wanyonge hauonekani kuishia katika awamu ya Azimio la Arusha pekee. Bali unaonekana kujitokeza hata katika awamu ya soko huria. Jambo hili linaonekana kujitokeza vilevile katika tamthilia teule za awamu ya soko huria ambazo ni *Safari ya Chinga* (2009), *Changamoto* (2010), na *Nje – Ndani* (2016). Tamthilia ya *Safari ya Chinga* ndiyo tamthilia teule inayolijadili tatizo la hali ngumu ya maisha ya wanyonge kwa uwazi na upana zaidi. Katika tamthilia hii mwandishi Shani Omari anaonesha kuwapo kwa huduma chache na duni zaidi miongoni mwa wananchi wa kipato duni.

Mwandishi anaonesha namna wakulima wanavyonyonywa kupitia mazao wanayovuna na kuuza. Pia, wananyonywa kupitia bidhaa wanazonunua. Mambo mengine ni kukosekana kwa fursa ya watu kupata elimu hata ya kujua kusoma na kuandika, uhakika wa mawasiliano bora kati ya miji na vijiji, kilimo duni, pamoja na ulinzi duni wa mali na mitaji ya wanyonge. Mwandishi ameonesha pia changamoto

ya ajira, maradhi, barabara na maji kuwa ni matatizo makubwa yanayoigharimu jamii kubwa. Ushahidi wa mambo haya unaonekana kupitia data ifuatayo: -

**Mata:** (*Anampa mama yake kikombe*). Mama naomba niongezee uji.

**Bi. Somoe:** (*Anamtilia*). Kunywa taratibu, wenzako wakirudi kisimani watahaha kwa njaa kama mbwa.

**Uruka:** (*Anaenda jikoni na kurudi na vikombe na ming'oko kwenye sinia la bati lililokatikatika kwa uchakavu. Anaweka chini*). Mama na leo umepika ming'oko?! Afadhali ungepika mihogo. Mi nimechoka kula ming'oko kila siku. (uk. 2)

**Bi. Somoe:** (*Anainuka*). Ngoja niwatue. Kijasho kinawatoka. Mmechoka sana. Jua limeshapanda (*Akiwatua mmoja baada ya mwingine*). Vipi mbona mmechelewa sana leo?

**Singilipo:** (*Akijifuta jasho na maji usoni*). Kisimani kulikuwa na foleni. Tulikuta watu wa kule juu wameshafika. Na bado hawajachota. Si unajua kiangazi hiki maji ya tabu mama? Ni ya kungojea.

**Sijaona:** (*Anakaa kwenye mkeka karibu na mama yake*). Uhf! Halafu kuni pia zimekuwa shida. Ilibidi twende kule kilimani. Kule bondeni ziko ndogondogo sana. (uk. 3 & 4)

**Joffu:** Nasikia huko njini barabara zote zina lami. Tofauti na huku kwetu tunalima korosho lakini bado kila kitu ni shida. Maji safi, umeme, barabara nzuri bado kwetu ni kitendawaili. Kazi ndo kama hivyo hakuna, kisomo hatuna. Basi maisha yamekuwa kama shubiri. (uk. 8-9)

**Mata:** Mi naamini maisha ni popote tu. Ndugu utawapata mbele kwa mbele. Jirani yako, rafiki yako ndo ndugu

zako. Hata nikiendelea kukaa hapa kijijini hakuna ntakachopata. Elimu ya darasa moja sina. Ndugu zangu pia hawana elimu. Kazi ya maana sina. Sasa nitakaa hapa kijijini tunaangaliana mpaka lini? Nami nahitaji kuwa na nji wangu. Na wazazi ndo wameshakuwa wazee. Nami ndo ntoto wao nkubwa. (uk. 10)

**Mata:** (*Huku mate yakimtoka*). Eh bwana sirikali kiboko. Kweli ikiamua jambo lake haishindwi. Yaani imesafisha jiji zima. Wamachinga, wapiga debe, machangudoa, mama ntilie, mateja, gereji bubu, vituo vidogo vya mafuta... (uk. 50)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Safari ya Chinga*, 2009)

Kupitia data katika nukuu hii tunabaini namna watu wa vijijini wanavyopata taabu katika kuzitafuta na kuzipata huduma za kijamii. Maelezo ya wananchi hawa yanaonesha ugumu wa kuzipata huduma za kijamii hata zile zisizokuwa bora. Mbali ya hali duni ya huko vijijini, mwandishi kupitia Mata anaonesha ya kwamba, hata mjini, maisha ya mtu wa hali ya chini ni duni na magumu kama anavyosema, “unajua watu wengi wa vijijini tunafikiri maisha ya njini ni rahisi na mazuri sana.” Kauli ya Mata inaungwa mkono na Ntumusha anayekiri hivi, “[...] Ni kweli lakini kwa wachache tu. Si kwa kila ntu. Walalahoi wengi maisha yetu ndo kama hivi” (uk. 27 - 28).

Ngwale na Kironde (2000) wanaiona hali hii kama zao la viongozi na watendaji kushindwa kutambua mahitaji halisi, raslimali sahihi, wakati halisi na mipango halisi katika kuteua, kutekeleza na kusimamia mgawanyo wa raslimali na vipaumbele. Aidha, utafiti umebaini kuwa, utambuzi wa matatizo ya kijamii uliojadiliwa na Shani

Omari unafungamana na ripoti ya Economic and Social Research Foundation (2018). Katika ripoti hii, kunaoneshwa kuwa hali ya umasikini vijijini bado ni kubwa kuliko maeneo ya mijini. Vijiji vingi vinakabiliwa na miundombinu duni na kwingine hakuna kabisa baadhi ya huduma za msingi. Ripoti hii inaonesha hata mijini, hali siyo bora sana katika maeneo mengi - ijapokuwa ni ahueni ikilinganishwa na vijijini.

Ugumu wa maisha na changamoto lukuki za kijamii zinazowakabili watu wa tabaka la chini unasawiriwa pia katika tamthilia ya *Changamoto*. Katika tamthilia hii, tunaona watu wa hali ya chini aghalabu watu wenye ulemavu wakishindwa kupata huduma sahihi na bora kutokana na kuwapo kwa changamoto tofauti tofauti. Baadhi ya changamoto hizo ni miundombinu isiyorafiki kwa hali ya maumbile yao, unyanyapaa, ubaguzi na hujuma. Changamoto hizi na nyingine zimesababisha watu wenye ulemavu kuwa na maisha duni. Huku baadhi ya watu wa tabaka la chini wasiokuwa na ulemavu wanatumia mbinu ovu kusaka utajiri kupitia watu wenye ulemavu. Matokeo yake, usalama na ulinzi wa mtu mnyonge unazidi kuwa shakani zaidi. Mathalani, tukio la Abuu linatupa picha kamili juu ya hali ya mtu mnyonge kijamii. Data ifuatayo inatupatia picha kamili: -

**Mganga:** (*Akimwangalia Abuu kwa macho ya ukali*) Unasikia kijana, waungwana wamesikia shida yako. Wanasema utakuwa tajiri ndani ya siku mbili zijazo. Kinachotakiwa ni kuzingatia maagizo.

**Abuu:** Sawa mzee.

**Mganga:** Wanataka mkono wa albino.

**Abuu:** Sawa mzee.

**Mganga:** Uulete kesho kabla mizimu haijakasirika na kukugeuzia kibao.

**Abuu:** Sawa mzee. (uk. 15)

*([...] Kuko kimya. Anaonekana Abuu akizunguka zunguka jukwaani. Mkononi ameshika panga. [...] Chuni anapigwa panga la usoni na anaanguka chini. Chuni anapiga kelele kuomba msaada. Abuu anamnyakua Kauye na anakimbia na kutokomea nyuma ya jukwaa...) [...] (uk. 19)*

*[...] Pazia linafunguliwa panaonekana ni kiringeni kwa mganga wa kienyeji... Abuu ameshika mkono wa mtoto albino na anamkabidhi mganga.*

**Mganga:** *(Akiupokea)* Marahaba... Sasa shida zako zimekwisha tangu sasa. Utaona utajiri ukimiminika tangu dakika hii.

**Abuu:** Sawa mzee. (uk. 21)

**(Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Changamoto*, 2010)

Data hii inaonesha changamoto ya maisha duni yaliyojaa imani potofu. Kitendo cha Abuu kwenda kwa Mganga wa kienyeji kusaka utajiri, kuamini na kutii maagizo ya mganga, na kitendo chake cha kumuua Kauye – mlemavu wa ngozi – albino; kama sharti la kupata utajiri baada ya kupeleka mkono, kunaonesha ukubwa wa tatizo la maisha duni yanayowakabili watu wa tabaka la chini. Matokeo ya ugumu huo wa maisha, yanazalisha imani potofu. Hatimaye Imani potofu inaishia kuhujumu haki ya kuishi ya watu wanyonge zaidi katika jamii kama mwandishi anavyosema kupitia Mganga, “Unasikia kijana, waungwana wamesikia shida yako. Wanasema utakuwa tajiri ndani ya siku mbili zijazo. Kinachotakiwa ni kuzingatia maagizo.” Mganga anaongeza, “Wanataka mkono wa albino.” Baada ya mkono wa albino kuletwa, Mganga anasema, “Sasa shida zako zimekwisha tangu sasa. Utaona utajiri ukimiminika tangu dakika hii.”

Utafiti umebaini kuwa, laiti kama kipato cha watu wa tabaka la chini kingekuwa kizuri, basi watu hawa wasingeweza kufikiria kufanya hata mauaji ya watu wanyonge zaidi katika jamii yao. Vilevile, kama mfumo wa maisha ya kijamii ungekuwa rafiki kwa watu wote, basi maisha ya watu wa tabaka la chini wasingeweza kushuhudia wala kuishi maisha yaliyojaa utabaka, ukatili, ubaguzi, chuki na dharau kwa watu wanyonge zaidi. Kitendo cha kuwapo kwa mateso ya namna hii miongoni mwa watu wa tabaka la chini, kinathibitisha ugumu na changamoto katika maisha wanayopitia watu hawa kinyume na wale wa tabaka la juu. Wazambi na Mikongoti (2018) wanakiri kuwapo kwa mauaji ya watu wasio na hatia katika jamii kwa kile kinachoitwa imani potofu pamoja na tabia ya baadhi ya watu kujichukulia sheria mkononi kunakofanywa na jamii ambayo haijaelimika vya kutosha au kushuhudia haki ikitendeka pasipo kuacha shaka yoyote.

Tatizo la mauaji ya wanyonge hususani watu wenye ulemavu hasa wa ngozi limejitokeza hata kwenye tamthilia ya *Nje – Ndani* (uk. 58 & 60). Zaidi ya tukio hilo, waandishi wanaonesha namna viongozi walivyoshindwa kuondoa umasikini, maradhi na ujinga miongoni mwa wananchi wanyonge. Badala yake, dhuluma na unyonyaji vimeshika hatamu. Jambo linalosababisha hali ya maisha ya watu wengi kuzidi kuwa ya kijungujiko kama siyo ya pangu pakavu tia mchuzi. Hali hii ya unyonge na ugumu wa maisha ya watu hasa wale wa tabaka la chini inafafanuliwa kwa ustadi kupitia mazungumzo baina ya Njozi na Utashi-Nafsi. Data ifuatayo inasawili hali ya unyonge na ugumu wa maisha: -

**Utashi-Nafsi:** Nusu itakayobaki itakuwa ni ya mkate. Ona tulowapa, walivyoharibu mchele wetu, hakuna nusu yetu wala yao haina baraka. [*Anaimba*] Maadui zetu ni marafiki...

Wote watatu twawafikii...

Abah aba ba ba ba...

Alo ho ha heeeee...

Maradhi kipenziii

Ujinga laaziziii...

Umasikiniiii...

**Njozi:** Maradhi? Ujinga? Umasikini? Maadui? Marafiki? ...  
Loh!

**Utashi-Nafsi:** Wastaafu Mhenga.

**Njozi:** Wepi? Walimu? Wanajeshi? Wauguzi? Madaktari? au watumishi wengine wa umma?

**Utashi-Nafsi:** Wakatunza amana, wakadhani itakuja kutumika kwa huruma, upole, uangalifu, uadilifu, utu, wema na haki ya kweli. Eti ingewakuta uzeeni.

**Njozi:** Sasa je?

**Utashi-Nafsi:** Takataka, mapambo, fakhari, sifa, udhaifu na kero. Haikufaa jana, leo wala haitasaidia kesho. (uk. 55 - 57)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Nje – Ndani*, 2016)

Data tuliyoinukuu inadhihirisha namna wananchi walio wengi walivyokata tamaa na kupoteza tumaini la kupata ustawi na maendeleo endelevu na ya kweli kupitia viongozi wao. Mwandishi anasema, “Maadui zetu ni marafiki... Wote watatu twawafikii... Abah aba ba ba ba... Alo ho ha heeeee... Maradhi kipenziii Ujinga laaziziii... Umasikiniiii...” Kupitia nukuu hii, utafiti umebaini kwamba, badala ya



maradhi, ujinga na umasikini kuendelea kuwa maadui wakuu wa taifa, sasa wamegeuka kile kinachoweza kutazamwa kama marafiki wapenzi wasioweza kutengana na wananchi wengi walio masikini. Viongozi wengi wamewageuza maadui hawa wakuu wa taifa kuwa fursa, ngazi na daraja la msingi katika kuwafikia wapigakura kwa kuendelea kuwahadaa kwamba watawasambaratisha maadui hao. Uchunguzi tulioufanya katika tamthilia zote sita (6) teule, unatufanya tugundue ya kwamba kila tamthilia imeyatambua maisha ya kijamii ya mtu wa tabaka la chini.

Pia, waandishi wote yanaonekana kukubaliana ya kwamba, maisha ya mtu wa tabaka la chini ni duni na humfanya awe kiumbe mnyonge hata kwa kile kilicho cha halali yake. Vilevile, waandishi kwa namna tofauti tofauti wameonesha sababu na changamoto za ugumu huo wa maisha. Waandishi wanadhihirisha kuwa, ugumu wa maisha ya mtu mnyonge ni tokeo la usaliti, dhuluma, unyonyaji, ufidhuli, ghiribu, rushwa, wizi na ubinafsi. Pia, tamaa za watu wachache yanaofungamana na mfumo wa kinyonyaji na kifedhuli uliokumbatiwa na tabaka la juu kumechangia umaskini kuendelea kukomaa. Haya yote ni kwa sababu ya watu wengi wa tabaka tawaliwa kutokujikomboa kifikra.

Kupitia data za utafiti wetu, tumebaini kuwa matatizo tuliyoabainisha awali yanaonekana kuwa sugu na endelevu kwani kila tamthilia teule imeendelea kuimba wimbo ule ule wa maisha magumu na duni ya kijamii miongoni mwa wananchi wa tabaka la chini. Kwa hiyo, waandishi hawa wanazidi kupaza sauti juu ya umuhimu wa kuwapo kwa ukombozi wa kweli wa kifikra kwa faida ya jamii nzima. Ili kwamba, kila mtu aweze kufurahia na kushiriki kikamilifu katika uzalishaji na utumiaji wa fursa na huduma bora na sahihi. Mambo haya yote yamewasilishwa

kiubunifu wala hakuna mkururo miongoni mwa waandishi wa tamthilia zote sita (6) teule. Mambo haya yote si ya uongo bali yapo hata katika ripoti za serikali, taasisi na mashirika mbalimbali yanayojishughulisha na maisha ya watu. Mfano wa ripoti hizo ni United Nations Economic Commission for Africa (2016), Economic and Social Research Foundation (2018) na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (2019).

### **Dhamira za Kiutamaduni**

Waandishi wa tamthilia zote sita (6) teule, wanaonekana kutambua na kujadili changamoto na sababu zinazoibuka kutokana na kuwapo kwa tamaduni kinzani miongoni mwa Watanzania. Waandishi wanaonesha kuwapo kwa mgongano baina ya utamaduni asili na utamaduni mpya unaotokana na athari ya ukoloni na ukoloni mamboleo miongoni mwa wazawa. Jambo hili linaonekana kushika mizizi kiasi cha kuathiri mifumo na maisha ya asili ya Mwafrika, hasa Mwafrika wa zama hizi. Wengi wa vijana wanaonekana kutokuwa sehemu ya kuenzi utamaduni wa asili yao. Badala yake, kumeibuka kasumba ya kuenzi mambo na vitu vya kigeni na kudharau vile vya asili ya Mwafrika.

Vijana wanaonekana kutokuwa na imani dhidi ya mapokeo na desturi za Kiafrika. Jambo hili linamaanisha hali ya kuwapo kwa mgongano mkubwa wa kitamaduni baina ya kizazi cha wazee – kizazi cha utamaduni mkongwe / asili ya Mwafrika na kizazi kipya – kizazi cha utamaduni wa kigeni. Hali hii inabainishwa kupitia mazungumzo kati ya Kitaru na Mfaume, kama yalivyojitokeza katika tamthilia ya *Mashetani*. Tunanukuu: -

KITARU: Eti unaamini kama wapo mashetani?

MFAUME: Unaniuliza mimi? Nyinyi wataalamu ndiyo mutwambie sisi.

KITARU: Siyo hivyo. Hujaelewa. ‘Na maana’, je wewe unaamini mashetani wapo?MFAUME: Mimi... Mimi ninaamini kama mashetani wapo. Juzi juzi hapa, dereva mmoja bwana, anatoka sehemu za huko Magomeni huko. Basi kafika pale karibu ya Jangwani. He! Mara peke yake bwana, kachepuka njia akenda kulilaza basi miguu juu chini. Kaulizwa. Kwani kasema nini? Kasema, ‘Shetani; kazi ya Shetani.’ Kaona njia mbili. Mchezo nini! Mashetani wapo. [...] Wapo sana lakini tumezibwa macho tu, hatuwaoni. (*Anaondoka.*) Wapo sana. Mimi ninaamini... (uk. 29)

**(Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Mashetani*, 1971)

Data tuliyoinkuu hasa kauli ya mwisho ya Mfaume kwa Kitaru inathibitisha ya kwamba, bado imani za asili zipo katika jamii ijapokuwa Kitaru haelekei kuikubali sana imani hii. Mfaume anasema, “Mimi ninaamini kama mashetani wapo. [...] Kasema, ‘Shetani; kazi ya Shetani.’ Kaona njia mbili. Mchezo nini! Mashetani wapo. [...] Wapo sana lakini tumezibwa macho tu, hatuwaoni. (*Anaondoka.*) Wapo sana. Mimi ninaamini...” Mfaume haamini katika uzembe wa dereva, ubovu wa chombo au, na barabara wala mwendo kasi. Badala yake anaamini katika nguvu za sihiri. Hii inathibitisha bado baadhi ya watu hawajakomboka kifikra. Mvutano wa namna hii ndio unaojitokeza hata kwa wazazi wa Kitaru na ushauri uliokuwa ukipenyezwa na majirani (rej. uk. 28 - 31).

Pia, mwandishi anaonesha kuwapo kwa utamaduni mbaya wa wenye nguvu kuwadhhibiti wale wanyonge kwa kila hali na mali (uk. 1 – 3). Aidha, utafiti umebaini kuwa mwandishi amegusia athari ya mtazamo wa baadhi ya watu kusoma au kujiendeleza kitaaluma kwa lengo la kujilimbikizia kipato na mali badala ya kufikiria kusoma kwa lengo la kuvuna maarifa, stadi na maono ya kumkomboa mtu wa tabaka la chini (uk. 16 – 17). Haya yote yameonesha changamoto ya mapambano kati ya utamaduni wa asili wa Mwafrika na utamaduni mpya – utamaduni wa kigeni – utamaduni wa kikoloni. Kwa mujibu wa Arowolo (2010), kwa nyakati za leo, utamaduni wa kigeni umeuzidi nguvu utamaduni wa asili ya Mwafrika. Na hali haionekani kuja kuwa kinyume chake. Kwa hiyo, utamaduni wa Mwafrika ni lazima upiganiwe ili usipotee kabisa.

Tatizo hili la mgongano wa tamaduni limejitokeza hata katika tamthilia ya *Kijiji Chetu*. Ndani ya tamthilia hii, kunabainika kuwapo kwa mvutano wa kifikra baina ya Mzee na Vijana. Mwandishi anaonesha jamii bado zinaamini katika nguvu za asili mfano uchawi na mashetani. Lakini utii wa vijana kwa wazee unaonekana kushuka sana kutokana na sumu waliyolishwa na baadhi ya watu wazima wanaowatumia vijana kwa maslahi yao wenyewe kupitia elimu isiyo na tija kwa matatizo na changamoto za jamii duni. Tunaliona hili kupitia data ifuatayo: -

**MZEE I:** ... Leo huu ujamaa tunaajaribu kuishi ni ujamaa wa aina mpya...

**MTU 2:** Kwani ujamaa wa zamani una tofauti gani na ujamaa huu wa sasa!

**MTU 3:** Wa kwao ulijaa uchawi... (uk. 16)

**MTU 3:** Riziki, maliza mkutano kabla mashetani hawajatuzengea...

**RIZIKI:** Nadhani saa zimepita na wengi wameanza kuchokachoka.... (uk. 21)

*Kama sehemu ya pili. Lakini wanaongezeka Mwenyekiti wa kijiji, makamu wake na viongozi wengine. Wanakijiji wengi sana wamekwishakaa na wanawangojea kufika. Wingu kubwa jeusi linapita na kwa muda kunakuwa na giza la kutisha. Watu wote wanatazama mbinguni kwa ukimya uliochanganyika na hofu. Halafu zogo linaanza tena.*

**SAUTI:** Shetani kapita. – Balaa hiyo, mkutano unaanza na vitisho vya mashetani. – Aaah! Ondokeni huko na imani zenu za mashetani! Kitu kidogo tu mashetani! (uk. 40)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Kijiji Chetu*, 1975)

Data tuliyoinukuu kutoka ukurasa wa 16, ukurasa wa 21, na ukurasa wa 40 zinaonesha kuwapo kwa baadhi ya watu katika jamii wanaoamini kuwapo kwa uchawi na mashetani. Mtazamo huu unaonekana kupingwa na wengine pale wanaposema, “Aaah! Ondokeni huko na imani zenu za mashetani! Kitu kidogo tu mashetani!” Kumbe basi, imani dhidi ya nguvu ya mapokeo ya miviga na visasili vya Kiafrika bado imo vichwani mwa watu ijapokuwa kuna tabaka la kizazi kipya linalojitenga na imani hizo. Jambo la pili tunaloliona hapa ni kitendo cha Mtu 2 kudakia hoja ya Mzee wakati Mzee husika ndiyo kwanza ameanza kuongea. Kisha Mtu 3 anadakia kwa kusema “Wa kwao ulijaa uchawi...”

Hali hii inaonesha namna vijana walivyokiuka utamaduni wa asili. Kwa mila za Kiafrika, kijana au mwanamke hawezi kuzungumza wakati Mzee anazungumza (Mbiti, 1969; Mirikau, 2011). Utamaduni huu wa vijana kutokuwasikiliza wala

kutokuwa tayari kuzitathmini kauli za wazee kumesababisha uhai wa kijiji cha ujamaa kupotea, kama ilivyooneshwa katika tamthilia hii. Matukio haya mawili yanathibitisha kuwapo kwa mivutano ya tamaduni mbili tofauti zinazoishi katika jamii moja iliyogawanyika.

Tatizo la utamaduni mpya unaowafanya vijana kutokutambua, kuheshimu wala kusikiliza ushauri wa wazee limejirudia pia katika tamthilia ya *Harakati za Ukombozi*. Vijana wameathiriwa na utamaduni wa kigeni uliowajengea falsafa ya kuamini kwamba mambo ya Kiafrika ni ya kishenzi na kamwe hayawezi kuwaletea maendeleo na ustawi endelevu. Ndiyo maana vijana hawa wanaonekana kuwasikiliza viongozi ambao ni mawakala wa utamaduni wa kikoloni wakiamini huko ndiko kuna suluhu ya matatizo yao. Mfano ufuatao unaosawiri mvutano baina ya Mzee (ukale) na Vijana (usasa). Data ifuatayo inalisawili suala hili. Tunanukuu: -

**MZEE:** Wananchi nipeni masikio.  
 Kizazi kipya kimeazimia kutenda  
 Wapeni uwanja!  
 Lakini mazingira kilichomo,  
 Chombo kipya ni yale yale.  
 Visiki bado havijang'olewa  
 na mnunuzi wa zana za kung'olea visiki ni yule yule.  
 Kizazi kipya chaelekezwa,  
 Katika mkondo ule ule.  
 Kizazi kipya chaimba,  
 Nyimbo zile zile.  
 Wapiga makofi wakiwa katika  
 hali ile ile.

**KIJANA 1:** Siafu! Mchwa! Nyuki! Meli!

Sisi si wana wa TANU tu  
wala si wana wa Afro – Shirazi tu,  
Sisi matokeo ya wazazi  
hao wawili...  
Tukilenga tumetungua  
Ndugu tupeni nafasi.

**MZEE:** Nafasi mnaweza pewa, lakini je mtaweza?

**KIJANA 2:** Kuweza tutaweza kwa vile tumeazimia.

**MZEE:** Hata sisi babu zenu tuliazimia lakini tukashindwa.

**KIJANA 3:** Mlishindwa kwa sababu mlikuwa na kasumba ya ukoloni.

**MZEE:** Je ninyi mmeshafuta hiyo kasumba?

**KIJANA 4:** Ndiyo tumeifutilia mbali, tumeitupilia mbali. Sasa tutaleta mapinduzi.

**MZEE:** Haya vijana ukumbi ni wenu, kazi kwenu, jaribuni!

**KIJANA 1:** Siyo tujaribu, bali tutaleta mapinduzi kwa kutekeleza kwa vitendo maazimio na maamuzi yote ya Chama. (uk. 23-24)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Harakati za Ukombozi*, 1982)

Data hii inaonesha hofu na tahadhari anayoitoa Mzee kwa vijana. Mzee anaonekana kutokuwa na imani na kile wanachokishadadia vijana. Pamoja na tahadhari anayoitoa Mzee, vijana wanaonekana kutokuwa tayari kumsikiliza. Wao wanaamini kuwa, kizazi cha Mzee kilishindwa “kwa sababu mlikuwa na kasumba ya ukoloni.”Jambo linaloonesha matokeo kutokuwa tofauti kati ya CCM na yale ya TANU na Azimio la Arusha. Kwa kuwa wasimamizi wakuu wengi wa chama kipya ndiyo haohao

walioanzisha na kuzika maazimio ya utu, haki, amani, usawa, umoja na ushirikiano miongoni mwa wanajamii, chini ya vikao na utendaji wa TANU. Haya hayakutokea kwa bahati mbaya. Yalikuwa ni sehemu ya mpango mkakati wa wageni kukita mizizi yao Afrika (Rodney, 1972). Wakoloni wamefanikiwa katika hili kwani leo hii, ukoloni mamboleo unazidi kuua utamaduni mkongwe wa Mwafrika na kuwafanya vijana kugeuka waigaji wa kila kinachozaliwa magharibi (Wollaeger, 2006).

Kwa upande wa tamthilia za awamu ya soko huria, tunabaini kuwapo kwa mwendelezo wa mvutano baina ya utamaduni mkongwe na utamaduni mpya. Katika tamthilia ya *Safari ya Chinga* tunaona kuwapo kwa mvutano baina ya ukale na usasa. Mivutano ya kitamaduni inayojitokeza katika tamthilia hii inahusu imani kuhusu watu kuugua (uk. 1 - 2). Pia, wanaume hasa wazee wanaopenda kuoza mabinti wa kileo na kujikuta wakiachwa halafu wanaishia kuamini katika ulozi (uk. 2 & 19). Utamaduni mwingine ni imani kuhusu mtoto kukalia mwichi (uk. 38 - 39) na utamaduni wa watoto hasa wa kiume kulea wazee wao (uk. 13). Vilevile, imani kuhusu maisha mazuri mijini (uk. 8 - 11 & 27 - 28 & 37), utamaduni wa vijana kutokuteteana katika jambo linalogusa maslahi yao na taifa (uk. 24, 46 & 51) na utamaduni wa kuoza watoto (uk. 20 & 40 - 42).

Suala la ndoa za utotoni ndilo linaonekana kuwa na mvutano mkali baina ya wanaukale (Che Mundu) na wanausasa (Bi Somoe na binti zake - Sijaona na Singilipo), tofauti na zama za asili ya Mwafrika kutamalaki. Mzee Che Mundu anaonekana kuutetea utamaduni wa kuoza watoto wa kike bila ridhaa yao ilhali Bi Somoe na binti zake wanampinga kwa nguvu zote. Hali hii isingewezekana wakati ambao utamaduni wa kigeni haukuwapo (Wakota, 2018). Lakini, hali iko hivi kwa



sababu ya athari ya mabadiliko ya kijamii yanayotokana na mwingiliano mkubwa wa watu. Hapa tunanukuu malumbano baina ya Che Mundu na Bi Somoe na binti zake, kuthibitisha hoja yetu kama ifuatavyo: -

**Singilipo:** Pengine mwaka huu kaka anaweza kuja.

**Che Mundu:** Ni vema aje kusoma barua zenu za posa.

**Sijaona:** Posa ya nani?

**Che Mundu:** Wewe na dada yako Singilipo.

**Singilipo:** (*Singilipo na Sijaona wanakaa chini*). Hapana baba. Mimi wala sitaki kuolewa sasa. Kwanza nna nchumba wangu.

**Sijaona:** Mi pia wala sitaki kuolewa. Nataka kwenda njini. Kaka akirudi tutaondoka wote.

**Bi. Somoe:** Hayo mambo ya watoto kuolewa mbona hata nami hujaniambia? Au ndo hivyo vikao vyenu vya kucheza bao vigengeni ndo vimezaa hayo?

**Che Mundu:** Haya ni masuala ya kiume. We utaambiwa wakati ukifika ili uwaandae wanao kwa harusi.

**Bi. Somoe:** Mume wangu hata ukifoka haisaidii. Ni vema tukae na watoto wetu tuwasikilize juu ya misimamo yao. Siku hizi wanawake hawategemei kuletewa kila kitu na waume zao kama zamani. Hata hiyo zamani si kwamba tulikuwa tunakaa bure. Tulilima, tulipanda, tulivuna na shughuli nyingine nyingi. Ntoto wa kike kama alivyo wa kiume, ana haki ya kutafuta nchumba ampendaye. Unaweza kunlazimisha ntoto kuolewa na akapata madhara makubwa.

**Che Mundu:** Sasa hao wanao wamesoma mpaka watafute wachumba wao wenyewe? Unafikiri na uzee ulionao,

hiyo elimu ya akina mama unayoipata itakusaidia nini?  
Wanawadanganya tu.

**Bi. Somoe:** Siku hizi maisha yamebadilika mume wangu. Sio kama wakati ulionioa mimi. Tulikuwa tunachukuliwa nzobenzobe kama gunia la korosho. Siku hizi vijana wengi wachumba wanatafuta wenyewe. Sio kutafutiwa kama zamani.

**Che Mundu:** (*Huku akichomachoma bakora yake chini ardhini*).  
Watoto wameshavunja ungo na wameshachezwa ngoma sasa wanasubiri nini? Si bora waolewe tu wasije kupata mimba bure? (*Anawaangalia akina Singilipo. Uruka anasogea karibu, anakaa chini*).  
Unafikiri hata huko njini mnakotaka kwenda ndo kuna waume? Safari zenu zitazaa mimba tu. Hapa kijijini mwaona jinsi wasichana wenzenu wanavyopata mimba na kutelekezwa. Nyinyi mmepata bahati nimewatafutia wachumba mwataka kuleta nchezo. Ni wale watoto wa nzee Tangusha na nzee Nchepange. Kila ntu hapa kijijini alikuwa anapigania wanawe waolewe na watoto wale. Ni watu ambao hawana shida hapa kijijini...  
Hata kama hawakukaa mi inanihusu nini? Mi sintakuwa nimeshakula mahari yangu. Mbona wanawake wengi tu wanaolewa na kuachika? Yaani tunakula kisamvu kila siku na uchumi tunao? (*Anaongeza sauti ya redio kidogo*). Ni afadhali nisikilize makelele ya redio kuliko kusikiliza makelele yako. Mwananke una gubu kama nini?! We mbona ulilazimishwa kuolewa na wazazi wako? Nilikuoa bado ndogo? (uk. 40-42)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Safari ya Chinga*, 2009)

Data tuliyoinkuu inatuonesha Che Mundu akitetea ukale ilhali Bi Somoe, Sijaona na Singilipo wanapingana na maamuzi ya mzee Che Mundu. Mzee Che Mundu anasimamia utamaduni wa mfumo dume lakini amejikuta kizazi anachokitaka kiishi kikale, hakiko tayari kutii ukale wake. Hali hii inatokana na athari za utamaduni wa kigeni mathalani utamaduni wa Kimagharibi kwa jamii ya Mwafrika. Utamaduni wa asili unaonekana bado unashikiliwa kwa kiasi na wazee lakini baadhi ya wanawake na vijana wengi wanataka mabadiliko. Mwandishi analithibitisha hili kupitia kinywa cha Bi Somoe anayesema, “Siku hizi maisha yamebadilika mume wangu. Sio kama wakati ulionioa mimi. Tulikuwa tunachukuliwa nzobenzobe kama gunia la korosho. Siku hizi vijana wengi wachumba wanatafuta wenyewe. Sio kutafutiwa kama zamani.” Hata hivyo, ukale bado unaonekana kuwatawala watu wazima ambalo wanatamani kuona mabadiliko ya kiutamaduni yakitokea katika jamii. Mathalani, pamoja na Bi Somoe kutetea binti zake wasiozwe bila ridhaa yao, bado anamsihi kijana wake wa kiume (Mata) asijethubutu kuo binti wa jamii nyingine wasiyoifahamu au kumfahamu binti husika kwa kina.

Mawazo na imani hii tunaipata kupitia kinywa cha Bi Somoe, anayesema: “Kumbuka mimi baba yako amenioa toka nna miaka kumi na tano. Mpaka leo bado tunaishi vizuri. Kwa sababu wazazi wetu walikuwa wanajuana. Usituletee nke hata kutwanga au kuchota maji hajui. Nke ambaye anaongea kizungu. Sisi hatujui kizungu. Hatutamwelewa.” Kauli ya Bi Somoe inapingwa pale pale na Mata kwa kusema “Si ndo atawafundisha kizungu?” Huku akiungwa mkono na dada zake ambao ni zao la utamaduni mpya, kama asemavyo Sijaona, “Nlete huyo huyo nzungu kaka tuongee ‘yes yes nzungu kala mafenesi” (uk. 14). Kinachojitokeza katika

mvutano huu ndiyo kile alichowahi kusema Hussein (1967/1973) ya kuwa, minyukano ya kizazi kipya na kile cha zamani haina budi kutatuliwa kwa hekima na busara. Kwa kuwa, kila kipindi cha maisha ya mwanadamu na maingiliano ya kitamaduni huwa na nguvu kubwa ya kusababisha uziwi na jeuri miongoni mwa vijana mbele ya wazee wao.

Mvutano kati ya kizazi kipya na kizazi cha zamani umebainika pia katika tamthilia ya *Changamoto*. Katika tamthilia hii, mwandishi anaonesha kiubunifu kuwapo kwa mivutano kati ya vijana wenye ulemavu wakisaidiwa wa watu wazima wachache kudai haki yao ya kuishi na kupata fursa ya kuheshimika na kuthaminiwa hata kama kimaumbile wana mapungufu (uk. 3 - 7). Pia, kupata nafasi ya kugombea na kupigiwa kura (uk. 5 - 6), kupata nafasi ya elimu (uk. 8 - 9) na kupata nafasi ya kuajiriwa (uk. 13 - 14). Vilevile, nafasi ya kulindwa (uk. 15 - 31) tofauti na mtazamo wa kale juu ya watu wenye ulemavu.

Utafiti umebaini, kabla ya ujio wa utamaduni wa kigeni, kiumbe yeyote yule – binadamu au mnyama, aliyegundulika kuwa na ulemavu, aliuliwa kwa imani kwamba ni nuksi katika jamii (Ngomoi, 1977; Hanson, 1997). Kwa hiyo, bila jamii kukomboka kifikra na kuachana na utamaduni wa kuwaangamiza viumbe vyenye kasoro, hakika jamii ya watu wenye ulemavu itaendelea kuumia. Katika tamthilia hii, mwandishi anaonekana kuwatambua baadhi ya watu wakiwa wamekomboka kifikra dhidi ya utamaduni kandamizi hasa kwa watu wenye ulemavu. Baadhi yao ni Malkia (japo anaonekana si mtendaji wa dhati katika kufikia mabadiliko ya kweli), Mwanamke dereva, Mpita njia, Godwin Laurent, Chuni, Afande 1, Hakimu na Wazee wa Baraza.

Hata hivyo, ukombozi huu wa kiutamaduni unakumbana na vikwazo kutoka kwa miundombinu isiyorafiki kwa watu wenye ulemavu na mapokeo ya kimtazamo na kiimani kutoka kwa jamii kubwa ya wanajamii. Mathalani Madereva katika barabara kuu, watendaji wa hospitali, Katibu Muhtasi, Mtendaji wa kata, Mkuu wa Shule, Mganga, Abuu, Kimweri, Rajab, Masumbuko na hadhira. Kundi hili linaonekana kupambana na wanamabadiliko kutokana na kasumba iliyojengeka vichwani mwao juu ya watu wenye ulemavu kuwa ni balaa na masikini wa kutupwa – ombaomba. Tena wanaonekana kuwa watu wasumbufu wasiokuwa na haki ya kupata fursa ya kugombea uongozi, kuishi, kuajiriwa, kujiendeleza kielimu, kumiliki mapato wala mali yoyote. Ndiyo maana katika mapambano ya kuupindua utamaduni huu, sehemu kubwa ya wanajamii ilionekana kutokushiriki kuwatetea watu wenye ulemavu. Mfano mmojawapo wa ubaguzi kutokana na mapokeo ya kiutamaduni ni data ifuatayo: -

- Peti:** Mwongo huyu! Tena tummwagie petrol kabisa, tumwue!
- Godwin:** Hapana! Sheria itamhukumu akikutwa na hatia. Sio vizuri kulipiza kisasi – tunaamini mahakimu wetu huko mahakamani wanahukumu kwa haki!
- Rajabu:** *(Akimsihi Godwin)* Niache tafadhali nitakupa kitu kidogo!
- Godwin:** Maisha yangu hadi leo hii sijawahi kuhongwa kitu chochote. Huwezi kunishawishi. Twende! *(Akimburuta Rajab na kuiacha baiskeli yake pale pale)*. Twende mbele ya sheria. Lazima unyanyaswaji na uonevu dhidi ya watu wenye ulemavu ukomeshwe.

**Rajabu:** (*Akimwamrisha*) Niachie mzee! Nasema niachieee!  
 (*Rajabu anafurukuta kujitoa mikononi mwa Godwin na anampiga teke la tumboni. Godwin anagugumia kwa maumivu na anaanguka chini. Rajabu anakimbia kuelekea walikokaa hadhira. Wakati huo huo Kimweri anapurukushana na Chaazye na anajitoa mikononi mwake na anakimbia. Walemavu waliokuwapo jukwaani wanapiga kelele za kuomba msaada. Wanasikika wakisema: **KAMATA! KAMATA! KAMATA!** Lakini hakuna mtu anayejitokeza kumkamata mhalifu yeyote anayekimbia. Pazia linafungwa*). (uk. 27 – 28)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Changamoto*, 2010)

Data hii inathibitisha ya kwamba bado wapo wanajamii wengi wanaoishi kwa kasumba na mtazamo hasi dhidi ya watu wenye ulemavu. Kitendo cha Godwin na Peti kupambana na Rajabu bila mafanikio huku jamii kubwa ikibaki kuwa watazamaji kinathibitisha changamoto iliyopo miongoni mwa jamii zetu katika kumkomboa mnyonge mlemavu kutoka katika makucha ya utamaduni mkongwe. Haya tunayaona kupitia mwandishi anaposema, “*Rajabu anafurukuta kujitoa mikononi mwa Godwin na anampiga teke la tumboni. Godwin anagugumia kwa maumivu na anaanguka chini. Rajabu anakimbia kuelekea walikokaa hadhira. Wakati huo huo Kimweri anapurukushana na Chaazye na anajitoa mikononi mwake na anakimbia. Walemavu waliokuwapo jukwaani wanapiga kelele za kuomba msaada. Wanasikika wakisema: **KAMATA! KAMATA! KAMATA!** Lakini hakuna mtu anayejitokeza kumkamata mhalifu yeyote anayekimbia.*” Kumbe basi, hapa napo pana mvutano baina ya ukale na usasa katika kuleta mabadiliko na maendeleo ya kweli na endelevu kwa ustawi wa jamii nzima bila ubaguzi wala matabaka.

Nayo tamthilia ya *Nje – Ndani* haikubaki nyuma katika kulisawiri suala la changamoto zinazotokana na migongano ya kitamaduni baina ya tabaka moja na jingine ndani ya jamii ileile. Waandishi wa tamthilia hii wanaonekana kuonesha namna utamaduni wa kigeni ulivyofanikiwa kukita mizizi hata kuwaathiri wasomi na viongozi kiasi cha kujikuta wakiusaliti Uafrika wao. Mjadala huu unaonekana kupewa msukumo mkubwa kupitia sehemu ya mazungumzo baina ya Akili na Moyo kama yanavyojidhihirisha katika nukuu ifuatayo: -

**Akili:** [*Sura imesawajika kwa hasira*]. Mimi nimechoka maigizo haya, ninaona kama hayana maana yoyote na yanamidhalilisha. Nimezoea kusema ung'eng'e lakini hapana. Ukitaka tufanye maigizo kwa Kimombo.

**Moyo:** Siwezi kuwa mtumwa katika ardhi yangu huru, shida ya kujiumauma ya nini? Kimombo kina maana gani ikiwa bado tuna shombo? Ninajua tunakipenda na ni muhimu lakini sifikiri kuwa ni busara kutusemea au kutuwakilisha. Ni bora tutamatishe maigizo haya kama sharti lako ndilo hilo. [...] Umekuja huku kwetu bado unanichagulia namna ya kusema? Ebo! [...]. (uk. 24)

**Njozi:** Utashii Utashiii. Albino wamefanya nini? Bado ni mkosi kwenye familia na hutupwa wakizaliwa?

**Utashi-Nafsi:** Huokotwa.

**Njozi:** Ndo vizuri, naam naaam.

**Utashi-Nafsi:** Mama huporwa akiwa naye, hukabwa, au huibwa, hukatwakatwa, hupasuliwa, huuawa, iiii jamani Afrikaaaaaa!... Afrika ulinzi, usalama, uhuru, unyama, ubaki, ujamaa potelea mbaliii. (uk. 58 & 60)

**Akili:** Unajua utamaduni ni jambo changamani sana.

**Moyo:** Mimi sioni hivyo.

**Akili:** Huwezi kuona kwa macho jambo hili. Hivi unajua kule kibali wamenyimwa kabisa. Na wale kule wakipita wala hawabaguliwi kihiiyo eti wana kibali tangu enzi za kale. (uk. 67)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Nje - Ndani*, 2016)

Kupitia nukuu hii tunabaini kuwapo kwa tamaduni mbili zinazoishi na kutenda kazi katikati ya jamii moja ya Mwafrika. Utamaduni mmoja ni wa kigeni na mwingine ni wa Kiafrika. Katika hiyo, waandishi wanaonesha mabaya yaliyomo katika utamaduni wa kigeni na mabaya ya utamaduni wa Kiafrika. Huku ndiko kumaanisha ya kwamba, kila utamaduni una mabaya na mazuri yake. Lakini, utamaduni wa kigeni umetugeza mazuzu kwa kuacha kila jema linalopatikana katika utamaduni wa Mwafrika. Ndiyo maana Akili na Moyo wanapigania umuhimu wa mtu kujitambua kwa kuamua kujitenga na maigizo ya maisha yaliyojaa unafiki. Akili na Moyo hawako tayari kuendelea kuwa watumwa wa utamaduni mbaya wa Mwafrika lakini zaidi sana, utamaduni mbaya wa kigeni.

Kwa jumla, tamthilia zote sita (6) teule tulizojadili zinathibitisha bado pana changamoto nyingi zinazotokana na mifumo ya maisha inayohusiana na utamaduni wa asili ya Mwafrika na ule wa kigeni. Kila mwandishi ameonesha kuwapo kwa mazuri na mabaya katika kila mfumo wa utamaduni – mkongwe na mpya unaotawala maisha ya kila siku ya watu. Hivyo, kuna umuhimu mkubwa wa kuisaidia jamii kujikomboa kiutamaduni kwa kuunda mfumo rafiki utakaokuwa na mazuri pekee kutoka katika kila utamaduni, kwa faida ya kizazi cha jana, leo na vijavyo. Thuraniira (2017) analitaja tatizo la migongano ya kitamaduni kama jambo mojawapo katika mambo yanayojitokeza katika kazi bunilizi nyingi za Kiswahili. Hivyo hili siyo



tatizo dogo bali ni tatizo kubwa linaloathiri utangamano na ustawi wa jamii katika kila uga wa maisha.

### **Dhamira za Kisiasa**

Utafiti huu umebaini kuwa katika tamthilia zote sita (6) teule kuna masuala yanayohusu siasa. Masuala hayo ni yale yanayohusu utashi, uandaaji, utekelezaji, usimamizi na tathmini ya matamko, sera, na sheria zinazozalishwa na watendaji wanaotokana na siasa. Katika tamthilia zote sita (6) teule, kumbainika kuwapo kwa viongozi wengi wasiokuwa waaminifu na hawaishi katika matamko, sera na sheria wanazozianzisha wao wenyewe (kwa namna moja au nyingine). Badala yake wamekuwa wakitazama manufaa yao wenyewe. Na pale panapotokea kiongozi mwenye dhamira ya dhati ya kusimamia na kutekeleza makubaliano, kiongozi wa namna hii huishia kutupwa nje ya mfumo na huonekana ni msaliti tena mtu hatari kwa taifa na jamii.

Kinyume chake, viongozi wengi wanaonekana kusimamia na kutekeleza matamko, sera na sheria hufanya kinafiki kwa manufaa yao na kundi la wachache wenye malengo na maslahi sawa na viongozi husika. Huku ndiko kusema ya kuwa, sehemu kubwa ya wanasiasa na aina ya siasa inayotekelezwa katika taifa imezalisha na kujaza viongozi wachafu na maharamia wanaosimamia na kutekeleza siasa chafu iliyoundiwa sera chafu. Kisha ikahuishwa katika sheria chafu yenye kunadiwa kupitia matamko machafu yanayobebwa katika mfumo mchafu na kuwasilishwa kwa umma kwa njia chafu kwa maslahi ya wachache.

Hii ina maana ya kwamba, viongozi wengi siyo wazalendo kwa taifa na jamii yao. Hivyo, taifa haliwezi kupiga hatua chanya kwa ustawi na maendeleo endelevu kwa

kutegemea aina hii ya viongozi na siasa. Kwani wengi wanaishi kinyume na matamko, sera na sheria zinazolenga kulikomboa taifa katika nyanja zote za maisha ya mwanadamu. Badala yake, wamejaa na kunuka tamaa, ubinafsi, rushwa, wizi, ufiti, usaliti, dhuluma, chuki, visasi na usambaratishaji wa umoja na mshikamano wa kweli katika jamii. Mengine ni unyonyaji, uporaji wa raslimali, ukibaraka kwa mabepari, unafiki, uonevu, ujuaji, ukiukaji wa haki na sheria, majivuno. Haya yote yanathibitishwa ndani ya tamthilia zote sita (6) teule. Katika tamthilia ya *Mashetani* kwa kuanzia kama ushahidi, tunakutana na nukuu ya data ifuatayo: -

BABA KITARU: Shhh.... Njoo, njoo nikuonesheni kitu.

MAMA KITARU: Nini?

BABA KITARU: Ndege wangu.

JUMA NA KITARU: Ndege!

BABA KITARU: Njoni hapa dirishani. Unaiona nini?

MAMA KITARU: Gari mpya! Benzi!

BABA KITARU: Yangu! Naam! Mali yangu, jasho langu. Kitaru, njoo uitazame. Juma, njoo. Mnaiona? Tazama ilivyotulia. Basi pale itoneshe tu – waaaah, linaruka kama ndege. Twende tukatembee, mnasemaje? Twendeni. Twendeni, twende. (uk. 22)

MTU 1: [...] (*Mlio wa gari inapita.*) Doo doo! Salaale! Umeona mdudu ule?

MTU 2: Nini? Ile gari? Nimeiona. Aah, ataiuza kesho ile. We ngoja tu.

MTU 1: Kwani we unamjua yule?

MTU 2: Kwani we humjui?

MTU 1: Hata.

- MTU 2: Jana hatukuwa wote pamoja, alipokuwa akitusimulia Bwana Mathew juu ya kufungwa kwa ile kampuni.
- MTU 1: Aah! Aah! Ndiyo, ndiyo, ndiyo. Aha! Kwani ndiye huyu bwana wenyewe?
- MTU 2: Eh. Pesa chungu nzima bwana zimepotea. Lakini ndiyo haijulikani kuwa zimeibiwa au zimepotea katika mahisabu.
- MTU 1: Alaa. Kumbe ndiye huyu? Shetani kweli kweli... (uk. 42 – 43)

(**Chanzo:** Data za Utafiti tamthilia ya *Mashetani*, 1971)

Kupitia data tuliyo inukuu tunagundua kuwapo kwa tatizo kubwa katika uaminifu miongoni mwa watendaji wa umma ambao ni zao la siasa chafu. Baba Kitaru ni mmoja wa viongozi wazawa na “wazalendo” walioaminiwa na chama na serikali kisha kupewa jukumu la kusimamia kampuni ya umma kwa faida ya taifa zima. Badala yake akafuja mali za kampuni hadi taasisi husika ikafilisika. Mwandishi analithibitisha kwa kusema “Jana hatukuwa wote pamoja, alipokuwa akitusimulia Bwana Mathew juu ya kufungwa kwa ile kampuni. [...] Pesa chungu nzima bwana zimepotea. Lakini ndiyo haijulikani kuwa zimeibiwa au zimepotea katika mahisabu.” Kufungwa kwa kampuni hii kunamaanisha kupotea kwa ajira za moja kwa moja na zile zisizo za moja kwa moja, kushuka kwa pato la taifa kupitia kodi katika bidhaa, marupurupu na mishahara ya waajiriwa. Pia, kuongezeka kwa wananchi tegemezi kiuchumi na kijamii.

Changamoto nyingine ni kwa serikali na wananchi mmoja mmoja kushindwa kutoa na kusimamia huduma bora na sahihi za kiuchumi na kijamii, kutaja kwa uchache. Ripoti za Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia masuala ya ajira na kazi,

linatujaza kwamba, watu wengi walio katika utumishi wa ajira hawapati haki na maslahi bora kama wanavyotumikishwa na waajiri. Waajiri wengi wamekuwa wanyonyaji na wadhulumati kwa wafanyakazi wao (International Labour Organisation, 2016). Taarifa hii inamaanisha kuwa, nchi haiwezi kufanikiwa kutekeleza matamko, sera na sheria ilizojiwekea kama sehemu ya dira na maono ya kujenga taifa bora lenye kutoa haki, usawa na utu stahiki kwa kila mwananchi. Usaliti, ufiadini na ubinafsi wa viongozi wengi waliorithi kijiti kutoka kwa wakoloni umefanyika jipu lililogeuka kansa katika taifa mpaka leo hii. Ndiyo maana, Sitta (2013) anasisitiza kwamba, mwanasiasa mwadilifu hawezi kuwa tajiri katika nchi maskini yenye kufuata mfumo wa siasa ya ujamaa na kujitegemea. Kumkuta mwanasiasa tajiri katika nchi ya namna hii ni dhahiri kuwa, utajiri huo una makandokando nyuma yake.

Jambo hili linaonekana pia katika tamthilia ya *Kijiji Chetu*. Mwandishi anaonesha namna uongozi wa kijiji ulivyokuwa ukikiuka maazimio ya kijiji, sera na sheria zilizotungwa kwa lengo la kuongoza kijiji cha ujamaa kwa faida ya wananchi wa kijiji husika na taifa zima. Tunalithibitisha hili kwa kurejelea malumabano katika kikao cha kijiji husika. Data ifuatayo inaathibitisha ukweli wa hiki tukisemacho: -

**MTU I:** Ndugu Mwenyekiti, ndugu wanakijiji. Tatizo letu hapa ni mfarakano wetu wenyewe. Maazimio tunayopitisha kwa pamoja mara nyingi yameishia midomoni na kusahauliwa mara baada ya kutoka mikutanoni. Mara ngapi tumesema wasioishi kijijini siyo wanakijiji? Lakini badala yake viongozi wetu wanakubali hongo na kuwapokea watu hao kama wanakijiji kwa fedha.

**MAKAMU:** Fedha ndugu zinahitajika sana. Hatuwezi kufanya lolote bila fedha....

**MTU I:** Soma kifungu katika Azimio “Tusitegemee fedha kuleta Maendeleo”. Unapinga serikali wewe?

**MAKAMU:** Sipingi serikali. Wakati serikali inasema hivyo inataka sisi wananchi tusitegemee sana fedha kwa kuleta maendeleo.

**SAUTI:** Ala! Mwone anataka nini na anasema nini! (uk. 45)

**PINDUO:** Watu husema unapochokozwa usikae kimya kwani ukifanya hivyo itachukuliwa kuwa woga au kudhibitisha ukweli wa maneno yanayosemwa. Nami siwezi kuwa kisingizio cha vyeo. Kwa nini nilijiuzulu kutoka Kamati Kuu! Kwa nini niliamua kuacha vyeo vyote mlivyonipa! Mwenyekiti ananiita mwongo. Kama kusema kuwa Bwana Mwenyekiti amefuga kuku wengi kinyume cha maazimio ya kijiji ni uwongo basi ndugu wanakijiji mnaweza kuniadhibu. Ndugu wanakijiji inasemekana kuwa mmeamua kunifukuza kwa kuwa mvivu. Nami nakubali. Lakini heri ya uvivu wangu kuliko miiko inayofanywa na Mwenyekiti. Sasa hivi ndugu Kizito ametaja mbinu anazozitumia Mwenyekiti kutunyonya. Duka lake linauzwa na mke wake hupata vitu kutoka wapi? Kwa nini alisimamisha uchunguzi wa vitu vilivyopotea mwaka jana. (uk. 49)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Kijiji Chetu*, 1975)

Kupitia nukuu hii, tunabaini namna uongozi wa kijiji ulivyohujumu maazimio, sera na sheria za ukuzaji wa vijiji vya ujamaa. Kumbe basi, ujinga wa wananchi wengi, imani kubwa kwa viongozi, ukasuku, ufisadi, hujuma, ubinafsi wa viongozi na wananchi wengi umesababisha kufa kwa vijiji vya ujamaa. Halafu kukazidisha

kukua kwa ubaguzi, matabaka, ugumu wa maisha miongoni mwa wananchi wengi kwani wananchi wengi walikuwa makasuku wa matamko ya viongozi. Matamko, sera na sheria nyingi zinaonekana kutungwa pasipo kusawiri aina ya jamii itakayopaswa kuziishi kama anavyobainisha mwandishi, “Tatizo letu hapa ni mfarakano wetu wenyewe. Maazimio tunayopitisha kwa pamoja mara nyingi yameishia midomoni na kusahuliwa mara baada ya kutoka mikutanoni. Mara ngapi tumesema wasioishi kijijini siyo wanakijiji? Lakini badala yake viongozi wetu wanakubali hongo na kuwapokea watu hao kama wanakijiji kwa fedha.” Inavyoonekana matamko, sera na sheria nyingi siyorafiki kwa mazingira ya jamii za asili ya Mwafrika. Bali zimenakiliwa kutoka mataifa ya kibepari na kuletwa kutekelezwa bila kufanya tathmini ili ikiwezekana zifanyiwe marekebisho yenye tija kwa mazingira, watu na asili ya jamii inayokwenda kupelekewa mambo ya kutekeleza. Vilevile maandalizi na utoaji wa elimu ya uraia kwa kila mwananchi ili kutambua, kuchuja na kushiriki kutunga, kusimamia na kuziishi sera na sheria husika huwa haupo. Matokeo yake wadhaliwa hutumia fursa hii kulisambaratisha taifa na jamii, kama asemavyo mzee: -

**MZEE I:** [...] Leo huu ujamaa tunaajaribu kuishi ni ujamaa wa aina mpya... Ujamaa mpya mwingi ni wa kwenye kitabu. Na hatari yake ni kama hii. (*Akionyesha mdomo*). Maneno mengi na mikutano kila siku bila vitendo. Kufika hapa na kujirundika pamoja twadhani tunaishi kijamaa. Ingawa babu zetu hawakujirundika kama sisi walikuwa wakiishi kijamaa kuliko sisi. Ujamaa ulikuwa ni maisha yao. Kulikuwa hakuna shamba la ushirika kama yetu hapa. Kila mtu alikuwa na lake lakini lilikuwa likilimwa na kijiji, siyo mtu mmoja. Ushirikiano uliendelea mpaka kwenye ulinzi.

Mtu mmoja akipiga mbinja ya kutaka msaada wote hutoka kusaidia. [...] Usinielewe vibaya mwanangu. Usirukie kitu kabla hujasikia mwisho wake. Ndiyo maana nawaambieni mna kitabu tu mbele yenu, lakini mawazo yenu si ya kijamaa. Watu wote siyo sawa ingawa binadamu wote ni sawa. (uk. 16 – 18)

[...] Viongozi wetu wanatufanya tuishi maisha ya kijamaa na wanaona upande mmoja zaidi nao ni wa siasa [...]. (uk. 46)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Kijiji Chetu*, 1975)

Katika data hii tunabaini kuwapo kwa ufafanuzi muhimu kutoka kwa Mzee. Ufafanuzi huu unaashiria kuwapo kwa ukurupukaji mkubwa wa viongozi katika kutunga na kutangaza matamko, sera na sheria zao. Mwandishi anasema kupitia Mzee “Usinielewe vibaya mwanangu. Usirukie kitu kabla hujasikia mwisho wake. Ndiyo maana nawaambieni mna kitabu tu mbele yenu, lakini mawazo yenu si ya kijamaa. Watu wote siyo sawa ingawa binadamu wote ni sawa. [...] Viongozi wetu wanatufanya tuishi maisha ya kijamaa na wanaona upande mmoja zaidi nao ni wa siasa [...]” Kauli hii inamaanisha kuwa, wakati wananchi maamuma wakishangilia na kulibeba tamko kama dodoki lililomwagiwa maji, viongozi wachache wasiokuwa na dhamira njema hugeuka na kulitumia pengo la uelewa na utambuzi wa mambo unaowakabili wananchi wengi, hasa vijana, kujinufaisha na kuhujumu sera au sheria husika. Matendo ya namna hii ya wananchi maamuma kutumika kama madodoki kufyonza maji kwa manufaa ya anayelitumia dodoki hilo yamejitokeza hata katika tamthilia ya *Harakati za Ukombozi*.

Katika tamthilia ya *Harakati za Ukombozi* kunaoneshwa namna wanasiasa wengi na aina ya siasa inayotawala katika taifa isivyokuwa shirikishi, isivyokuwa rafiki, isivyokuwa wezeshi, wala isivyotekelezeka. Matamko, sera na sheria zinazotungwa zinaonekana kutungwa kwa lengo la kuleta upofu kwa wananchi wanaoamini katika akili, uwezo na utashi wa viongozi waliowakabidhi mamlaka na madaraka. Matokeo yake, utekelezwaji wake hauleti afya kwa ustawi na maendeleo endelevu, bora na sahihi kwa faida ya taifa na mtu mmoja mmoja katika taifa. Kwani mfumo wa siasa na maamuzi yatokanayo na siasa na wanasiasa unaonekana kujaa ubaguzi, usaliti, unafiki, rushwa, ufedhuli, udhulumati, chuki, unyonyaji, ulanguzi na mazingaombwe ya kila namna. Haya yanathibitishwa kupitia tukio lifuatalo: -

**KIONGOZI 2:** Hivi Bwana Meneja, kwenye kiwanda chako bado mnasafirisha vitu nje?

**MENEJA:** Siyo kiwanda changu, chetu.

**KIONGOZI 2:** Ee ndiyo! Chetu.

**MENEJA:** Ndiyo, bado tunapeleka bidhaa Marekani, Uchina, Ujerumani na pia Uingereza. Vipi?

**KIONGOZI 2:** Nilitaka unisafirishie mzigo wangu kwenda Marekani. Je, si inawezekana?

**MENEJA:** Tunaweza, lakini juzi tu serikali ilimleta kijana mmoja kufagiafagia pale ofisini kwangu. Bali ninavyomwona kijana huyo, sidhani kama mfagiaji.

**KIONGOZI 2:** Wewe unafikiri ni nani.

**MENEJA:** Mimi naona ni kati ya wale... (*Anapiga mkono mkono kama vile anaua mbu anayemuuma*).

**KIONGOZI 2:** Aa! Usiwajali hao, wote wako chini ya Chama wale.



**MENEJA:** Kama ni hivyo, basi hamna taabu, maana yake nyie ndio viongozi wa Chama na serikali, mtume mtoto kesho aje achukue fomu za kujaza.

**KIONGOZI 2:** Tena umenikumbusha wakati bado Mkurugenzi wa Wizara tunaye hapa. Bwana Mkurugenzi, mtoto wangu, yule kijana wako amefeli tena mtihani, fanya fanya basi.

**MKURUGENZI:** Yupi, yule kijana aliyekuwa darasa la saba?

**KIONGOZI 2:** Eee, huyo huyo.

**MKURUGENZI:** Hamna shida. Wewe unataka nimpeleke wapi, Sekondari? Au nimpeleke ng'ambo kabisa.

**KIONGOZI 2:** Eheh! Mpeleke ng'ambo bwana. Hii elimu yetu hapa imeshuka sana.

**MKURUGENZI:** Basi nitampeleka ng'ambo. (uk. 20 – 21)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Harakati za Ukombozi*, 1982)

Kupitia majadiliano haya, tunabaini kuwapo kwa matumizi mabaya ya madaraka ili kupindisha sheria na taratibu kwa maslahi binafsi kama asemavyo “Aa! Usiwajali hao, wote wako chini ya Chama wale.” Pia, tunaona kuwapo kwa udanganyifu na ukwepaji wa uwazi wa kodi unaofanywa na viongozi wa umma. Badala ya kulinda na kutetea kwa dhati raslimali za taifa kwa faida ya vizazi vya sasa na vijavyo. Viongozi hawa ni zao la siasa na wayatendayo hapa ni kinyume na yale wanayoyanadi majukwaani. Tunayaona yote hayo katika nukuu ifuatayo: -

**KIONGOZI 2:** (*anahutubia mkutano wa hadhara*) Azimio la Arusha Oyee!

**WANANCHI:** Oyee!

**KIONGOZI 2:** Wanyonyaji wote

**WANANCHI:** Ziii!

**KIONGOZI 2:** Mabepari wote

**WANANCHI:** Ziii!

**KIONGOZI 2:** Wapinga Azimio

**WANANCHI:** Ziii!

**KIONGOZI 2:** [...]. Ndugu wananchi, Azimio letu haliishii katika matamko, linaendelea siku hadi siku kutekelezwa kwa matendo. Kazi bado tunayo kubwa, magugu bado yapo. Tena yapo mengi sana. Hata hapa nayaona. Hivyo bado tuna kazi kubwa. (*Anamuonyesha mwananchi mmoja kati ya wanaomsikiliza ambaye ni mnene.*) Hebu wewe hapo simama. Wewe hapo. (*Mwananchi anasimama*) Njoo hapa. (*Mwananchi anakuja mpaka alipo kiongozi. Kiongozi anamtazama tangu juu hadi chini*). Hivi wewe unakula nini? Unazo nyumba ngapi? Magari? Unayo mashamba mangapi? Hii suti inakupendeza, umeitoa wapi? Unazo ngapi? (*Mwananchi ameshangaa tu, hajibu*). Wananchi hebu mtazameni mtu huyu mtazameni!

Huyu mtu ni mmoja wa mifano mizuri ya wale wanaotunyonya. Angalieni wanavyofutuka na kumea vinundu. Hii yote kwa sababu ya kutunyonya sisi. Ndugu wananchi, tutanyonywa namna hii kwa muda gani? Hawa ndiyo wanatunyonya! Haya ndiyo makupe! Ndiyo mabomba hasa! Haya rudi...

(*Kiongozi 2 anaondoka huku akiwapungia wananchi. Kiongozi 2 anafika kwenye bar.*)

*Anawakuta Mkurugenzi na Meneja wanakunywa pombe).* (uk. 17)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Harakati za Ukombozi*, 1982)

Data hii imebeba hotuba ya Kiongozi 2 anayeonekana kuwa mwimba ujamaa. Wakati huo huo anaonekana kupingana na ujamaa kwa kutokujali utu wa mtu, tofauti za kimaumbile na hali za watu katika jamii. Kiongozi 2 anajaribu kuwaaminisha wananchi kwamba adui wa ujamaa anaweza kuonekana kwa umbile la mwili wake. Hapa ni dhahiri kwamba kiongozi huyu anatumia udhaifu wa ujuzi, utambuzi na maumbile ya wananchi walio wengi kuwabagua na kuwachonganisha wananchi ili wafarakane na kushindwa kuwa wamoja katika kujenga ujamaa na taifa. Mwandishi anasema, “Hivyo bado tuna kazi kubwa. (*Anamuonyesha mwananchi mmoja kati ya wanaomsikiliza ambaye ni mnene.*) Hebu wewe hapo simama. Wewe hapo. (*Mwananchi anasimama*) Njoo hapa. (*Mwananchi anakuja mpaka alipo kiongozi. Kiongozi anamtazama tangu juu hadi chini.*)” Mwandishi haishii hapo, anaendelea kumjenga mhusika wake kwa maneno ya dharau na udhalilishaji. Mwandishi anasema, “Hivi wewe unakula nini? Unazo nyumba ngapi? Magari? Unayo mashamba mangapi? Hii suti inakupendeza, umeitoa wapi? Unazo ngapi? (*Mwananchi ameshangaa tu, hajibu.*)”

Mwandishi anaongeza kusema, “Wananchi hebu mtazameni mtu huyu mtazameni! Huyu mtu ni mmoja wa mifano mizuri ya wale wanaotunyonya. Angalieni wanavyofutuka na kumea vinundu. Hii yote kwa sababu ya kutunyonya sisi. Ndugu wananchi, tutanyonywa namna hii kwa muda gani? Hawa ndiyo wanatunyonya! Haya ndiyo makupe! Ndiyo mabomba hasa! Haya rudi...” Nukuu hii inathibitisha

kuwa, Kiongozi 2 ni mfano wa viongozi wanafiki, wachonganishi, waliojaa ghiribu, fitina, uzushi, na dharau kwa wananchi wanaowaongoza ilhali viongozi hao wakijinufaisha na kujilimbikizia mali. Mfano mzuri wa ghiribu za kiongozi huyu zinajionesha kupitia matendo na kauli zifuatazo: -

**KIONGOZI 2:** (*Anakaa*). Ah! Nilikuwa kwenye shughuli za Chama, halafu nikapitia kwenye miradi yangu kuangalia isianguke. (*Wote wanacheka*).

**MENEJA:** Unajua bwana kiwanda changu kimechukuliwa?

**MKURUGENZI:** Ala! Tayari?

**MENEJA:** Hasa. Lakini mwenzenu Azimio hili linaniumiza kichwa. (*Wanacheka*).

**KIONGOZI 2:** .... Kwani Bwana Meneja una nyumba ngapi?

**MENEJA:** Nina nyumba nne.

**KIONGOZI 1:** Nne tu?

**MENEJA:** Nne.

**KIONGOZI 2:** Aa! Mimi nilidhani una nyumba nyingi sana kumbe nne tu. Mbona mimi ninazo kumi (*anacheka*) na sina tatizo.

**MKURUGENZI:** Kwani ndugu Meneja huna watoto wowote?

**MENEJA:** Nina watoto wanne. Huyu wa nne kazaliwa juzi tu, hata siku kumi hajafikisha.

**MKURUGENZI:** Sasa kumbe una shida gani. Wagawie hao watoto hizo nyumba.

**KIONGOZI 1:** Eee! Kila mtoto mpe nyumba moja.

**MENEJA:** Eti kweli. Kwa nini sikufikiria jambo hili. (uk. 18 – 19)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Harakati za Ukombozi*, 1982)

Katika nukuu hii tunaona mazungumzo ya viongozi ambayo yanaonesha nguvu ya madaraka na mamlaka waliyopewa kiasi cha kudiriki hata kupindisha taratibu na sheria kwa makusudi kwa maslahi yao binafsi. Kwa mfano kauli ya Mkurugenzi isemayo “Sasa kumbe una shida gani. Wagawie hao watoto hizo nyumba” na ile ya Kiongozi 1 isemayo, “Eee! Kila mtoto mpe nyumba moja” ni ushahidi tosha juu ya mienendo isiyofaa kwa taifa na jamii. Hii inaonesha hata mfumo wa ujasusi katika taifa hauna nguvu mbele ya aina na mfumo wa kisiasa na wanasiasa waliokabidhiwa dhamana ya kuamua hatima ya maisha ya wananchi wenzao. Huku kunaonesha ya kwamba, wananchi wengi wameweka rehani dhamana ya maisha yao ili ibebwe na kustawishwa kupitia mikono ya viongozi wachafu wanaosimamia na kutekeleza siasa chafu, sera chafu, sheria chafu, matamko machafu, mfumo mchafu, na njia chafu. Kwa maneno mengine, sheria, matamko na sera zinatungwa na kutekelezwa kibaguzi huku viongozi husika wakipaa na kuketi juu ya sheria, matamko na sera zinazoshushwa chini kuwadhibiti wanyonge ili wazidi kuwa duni zaidi na zaidi.

Aina hii ya siasa na wanasiasa wabaradhuli, wabinafsi, wasaliti, wenye kujilimbikizia na kufuja raslimali za taifa kwa maslahi ya kundi dogo, inaonekana pia katika tamthilia ya *Safari ya Chinga*. Katika tamthilia hii, mwandishi anaonesha namna matamko, sera na sheria zinazotungwa katika taifa zinavyosababisha ufukara na utegemezi endelevu miongoni mwa wananchi wengi. Huku waliozitunga wakiendelea kuamini kwamba hayo ndiyo maendeleo. Uthibitisho wa jambo hili unapatikana katika nukuu ifuatayo: -

**Mata:** (*Kwa haraka*). Mweshimiwa hakimu, mi nimekamatwa kibandani kwangu nikifanya biashara.

**Hakimu:** Kumbe kosa unalijua halafu unaleta mzaha.

**Mata:** Mweshimiwa hakimu, sidhani kama ni kosa kufanya biashara. Nilikuwa najitafutia riziki. Na riziki ni popote.

**Hakimu:** Kama riziki ni popote kwa nini usiuzie nyumbani kwako.

**Mata:** Njini nilikuwa nafata wateja.

**Hakimu:** Huoni kwamba ulikuwa unavunja sheria za jiji kifungu namba 005 cha mwaka 2008.

**Mata:** Sikubahatika kuzisoma. Kama sheria ningepewa nikazisoma, wala nisingezivunja mweshimiwa hakimu.

**Hakimu:** Kwa kuvunja sheria za usafi miji, unatakiwa kulipa faini ya shilingi laki moja. Au kifungo cha miezi mitatu jela na kazi ngumu.

**Mata:** (*Kwa huzuni*). Mweshimiwa hakimu sina uwezo wa kulipa faini. Ndio kwanza nilianza biashara. Na sina ndugu hapa njini. Na kama ni kazi ngumu afadhali niachiwe nikapalilie mikoroshu yangu Kadengwa. Nna njomba wangu anaitwa Chupaku anakaa Manzese. Naomba nkantafute anilipie faini.

**Hakimu:** Kesi kama hii si ya kusikilizwa mara mbili. Umeshindwa leo kutoa faini unaenda ndani miezi mitatu. Ili iwe fundisho kwa vijana wengine wanaokimbilia mijini bila shughuli maalumu za kufanya.

**Mata:** (*Akilia na kupenga kamasi*). Mweshimiwa hakimu, naomba huruma yako. Kukaa kijijini kulima pia tumechoka. Nilikuja njini kutafuta kazi. Wazazi wangu kijijini wananitegemea. Sasa kibanda changu cha biashara kimevunjwa. Mali zangu zote zimepotea. Mweshimiwa hakimu, nyie wa juu tusaidieni. Sisi vijana wenu tunataabika. Hatuna kazi. (uk. 47 - 48)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Safari ya Chinga*, 2009)

Nukuu hii inayohusu maelezo ya Mata kwa Hakimu yanathibitisha namna viongozi walivyoshindwa kuweka mifumo bora na sahihi inayowawezesha wananchi kunufaika na raslimali zinazopatikana katika maeneo yao ya asili badala ya kukimbilia maeneo mengine. Kama hilo haliwezekani, basi mamlaka zingetenga maeneo mahususi, toshelevu na rafiki kwa ajili ya biashara za wajasiriamali wadogo kukua na kustawi. Kinyume na maono ya Mata, Hakimu ambaye ni sehemu ya watungaji, wasimamizi, watekelezaji na watoa matamko, sera na sheria anashindwa kuliona tatizo hili. Badala ya Hakimu kutoa hukumu yenye kuiadhibu serikali na kuiamuru kutunga sera na sheria rafiki zenye kutekelezeka kwa kupeleka huduma bora na sahihi katika kila kona ya nchi, yeye anamuhukumu Mata kwenda jela miezi mitatu ama kulipa faini ya Tsh. 100,000/=.

Hapa panaibua maswali lukuki ya kujiuliza, mathalani; huko gerezani hawa wafungwa wanatoa faida gani kwa taifa? Je, siku wakimaliza vifungo vyao, wafungwa hawa watakuwa wametajirika ama umasikini utakuwa umepungua au kuisha, au kubaki pale pale? Je, kufungwa kwa akina Mata ndiyo kutakuwa suluhisho la wajasiriamali wadogo kukimbilia mijini na kufanyabiashara popote wanapoona kunawafaa? Je, wakitoka gerezani watarudije huko kwao au wataendelea kuzurura humo humo mjini? Kama watabaki mjini, serikali na mahakama watakuwa wametatua au wameongeza matatizo yanayowakabili watu wa tabaka la chini? Hii ni mifano michache katika mingi inayoonesha namna aina ya watendaji chini ya siasa na wanasiasa tulionao katika taifa wasivyokuwa weledi, wabunifu wala suluhu sahihi ya ukombozi wa mtu wa tabaka la chini. Badala yake, siasa iliyopo na wanasiasa waliopo wanafikiria uungu wao na maslahi yao, daima. Mahakama nayo haina budi

kuongozwa na busara katika kutoa hukumu, badala ya kuzitekeleza sheria kama zilivyoandikwa. Kauli ya Mata isemayo, “Mweshimiwa hakimu, naomba huruma yako. Kukaa kijijini kulima pia tumechoka. Nilikuja njini kutafuta kazi. Wazazi wangu kijijini wananitegemea. Sasa kibanda changu cha biashara kimevunjwa. Mali zangu zote zimepotea. Mweshimiwa hakimu, nyie wa juu tusaidieni. Sisi vijana wenu tunataabika. Hatuna kazi” ni nzito kwa mhimili unaoongozwa na hekima, ukweli na utu katika maamuzi. Lakini hali haikuwa hivyo.

Changamoto ya taifa kujaa watendaji, wanasisia na aina ya siasa inayobeba matamko, sera na sheria zisizokuwa shirikishi na wezeshi, wala kuwa na maandalizi ya kutosha kuwaandaa watendaji na wananchi kushirikiana kwa umoja na mshikamano katika kuzisimamia na kuzitekeleza sera, sheria na matamko inaonekana hata katika tamthilia ya *Changamoto*. Ndani ya tamthilia hii ya *Changamoto* mnaonekana kuwapo kwa viongozi wenye kutoa kauli huku wengine wakitakiwa kutekeleza. Kauli za viongozi wakuu wenye kutoa matamko kwa mfano Malkia inaonekana ni ya kisiasa zaidi isiyovuka mipaka ya jengo mlimotolewa kauli husika. Kauli ya Malkia kwa watu wenye ulemavu imejaa hamasa na matumaini kwa wanyonge hasa ikizingatiwa mtoa hamasa na tamko ndiye kiongozi mkuu wa nchi. Haya yanathibitishwa kupitia nukuu ifuatayo: -

**Malkia:** Ni furaha yangu kuwapo mahali hapa na kukutana nanyi. Leo ni siku ya mwaka mpya na nimeonelea ni jambo jema tuwe na utaratibu wa kukutana kila mwaka. Lengo la siku hii ni kutiana moyo na kutakiana heri katika mwaka mpya unaoanza na siku ya leo. (*Hadhira ambayo ni walemavu na wasio na ulemavu inapiga makofi na kushangilia*). Jambo la msingi ni kuwaomba msitumie upungufu wenu wa viungo



kama kikwazo, hapana. Upungufu huo uwe ni changamoto ya kukuleteeni maendeleo. Hakuna haja ya kulilia mkono au mguu uliopotea. Bali ni kutumia viungo vilivyobakia katika kuchakarika ili kujitafutia riziki. (*Walemavu wanapiga makofi*). Kwa hayo machache, nawakaribisha sana kwenye hafla hii niliyowaandalieni ili tule, tunywe, na tufurahi. Asanteni. (*Anaondoka na kurudi mahali pake na anakaa. Watu wanapiga makofi sana na kushangilia*). (uk. 2 – 3)

**(Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Changamoto*, 2010)

Kauli hii ya Malkia kama kiongozi mkuu wa nchi inaonesha kuwapo kwa mabadiliko makubwa na ya makusudi katika taifa na serikali nzima kwa faida ya wanyonge, hususani watu wenye ulemavu. Hata hivyo, kinyume na matarajio ya wengi, kauli hii ya malkia inakuja kubainika kuwa ni sawa na zile kauli za majukwaani zilizokwisha kutolewa sana katika kuwapa matumaini na hamasa wananchi. Lengo likiwa ni kuhakikisha wananchi wanaendelea kuwa waaminifu na watiifu kwa viongozi hasa viongozi wakuu. Hata hivyo, hakuna mabadiliko wala dhamira ya dhati ya kimtazamo, kiseria na kisheria iliyowekwa kwa faida ya taifa na mwananchi mmoja mmoja. Malkia anatamka bila kusimamia matamko yake ili kuhakikisha yanaundiwa sera na sheria za kuwalinda, kuwahifadhi na kuwastawisha kwa dhati watu wa tabaka la chini hususani watu wenye ulemavu. Tunayaona madhira yanayowakumba watu wenye ulemavu baada ya kuhamasishwa na Malkia kupitia nukuu ifuatayo. Tunanukuu: -

**Maimatha:** (*Amekaa karibu na Godwin, anamtazama*) Baba.

**Godwin:** Naaam!

**Maimatha:** Nafikiri kwenda kuandikisha kesi kwa ajili ya yule Mwalimu wa Kikulacho...

**Godwin:** Sawasawa, tena tukitoka hapa liwe ndilo jambo la kufanya.

**Maimatha:** Kweli, maana namwona hapa mahakamani Yule Mwalimu, ningekuwa nimemripoti Polisi na yeye leo angewekwa kitimoto.

**Godwin:** Hatujachelewa. Tukitoka hapa tutalishughulikia jambo hilo.

**Maimatha:** (*Akitazama alipokaa Chazye, Peti, Meliza, na Msomaji*). Pia ulisema na wale vijana pale (*akionyesha kidole walipokaa*) walikuambia kuhusu manyanyaso waliyoyapata kwa Mwalimu yule?

**Godwin:** Ndiyo, na pia tutawashauri ili tulipeleke jambo lao Polisi. Lazima watu wenye mtazamo mbaya kwa walemavu wakumbane na mkondo wa sheria ili wabadilike, na ili liwe fundisho kwa wengine wanaowanyima haki ya elimu, haki ya ajira, na ubaguzi kwa walemavu.

**Maimatha:** (*Akifikiria kitu*) Hivi ukienda kuandikisha kesi unapaswa kutoa pesa ya kufungulia kesi?

**Godwin:** Hapana. Wewe unaripoti na maelezo yanaandikwa, kasha unapewa mpelelezi wa kesi yako. Huyu ni Polisi ambaye atatafuta habari zinazohusiana na tuhuma zinazomkabili mtu pamoja na kumkamata mtuhumiwa ili kumfikisha Polisi. (uk. 8 – 9)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Changamoto*, 2010)

Nukuu hii inaonesha unyanyapaa na ukatili wanaofanyiwa wanyonge, hususani watu wenye ulemavu, ingawa Malkia alikuwa ametoa tamko tayari. Unyanyapaa na ukatili

huo umefanywa na watendaji wa serikali na wananchi wengine (wasiokuwa na ulemavu) wenye kasumba ya kuwaona watu wenye ulemavu kuwa viumbe wasiokuwa na maana katika jamii. Mwandishi analibainisha tatizo hili kupitia kauli isemayo, “(Akitazama alipokaa Chazye, Peti, Meliza, na Msomaji). Pia ulisema na wale vijana pale (*akionyesha kidole walipokaa*) walikuambia kuhusu manyanyaso waliyoyapata kwa Mwalimu yule?” Unyanyapaa na ukatili huo ni wa Mtendaji wa kata akimdhaliisha Megno kwa kumnyima fomu ya kugombea uongozi, kumuita ombaomba, pia kilema asiyeweza kumuongoza yeyote (uk. 5). Waendesha vyombo vya usafiri wanakataa kusimama ili Megno aweze kupita kwenye zebra hadi dereva mwanamke mmoja aliposimama na kuwasimamisha madereva wengine ilhali Megno alijitahidi sana kuyasimamisha magari kwa kupunga mkono ishara ya kuwataka wasimame (uk. 6 – 7).

Unyanyapaa na ukatili mwingine ni ule wa Peti, Msomaji na Meliza walioitwa ombaomba, kutokaribishwa ofisini, kutokujuliwa hali, kufukuzwa na kunyimwa nafasi ya kujiunga na elimu ya sekondari ofisini kwa Mkuu wa Shule. Yote yalitendwa kwa sababu tu, wao ni watu wenye ulemavu (uk. 7 - 9). Naye Maimatha anadhulumiwa ajira yake na kukejeliwa, kwa sababu ni mlemavu, tena anaitwa ombaomba ofisini kwa Mkuu wa Shule (uk. 13 - 14). Mganga na Abuu wanadhulumu uhai na nafsi ya Kauye kisa tu, yeye ni mlemavu wa ngozi. Tamaa ya mali na utajiri inamnyang’anya Kauye haki ya kuishi na kufurahia maisha pamoja na binadamu wengine (uk. 31). Zaidi, watu wenye ulemavu wanakejeliwa kwa majina ya kidhalilishaji kama vile kipofu (uk. 22), kilema (uk. 23 & 24) na wenye dhambi na kiwete (uk. 24). Pamoja na udhalilishaji huu, bado vijana wenye nguvu na wasio

na ulemavu wowote (mathalani Kimweri na Rajab, uk. 23 – 27) wanathubutu kuwapiga, kuwatukana, hata kuwapora mali watu wenye ulemavu.

Mbaya zaidi, jamii inayotegemewa kuwasaidia watu wenye ulemavu, nayo haioneshi kuguswa na matatizo ya jamii hii maalumu. Hata wengi wa wazazi na ndugu wa watu wenye ulemavu hawaonekani kuwasaidia watu wenye ulemavu kupata haki zao pindi wanaponyanyaswa. Ni familia ya marehemu Kauye na baba mzazi wa Maimatha ndio wazazi pekee wanaonekana kujali hali, ulinzi, usalama na hatima ya maisha ya watoto wao ambao ni watu wenye ulemavu. Hili linathibitishwa kwa nukuu hii: -

**Rajabu:** *(Akimwamrisha) Niachie mzee! Nasema niachieeee! (Rajabu anafurukuta kujitoa mikononi mwa Godwin na anampiga teke la tumboni. Godwin anagugumia kwa maumivu na anaanguka chini. Rajabu anakimbia kuelekea walikokaa hadhira. Wakati huo huo Kimweri anapurukushana na Chaazye na anajitoa mikononi mwake na anakimbia. Walemavu waliokuwapo jukwaani wanapiga kelele za kuomba msaada. Wanasikika wakisema: **KAMATA! KAMATA! KAMATA!** Lakini hakuna mtu anayejitokeza kumkamata mhalifu yeyote anayekimbia. Pazia linafungwa).* (uk. 28)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Changamoto*, 2010)

Nukuu hii inathibitisha ya kwamba jamii haina umoja wala ushirikiano katika kumkomboa mtu mwenye uhitaji maalumu. Wala hawaoni thamani na wajibu wa kuwalinda na kuwatetea. Kila mmoja anajiona kutokuwa sehemu muhimu katika kumtetea na kumpigania mnyonge huyu. Haingii akilini kuona maagizo ya kiongozi

mkuu wa nchi yakikiukwa kwa ujasiri na watendaji wa serikali. Watendaji hawa wameteuliwa na wanalipwa mishahara na marupurupu na serikali ileile. Wanaposhindwa kutekeleza au kutunga sera na sheria rafiki kwa umma wote, kunafungua fursa ya watu kuamini kuwa watendaji na wanasiasa husika ni zao la siasa chafu iliyoundiwa sera chafu na kunadiwa kupitia matamko yanayobebwa katika mfumo mchafu na kuwasilishwa kwa umma kwa njia chafu kwa maslahi ya wachache.

Mtoa kauli ambaye ni kiongozi mkuu wa serikali – Malkia anaonekana kupuuzwa na wasaidizi wake na wananchi walio wengi. Picha hii inaonesha kutokuwapo kwa mfumo sahihi na bora wa kimawasiliano, kinidhamu, kiintelenjesia na kiutendaji miongoni mwa watendaji ndani ya serikali na wanajamii kwa faida ya taifa zima na raslimali zake za kila aina. Na kwamba, matamko yanayotolewa mbele ya kusanyiko la watu wa tabaka la chini huwa siyo kusudio la dhati hasa la mtamkaji wala siyo sehemu ya maamuzi wala utekelezaji wa sera na sheria zilizotungwa. Huku ndiko kusema ya kwamba, hata kukamatwa na kufungwa kwa Mganga na Abuu (uk. 29 – 31 & 36 - 39) kutokana na mauaji ya Kauye, binti mdogo na mlemavu wa ngozi, siyo kwamba lilikuwa lengo la kumkomboa mtu wa tabaka la chini. Bali ni sehemu ya hukumu zinazotolewa kwa watu wa tabaka la chini kwa sababu hata washitakiwa ni sehemu ya tabaka la chini lililotenda unyama.

Laiti tukio hili lingewahusisha watu wa tabaka la juu, basi wahusika wakuu wasingepatikana. Endapo wangepatikana, mchakato wa kesi, upelelezi na hukumu vingejaa uvulivuli na mwisho wahusika kuishia kulipa faini badala ya kifungo. Au wangethibitika kutokuwa na hatia hivyo kuachiwa huru. Matukio ya namna hii

yamewahi kujitokeza katika kesi nyingi za mauaji yaliyohusishwa na watu wa tabaka la juu (Wazambi na Mikongoti, 2018). Aina ya siasa na wanasiasa wanaoishi kwa matamko huku sera na sheria zikikanyangwa kwa maslahi ya kundi dogo yanaonekana kuendelea kuliangamiza taifa na wananchi wengi wanaoangukia katika tabaka la chini. Uongozi wa siasa za namna hii ni hatari kwa ustawi wa jamii kwani hazijawahi kuwa mwarobaini wa changamoto za taifa, mahali popote duniani (Mukandala na Gasarasi, 2000).

Jambo hili limebainika kuwapo hata katika tamthilia ya *Nje – Ndani*. Waandishi wanaonesha kuna sera na sheria kadha wa kadha zinazozidi kumnyang’anya utu, maarifa, raslimali, ustawi na maendeleo hata yale madogo anayoyapata mtu wa tabaka la chini. Wakati huo huo, viongozi na watendaji wengi wakizidi kuifisadi nchi kwa faida ya matumbo yao na makundi yao. Madai haya yanathibitishwa kupitia nukuu ifuatayo: -

**Utashi-Nafsi:** Nusu itakayobaki itakuwa ni ya mkate. Ona tulowapa, walivyoharibu mchele wetu, hakuna nusu yetu wala yao haina baraka. [*Anaimba*] Maadui zetu ni marafiki...

Wote watatu twawafikii...

Abah aba ba ba ba...

Alo ho ha heeeee...

Maradhi kipenziii

Ujinga laaziziii...

Umasikiniiii...

**Njozi:** Maradhi? Ujinga? Umasikini? Maadui? Marafiki? ...

Loh!

**Utashi-Nafsi:** Wastaafu Mhenga.

**Njozi:** Wepi? Walimu? Wanajeshi? Wauguzi? Madaktari? au watumishi wengine wa umma?

**Utashi-Nafsi:** Wakatunza amana, wakadhani itakuja kutumika kwa huruma, upole, uangalifu, uadilifu, utu, wema na haki ya kweli. Eti ingewakuta uzeeni.

**Njozi:** Sasa je?

**Utashi-Nafsi:** Takataka, mapambo, fakhari, sifa, udhaifu na kero. Haikufaa jana, leo wala haitasaidia kesho. (uk. 55 - 57)

**Utashi-Nafsi:** Yaani wao ni kukosoa tu pasi na kusahihisha na kuonesha matatizo bila ya suluhu. Ni kuangalia udhaifu badala ya uimara. Ni kutazama sura badala ya kichwa. Kama hii ndiyo maana kamili ya usomi, sioni haja kupekuwa kurasa hizi. [*Kwa hasira na pupa anafunga kurasa za kitabu chake*] ... Kama kipimo chao ni *ubize* hata kama hawana shughuli za dhati za kufanya. Kuwa na majibu na kukosa majawabu, kupenda vya watu na kupuuza vya kwao. Sifikiri ni busara ya kuvaa joho hili. [*Analitupa joho chini, puuuh! Anatembea huku anasema maneno yasiyofahamika vizuri*].

Ninajiuliza bila majibu, hivi na wao  
hujiuliza swali hili?

**Moyo:** Nchi zatusomesha?

**Akili:** Bure kabisa

**Moyo:** Zatuhusia.

**Akili:** Kutumikia kwa manufaa ya nchi. Kale tuliimba hongo ni adui wa haki. Sasa wimbo huu ni zilipendwa. (uk. 63 – 64, 83)

**Utashi-Nafsi:** Akina mama, wafanya biashara wadogo wadogo, vijana, misukule na manamba wa miamala.

- Moyo:** Chukua moja rudisha mbili, yaani mara mbili!!
- Macho:** Tena ulete mbili kabla hiyo moja haujaipata vizuri.
- Moyo:** Duuuh! Ni ukatili, unyama na ufedhuli mkuuu. [*Anatikisa kichwa kwa masikitiko*]. (uk. 69 – 70)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Nje - Ndani*, 2016)

Nukuu hii inaonesha namna aina ya siasa na viongozi watokanao na mfumo mbovu wa kisiasa wanavyoshindwa kutetea maslahi ya taifa. Siasa, sera na sheria zinazotumika mpaka sasa zimekosa utashi wa kisiasa kuwatetea wanyonge wakiwemo wajasiriamali wanaotaabika kila kukicha. Mbaya zaidi, sera na sheria zilizopo zinaonekana kuzidi kuwafilisi wanyonge badala ya kuwainua kiuchumi na kijamii. Hapa tunagundua ya kwamba, viongozi wengi hawana uzalendo, utashi wa kisiasa, nidhamu, utu na dhamira ya dhati ya kuwakomboa wananchi wanyonge. Badala yake, wanaona fahari kuwatumia wanyonge hawa kama daraja na ngazi ya wao kuingia katika ulimwengu wa tabaka la juu kufaidi mema ya nchi. S. S. Massoud (2018) anakubaliana nasi kupitia utafiti wake kwamba, hali ya mnyonge kuwa daraja la tabaka tawala kwa nyakati hizi siyo jambo la kuuliza. Katika mazingira ya namna hii, mwandishi hana budi kutumia kalamu na ubunifu wake kuutaarifu, kuupigania na kuufunda umma wa mtu mnyonge juu ya umuhimu wa kupigania haki na usawa katika nyanja zote za maisha (Nazareth, 1978).

Kwa jumla, uchunguzi wetu umebaini tamthilia zote sita (6) teule zinajadili kwa kina na uchungu namna aina ya siasa na wanasiasa wengi waliopewa dhamana ya madaraka na mamlaka, wanavyoyatumia madaraka na mamlaka hayo kujinufaisha wao wenyewe na kundi dogo la kibepari. Huku wakiishia kutoa matamko na kutunga sera na sheria zinazotekelezeka kwa faida ya kundi teule badala ya kumkomboa mtu



wa tabaka la chini. Tamthilia hizi zote zimethibitisha kiweledi na kiubunifu kwamba, wengi wa viongozi na watendaji wa kisiasa wamejaa ubinafsi na dhuluma kwa wanyonge. Matendo yao hayana tija wala matumaini kwa ukombozi wa kweli, ustawi na maendeleo ya kweli na endelevu kwa faida ya taifa na mtu mmoja mmoja katika nchi. Matendo hayo ni pamoja na: tamaa, uzembe, ubinafsi, usaliti, dhuluma, chuki, ubaguzi, ufisadi, rushwa, ushirika na mabepari, dharau, uporaji na ujilimbikiziaji wa raslimali za taifa.

Huku ndiko kusema ya kwamba, kwa aina hii ya viongozi, wanasisia na siasa, kamwe taifa haliwezi kupiga hatua mbele kimaendeleo na kiustawi. Hivyo, pana haja ya kufanya mapinduzi ya kweli na sahihi kupitia watu sahihi na njia sahihi zenye kuleta mapinduzi sahihi na bora kwa faida ya taifa na mtu mmoja mmoja. Mapinduzi ya kweli yatapatikana tu endapo kila kiongozi na mwanajamii atakomboka kifika katika kutambua thamani ya utu, haki, usawa na kujikina kwa faida ya jamii nzima (Nyerere, 1994). Tofauti na hivyo, hakuna mapinduzi ya kisiasa yatakayoleta ukombozi sahihi kwa maendeleo sahihi na ustawi bora, sahihi na endelevu kwa taifa na mtu mmoja mmoja. Dhamira katika tamthilia za awamu ya soko huria ni mwendelezo wa ajenda ya dhamira zilizotawala tamthilia nyingi za awamu ya Azimio la Arusha. Kwa hiyo, tunaweza kusema kuwa utafiti wetu umebaini kuwa tamthilia hizi zote sita (6) teule zinalenga kujenga jamii mpya na endelevu.

Tunapochunguza kufanana kwa dhamira ndani ya tamthilia sita (6) teule huku tukiyahusisha na mapitio ya maandiko mbalimbali tuliyoyatalii kwa pamoja na nadharia teule ya utafiti huu (nadharia ya Uhistoria Mpya), tunabaini hakuna kitu hata kimoja kilichojitokeza kwa bahati mbaya akilini mwa kila mwandishi. Kwa

sababu, tunaposoma maandiko kwa mfano, Nauta (1972), Rodney (1972), Juhani (1988), Hancock (1991), Independent Commission of the South on Development Issues (1992), Arkadie (1995), Helge (1996), Settles (1996), na Chachage (2000, 2002, 2014) tunagundua kuwa, Mwafrika akiwemo Mtanzania amezungukwa na changamoto nyingi za kisiasa, kiuchumi, kitamaduni na kijamii.

Maandiko mengine ni Arowolo (2010), Ally na wenzake (2013), Fouéré (2014), Gromov (2014), International Labour Organisation (2016), Economic and Social Research Foundation (2018), Farnsworth (2019), International Organization for Migration (2019), Maake (2006), Msekwa (2013), Mwiru (2013), na Masabo (2014). Pia, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (2018), Pearson (2000), Pamba (2012), Raiamwema (Juni 01, 2012), Sharma (2015), na Sitta (2013). Vilevile, United Nations Economic Commission for Africa (2016), Tanzania Commission for AIDS (2018), Wakota (2018), Wazambi na Mikongoti (2018) kutaja kwa uchache kunathibitisha kuwapo kwa changamoto hizi. Changamoto hizi zinajitokeza kwa namna inayofanana lakini zikizidiana viwango kutokana na wakati, mazingira na aina ya uongozi na utawala wa ndani na nje ya nchi na taifa husika.

Wanafasihi Linganishi wanalifafanua vema tukio hili tulilibaini la kufanana kiutunzi kwa dhamira miongoni mwa waandishi wa tamthilia sita (6) teule. Kwa mfano, Guyard (katika Cao, 2013) anasema ulinganishaji wa fasihi za jamii moja au tofauti tofauti unapofungamanishwa na historia ya mahusiano ya fasihi kitaifa na kimataifa huibua kufanana na kutofautiana. Kwa sababu jamii zinazohusiana huwa na tabia ya kuathiriana moja kwa moja au kwa kiasi katika nyanja mbalimbali za maisha. Kuathiriana huko kunaweza kuwa kwa kufanana au kutofautiana (Cao,

2013). Hali hii hutokana na tofauti au mfanano wa mawasiliano ya dhati yanayohusisha pande mbili au zaidi za jamii na, au sanaa. Mawasiliano hayo ni kati ya kazi na kazi, pia misukumo na maisha ya waandishi wa fasihi kadhaa ndani na nje ya mipaka ya fasihi hizo ndani ya wakati na mazingira mahususi (Carrer, katika Cao, 2013). Mambo haya yote yanapomsonga mwandishi, humfanya mwandishi husika achague mwelekeo wa mwono wa sanaa yake kiubunifu – ama kwa kujua au kwa kutokujua. Hatimaye, mwandishi huyo hutoa kazi inayofanana au kutofautiana na waandishi wengine au kazi zake nyingine - ama kwa karibu au kwa mbali (Cao, 2013).

Kwa muktadha huu, matokeo ya kufanana kiubunifu kwa dhamira za tamthilia sita (6) teule ni athari ya mawasiliano ya misukumo na mikingamo inayoishi katika jamii husika iliyomlea na kumshurutisha mwandishi kuandika kile alichokiandika. Kwa sababu, mwandishi huandika kile alichokiona, alichokiishi, alichosimuliwa, alichooteshwa, alichohisi, alichofundishwa na alichokivuna kutoka kwa watunzi wengine (Sanchez, 1973; Abdulla, 1974; Nazareth, 1978; Soyinka, 1979; Senkoro, 1987; Mbise, 1996; Culpeper, na wenzake, 1998). Zaidi ya hayo, mwandishi yeyote yule huathiriwa na kani ama za ndani au za nje ya nafsi na akili yake kutegemeana na mazingira na wakati (Soyinka, 1979; Thiong'o, 1986; Senkoro, 1987; Mlama, 2003; Maake, 2006; Ruhumbika, 2006; Jilala, 2012, Adeseke, 2016). Kwa hiyo, hakuna utunzi usiosemezana na historia ya wakati na mazingira ya kiroho na kimwili yanayomuumba mwandishi - kwa karibu au mbali (Masatu, na wenzake; 2020).

### 4.3.2 Kutofautiana kwa Ubunifu katika Ujenzi wa Dhamira katika Tamthilia

#### Teule

Utafiti umebaini kuwa kuna tofauti katika njia na uzito wa kutathmini, kujadili na kufikia suluhisho la matatizo yanayoikabili jamii iliyokwama kufikia maisha bora na endelevu. Hivyo, data za utafiti huu zinadhihirisha kwamba kila tamthilia imejadili mambo yale yale kwa ubunifu tofauti tofauti. Utafiti huu umebaini kuwa, sababu kuu ya kutofautiana kwa dhamira zinazowasilishwa katika tamthilia hizo ni matukio na wakati mahususi ambao unatawala maisha ya vizazi vya mwanadamu. Kwani wakati na mazingira yaliyomlea mwandishi huchangia sana mwandishi mmoja au tofauti tofauti kuandika jambo lilelile kwa namna ama ileile au tofauti (Maake, 2006; Ruhumbika, 2006; Adeseke, 2016; Senyamanza, h. m.).

Ruhumbika (2006) na Jilala (2016) wanaongeza kuwa, mifumo ya kiutawala ina mchango mkubwa katika kumfanya mwandishi kuwa huru au mtumwa katika kubuni na kuwasilisha wazo lake kwa namna anayoona inafaa. Kwa muktadha huu, njia ya uwasilishaji wa dhamira kati ya mwandishi mmoja na mwingine, au mwandishi yuleyule mmoja katika kazi zake kadhaa ndiyo huleta utofauti kiubunifu. Kwani wakati, mazingira na mifumo ya kiutawala ndani ya jamii anamoishi mwandishi huamua hatima ya mwandishi kisanaa.

Mathalani, tamthilia zote tatu (3) za awamu ya Azimio la Arusha – *Mashetani, Kijiji Chetu* na *Harakati za Ukombozi*, zimejadili na kutathmini kwa kina namna wengi wa viongozi wa Kiafrika ambao ni zao la kipindi cha ukoloni (1890 – 1960) walivyosaliti mipango na sera za ujenzi wa mataifa huru ya Kiafrika baada ya wakoloni kuwakabidhi wazawa mamlaka ya kuongoza mataifa yao kwa niaba ya

Wafrika wenzao. Badala ya viongozi hawa wazawa kuwatumikia wananchi wazawa wenzao, wao wakakengeuka na kuwa mbwa mwitu ndani ya ngozi na mwonekano wa kondoo. Kwa kuishi maisha na tabia za wakoloni weupe ndani ya ngozi nyeusi. Mambo haya si ya kufikirika au kuhadaa jamii. Yamekuwa yakitamkwa na viongozi kadha wa kadha katika majukwaa na maandishi kuonesha namna watendaji na viongozi wasiokuwa waaminifu walivyochangia kuuu ndoto za waasisi wa mataifa. Baadhi ya viongozi hao ni Khatib (1988), Nyerere (1994), Mwiru (2013), Shivji (2013), Sitta (2013), Mkapa (2019), kutaja kwa uchache.

Nazo tamthilia za awamu ya soko huria - *Safari ya Chinga, Changamoto na Nje – Ndani* zimejikita zaidi katika kutathmini namna wengi wa viongozi tena wasomi ambao ni zao la Tanzania huru ndani ya ukoloni mamboleo wanavyolinajisi taifa kwa kushindwa kujifunza kutokana na makosa yaliyofanywa na watangulizi wao wa awamu ya Azimio la Arusha. Wakati viongozi wengi wa awamu ya Azimio la Arusha wakigeuka wakoloni weusi wa kianalogia, viongozi wengi wa awamu ya soko huria wamegeuka wakoloni weusi wakidijitali kwa kukumbatia ukoloni mamboleo chini ya mfumo wa utandawazi. Mambo haya ni ya kweli tena yanaungwa mkono na marejeo mengi kutoka wasomi na viongozi wanaoona hali hii siyo sawa kama tulivyothibitisha katika aya tangulizi kabla ya aya hii. Maumivu na mijadala ya usaliti kwa namna tofauti tofauti, kiwango na aina za dhamira zinabainishwa katika tathmini yenye ushahidi wa nukuu kutoka kila tamthilia teule, kama tutakavyoona hivi punde.

Utafiti umebaini ya kwamba tamthilia ya *Mashetani* imejichimbia zaidi katika kutathmini ugumu uliopo katika kuwapata viongozi wanamapinduzi na wazalendo

wa dhati. Viongozi wengi wanaojinadi kuwa wazalendo na wanamapinduzi, mioyoni mwao mmejaa njaa, tamaa, ufisadi, ubaradhuli, hinda, ubinafsi na unafiki. Na kwamba, kinachoitwa mapinduzi matukufu na ya kizalendo kwa sehemu kubwa siyo mapinduzi sahihi bali ni mapinduzi ya kundi maslahi dogo ili kukidhi hamu na tamaa yake ya kuhodhi mamlaka na madaraka. Pindi kundi hili lipatapo fursa ya kupindua utawala uliopo kisha kujihakikishia mamlaka na madaraka kamili, kundi hili huanza kuonesha “uzalendo” na “uwanamapinduzi” wake kwa kuanza kutibu njaa na kiu yao pasipo kujali utu, haki, usawa, na ustawi wa jamii nzima. Haya yanathibitika kupitia nukuu ifuatayo: -

MTU 1: [...] (*Mlio wa gari inapita.*) Doo doo! Salaale! Umeona mdudu ule?

MTU 2: Nini? Ile gari? Nimeiona. Aah, ataiuza kesho ile. We ngoja tu.

MTU 1: Kwani we unamjua yule?

MTU 2: Kwani we humjui?

MTU 1: Hata.

MTU 2: Jana hatukuwa wote pamoja, alipo akitusimulia Bwana Mathew juu ya kufungwa kwa ile kampuni.

MTU 1: Aah! Aah! Ndiyo, ndiyo, ndiyo. Aha! Kwani ndiye huyu bwana wenyewe?

MTU 2: Eh. Pesa chungu nzima bwana zimepotea. Lakini ndiyo haijulikani kuwa zimeibiwa au zimepotea katika mahisabu.

MTU 1: Alaa. Kumbe ndiye huyu? Shetani kweli kweli... (uk. 42-43)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Mashetani*, 1971)

Nukuu iliyotolewa hapo awali inaonesha kuwapo kwa tatizo kubwa katika uaminifu miongoni mwa watendaji wanaopewa dhamana ya kusimamia na kuzistawisha taasisi za umma. Mjadala nukuliwa unathibitisha namna baadhi ya watendaji wa ofisi,

mashirika na taasisi za umma wanavyoiba na kufisadi miradi waliyokabidhiwa huku wanaopaswa kuwawajibisha wakisita kuchukua hatua za kinidhamu. Matokeo yake, mashirika yanakufa ilhali wabadhirifu wakibaki na mavuno waliyojilimbikizia. Kumbe, wizi na ufisadi ulikuwapo hata awamu ya Azimio la Arusha. Tena hujuma hizo zilifanywa na wazawa walioaminiwa na kupewa fursa ya kutumikia taifa kupitia vyeo vyenye maslahi na mamlaka huru ya kiutendaji. Badala ya kufanya kwa tija - kwa faida ya taifa, wao wakafanya kazi kwa faida ya matumbo yao bila kujali vizazi vijavyo vitaishije. Maisha mapya ya anasa yanawafanya wafurahie ufisadi na anasa pasipo kujali hatima ya vizazi vya leo na kesho. Kwa kuwa kwa wao, maisha ni leo na siyo vinginevyo. Mfano wa tabia ya ubinafsi na kufurahia ufisadi na kujilimbikizia mali tunaupata pia katika nukuu ifuatayo: -

BABA KITARU: Shhh.... Njoo, njoo nikuonesheni kitu.

MAMA KITARU: Nini?

BABA KITARU: Ndege wangu.

JUMA NA KITARU: Ndege!

BABA KITARU: Njoni hapa dirishani. Unaiona nini?

MAMA KITARU: Gari mpya! Benzi!

BABA KITARU: Yangu! Naam! Mali yangu, jasho langu. Kitaru, njoo uitazame. Juma, njoo. Mnaiona? Tazama ilivyotulia. Basi pale itoneshe tu – waaaah, linaruka kama ndege. Twende tukatembee, mnasemaje? Twendeni. Twendeni, twende. (uk. 22)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Mashetani*, 1971)

Hali hii inaonesha BABA KITARU anafurahia kuishi maisha ya anasa na anaona fahari kujilimbikizia mali kwa kadri apendavyo ilhali jamii anayoiongoza inaishi

maisha ya pangu pakavu tia mchuzi. Suala hili la matumizi mabaya ya mamlaka na madaraka katika uongozi kwa kujilimbikizia mali linathibitisha kuwapo kwa maadui wa haki, usawa na maendeleo endelevu wanaojificha katika koti la ukombozi na mapinduzi. Huu ni uthibitisho kuwa hata kabla, wakati na baada ya mapinduzi ya Zanzibar na kuasisiwa kwa Azimio la Arusha, baadhi ya viongozi wa Kiafrika hawakuwa tayari kutenda haki na kutoa nafasi sawa kwa ustawi wa jamii nzima. Kupitia mazungumzo kati ya Juma na Kitaru hoja hii inajipambanua vema. Data ifuatayo inalisawili jambo hili: -

JUMA: Hatuwezi kusahau. Kila siku tunafunguliwa vifua na kujazwa sumu ya mambo ya jana.

*(Kitaru anaitikia. Kimya.)*

JUMA: Kwa heri.

KITARU: Hatuonani tena?

JUMA: Hatuonani tena.

KITARU: Kwa nini?

JUMA: Sababu nyingi.

KITARU: Mojawapo?

JUMA: Mpanda ngazi na mshuka ngazi hawewezi kushikana mikono.

KITARU: Pili?

JUMA: Wewe unaishi leo mimi naishi jana. Tutakuwaje marafiki? Na kila leo yako ni kidato cha kesho yako. Mimi, kila leo yangu ni kidato cha jana zangu. Na kila nikienda huko, nikirudi ninarudi na hadithi... hadithi za mashetani. (uk 56)

**(Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Mashetani*, 1971)



Nukuu hii inathibitisha kuwapo kwa tofauti ya kimamlaka, kiuchumi na kihistoria kati ya matabaka mapya - tabaka tawala na tabaka tawaliwa, baada ya kile kinachoitwa mapinduzi matukufu ya wazalendo wa Kiafrika. Mwandishi anasema, “Mpanda ngazi na mshuka ngazi hawewezi kushikana mikono.” Kauli hii inathibitisha kuwapo kwa matabaka. Tofauti hii imesababisha kuwapo kwa shida kubwa katika jamii kwa kujenga matabaka na ubaguzi katika mahusiano kati ya walionacho na wale wasionacho. Ubaguzi huu baada ya ukoloni na mapinduzi ya Zanzibar unathibitisha kuwapo kwa mwendelezo endelevu wa chuki na ubinafsi miongoni mwa wanajamii.

Katika utafiti wetu tumebaini kuwa, badala ya kujenga umoja wa kitaifa baada ya mapinduzi, “wanamapinduzi” wanazidisha ubinafsi, unyonyaji, ufnisadi, visasi na ubaguzi kwa wale wote ambao walikuwa wanatawala au kuunga mkono utawala uliokuwapo awali (Hettiger, h. m; Lukumbo, 2008). Hili ni jambo linalozidisha machungu na makovu hata kwa wananchi wasiokuwa na hatia wala wasiokuwa wafuasi wa watawala wa jana wala wa leo (Chachage, 2000). Nukuu hizi zote zinathibitisha aina ya mkito na kiini cha ubunifu aliouchagua na kuusisitiza Ebrahim N. Hussein kupitia uteuzi na ujenzi wa maudhui; ambao ni uzalendo feki na uwanamapinduzi feki.

Nayo, tamthilia ya *Kijiji Chetu* inalitazama tatizo la tafsiri na utekelezwaji wa maazimio na sera katika ngazi za chini kabisa za utawala na uongozi katika jamii. Katika utafiti wetu tulibaini kuwa, mwandishi anabainisha kuwapo kwa ombwe la uongozi na usimamizi thabiti katika serikali za mitaa na serikali kuu. Pia, mwandishi ameonesha ombwe la maendeleo na ustawi wa jamii (ngazi za chini) katika nyanja za

kiuchumi, kijamii, kiutamaduni, kisayansi na teknolojia na kisiasa. Vilevile tunaona kwamba, athari ya ombwe hili ni kuibuka kwa kundi la wajanja wachache kwa ushirikiano na viongozi wachache wa ngazi za chini kutumia adui ujinga na umasikini kuwagawa, kuwanyonya na kukwamisha juhudi, maarifa na stadi za kuwaunganisha watu dhidi ya maendeleo na ustawi endelevu, kwa faida ya jamii nzima. Katika tamthilia hii ya *Kijiji Chetu*, mwandishi anawachora viongozi wa kijiji kama chanzo cha uhujumu na usaliti wa raslimali, sera na maamuzi yanayotolewa na viongozi wa juu wa chama na serikali.

Utafiti umegundua, mambo haya yanatendwa na baadhi ya viongozi kwa makusudi kabisa. Kwa sababu panaonekana kutokuwapo kwa mfumo mzuri na endelevu wa viongozi wa juu kufuatilia kile kinachoendelea katika ngazi za chini za uongozi na utawala. Jambo hili limesababisha wanyonge kuendelea kuhangaika katika lindi la umasikini huku serikali za mitaa zikishindwa kuwa chanzo cha ukombozi wa mwananchi mnyonge. Kwa kuwa, wamejigeuza vibaraka wa tabaka la mabepari uchwara wanaotumia fedha zao kuyumbisha maamuzi, umoja, ushirikiano na ujasili wa wanyonge waliotengwa na maendeleo ya kiuchumi, kielimu na kiteknolojia. Huku ni kinyume kabisa na malengo ya kuanzishwa kwa vijiji vya ujamaa (Nyerere, 1970; 1976). Tunathibitisha hoja hii kupitia nukuu ifuatayo: -

**MWANAMKE I:** [...] zaidi kuna jambo ambalo limenikera siku nyingi sana ambalo Kamati yetu inaelekea kuridhika na kuna watu wanaokaa nje ya kijiji hiki – wengine mjini kabisa. Wengi wako Dar es Salaam. Sikuwa nafahamu kuwa watu hawa wanaitwa wanakijiji wa hapa mpaka wiki iliyopita wakati tunagawana faida ya mwaka. Wao walifika kuchukua faida yao na kuondoka. Wengine walipelekewa. Wengi

tulistushwa na jambo hili. Itawezekanaje watu wasioishi kijijini wawe wanakijiji... tulipouliza tukaelezwa kuwa eti wanaleta fedha. Ah! Fedha. Kwa hiyo unaweza kununua uanakijiji! (uk. 14)

**MTU I:** Ndugu Mwenyekiti, ndugu wanakijiji. Tatizo letu hapa ni mfarakano wetu wenyewe. Maazimio tunayopitisha kwa pamoja mara nyingi yameishia midomoni na kusahauliwa mara baada ya kutoka mikutanoni. Mara ngapi tumesema wasioishi kijijini siyo wanakijiji? Lakini badala yake viongozi wetu wanakubali hongo na kuwapokea watu hao kama wanakijiji kwa fedha.

**PINDUO:** Watu husema unapochokozwa usikae kimya kwani ukifanya hivyo itachukuliwa kuwa woga au kudhibitisha ukweli wa maneno yanayosemwa. Nami siwezi kuwa kisingizio cha vyeo. Kwa nini nilijiuzulu kutoka Kamati Kuu! Kwa nini niliamua kuacha vyeo vyote mlivyonipa! Mwenyekiti ananiita mwongo. Kama kusema kuwa Bwana Mwenyekiti amefuga kuku wengi kinyume cha maazimio ya kijiji ni uwongo basi ndugu wanakijiji mnaweza kuniadhibu. Ndugu wanakijiji inasemekana kuwa mmeamua kunifukuza kwa kuwa mvivu. Nami nakubali. Lakini heri ya uvivu wangu kuliko miiko inayofanywa na Mwenyekiti. Sasa hivi ndugu Kizito ametaja mbinu anazozitumia Mwenyekiti kutunyonya. Duka lake linauzwa na mke wake hupata vitu kutoka wapi? Kwa nini alisimamisha uchunguzi wa vitu vilivyopotea mwaka jana. (uk. 44 – 45)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Kijiji Chetu*, 1975)

Nukuu hii inaonesha tofauti iliyopo kati ya msimamo wa wanakijiji walio wengi na viongozi wao. Uamuzi na msimamo wa kijiji ni kuwa mtu asiyeishi kijijini hapaswi kuhesabika kuwa mwanakijiji. Kinyume chake, viongozi wanakiuka maamuzi na

msimamo wa kijiji na kuwatambua watu wenye fedha wanaoishi mjini na kuwapa haki ya kugawiwa mavuno katika mazingira yasiyo na uwazi. Tatizo hili limewasilishwa na mwandishi kupitia MTU I anayesema, “Tatizo letu hapa ni mfarakano wetu wenyewe. Maazimio tunayopitisha kwa pamoja mara nyingi yameishia midomoni na kusahuliwa mara baada ya kutoka mikutanoni. Mara ngapi tumesema wasioishi kijijini siyo wanakijiji? Lakini badala yake viongozi wetu wanakubali hongo na kuwapokea watu hao kama wanakijiji kwa fedha.” Ni kweli fedha inahitajika katika maisha, lakini fedha hiyo inapaswa ifuate utaratibu ulioridhiwa kwa pamoja baina ya pande zote zinazohitaji fedha husika kwa faida ya pamoja, na siyo kwa faida ya wachache. Kinachotokea hapa ni ubaguzi na kiburi cha wenye fedha kutumia fedha yao kuwakamata viongozi kwa njia haramu kupindisha uamuzi na msimamo wa kijiji. Matokeo yake, kunaibuka chuki, malumbano, matabaka na ubaguzi wa kipato miongoni mwa wananchi wajenga ujamaa.

Vilevile, utafiti umebaini kuwa, rushwa imepofusha na kusambaratisha maisha ya pamoja yenye furaha na amani miongoni mwa wanajamii. Badala yake, rushwa imejenga matabaka na ubaguzi miongoni mwa wanajamii wa jamii moja. Kumbe basi, hata awamu ya Azimio la Arusha ubaguzi wa kipato na tabaka la wenye nacho na wasiokuwa nacho liliendelea kuishi. Hivyo, kuufanya ujamaa kuonekana ni wimbo wa vitabuni. Tafsiri na utekelezwaji wa sera za Azimio la Arusha kumegeuka ukoma kwa maendeleo na ustawi chanya na wa kasi wa jamii nzima. Kwa sababu viongozi wameshindwa kuhawilisha maarifa, stadi na tafiti zilizoweza jamii za kale kuishi kwa umoja, upendo na ushirikiano. Matokeo yake, viongozi wa zama hizi wanaamua kuja na mifumo isiyo shirikishi wala rafiki huku wakiruhusu ombwe la

kimawasiliano, kitathmini na kiuongozi kutawala utekelezaji wa mifumo na sera hizo mpya. Tunayapata haya kupitia kauli ya Mzee I. Tazama nukuu ifuatayo: -

**MZEE I:** Ujamaa mpya mwingi ni wa kwenye kitabu. Na hatari yake ni kama hii. (*Akionyesha mdomo*). Maneno mengi na mikutano kila siku bila vitendo. Kufika hapa na kujirundika pamoja twadhani tunaishi kijamaa. Ingawa babu zetu hawakujirundika kama sisi walikuwa wakiishi kijamaa kuliko sisi. Ujamaa ulikuwa ni maisha yao. Kulikuwa hakuna shamba la ushirika kama yetu hapa. Kila mtu alikuwa na lake lakini lilikuwa likilimwa na kijiji, siyo mtu mmoja. Ushirikiano uliendelea mpaka kwenye ulinzi. Mtu mmoja akipiga mbinja ya kutaka msaada wote hutoka kusaidia [...]

[...] Usirukie kitu kabla hujasikia mwisho wake. Ndiyo maana nawaambieni mna kitabu tu mbele yenu, lakini mawazo yenu si ya kijamaa. Watu wote siyo sawa ingawa binadamu wote ni sawa [...]. Kosa kubwa katika kuanzisha kijiji chetu na ndiyo ukweli katika vijiji vingi ni kuwa tunaishi maisha ya upande mmoja. Hatuishi ubinadamu wote. Viongozi wetu wanatufanya tuishi maisha ya kijamaa na wanaona upande mmoja zaidi nao ni wa siasa... (uk. 16, 18, 46)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Kijiji Chetu*, 1975)

Nukuu hii imebeba mawaidha ya Mzee I. Kupitia data tuliyonukuu ni wazi kwamba, chanzo cha umasikini na ufisadi katika jamii iliyodumaa kimaendeleo na kiustawi ni kuwapo kwa ombwe la uongozi bora, mfumo bora wa upatikanaji viongozi, mawasiliano bora, na wananchi wanaojitambua kifikra. Kwa sababu, viongozi walio wengi hawana sifa za kuwa viongozi bora na sahihi kwa wananchi wanaowaongoza.

Viongozi wengi na aina ya siasa inayotawala mfumo wa maisha ya nchi na taifa umeshindwa kuzingatia mifumo asili iliyoongoza jamii kwa faida na maslahi mapana ya jamii nzima.

Katika hili mwandishi anasema, “Ndiyo maana nawaambieni mna kitabu tu mbele yenu, lakini mawazo yenu si ya kijamaa. Watu wote siyo sawa ingawa binadamu wote ni sawa [...]. Kosa kubwa katika kuanzisha kijiji chetu na ndiyo ukweli katika vijiji vingi ni kuwa tunaishi maisha ya upande mmoja. Hatuishi ubinadamu wote. Viongozi wetu wanatufanya tuishi maisha ya kijamaa na wanaona upande mmoja zaidi nao ni wa siasa...” kupitia nukuu hii, tunabaini kuwa na viongozi wasiojua kwa kina aina ya mfumo rafiki unaoweza kuwapa uhakika wa kuishi wananchi na taifa. Inavyoonekana kwa sasa, kila ngazi ya mamlaka na uongozi imejaa watendaji ambao hawana ufuatiliaji. Pia, hakuna mawasiliano sahihi wala haja ya kumsaidia mwananchi mnyonge na taifa zima kujikomboa kutoka katika minyororo na kani za umasikini, maradhi, ujinga wa kila namna. Taifa lenye viongozi wa namna hii, haliwezi kupiga hatua chanya na endelevu katika kutafuta suluhisho la changamoto zinazomkabili mtu mnyonge (Hancock, 1991; Chachage, 2014).

Utunzi wa tamthilia ya *Kijiji Chetu* unaonekana kufungamana kidhamira na madhumuni ya TANU. Madhumuni ya TANU kama tunavyoyanukuu hivi punde, mbali na changamoto za utekelezekaji wake machoni pa mfumo wa kibepari na kiliberali, yalikusudia viongozi wa chama na serikali kwa kushirikiana na wananchi kubeba wajibu ufuatao: -

- (a) Kuudumisha uhuru wa nchi yetu na raia wake;
- (b) Kuweka heshima ya mwanadamu kwa kufuata barabara kanuni za Tangazo la Ulimwengu la Haki za Binadamu;
- (c) Kuhakikisha kwamba nchi yetu inatawaliwa na Serikali ya watu ya kidemokrasia na ya kisoshalisti;
- (d) Kushirikiana na vyama vyote vya siasa katika Afrika vinavyopigania uhuru wa bara lote la Afrika;
- (e) Kuona kwamba Serikali inatumia mali yote ya nchi yetu kwa kuondoshea umaskini; ujinga na maradhi;
- (f) Kuona kwamba Serikali inasaidia kwa vitendo kuunda na kudumisha vyama vya ushirika;
- (g) Kuona kwamba kila iwezekanapo Serikali inashiriki hasa katika maendeleo ya uchumi wa nchi yetu;
- (h) Kuona kwamba Serikali inatoa nafasi zilizo sawa kwa wote, wake kwa waume, bila kujali rangi, kabila, dini au hali;
- (i) Kuona kwamba Serikali inaondoa kila namna ya dhuluma, vitisho, ubaguzi, rushwa na upotofu;
- (j) Kuona kwamba Serikali ya nchi yetu inasimamia barabara njia kuu za kuzalisha mali na inafuata siasa ambayo itarahisisha njia ya kumiliki kwa jumla mali za nchi yetu;
- (k) Kuona kwamba Serikali inashirikiana na dola nyingine katika Afrika katika kuleta Umoja wa Afrika;
- (l) Kuona kwamba Serikali inajitahidi kuleta amani na salama ulimwenguni kwa njia ya Chama cha Umoja wa Mataifa (TANU, 1967; uk. 2 - 4).

Tunapoyatafakari kwa makini madhumuni haya ya TANU, tunaona kuwa dira ya siasa ya ujamaa ililenga kuhakikisha jamii inaishi chini ya misingi minne (4) ambayo ni: - (a) kutokuwapo kwa unyonyaji, (b) njia kuu za uchumi kuwa chini ya wakulima

na wafanyakazi, (c) kuwapo kwa demokrasia, na (d) ujamaa ni imani (TANU, 1967). Aidha, mwongozo huu wa TANU unaonesha kuliwekwa masharti ya kuisaidia jamii kuhakikisha wanapata maendeleo. Masharti hayo yalikuwa ni kila kiongozi na mwananchi kutenda kwa: - (a) juhudi, na (b) maarifa. Sehemu ya mwongozo huo inasomeka hivi, “Tangu sasa tutasimama wima na kutembea kwa miguu yetu badala ya kupinduka na kuwa miguu juu vichwa chini. Viwanda vitakuja, na fedha zitakuja, lakini msingi wake ni WANANCHI na JUHUDI yao na hasa katika KILIMO. Hii ndiyo maana ya kujitegemea. Kwa hiyo basi, mkazo wetu na uwe: - (a) Ardhi na Kilimo (b) Wananchi (c) Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea, na (d) Uongozi bora” (TANU, 1967; uk. 28). Haya yote yalipewa nguvu ya ufafanuzi juu ya maendeleo kwa kujitegemea katika vichocheo vikuu vinne (4). Vichocheo hivyo ni: - (a) ardhi (b) watu (c) siasa safi, na (d) uongozi bora (uk. 28 – 31).

Nukuu zote hizi pamoja na zile zilizonukuliwa kutoka tamthilia ya *Kijiji Chetu* zinaonesha kubeba ubunifu katika uteuzi na ujenzi wa dhamira zinazohusiana na athari ya viongozi wa chini kuwasaliti wananchi kwa kutokusimamia maamuzi yanayopitishwa katika vikao halali vya maamuzi. Badala yake viongozi wa ngazi za chini wamegeuka vibaraka wa mabwanyenye na mabepari uchwara katika taifa na nchi. Viongozi wa aina hii katika jamii huwa ni vinara wa dhuluma, unyonyaji, rushwa, ufisadi, matabaka, ubaguzi, chuki, uonevu, visasi na hujuma dhidi ya mwananchi hohehahe. Kumbe tunagundua kwamba, dhamira za tamthilia hii ya *Kijiji Chetu* zinawatazama zaidi viongozi wa serikali za mitaa katika kutafsiri na kusimamia amali za jamii wakati katika tamthilia ya *Mashetani* mkito umewekwa



kwa viongozi waandamizi katika serikali kuu kuwa chanzo cha kila uozo katika jamii na taifa.

Kwa upande wa tamthilia ya *Harakati za Ukombozi*, yenyewe imejikita zaidi katika kujadili namna viongozi wengi - wakuu na waandamizi, katika ngazi za juu za maamuzi za chama na serikali kuu wanavyowasaliti wananchi. Wanawasaliti wananchi kwa kisingizio cha harakati za ujenzi wa nchi na taifa jipya lenye kuleta maendeleo, haki sawa na ustawi endelevu kwa wananchi wote. Kwa maneno mengine, waandishi wanaonesha ya kwamba, chanzo cha mabaya katika jamii ni viongozi na watendaji wakuu na waandamizi katika jamii. Hawa wamekuwa ni nyoka wenye vichwa viwili na ndimi mbili, kama inavyobainika kupitia data nukuliwa ifuatayo: -

**KIONGOZI 2:** [...]. Ndugu wananchi, Azimio letu haliishii katika matamko, linaendelea siku hadi siku kutekelezwa kwa matendo. Kazi bado tunayo kubwa, magugu bado yapo. Tena yapo mengi sana. Hata hapa nayaona. Hivyo bado tuna kazi kubwa. (*Anamuonyesha mwananchi mmoja kati ya wanaomsikiliza ambaye ni mnene.*) Hebu wewe hapo simama. Wewe hapo. (*Mwananchi anasimama*) Njoo hapa. (*Mwananchi anakuja mpaka alipo kiongozi. Kiongozi anamtazama tangu juu hadi chini*). Hivi wewe unakula nini? Unazo nyumba ngapi? Magari? Unayo mashamba mangapi? Hii suti inakupendeza, umeitoa wapi? Unazo ngapi? (*Mwananchi ameshangaa tu, hajibu*). Wananchi hebu mtazameni mtu huyu mtazameni!

Huyu mtu ni mmoja wa mifano mizuri ya wale wanaotunyonya. Angalieni wanavyofutuka na kumea

vinundu. Hii yote kwa sababu ya kutunyonya sisi. Ndugu wananchi, tutanyonywa namna hii kwa muda gani? Hawa ndiyo wanatunyonya! Haya ndiyo makupe! Ndiyo mabomba hasa! Haya rudi...

*(Kiongozi 2 anaondoka huku akiwapungia wananchi. Kiongozi 2 anafika kwenye bar. Anawakuta Mkurugenzi na Meneja wanakunywa pombe). (uk. 17)*

**(Chanzo: Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Harakati za Ukombozi*, 1982)**

Ukichunguza nukuu hii, utaona hotuba ya Kiongozi 2 inaonesha kauli thabiti ya mwimba ujamaa lakini wakati huo huo anaonekana kupingana na ujamaa kwa kutokujali utu wa mtu, tofauti za kimaumbile na hali za watu katika jamii. Kiongozi anajaribu kuwaaminisha wananchi kwamba adui wa ujamaa anaweza kuonekana kwa umbile la mwili wake. Hapa ni dhahiri kwamba kiongozi huyu anatumia udhaifu wa ujuzi, utambuzi na maumbile ya wananchi walio wengi kuwabagua na kuwachonganisha wananchi ili wafarakane na kushindwa kuwa wamoja katika kuujenga ujamaa. Kiongozi 2 ni mfano wa viongozi wanafiki, wachonganishi, waliojaa ghiribu, fitina, uzushi, na dharau kwa wananchi wanaowaongoza ilhali viongozi hao wakijinufaisha na kujilimbikizia mali. Mfano mzuri wa ghiribu za kiongozi huyu zinajionesha kupitia matendo na kauli zifuatazo: -

**MKURUGENZI:** Karibu bwana.

**KIONGOZI 2:** Habari za kutangulia?

**MKURUGENZI:** Mzuri sana. Vipi mbona umechelewa?

**KIONGOZI 2:** *(Anakaa)*. Ah! Nilikuwa kwenye shughuli za Chama, halafu nikapitia kwenye miradi yangu kuangalia isianguke. *(Wote wanacheka)*.

- MENEJA:** Unajua bwana kiwanda changu kimechukuliwa?
- MKURUGENZI:** Ala! Tayari?
- MENEJA:** Hasa. Lakini mwenzenu Azimio hili linaniumiza kichwa. (*Wanacheka*).
- KIONGOZI 2:** .... Kwani Bwana Meneja una nyumba ngapi?
- MENEJA:** Nina nyumba nne.
- KIONGOZI 1:** Nne tu?
- MENEJA:** Nne.
- KIONGOZI 2:** Aa! Mimi nilidhani una nyumba nyingi sana kumbe nne tu. Mbona mimi ninazo kumi (*anacheka*) na sina tatizo.
- MKURUGENZI:** Kwani ndugu Meneja huna watoto wowote?
- MENEJA:** Nina watoto wanne. Huyu wa nne kazaliwa juzi tu, hata siku kumi hajafikisha.
- MKURUGENZI:** Sasa kumbe una shida gani. Wagawie hao watoto hizo nyumba.
- KIONGOZI 1:** Eee! Kila mtoto mpe nyumba moja.
- MENEJA:** Eti kweli. Kwa nini sikufikiria jambo hili. (uk. 18 – 19)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Harakati za Ukombozi*, 1982)

Data hii juu ya majadiliano kati ya Kiongozi 1, Kiongozi 2, Mkurugenzi na Meneja inathibitisha unafiki, usaliti, dhuluma na unyonyaji wa viongozi kwa wananchi wao. Mbaya zaidi, viongozi wanaonekana kuwafundisha uovu watendaji wanaoonekana kujaribu kutii na kulitekeleza Azimio la Arusha. Kumbe basi, kufa kwa Azimio la Arusha kulitokana na viongozi wengi, wakuu na waandamizi katika chama na serikali ambao walishiriki vikao vya kuzaliwa kwa azimio hilo kusaliti kwa

makusudi maazimio ya vikao halali na utekelezwaji wa azimio kwa maslahi binafsi. Kitendo cha viongozi kutenda kinyume na utu na usawa wa mtu ni kukanyaga hata imani ya TANU inayosema: -

- (a) Kwamba binadamu wote ni sawa;
- (b) Kwamba kila mtu anastahili heshima;
- (c) Kwamba kila raia ni sehemu ya Taifa na anayo haki ya kushiriki sawa na wengine katika Serikali tangu ya Mitaa, ya Mikoa hadi Serikali Kuu;
- (d) Kwamba kila raia anayo haki ya uhuru wa kutoa mawazo yake, ya kwenda anakotaka, wa kuamini dini anayotaka na wa kukutana na watu mradi havunji Sheria;
- (e) Kwamba kila mtu anayo haki ya kupata kutoka katika jamii hifadhi ya maisha yake na ya mali yake aliyonayo kwa mujibu wa Sheria;
- (f) Kwamba kila mtu anayo haki ya kupata malipo ya haki kutokana na kazi yake
- (g) Kwamba raia wote kwa pamoja wanamiliki utajiri wa asili wanamiliki utajiri wa asili wa nchi hii ukiwa kama dhamana kwa vizazi vyao;
- (h) Kwamba ili kuhakikisha kuwa uchumi wa nchi unakwenda sawa Serikali lazima iwe na mamlaka kamili juu ya njia muhimu za kuukuza uchumi; na
- (i) Kwamba ni wajibu wa Serikali, ambayo ni watu wenyewe, kuingilia kati kwa vitendo maisha ya uchumi ya Taifa ili kuhakikisha usitawi wa raia wote na kuzuia mtu kumnyonya mtu mwingine au kikundi kimoja kunyonya kikundi kingine na kuzuia limbikizo la utajiri kufikia kiasi ambacho hakipatani na siasa ya watu wote kuwa sawa. (TANU, 1967; uk.1-2)

Nukuu hii juu ya imani ya TANU tunapoilinganisha na matendo ya viongozi wa chama na serikali kupitia nukuu tulizozinukuu, tunabaini pasipo shaka kwamba Azimio la Arusha na siasa ya ujamaa na kujitegemea vilikuwa ni vitu dhahania miongoni mwa viongozi wengi. Usaliti na uzandiki huu ni ishara kwamba, viongozi wengi hawakuwa sehemu ya Azimio la Arusha (Mwiru, 2013). Ndiyo maana viongozi wengi waliishia kuliimba azimio katika majukwaa ya kisiasa huku wakitenda kinyume na matamko yao. Usaliti huo ulikuwa ni kinyume na msisitizo wa mwongozo wenyewe wa TANU unaosema, “utimizaji wa shabaha hizo na nyinginezo zinazofuatana na siasa ya ujamaa unategemea sana viongozi kwa sababu ujamaa ni imani na ni vigumu kwa viongozi kujenga siasa ya ujamaa ikiwa hawaikubali imani hiyo” (TANU, 1967; uk. 8). Kupitia imani ya TANU na msisitizo wake tulionukuu, tunasema pasipo shaka kuwa, tamthilia hii ya *Harakati za Ukombozi* sawa na ile ya *Kijiji Chetu* zimetazama na kujadili athari ya chama kushika hatamu katika kila uga wa maisha na maendeleo wakati wengi wa viongozi wanaotokana na chama siyo wasafi. Nukuu zote tulizozirejelea zinatufungia katika uozo wa viongozi wa chama na serikali, na athari ya matokeo yake kwa umma.

Kwa ujumla, tunagundua kwamba, tamthilia za awamu ya Azimio la Arusha zilikuwa zikiwalenga wanyonge na viongozi watendaji katika chama na serikali. Dhamira za tamthilia ya *Mashetani* zimekita katika kuwatathmini viongozi waandamizi katika serikali kuu kuwa chanzo kikuu cha kila uozo katika jamii na taifa. Nayo tamthilia ya *Kijiji Chetu* inawatazama zaidi viongozi wa serikali za mitaa kuwa chanzo cha kusambaratisha jamii na maendeleo yake kwa kutumia kutokuwapo kwa mfumo madhubuti na bora wa mawasiliano na ufuatiliaji wa maelekezo,

kutafsiri na kusimamia amali za jamii. Kwa upande wa tamthilia ya *Harakati za Ukombozi*, yenyewe imekita zaidi katika kuonesha namna viongozi wengi - wakuu na waandamizi, walivyojilimbikizia vyeo ndani ya serikali na chama ilhali si wazalendo. Hali iliyosababisha viongozi hawa kutumia vyeo hivyo kujinufaisha kinyume cha matamko yao mbele ya wananchi wanyonge.

Tamthilia ya *Safari ya Chinga* inajadili athari ya sera mbovu, sheria mbovu, usimamizi na mipango mibovu, mgawanyo mbovu na usimamizi mbovu na wa kibaguzi wa raslimali na huduma zinazotakiwa kuchochea ukuaji wa miji na watu kijamii, kisiasa, kiutamaduni na kiuchumi. Ubovu huo unaonekana kuendelea kulizamisha taifa kwa wengi kuendelea kuishi katika lindi la umasikini. Pia, tamthilia hii imeangazia kutokuwapo kwa haki na taarifa sahihi huku wachache wakinufaika kupitia jasho la wengi. Hali inayosababisha kuibuka kwa wimbi kubwa la wahamiaji haramu kutoka vijijini kwenda mijini kwa lengo la kutafuta maisha bora na sahihi. Nukuu ifuatayo inalibainisha wazo hili: -

**Joffu:** Nasikia huko njini barabara zote zina lami. Tofauti na huku kwetu tunalima korosho lakini bado kila kitu ni shida. Maji safi, umeme, barabara nzuri bado kwetu ni kitendawaili. Kazi ndo kama hivyo hakuna, kisomo hatuna. Basi maisha yamekuwa kama shubiri.

**Mata:** Mi naamini maisha ni popote tu. Ndugu utawapata mbele kwa mbele. Jirani yako, rafiki yako ndo ndugu zako. Hata nikiendelea kukaa hapa kijijini hakuna ntakachopata. Elimu ya darasa moja sina. Ndugu zangu pia hawana elimu. Kazi ya maana sina. Sasa nitakaa hapa kijijini tunaangaliana mpaka lini? Nami nahitaji kuwa na nji wangu. Na wazazi ndo wameshakuwa wazee. Nami ndo ntoto wao nkubwa.

**Bi. Somoe:** Ehe mara nyingi nkulima huwa hafaidiki sana. Si unaona korosho tunapata nazo tabu sana. Tunahangaika kufyekea na kupulizia dawa. Lakini ukija kuuza kilo shingi mia mbili. Eti korosho zetu hazina ubora. Mara soko la dunia limeshuka. Lakini wenzetu huko njini, kwenye kifuko kidogo tu korosho zinauzwa shingi elfu tano.

**Che Mundu:** Natamani siku moja ningepata nafasi ya kwenda huko soko la dunia! Nikawaeleze tabu tunazopata. Ndo mana watu wengine wanaamua kutokupalilia kabisa mikorosho yao. Bei duni na bado tunauza kwa nkopo na kulipwa kwa awamu. Pembejeo na madawa bei kubwa. Wakulima tutaendelea kweli?

**Mata:** (*Akilia na kupenga kamasi*). Mweshimiwa hakimu, naomba huruma yako. Kukaa kijijini kulima pia tumechoka. Nilikuja njini kutafuta kazi. Wazazi wangu kijijini wananitegemea. Sasa kibanda changu cha biashara kimevunjwa. Mali zangu zote zimepotea. Mweshimiwa hakimu, nyie wa juu tusaidieni. Sisi vijana wenu tunataabika. Hatuna kazi. (uk. 8, 9, 10, 12, 48)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Safari ya Chinga*, 2009)

Data iliyowasilishwa kupitia nukuu hii, inaonesha mazungumzo ambayo yanathibisha kiwango cha matumaini na vilio vya watu wanyonge ambao wametengwa na mifumo bora yenye kuleta haki, usawa na maendeleo. Mbaya zaidi, watu hawa wanaonekana kukosa hamasa ya kujikomboa kwani kila mbinu wanayoitumia haionekani kuwasaidia kuinuka kimaisha. Badala yake wamebakia kufanya majaribio yasiyo na tija kwao. Matokeo ya ubovu huu, mwandishi ameyaonesha kuwa ni pamoja na uhamiaji holela wa watu wengi kutoka vijijini kwenda mijini. Pia, ongezeko kubwa na la kasi la watu mijini lisiloendana na

maandalizi, mipango mkakati na utekelezaji wa miradi ya ukuzaji wa miji. Kama anavyosema mwandishi kupitia Mata, “Mweshimiwa hakimu, naomba huruma yako. Kukaa kijijini kulima pia tumechoka. Nilikuja njini kutafuta kazi. Wazazi wangu kijijini wananitegemea. Sasa kibanda changu cha biashara kimevunjwa. Mali zangu zote zimepotea. Mweshimiwa hakimu, nyie wa juu tusaidieni. Sisi vijana wenu tunataabika. Hatuna kazi.”

Kupitia nukuu hii, tunabaini kuwapo kwa tokeo jingine ambalo ni umasikini kuongezeka katika jamii ambazo zimetengwa. Pia, usaliti unaotendwa na watendaji wasomi waliosomeshwa kwa jasho la wanyonge. Matokeo mengine ni utunzi, usimamizi na tafsiri kavu za sheria, mauaji ya Albino, athari ya mkopo kwa wajasiriamali, usaliti katika mapenzi kati ya mwanamke na mwanaume na athari za UKIMWI / VVU. Mambo haya yapo katika jamii na yamekuwa yakipigiwa kelele mara kwa mara bila kupatiwa ufumbuzi wa kudumu na wa uhakika (Tanzania HIV Impact Survey, 2017; Tanzania Commission for AIDS, 2018; Wazambi na Mikongoti, 2018). Haya yote yanatokana na ugawaji usio sawa wa raslimali pamoja na utendaji usiozingatia weledi wala utashi wa kisiasa (Mukandala na Gasarasi, 2000).

Tamthilia ya *Changamoto* imejikita zaidi katika ukombozi na ujenzi wa jamii mpya na endelevu yenye kutoa haki sawa katika kila uga wa maisha ya mwanadamu kwa kuheshimu hali zote za maumbile ya wanajamii, hususani watu wenye ulemavu. Tamthilia hii imewatumia watu wenye ulemavu wa viungo kuwakilisha kundi kubwa la wanyonge ambao wamekuwa walemavu wa mwili na fikra. Mwandishi anawachora watu wenye ulemavu kama wananchi wanaonyanyapaliwa na mifumo ya



kiserikali na kibunge katika nyanja mbalimbali za maisha kwa msaada wa historia, na utamaduni wa Mwafrika. Aidha, mwandishi anaonesha haja ya kuwahimiza watu wenye ulemavu kuinuka na kupigania haki na fursa pasipo hofu. Badala ya kumeendelea kuwapo kwa manung'uniko huku wananchi wanaonekana kukubali kubaguliwa. Uthibitisho wa madai haya tunaupata kupitia mazungumzo yafuatayo kati ya Chaazye na Peti: -

**Malkia:** Ni furaha yangu kuwapo mahali hapa na kukutana nanyi. Leo ni siku ya mwaka mpya na nimeonelea ni jambo jema tuwe na utaratibu wa kukutana kila mwaka. Lengo la siku hii ni kutiana moyo na kutakiana heri katika mwaka mpya unaoanza na siku ya leo. (*Hadhira ambayo ni walemavu na wasio na ulemavu inapiga makofi na kushangilia*). Jambo la msingi ni kuwaomba msitumie upungufu wenu wa viungo kama kikwazo, hapana. Upungufu huo uwe ni changamoto ya kukuleteeni maendeleo. Hakuna haja ya kulilia mkono au mguu uliopotea. Bali ni kutumia viungo vilivyobakia katika kuchakarika ili kujitafutia riziki. (*Walemavu wanapiga makofi*). Kwa hayo machache, nawakaribisha sana kwenye hafla hii niliyowaandalieni ili tule, tunywe, na tufurahi. Asanteni. (*Anaondoka na kurudi mahali pake na anakaa. Watu wanapiga makofi sana na kushangilia*). (uk. 2 - 3)

**Chaazye:** Mnaelekea wapi dada zangu?

**Peti:** Tunaelekea mahakamani. Kuna wapumbavu tunakwenda kuwashitaki.

**Chaazye:** Naenda kumchukua Megno, tuko safari moja kwenda kwenye mashitaka! Tunataka watu watuthamini, hatutaki kunyanyaswa. (uk. 22-23)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Changamoto*, 2010)

Nukuu ya kwanza (uk. 2 - 3) imebeba tamko la kiongozi mkuu wa nchi (Malkia) ilhali nukuu ya pili (uk. 22 - 23) ni kauli za watu wenye ulemavu wa viungo – Chaazye na Peti. Tunapozichunguza nukuu hizi tunagundua ya kwamba, viongozi wengi wa kisiasa na kijamii ni mafundi wa kutoa matamko mbele ya kaumu ya watu ilhali hawana utashi wa dhati wa kusimamia, kufuatilia wala kutekeleza kwa vitendo yale yote wanayoyasema. Hapa tunaona jinsi Chaazye na Peti wanavyoanza harakati za kutafuta haki zao za msingi kwa kuridhia kwenda mahakamani kuwashitaki wanaowanyanyasa. Mwandishi kupitia Chaazye anasema, “Naenda kumchukua Megno, tuko safari moja kwenda kwenye mashitaka! Tunataka watu watuthamini, hatutaki kunyanyaswa.” Hapa mwandishi anaonesha namna mifumo mingine ya kisera – serikali na bunge inavyoshindwa kuwakomboa wanyonge kutoka katika lindi la mateso. Kwa hiyo njia pekee iliyobaki ni kupitia mfumo wa kimahakama kabla ya kutafuta njia nyingine nje ya serikali, bunge na mahakama. Hii inamaanisha kwamba, mifumo ya serikali na bunge imeshindwa kuwatetea wanyonge. Hivyo, tumaini pekee lililobaki ni kupata msaada wa kisheria ili jamii ishurutishwe kutii na kutenda haki sawa kwa kila binadamu pasipo kujali nafasi wala hali yake ya kimaumbile - kiutamaduni, kiuchumi, kijamii au kisiasa.

Ujumbe anaoutoa mwandishi ni kwamba, hakuna marefu yasiyo na ncha. Na, tena mapinduzi ya kweli hayaletwi kwa maneno bali vitendo vyenye dhamiri safi na ya dhati. Kwa mujibu wa Lynch na Roberts (2010), mateso ya watu wenye ulemavu ni zao la kihistoria na kitamaduni katika jamii nyingi za Kiafrika. Kwa hiyo, mchakato wa kuwapa haki na usawa watu wenye ulemavu ni vita endelevu kwa kujitoa mhanga, pia kuhusisha elimu na subira. Kwa hiyo, jamii inapaswa ijifunze kuona

kuwa si vyema kuwanyanyapaa watu wenye ulemavu. Mtazamo huu unampa nafasi nzuri mwandishi Elizabeth Mahenge kupaza sauti japo serikali na bunge vingali usingizini – kivitendo. Ndiyo maana mwandishi anaigeukia mahakama kwa kuitazama kama chombo pekee chenye msaada kwa watu wenye ulemavu. Na kwamba, mahakama haina budi kuonesha kwa vitendo thamani ya haki na utu pasipo kuchelewesha. Kwani haki iliyochelewa ni sawa na kutokuwapo kwa haki (SIKIKA, 2013a & 2013b; Nicolini, 2016; Wazambi na Mikongoti, 2018).

Nayo tamthilia ya *Nje – Ndani* imejadili suala la usaliti unaotendwa na watendaji wasomi waliosomeshwa kwa jasho la wanyonge. Lakini hushindwa kutetea wala kulinda hadhi na raslimali za taifa mbele ya mataifa ya kibeberu na mawakala wao. Matokeo yake, nchi inazidi kufilisiwa huku maisha ya wengi yakitawaliwa na unyonyaji, rushwa, ufidadi na umasikini wa kutupwa. Huku pengo la wenye nacho na wasiokuwa nacho likizidi kutanuka maradufu. Matokeo mengine ni: - taifa kujaa maumivu ya dhuluma, mauaji ya Albino, athari ya mkopo kwa wajasiriamali, usaliti katika mapenzi ya mwanamke na mwanaume. Mengine ni athari za UKIMWI / VVU, ubunifu kufa, ongezeko la utegemezi wa: - maamuzi, mifumo na mazao kutoka nje, kutaja kwa uchache. Haya yote yanasadifiwa kupitia nukuu ifuatayo: -

**Akili:** Bado haijatiwa kwenye mtaala wetu.

**Moyo:** Bado hadi leo? [*Anatabasamu*] Mnasubiri nini? Mnataka ushauri kutoka kwa wajomba zenu?

**Akili:** Wajomba gani tena hao? [*Anaonyesha kutoelewa kabisa*] Kwani tuna wajomba sisi?

**Moyo:** Si wa kule mlukoitoa lugha yenu ya elimu. Mnakokopa pesa na kuhifadhi nyingine, mnakokopa maarifa, mnakoazima hadi lugha ya kukuwakilisheni na kukusemeeni... Na unasemaje

basi kuhusu kuazima kucha, nywele, rangi, kope, makalio, vyote kutoka huko huko? .... Umesahau, hata madodoki, vijiti vya kutogea mishikaki. [*Anacheka kinafiki*] Hata ukitaka kuwasha mkaa wako, viwashio umeletewa, yaani mnapendwa ninyi ila hamjui tu. (uk. 18, 19, 22)

**Akili:** Umejuwaje mambo haya yote? [*Anakaa chini kwa kujitupa kwa kuchoka*] Unajua tusingewaona Wazungu mara kwa mara tungewaita Mungu. (uk. 23)

**Moyo:** Hata hivyo, viazi vyenyewe si vingi kwa wote. Sisi wengine faida tuiapatayo ni mashimo kwa ajili ya kujengea vyoo vyetu baada ya viazi kuchimbwa.

**Macho:** Hata kule nilikotoka hakuna tofauti kubwa na hapa.

**Akili:** Kama twiga na faru.

**Akili:** Haya ndovu na pembe zao

**Moyo:** Wamefanyaje?

**Akili:** Wanapaa. (uk. 72 - 74)

**Akili:** Afadhali mashimo, hawa si mkia, si ngozi, si kwato.

**Moyo:** Ubeberu.

**Akili:** Ubeberu wa mbuzi au kondoo?

**Moyo:** Si mbuzi wala kondoo. Ni makuwadi wa soko holela. Hula njama na wanyonyaji. Sasa ili uwalinde basi wahitajika kuwa watu. (uk. 75)

**(Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Nje - Ndani*, 2016)

Nukuu hii inaonesha tatizo kubwa linaloyakabili mataifa yaliyotawaliwa na mataifa ya kibepari. Mataifa yaliyotawaliwa yanaonekana kutokuwa na ujasiri wala uwezo wa kufikiri, kupanga, kuamua na kutekeleza mambo yenye tija kwa watu wao. Badala yake, mataifa haya yamebaki kungoja mipango na miradi inayoletwa na mataifa yaliyowatawala. Kwa kiasi kikubwa, mipango na miradi hiyo hushindwa

kutoa tija endelevu kwa ukombozi wa kweli kwa mzawa katika nyanja zote za maisha. Kwani wasimamizi wengi wanaonekana kuwa vibaraka wa wanyonyaji na wadhulumati. Mwandishi anasema, “Si mbuzi wala kondoo. Ni makuwadi wa soko holela. Hula njama na wanyonyaji. Sasa ili uwalinde basi wahitajika kuwa watu.” Nukuu hii inathibitisha namna wazawa baadhi wanavyotumika katika kuua hatima ya taifa na nchi kisa kukumbatia maslahi binafsi. Nchi na taifa lenye mfumo wa uongozi uliojaa vibaraka wa wanyonyaji hufanya mali asili za taifa zizidi kuchotwa kana kwamba nchi haina viongozi, wananchi wala vikosi vya ulinzi na usalama wa nchi na taifa (Rodney, 1972; Chachage, 2014; *Raia Mwema*, 2012).

Kwa jumla, kutokana na data mbalimbali tulizoziwasilisha kupitia nukuu, matokeo ya utafiti yamebaini kuwapo kwa changamoto ya ufasidi na udhulumati inayoonekana kuwa ni donda sugu lililokita mizizi katika mfumo mzima wa maisha ya watu wengi hasa wasomi na matajiri ambao wameathiriwa na elementi za ukoloni na ukoloni mamboleo. Utafiti wetu umegundua kuwa, waandishi wanaonesha kwamba, jambo hili ni hatari kwa ustawi na maendeleo endelevu ya jamii zinazotarajia maendeleo ya kweli kupitia viongozi wasomi na matajiri ambao ni zao la ubepari wa Kimagharibi. Kwa hiyo, uwezekano wa kulisambaratisha kabisa kundi hili ni mgumu sawa na kusambaratisha misingi ya mji wa Vatikani au Roma (Eagleton, 2008).

Vilevile, kutokana na data mbalimbali tulizoziwasilisha kupitia nukuu, utafiti umebaini kuwa, tofauti nyingine ya kidhamira ni baadhi ya dhamira kuendana na wakati na uzito wa jambo husika katika muktadha husika. Mathalani, mtafiti amegundua kuwapo kwa mjadala kuhusu UKIMWI / VVU katika tamthilia za *Safari*

ya *Chinga* na *Nje – Ndani*. Pia, mauaji ya Albino katika tamthilia za *Changamoto* na *Nje – Ndani*. Na, hofu ya ubakaji katika tamthilia ya *Changamoto*. Vilevile, dharau, unyanyapaaji wa watu wenye ulemavu na utumiaji ulemavu kama chanzo cha kujipatia kipato katika tamthilia za *Safari ya Chinga, Changamoto* na *Nje – Ndani*. Aidha, athari za ndoa za mitala na ndoa za utotoni zimebainika katika tamthilia za *Safari ya Chinga, Changamoto* na *Nje – Ndani*. Na athari za ukoloni mamboleo na utandawazi kwa nchi za ulimwengu wa tatu katika tamthilia za *Safari ya Chinga, Changamoto* na *Nje – Ndani*.

Pia, kutokana na data mbalimbali tulizoziwasilisha kupitia nukuu, matokeo ya utafiti wetu yanaonesha kuwa, dhamira hizi hazijitokezi katika tamthilia teule za awamu ya Azimio la Arusha ambazo kwa sehemu kubwa zimejikita katika kutathmini njozi ya tumaini jipya baada ya mkoloni kuondoka. Sababu kubwa ya dhamira hizi kujitokeza katika awamu ya soko huria ni pamoja na kuibuka kwa vuguvugu la vyama na majukwaa kinzani ya kijamii na kisiasa. Mengi ya majukwaa haya yana mrengo wa kiliberali ambayo kwa sehemu kubwa yameongeza kiwango cha ufadhili kwa asasi na taasisi za kijamii na kisiasa. Huku yakitumia fursa ya ukoloni mamboleo kutetea maslahi na tamaduni “mpya” dhidi ya makundi yaliyonyimwa fursa ya kuwa huru na kupata haki sawa katika mifumo na nyanja za maisha ndani ya jamii zao za asili (Thuranira, 2017).

Aidha, kutokana na data mbalimbali tulizoziwasilisha kupitia nukuu, utafiti huu umebaini suala la UKIMWI / VVU ni ajenda inayotokana na kuibuka kwa ugonjwa tishio kwa dunia katika miaka ya 1980 hivyo isingekuwa rahisi ugonjwa huu kuukuta katika kazi bunilizi za miaka ya kabla 1980 (Mutembei, 2009; Nicolini, 2016).

Vilevile, kwa jamii nyingi za Kiafrika, zamani ilikuwa ni vigumu kuyatamka hadharani mambo yanayohusu faragha (Lynch na Roberts, 2010). Hata kampeni za afya hazikupewa hamasa wala nafasi kubwa kama ilivyo kwa sasa. Kwa hiyo, hata waandishi wengi wa zama hizo wasingeweza kuthubutu kuyajadili hadharani magonjwa yanayotokana na ngono. Kwa sababu mambo ya faraghani, kwa tamaduni za jamii nyingi za Kiafrika yalikuwa hayasemwi hadharani - kwa kila mtu au popote pale (Ofisi ya Waziri Mkuu, 2018).

Faukwa ya hayo, kutokana na data mbalimbali tulizoziwasilisha kupitia nukuu, utafiti wetu umebaini tofauti nyingine ambayo ni kwamba tamthilia teule za awamu ya Azimio la Arusha – *Mashetani*, *Kijiji Chetu* na *Harakati za Ukombozi* zimeiweka siasa kuwa kiini cha mjadala na tathmini. Kila jambo limeumbwa na kuhusishwa na siasa kama kitovu cha kukosekana kwa maendeleo na ustawi wa jamii nzima katika nyanja zote za maisha. Wakati huo, tamthilia teule za awamu ya soko huria zimekita mjadala na tathmini yake katika utendaji wa viongozi na sosholojia ya utandawazi wa ukoloni mamboleo kama kiini cha kukosekana kwa maendeleo na ustawi wa jamii nzima katika nyanja zote za maisha ya watu waishio katika nchi masikini. Ndiyo maana tamthilia zote tatu (3) za awamu ya Azimio la Arusha zinaonekana wazi kabisa kurusha mikuki kwa viongozi wakuu na waandamizi wa chama na serikali. Tamthilia teule za awamu ya soko huria zinaonekana wazi kabisa kurusha makombora kwa watendaji wasomi wa serikali na wananchi wenyewe huku zikikwepa kuwahukumu moja kwa moja wanasiasa na viongozi wakuu.

Zaidi ya hayo, kutokana na data mbalimbali tulizoziwasilisha kupitia nukuu, utafiti wetu umebaini kwamba, hali ya waandishi wapya kuwakwepa wanasiasa kama

ilivyokuwa wakati wa vuguvugu la ukombozi ni jambo la kimazingira na kisanaa. Kwa kazi ambazo hazijatumia lugha ya mficho kwa wingi, kama tulivyobaini katika tamthilia ya *Safari ya Chinga* siyo rahisi kuligusa tabaka tawala kwa dhamira na lugha inayoliudhi tabaka hili moja kwa moja. Haya yanatokea kwa sababu tabaka hili lina nguvu ya kudhibiti na kuhodhi uhuru wa kile kinachotakiwa kutendwa na kunenwa na mwandishi anayeiwaza kesho yake (Soyinka, 1979; Maake, 2006; Ruhumbika, 2006; Jilala, 2012). Bila shaka, hii ndiyo sababu inayozifanya tamthilia teule za awamu ya Azimio la Arusha kutumia ama lugha ngumu (au lugha ya kawaida bila kuliumiza tabaka hili) ili kukwepa mkono wa dola. Huku zile za awamu ya soko huria zikitumia lugha hiyo hiyo kuwajadili wanasiasa na viongozi wa ngazi za kati na chini badala ya wale wa tabaka la juu – moja kwa moja.

Tofauti nyingine ya kidhamira iliyobainika katika utafiti wetu ni ile ya waandishi wa tamthilia teule za awamu ya Azimio la Arusha kuwa na ujasiri wa kuwanyooshea kidole wanasiasa wazawa kuwa ndiyo chanzo cha matatizo endelevu yanayowakabili wananchi walio wengi. Wakati waandishi wa tamthilia teule za awamu ya soko huria wanaonekana kukosa ujasiri wa kuwakabili wanasiasa. Badala yake wanaita jamii nzima, hasa jamii ya wasomi kama kitovu cha chanzo cha matatizo endelevu yanayowakabili wananchi walio wengi kwani wameonekana kukwamisha matamko na malengo ya viongozi waandamizi wa kisiasa yenye tija kwa taifa.

Kama tulivyoeleza awali kutokana na data mbalimbali tulizoziwasilisha kupitia nukuu, utafiti umebaini kuwa pia msingi mkuu wa utofauti wa dhamira unatokana na matukio yanayojitokeza na kutawala nyakati mahususi za maisha ya vizazi vya mwanadamu. Kwani wakati na mazingira yaliyomlea mwandishi huchangia sana



mwandishi mmoja au tofauti tofauti kuandika jambo lile lile kwa namna ama ile ile au tofauti (Soyinka, 1979; Culpeper na wenzake, 1998; Maake, 2006; Ruhumbika, 2006; Adeseke, 2016; Senyamanza, h. m.) Soyinka (1979), Ruhumbika (2006) na Jilala (2012) wanaongeza kuwa, mifumo ya kiutawala ina mchango mkubwa katika kumfanya mwandishi kuwa huru au mtumwa katika kubuni na kuwasilisha wazo lake kwa namna anayoona inafaa. Kwa muktadha huu, njia ya uwasilishaji wa dhamira kati ya mwandishi mmoja na mwingine, au mwandishi yuleyule mmoja katika kazi zake kadhaa ndiyo huleta utofauti kiubunifu. Kwani wakati, mazingira na mifumo ya kiutawala ndani ya jamii anamoishi mwandishi huamua hatima ya mwandishi kisanaa.

Mjadala huu unaungwa mkono na Wanafasihi Linganishi wa mlengo wa Kifaransa na zaidi sana wale wa Kimarekani. Kwa Guyard (katika Cao, 2013), ulinganishaji wa fasihi za jamii moja au tofauti tofauti unapofungamanishwa na historia ya jamii kupitia mahusiano ya fasihi kitaifa na kimataifa huibua kufanana na kutofautiana. Kwa sababu jamii zinazohusiana huwa na tabia ya kuathiriana moja kwa moja au kwa kiasi katika nyanja mbalimbali za maisha. Kuathiriana huko kunaweza kuwa kwa kufanana au kutofautiana (Cao, 2013). Hali hii hutokana na tofauti au mfanano wa mawasiliano ya dhati yanayohusisha pande mbili za sanaa au zaidi. Mawasiliano hayo ni kati ya kazi na kazi, pia misukumo na maisha ya waandishi wa fasihi kadhaa ndani na nje ya mipaka ya fasihi hizo ndani ya wakati na mazingira mahususi (Carrer, katika Cao, 2013). Mambo haya yote yanapomsonga mwandishi, humfanya mwandishi husika achague mwelekeo wa mwono wa sanaa yake kiubunifu – ama kwa kujua au kwa kutokujua. Hatimaye, mwandishi huyo hutoa kazi inayofanana au

kutofautiana na waandishi wengine au kazi zake nyingine - ama kwa karibu au kwa mbali (Cao, 2013).

Kwa mantiki hii basi, matumizi ya nadharia ya Fasihi Linganishi yametusaia sana katika kubaini kwa vipi, ya nini, kwa nini, lini na wapi dhamira za tamthilia zote sita (6) teule zinafanana, kutofautiana na kuhusiana. Tamthilia zote sita (6) teule zimebainika kujadili dhamira zinazofanana ambazo ni mwendelezo wa kilio cha watu wanyonge katika jamii. Dhamira hizo ni zile zinazojikita zaidi katika kutambua na kutathmini mateso ya mtu mnyonge kiuchumi, kijamii, kisiasa, kiutamaduni na kiteknolojia. Baadhi ya mambo hayo ni ubaguzi, matabaka, dhuluma, chuki, unyonyaji na umasikini. Dhamira nyingine ni maradhi, ujinga, mifumo dhaifu ya ulinzi na usalama, hofu na woga wa wananchi kwa viongozi miunguwa, usaliti, rushwa, ufisadi, imani potofu, dharau, mila potofu, changamoto katika ndoa na mapenzi, ombwe la uongozi, na ukoloni mamboleo.

Aidha, utafiti umebaini kuwapo kwa utofauti wa kidhamira unaotokana na matukio na msisitizo unaojitokeza katika nyakati mahususi za maisha ya vizazi tofauti tofauti vya mwanadamu. Hata hivyo, tamthilia teule za awamu ya Azimio la Arusha zimekita zaidi katika athari za siasa na ukoloni kwa taifa. Tamthilia hizi zinawalaumu viongozi na watendaji wa kisiasa kuwa kitovu cha umasikini na mateso yote ya mwanajamii mnyonge. Wakati, tamthilia za awamu ya soko huria zimejikita zaidi katika kujadili masuala ya kijamii. Zenyewe zinawalaumu watendaji wa serikali na wasomi kuwa kiini cha kukosekana kwa maendeleo na ustawi wa jamii nzima katika nyanja zote za maisha ya watu waishio katika nchi masikini.

#### **4.4 Hitimisho**

Sura hii imewasilisha matokeo ya utafiti juu ya ubunifu wa ujenzi wa dhamira katika tamthilia sita (6) teule. Kama asemavyo Mohamed (1990), “ubunaji ni hali inayompa msanii kuja na muundo au umbo fulani kutokana na hisi au mawazo fulani, umbo ambalo kwa namna fulani lina upya wa kimawazo na kimuundo au wa utumizi wa maneno au upya wa zana yoyote ile inayotumika kuundia au kubunia sanaa fulani” (katika Senkoro, 1995; uk. 85). Na kwamba, upya huo hautoki hewani tu. Bali hutokana na hali halisi ya mambo ambayo mtunzi ameyasoma mahali fulani, ameyasikia, ameyaishi, ameyahisi, ameyanusa, ameyaona na, au ameyaonja. Kutoka katika uzoefu huo, ndipo mtunzi kwa uweza aliokirimiwa na Mungu huanza “kuyafinyanga upya mambo hayo ili kuunda umbo la kisanaa” (katika Senkoro, 1995; uk. 85). Ndivyo ilivyodhihirika katika matokeo yetu ya utafiti. Matokeo yamethibitisha kuwapo kwa ubunifu endelevu miongoni mwa tamthilia zote sita (6) teule katika ubunaji na ujenzi wa dhamira. Kila tamthilia ina mfanano na tamthilia nyingine pamoja na upekee wake katika kuyawasilisha mambo yanayoigusa jamii. Sura inayofuata inawasilisha matokeo ya utafiti juu ya kufanana na kutofautiana kwa matumizi ya lugha katika tamthilia sita (6) teule.

## SURA YA TANO

### UBUNIFU KATIKA MATUMIZI YA LUGHA YA TAMTHILIA TEULE

#### 5.1 Utangulizi

Sura hii inahusu lengo la pili la utafiti huu kama lilivyobainishwa katika sura ya kwanza. Nalo ni kulinganisha ubunifu katika matumizi ya lugha yanayojitokeza katika tamthilia teule za Kiswahili za awamu ya Azimio la Arusha na zile za soko huria ili kubaini kama kuna ubunifu endelevu. Hivyo, sura inawasilisha, kuchambua na kujadili data na matokeo ya utafiti huu kuhusu ubunifu katika matumizi ya lugha. Kwa ujumla, sura hii inajibu swali la pili la utafiti wetu ambalo ni “Je, ubunifu katika matumizi ya lugha yanayojitokeza katika tamthilia teule za awamu ya Azimio la Arusha unafanana na kutofautiana vipi na ule wa tamthilia teule za Kiswahili za awamu ya soko huria?” Kupitia swali hili mtafiti alilenga kuzizamia tamthilia zote sita (6) teule ili kubaini kama kufanana na kutofautiana katika uteuzi na ujenzi wa matumizi ya lugha kunaonesha kuna maendeleo ya ubunifu katika utunzi wa tamthilia ama la. ubunifu endelevu katika kukua na kustawi kiutunzi kwa Tamthilia ya Kiswahili nchini Tanzania ama la.

Uchunguzi wetu uliongozwa na nadharia ya Fasihi Linganishi. Uwasilishaji wa matokeo umeongozwa na mkabala wa kiufafanuzi kwa kuhusisha maelezo, majedwali, nukuu na ufafanuzi mwingine kutoka vyanzo mbalimbali vya kihistoria. Vyanzo hivi vyote kwa pamoja vimetusaidia kupata majibu ya maswali: “kwa vipi? Ya nini? Kwa nini? Lini? na wapi?” ambayo ndiyo roho ya nadharia ya Fasihi Linganishi (Jilala, 2016).

## **5.2 Kufanana na Kutofautiana katika Ubunifu wa Matumizi ya Lugha katika Tamthilia Teule**

Matumizi ya lugha ni nyenzo muhimu sana katika uumbaji wa kazi bunilizi za kisanaa (Senyamanza, h. m.). Mbinu za kisanaa huhusisha lugha inayoumba wazo na kulifinyanga kiubunifu. Miongoni mwa lugha ya kisanaa ni ucheshi, misimu, uchanganyaji ndimi na ugumu au wepesi wa lugha. Matokeo ya utafiti yamewasilishwa kwa kuanza na ucheshi kisha misimu halafu uchanganyaji ndimi na tumemaliza na ugumu na wepesi wa lugha. Uwasilishaji umetumia maelezo, majedwali (pale ilipolazimu) na nukuu ili kuthibitisha ubunifu unaojitokeza katika kila tamthilia sita (6) teule.

### **5.2.1 Matumizi ya Ucheshi**

Kiutunzi, kila aina ya ucheshi huwa na maana yake na kusudio lake. Kwa hiyo, mwandishi huwa habahatishi katika kuamua, kuteua na kutumia lugha inayojitambulisha katika kazi yake kwa kiwango husika. Mathalani, kwa kurejelea aina za ucheshi na sababu za kuwako kwake, Wamitila (2008) anaeleza kuwa, ucheshi wa kibeuzi unatokana na ubinafsi wa mhusika mwenyewe kujikinai, kujidhihaki, kujitweza au kujiumiza kutokana na tendo, kauli, neno, tamko au mchoro wake. Mchoro huo humchokonoa yeye mwenyewe hadi akajikuta akicheka pasipo kutarajia. Kicheko hiki hutokea baada ya mhusika kutambua ya kwamba kauli au tendo alilolifanya ni la kijinga au kizembe. Kwani kiuhalisi asingeweza kulitamka au kulitenda kwa namna ile endapo angekuwa ametuliza akili na kutafakari kama mtu mwenye akili na utambuzi timamu kabla ya kuchukua uamuzi alioufanya.

Nao ucheshi wa kitanzia kwa mujibu wa Wamitila, hutokea pale ambapo tukio la kuhuzunisha hujengewa taswira ya mhusika kutenda jambo au kutamka neno kama mtu asiyejitambua wala kuchuja. Huku mhusika mwenyewe akiamini kwamba anachokifanya au kukisema ni sahihi na chenye kukubalika kiasi cha kumjengea heshima. Mhusika huyo huyatenda au kuyanena mambo bila kutambua wale wanaomtazama wanamshangaa na kumsikitikia. Na kwamba, matendo yake huwachochea watazamaji kumdharau na kuishia kumcheka au kusifu kwa ghiribu. Lakini ucheshi wa kimazungumzo kwa mujibu wa Wamitila, huzaliwa pale tu wahusika wa kifasihi wanapotumia dailojia yenye kauli zinazoamsha hisia za furaha, raha na vicheko katika muktadha mahususi.

Aidha, Wamitila (2008) anaendelea kufafanua kwamba, kuna ucheshi wa kimwingiliano. Huu hutokana na kazi ya kifasihi kuchopeka katika kazi yake usemi, mchoro, simulizi, vionjo, sanaa, wazo, tukio au fikira fulani ambayo msomaji ama msikilizaji au mtazamaji anatambua chanzo cha matini yaliyochopekwa. Kitendo hiki cha kuyang'amua matini chanzi humfanya ajione kuwa ni mtu makini, mwerevu na mjanja kumshinda au kuwa na hadhi sawa au zaidi ya mtunzi aliyeyatumia matini teule. Hivyo kuishia kucheka na kujihisi mwenye raha sana. Vilevile, kuna ucheshi zimbwe (au kibwege). Huu ni ucheshi unaowakutanisha wahusika wenye viwango tofauti vya uelewa, ustaarabu na stadi zinazotokana na ujuzi na maarifa ya kitaaluma.

Katika aina hii ya ucheshi, mhusika mmoja aghalabu mwenye mamlaka hutenda na kunena kwa usahihi na ustaarabu kutokana na weledi wa kitaaluma. Wakati mhusika wa pili hutenda na kunena kwa wasiwasi, hofu, mashaka, mkanganyiko, makosa na kuonekana kuwa mgeni wa mambo mengi kutokana na kutokuwa na tajiriba, ujuzi,

stadi na maarifa yanayoumbwa kupitia taaluma husika (Wamitila, 2008). Lengo la ucheshi wa namna hii ni kuchochea fikra, mawazo, uwazaji na tathmini ambayo ni ya kitaaluma. Kwa mantiki hii, tunagundua ya kwamba, kuna uhusiano mkubwa kati ya maudhui, wahusika, mandhari, muktadha, mazingira, wakati na aina ya ucheshi anaoutumia mwandishi.

Kwa mujibu wa Provine (1996), hakuna ucheshi unaotokea pasipo kuwapo kwa sababu. Pia, ucheshi husika huacha au kuzaa athari kwa mchekeshwaji au, na mchekeshaji. Matokeo ya utafiti yanaonesha ya kwamba, tamthilia zote zimehusisha matumizi ya ucheshi kwa namna na viwango tofauti. Na kwamba, upo mfanano wa matumizi ya ucheshi wa kimazungumzo katika tamthilia moja ya awamu ya Azimio la Arusha na mbili za awamu ya soko huria. Utangulizi huu unatusaidia sana katika kutoa picha kamili ya kile kilichobainika na kuwasilishwa kupitia data za utafiti wetu.

Utafiti huu ulibaini matumizi ya ucheshi katika tamthilia ya *Mashetani* uliosukwa kwa ubunifu mkubwa na kufanya isiwe jambo rahisi kuubainisha. Hivyo, yamtaka msomaji kusoma kwa makini zaidi na kuhusisha mbinu na nadharia mbalimbali za kubaini uchezi ili kuweza kusema huu ni ucheshi ama la. Utafiti huu ulitumia mwongozo wa Wamitila (2008) kuhusu aina ya ucheshi na ubainishaji wake. Hivyo, kupitia mbinu ya usomaji makini tuliweza kubaini kuwapo kwa ucheshi ambao unajitokeza kwa mdafao wa 52. Na aina ya ucheshi iliyojitokeza zaidi ni ucheshi wa kibeuzi na ucheshi wa kitanzia. Ucheshi mwingine uliobainika katika tamthilia hii ni ucheshi wa kizimbwe, ucheshi wa kimazungumzo na ucheshi wa kimwingiliano.

Muhtasari wa utokeaji wa ucheshi unapambanuliwa kupitia Jedwali 5.1 la mdaafao lifuatalo: -

**Jedwali 5.1** Mdaafao wa Utokeaji wa Lugha ya Ucheshi katika *Mashetani*

N/M	Aina ya Ucheshi	Kurasa Zilizobeba Ucheshi	Mdaafao wa Utokeaji
1.	Kimazungumzo	15, 16, 18, 21-22, 32-35, 36-39, 40-41, 50-51	8
2.	Kibeuzi	3, 4, 5-6, 8-9, 10-12, 16, 21, 30, 33, 41-42, 47, 48-49, 50-51, 52, 55-57	15
3.	Kitanzia	1, 2, 3, 6, 8, 9, 19, 21, 30-31, 41-43, 45-46, 47, 54-57	13
4.	Zimbwe	5, 6, 7, 16, 17, 21, 22, 33-35, 36, 40-43, 52-54	11
5.	Kimwingiliano	12, 28, 29, 33-34, 55-57	5
<b>Jumla ya Utokeaji wa Lugha ya Ucheshi</b>			<b>52</b>

**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Mashetani*, 2018

Jedwali 5.1 linaonesha mdaafao wa utokeaji wa lugha ya ucheshi kwa jumla na kimahususi. Mdaafao unaonesha kuwapo kwa jumla ya lugha ya ucheshi inayozidi asilimia 50. Lugha ya ucheshi imetawaliwa na ucheshi wa kibeuzi na kufuatiwa na ucheshi wa kitanzia halafu ucheshi wa kizimbwe. Kisha ucheshi wa kimazungumzo na mwisho ni ucheshi wa kimwingiliano. Tunapotazama kiwango cha utokeaji wa lugha ya ucheshi wa kibeuzi, lugha ya ucheshi wa kitanzia na lugha ya ucheshi wa kizimbwe kwa pamoja, tunagundua kiwango cha juu cha ubunifu uliobeba ukubwa na uzito wa lugha ya kitaswira iliyojengwa katika kuikamilisha tamthilia hii. Aina hizi tatu (3) za ucheshi - yaani ya ucheshi wa kibeuzi, ucheshi wa kitanzia na ucheshi wa kizimbwe; lengo lake kuu huwa siyo kuleta burudiko la kawaida kwa msomaji



bali kujenga udadisi na tafakuri ya kina kwa kile kilichomfanya acheke au kutabasamu (Wamitila, 2008; Senyamanza, h. m.).

Kwa ujumla tunaweza kusema kwamba, ucheshi uliosukwa na mwandishi Ebrahim N. Hussein katika tamthilia ya *Mashetani* siyo wa kiwango cha kubeba lengo la kuwafurahisha wasomaji, wasikilizaji au watazamaji, ama kuiepushia uchovu hadhira. Bali ni ucheshi wa kiwango cha kujenga kejeli na utulivu wa kulitazama jambo kwa sura ya tatizo na kujikinai au kujidharau ili kuleta mabadiliko ya kweli. Mabadiliko hayo ni yale chanya na endelevu kwa faida ya kizazi cha leo na vijavyo. Ucheshi uliojengwa katika ubunifu wa hali ya juu hupatikana katika tamthilia zenye matumizi makubwa ya lugha ya kisitiari na kitamathali kama ilivyo katika tamthilia hii ya *Mashetani*. Nukuu ifuatayo inathibitisha jinsi ucheshi ulivyotumika katika tamthilia ya *Mashetani*:

SHETANI: Umeshuhudia miujiza. Nimekuonesha miujiza ili uamini uwezo wangu. (*Anakaa juu ya kiti kwa upole na huruma.*) usiogope, usiogope. Kwako wewe mimi rafiki. Wala hutapata rafiki kama mimi. (*Anabadilika kwa ukali.*). Unaniogopa?

BINADAMU: Ndiyo.

SHETANI: Unanicha?

BINADAMU: Ndiyo.

SHETANI: Unaninyenyekea?

BINADAMU: Ndiyo.

SHETANI: Mbona siuoni unyenyekevu wala uoga katika uso wako?

BINADAMU: Kipitacho moyoni si lazima kionekane usoni.

SHETANI: Sijali kipitacho moyoni. Ninajali kionekanacho usoni. Onesha kwa dhahiri ninachotaka kukiona. (*Anacheka.*) Baadaye utafahamu kuwa uso ukizoea kuonesha kinachotakiwa kuonekana, na sicho kinachopita moyoni, basi wakati utauzoeza moyo usifarikiane na uso wake. Unaelewa nasema nini?

BINADAMU: Naelewa.

SHETANI: Weka akilini hilo. Utakuja kulitaka baadaye. (*Kwa ukatili*) Njoo hapa! (*Binadamu anakuja.*) Sivyo, sivyo, sivyo! Sivyo hata kidogo. Jaribu tena. We, njoo hapa. (*Binadamu anakuja mbio.*) Ah, sivyo hata kidogo. Jaribu tena. We, njoo hapa. (*Binadamu anakuja mbio. Akifika karibu, anakuja kwa kukwawa.*) Hebu tujaribu tena. We, njoo hapa. (*Binadamu anakuja mbio. Akifika karibu, anakuja kwa kukwawa. Anasujudu.*) Ndiyo sasa sawa. Hivi sawa sawa. (*Shetani anacheka. Binadamu anafuatisha. Shetani ananyamaza kucheka ghafla. Binadamu naye ananyamaza kucheka ghafla. Shetani anacheka, na kicheko chake hivi sasa kinatisha. Mara anabadilika; kawa mpole, mtu rahimu kabisa.*). (uk. 2 - 3)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Mashetani*, 1971)

Ukichunguza nukuu hii, utagundua kuwa nukuu imebeba majonzi, hofu, karaha, mashaka, kukata tamaa na uzumbukuku au utii wa mtumwa kwa bwana wake. Hapa Binadamu amejaa hofu na mashaka ilhali kwa Shetani ni kicheko, raha, fahari na kiburi kisicho na kifani. Matendo na mazungumzo haya yanafanana na maisha ya kila siku ya mtumwa / mtwana mbele ya bwana wake. Mjadala huu unatufanya tusikitike, tukasirike na kucheka kwa wakati mmoja au kwa awamu kutegemeana na athari za kihisia anazozipata msomaji au, na mtazamaji. Kwani, mhusika ‘Binadamu’

anaonekana kufanywa zuzu na msukule wa mhusika ‘Shetani’ kiasi cha kutendwa na kujibu kwa namna ambayo inamuondolea utu, heshima, utashi, ufahamu na uwezo wa kufikiri.

Namna mhusika Binadamu anavyojibu maswali na kutekeleza maelekezo ya mhusika Shetani ni kichekesho tosha na huruma tosha lakini ni dharau tosha kwa Binadamu. Pia kunaibua hasira, dharau na chuki miongoni wa wasomaji na watazamaji dhidi ya Shetani anayejiona kuwa ni kila kitu na kiumbe sahihi, anayejitambua, kutenda na kunena kwa usahihi kamili. Kupitia nukuu hii tunabaini kuwapo kwa matumizi ya lugha ya ucheshi wa kizimbwe, ucheshi wa kitanzia na ucheshi wa kibeuzi. Mfano mwingine unaoibua huzuni, hasira na kicheko kwa wakati huo huo ni nukuu ifuatayo inayobeba mazungumzo baina ya Daktari na familia ya Kitaru – Baba, Mama. Tazama nukuu ifuatayo: -

DAKTARI: Kama nilivyokuwa nikisema, ugonjwa huu mimi siwezi kuutibu. Maana haina haja kuja kila siku nikachukua pesa za bure.

(*Wanacheka.*)

BABA: Hapana, hapana. Wewe huwezi kufanya hivyo.

MAMA: Hata kidogo.

(*Wanacheka.*)

DAKTARI: Ugonjwa huu, ninavyofikiri mimi... Kwa kweli, pengine ni kuchoka kwa akili tu. Watoto wa Chuo Kikuu bwana, wana mengi wanayoyasoma na kuyafikiria. Pengine amepata, labda, *neurosis*.

MAMA: *Neurosis!* Ndiyo nini tena. Wazimu?

BABA: Siyo wazimu bibi we.

(*Wanacheka*)

DAKTARI:Hapana. Siyo wazimu. Ni – hata sijui nisemeje kwa Kiswahili – machofu makubwa ya akili. Mtu anafikiria mambo, pengine hata hayapo. Akipumzika vizuri, basi mtu anarudia hali yake ya kawaida.

MAMA: Na unadhani kuwa hii ndiyo n-neo... nini sijui hiyo?

DAKTARI:*Neurosis*. Inaweza kuwa. Ndiyo maana nimempa dawa za usingizi; akili ipoe. Lakini taabu yenyewe ni kwamba ingawa nimefanya hivyo, Kitaru haonyeshi alama za *neurosis*.

MAMA: Sasa kama si ugonjwa huo, ni nini basi?

DAKTARI:Sijui, lakini kuna kitu kinamtaabisha.

*(Baba na Mama wanatazamana. Kimya.)*

MAMA: Lakini kitu gani basi?

DAKTARI:Ndilo hilo nikitaka kuongea naye. Lakini sifikiri kama ingefaa kitu, maana mara nyingi hasemi ukweli wake. Anasema lile unalolitaka wewe kusikia. Ukimuuliza, ‘Nini kinakupa taabu?’ Hawezi, au hataki kujibu. Lakini ukimuuliza swali lile lile ukaongeza neno moja au mawili ya kumsaidia, oh, jawabu mara moja. Ukimuuliza, ‘Nini kinakupa taabu? Kichwa?’ anaitikia mara moja, ‘Eh, kichwa.’ Halafu atakuuliza wewe, ‘Je, ugonjwa gani?’ Lakini huwezi kujibu, maana ukimpima hana kichwa wala chochote. Lakini anataka wewe umwambie yeye anaumwa na nini. Na mimi, kusema kweli, siwezi kumwambia; maana sijui. Lakini kitu kimoja ninafahamu – ana shaka kama anaumwa. Lakini sielewi kwa nini mtu mzima na akili yake atie shaka tu kama anaumwa. Tena siyo hivyo tu. Anahiari ugonjwa kuliko wasiwasi. *(Baba na Mama wanatazamana.)* Anaogopa kuwa katika hali ya wasiwasi. Sijui; labda kwake yeye, ninavyofikiri mimi, wasiwasi una hatari zaidi kuliko ugonjwa.

BABA: Na wewe unafikiri vipi?

DAKTARI: Mimi ninafikiri kuwa huku ni kuidekeza akili tu. Mtu akiifuata na kuidekeza akili, na kuipa mawanda fikira, basi huenda akaja akaamini kile kilichobuniwa na akili yake. Kwa mfano, akijiendekeza anaweza mwishowe kupata kiarusi. Siyo kiarusi cha kiwiliwili bali kiarusi cha vitendo. Mtu anayekuwa na wasiwasi, vitendo vyake havina hakika, na mara nyingi hawezi kufanya lolote.

MAMA: Sasa, ikiwa daktari hafai kitu tufanyeje basi?

BABA: Tupe maarifa, sasa tufanye nini?

DAKTARI: (*Kimya*) Mimi naona afadhali tungoje siku moja mbili. Pengine hizi dawa zitamfaa. Itakuwa haina haja tena. Na kama ataendelea hivi hivi, basi tutampeleka kwa mganga wa akili. Lakini naona tungoje kwanza.

BABA: Basi tutatazama. Ikiwa mambo yako vilevile, basi tutakueleza. (uk. 33 - 34)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Mashetani*, 1971)

Ukichunguza nukuu hiyo, utagundua kuwa mazungumzo kati ya Daktari, Baba na Mama yanaonesha kuwapo kwa mambo kadhaa yanayojenga masikitiko, hali ya kukata tamaa, tafakuri, hasira na maswali yasiyajibika. Mambo hayo ni pamoja na Daktari kupata hofu na kutokujiamini kutokana na hisia iliyompata ghafla juu ya namna wenyeji wake wanavyomchukulia dhidi ya hali ya kijana. Wenyeji wanamuona kama daktari anayepokea malipo kutoka kwao ili kumtibu Kitaru ilhali mgonjwa haoneshi kupata unafuu wa hali. Jambo la pili ni Daktari kukiri kutokuujua ugonjwa husika hivyo hata matibabu yake ni sawa na ya mganga feki wa kienyeji mwenye kupiga ramri chonganishi. Jambo la tatu ni kitendo cha mgonjwa – Kitaru, kutokuonesha ushirikiano kwa kutokuweka bayana kile kinachomsibu. Ilhali moyoni mwake anajua chanzo cha yeye kufika hapo alipofika. Badala yake, Kitaru amegeuka

zuzu wa kujibu “sijui,” “eeh, ndiyo hivyo” hali inayoongeza hofu na mashaka kwa wazazi na daktari.

Jambo la nne ni kitendo cha mama kushindwa kutamka neno “*neurosis*.” Jambo la tano ni kitendo cha Mama kuonesha unafiki kwa kujifanya mtulivu na mchunguaji makini wa hali ya kijana wake. Wakati katika mazungumzo kati yake na mumewe, kabla ya ujio wa daktari, mama huyu alikuwa ni mbogo kwelikweli. Hadi akafikia hatua ya kutaka kuitwa kwa mganga wa asili kwa hoja kuwa “afadhali tutafute dawa za kienyeji basi. Imekuwa dawa za Kizungu hazifai [...]” Na, “[...] kuliko hivi kumpa madawa haya ya usingizi. Hayana maana yoyote. Kupona haponi, matata moja kwa moja. Pesa zinapotea bure” (uk. 30-31). Lakini daktari alipofika na kutamka kwamba, “Kama nilivyokuwa nikisema, ugonjwa huu mimi siwezi kuutibu. Maana haina haja kuja kila siku nikachukua pesa za bure.” Wote watatu waliangua kicheko na kupingana na mtazamo wa Daktari!

Matarajio ya wasomaji na watazamaji, bila shaka, ni kumuona Mama akimkabili daktari kama alivyofanya kwa mumewe. Hata kama siyo kwa ukali lakini kutoa maoni yake juu ya wapi pa kumpeleka mgonjwa kama alivyokuwa amefikiria awali. Kinyume na matarajio haya ya hadhira, Mama ameamua kufa na tai yake shingoni. Bila shaka amefanya hivi ili kungoja daktari aondoke ili alianzishe upya kwa mumewe. Kwa hiyo, kicheko cha mume na mke kilitokana na kauli iliyotawala kinywa cha Mama kabla ya daktari kuingia, na kukomesha tufani ya malumbano yaliyokuwa yakiendelea.

Kwa hisia zetu, tunadhani kuwa kuna uwezekano kicheko cha Mama kilisindikizwa na maneno ya kimoyomoyo. Kwamba, Mama alijisuta mwenyewe huku akijisemea,

“mmmh! Wewe Daktari wewe...! Utasutwa hadi mtandaoni. Kama ulikuwapo vile. Maana wewe na mshenzi mwenzako... (*anasonya kimyakimya*). Kwanza, umejuaje kama hili ndilo wazo nililonalalo! Au umenisikia nini?”<sup>5</sup> Huku Baba Kitaru akijichekesha na kujisemea, “Looh! Daktari mbona unamvua nguo mke wangu mchana kweupe peee! Maana ni punde tu katoka kuninyea uharo wa mayai viza na kunitapikia...!”<sup>6</sup>

Kwa hiyo, katika utafiti huu, kupitia mazungumzo kati ya watu hawa watatu – Daktari, Baba na Mama tunaweza kuhitimisha kuwa katika tamthilia ya *Mashetani* kuna matumizi makubwa ya lugha ya ucheshi wa kimazungumzo, ucheshi wa kitanzia, ucheshi wa kizimbwe, na ucheshi wa kibeuzi (muunganiko mzuri unaanzia uk. 30 -35). Mfano mwingine wa matumizi ya lugha ya ucheshi wa kitanzia ni huu: -

(*Kimya. Mlio wa gari. Gari inasimama. Sauti ya Baba Kitaru*)

BABA KITARU: (*Anaimba*)

*Papa pa pa pa pa*

*I like some money.*

*Papa pa pa pa pa*

*I like some honey.*

*Papa pa pa pa pa*

(*Mama Kitaru anaingia*)

*A very good life.*

*Papa pa pa pa pa*

(*Anamchukua mkewe kucheza.*)

*A very beautiful wife.*

*Papa pa pa pa pa*

*A very good wife.*

*Papa pa pa pa pa*

<sup>5</sup> Nukuu hii ni sehemu ya ufafanuzi wa mtafiti. Siyo kauli iliyomo katika tamthilia ya *Mashetani*

<sup>6</sup> Nukuu hii ni sehemu ya ufafanuzi wa mtafiti. Siyo kauli iliyomo katika tamthilia ya *Mashetani*

*A very good life.*

MAMA KITARU: Una nini leo? Mbele ya watoto wako unafanya mambo ovyo!

BABA KITARU: Shhh.... Njoo, njoo nikuonesheni kitu.

MAMA KITARU: Nini?

BABA KITARU: Ndege wangu.

JUMA NA KITARU: Ndege!

MAMA KITARU: Ndege?

BABA KITARU: Njoni hapa dirishani. Unaiona nini?

MAMA KITARU: Gari mpya! Benzi!

BABA KITARU: Yangu! Naam! Mali yangu, jasho langu. Kitaru, njoo uitazame. Juma, njoo. Mnaiona? Tazama ilivyotulia. Basi pale itoneshe tu – waaaah, linaruka kama ndege. Twende tukatembe, mnasemaje? Twendeni. Twendeni, twende. (*Yeye na mkewe wanatangulia.*)

(*Kimya. Baada ya muda.*)

BABA KITARU: (*Anaita kutoka chini*) Kitaru! (*Mazungumzo kwa sauti ya juu. Mcheko unatisha.*). (uk. 21-22)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Mashetani*, 1971)

Sehemu ya kwanza ya data kupitia nukuu hii inaonesha furaha aliyonayo BABA KITARU. Lakini sehemu ya pili inayobeba mazungumzo inaweza kuonekana siyo ya kicheshi kama msomaji ataisoma kwa hali kavu bila kujenga picha ya utendaji dhahiri akilini mwake. Kiutendaji dhahiri, kauli ya BABA KITARU kwa MAMA KITARU inaendana na mtu mwenye furaha, mikogo, anayejisikia wa tofauti na kutamani dunia nzima ione na kuheshimu kile alichokitenda. Hapa ndipo tunapopata ucheshi wa kimazungumzo. Utafiti umebaini kuwa, wakati watazamaji wakimkinai



BABA KITARU yeye anaonekana kutenda na kutamka maneno ya kujifariji kwa raha kama mtu asiyejitambua wala kuchuja mambo kwa busara, maarifa na hekima.

Kauli kama “Yangu! Naam! Mali yangu, jasho langu. Kitaru, njoo uitazame. Juma, njoo. Mnaiona? Tazama ilivyotulia. Basi pale itoneshe tu – waaaah, linaruka kama ndege. Twende tukatembee, mnasemaje? Twendeni. Twendeni, twende” zinathibitisha kutotambua hasara aliyoitia nchi na taifa mradi yeye ajipe raha. Aidha, utafiti umebaini kuwa BABA KITARU anaonekana kuamini kwamba anachokifanya au kukisema ni sahihi na chenye kukubalika kiasi cha kumjengea heshima kutokana na ununuzi wa gari la kifahari kwa fedha haramu zilizotokana na uufisadi alioufanya katika kampuni aliyokuwa anaisimamia.

Wakati BABA KITARU akifurahia tukio hilo, tunabaini kuwa BABA KITARU hatambui wale wanaomtazama wanamshangaa, kumsikitikia na kuishia kumdharau, kumcheka na, au kumsifu kwa ghiribu. Haya yanathibitishwa kupitia mazungumzo baina ya MTU 1 na MTU 2. MTU 2 anasema, “Aah! Aah! Ndiyo, ndiyo, ndiyo. Aha! Kwani ndiye huyu bwana mwenyewe?” kisha MTU 1 anajibu, “Eh. Pesa chungu nzima bwana zimepotea. Lakini ndiyo haijulikani kuwa zimeibiwa au zimepotea katika mahisabu.” Halafu MTU 1 anaendelea “Alaa. Kumbe ndiye huyu? Shetani kweli kweli...” (rej. tamthilia ya *Mashetani*, 1971; uk. 43). Kwa kauli hizi, mtu anayemtazama BABA KITARU akijifariji kwa kununua gari, ilhali ameitia hasara nchi na taifa; mtu huyo ataishia kutoa kicheko au tabasamu lisilo na furaha bali majonzi. Hapa ndipo tunapata ucheshi wa kitanzia na kizimbwe. Kwani baadhi ya watu watamuona BABA KITARU sawa na mtu punguani asiye na akili wala

huruma. Hasa ikizingatiwa ya kwamba vyanzo vya fedha ya kununua hilo gari ni ufiisadi uliolitia taifa na nchi hasara kubwa.

Kwa ujumla, matumizi ya ucheshi katika tamthilia ya *Mashetani* yanasadifu mbinu ya uwasilishaji ujumbe kwa njia ya utani na mizaha kwa tabaka linaloogopwa. Mbinu hii ni sehemu mojawapo ya mbinu za kitaswira zinazojishughulisha na lugha-msimbo. Kifasihi, lugha ya kitaswira hujengwa na kutambuliwa kupitia matumizi ya lugha ya picha yenye kubeba maana ya ndani – maana iliyofichika – maana isiyokuwa ya kawaida (Selden, 1985).

Kwa upande wa Tamthilia ya *Kijiji Chetu* utafiti umebaini kuwapo kwa ucheshi mwingi wa kimazungumzo. Pia, mwandishi ametumia ucheshi wa kitanzia, ucheshi wa zimbwe na ucheshi changamani. Ucheshi wa kibeuzi na ucheshi wa kimwingiliano haukubainika kutumika ndani ya tamthilia hii ya *Kijiji Chetu*. Mdafao wa utokeaji wa ucheshi huu unawasilishwa kama ifuatavyo kupitia Jedwali 5.2: -

**Jedwali 5.2** Mdafao wa Utokeaji wa Lugha ya Ucheshi katika *Kijiji Chetu*

N/M	Aina ya Ucheshi	Kurasa Zilizobeba Ucheshi	Mdafao wa Utokeaji
1.	Kimazungumzo	1-2, 7, 8, 22, 28, 31, 35, 41-42, 52-53	8
2.	Kibeuzi	—	0
3.	Kitanzia	16-17, 19	2
4.	Zimbwe	9, 11, 52-53	3
5.	Changamani	51, 54-55	2
6.	Kimwingiliano	—	0
<b>Jumla ya Utokeaji wa Lugha ya Ucheshi</b>			<b>15</b>

**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Kijiji Chetu*, 2018

Jedwali 5.2 linaonesha kiwango cha mdaafao wa utokeaji wa lugha ya ucheshi katika tamthilia ya *Kijiji Chetu*. Jedwali hili linaonesha kuwapo kwa ucheshi wa kimazungumzo wa kiwango cha juu kuliko aina nyingine za ucheshi. Hii inamaanisha ya kwamba, tamthilia ya *Kijiji Chetu* haijajikita sana katika dhima ya uburudishaji. Ijapokuwa, haijajitenga kabisa na dhima ya uburudishaji wa hadhira pindi inapojadili mambo mazito yanayohusu jamii. Hii inajionesha kupitia mazungumzo yafuatayo kati ya Mtu 3, Riziki na Sauti: -

**MTU 3:** Tunajua sisi, Kamati itapendelea upande mmoja tu!

**RIZIKI:** Ndugu, huna imani na Kamati na wajumbe uliowachagua we mwenyewe?

**SAUTI:** Funga mkutano tumechoka kukaa. Matako yameuma kukaa mahali pamoja. – Mnataka mpaka tuunguze majani. (*Na watu wanaanza kusimama na kuondoka mmoja mmoja*). (uk.22)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Kijiji Chetu*, 1975)

Nukuu hii inaonesha kauli inayotolewa na Sauti zinazowakilisha wananchi waliochoshwa na vuta nikuvute katika kikao hicho ndiyo iliyoibua lugha ya ucheshi. Mazungumzo baina ya Mtu 3 na Riziki hayaoneshi kuwafurahisha wajumbe walio wengi. Badala ya kuwakaripia wajumbe hawa, wananchi wanaamua kutaka mkutano ufunge kwani wamechoka kukaa (tena chini) kiasi cha kuumia makalio na nyasi nazo kupata kashikashi. Ucheshi wa namna hii pia unajitokeza katika ukurasa wa 51 hadi 54 wa tamthilia hii. Ambapo, wajumbe wanaonekana kutofautiana kutokana na maamuzi kuchukuliwa kinyume na mazingira halisi ya mikutano. Nukuu ifuatayo hapa chini inathibitisha hoja hii: -

**PINDUO:** Hatukukubaliana kuwa kila mwanakijiji atakuwa mfanyakazi?

**SAUTI:** (*Kwa pamoja*). Ndiyoooooooooooooooooooooooooooo!

**PINDUO:** Niambieni ndugu, tulipowaondoa wale wadhalimu tulikuwa na maana kuwa wengine wachukue nafasi zao?

**SAUTI:** Sanaaa. (uk. 51)

\*

**PINDUO:** Kabisa ndugu. Na bado nina imani ile ile kamili kwa ujamaa. Lakini, je, unaoendeshwa hapa na Mwenyekiti, wewe hapo Makamu na wachache wetu, wa kuendelea kumiliki biashara ni ujamaa? Kama wote tunataka kuendelea vipi basi tuwaache watu wachache wanufaike na watupe hata sisi tamaa ya kutaka mali!

**MTU 2:** (*Huku akicheka*). Hakika unadhihirisha jinsi ulivyokosa akili. Hilo ni jambo la kusema hapa kweli! Hasa wewe wamekusifia kuwa ulikuwa mwanamapinduzi! Kumbe wako ni wivu na kuona wengine wanafaidi nawe tamaa imekushika. Ndugu wananchi mwamueni mwanamapinduzi huyu.

**SAUTI:** Aondoke. – wote hao ni sawa, wanatupotezea wakati.... (*Wanakijiji wengine wanacheka wengine wanamkabili kwa ghadhabu wakiongozwa na Mtu 3.*) Mwisho sasa. – Mwondoeni. – mwondoeni. – Na Pinduo. – Wote, na Mwenyekiti na Makamu wake. (*katika vurumai hiyo vikundi mbalimbali vya wanakijiji vinawakusanya wanaohusika na kijana mmoja anaanzisha aina ya wimbo jukwaani*). Kizito aondoke, Pinduo. – aondoke. – Mwenyekiti. – aondoke. - wavivu. – Waondoke. (uk. 54 - 55)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Kijiji Chetu*, 1975)

Ukichunguza nukuu hii, katika sehemu ya kwanza ya nukuu hiyo (uk. 51) inaonesha wananchi wanavyomkubali Pinduo na kumshangilia kila alipoinuka kuzungumza. Sehemu ya pili ya nukuu (uk. 54 - 55) inaonesha wananchi walewale wamemgeuka Pinduo na kuamua kumjumuisha katika kundi la watu wanaotakiwa kufukuzwa kijijini. Hiki ni kichekesho kinachoonesha tatizo la kutokujikomboa kifikra kwa wananchi katika Kijiji cha Ujamaa. Wananchi wanaonekana kuwa ni wanabendera-fuata-upepo. Wananchi wanaonekana kutokujua ukweli na usahihi wa mambo na maazimio kwa faida yao na vizazi vyao. Mfano mwingine ni ule unaoonesha kuwapo kwa lugha ya ucheshi wa kimazungumzo katika tamthilia hii kupitia mazungumzo kati ya Mwanamke I, Mwanamke 2 na Mwanamke 3. Tazama nukuu ifuatayo hapa chini: -

**MWANAMKE I:** Basi mwana wa watu akajifunga kibwewe, mwiko mkononi! Akamnyima chakula cha usiku mumewe!!

**MWANAMKE 3:** Chakula cha usiku (*Anakauka kucheka kiasi cha kuwashangaza wenzake*).

**MWANAMKE 2:** Ala babu wee – kitu gani cha kukuchekesha namna hiyo?

**MWANAMKE 3:** Aibu hiyo. Anamchukia kiasi cha kumnyima... (*Anapasuka tena*).

**MWANAMKE I:** Waswahili bwana, wanataka kulipindua kila neno. Husemi neno likabaki na maana ile ile uliyokusudia

**MWANAMKE 2:** Ai babu we!! Ndiyo cha kukufanya upasuke mbavu, hicho tu! Kumbe ulitaka asemeje?

**MWANAMKE 3:** Ugali.

**MWANAMKE I:** Na kama hali ugali? (uk. 35)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Kijiji Chetu*, 1975)

Data za nukuu hii inadhihirisha kuwapo kwa mbinu ya ucheshi ambao mwandishi ameutumia katika kueleza changamoto zilizotokana na utekelezwaji mbaya wa Azimio la Arusha. Vile vile, nukuu hii inaonesha mazungumzo ambayo yana kauli yenye ukakasi lakini lugha yake hupendwa sana na watumiaji wa lugha hasa watu wa kundi maslahi moja wanapokutana. Kauli hiyo ni “[...] akamnyima chakula cha usiku mumewe!!” Kauli hii ina utata kimaana unaoibuliwa na Mwanamke 3. Utata huu unatokana na maana ya msingi (chakula cha usiku au chakula cha jioni) kukutana na maana ya ziada inayobebwa na msemu / tafsida ya “chakula cha usiku” inayomaanisha tendo la ndoa.

Kuwapo kwa Mwanamke I na Mwanamke 2 kumesaidia kutambua maana ya ziada iliyofikiriwa na Mwanamke 3. Palepale, wanawake hawa wawili (2) wakatambua na kutoa ufafanuzi unaosaidia kutoa picha kamili kwa usahihi na haraka pasipo kuacha chembe ya shaka kumea. Huu ni ubunifu katika matumizi ya lugha ya ucheshi kwa kutumia tamathali ya usemi yenye kufumbata lugha ya picha na hapo hapo mwandishi anamleta mhusika mwingine kuondoa utata wa kimaana. Kwa mujibu wa Low (2011), matumizi ya ucheshi kupitia lugha ya picha yanaweza kujitokeza kupitia misimu, lugha ya ucheshi yenyewe, tamathali za usemi, vitendawili, nahau, maana funge ya neno la kawaida, vitu halisi na dhahania.

Pia, lugha ya ucheshi hufumbata historia, saikolojia ya wahusika, mandhari, muktadha, mazingira, maudhui, uchanganyaji ndimi na matumizi mengine ya mbinu za kisanaa ili kufumba jambo na kujenga tafakuri ya kina katikati ya burudani. Tunapotumia nadharia ya Fasihi Linganishi kuchunguza ucheshi wa namna hii

tunabaini ya kwamba, kwa jamii za Mwambao matumizi ya lugha ya ucheshi yenye kufungamana na tafsida ni kitu cha kawaida kabisa kwao (Nguti, 2013; Yussuf, 2017). Kwa hiyo, si ajabu ubunifu huu wa mwandishi umetokana na mazingira yaliyoibua fikra ya wazo aliloliwasilisha kisanaa.

Nayo tamthilia ya *Harakati za Ukombozi* imebainika kuwa na ucheshi wa kimazungumzo, kitanzia na ucheshi wa kizimbwe. Pamoja na kuwapo kwa aina hizi, utafiti umebaini kwamba mdafoa wa utokea wake una jumla ya ucheshi nane (8) pekee. Huku ucheshi wa zimbwe ukionekana kutawala zaidi kuliko aina nyingine. Ijapokuwa, ucheshi wa kitanzia unatofautiana na ule wa kizimbwe kwa ucheshi mmoja pekee. Muhtasari wa mdafoa wa utokeaji wa ucheshi huu unawasilishwa katika Jedwali 5.3 kama ifuatavyo: -

**Jedwali 5.3** Mdafoa wa Utokeaji wa Lugha ya Ucheshi katika *Harakati za Ukombozi*

N/ M	Aina ya Ucheshi	Kurasa Zilizobeba Ucheshi	Mdafoa wa Utokeaji
1.	Kimazungumzo	17- 19	1
2.	Kibeuzi	—	0
3.	Kitanzia	15-16, 22, 23-25	3
4.	Zimbwe	6, 12, 17, 19	4
5.	Kimwingiliano	—	0
<b>Jumla ya Utokeaji wa Lugha ya Ucheshi</b>			<b>8</b>

**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Harakati za Ukombozi*, 2018

Jedwali 5.3 linaonesha kuwapo kwa kiwango cha chini cha matumizi ya lugha ya ucheshi. Utafiti umebaini kuwapo kwa ucheshi wa kizimbwe zaidi kuliko aina nyingine za ucheshi. Bila shaka, kiwango hiki cha chini kimetokana na waandishi

husika kujenga darasa lenye chujio ambalo wasomaji watatakiwa kutafakari zaidi ni wapi na nini kilisababisha anguko la Azimio la Arusha. Hoja hii inaungwa mkono na Wamitila (2008) ambaye anabainisha kuwa, daima lengo la ucheshi wa zimbabwe huwa ni kuchochea fikra, mawazo, uwazaji na tathmini ambayo ni ya kitaaluma zaidi kuliko kuleta burudani ya kawaida katika jamii. Mfano wa ucheshi wa aina hii unajidhihirisha katika nukuu ifuatayo: -

**MZEE:** (*Anacheka sana*). Vijana mnanichekesha. Sisi mababu zenu tumekumbana na mambo mengi. Lakini hatukuweza kuleta mapinduzi. Walikuja Waarabu wakatuswaga na kutuuza kama ng'ombe. Wakaja Wajerumani wakatulimisha kwa viboko. Akaja Mwingereza akatulipisha kodi. Eti sisi tumlipe kodi, badala ya yeye kutulipa sisi kodi kwa kuingia nchini mwetu. Lakini wapi, wajukuu zangu, tulishindwa kufanya mapinduzi. Na ninyi leo mnajigamba "Tutaleta mapinduzi, tutaleta mapinduzi". Mapinduzi siyo rahisi. (*Anacheka*) Lakini nikiyakumbuka yote haya, siwezi kusahau wakati mbaya wa utumwa. (uk. 6)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Harakati za Ukombozi*, 1982)

Ukirejelea nukuu iliyowasilishwa hivi punde, utaona kuwa mwandishi anaonesha jinsi vijana wanavyopania kupambana na ukoloni mamboleo na vibaraka wake pasipo kujua chanzo hasa na mzizi mkuu wa anguko la Azimio la Arusha chini ya TANU na ASP. Ndiyo maana Mzee anaonekana ni kichekesho kwa vijana makasuku (na kinyume chake) wanaotunisha misuli tayari kupambana na hewa na kiza kilicho mbele yao. Tunasema kupambana na hewa na kiza kwa sababu, vijana hawa wameshindwa kung'amua ya kwamba walioliua Azimio la Arusha ndio haohao waliolianshiza. Tena, ndiyo haohao walioua TANU na ASP na kuzalisha chama



kipya – CCM. Huu ni ucheshi wa kizimbwe ambao mchekaji anacheka huku akiwa na majonzi na huruma kwa kutambua hatari wanayoiendea vijana wanaoonekana kutumika kama vikaragosi mikononi mwa maadui “wanaowapenda.” Hapa Mzee ameonesha kiwango cha juu cha uelewa dhidi ya kiwango cha chini cha vijana katika kuyaelewa malimwengu na walimwengu. Jambo linalothibitisha kuwapo kwa matumizi ya ucheshi wa kizimbwe.

Aina nyingine ambayo waandishi wameitumia ni ucheshi wa kitanzia. Ucheshi huu umetumika sana kuonesha kiwango cha uelewa wa vijana katika kupambana na maadui wa Azimio la Arusha. Vijana wamejaa mihemko zaidi kuliko busara, hekima na uelewa wa kina wa malimwengu. Tazama nukuu ifuatayo: -

**KIJANA 1:** Siafu! Mchwa! Nyuki! Meli!  
 Sisi si wana wa TANU tu  
 wala si wana wa Afro – Shirazi tu,  
 Sisi matokeo ya wazazi  
 hao wawili...  
 Nguvu zetu ni za kipekee,  
 Mbinu zetu ni mpya,  
 Hatutasafiri kwa ngalawa tena.  
 Tumeunda meli ambayo  
 Mwendo wake ni wa kasi  
 Mbinu zetu za mashambulizi  
 Hazitokei sehemu moja,  
 Zinatoka kila pembe  
 Tukilenga tumetungua  
 Ndugu tupeni nafasi.

**MZEE:** Nafasi mnaweza pewa, lakini je mtaweza?

**KIJANA 2:** Kuweza tutaweza kwa vile tumeazimia.

**MZEE:** Hata sisi babu zenu tuliiazimia lakini tukashindwa.

**KIJANA 3:** Mlishindwa kwa sababu mlikuwa na kasumba ya ukoloni.

**MZEE:** Je ninyi mmeshaifuta hiyo kasumba?

**KIJANA 4:** Ndiyo tumeifutilia mbali, tumeitupilia mbali. Sasa tutaleta mapinduzi.

**MZEE:** Haya vijana ukumbi ni wenu, kazi kwenu, jaribuni!

**KIJANA 1:** Siyo tujaribu, bali tutaleta mapinduzi kwa kutekeleza kwa vitendo maazimio na maamuzi yote ya Chama. (uk. 23-24)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Harakati za Ukombozi*, 1982)

Nukuu iliyowasilishwa hivi punde inaonesha kiwango cha umaamuma uliowajaa vijana wanaojitapa kwa ujasiri kwamba wataweza kupambana na hila za kila aina za ukoloni. Huku wakiamini kizazi cha Mzee kilishindwa vita hiyo kutokana na kukumbatia kasumba za kikoloni. Hapa ni dhahiri kwamba, wasomaji wabobevu wa mambo, hasa ya kihistoria na kiuchumi wasioegemea upande wowote wanaoisoma tamthilia hii wataishia kuwadharau na kuwacheka vijana hawa (Kijana 1, Kijana 2, Kijana 3 na Kijana 4). Huku wakimheshimu na kumuona Mzee kuwa ni mwananchi anayezungumza kitafakuri na kihistoria bila kuongozwa na propaganda wala siasa za majitaka.

Utafiti wetu umebaini kuwa, uelewa na imani ya Mzee kwa vijana hawa inatokana na matendo dhahiri ya kibepari na kishetani yanayofanywa na waasisi na walezi wa vijana hawa ambao ni masikini wa kipato na fikra. Walezi wa vijana hawa ndiyo wanaopaswa kulisimamia na kulipeleka mbele azimio la kuleta haki, usawa, umoja na mshikamano katika jamii. Kinyume chake, wao ndiyo mabepari na wahujumu uchumi na azimio - wa kutupwa. Tazama nukuu inayofuata hapa chini:-

**KIONGOZI 2:** (*anahutubia mkutano wa hadhara*) Azimio la Arusha  
Oyee!

**WANANCHI:** Oyee!

**KIONGOZI 2:** Wanyonyaji wote

**WANANCHI:** Ziiii!

**KIONGOZI 2:** Mabepari wote

**WANANCHI:** Ziii!

**KIONGOZI 2:** Wapinga Azimio

**WANANCHI:** Ziiii!

\*

**KIONGOZI 2:** [...] Ndugu wananchi, Azimio letu haliishii katika matamko, linaendelea siku hadi siku kutekelezwa kwa matendo. Kazi bado tunayo kubwa, magugu bado yapo. Tena yapo mengi sana. Hata hapa nayaona. Hivyo bado tuna kazi kubwa. (*Anamuonyesha mwananchi mmoja kati ya wanaomsikiliza ambaye ni mnene.*) Hebu wewe hapo simama. Wewe hapo. (*Mwananchi anasimama*) Njoo hapa. (*Mwananchi anakuja mpaka alipo kiongozi. Kiongozi anamtazama tangu juu hadi chini.*) Hivi wewe unakula nini? Unazo nyumba ngapi? Magari? Unayo mashamba mangapi? Hii suti inakupendeza, umeitoa wapi? Unazo ngapi? (*Mwananchi ameshangaa tu, hajibu.*) Wananchi hebu mtazameni mtu huyu mtazameni! Huyu mtu ni mmoja wa mifano mizuri ya wale wanaotunyonya. Angalieni wanavyofutuka na kumea vinundu. Hii yote kwa sababu ya kutunyonya sisi. Ndugu wananchi, tutanyonywa namna hii kwa muda gani? Hawa ndiyo wanatunyonya! Haya ndiyo makupe! Ndiyo mabomba hasa! Haya rudi... (*Kiongozi 2 anaondoka huku akiwapungia wananchi.*)

*Kiongozi 2 anafika kwenye bar. Anawakuta Mkurugenzi na Meneja wanakunywa pombe).*

**MKURUGENZI:** Karibu bwana.

**KIONGOZI 2:** Habari za kutangulia?

**MKURUGENZI:** Mzuri sana. Vipi mbona umechelewa?

**KIONGOZI 2:** (*Anakaa*). Ah! Nilikuwa kwenye shughuli za Chama, halafu nikapitia kwenye miradi yangu kuangalia isianguke.

*(Wote wanacheka)*

**MENEJA:** Unajua bwana kiwanda changu kimechukuliwa?

**MKURUGENZI:** Ala! Tayari?

**MENEJA:** Hasa. Lakini mwenzenu Azimio hili linaniumiza kichwa.

*(Wanacheka).*

**KIONGOZI 2:** [...] Kwani Bwana Meneja una nyumba ngapi?

**MENEJA:** Nina nyumba nne.

**KIONGOZI 1:** Nne tu?

**MENEJA:** Nne.

**KIONGOZI 2:** Aa! Mimi nilidhani una nyumba nyingi sana kumbe nne tu. Mbona mimi ninazo kumi (*anacheka*) na sina tatizo.

**MKURUGENZI:** Kwani ndugu Meneja huna watoto wowote?

**MENEJA:** Nina watoto wanne. Huyu wa nne kazaliwa juzi tu, hata siku kumi hajafikisha.

**MKURUGENZI:** Sasa kumbe una shida gani. Wagawie hao watoto hizo nyumba.

**KIONGOZI 1:** Eee! Kila mtoto mpe nyumba moja.

**MENEJA:** Eti kweli. Kwa nini sikufikiria jambo hili. (uk. 17-19)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Harakati za Ukombozi*, 1982)

Matukio ya maneno na matendo yanayojitokeza katika nukuu hii yanathibitisha kuwapo kwa ucheshi wa kizimbwe na kitanzia aliojengewa Mzee dhidi ya vijana wanaojitahidi kuonesha ubabe na uongaji wa kipropaganda. Wakati, viongozi wanaowategemea kuwashika mkono ili kutimiza azma yao ya kuleta mapinduzi ya kweli na endelevu wako kinyume chao. Mifano hii kwa pamoja inadhihirisha kuwapo kwa matumizi makubwa ya ucheshi wa kizimbwe na kitanzia kuliko aina nyingine zote za ucheshi. Matumizi haya ya lugha ya ucheshi yamekwenda sawia na ujenzi wa dhamira zenye kutafakarisha na kutathmini malengo na utekelezwaji wa kuanzishwa kwa CCM, kama ilivyopambanuliwa na waandishi wenyewe katika utangulizi / dibaji ya tamthilia hii (rej. Lihamba, Balisidya na Mhando, 1982).

Uchunguzi wetu umebaini kuwa, ucheshi katika tamthilia ya *Harakati za Ukombozi* unabebwa na hisi zinazotambuliwa na watu wenye kujaa hisia. Riemer (2010) anasema, lugha kama mfumo wa ishara wa vitu na matukio huja kutambuliwa kama kiashiria cha jambo halisi kupitia kiumbe hai ambacho kinahisi. Na kupitia hisi, kiumbe husika hupata ujumbe, ari, hali, na burudiko. Kwa hiyo, kupitia msaada wa nadharia ya Fasihi Linganishi, uchambuzi wetu umenufaika. Utunzi wa namna hii unahusishwa na athari ya maisha ya miaka ya 1970. Utunzi huu ulibeba mwelekeo mkubwa wa kuuasi na kuuacha umuundo mkongwe uliokuwa umetawala uhakiki wa kifasihi katika miaka ya 1960 (Wamitila, 2008). Tamthilia teule za awamu ya Azimio la Arusha kati ya mwaka 1971 na 1982 ni miongoni mwa matini bunilizi yanayoonekana kuupiga kumbo umuundo mkongwe. Umuundo mkongwe, kwa

sehemu kubwa ulishikilia zaidi shuruti za Kiaristotle kuliko uhuru wa mtunzi kiubunifu (Mlama, 2003; Mulokozi, 2017). Kwa hiyo, utunzi wa tamthilia ya *Harakati za Ukombozi* bila shaka ulikwenda sambamba na msukumo wa matumizi ya ishara mahususi kwa sababu mahususi, kiutunzi.

Katika tamthilia ya *Safari ya Chinga*, tumechunguza na kubaini kuwapo kwa matumizi makubwa sana ya ucheshi, hasa ucheshi wa kimazungumzo na ucheshi wa kizimbwe kuliko aina nyingine za ucheshi. Ucheshi huo unaonekana kujitokeza katika kurasa nyingi. Hii ni ishara kuwa, tamthilia hii inao utajiri mkubwa wa matumizi ya lugha ya ucheshi. Jedwali 5.4 lifuatalo linaonesha mdafao wa utokeaji wa lugha ya ucheshi katika *Safari ya Chinga*, kama ulivyobainika wakati wa utafiti: -

**Jedwali 5.4** Mdafao wa Utokeaji wa Lugha ya Ucheshi katika *Safari ya Chinga*

N/M	Aina ya Ucheshi	Kurasa Zilizobeba Ucheshi	Mdafao wa Utokeaji
1.	Kimazungumzo	1-2, 3, 4, 5, 8, 9, 10, 11, 13-14, 14-15, 16, 24-25, 26-27, 28, 29-30, 35, 36, 38-39, 40-41, 43, 45-46, 47-48, 50-52	23
2.	Kibeuzi	1-2, 12, 14-15, 36, 45, 47-48, 50	7
3.	Kitanzia	8-9, 10, 11, 13, 16, 29, 30, 41, 45-46, 47-48	10
4.	Zimbwe	1-3, 13-14, 14-15, 16, 17, 19, 20, 24-25, 27-28, 29-30, 34-35, 36, 47-48, 52-54	14
5.	Kimwingiliano	4-5, 14, 27-28, 29-30, 32-34, 35-37, 45-46, 47-49, 52	9
<b>Jumla ya Utokeaji wa Lugha ya Ucheshi</b>			<b>63</b>

**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Safari ya Chinga*, 2018

Jedwali 5.4 linaonesha matumizi makubwa ya uteuzi na uumbaji wa matumizi ya lugha ya ucheshi katika tamthilia ya *Safari ya Chinga*. Matokeo ya utafiti yanaonesha ya kuwa, tamthilia ya *Safari ya Chinga* imetajirishwa zaidi na ucheshi wa kimazungumzo na kufuatiwa kwa mbali na ucheshi wa kizimbwe. Kisha ucheshi wa kitanzia, ucheshi wa kimwingiliano na mwisho ni ucheshi wa kibeuzi. Aidha, tunapotazama kurasa zinazoonesa kuwapo kwa matumizi ya ucheshi, tunagundua kuwapo kwa mafungamano ya karibu sana katika uumbaji wa ucheshi. Kwani ndani ya aina moja ya ucheshi, mwandishi ameonekana kuzalisha aina nyingine ya ucheshi. Hali hii humvuta msomaji na kumfanya asichoke pindi aisomapo au kutazama kazi bunilizi iliyojaa ucheshi (Provine, 1996) kama ilivyo kwa tamthilia hii *Safari ya Chinga*.

Aidha, utafiti umebaini kuwa kuna ucheshi mwingi katika tamthilia hii kutokana na ujenzi wa aina ya wahusika hususani vijana na wazee wanaoishi vijijini ambako hali ya maisha ni duni. Lakini wachache waishio mijini wanaficha ukweli wa hali ya maisha yao huko mjini. Matokeo yake, jamii ya kijijini inawaza kuhamia mjini kwa imani ya kupata maisha bora. Uteuzi huu wa wahusika, lugha, muktadha, mandhari, wazo, wakati na ploti kunaifanya tamthilia hii kubeba ucheshi mwingi kuliko tamthilia nyingine zote tano (5) teule tulizozichunguza. Tena, ucheshi uliomo kwenye tamthilia hii unaonekana kuwa changamani zaidi na wenye kutambaa vilivyo kimafungamano na kimwitiko pindi msomaji anapoisoma kazi hii. Ushahidi wa hoja hizi unapatikana katika kazi nzima. Hapa tunanukuu kauli chache kama ifuatavyo: -

**Bi. Somoe:** Ukienda huko utafikia kwa nani na kwa njomba wako  
Chupaku hukujui?

**Mata:** Ntafikia kwa rafiki yangu Ntumusha, ntoto wa nzee Nankuchu.

**Bi. Somoe:** Ukimaliza kujiandaa nkaangie njomba wako korosho, unchukulie zawadi?

**Mata:** Mama, si zitaharibika. Anapokaa sipajui na sijui ntamwona lini. (uk. 14 - 15)

**Bi. Somoe:** Kumbuka mimi baba yako amenioa toka nna miaka kumi na tano. Mpaka leo bado tunaishi vizuri. Kwa sababu wazazi wetu walikuwa wanajuana. Usituletee nke hata kutwanga au kuchota maji hajui. Nke ambaye anaongea kizungu. Sisi hatujui kizungu. Hatutamwelewa.

**Mata:** Si ndo atawafundisha kizungu?

**Sijaona:** Nlete huyo huyo nzungu kaka tuongee ‘*yes yes nzungu kala mafenesi.*’

**Wote:** (*wanacheka*). He he he! Ha ha ha! (uk. 14)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Safari ya Chinga*, 2009)

Tunapochunguza data tuliyoinukuu hivi punde, tunabaini kuwapo kwa ucheshi wa kimazungumzo lakini pia kuwapo kwa ucheshi wa kizimbwe na ucheshi wa kimwingiliano (nukuu ya pili, uk. 14). Bi. Somoe anaonekana kuwa na hofu, mashaka na wasiwasi mwingi ilhali Mata anaonekana kujiamini na kujua kile anachokifanya. Matokeo ya hofu, mashaka na wasiwasi uliomjaa Bi. Somoe kunamfanya afanye makosa yasiyotarajiwa. Yeye mwenyewe anakiri kwamba Mata hapajui kwa mjomba wake (Chupaku). Baadaye anajisahau na kumtaka Mata aandae korosho za kumpelekea mjomba wake! Pia, Bi. Somoe anahofia Mata kuleta



mchumba asiyefahamika katika ukoo na familia. Kwa madai kwamba, kuletwa kwa mchumba asiye wa asili yao kunaweza kuleta matatizo katika familia na ukoo wa mme au mwanamke huyo. Bi Somoe anapinga kuletwa kwa mchumba asiye na asili ya jamii zao kwa sababu ya hofu ya kuja kukutana na changamoto ya mawasiliano kati ya mwolewaji na jamii ya mwoaji.

Tofauti na mawazo ya Bi. Somoe, Mata na Sijaona wanatamani familia yao ipokee mwanamke anayeongea lugha tofauti mathalani Kiingereza kwa lengo la kuleta mabadiliko katika jamii. Hiki ni kichekesho kweli kweli kinachoibua ucheshi wa kimazungumzo na kwa wakati huo huo tunapata ucheshi wa kizimbwe, ucheshi wa kimwingiliano na ucheshi wa kibeuzi. Namna hii ya uteuzi na uumbaji wa lugha ya ucheshi imejirudia katika ukurasa wa 43 ambapo jamii ya kijijini inaonekana kuamini kwamba mfumo wa maisha yao ndivyo ulivyo hata kwa mjini. Kwamba, hata ukitupa barua barabarani, watu huiokota na kuifikisha kwa mhusika au kuipeleka kwa wanaojua kusoma ili watoe maelekezo ya wapi anwani imeelekeza. Hali hii siyo rahisi sana kuikuta mjini. Tazama nukuu hapa chini: -

**Uruka:** Au tuandike barua tutume kwenye basi kama yeye anavyotutumia?

**Bi. Somoe:** *(Akiwa ni mwenye kukata tamaa).* Haitakuwa rahisi kuipata.

**Singilipo:** Si tunaandika Mata wa Manzese.

**Bi. Somoe:** Alisema kwamba angehama Mbagala kwenda Manzese. Sasa hatujui kama ameshahama au la.

**Uruka:** Ingekuwa Manzese ingekuwa rahisi. Tungeagiza waiweke hapo darajani na angeweza kuipata! (uk. 43)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Safari ya Chinga*, 2009)

Ukichunguza mazungumzo katika nukuu hii, utaona kuwa ni mazungumzo ya kiucheshi zaidi. Wazungumzaji wanazungumza kwa kujiamini na kudhani mawazo yao yako sahihi. Kumbe hali na mfumo wa maisha ya mjini ni tofauti kabisa na kile wanachokiwaza. Kupitia nukuu teule tunapata ucheshi wa kimazungumzo na ucheshi wa kitanzia. Mfano mwingine wenye kubeba ucheshi unaothibitisha tamthilia hii kujaa ucheshi, hasa ucheshi wa kimazungumzo, ucheshi wa kitanzia na ucheshi wa kizimbwe ni katika nukuu ya mazungumzo yafuatayo kati ya Mata na Ntumusha: -

**Mata:** Tukifika Manzese niambie. Kuna njomba wangu anakaa huko. Nataka ninsalimie na kula ugali wa nchana nyumbani kwake.

**Ntumusha:** Kwa leo na hapa tulipo haiwezekani. Ni maeneo mawili tofauti. Je, unajua njomba wako anakaa Manzese gani? Mana Manzese ni kubwa. Bila kujua alipo itakuwa ni ngumu kumpata.

**Mata:** Hapana sifahamu ila ntauliza tu kwa watu. Nimeambiwa anakaa kwa Nfuga Mbwa karibu na daraja.

**Ntumusha:** Kwa hapa njini sio rahisi... (uk. 30)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Safari ya Chinga*, 2009)

Nukuu hii inaonesha ya kwamba, mfumo wa maisha ya mjini ni maisha ya kila mtu kupambana na hali yake. Watu hawana ukaribu wala kutaka kujulikana. Kwa hiyo kama hupajui nyumbani kwake, na, au huna mawasiliano yake basi siyo rahisi kumpata mhusika. Ntumusha anaujua ukweli maridhawa juu ya ugumu huu. Kwa

vile hakumpa taarifa sahihi Mata tangu awali alipomshawishi Mata kuja mjini, basi kunamfanya Mata aonekane kichekesho katika mazungumzo yao kama ilivyokuwa kwa mazungumzo kati ya Mata na Bi. Somoe, na mazungumzo kati ya Uruka, Bi. Somoe na Singilipo. Kupitia nukuu hizi zote teule, tunapata ucheshi wa kimazungumzo, ucheshi wa kizimbwe, ucheshi wa kibeuzi na ucheshi wa kitanzia. Uteuzi na ujenzi wa wahusika ambao hawajawahi kuishi wala kufika mjini, kunawafanya waonekane kituko machoni pa watu wanaotambua mfumo wa maisha ya mjini.

Baada ya Mata kuzoea maisha ya mjini, hatimaye alitambua ukweli halisi punde tu hali yake huko mjini ilipozidi kuwa ngumu kuliko alivyokuwa ameaminishwa hapo awali. Kwa mfano, mojawapo ya kauli za awali za Mata ni pamoja na hii: - “Aha! Nakwambia town si nchezo. Yule (Hapa anarejelewa Ntumusha)<sup>7</sup> alienda mwaka juzi tu kama nchezo. Lakini leo ukincheki mambo yake yamenyooka. Town bwana hakunkatai ntu” (uk. 8). Kauli hii ni kichekesho machoni mwa mtu yeyote anayeyajua maisha halisi ya watu walio wengi waishio mijini. Baada ya kufika mijini, mambo yakawa ni tofauti na alichokuwa anafikiria awali. Hali hii inathibitika kupitia nukuu ifuatayo ambayo nayo inaibua ucheshi wa kimazungumzo, ucheshi wa kitanzia na ucheshi wa kizimbwe ufuatao: -

**Mata:** Naanza kuhisi njaa. Ningepata angalau kipande cha muhongo. Mana hatujatia kitu chochote tumboni.

**Ntumusha:** Mbona bado ni mapema? Ndo kwanza saa tano na nusu. Tusubiri tutembeee tembee kidogo ili tule chakula cha nchana moja kwa moja. Hapa ni njini lazima ubadilishe ratiba ya kula. Wengi hatuli kutwa mara tatu. Huwa

---

<sup>7</sup> Ufafanuzi katika mabano ni wa mtafiti.

tunafanya *diet*. Ukikaa mwezi tu utakuwa ushazoea maisha ya Bongo.

**Mata:** Unajua watu wengi wa vijijini tunafikiri maisha ya njini ni rahisi na mazuri sana.

**Ntumusha:** Ni kweli lakini kwa wachache tu. Si kwa kila ntu. Walalahoi wengi maisha yetu ndo kama hivi. Beba tu hivyo hivyo utazoea. (*Akimwonyesha mfuko*). Huu nfuko usiutupe. Jioni tukikaribia kufika nyumbani tutawekea nguo humu. Mi ntaani kwangu wala hawajui kama ni chinga, natembeza nguo barabarani. Wananiona tu asubuhi natoka, jioni naingia kama kuku. (uk. 27-28)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Safari ya Chinga*, 2009)

Nukuu hii inaonesha kuwapo kwa ucheshi unaotokana na majuto anayokutana nayo Mata baada ya kukutana na dhahama ya maisha ya mjini. Mawazo aliyokuwa nayo Mata kabla ya kuja mjini (uk. 8 – 10) ni tofauti kabisa na maisha aliyoyakuta huko mjini (uk. 27 – 28). Tofauti kati ya maisha ya mjini na vijijini na taarifa zinazotolewa kwa watu wa vijijini kunaongeza vichekesho kwa wasomaji. Kupitia nukuu teule tunapata ucheshi wa kimazungumzo, ucheshi wa kizimbwe, ucheshi wa kibeuzi na ucheshi wa kitanzia. Mfano mwingine wa ucheshi unaotokana na mafunzo aliyoyapata Mata huko mjini ni nukuu ifuatayo: -

**Ntumusha:** Ndo hivyo njini tunavyoishi. Maisha ni ujanja na kusaidiana. Ni kama zile nguo alizotupa Beka. Unauza na nnagawana pesa kidogo. Hivi ni baadhi ya vitu ambavyo vinatupatia faida.

**Mata:** Ikitokea siku tukagundulika na tajiri?

**Ntumusha:** Sio rahisi. Usiwe mwoga. Wenzako wanaiba mabilioni we unaogopa hivi vijisenti tu? Bila hivyo hapa njini hatuwezi kuishi. Ukikamatwa unalipa.

**Mata:** Baba alisema nisiibe. Wahenga pia hawatafurahi nikiwa na tabia hiyo. Inaweza kuniletea matatizo.

**Ntumusha:** Sisi hatuibi ila tunakula kazini. Na unakula kwa urefu wa si italikikamba yako. Mwizi ni yule anayetumia nguvu. (uk. 31-32)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Safari ya Chinga*, 2009)

Ukichunguza nukuu hii, utagundua imebeba ucheshi unaoonesha namna wizi unavyohalalishwa na kuwa jambo la kawaida na lenye tija kwa wezi husika. Kitendo cha mwandishi kubeba maneno haya “Sisi hatuibi ila tunakula kazini. Na unakula kwa urefu wa kamba yako. Mwizi ni yule anayetumia nguvu” ni ushahidi wa ucheshi unaobeba tafakuri. Kupitia nukuu hizi teule tunapata ucheshi wa kimazungumzo, ucheshi wa kizimbwe na ucheshi wa kitanzia. Mfano mwingine unaothibitisha kwamba tamthilia hii imejaa ucheshi katika kujadili mambo mazito yanayowakumba watu wa tabaka la chini ni kupitia mazungumzo kati ya Mata na Ntumusha. Haya yanathibitishwa kupitia data ifuatayo tunayoinukuu: -

**Mata:** Sawa. Lakini mi nina hamu ya wali.

**Ntumusha:** Mi hupenda sana makoko ya ugali. Ukiyatia nchuzi yanalainika vizuri na unashiba vizuri.

**Mata:** Sio magumu sana?

**Ntumusha:** Ukizoea siyo magumu. Kila kitu ni mazoea tu. Pia, bei yake ni rahisi. Shilingi mia mbili tu, wakati sahani ya wali ni shilingi alfu.

**Mata:** Ni kweli mazoea yana tabu.

**Ntumusha:** Na pia anauza ndaza.

**Mata:** Ndaza ndio nini?

**Ntumusha:** Chakula cha jana. (uk. 37)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Safari ya Chinga*,  
2009)

Katika nukuu hii, tunaona kuwa kauli za Ntumusha kwa Mata zinaibua ucheshi unaomfanya msomaji na msikilizaji kujikuta akicheka na kufurahi pasipo kupenda. Ntumusha anaonekana kutokuweka wazi changamoto zinazomkuta kijana asiye na mbele wala nyuma lakini asiyetaka kurudi kijijini. Ntumusha anaona ni mara mia abaki kuhaha mjini ambako akili yake itamsaidia kufanya biashara huku akipambana hivyo hivyo na changamoto za mjini. Katika hali ya kawaida, mtu hawezi kupenda ukoko wa ugali kama chakula chake kikuu. Ukweli wa kauli ya Ntumusha ni kumuandaa Mata kisaikolojia kwani kipato chao ni kidogo kukidhi mahitaji ya kula chochote wakipendacho. Badala yake, wale hata ukoko ili kutunza akiba na kukuza mtaji. Msomaji aliyemakini atang'amua mantiki ya Ntumusha na kujikuta akicheka.

Kinachochekesha ni ile maana ya ndani iliyomo katika kauli ya Ntumusha ya kumtambulisha Mata kuwa ni mtu asiyejua mbichi na mbivu kwa haraka, hasa katika eneo la falsafa ya ujasiriamali na maisha halisi ya mjini. Hapa tunabaini kuwapo kwa ucheshi wa kizimbwe na kwa namna fulani kuna uchezi wa kitanzia. Mwandishi kwa kutumia lugha ya ucheshi anaelezea changamoto zinazowakumba watu wasio na mbele wala nyuma. Kupitia nukuu teule tunapata ucheshi wa kimazungumzo, zimbwe na ucheshi wa kitanzia. Mfano mwingine wa ucheshi unajitokeza mahakamani, kama tunavyoona katika nukuu ifuatayo: -

**Mata:** (*Kwa haraka*). Mweshimiwa hakimu, mi nimekamatwa kibandani kwangu nikifanya biashara.

**Hakimu:** Kumbe kosa unalijua halafu unaleta mzaha.

**Mata:** Mweshimiwa hakimu, sidhani kama ni kosa kufanya biashara. Nilikuwa najitafutia riziki. Na riziki ni popote.

**Hakimu:** Kama riziki ni popote kwa nini usiuzie nyumbani kwako.

**Mata:** Njini nilikuwa nafata wateja.

**Hakimu:** Huoni kwamba ulikuwa unavunja sheria za jiji kifungu namba 005 cha mwaka 2008.

**Mata:** Sikubahatika kuzisoma. Kama sheria ningepewa nikazisoma, wala nisingezivunja mweshimiwa hakimu.

**Hakimu:** Kwa kuvunja sheria za usafi miji, unatakiwa kulipa faini ya shilingi laki moja. Au kifungo cha miezi mitatu jela na kazi ngumu.

**Mata:** (*Kwa huzuni*). Mweshimiwa hakimu sina uwezo wa kulipa faini. Ndio kwanza nilianza biashara. Na sina ndugu hapa njini. Na kama ni kazi ngumu afadhali niachiwe nikapalilie mikorosho yangu Kadengwa. Nna njomba wangu anaitwa Chupaku anakaa Manzese. Naomba nkantafute anilipie faini.

**Hakimu:** Kesi kama hii si ya kusikilizwa mara mbili. Umeshindwa leo kutoa faini unaenda ndani miezi mitatu. Ili iwe fundisho kwa vijana wengine wanaokimbilia mijini bila shughuli maalumu za kufanya.

**Mata:** (*Akilia na kupenga kamasi*). Mweshimiwa hakimu, naomba huruma yako. Kukaa kijijini kulima pia tumechoka. Nilikuja njini kutafuta kazi. Wazazi wangu kijijini wananitegemea. Sasa kibanda changu cha biashara kimevunjwa. Mali zangu zote zimepotea. Mweshimiwa

hakimu, nyie wa juu tusaaidieni. Sisi vijana wenu tunataabika. Hatuna kazi. (uk. 47 - 48)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Safari ya Chinga*, 2009)

Mfano huu ni mazungumzo kati ya Mata na Hakimu. Majibizano haya yanaonesha namna Mata alivyo katika kiwango cha chini cha uelewa wa mambo ya kisheria na uendeshaji wa mahakama. Kutokujua mambo na mifumo ya uendeshaji na maamuzi ya mahakama, hususani mahakama za nchi za ulimwengu wa tatu, kunamfanya Mata aonekane kituko, mkorofi, mbumbumbu, zuzu na limbukeni mbele ya hakimu na wasomaji wa tamthilia hii. Tukio hili limebeba simanzi na kwa upande mwingine limebeba ucheshi. Kupitia nukuu teule tunapata ucheshi wa kimazungumzo, ucheshi wa kizimbwe na ucheshi wa kitanzia. Ucheshi mwingine upo katika mifano ifuatayo:

-

**Bi. Somoe:** Baba Mata si ungenchinjia ntoto kuku anaondoka safari ya mbali?

**Che Mundu:** Pikeni tu chikandanga au ming'oko huko njini atakula sana nyama. Kuku atuachie sisi tuuze. (uk. 16)

**Mugambo 1:** (*Akimfuata Mata na kumpiga virungu usoni*). We ndo unajifanya jeuri eh.

**Mugambo 2:** Kama rinaleta ubishi mvunje unywele.

**Mugambo 3:** (*Ghafla anapigwa jiwe la kichwa*). Mamaa! (*Anagutilia huku akishika kichwa. Anajikakamua anawageukia vijana na rungu lake. Vijana wanakimbia*).

**Vijana:** (*Wakipiga kelele na kupora mali na kukimbia*). Ehe ehe ehe! Mwanangu leo ubweche! Kifo cha panzi... (*Vumbi limetanda. Sauti ya tingatinga inasikika*)



*ikiendelea kuvunja vibanda. Sasa linavunja kibanda cha Ntumusha).*

**Ntumusha:** *(Amesimama pembeni na baadhi ya vitu vyake. Amechanganyikiwa. Anaifuata sauti ya tingatinga inapotokea. Niueni niueni! Nasema niueni. (Akisema kwa uchungu). Hatuna kazi nyingine. Mnataka niende wapi? Au mnataka niwe mwizi? (Sauti ya tingatinga inazidi. Ntumusha bado amesimama. Sauti inazidi kuongezeka. Ntumusha anakimbia kwa hofu na woga. Anaanguka na kuanguka baadhi ya vitu alivyoshika. Anainuka na kukimbia huku akichechemea. Anatoka).*

**Vijana:** *(Wamejaa vumbi. Wanaokota mali za Ntumusha bila kuogopa tingatinga wala Mugambo). Zali mwanangu! Fasta! Fasta! (uk. 45 - 46)*

**(Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Safari ya Chinga*, 2009)

Data katika nukuu tuliyoiwasilisha hivi punde inaonesha kuwapo kwa ucheshi wa kitanzia ambapo jamii inajikuta ikiishia kumdharau na kumghiribu Che Mundu kutokana na matendo yake yasiyokuwa ya kiungwana na kiutu kwa mwanaye na familia (uk. 16). Ucheshi wa kitanzia pamoja na ucheshi wa kimazungumzo unajitokeza katika mazungumzo ya Mgambo 1, Mgambo 2 na Mgambo 3 na Vijana kama ilivyonukuliwa awali. Ucheshi wa kitanzia hutokea pale ambapo mhusika huyatenda au kuyanena mambo bila kutambua wale wanaomtazama wanamshangaa na kumsikitikia. Mhusika huamini yuko sahihi lakini matendo yake huwachochea watazamaji kumdharau na kuishia kumcheka au kumsifia kwa ghiribu. Wakati ucheshi wa kimazungumzo huzaliwa pale tu wahusika wa kifasihi wanapotumia dailojia yenye kauli zinazoamsha hisia za furaha, raha na vicheko katika muktadha

mahususi. Pia, kauli za Ntumusha dhidi ya mgambo zinaibua ucheshi wa kizimbwe na ucheshi wa kibeuzi.

Ucheshi zimbwe (au kibwege) ni ucheshi unaowakutanisha wahusika wenye viwango tofauti vya uelewa, ustaarabu na stadi zinazotokana na ujuzi na maarifa ya kitaaluma. Hivyo, mhusika mmoja aghalabu mwenye mamlaka hutenda na kunena kwa usahihi na ustaarabu kutokana na weledi wa kitaaluma wakati mhusika wa pili hutenda na kunena kwa wasiwasi, hofu, mashaka, mkanganyiko, makosa na kuonekana kuwa mgeni wa mambo mengi. Hii ni kutokana na kutokuwa na tajiriba, ujuzi, stadi na maarifa yanayoumbwa kupitia taaluma husika. Nao ucheshi wa kibeuzi hutokea baada ya mhusika kutambua ya kwamba kauli au tendo alilolifanya ni la kijinga au kizembe. Kwani, kiuhalisi asingeweza kulitamka au kulitenda kwa namna ile endapo angekuwa ametuliza akili na kutafakari kama mtu mwenye akili na utambuzi timamu kabla ya kuchukua uamuzi alioufanya.

Kwa upande mwingine, kipigo na ukali wa Mgambo kwa wamachinga, hasira za ukaidi na uzembe wa wamachinga (kwa mfano hasira za Ntumusha tunazoweza kuziita hasira za kuku au za mkizi), na vitendo vya vijana kukwapua mali za wavujajasho wenzao bila huruma kunatufanya tuseme tamthilia hii imebeba majonzi. Lakini, majonzi hayo kwa wengine ni burudani. Nukuu zote tulizoziweka katika mjadala huu zinathibitisha kuwapo kwa matumizi makubwa ya lugha ya ucheshi ndani ya tamthilia ya *Safari ya Chinga*. Picha tunayoipata hapa ni kwamba, bila shaka, kama mhakiki mwingine akiisoma kwa utulivu kazi hii, si ajabu mhakiki huyo akaja na idadi kubwa zaidi au ndogo ya kiwango tulichokibaini cha mdafoa wa utokeaji wa ucheshi wa 63. Idadi hii ya utokeaji wa matumizi ya semi ni zaidi ya

wastani wa asilimia 50. Hiki ni kiwango kikubwa zaidi cha mdafoa wa matumizi ya lugha kwa kulinganisha na hali ya mdafoa katika tamthilia nyingine tano (5) tulizozichunguza katika utafiti wetu - *Mashetani, Kijiji Chetu, Harakati za Ukombozi, Changamoto na Nje – Ndani*.

Kupitia uchunguzi tuliofanya, tumebaini ya kwamba, mdafoa wa kiwango hiki umetokana na uteuzi wa wahusika wengi kutoka jamii ya watu wa kusini mwa Tanzania hususani Wamakonde. Ambapo, Kiswahili chao hubeba baadhi ya matamshi na lafudhi ya lahaja ya Kimgao inayovutia masikioni mwa wasikilizaji. Vilevile, kundi kubwa la wahusika ni vijana ambao hawakubahatika kupata elimu rasmi. Tena, vijana hawa wako katika mazingira duni. Hawana mbele wala nyuma. Lakini wanaonekana ni watu wenye ndoto za kulala masikini na kuamka asubuhi wakiwa matajiri. Hivyo, daima kundi hili la vijana hukaa kungoja bahati ya mtende kwa kujifariji kutokana na kile wanachokisikia au kukiona kwa vijana wachache waliobahatika kubadili historia ya maisha yao. Vijana hawa wako tayari kufuata njia halali au zisizohalali, mradi tu wafanikishe ndoto zao.

Zaidi, tumebaini ya kuwa uteuzi mzuri wa mandhari, muktadha, mazingira, aina ya wazo alilolikusudia mwandishi, ploti, aina ya hadhira aliyoilenga mhusika na wakati unaoibeba tamthilia hii na matukio aliyoyajenga mwandishi, vinaifanya tamthilia hii kuwa na matumizi makubwa ya lugha ya ucheshi. Changamoto pekee inayoweza kujitokeza kwa wasomaji wasio makinikia jambo, pindi wakutanapo na kazi ambazo zina utajiri mkubwa wa lugha ya ucheshi, daima hujikuta wakishindwa kuweka mizani sawia kati ya dhamira na fani. Kwani wao kujikuta wakiburudika zaidi na kuiona kazi ya namna hii kuwa ya kuburudisha (kifutuhi / kivichekesho) badala ya

kujifunza mambo mazito yaliyowasilishwa kupitia ufutuhi huo (Nell, 1988). Kwa kuwa, binadamu huweza kuchagua cha kuchota kutokana na hali inayomtawala na kumdhibiti kwa muda mrefu (Bandura, 1977).

Katika mazingira ya namna hii, bila shaka lengo la mwandishi litakuwa limeshindwa kuifikia jamii (endapo lengo hilo lilikuwa ni kuifundisha na kuihabarisha jamii juu ya changamoto zinazowakabili wananchi wa tabaka la chini. Kwa maana kwamba, hii ni sababu mojawapo ya uhamaji holela wa watu kutoka vijijini kwenda mijini.). Lakini, kama lengo la mwandishi litakuwa ni kutoa burudani kwa wasomaji, basi lengo hilo litakuwa limefanikiwa. Endapo wasomaji wataburudika zaidi kuliko kufyonza mafunzo yaliyomo katika tamthilia, basi kuna uwezekano kwa baadhi ya wasomaji wakaihesabu tamthilia hii ya *Safari ya Chinga* kuwa ni tamthilia ya kifutuhi au ucheshi. Huku wakisahau kubeba dhamira zilizomo ndani ya ucheshi huo. Kwa uchunguzi wetu, tunaona mwandishi wa tamthilia hii imetumia lugha ya ucheshi kwa umakini wa hali ya juu kiasi cha kutokuyafunika maudhui. Yaani, msomaji wa tamthilia hii hawezi kuishia kuburudika peke yake pasipo kujifunza jambo. Msomaji ataburudika huku akiendelea kuvuna mafunzo kila anapoburudika.

Jambo hili limetambuliwa na wanataaluma kadhaa wakiwemo Mlama (2003), Semzaba (2003) na S. M. A. Massoud (2013) punde wanapoitazama tamthilia yenye kubeba ucheshi. Mathalani, S. M. A. Massoud (2013) anasema kwamba, watu wengi wanadhani dhima ya ucheshi ni kuburudisha pekee lakini usahihi ni kuwa ndani ya ucheshi, maudhui ya dhati yanapatikana. Mfano wa maudhui hayo ni ubaya wa matabaka, athari za sayansi na teknolojia na kadhalika. Hoja ya S. M. A. Massoud (2013) inathibitisha kuwapo kwa changamoto ya walaji kujikuta wakifurahi na

kudhani ya kwamba tamthilia zenye ucheshi haziwezi kuwa na mafunzo mazito kwa jamii. Kumbe ukweli ni kwamba, hata tamthilia zenye ucheshi mwingi hubeba mambo mazito yanayoihusu jamii husika. Kwa hiyo basi, wasomaji hawana budi wanaposoma tamthilia za namna hii kuhakikisha wanafurahi huku wakifyonza mafunzo yaliyomo ndani ya tamthilia husika. Kwa sababu, ndani ya utamu mna mafunzo pia.

Wasomaji wanapaswa kutambua pia, watunzi wa kazi bunilizi za kitamthilia huwa hawakurupuki katika kuteua na kuumba lugha itakayobeba maudhui yanayotawala utunzi na uwasilishaji wa kazi husika kwa wasomaji (Wafula, 1999). Ucheshi ni njia nzuri inayomsaidia mwandishi kuliumba wazo lake pasipo hofu yoyote ya kukutana na mkono wa chuma wa mtawala asiyependa kukosolewa wala kuambiwa ukweli. Kwani, uhuru wa mwandishi bado haujawa huru kwa kiwango cha yeye kuwaza na kunena kwa kiwango akitakacho katika kujiamini (Kezilahabi, 1993; Ruhumbika, 2006). Kwa hiyo, matumizi makubwa ya ucheshi, kejeli na taswira ni siha kwa mwandishi anayetafuta uhuru katika kuliumba wazo linalolenga kulikosoia tabaka tawala. Kwa kuwa, hata mtawala huishia kufurahi na kuisifia kazi husika pasipo kujihesabu kuwa mmoja wa wahusika waliolengwa ndani ya mchezo husika. Mtawala huyo hatajiona kuwa mlengwa lakini atajifunza kuwapo kwa watu au watendaji wasiotenda haki na wajibu wao kama inavyowapaswa kuenenda. Ijapokuwa, mtawala huyo anaweza asitilie maanani ujumbe aupatao. Hasa, kama ujumbe huo umewasilishwa kwa njia ya kumdhihaki mtawaliwa aliyechini ni ya nira ya utumwa.

Hoja hii inaungwa mkono na Semzaba (2003) anapotathmini historia na maendeleo ya Tamthilia ya Kiswahili. Semzaba akinukuliwa na S. M. A. Massoud (2013) anasema, “maigizo ya mlengo huu hayakuwatia hofu watawala kwani yaliwaonesha Waafrika jinsi ambavyo hawajaendelea kuwasilisha maigizo yao kwa mtindo faraguzi. Na kwamba, maigizo haya yaliishia kuchekesha hadhira na kuacha kuzungumzia matatizo ya msingi yaliyomkabili mtawaliwa” (uk. 31). Semzaba anatuonesha kihistoria, aina hii ya tamthilia (futuhi) ilikuwapo kwa sababu ya hofu ya tabaka tawala la wakoloni Waingereza na vibaraka wao. Matokeo yake, ujumbe uliokusudiwa na waandishi ukawa hauifikii jamii lengwa. Hivyo, kushindwa kuwa msaada kwa watu wa tabaka la chini.

Hivyo, siyo busara hata kidogo kwa watunzi kutumia lugha yenye kujaa ucheshi mwingi ili kuepuka wasomaji wakiwemo walengwa kuishia kucheka badala ya kujifunza changamoto zinazowakuta watu wa tabaka la chini. Pamoja na hatari inayoweza kuwakuta walaji wa kazi hii, bado tunaona ya kuwa mwandishi hajajaza ucheshi kwa asilimia 100. Kwa mantiki hii, tunagundua ya kwamba, mwandishi ametumia lugha ya ucheshi kwa kiwango ambacho hakisababishi asilimia kubwa ya dhamira kufunikwa na vichekesho. Kwa mantiki kwamba, kiwango na namna ya matumizi ya kicheko huweza kuwa ni ishara ya kuwapo kwa mtu, jambo au kitu fulani. Hivyo, kupitia uchekaji maalumu na makini mtu anaweza kubaini uwezekano wa hali, jambo, kitu au mtu kuwapo au kutokea (Peirce katika Short, 2007).

Kwa upande wa tamthilia ya *Changamoto*, utafiti ulichunguza na kubaini kuwa, tamthilia hii imetumia lugha ya ucheshi kwa mdafao wa 38 kutokana na kuwapo kwa utokeaji wa aina tano (5) za ucheshi. Huku ucheshi wa kitanzia ukitawala zaidi

kuliko aina nyingine za ucheshi. Matokeo ya uchunguzi wa utokeaji wa lugha ya ucheshi katika tamthilia ya *Changamoto* unawasilishwa kimuhtasari kupitia Jedwali

5.5 lifuatalo: -

**Jedwali 5.5** Mdafao wa Utokeaji wa Lugha ya Ucheshi katika *Changamoto*

N/M	Aina ya Ucheshi	Kurasa Zilizobeba Ucheshi	Mdafao wa Utokeaji
1.	Kimazungumzo	1, 2, 10, 11, 12, 18, 22, 26, 33, 34	10
2.	Kibeuzi	4	1
3.	Kitanzia	5, 8, 13, 14, 15, 17, 20, 23, 24, 27, 28, 30-31, 37, 38	14
4.	Zimbwe	13, 15, 22, 28, 30-31,	5
5.	Kimwingiliano	1-2, 3, 16-17, 18-19, 20-21, 30-31, 35-36, 37-39	8
<b>Jumla ya Utokeaji wa Lugha ya Ucheshi</b>			<b>38</b>

**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Changamoto*, 2018

Jedwali 5.5 linaonesha mdafao wa uteuzi na uumbaji wa matumizi ya lugha ya ucheshi katika tamthilia ya *Changamoto*. Matokeo ya utafiti yanaonesha kiwango cha 38 cha utokeaji wa lugha ya ucheshi ambapo ucheshi wa kitanzia unaonekana kujitokeza zaidi kuliko aina nyingine za ucheshi. Ucheshi wa kimazungumzo unaonekana kufuatia kwa kiwango cha utokeaji huku ukifuatiwa kwa karibu na ucheshi wa kimwingiliano. Kiwango cha jumla cha utokeaji wa lugha ya ucheshi ni chini ya asilimia 50 jambo linaloonesha ya kwamba tamthilia hii haina ucheshi mwingi. Utafiti umebaini ya kwamba hali hii imetokana na athari ya uteuzi na uumbaji wa wahusika na maudhui. Sehemu kubwa ya tamthilia hii imejengwa juu ya mateso na changamoto wanazozipata wahusika wenye ulemavu wa viungo tofauti tofauti kutokana na matendo na kauli za wahusika wasio na ulemavu.

Aina hii ya uteuzi na uumbaji wahusika inajenga hisia kali ya hasira, huzuni na chuki kwa msomaji mwenye utu na busara. Kamwe mtu makini hawezi kufurahia kundi



moja kuonekana kunyanyapaliwa na kutendewa unyama na kundi jingine ambalo halijui kesho yake itakuwaje kimaumbile. Mateso wanayoyapata watu wenye ulemavu ni mazito sana. Hata hivyo, kwa jicho jingine, msomaji anaweza kusahau shida za watu wenye ulemavu na kujenga picha ya tukio halisi. Hatimaye atajikuta akitabasamu au kucheka mara kadhaa bila hiari yake - kabla ya kurudia huzuni na, au hasira. Hali hii itamkuta kwa sababu ndani ya tamthilia ya *Changamoto* mna mambo yanayobeba matukio yenye ucheshi japo yanaambatana na majonzi.

Mambo hayo ni pamoja na tukio la watu wenye ulemavu kufurahia hotuba na dhifa ya Malkia wao ilhali baada ya dhifa hiyo wanajikuta wakirudia mateso yao (uk. 2 - 3). Tukio jingine ni tukio la namna Mpitanjia alivyohangaika kumpandisha Megno (mlemavu wa viungo- miguu bila shaka) katika jengo lenye ghorofa kadhaa. Halafu, akajikuta akichoka na kushindwa kuzuia baiskeli ya Megno hali inayosababisha wote wawili kuporomoka kutoka ngazi za ghorofa ya pili hadi chini kwenye ngazi ya kwanza walipoanzia (uk. 4 - 5). Tukio jingine ni la Peti (msichana mlemavu wa macho) kuwaongoza wenzake kwenda kupata haki ya elimu ya sekondari na haki ya kisheria lakini wakaishia kutendewa ubaya (uk. 7 - 9, 22 - 28).

Haya ni matukio machache katika mengi ambayo watu wenye ulemavu wanakutana nayo kama sehemu ya changamoto kutokana na hali ya maumbile yao. Sehemu kubwa ya wanajamii wasio na ulemavu wanaonekana kuwatendea vibaya watu wenye ulemavu kwa sababu ya kukosekana kwa uelewa, utu, busara, haki na usawa. Pamoja na changamoto hizo, bado tunaona baadhi ya watu wenye ulemavu wakiwa na ujasiri wa kutetea haki, heshima na thamani yao, pasipo kujali hali zao. Matokeo ya ujasiri huo ni kuonekana kituko na kichekesho kwa watazamaji / wasomaji

wanaoayaona matambo hayo kama yenye kujaa dhihaka na dharau sawa na dua la kuku mbele ya mwewe. Jambo hili limekabidhiwa kwa Peti ambaye anaonekana kuwa mkali, mwenye kujiamini na kujifanya kujua na kutaka kile akitakacho kiwe. Hata pale ambapo kiuhalisi inaonesha nguvu zake za kutumia mdomo kuagiza na kukaripia hazitamsaidia zaidi ya kumuumiza. Mfano wa matukio ya namna hii yanaonekana kupitia nukuu ifuatayo: -

**Katibu Muhtasi:** Ondokeni msinisumbue. (*Huku akikunja sura*)  
Ondokeni hapa!

**Peti:** Hivi wewe, (*akinyamaza kidogo*) unajua kilichotuleta hapa?

**Katibu Muhtasi:** Wala sihitaji kukijua.

**Peti:** Hebu twende kwa Mkuu, huyo achana naye!  
(*Peti akianza kuondoka, hajui anakoelekea. Anatafutatafuta na fimbo yake ya kutembelea.*)  
Hebu nionyeseni mlango uko wapi?

**Msomaji:** (*Baada ya kusoma mlango*) Hapa. (*Wanaenda na kugonga mlango wa Mkuu wa Shule*)

**Mkuu wa shule:** Ingia!

**Peti na Msomaji:** Shikamoo.

**Mkuu wa shule:** Marhaba. Mnataka nini?

**Peti:** (*Akiguna*) Mmh! Hata hutukaribishi viti kwanza?

**Mkuu wa shule:** Nawauliza mnataka nini?

**Peti:** Nataka kujiunga na shule hii.

**Mkuu wa shule:** (*Akisimama na kuanza kuwasukuma Meliza, Peti na Msomaji wa Peti*). Haya ondokeni upesi, hatupokei watu kama nyie.

**Peti:** Tutasoma wapi kama ndio mnatufanyia hivi?

- Mkuu wa shule:** Hamnielewi? Mnataka nifungulie mbwa awang'ate? (*Anawatisha*) Niwafungulie mbwa awatoe steki sasa hivi?
- Peti:** Hapana, tunaondoka baba usimfungulie. (*Peti akiongozwa na Msomaji wake pamoja na Meliza wanaondoka, Mwalimu Mkuu anatoka ofisini kwake na anamwendea Katibu Muhtasi*).
- Mkuu wa shule:** (*Anaongea kwa ukali*) Nani amekuambia uwaruhusu hawa?
- Katibu Muhtasi:** (*Akionyesha woga*) Wameingia kwa ubishi na dharau, sikuwaruhusu.
- Mkuu wa shule:** Nisiwaone tena ofisini kwangu.
- Katibu Muhtasi:** Sawa... (uk. 8 - 9)
- (**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Changamoto*, 2010)

Tunapoichunguza data hii ya nukuu, tunaona kuwa inathibitisha namna Peti anavyojiamini na kuutumia mdomo kupambana na yeyote anayeonekana kumdharau au kuwadhibiti watu wenye ulemavu. Juhudi zake ni katika harakati zao za kusaka heshima, thamani, utu na haki ya kuishi na kutenda sawa na mwanadamu mwingine asiye kuwa na ulemavu. Tabia ya Peti ambaye ni msichana mlemavu wa macho kugeuka mtoa amri na kiongozi wa wenzake kunaibua hisia ya ukiherehere na kicheko. Ujasiri wake unakoma punde alipofokewa na Mkuu wa shule. Hali hii inajenga huruma na wakati huo huo hali ya ucheshi akilini mwa msomaji. Ujenzi wa mhusika Peti umejaa ucheshi kiasi cha kuleta burudani na majonzi kwa wakati mmoja. Hivyo, kuzalisha ucheshi wa kimazungumzo na ucheshi wa kitanzia. Mfano mwingine unaoonesha tabia ya Peti ya kujiamini kupita kiasi kwa mdomo kuzungumza bila breki wala kujitathmini na kutoa vitisho kama mbwa muoga

mwenye kubweka wakati adui akimsogelea hujikuta akiufyata mkia na kutokomea kusikojulikana, ni huu ufuatao. Data ifuatayo inathibitisha haya tuyasemayo: -

**Peti:** (*Anapapasa sakafu kwa fimbo nyeupe ya kutembelea*)  
Hapa ni wapi Meliza?

**Meliza:** (*Anamwangalia tu hasemi kitu, mara anashituka anapomwona Chaazye*) Chaazye yulee! (*Akimwonyesha kwa kidole*).

**Peti:** (*Anapapasa mikono yake hewani akimtafuta Chaazye ili amguse*). Wewe Chaazye hebu njoo nikuone ulivyovaa.

**Chaazye:** (*Kwa utani*) Utanionaje Peti wakati wewe huoni? Kipofu!

**Peti:** (*Kwa hasira*) Kwenda zako, mimi ni ‘Asiyeona’  
Siyo Kipofu. Ebo! Utaelimika lini?

**Chaazye:** Basi bwana yaishe. Leo nimevaa nguo unayoipenda sana.

**Peti:** Hebu njoo nikuone jamani Chaazye (*Chaazye amemshika Peti mikono. Peti anampapasa kuanzia kichwani*) Ebo! Wewe (*akiendelea kupapasa*) Eeh! Ndiyo umevaa tai. (*Anashikashika tai aliyoivaa Chaazye*). Nzuri hivyo? (uk. 22)

**Meliza:** Mmh! [...] mtu huyu anaonesha ana wasiwasi, kama jambazi vile.

**Peti:** Ni nani huyo hebu nimshike (*akipapasa hewani kutaka kumshika*) Yuko wapi?

**Megno:** Habari yako mzee!

**Kimweri:** Nyie vilema mnangoja nini hapa?

**Peti:** Koma! Kilema ni wewe. Sisi sio vilema, sisi ni walemavu.

**Kimweri:** Sasa unakataa nini? Tena wewe una dhambi sana ndiyo maana macho yako yamefumbika! Lione kwanza.

**Peti:** (*Akicheka kwa kejeli*). Hee! Ungejua sikununua upofu? Hongera zako uliyewekeana mkataba na Mungu!

- Kimweri:** Tena wewe ndio unajidai sana (*Akampiga mweleka Peti*).
- Peti:** Mama wee! Nafaa...
- Kimweri:** Tena lete hii. (*Akiupokonya mkoba na kuanza kukimbia, akiufungua*). Siye tuna shida nyie mna pesa zote hizi umezipata wapi wewe kilema?
- Peti:** Wewe laana yako! Na hutaendelea kamwe!
- Kimweri:** Na wewe unasemaje? (*Akielekea alipoketi Megno*) Hamjakoma tu?
- Megno:** Sasa unataka nini? Sema!
- Kimweri:** Wewe kiwete utanifanya nini? (*Akambinua kutoka kwenye baiskeli yake*)
- Megno:** Jamani! Nauawaa! (*Anagaragara chini; Kimweri anachukua baiskeli, anaikunja kunja na anajitwika kichwani na kukimbia nayo*).
- Meliza:** (*Anashangaa shangaa tu hasikii lolote*) Hapa akitukuta Masumbuko, mbona tutakoma!
- Peti:** Aaa! Aishie zake huko! Japo sioni, lakini akija tutashirikiana kumvuta madodoki yake, wee mwache aje.
- Megno:** (*Akiwashangaa*) Masumbuko ni nani?
- Peti:** Chizi mmoja, anasifika sana kwa kubaka wanawake, ngoja aje tutamshikisha adabu zake. (uk. 22, 23-24, 26)
- (**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Changamoto*, 2010)

Data hii ni malumbano. Malumbano haya yanaonesha namna Peti anavyojikakamua kama ishara ya kukataa unyonge na dharau inayosababishwa na utamaduni mbaya uliokita mizizi katika jamii. Peti anayapinga majina wanayoitwa watu wenye ulemavu ambayo yanaudhalilishaji na anapendekeza majina sahihi. Mbali ya hali ya kutokuona, bado yuko tayari kupambana na yeyote anayetaka kumnyanyasa,

kumdhulumu ama kumuonea yeye au mlemavu mwingine. Kauli za Peti na matendo yanayotokea katika mapambano husika dhidi yake na kwa watu wenye ulemavu wengine yanaibua huzuni, hasira dhidi ya wadhulumati lakini pia ucheshi. Kwani “ubabe” uliomo kinywani mwa Peti hauendani na uhalisi wa uwezo wake wa kupambana na yeyote mwenye nia ova dhidi yake na wenzake.

Ubabe huu wa Peti unamfanya aonekane sawa na debe tupu. Hivyo, kumfanya msomaji asiyebeba maumivu halisi ya ulemavu kujikuta akiangua kicheko kabla ya kurudia masikitiko na hasira. Huu ni ubunifu wa kipekee katika kujenga mjadala unaohusisha changamoto pasipo kusahau kujenga burudani yenye kiasi. Mfano mwingine unaofanana na tukio la Peti na wenzake kutendewa ubaya lakini kunaibuka ucheshi wa kitanzia ni lile la Maimatha kufaulu usaili kwa njia ya simu ilhali anayemsaili hajui hali ya maumbile ya Maimatha. Awali, msaili hakutaka kujua habari yoyote ya maumbile ya binti huyu. Lakini anaporipoti kazini ili kuanza kazi, anakutana na unyanyapaa kiasi cha kunyimwa ajira na kufukuzwa ofisini kama mbwa. Data ifuatayo inawasilisha ushahidi wa kile kilichothibitishwa na utafiti huu:

-

**Maimatha:** Jina langu ni Maimatha Godwin. Mwajiriwa mpya wa hapa ofisini kwenu. Jana nilipigiwa simu na Mkuu wa Shule na aliniambia nije leo kuripoti.

**Katibu Muhtasi:** (Kwa mshangao) Alikupigia wewe?

**Maimatha:** Ndiyo.

**Katibu Muhtasi:** Anti umepotea siyo hapa.

**Maimatha:** Tafadhali anti, niruhusu nikamwone mhusika.

- Katibu Muhtasi:** *(Akionyesha mlango kwa kidole bila kuongea kitu. Maimatha na Godwin wanakwenda kugonga mlango walioonyeshwa. Wanafungua na kuingia ndani).*
- Mkuu wa Shule:** *(Kabla hawajasalimiana wala hawajaketi anaongea nao kwa jazba)* Mmefuata nini ofisini kwangu?
- Maimatha:** Samahani Mheshimiwa. Hata hukupenda kusalimiana nasi japo ujue kilichotuleta?
- Mkuu wa Shule:** Jamani hapa hatutoi misaada kwa walemavu. Ondokeni kabla sijafungulia mbwa.
- Godwin:** Hebu acha wazimu wewe Mzee. Ninyi ndio wasomi mnaoteketeza kodi zetu halafu hamwelimiki! Msomi kama wewe usingetarajiwa kuongea upuuzi kama huo. *(Akiongea kwa ukali)* Aliyekuambia tumekuja kuomba msaada ni nani?
- Mkuu wa Shule:** Haya, semeni shida iliyowaleta.
- Maimatha:** Mimi ni Maimatha Godwin. Nilizungumza na wewe jana kwenye simu kwa ajili ya kuja kuanza kazi rasmi.
- Mkuu wa Shule:** *(Akisimama kwa mshangao)* He! Ni wewe niliyeongea nawe kwenye simu jana?
- Maimatha:** Ndiyo, ajabu iko wapi?
- Mkuu wa Shule:** Hapana. Haiwezekani kabisa.
- Maimatha:** Kwa vipi?
- Mkuu wa Shule:** Hatuwezi kukuajiri. Wewe ni mlemavu.
- Maimatha:** *(Akiongea kwa mshangao)* Ulemavu wangu unahusiana vipi na kazi nitakayoifanya?
- Mkuu wa Shule:** Nimesema hapana. Ondoka kwenye ofisi yangu. (uk. 13 - 14)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Changamoto*, 2010)

Kupitia data ya utafiti tuliyoinkuu hapo hivi punde, tunabaini kuwa malumbano yanayojitokeza hapa yanaonesha matokeo hasi anayokutana nayo Maimatha na Godwin tofauti na hali ilivyokuwa wakati wa usaili na maandalizi ya kwenda kuripoti tayari kuanza kazi (uk. 11 - 12). Tunapopiga picha ya mtu mwenye furaha na kujiamini ambaye anatumia ubabe kuruka kihunzi cha Katibu Muhtasi kwa imani kwamba bosi atampokea kwa mikono miwili; mara anajikuta akiambulia matusi, dhikaka, kejeli, na vitisho kutoka kwa aliyeaminiwa kumsitiri mnyanyaswaji! Bila shaka, kwa mtu kama Katibu Muhtasi huku kutakuwa ni kicheko na kusonya. Ilhali kwa Maimatha, Godwin na wasomaji wanaopenda usawa watajisikia kulowa aibu, hofu na huzuni kiasi cha kutamani ardhi ipasuke ili wazame kuficha nyuso na hali zao. Ndiyo maana tunaona ya kwamba tukio hili limebeba ucheshi wa kitanzia.

Kwa jumla, mifano tuliyoiweka kama nukuu katika kujenga uthibitisho wa madai ya kuwapo kwa ucheshi mwingi wa kitanzia kuliko aina nyingine za ucheshi, ni ushahidi tosha kwamba mwandishi hakukosea katika kuteua maeneo machache na kuyapa ucheshi. Endapo mwandishi angejaza ucheshi, hasa ucheshi wa kimazungumzo usiobeba huzuni, maumivu wala uzito wa changamoto anazozipitia mlemavu, sina shaka kwamba wasomaji wangeishia kuburudika zaidi pasipo kuguswa na madhila ya watu wenye ulemavu. Na kwamba, lengo la kuleta ukombozi wa kweli na endelevu kwa faida ya jamii ya watu wenye ulemavu na jamii ya wasio na ulemavu lisingekuwa limefanikiwa. Kwa hiyo mwandishi ameonekana kuumba mawasiliano ya kisanaa yanayomtetea mlemavu na kumsuta mtu asiye mlemavu mwenye tabia chafu dhidi ya mtu mwenye ulemavu. Haya yote ameyajenga kwa



ubunifu wenye kuchanganya madhila na ucheshi kiasi – ama kwa kujua au kutokujua.

Kwa upande wa *Nje-Ndani*, utafiti wetu umebaini kuwapo kwa matumizi ya lugha ya ucheshi kwa kiwango cha kutosha. Ucheshi mkubwa upo katika matumizi ya lugha ya ucheshi wa kimwingiliano kuliko aina nyingine za ucheshi. Mdafao wa utokeaji wa lugha ya ucheshi katika *Nje-Ndani* unawasilishwa kimuhtasari kupitia Jedwali 5.6 lifuatalo: -

**Jedwali 5.6** Mdafao wa Utokeaji wa Lugha ya Ucheshi katika *Nje-Ndani*

N/M	Aina ya Ucheshi	Kurasa Zilizobeba Ucheshi	Mdafao wa Utokeaji
1.	Kimazungumzo	7, 13, 15, 40, 65, 72-73, 76, 84	8
2.	Kibeuzi	37, 62	2
3.	Kitanzia	57-58	1
4.	Zimbwe	25-26, 52-53, 85-86	3
5.	Kimwingiliano	1-2, 3-4, 5-6, 11-13, 15-16, 17-18, 19-20, 21-22, 24, 28-29, 30-33, 37- 38, 39-40, 43-45, 47-48, 51-53, 54- 57, 58-60, 61-62, 63-64, 65-66, 67- 68, 69-70, 71-72, 73-74, 75-76, 83- 84, 85-87	28
<b>Jumla ya Utokeaji wa Lugha ya Ucheshi</b>			<b>42</b>

**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Nje-Ndani*, 2018

Jedwali 5.6 linaonesha mdafao wa uteuzi na uumbaji wa matumizi ya lugha ya ucheshi katika tamthilia ya *Nje-Ndani*. Matokeo ya utafiti yanaonesha ya kuwa, tamthilia ya *Nje-Ndani* imejaa ucheshi wa kimwingiliano zaidi ya aina nyingine za ucheshi. Matumizi ya lugha ya ucheshi wa kimwingiliano yanabainika kiurahisi katika tamthilia hii, endapo tu, msomaji anajua na kufuatilia matukio ya kihistoria na

kijamii yaliyotokea na yanayotokea katika jamii mathalani jamii ya Kitanzania. Ushahidi wa hoja hii unapatikana katika mifano teule michache katika mingi iliyomo kitabuni. Tunanukuu: -

**Utashi-Nafsi:** Afrikani...  
 Wa rozali, vikofia na vilemba...  
 [...]  
 ... beburu... makuwadi... (uk. 1 - 2)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Nje-Ndani*, 2016)

Nukuu hii inaonesha lugha ya ucheshi kwa yeyote anayeyaelewa maneno na nafasi ya uundaji wa kejeli na misimu katika jamii. Mtu huyu punde akutanapo na kauli ya namna hii, hatuna shaka ya kwamba atajikuta anaanza kucheka kabla ya kutafuta mantiki ya mwandishi kuyatumia. Sababu ya kucheka ni kutokana na maneno kama vile “wa rozali,” “vikofia na vilemba” atatambua ni mtu gani anayerejelewa hapa. Maneno haya yanawarejelea viongozi wa kidini na watawa hasa wale wa Kikristo wanaotumia kofia maalumu (maaskofu), rozali (Wakristo aghalabu Wakatoliki), na vilemba (watawa wa kike). Huu ni mfano wa ucheshi wa kimwingiliano uliodhahiri kabisa.

Ucheshi wa kimwingiliano unatokana na msomaji ama msikilizaji au mtazamaji kuyang’amua matini chanzi yaliyochopekwa katika matini anayoyasoma au kuyarejelea. Kitendo cha kuyang’amua humfanya ajione kuwa ni mtu makini, mwerevu na mjanja kumshinda au kuwa na hadhi sawa au zaidi ya mtunzi aliyeyatumia matini teule hivyo kuishia kucheka na kujihisi mwenye raha sana (Wamitila, 2008). Mfano mwingine unaoonesha kuwapo kwa ucheshi wa

kimwingiliano ni huu ufuatao tunaonukuu majadiliano kati ya Macho, Moyo na

Akili: -

**Macho:** [*Kwa upole na ufukunyuzi*], Vipi mmeanza kuchimba?

**Moyo:** Kuchimba kitu gani?

**Macho:** Mali ya ardhini.

**Moyo:** Aaaaah! Viazi, mbona kitambo?

**Macho:** Hongereni sana.

**Moyo:** Kwa lipi tuhongere? Hatupiki wala hatuli zaidi ya kupakua.

**Moyo:** Hata hivyo, viazi vyenyewe si vingi kwa wote. Sisi wengine faida tuiapatayo ni mashimo kwa ajili ya kujengea vyoo vyetu baada ya viazi kuchimbwa.

**Macho:** Hata kule nilikotoka hakuna tofauti kubwa na hapa.

**Akili:** Kama twiga na faru.

**Akili:** Haya ndovu na pembe zao

**Moyo:** Wamefanyaje?

**Akili:** Wanapaa.

**Akili:** Afadhali mashimo, hawa si mkia, si ngozi, si kwato.

**Moyo:** Ubeberu.

**Akili:** Ubeberu wa mbuzi au kondoo?

**Moyo:** Si mbuzi wala kondoo. Ni makuwadi wa soko holela. Hula njama na wanyonyaji. Sasa ili uwalinde basi wahitajika kuwa watu.

**Moyo:** Haya baada ya hapo faida gani kubwa yaja?

**Akili:** Kujipendekeza tu. (uk. 72, 73, 74, 75)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Nje-Ndani*, 2016)

Data za utafiti katika nukuu hii zinaonesha kauli zilizojaa mafumbo. Kwa mtu anayesoma nukuu hii kwa utulivu kisha akatazama matukio yanayotokea katika

jamii, atakumbuka kelele zinazopigwa na wananchi wazalendo dhidi ya wawekezaji katika sekta ya madini wanavyovuna madini. Taarifa zinaonesha jamii zinazozunguka migodi katika nchi nyingi za ulimwengu wa tatu huambulia mashimo, vumbi na miradi midogo midogo ya kijamii isiyoendana na mali zinazovunwa (SID, 2009; Poncian na George, 2015; United Nations Economic Commission for Africa, 2016). Kwa hiyo, Mtanzania anayejua ukweli huu, halafu akakutana na kazi bunilizi iliyochopeka tatizo halisi linaloikabili jamii; kwa hakika, atajikuta akiifurahia kazi husika na kumkubali mwandishi kuwa ameitendea haki jamii na sanaa inayotambulika kama kipaza sauti cha mnyonge.

Vilevile, nukuu hii inatukumbusha tukio lililotokea nchini Tanzania mnamo saa saba za usiku wa Novemba 26, 2010 na kuripotiwa na gazeti la *Raiamwema* la Juni 01, 2012. Tukio hilo lilihusisha ndege ya Jeshi la Anga la Qatar almaarufu kama Qatar Emir Air Force. Gazeti tajwa linaripoti kwamba, ndege tajwa ilitua katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA – Kilimanjaro International Airport) mnamo Novemba 24, 2010 na kuondoka mnamo saa saba za usiku wa Novemba 26, 2010. Kuondoka kwa ndege hii kulihusisha utoroshwaji wa maliasili za taifa wakiwemo wanyamapori hai 130 wa aina 14 tofauti tofauti wakiwemo twiga na faru waliohai, pamoja na shehena kubwa ya nyamapori iliyokaushwa (*Raiamwema*, Juni 01, 2012). Tukio hili lilikuwa ni kashfa kubwa na ya kifisadi ambayo ilitawala sana katika vyombo vya habari na bungeni, nchini Tanzania.

Hivyo, kila mtu anayelikumbuka tukio hili, akikutana na kazi bunilizi yenye kugusa tukio hili ama moja kwa moja au kwa uficho, palepale msomaji au msikilizaji atalikumbuka na kujikuta akicheka na kufurahia. Hali hii inatokana na namna

mwandishi alivyomudu kujenga mwingiliano wa matini unaogusa tukio ambalo msomaji makini analitambua na kulikumbuka vizuri. Vivyo hivyo kwa mtu makini anayependa kujisomea, hasa hasa aliyewahi kusoma riwaya ya *Makuadi wa Soko Huria* (Chachage, 2002). Halafu, akakutana na mwandishi ameyatumia maneno aliyowahi kuyatumia Chachage ndani ya riwaya tajwa – “*makuwadi wa soko holela,*” atajikuta akijirejesha katika riwaya tajwa. Kisha, atajikuta akicheka na kufurahia kama njia ya kuonesha umakini wake katika kuyang’amua mambo kwa kuunganisha matukio halisi na matini aliyokutana nayo. Mfano mwingine wenye ucheshi wa kimwingiliano ni huu: -

**Utashi-Nafsi:** Hahahah [*Anatabasamu*] sawa bwana. Kwa heshima yako ni lazima upate ukaribisho rasmi kwa wimbo wa Afrika? [*Kwa makini na kujali*]

**Njozi:** Haswaa.... Mie Mhenga bwana, tena usimame kwa heshima ya Wahenga wote waliotangulia.

**Utashi-Nafsi:** Siku hizi twaimba tumelala Mhenga. Tena wimbo wenyewe umetiwa gugoni.

**Njozi:** Mmmmmh, mmelala? Gugo ndo wapi? Potelea mbali, Aya imba nisikie.

**Utashi-Nafsi:** [*Huku akitabasamu na wasiwasi kwa mbali*] Mungu ibadili Afrikaaa  
Wabadili viongozi wakeee  
Unyama, Vioja vitowekeee [*Anakatishwa*]

**Njozi:** Mmh, loh loh loooh! [*Anaguna*]. Nini hicho unaimba?

**Utashi-Nafsi:** Wimbo wa Afrika.

**Utashi-Nafsi:** Tuliimba ibariki Afrika, ilistahili kubarikiwa, tukasema wabariki viongozi wake mlistahili kubarikiwa. Hata tulizoziita ngao kweli zililinda

damu na heshima ya Mwafrika. Kwa sasa si hivyo tena.

**Njozi:** Enhee na hii “ibadili Afrika?”

**Utashi-Nafsi:** Vyote hivyo vinastahili kubadilika. Na Mungu atubadilishie viongozi wetu. Kwani tunaowataka hatuwapati na tunaowapata hatuwaamini.

**Njozi:** Asalalaa!...

**Utashi-Nafsi:** Ama kweli mpe mpika mkate akupikie mkate wako hata akila nusu yake.

**Njozi:** Alaah! Mbona sielewi? [*Anakaa vizuri zaidi sasa pale mkekani*]. Mpika mkate, apike na ale nusu! [*Anashangazwa na maneno yale*]

**Utashi-Nafsi:** Nusu itakayobaki itakuwa ni ya mkate. Ona tulowapa, walivyoharibu mchele wetu, hakuna nusu yetu wala yao haina baraka. [*Anaimba*] Maadui zetu ni marafiki...

Wote watatu twawafikii...

Abah aba ba ba ba...

Alo ho ha heeeee..

Maradhi kipenziii

Ujinga laaziziii...

Umasikiniiii.... (uk. 52 - 55)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Nje-Ndani*, 2016)

Nukuu hii ina mjadala unaohusisha muonekano wa watu kukata tamaa ya kujivunia Uafrika wao kutokana na viongozi walio wengi kwenda kinyume na matumaini ya wananchi walio wengi. Wananchi wengi waliamini matokeo ya kumuondoa mkoloni yangeleta ustawi na maendeleo endelevu yenye kuzingatia haki, usawa na utu kwa watu wote. Sehemu mojawapo iliyotafsiri matumaini hayo ni kupitia nyimbo za

mataifa husika. Lakini kinyume na matarajio ya wananchi waliowengi, viongozi wadhhalimu wameonekana kusaliti matumaini ya kundi la wananchi hao. Kwa hiyo mtu yeyote, mathalani Mtanzania anayejua vema wimbo wa Taifa la Tanzania, akikutana na wimbo ulioimbwa na Utashi-Nafsi, atakumbuka wimbo wa taifa la Tanzania. Halafu, atagundua kuwapo kwa ukengeushi wa makusudi unaolenga kuwakejeli na kuwaonya viongozi wanafiki wanaowaimbisha wananchi wimbo wenye dhamira njema. Wakati matendo yao (viongozi) yanaonesha viongozi husika wametunga wimbo mbadala. Kwa utambuzi huu, msomaji makini lazima atacheka tu.

Hali hii imeondoa kwa kiwango kikubwa hamasa, ladha, imani, shime, uzalendo na utii wa wananchi kwa viongozi na nembo za taifa. Wengi hawataki kusikia maudhui ya wimbo au maneno ya viongozi wanafiki kupitia nukuu za hotuba na nyimbo za kuwapa hamasa, mori, vuguvugu, hisia za uzalendo na matumaini ya kuingia katika dunia mpya ya maisha mapya chini ya viongozi wazawa kwa faida ya kila mwananchi mzalendo (Ally na wenzake, 2013). Kwa hiyo, ukengeushi huu una mkuno na mguso mkubwa kwa msomaji aliyeamini na, au anayeamini katika ari, hamasa, uzalendo, utaifa, na harakati zote za kumkomboa mzawa kutoka katika makucha ya mkoloni na maajenti wake. Tukio la utambuzi huu, litamfanya msomaji kujikuta akicheka kwa kuona namna mwandishi alivyoumba wazo lake kiubunifu kwa kutumia matini yanayotokana na wimbo wa taifa. Kwa sababu atamuona mwandishi kuwa amefanya ukengeushi unaoakisi hali halisi ya maisha ya kijamii, kisiasa na kiuchumi ya mwananchi mnyonge.

Mfano mwingine wenye kubeba lugha ya ucheshi hususani ucheshi wa kimwingiliano lakini pia ucheshi wa kimazungumzo na ucheshi wa kizimbwe ni huu uliobebwa katika fumbo na ishara zilizosaidia kutoa picha na tafsiri ya haraka kwa msomaji makini. Msomaji anaweza kutambua maana ya lugha ya ishara kwa kusoma kimkakati majadiliano husika ili kubaini kilichofichika ndani ya mazungumzo ya kimaumbo. Hapa tunanukuu mazungumzo kati ya Moyo na Akili ili kuthibitisha kuwapo kwa lugha ya ucheshi: -

**Moyo:** Mapumziko yako vipi?

**Akili:** Ya Krisimasi au mwaka mpya?

**Moyo:** Hujanielewa.

**Akili:** Umezidi mafumbo nawe, liweke labana<sup>8</sup> basi.

**Moyo:** Inaendeleaje mipango kando yako? [*Anaonesha vidole viwili kifuani kama ishara ya matiti*]

**Akili:** Wako sawa kabisa ingawa sasa changamoto ni nyingi.

**Moyo:** Wanajuana?

**Akili:** Kwani wanataka, ni kuhisi tu.

**Moyo:** Hawapendi urasmi ingawa wana hakika kuwa, *cha mtu huliwa na mtu*, katu hakiliwi na kutu.

**Akili:** Kama wa nje haingii ndani hamna shida, kuna hoja ya mkubwa nani na swali la kwa nini?

**Moyo:** Kwa nini ni mwanzo wa ugomvi!

**Akili:** Hapo sasa, nami nisingependa ugomvi utokee. Nusu shari huwa ni bora katika juhudi za kunusuru shari kamili.

**Moyo:** Akili bila shaka inataka lakini moyo unakataa. Si busara kumwaga mboga kwa kumkomoa aliyemwaga ugali.

**Akili:** Ni kama mshumaa, nuru kwa jirani mwenyewe anateketea.  
(uk. 65 - 66)

**(Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Nje-Ndani*, 2016)

<sup>8</sup> Bila shaka hili ni kosa la kiuandishi yaani inapaswa iwe “bayana” badala ya “labana.”



Kupitia nukuu hii yenye mazungumzo tuliyoyanukuu kati ya Moyo na Akili, utafiti umebaini kuwapo kwa kitendo cha usaliti wa kimapenzi. Kupitia mazungumzo ya wawili hawa, tunamwona hapa mhusika Akili akimwakilisha mwanaume au mwanamke mwenye tabia ya kuchepuka kwa kuwa na mpenzi zaidi ya mmoja. Mhusika Akili anaonekana kuwa na mahusiano yasiyo ya kiafya katika kulinda uaminifu wa mapenzi yake. Akili anaonekana kuwa na mpenzi mwingine asiye rasmi mbali ya yule anayetambulika rasmi. Pamoja na tabia hii, bado Moyo anamtia moyo Akili na kumtahadharisha kuwa makini na tabia hii inayoweza kusababisha ugomvi na majuto miongoni mwa wapenzi hao watatu.

Maneno kama vile “Anaonesha vidole viwili kifuani kama ishara ya matiti,” “Wanajuana?” “Kwani wanataka, ni kuhisi tu,” “Hawapendi urasmi ingawa wana hakika kuwa, cha mtu huliwa na mtu, katu hakiliwi na kutu” na “Kama wa nje haingii ndani hamna shida, kuna hoja ya mkubwa nani na swali la kwa nini?” yanaweza kuwa msaada mkubwa kwa msomaji kuunganisha doti na kubaini kinachozungumziwa hapa. Yaani, kuna mahusiano yaliyojaa usaliti ambapo mpenzi mmoja bila shaka mwanandoa ameamua kwa makusudi kuchepuka kwa lengo la kupata pumziko kama Moyo alivyouliza, “Mapumziko yako vipi?”

Maneno haya yanaweza kumrejsha msomaji katika ulimwengu halisi anamoishi na kujikuta akikumbuka maneno kama vile “mchepuko,” “kiburudisho,” “bi. mdogo,” “njia kuu” kutaja kwa uchache. Pia, anaweza kujikuta akikumbuka au kurejelea maisha yake au ya mtu mwingine aliye katika mahusiano ya kimapenzi ya namna ya Akili na kuanza kufanya ulinganifu na tathmini. Kwa hakika, baada ya ulinganifu na tathmini husika, msomaji atajikuta akicheka na kujiona kama mhusika Akili katikati

ya maisha ya raha na karaha za usaliti katika mahusiano ya kimapenzi. Kumbasi, mwandishi ametumia lugha “ngumu” iliyojaa mafumbo na isitiara lakini ndani ya lugha hiyo mna utajiri mkubwa wa ucheshi kwa msomaji anayesoma kimkakati. Hali hii huja kwa msomaji mwenye uwezo wa kutambua maisha halisi yanayotawala na kuzaa matukio katika jamii kuweza kuunganisha matukio kiufundi (Selden, 1985). Msomaji wa namna hii, daima ataiona kazi hii kuwa nyepesi lakini yenye mficho bila shaka kwa watawala wadhalimu wenye upeo finyu dhidi ya maisha halisi ya watu katika jamii wanaowakilishwa kupitia kazi bunilizi husika.

Kwa kweli, uteuzi na uumbaji wa wazo na lugha aliyoitumia mwandishi ni uthibitisho kwamba, tamthilia za zama hizi za awamu ya soko huria hazijapwaya kiubunifu. Bali ni tamthilia zinabeba maendeleo endelevu ya uumbaji wa tamthilia zinazoakisi maisha halisi ya watu kwa faida ya watu hasa watu wanyonge - kiubunifu. Ushahidi huu unapinga madai yasiyorasmi tuliyoyabainisha katika usuli na tamko la utafiti. Kwamba, tamthilia za awamu ya soko huria zimekosa ubunifu kiutunzi hivyo kudhoofisha ukuaji na ustawi wa Tamthilia ya Kiswahili, nchini Tanzania. Baada ya kuchunguza matumizi ya ucheshi katika tamthilia sita (6) teule, kipengele kinachofuata ni uchunguzi wa matumizi wa misimu katika tamthilia sita (6) teule.

### **5.2.2 Matumizi ya Misimu**

Misimu au simo ni semi za muda na mahali maalumu zinazozuka na kutoweka kulingana na mazingira mahususi. Misimu husika ikitumiwa mara nyingi na kwa muda mrefu huzoeleka na hatimaye husanifiwa hata kugeuka msamiati, methali au vitendawili (Samwel, 2013). Misimu inaweza kuwa ni neno jipya au kauli mpya

iliyoundwa na mtu au kundi fulani la watu linalojulikana au lisilojulikana. Lakini pia, misimu inaweza kuwa ni neno au kauli iliyopo katika jamii lakini ikatanuliwa maana, ambapo maana hiyo mpya huvuma na kuonekana kupata msisitizo na msisimko wa kipekee kiutumizi katika kipindi husika (John na Mduda, 2014).

Kuzuka kwa misimu huendana na wakati, mazingira na tukio. Kwa hiyo, semi hizi hutusaidia kutambua historia za jamii katika vipindi tofauti tofauti vya uhai wa maisha ya jamii husika (Mulokozi, 2017). Misimu imegawanyika katika aina kadhaa – kutegemeana na uanishaji uliofanywa na mtaalamu husika. Kuna kigezo cha mada, kigezo cha makundi ya watu, kigezo cha jumla au kawaida (misimu ya pekee, misimu ya kitarafa na misimu zagao / misimu ya kitaifa/kikanda/kimataifa) (Masebo na Nyangwine, 2016). Kwa minajili ya andiko hili, tulichunguza na kubainisha (aina za) misimu kwa kuzingatia kanuni za maumbo ya semi husika. Yaani semi hiyo ni neno moja au kikundi cha maneno.

Misimu neno kwa mtazamo wa mtafiti ni dhana au istilahi inayojitosheleza kimaana bila kuhitaji neno la ziada ili kukamilisha maana iliyokusudiwa. Misimu kikundi ni kauli au semi zinazozuka katika jamii ambazo zinaonekana kuwa katika umbo la virai, vishazi au sentensi yaani kauli nzima hubeba tungo yenye maneno yote au baadhi kuwa mapya kidhana au kimaana.

Katika tamthilia ya *Mashetani*, utafiti umebaini kuwapo kwa misimu neno saba (7) na misimu kikundi mmoja (1). Misimu hii inaonekana kuwa maarufu zaidi katika ukanda wa Pwani kuliko ukanda wa bara ya Tanzania. Jambo linalofanya baadhi ya misimu hii kutokufahamika kwa urahisi na uwepesi miongoni mwa watu wa bara.

Jedwali 5.7 lifuatalo linawasilisha misimu neno iliyobainika kuwemo ndani ya tamthilia hii ya *Mashetani*.

**Jedwali 5.7** Misimu Neno katika *Mashetani*

Misimu	Kurasa Zilizobeba Misimu	Maana ya Msimu Husika
Mcheko	13, 15, 18, 19, 20, 22, 23	Kicheko
Utaufyonda	15	Utaufyata, utasalimu amri
Ndege	22	Gari mpya aghalabu ya kifahari
Mzuka	31	Hamu, hisia, utashi, utayari, mori, ari
Mwananchi	41	Salamu na utambulisho wa raia mzalendo
Mdudu	42	Gari ya kifahari
Manyoya	48, 49	Maisha mazuri na rahisi; anguko

**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Mashetani*, 2018

Jedwali 5.7 linabainisha misimu neno saba iliyobainika kutumika katika tamthilia ya *Mashetani* ikiwa ni sehemu muhimu ya uteuzi na ujenzi wa tamthilia teule. Misimu neno iliyotumika zaidi ni “mcheko” (mara 15) na kufuatiwa kwa mbali na “manyoya” (lililorudiwa mara mbili). Sehemu kubwa ya misimu hii inaonekana kuwa na maneno yanayoishi katika jamii. Lakini katika awamu ya Azimio la Arusha yalipata kutanuliwa maana. Baadhi ya maneno hayo ni pamoja na “ndege,” “mzuka,” “mwananchi,” “mdudu,” na “manyoya.” Maneno haya siyo mapya hata kwa zama hizi. Baadhi yake bado yanaonekana kutumika mpaka sasa kwa maana ile ile, kwa mfano neno “mzuka” hadi leo hii linatumika kwa maana rasmi na isiyorasmi kama tulivyobainisha katika Jedwali 5.7.

Kwa upande wa misimu kikundi, imebainika mwandishi ametumia msimu mmoja pekee ambao ni “ukenda do shahi” wenye maana ya “ukienda ujue huna chako hapa. Kwa hiyo usirudi.” Msimu huu kama ilivyo kwa ile ya awali, unaonekana kutokuwa maarufu katika zama hizi hasa katika ukanda wa wanajamii za Tanzania bara. Hali hii inatokana na ukweli kuwa, mwandishi ni mzaliwa wa Pwani ya Afrika Mashariki.

Hali inayompa wepesi na urahisi sana wa kutumia maneno ya kipwani zaidi (S. M. A. Massoud, 2013). Kuwapo kwa misimu hii kunaongeza utamu wa kihistoria kwa wasomaji wa kipindi cha awamu ya Azimio la Arusha. Pia, matumizi ya misimu huonesha historia ya matumizi ya lugha ya kisanaa katika jamii. Hivyo kufanya waandishi wa zama hizi kutokuhesabika kuwa wahuni mara watumiapo misimu iliyomaarufu na isiyomaarufu ndani ya tamthilia zao. Kwa sababu, kwa asiyejua mawanda ya misimu daima huishia kuinasibisha na vijana wa mitaani au watu wahuni jambo ambalo si sahihi. Kwani ndani ya hicho kinachoonekana kuwa cha kihuni, wanaisimu wanakiona kuwa ni chanzo kimojawapo cha msingi katika kukuza lugha, mawasiliano na sanaa ya jamii fulani (Malima, 2018).

Hata hivyo, mtazamo maarufu unasisitiza kwamba misimu hujitokeza sana katika lugha za mitaani. Nayo huwa na lengo la kurahisisha mawasiliano baina ya wazungumzaji. Lugha hii huweza kuhudumu kama misemo, mafumbo na ishara miongoni mwa wahusika wake kama njia ya kutunza siri (Malima, 2018). Matumizi na maana ya neno ambalo ni msimu haitegemei uwezo au kiwango cha elimu ya darasani bali mazingira na mahusiano ya watumia lugha ya misimu husika. Ndiyo maana ni kawaida kuwakuta watu wa rika zote, viwango tofauti vya elimu, imani na mapokeo wakitumia na kuzalisha misimu kwa sababu ya shughuli maalumu na mahususi yanayowaunganisha kitabia na kimawasiliano (Sengo, 1973). Naye Nauta (1972) anasisitiza kuwapo kwa mfumo rafiki, rahisi na sahihi wa kuwasiliana miongoni mwa watumia lugha ili kuruhusu mawasiliano yenye tija na maana kwa jamii husika. Huu ndiyo msingi uliomwongoza hata mwandishi kuteua misimu na kuitumia katika kuisana tamthilia yake. Kwa sababu uhusika wa mhusika

unafungamana vizuri kama mhusika anapitishwa katika lugha inayoambatana na wahusika, mandhari, miktadha, na mazingira mahususi ndani ya tukio mahususi.

Nayo tamthilia ya *Kijiji Chetu* imebainika kuwa na misimu neno mitano (5) na msimu kikundi mmoja (1). Misimu hii ilikuwa ni maarufu sana wakati wa Azimio la Arusha. Maneno haya kwa sasa yanaweza kuonekana kuwa siyo misimu. Tena yanapatikana katika kamusi za Kiswahili za mwanzo. Lakini matumizi yake yalichagizwa kisiasa zaidi kuliko uhalisi wake. Mathalani, mtu yeyote aliyekwenda kinyume na sera ya ujamaa na kujitegemea aliitwa kupe, mnyonyaji au mvivu (hata kama alikula jasho lake). Lakini aliyeishi kwa kufuata sera hii (hata kama sirini alifanya kinyume) aliitwa mjamaa na ndugu. Kwa hiyo, tunadhani tamthilia hii ina misimu kwa vile maneno haya yalikuwa maarufu yakivuma vinywani na masikioni mwa watu wa zama hizo. Kimatumizi, maneno haya yalipata maana ya ziada pia. Jedwali 5.8 lifuatalo linaonesha misimu neno iliyotumiwa na mwandishi kuumba kazi yake.

**Jedwali 5.8** Misimu Neno katika *Kijiji Chetu*

Misimu	Kurasa Zenye Misimu	Maana ya Msimu Husika
Mvivu	1, 2, 4, 6, 12	Mtu yeyote aliyegoma kufanya kazi katika mfumo wa kijamaa.
Ujamaa	3, 7	Mfumo wa maisha uliokinyume cha mfumo wa ubepari. Watu huishi kwa kufuata mfumo wa kuzalisha na kumiliki mali kwa pamoja, kushirikiana katika mambo yote ya kiuchumi, na kijamii kama jamii moja pasipo kubaguana wala kudhulumiana.
Ndugu	10, 11, 12, 13, 18, 20, 21, 22, 24, 25, 26, 27, 41, 42, 43, 44, 45, 48, 49, 51, 52, 53, 54, 55	Mtu yeyote anayeishi kijamaa bila kujali ambali, rika, jinsi, hadhi au kitu chochote kile. Lengo likiwa ni kuonesha thamani ya utu na usawa miongoni mwa wanajamii. Neno “ndugu” ni kinyume cha neno “Bwana,” “Mheshimiwa,” “Bosi,” “Mzee,” “Mfalme,” “Mtukufu,” “Mkubwa” au “Chifu.”
Wanyonyaj	10, 14, 31, 34, 50	Mtu yeyote anayefaidi mazao ya wajamaa ilhali hakushiriki katika uzalishaji wa mali husika. Pia, waliitwa <i>makupe</i> .
Wajamaa	12, 56	Watu walioamua kuishi kinyume cha mfumo wa kibepari. Hawa huishi kwa kufuata mfumo wa kuzalisha na kumiliki mali kwa pamoja, kushirikiana katika mambo yote ya kiuchumi, na kijamii kama jamii moja pasipo kubaguana wala kudhulumiana.

**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Kijiji Chetu*, 2018

Jedwali 5.8 linabainisha misimu neno iliyotumika katika tamthilia ya *Kijiji Chetu*.

Misimu hii siyo mingi sana lakini msimu neno “ndugu” unaonekana kutumika mara ishirini na nne (24). Matumizi ya neno “ndugu” kwa kiwango hiki yanaonesha jinsi mwandishi alivyoitendea haki awamu ya Azimio la Arusha. Kwani neno hili lilikuwa



ni utambulisho na korasi ya wimbo wa ujamaa miongoni mwa wananchi na wahubiri ujamaa - kama njia mojawapo ya kuonesha utekelezaji wa Azimio la Arusha. Kwa kuwa itikadi na imani ya mjamaa ilikita katika kuamini kwamba, binadamu wote ni sawa na lazima utu wa binadamu uheshimiwe na kulindwa kwa kila hali na namna (TANU, 1967). Kwa hiyo, matumizi ya “ndugu” na kufungamanishwa na maneno mengine mfano “mvivu,” “ujamaa,” “wanyonyaji,” na “wajamaa” kunaifanya tamthilia hii kuwa halisi kiubunifu yenye kubeba historia ya kipindi husika kwa usahihi na uhalisi kamili.

Kwa upande wa misimu kikundi, mtafiti amebaini kuwapo kwa kauli: “kuweka mirija” (uk. 34) ukiwa na maana ya kutengeneza mfumo, mtindo au mbinu za kufaidi jasho la wanyonge bila huruma mradi tu mnyonyaji anakidhi kiu na njaa yake. Huu ni ushahidi mwingine unaohibitisha kuwapo kwa uhusiano halisi kati ya uteuzi wa misimu na historia ya awamu ya Azimio la Arusha. Kauli kama hizi zilitumiwa na wajamaa kueleza ubaya wa ubepari kama njia ya kuwakejeli wale wote waliotumia hila kujenga mifumo ya kuwanyonya wengine (Mrikaria, 2010). Wanyonyaji hawa waliitwa “kupe” au “makupe” kama ilivyotumika katika tamthilia ya *Harakati za Ukombozi* (Lihamba, Balisidya na Mhando, 1982).

Kuelewa vema kile kilichofanywa na mwandishi anayetumia misimu kuisana kazi yake kiubunifu, lazima mhakiki na mtafiti watambue mawanda na umuhimu wa misimu katika lugha, sanaa na jamii. Reuster-Jahn na Kiebling (2006) wanafafanua vema suala hili. Kwa ufafanuzi wa wanataaluma hawa wawili, misimu kama maneno au maana iliyotanuliwa; huwa na utamaduni wa kuzuka katika jamii kulingana na wakati, mahali, tukio na, au mada. Kwa hiyo, hata kauli mbiu huweza kuzuka na

kuwa maarufu katika wakati fulani wa mahali fulani kwenye tukio fulani ili kuwakilisha na kuwasilisha mada fulani. John na Mduda (2014) wanafafanua zaidi kwa kusema, misimu inaweza kuwa ni neno au kauli iliyopo katika jamii lakini ikatanuliwa maana au ikapata msukumo mpya ili kukidhi lengo mahususi la mzalishaji au mtumiaji neno au kauli husika. Ambapo, maana hiyo au msukumo huo mpya huvuma na kuonekana kupata msisitizo na msimko wa kipekee kiutumizi katika kipindi husika. Naye Mulokozi (2017) anaongezea kwamba, kuzuka kwa misimu huendana na wakati, mazingira na tukio. Hivyo, semi hutusaidia kutambua historia za jamii katika vipindi tofauti tofauti vya uhai wa maisha ya jamii husika.

Kwa mantiki hii, watu wa sasa wanaweza wasielewe kama haya maneno tunayoyatambulisha kuwa ni misimu yalikuwa ni misimu maarufu katika kipindi husika aghalabu kipindi cha Azimio la Arusha. Kumbe maana maneno haya siyo maarufu kwa zama hizi za awamu ya soko huria lakini kabla ya kipindi hiki, maneno haya yalikuwa ni misimu kwelikweli. Maneno haya yalipata umaarufu kutokana na jukwaa la kisiasa la wakati huo kusukuma mbele sera ya ujamaa na kujitegemea (rej. TANU, 1967; Ally na wenzake, 2013). Lakini baada ya kuanguka kwa ujamaa, maneno haya yamebaki kuwa katika kamusi na vitabu au vinywa vya historia. Hata msukumo wake au maana ya ziada ya wakati huo haipatiwi uzito katika matumizi ya kila siku ya lugha - miongoni mwa watumiaji lugha wengi wa soko huria.

Kwa hiyo, kitendo cha mwandishi kuamua kuteua na kusana maneno yaliyotawala katika kipindi husika ni ushahidi mwingine unaothibitisha kuwapo kwa uhusiano wa kihistoria kati ya matukio halisi ya kijamii na ubunifu katika uumbaji wa mawazo yanayobebwa na kuwasilishwa kisanaa mbele ya jamii ya wasomaji na wasikilizaji.

Aidha, uchunguzi uliofanyika katika tamthilia ya *Harakati za Ukombozi*, umebaini kuwapo kwa misimu neno mitano (5) na kukosekana kwa misimu kikundi. Misimu yote inahusiana na mapambano na kutiana shime dhidi ya ubepari, dhuluma, chuki na unyonyaji kwa lengo la kumfariji na kumtia hamasa mwananchi mnyonge. Misimu iliyobainika kuwemo katika tamthilia hii imewasilishwa kupitia Jedwali 5.9 kama ifuatavyo: -

**Jedwali 5.9** Misimu Neno katika *Harakati za Ukombozi*

Misimu	Kurasa Zenye Misimu	Maana ya Msimu Husika
Ndugu	17	Mtu yeyote anayeishi kijamaa bila kujali ambali, rika, jinsi, hadhi au kitu chochote kile. Lengo likiwa ni kuonesha thamani ya utu na usawa miongoni mwa wanajamii. Neno “ndugu” ni kinyume cha neno “Bwana,” “Mheshimiwa,” “Bosi,” “Mzee,” “Mfalme,” “Mtukufu,” “Mkubwa,” au “Chifu.”
Jasho	17	Matunda yanayotokana na juhudi, maarifa, mshikamano na nguvu za Wajamaa.
Magugu	17	Watu wanaofaidi mazao/matunda ya wajamaa ilhali hawakushiriki kwa usahihi, umoja wala mshikamano katika uzalishaji wa mali husika.
Makupe	17	Watu wanaofaidi mazao/matunda ya wajamaa ilhali hawakushiriki kwa usahihi, umoja wala mshikamano katika uzalishaji wa mali husika.
Mabomba	17	Watu wanaofaidi mazao/matunda ya wajamaa ilhali hawakushiriki kwa usahihi, umoja wala mshikamano katika uzalishaji wa mali husika.

**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Harakati za Ukombozi*, 2018

Jedwali 5.9 linabainisha misimu neno iliyotumika katika tamthilia ya *Harakati za Ukombozi*. Kuwemo kwa misimu hii katika tamthilia tajwa kunathibitisha namna mwandishi alivyoteua na kuumba mawazo na lugha kwa kuzingatia historia ya awamu ya Azimio la Arusha. Kwa kufanya hivyo, tamthilia hii haiwezi kuonekana kama zao lililojitenga kutoka maisha halisi ya vizazi vya wakati husika. Misimu neno

inaonekana kutumika kwa kiasi. Kwa upande wa misimu kikundi, mtafiti hakufanikiwa kuibaini katika tamthilia hii. Huu ni ubunifu mzuri ambao haujajitenga na jamii husika. Kitendo cha mwandishi kutumia misimu hasa misimu maarufu kunaonesha utambuzi wa lugha inayotumiwa na walaji wake. Utafiti umebaini kuwa, misimu karibia yote tuliyoibaini katika tamthilia hii ya *Harakati za Ukombozi*, ndiyo ileile iliyojitokeza katika tamthilia ya *Kijiji Chetu*.

Hili ni jambo linaloonesha kuwapo kwa usemezano wa misimu ndani ya tamthilia za awamu moja. Pia, huu ni ushahidi kwamba, misimu husika ilijitokeza katika kipindi halisi cha historia ya vijiji vya ujamaa. Maneno haya yanaakisi kimantiki ahadi za Mwanatanu (rej. TANU, 1967) na mikakati ya vita dhidi ya unyonyaji, dhuluma, matabaka na chuki dhidi ya wanyonge (rej. Nyerere, 1970; Ally na wenzake, 2013). Kwa hiyo, maneno haya ni rahisi kuyasikia yakitoka vinywani mwa watu wa kizazi cha Azimio la Arusha kuliko kizazi cha soko huria. Hivyo, hata kiutunzi ni rahisi zaidi kuyakuta katika kazi bunilizi za awamu ya Azimio la Arusha na kuyatambulisha kama misimu. Huku yakikosekana katika kazi za awamu ya soko huria. Lakini, maneno hayohayo yanapojitokeza katika awamu ya soko huria, wahakiki na watafiti wengi hawawezi kuyatambulisha kama misimu kwa sababu kimaana na kimofolojia siyo maneno mapya.

Mtafiti alichunguza pia misimu inayopatika katika tamthilia ya *Safari ya Chinga*. Utafiti umebaini kuwapo kwa misimu ya aina mbili ambayo ni misimu neno na misimu kikundi. Misimu neno kwa mtazamo wa mtafiti ni dhana au istilahi inayojitosheleza kimaana bila kuhitaji neno la ziada ili kukamilisha maana iliyokusudiwa. Misimu kikundi ni kauli au semi zinazozuka katika jamii ambazo

zinaonekana kuwa katika umbo la virai, vishazi au sentensi. Yaani, kauli nzima hubeba tungo yenye maneno yote au baadhi kuwa mapya kidhana au kimaana. Misimu neno iliyojitokeza katika tamthilia ya *Safari ya Chinga* inabainishwa kupitia Jedwali 5.10 na kuongezewa taarifa zinazoonesha maana inayorejewa na watumia lugha.

**Jedwali 5.10** Misimu Neno katika *Safari ya Chinga*

Misimu	Kurasa Zenye Misimu	Maana ya Msimu
<b>Husika</b>		
Chinga	25, 28,	Mchuuzi/wachuuzi/wauzaji wa bidhaa wanaozunguka kila
Wamachinga	35, 36, 50	kona ya mji kusaka wateja wa bidhaa zao.
Fegi	7	Sigara (katika mazingira ya sasa, huweza kurejelea msokoto wa bangi au dawa za kulevya zilizohifadhiwa kwa muonekano wa sigara ya kawaida).
Kisojasoja	8	Kijeshijeshi.
Demu (umoja), mademu (wingi)	10	Mwanamke au msichana, mpenzi wa kike.
Machangu (wingi) (Changu – umoja)	10	Mwanamke / Wanawake malaya (kahaba).
Machangudoa (wingi)	50	
Vichangudoa (udogoishaji & wingi)	10	(i) Kauli ya kuwadogoisha au kuwabeza wanawake malaya. (ii) mabinti wadogo wanaofanya umalaya yaani kuuza miili yao kwa wanaume wapenda ngono.
Madaladala (wingi)	19	Vyombo vya usafirishaji abiria kwa umbali mfupi ndani ya mji, aghalabu magari. Mwanzoni mwa miaka ya 2000, kabla ya ujio wa gari na pikipiki zinazotoa huduma ya usafiri wa umma, baadhi ya mikoa (au maeneo fulani ndani ya mkoa) mfano mikoa ya

		Mara na Shinyanga baiskeli na pikipiki (kabla ya kuitwa bodaboda) ziliitwa (au zinaitwa mpaka sasa) daladala.
Wapiga debe	50	Watu wanaonadi magari au bidhaa kwa lengo la kuwashawishi abiria au wanunuzi kukubali kusafiri au kununua bidhaa husika.
Mama ntilie	50	Wafanyabiashara ndogo za huduma ya chakula kilichotayari kuuzwa na kuliwa na wahitaji (wateja). Aghalabu huwa ni wanawake. Wanaume huitwa baba ntilie.
Mateja	50	Watu walioathirika kutokana na matumizi mabaya ya dawa za kulevya.
Gereji bubu	50	Maeneo yasiyotambulika rasmi/kisheria yanayotumiwa kwa shughuli za marekebicho ya vyombo vya moto.
Mamwera	52	Askari polisi.
(Wingi. Umoja ni mwera)		

**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Safari ya Chinga*, 2018

Jedwali 5.10 linaonesha kuwapo kwa jumla ya misimu neno 12. Misimu hii kwa sasa inaweza kuitwa ni misimu ya kitarafa au isihesabike kuwa misimu kutokana na ukweli kwamba misimu hii (isipokuwa “mamwera”) imekuwa maarufu sana katika matumizi ya kila siku ya lugha. Kiasi kwamba sasa inaweza kuhesabika kuwa ni maneno ya kawaida miongoni mwa masikio ya watumiaji wa lugha. Lakini katika miaka ya 1990 maneno haya yalikuwa ni mapya kidhana na, au kimaana. Misimu tuliyoibaini inaonesha kuzaliwa kutoka mazingira, lahaja za Kiswahili na lugha ya Kiingereza. Aidha, baadhi ya maneno yana asili ya lugha sanifu ya Kiswahili lakini yamepewa maana ya ziada hivyo kuyafanya yahesabike kuwa ni misimu. Mathalani neno “demu” siyo jipya kwani linaonekana kuwemo katika msamiati uliokusanywa na kuingizwa katika Kamusi Sanifu ya Kiswahili (TUKI, 1981). Lakini maana

zinazobainishwa katika muktadha wa kamusi tajwa hazina uhusiano na maana inayorejelewa na watumiaji wa neno “demu” ijapokuwa kuna uhusiano fulani wa maana hizo na maana mpya ya mtaani.

Kwa mujibu wa Kamusi Sanifu ya Kiswahili (TUKI, 1981), demu ni: (1) nguo mbovu iliyopasuka; bwende, na (2) kitambaa ambacho zamani kilitumiwa na wanawake kuvaa kiunoni au kufunikia maziwa wakati wa kulima. Lakini maana inayojengwa katika muktadha wa tamthilia ya *Safari ya Chinga*, neno “demu” linaashiria mwanamke au msichana. Pia, linaashiria rafiki au mpenzi wa kike wa mwanaume / kijana wa kiume. Hii ndiyo maana aliyoirejea Mbululu katika nukuu hii, “Tatizo lako wewe unafikiria demu wako Suzy. Ndo mana hutaki kwenda town. [...]. Huko town ndo kuna mademu kibao wa kila aina” (uk. 10).

Kauli ya Mbululu inathibitisha maana ya ziada iliyoongezwa katika msamiati unaopatikana katika Kamusi Sanifu ya Kiswahili ya mwaka 1981 pia Kamusi Sanifu ya Kiswahili ya mwaka 2014. Huku kunaashiria kuwapo kwa ukaribu kimaana na kimatumizi kati ya maana ya msingi na maana ya ziada. Reuster-Jahn na Kiebling (2006) wanafafanua kuwa, misimu ya aina hii hutumiwa zaidi na watu wenye kuwakilisha kundi maslahi mahususi katika wakati, mahali na tukio mahususi kabla ya kusambaa na kukamata makundi yote ya watumia lugha. Mara nyingi waanzilishi wa maneno haya ni vijana. Hata hivyo, vijana hawa hawatabaki kuwa vijana milele kwani kesho yao ni kuitwa watu wazima au wazee. Kwa hiyo, misimu hii inaweza kudumu au kupotea kutegemeana na kiwango cha msambao wake kimatumizi.

Aidha, misimu neno katika tamthilia hii imezingatia pia tabia ya kizazi cha leo kinachopenda kuchanganya lugha zaidi ya moja katika mawasiliano yake. Hii ni

tabia inayotajwa kujengeka sana miongoni mwa vijana wa mijini na kwenye majiji kutokana na athari ya elimu na maingiliano makubwa ya watu wa jamii na mataifa tofauti tofauti (Reuster-Jahn na Kiebling, 2006). Ndiyo maana mwandishi Shani Omari hakujitenga na matumizi ya misimu neno kama vile “fegi,” na “kisojasoja.” Kitendo cha mwandishi kuchota misimu ya awamu ya soko huria na kuzingatia saikolojia ya kizazi cha soko huria kunaonesha ubunifu uliomo katika tamthilia hii. Ubunifu huu unamsogeza mlaji wa kazi hii kuwa siyo tu karibu tena, bali kuwa ni sehemu kamili ya uteuzi na uumbaji wa lugha ya kitamthilia wenye kufungamana na fanani husika.

Vilevile, mwandishi ametumia misimu kikundi katika kuitajirisha kazi yake kwa lengo la kumfanya msomaji kujisikia kuwa sehemu kamili ya tukio linalotendeka ndani ya tamthilia hii. Misimu kikundi iliyobainishwa katika tamthilia hii inawasilishwa kupitia Jedwali 5.11 lifuatalo: -

**Jedwali 5.11** Misimu Kikundi katika *Safari ya Chinga*

Misimu	Kurasa Zenye Misimu	Maana ya Msimu Husika
Kapiga pamba jinzi kali	8	Kavaa (kapiga) nguo (pamba) nzuri (kali) aina ya jinzi ( <i>jeans</i> ). Kapendeza kimavazi.
Nayamaindi kinoma	8	Ninayapenda (nayamaindi) mno/sana (kinoma). Wakati mwingine (naya)maindi huashiria kughadhibika au kumgombeza mtu kutokana na kitendo kilichokukasirisha.
Mademu kibao	10	Wasichana / wanawake (mademu) wengi (kibao).
Haina / hana noma	27	Haina / hana tatizo, madhara, hatari (noma).
Kisu mkononi	50	Rushwa.
Mamwera wakiwazukia	52	Askari polisi (mamwera) wakiwavamia /



wakiwafikia (wakiwazukia).

---

**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Safari ya Chinga*, 2018

Jedwali 5.11 linaonesha kuwapo kwa misimu kikundi sita (6) pekee. Hii inamaanisha kwamba, mwandishi hakutumia aina hii ya misimu kwa wingi kama alivyofanya katika misimu neno. Bila shaka, uchache huu unatokana na misimu kikundi kuzalishwa kwa uchache miongoni mwa watumiaji wa Lugha ya Kiswahili. Hivyo, mwandishi akaepuka kuunda misimu kikundi yake ambayo kusambaa kwake kungeweza kuanzia akilini mwake na kuishia machoni na akilini mwa wasomaji (wachache bila shaka) watakaoisoma tamthilia yake. Na, kwa vile mzalisha misimu hiyo angekuwa ni mwandishi mwenyewe kungeibuka changamoto ya kimaana kwa sababu wasomaji wake siyo sehemu ya waliozalisha na kuisambaza misimu hiyo. Matokeo yake, kila msomaji angeishia kuzalisha maana yake ambayo labda ingekuwa sawa au kinyume cha maana lengwa ya mwandishi. Hii ndiyo sababu inayowafanya waandishi kukwepa kuzalisha kauli tata au maneno mapya mengi. Kwani kwa kuzalisha maneno mapya mengi au kauli tata nyingi ndani ya matini kunaua ushirika wa mwandishi kwa wasomaji lengwa - kimaana na kimawasiliano.

Kwa kulitambua hili, mwandishi kama sehemu ya jamii, hujikuta kwa hiari au kutohiari akiathiriwa zaidi na matumizi ya misimu inayozalishwa ndani ya jamii (Malima, 2018) kuliko ile inayoweza kuzalishwa ndani ya ubongo wake. Tena, utajiri wa lugha na uchaguzi wa kipi cha kusema kwa namna gani ni zao la kisosholojia na kisaikolojia unaoambatana na haiba na tajiriba za mtumia lugha akiwemo mwandishi mwenyewe ndani na nje ya ulimwengu wake kiutunzi (Kioko, 2017). Pamoja na uchache huu, matumizi ya misimu yamekuwa chachu kubwa

katika kuvika nyama ya kisanaa lugha na dhamira zilizosadifiwa kupitia wahusika vijana walioteuliwa na kutumiwa kwa sehemu kubwa. Kiubunifu, uteuzi huu umesaidia kuonesha changamoto zinazowakabili vijana, hususani wale wanaotoka katika jamii zenye hali duni kimaisha ambao wengi wao wanapatikana vijijini.

Katika tamthilia ya *Changamoto*, mtafiti amebaini kuwapo kwa misimu sita (6). Misimu mitatu (3) ikiwa ni misimu neno na misimu iliyobaki mitatu (3) ikiwa ni misimu kikundi. Pamoja na uchache huu, bado lengo la mwandishi la kuielimisha jamii linaonekana kufanikiwa kimaudhui. Jedwali 5.12 linaonesha misimu neno na maana zake: -

**Jedwali 5.12** Misimu Neno katika *Changamoto*

Misimu	Kurasa Zenye Misimu	Maana ya Misimu
<b>Husika</b>		
<b>Kuchacharika</b>	2	Kupambana / kuhangaika / kuharakisha jambo
<b>Mangumbaru</b>	14	Kejeli: Watu wasiojua kusoma, kuandika na kuhesabu / Watu wazima wanaojiendeleza kielimu hasa elimu ya msingi na, au sekondari
<b>Madodoki</b>	26	Tafsida: mfuko wa korodani au korodani za binadamu

**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Changamoto*, 2018

Jedwali 5.12 linaonesha misimu neno iliyotumika katika tamthilia teule, ambayo ni “kuchacharika,” “mangumbaru” na “madodoki.” Uchache huu bila shaka siyo jambo la bahati mbaya alilolifanya mwandishi. Bila shaka, mwandishi amefanya hivyo ili kuepuka kuisuka kazi kwa namna itakayolifunga wazo lake kiasi cha kufanya lisieleweke vema. Pia, aina ya wahusika na mgogoro alioujenga, kama angetumia misimu inayowahusu watu wenye ulemavu, bila shaka, mwandishi angeonekana kuwa sehemu ya wanajamii wanaowadhhalilisha watu wenye ulemavu badala ya

kuwatetea na kuwapa staha stahiki. Kama ilivyo kwa misimu neno kuwa michache, mwandishi haonekani kujikita pia katika kutumia misimu kikundi mingi. Misimu kikundi iliyobainika katika tamthilia hii ni mitatu (3). Nayo imewasilishwa kupitia Jedwali 5.13 lifuatalo:

**Jedwali 5.13** Misimu Kikundi katika *Changamoto*

<b>Misimu</b>	<b>Kurasa Zenye Misimu</b>	<b>Maana ya Msimu</b>
<b>Husika</b>		
Njagu wa kike na kiume	1	Askari (njagu) wa kike au kiume.
Unaniwekea kiwingu	5	Unanizibia riziki, unaniharibia mipango yangu.
Akanyee debe	25	Apelekwe mahabusu ya polisi au gerezani ambako kwa sehemu kubwa wafungwa na mahabusu hujisaidia kwenye chombo maalumu ambapo kukipambazuka hutakiwa kukibeba na kwenda kumwaga haja ndogo na kubwa katika eneo lililotengwa.

**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Changamoto*, 2018

Jedwali 5.13 linabainisha misimu kikundi iliyotumika katika tamthilia ya *Changamoto*. Kuwapo kwa misimu kikundi michache kunaonesha namna mwandishi alivyoepuka matumizi ya lugha ya kimisimu. Pamoja na uchache huo, yawezekana mwandishi kwa mara nyingine alikwepa kuonekana akiwabeza wahusika ambao ni watu wenye ulemavu. Ijapokuwa, kulikuwa na nafasi ya ubunifu mbadala kwa mwandishi kuwapa misimu watu wenye ulemavu ili waitumie katika mazungumzo yao. Lakini, inawezekana mwandishi alitaka kuonesha athari za unyanyapaa kwa watu wenye ulemavu katika matumizi ya lugha. Kwa mantiki kwamba, kitendo cha jamii kuwanyanyapaa kwa kuwatenga na kuwaficha watu wenye ulemavu majumbani kunawakosesha fursa ya kujifunza, kubuni, kutumia na kutanua uwezo

wao katika kuimudu lugha ikiwemo misimu. Hivyo, kuwafanya washindwe kuongeza msamiati na semi za kutosha kiasi cha kushindwa kuichezea lugha kwa kadri wpendavyo.

Kwa mujibu wa Skinner (1957), mtoto anaweza kujifunza na kuimudu lugha pindi anapofungamanishwa na mazingira halisi kwa uhuru na nafasi. Naye, Chomsky (2004) anaongeza kwamba, mazingira ya nje ya mtoto kujifunza lugha ni sharti yachochewe na uwezo nasaba uliombika ndani ya mtoto mwenyewe. Kupitia uwezo nasaba wa maumbile asili ya mtoto na utajiri mkubwa wa maneno na kauli walizozipata ndani ya jamii yao humfanya mtoto kuzalisha na kutumia lugha kwa kadri ya jamii inayodhibiti makuzi ya mtoto husika (Clark, 2009). Kama hili ndilo lengo la mwandishi, basi huu ni ubunifu mkubwa alioufanya mwandishi katika kuteua, kujenga na kusawiri matumizi ya lugha bila kuathiri mtazamo wa msomaji. Ubunifu huu unamuacha mwandishi Elizabeth Godwin Mahenge akiwa ni mtu mwenye mikono safi isiyo na mawaa wala hatia mbele ya laumu la mpumbavu.

Kwa upande wa tamthilia ya *Nje-Ndani*, mtafiti amechunguza na kubaini kuwapo kwa misimu neno, misimu kikundi na misimu dailojia. Misimu iliyobainika kutumika katika tamthilia hii ni ile inayoonekana kuendana na awamu ya soko huria katika miaka ya 1990 hadi leo hii, 2022. Misimu neno iliyobainika inaonekana kuwa mingi kuliko misimu kikundi na misimu dailojia. Misimu neno iliyobainika inawasilishwa kupitia Jedwali 5.14.

**Jedwali 5.14** Misimu Neno katika *Nje – Ndani*

<b>Misimu</b>	<b>Kurasa Zenye Misimu</b>	<b>Maana ya Misimu</b>
<b>Husika</b>		
Makuwadi	2	Maharamia / mabepari / wanyonyaji wa jasho la wengine.
Upapo	11	Upo hapo. Kwa zama hizi ni kawaida kusikia vijana wakitumia muundo wa namna hii katika baadhi ya maneno.
Vumbasi	12	Pia, Mavumba. Ukwasi wa fedha / kuwa na fedha nyingi.
Shombo	12, 24	Maneno au jambo linalokera.
Utumbuzi	17	Utenguaji wa teuzi; kuwafukuza kazi au kuwavua vyeo wenye tuhuma au makosa kazini.
Ung'eng'e	24	Lugha za Kigeni hasa Kiingereza.
Kimombo	24, 47	Kiingereza.
Bondenii	44	Nchi ya Afrika Kusini.
Mhenga	52	Mtu anayeonekana kutenda au kujua mambo mengi hasa ambayo wengi wa rika lake hawayafahamu au kuyaweza. Matendo au mambo hayo ni sharti yafungamane na watu waliokula chumvi / rika la nyuma.
Nje ndani	58	Ukweli na uwazi usio na chembe ya uficho wa kitu au jambo.
Ujasiri-riba	69	Mfumo unaotumiwa na wakopeshaji fedha kuweka kiwango cha juu cha faida (riba) katika mikopo itolewayo kwa wafanyabiashara, hususani wafanyabiashara wadogo almaarufu wajasiriamali. Mfumo huu badala ya kumuinua mnyonge, umegeuka kaa la moto kwa kusababisha mkopaji kushindwa kurudisha mkopo na faida inayokusudiwa. Hivyo, kuishia kumfilisi mkopaji au wadhamini wake. Kwa hiyo mwandishi anaona huo siyo ujasiria-mali bali ujasiri-riba.
Umeshabeti (kubeti)	87	Aina ya mchezo wa ki-elektroniki wa kubashiri unaotumika kumbashiri mshindi na, au magoli katika mechi mbalimbali hususani mashindano ya mpira wa miguu.

Mikeka	87	Risiti za (au) malipo / kumbukumbu za malipo / malipo yanayofanywa ili kuweza kupata fursa ya kushiriki katika mchezo wa ubashiri.
--------	----	--

**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Nje – Ndani*, 2018

Jedwali 5.14 linaonesha misimu neno kumi na tano (15) iliyotumika katika tamthilia ya *Nje-Ndani*. Misimu neno iliyoonekana kutumika zaidi katika tamthilia hii ni “kimombo” ambalo limetumika mara tatu (mara mbili katika ukurasa wa 24, na mara moja katika ukurasa wa 47). Misimu neno mingine iliyojirudia kiutumizi ni “shombo” (mara mbili) na “bondeni” (mara mbili – katika ukurasa ule ule wa 44). Misimu neno hii inaonekana kuendelea kupata umaarufu na hamasa katika zama hizi kutokana na vijana wengi kuwa sehemu muhimu na kuu katika utumizi na uzalishaji wa misimu na semi nyinginezo zenye kufungaana na wakati kihistoria (Malima, 2018). Kitendo cha mwandishi kuteua na kutumia misimu hii kunathibitisha ubunifu katika matumizi ya lugha yenye kuendana na wakati, kizazi na teknolojia ya wakati husika. Maneno mathalani “utumbuzi,” “mhenga,” “kubeti,” “mikeka” yanatumika sana miongoni mwa vijana wa zama hizi kutokana na hamasa za kisiasa, kielimu, kiuchumi na kiteknolojia kama moja ya athari za utandawazi wa TEHAMA.

Aidha, mtafiti amegundua kuwapo kwa misimu kikundi nane (8) iliyotumika katika kazi hii. Misimu kikundi iliyobainika kutumika katika utunzi na uandishi wa tamthilia hii teule inaakisi kipindi teule cha awamu ya soko huria. Mingi ya misimu hii ilikuwa maarufu katika miaka ya mwishoni mwa 1990 lakini mpaka leo hii inaendelea kutumika na kutambulika miongoni mwa watumia lugha ya Kiswahili. Misimu kikundi hiyo inawasilishwa kupitia Jedwali 5.15.

**Jedwali 5.15** Misimu Kikundi katika *Nje – Ndani*

Misimu	Kurasa	Maana ya Msimu Husika
Zalenga mshiko	2	Kinachokusudiwa ni fedha (mshiko).
Nguo za mpalo	20	Mavazi ya kupendeza miongoni mwa kundi rika aghalabu vijana wa kizazi kipya kwa minajili ya kwendea mahali.
Unataka Kanani	kurudi 44	Unakusudia kujisahihisha na kuanza kutenda mambo mema baada ya kugundua ukengeushi wako.
Kusukuma damu	46	Moyo ufanye kazi moja tu – kupampu damu, kamwe usijishughulishe na kupenda (mapenzi).
Kilimo kwanza	60	Kauli mbiu mojawapo iliyovuma sana katika kipindi cha Rais Mstaafu Jakaya M. Kikwete (2005 – 2015). Kauli mbiu hii ilibeba dhamira na hamasa ya mapinduzi makubwa katika tasnia ya kilimo. Kwa sasa baadhi ya wazungumzaji huitumia kumaanisha fursa yoyote inayokupatia kipato.
Ya leo kali	62	Siyo hali / kitu / jambo la kawaida kunenwa / kutendwa.
Misukule manamba wa miamala	na 69	Watumwa wa mbinu / teknolojia ya biashara ya uhamishaji fedha.
Makuwadi wa holela	soko 75	Maharamia / mabepari / wanyonyaji wanaohodhi mfumo wa soko lisilodhibitiwa.

**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Nje - Ndani*, 2018

Jedwali 5.15 linaonesha misimu kikundi iliyotumika katika tamthilia hii teule.

Misimu kikundi hii nane (8) inaonesha muunganiko uliopo baina ya kazi bunilizi ya

kitamthilia na matumzi ya lugha katika awamu ya soko huria. Misimu hii imebeba misemo, kauli mbiu, kejeli, na sifa za jambo ama kitu au mtu katika jamii ya kizazi cha awamu hii ya soko huria. Kwa upande wa misimu dailojia, mtafiti amegundua kuwapo kwa maneno ya kimisimu ndani ya tafakuri ya mhusika Utashi-Nafsi. Maneno hayo yanaakisi uundaji wa maneno usiorasmi unaotumiwa na vijana wa awamu ya soko huria. Msimu huo ni huutunaounukuu kama unavyosomeka:

**Utashi-Nafsi:** Afrikani...  
 Wa rozali, vikofia na vilemba...  
 umojani... (uk. 1 – 2)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Nje-Ndani*, 2016)

Nukuu hii inaonesha kubeba maneno ambayo yanapatikana katika jamii ya kizazi cha awamu ya soko huria. Tena, umaarufu wake unaonekana kuongezeka kiutumizi kuliko ilivyokuwa katika miaka ya 1990. Baadhi ya maneno hayo ni “Afrikani” likimaanisha ama Waafrika au ndani ya Afrika huku neno “umojani” ikimaanisha ndani ya umoja. Neno “wa rozali” linamaanisha Wakristo hasa Wakatoliki (au Waislamu - kwa baadhi ya watumia lugha; ijapokuwa kwa Waislamu hutumika istilahi “tasbihi”). Nalo neno “vikofia” hutumika kuwatambulisha maaskofu. Huku neno “vilemba” likitumika kuwarejelea watawa wa kike. Uteuzi huu wa maneno unaonesha ubunifu wa waandishi katika kuteua na kuumba lugha ya kisanaa inayobeba misimu inayotumiwa na watu wa kizazi cha awamu ya soko huria.

Tunapohitimisha kuhusu matumizi ya misimu, hatuna budi kufanya muhtasari juu ya kufanana na kutofautiana kiubunifu kwa tamthilia sita (6) teule. Kutokana na data tulizowasilisha hivi punde, tunabaini kuwa tamthilia ya *Mashetani* ni ya tatu (3) ikiwa na misimu neno saba (7) pekee bila kuwapo kwa misimu kikundi. Huku neno



“Mcheko” likijirudia mara 15. Tamthilia ya *Kijiji Chetu* ni ya tano (5) ikiwa na misimu neno mitano (5) bila kuwapo kwa misimu kikundi. Huku neno “ndugu” likijitokeza mara 24. Tamthilia ya *Harakati za Ukombozi* ni ya sita (6) ikiwa na misimu neno mitano (5) bila kuwapo kwa misimu kikundi. Hakuna msimu unaojirudia. Tamthilia ya *Safari ya Chinga* ni ya pili (2) ikiwa na misimu neno 12 huku neno “Chinga” likijirudia mara tano (5). Pia, tamthilia hii ina misimu kikundi sita (6). Tamthilia ya *Changamoto* ni ya nne (4) kwa kuwa na misimu neno mitatu (3) na misimu kikundi mitatu (3). Hakuna msimu unaojirudia kote. Tamthilia ya *Nje – Ndani* ni ya kwanza (1) ikiwa na misimu neno 13 ambapo misimu miwili (2) inajirudia mara mbili (2) kila mmoja. Pia kuna misimu kikundi minane (8). Kwa data hii, tunagundua ya kwamba katika matumizi ya misimu, yapo maendeleo endelevu yanayokwenda na wakati kiubunifu na kimantiki. Kipengele kinachofuata baada ya uchunguzi na ubainishaji wa matumizi ya misimu ni matumizi ya uchanganyaji ndimi.

### **5.2.3 Matumizi ya Uchanganyaji Ndimi**

Uchanganyaji ndimi ni mbinu mojawapo katika matumizi ya lugha ambapo mtunzi hutumia lugha zaidi ya moja katika kutambulisha mhusika, wazo, muktadha na ulumbi katika kazi yake. Uchanganyaji ndimi unaweza kujitokeza kuanzia ngazi ya neno mpaka ngazi ya tungo huku idadi yake ikiwa siyo sahili (Muysken, 2000). Kwa ngazi ya neno tuna mfano “*nitaku-call*” badala ya “*nitakupigia (simu)*.” Kwa ngazi ya vikundi vya maneno, mfano ni “*you and Juma...*” Katika ngazi ya kishazi, mfano ni “*when I come, nitakueleza kila kitu.*” Kwa ngazi ya sentensi tuna “*don’t worry, I will be there before 2 o’clock. Kwa hiyo, usijali tafadhali.*” Uchanganyaji ndimi

unatokana na sababu tofauti tofauti. Nao unapendwa na watu tofauti tofauti kwa minajili tofauti tofauti miongoni mwa watumia lugha.

Kisanaa, mwandishi naye hulazimika kubuni lugha inayogusa mahitaji ya watumia lugha kwa viwango na sababu mahususi (Senyamanza, h. m.). Kwa mantiki hii, kisanaa, uchanganyaji ndimi ni mbinu mojawapo katika kazi bunilizi ikiwemo tamthilia. Mbinu hii ina athari kubwa kwa wasomaji wake. Utafiti wetu uliongozwa na nadharia ya Fasihi Linganishi ili kujibu maswali: Kwa vipi? Ya nini? Kwa nini? Lini? na wapi? Jilala (2016) anasisitiza kuwa, lengo la Fasihi Linganishi kama mbinu ya kisanaa, si jingine ila ni kuibua vipengele vinavyofanana, kutofautiana na kuhusiana kati ya kazi za fasihi za ulimwengu na Fasihi Linganishi za jamii mahususi.

Kwa kuanza na tamthilia ya *Mashetani*, utafiti umebaini kuwapo kwa matumizi ya uchanganyaji ndimi yanayoonesha ubunifu katika uteuzi na ujenzi wa wahusika, muktadha na mandhari. Uteuzi huu, siyo wa bahati mbaya kwa sababu uteuzi huo umezingatia mahusiano mapana ya uumbaji wa wazo la mwandishi. Mbali na ndimi ya Kiswahili, mwandishi ametumia maneno ya Kiingereza na ya kilahaja. Muhtasari wa haya tuyasemayo unapatikana katika Jedwali 5.16 ambalo ni kiambatisho A. Muhtasari wa uchanganyaji ndimi katika tamthilia ya *Mashetani* umewekwa kama kiambatisho kutokana na ukubwa wa data unaofikia kurasa mbili na zaidi kwa vipimo vya ukubwa wa maneno kuwa 11 katika muundo wa Times New Roman unaokubalika na chuo kwa jedwali lenye data zinazozidi ukurasa mmoja (1) (rej. OUT, 2022; uk. 4).

Jedwali 5.16 linaonesha utajiri mkubwa wa matumizi ya ndimi zaidi ya moja katika uteuzi na ujenzi wa lugha iliyotumika kubeba maudhui. Uteuzi wa maneno kutoka lugha ya Kiingereza, haujajitokeza kwa bahati mbaya. Kwa sababu tunaona wazo linalojadiliwa na mwandishi, pia uteuzi na ujenzi wa wahusika, mandhari, mazingira na wakati ndani ya tamthilia hii, kwa pamoja vinatambulisha maisha ya matabaka makuu mawili nchini Zanzibar yaliyoathiriana baada ya mapinduzi. Juma anawakilisha tabaka tawala la jana ilhali Kitaru na familia yake wanawakilisha tabaka tawala la leo baada ya mapinduzi. Kwa mujibu wa mwandishi katika ukurasa wa “YALIOMO,” Mahali pa mchezo ni Dar es salaam, Tanzania na wakati (kipindi) ni mwishoni mwa mwaka 1966, kabla ya Azimio la Arusha. Hii ina maana ya kwamba, mchezo ulichezwa miaka miwili baada ya mapinduzi matukufu ya Zanzibar ya Januari 9, 1964 na “kuungana” kwa nchi za Jamhuri ya Zanzibar na Jamhuri ya Tanganyika na kuzaa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mnamo Aprili 26, 1964.

Uchanganyaji ndimi wenye kubeba matumizi ya lugha ya Kiingereza kwa kiwango kikubwa katika tamthilia hii unathibitisha madai haya. Kwamba, baada ya kuondoka kwa wakoloni wa Kiingereza, Waafrika wengi hasa wasomi na wafanyakazi waliopewa madaraka walijigeuza kuwa wakoloni weusi kwa kujitahidi kuishi maisha ya wakoloni ilhali rangi za ngozi pekee zikibakia nyeusi (Mwiru, 2013). Uteuzi wa matumizi ya lugha ya Kiingereza badala ya lugha nyingine ya kikoloni au kigeni ni sehemu ya historia kutumia jukwaa la kifasihi kuhifadhi na kurithisha vizazi amali za kihistoria. Mbali na Mwarabu na Mreno, Mwingereza ndiye mgeni mtawala aliyekaa kwa muda mrefu katika ukanda wa Afrika Mashariki. Wakati wa utawala wake, Mwingereza alijenga na kuunganisha miundombinu, miundo ya kiutawala na

mifumo ya kijamii, kisiasa, kiutamaduni na kiuchumi ili kubeba falsafa, propaganda na itikadi ya mfumo walioulenga wa kuifanya dunia kuwa kijiji kupitia mfumo wa utandawazi (Helge, 1996; Yeo, 2010).

Kwa hiyo, kuwapo kwa matumizi makubwa ya Kiingereza katika tamthilia hii ni njia bunilizi ya kufungamanisha vilivyo uteuzi na uumbaji wa wahusika ili kulimudu vema tukio la kihistoria. Nalo si jingine, bali ni lile linalosadifu unafiki, matabaka, ujuaji, ubaguzi, na ubinafsi uliowajaa Waafrika wasomi ambao wameshindwa kujitenga na elementi za ukoloni zilizomkandamiza mwananchi wa Kiafrika kabla ya kupata uhuru (Davidson, (1978). Uteuzi wa lugha ya Kiingereza ndani ya tamthilia hii unarejelea athari ya mikakati rasmi ya matumizi rasmi na yasiyokuwa rasmi ya lugha za kikoloni wakati na baada ya ukoloni. Rodney (1972) anatujuza kuwa, kila mkoloni alihimiza na kuhakikisha lugha yake inapenya na kutumika kwa lazima katika shughuli rasmi na hata zisizorasmi miongoni mwa makoloni yake. Rodney anatambulisha mfumo wa elimu, dini na utawala kama baadhi ya mifumo iliyotumika barabara kuandaa na kuzalisha wasomi wanaotumia na kuenzi lugha na malengo ya mkoloni. Maelezo haya hayatofautiani na ufafanuzi wa wanataaluma mbalimbali wakiwemo p'Bitek (1975), Duerden na Pieterse (1988) na Maake (2006) juu ya athari za ukoloni kwa wasomi wazawa wa Afrika.

Hali hii imeonekana kumuathiri hata mwandishi Ebrahim N. Hussein. Mwandishi anaonekana kutokuamini istilahi za Kiswahili kiasi cha kuongezea istilahi za Kiingereza ili kurahisisha ufahamu wa kile alichokikusudia kieleweke kwa msomaji, kama tulivyobaini katika maelezo yake. Tunamnukuu: “Sehemu hii ya mchezo inachezwa katika akili ya Kitaru. Kwa hivyo mandhari (setting) yake imewekwa

mbele au ndani ya picha ya kichwa chake. Wachezaji wanaweza kutumia vioo (slides) na chombo cha kutupia picha (projector) kuikuza picha hii, na kuieneza pote” (uk. 13). Maneno “setting,” “slides” na “projector” yamewekwa kwenye mabano kuashiria ufafanuzi wa nyongeza anaotaka wasomaji aghalabu wasomi wanaojua Kiingereza waweze kuelewa kwa usahihi na urahisi.

Hii inaonesha ya kwamba, wakati wa Azimio la Arusha, Kiswahili kama chombo cha kubeba istilahi za kitaaluma, bila shaka hakikuwa na mizizi ya kutosheleza mahitaji ya kitaaluma. Au, hakikuwa kinaaminika na kueleweka vizuri miongoni mwa wanataaluma na wanazuoni. Hapa, tunapata picha mbili. Ya kwanza ni ile ya kuonesha kwamba kuna umasikini wa msamiati / istilahi katika lugha ya Kiswahili wenye kukidhi matakwa ya maneno ya kitaaluma na kiteknolojia ambayo mwandishi anayataka lakini hayapati isipokuwa tu kwa kutumia lugha za kigeni. Kwa imani kuwa hata sehemu kubwa ya wasomaji wake hasa wasomi wanayafahamu kwa lugha ya kigeni. Picha ya pili ni kuliona jambo hili kama tokeo la athari ya ukoloni kwa mwandishi juu ya muono wa lugha za wenyeji katika uumbaji wa kazi bunilizi. Kwa imani kwamba, lugha za wenyeji hazikidhi matakwa ya kitaaluma, kisayansi, kiteknolojia na kimawasiliano (Hoffman, 1991; Maake, 2006).

p’Bitek (1975), Thiong’o (1986) na Duerden na Pieterse (1988) wanakubaliana na picha hii ya pili. Kwa maelezo yao, jambo hili limekuwa likiwatesa sana wasomi wa Kiafrika – wakiwemo waandishi. Hili ni janga kubwa lililokita mizizi akilini mwa waandishi na wasomi wengi wa ndani na nje ya Afrika, hasa wale wa kizazi cha ukoloni na ukoloni mamboleo wa mwanzo. Vizazi hivi bado vinaamini katika nguvu ya lugha za kigeni katika kuumba na kuwasilisha mawazo yao mbele ya kaumu ya

watu wazawa lakini pia kwa wasiowazawa wa lugha mama za Kiafrika. Jambo hili ni kikwazo na hatari kwa harakati za ustawi na maendeleo endelevu ya jamii asili ya watu. Jamii inayoshindwa kujiamini wala kutumia raslimali asili zinazowazunguka kwa uhuru na ubunifu, kamwe haiwezi kupiga hatua kimaendeleo (Nyerere, 1973; Sharma 2005).

Kwa jumla, hata hivyo, tukiondoa ufafanuzi wa dhana katika mabano; kiubunifu, mwandishi anaonekana kufanikiwa kuonesha kiustadi namna wasomi wazawa wanavyojiona kuwa watu wa daraja la juu mbele ya ndugu zako. Tabia ambayo ni sawa na ile ya wasomi wa enzi za mkoloni na mkoloni mwenyewe mbele ya Mwafrika wazawa. Kwa maneno mengine, wasomi wazawa waliopata elimu ya kikoloni, wanaonekana kutokuitumia elimu yao kuakisi asili yao kwa faida ya jamii zao. Badala yake, elimu hiyo iliwafanya wabaki katika ulimwengu wa kikoloni kwa faida ya wakoloni, kwa wao kujigeuza wakoloni weusi. Ndiyo maana mwandishi ameteua sehemu kubwa ya wahusika kuwa wasomi na watu wa tabaka la juu waliolewa mali, vyeo, sifa, tamaa, dharau na hamu ya kusujudiwa na wananchi waliowaamini na kuwapa dhamana ya uongozi na utawala wa taifa na nchi.

Kumbe basi, kwa mawanda mapana, tunagundua ya kuwa mwandishi hajatumia uchanganyaji ndimi kwa bahati mbaya. Matumizi makubwa ya uchanganyaji ndimi ni uthibitisho tosha juu ya uwezo wa mwandishi katika kubuni, kuteua na kuumba lugha inayosawili historia halisi, mambo halisi na haiba ya wasomi wengi wa awamu ya Azimio la Arusha na sasa. Alichokifanya Ebrahim N. Hussein ndicho kilichowahi kuelezwa na Ruhumbika (2006) juu ya wajibu wa mwandishi. Kwa Ruhumbika, mwandishi ana wajibu mkubwa wa kuhawilisha maisha halisi kupitia umbo la

kifasihi ili kuisogeza zaidi jamii kuwa karibu na fasihi yake ili kuepuka ubaguzi wa kijamii na kifasihi. Mwandishi hana budi kuyaangazia matendo ya kweli ya wanajamii na kuyanena kisanaa bila kuzusha uongo. Lengo ni kuiokoa jamii badala ya kuiangamiza.

Kwa upande wa tamthilia ya *Kijiji Chetu*, utafiti umebaini kwamba hakuna matumizi ya moja kwa moja ya uchanganyaji ndimi bali kuna neno moja lenye asili ya Kiarabu. Neno hilo ni “Ahsante” lililotokea mara moja (uk. 11). Uandishi wa neno “Ahsante” unabeba umbo la matamshi ya Kiarabu hasa kwa kuwapo kwa sauti /h/ ambayo Waswahili wasiojua Kiarabu huwa hawaitamki; huidondosha. Kwa hiyo uandishi wa tahajia za neno “Ahsante” unaonesha elementi za uchanganyaji ndimi. Hii ndiyo maantiki ya kusema tamthilia hii inaweza kuibua mjadala kama kuna au hakuna matumizi ya uchanganyaji ndimi. Tahajia za Kiswahili za neno “Ahsante” ni “Asante.” Hivyo mtafiti hakubaini kuwapo kwa sababu za msingi za uandishi wa neno hili kwa kutumia athari ya matamshi ya Kiarabu katika sauti ya /h/ kwa maana ya kufikirika ya umbo “Akhsante.” Nje ya tahajia ya “Ahsante” mtafiti haoni kuwapo kwa matumizi ya uchanganyaji ndimi katika tamthilia ya *Kijiji Chetu*.

Uchunguzi wa mtafiti umebaini sababu za kutokuwapo kwa matumizi ya uchanganyaji ndimi (kama hoja ya tahajia katika neno “Ahsante” haitapewa mashiko) katika tamthilia hii. Kutokuwapo kwa uchanganyaji ndimi katika tamthilia hii, kumbainika ni kunatokana na uteuzi na uumbaji wa wazo, wakati, wahusika, mandhari, miktadha na mazingira. Mwandishi hajatumia wahusika wasomi wanaobeba elementi za kigeni wala za kikabila bali wahusika wanaowaza namna ya kujenga kijiji kipya chenye utaiifa, umoja, uzalendo, usawa kwa lengo la kuondoa

dhuluma na ubaguzi. Ndiyo maana wahusika waliokuwa wanapingana na sera na miongozo ya vijiji vya ujamaa na Azimio la Arusha walitambulika na kushughulikiwa. Bila shaka, hata ujasiri wa kutumia lugha ya Kiswahili na kikabila haukuwapo kwa hofu ya kuitwa mbaguzi, na majina au adhabu zinazowahusu wahujumu azimio. Tena mandhari ni ya kijijini ambayo yanatokana na kipindi cha kuanzishwa kwa vijiji vya ujamaa na utekelezaji wa sera ya Azimio la Arusha.

Kihistoria, kipindi hiki hakikuwa na maingiliano makubwa ya wageni na wenyeji huko vijijini. Pia, wananchi wengi hawakuishi mahali pamoja kama ilivyo sasa. Nyumba nyingi zilikuwa mbalimbali, na watu wengi hawakubahatika kupata elimu wala kuishi na wageni toka nje ya jamii zao (Juhani, 1988; Wakota, 2018). Hivyo, uteuzi na ujenzi wa wahusika wa haiba hii ni dhahiri uchanganyaji ndimi usingebeba lugha za kigeni. Uchanganyaji ndimi pekee ambao ungeweza kutokea katika tamthilia hii ungekuwa ni wa lugha ya Kiswahili na lugha za asili za wenyeji. Yaani, lugha za makabila husika kutokana na mchanganyiko wa jamii tofauti tofauti zinazounda kijiji cha ujamaa. Hata hivyo, tunaona mwandishi aliepuka hata kutumia lugha za makabila katika tamthilia yake. Bila shaka, mwandishi alizingatia sera ya kuumba utaiifa wa Mtanzania kama sehemu ya kuitika wito wa kupiga vita ubaguzi na matabaka kwa misingi ya lugha za makabila. Kitendo cha mwandishi, kutambua na kuzingatia sera ya lugha ya taifa na miongozo ya kitaifa (Wizara ya Elimu na Utamaduni, h.m) na ule wa siasa ya ujamaa na kujitegemea (TANU, 1967) katika kujenga vijiji vya ujamaa ni ushahidi wa uwezo mkubwa kiubunifu katika uteuzi na uumbaji wa matumizi ya lugha na maudhui.



Nayo tamthilia ya *Harakati za Ukombozi*, utafiti ulichunguza na kubaini kuwapo kwa matumizi ya kiwango cha chini cha uchanganyaji ndimi. Mwandishi ametumia Kiswahili sanifu na neno moja la Kiingereza. Neno hilo ni “bar” (uk. 18). Kuwapo kwa neno hili katika tamthilia nzima kunaonekana kwa hakikalilingia kwa bahati mbaya. Kwa maana kwamba, halikuwa kusudio hasa la mwandishi kufanya uchanganyaji ndimi. Hoja hii inapata uzito kutokana na mahali lilipotokea neno husika. Neno hili linaonekana kutokea siyo kinywani mwa mhusika mtendaji mchezoni bali limo katika mwongozo wa jukwaa na matuko ambao ni kauli ya mwandishi. Kwa maana hiyo, matumizi ya neno “bar” katika tamthilia hii yanaonesha uwezekano wa uteuzi unaotokana na sababu kuu mbili. Moja ni athari ya lugha za kigeni miongoni mwa watu wenye umilisi wa lugha zaidi ya moja kama ilivyo kwa mwandishi wa tamthilia hii. Pili ni mtazamo kihadhi na kimaana kwa maneno mbadala yanayowakilisha neno “bar.”

“Bar” ni neno la Kiingereza ambalo kwa Kiswahili huwakilishwa na neno “baa.” Neno “baa” lililotoholewa kutoka neno la Kiingereza “bar.” Kwa mujibu wa Kamusi ya Kiswahili Sanifu (TUKI, 2014), neno “baa” lina maana kuu tatu ambazo ni: - “(1) mtu au kitu kiletacho hasara, maafa, au shida; kisirani, nuksi, mkosi, nuhusi, muholelo, ukuba, beluwa; (2) mahali panapouzwa na kunywewa pombe – klabu cha pombe; na (3) teke la mtu aliyemo usingizini.” Kumbe basi, mwandishi alikuwa na nafasi ya kutumia neno “baa” badala ya “bar” kama maana namba mbili (2) inavyoonesha.

Lakini, tunatambua ya kwamba, watumiaji wengi wa lugha ya Kiswahili hutumia neno “klabu cha pombe” kurejelea mahali panapouzwa na kunyweka kwa pombe za

kienyeji ambazo kwa kiwango kikubwa hazina ubora kwa wanywaji wake ambao wengi ni watu masikini, waliochoka, na kukata tamaa ya maisha. Wakati “bar” hurejelea mahali panapouzwa na kunywewa pombe zilizotengenezwa viwandani na kuthibitishwa ubora wake kisayansi, ambazo bei yake ni ghali kuliko bei ya zile za asili. Wateja wa “bar” kwa kiwango kikubwa ni watu wenye kipato cha kati na juu, na hupewa heshima katika jamii. Kwa hiyo endapo mwandishi angetumia “klabu cha pombe” thamani ya wahusika bila shaka, ingeshuka na wangepanishwa na wanywaji matapatapu. Au, wasomaji wangeweza kuona kuna lugha ya mficho inayokejeli wasomi na matajiri wa kipindi hicho. Kwamba, tabaka hili limekwenda kunywa pombe za kienyeji lakini likaficha utambulisho wa pombe hizo kwa kuziita bia.

Kwa hiyo bado, mwandishi angeweza kutumia neno “baa” badala ya neno “bar” pamoja na ukweli kwamba, neno “baa” lina maana zaidi ya moja – eneo la unywaji pombe na janga kubwa hasa la asili mfano njaa na mafuriko. Vivyo hivyo, hata kwa neno “bar.” Kwa mujibu wa Kamusi ya Kiingereza ya Oxford (2020), neno “bar” humaanisha dhana kadhaa. Miongoni mwa maana hizo ni: (i) a place where you can buy and drink alcoholic and other drinks.<sup>9</sup> (ii) a long wide wooden surface where drinks, etc. are served.<sup>10</sup> (iii) (especially in compounds) a place in which a particular kind of food or drink is the main thing that is served.<sup>11</sup>

---

<sup>9</sup> Mahali unapoweza kununua na kunywa vinywaji vyenye kilevi na vinywaji vingine.

<sup>10</sup> Mahali penye ubao bapa na mrefu unaotumika kuwekwa vinywaji.

<sup>11</sup> (hasa katika mazingira) mahali ambapo aina mahususi ya chakula au kinywaji hutolewa kama huduma kuu.

Kwa fasili na tafsiri hizi, kwa hakika matumizi ya neno “bar” hayaonekani kuwa na uzito au msingi maalumu kwa mwandishi kuliteua na kulitumia neno hili. Kwa sababu, mbali ya neno “baa” kuwa na maana zaidi ya moja, bado maana ya kimuktadha ingetambulisha kile kilichokusudiwa hasa na mwandishi. Kwa hoja hizi, tunaweza kuhitimisha ya kwamba sababu za matumizi ya neno “bar” siyo ya kimuktadha wala kiubunilizi bali ni kwa sababu ya athari za lugha za kigeni miongoni mwa watu wenye umilisi wa lugha zaidi ya moja kama alivyo mwandishi. Adeseke (2016) anaiona hali hii kiubunaji kama sehemu ya matokeo ya athari ya mwandishi kuwa mumilisi wa lugha zaidi ya moja. Ambapo, wakati anaandika, ghafla umakini huhama huku kumbukumbu zikishindwa kurejesha akilini picha ya kitu kilichoandikwa. Matokeo yake mwandishi hupoteza uhusiano wa wazo na lugha inayotambulika miongoni mwa wasomaji wengi wa lugha inayokusudiwa kubeba maudhui. Athari hii huchangiwa pia na wandishi kuendelea kuishi ndani ya fikra na hisia za utamaduni wa kigeni (Duerden & Pieterse, 1988). Uchunguzi unaofuatia hivi punde ni ule unaohusu tamthilia tatu (3) teule za awamu ya soko huria.

Tamthilia ya *Safari ya Chinga* imechunguzwa na kubainika kuwa na matumizi makubwa ya uchanganyaji ndimi. Sehemu kubwa ya tamthilia hii imetumia lugha ya Kiswahili na lafudhi ya Kimakonde au lahaja ya Kingao. Pia, imetumia lugha ya Kiingereza. Lugha ya Kimakonde au lahaja ya Kingao huzungumzwa kusini mwa Tanzania. Uchanganyaji ndimi huu haukufanywa kwa bahati mbaya. Bali ni uamuzi wa makusudi kutokana na uteuzi wa wahusika, tukio, mandhari, mazingira na wakati wa kihistoria uliotumika kuiumba kazi husika. Matumizi ya uchanganyaji ndimi kwa

lugha za kibantu yanayoonekana kutumika katika dua ya kumuomba Mata kabla ya kwenda mjini. Tunanukuu: -

**Che Mundu:** (*Anachukua kata ya maji anakunywa, kisha anamrushia Mata yale maji ya kinywani utosini*). Phwaa! (*Anachukua mtama katika mkungu na kumwaga chini kidogokidogo*). Nangu Che Mundu chingutenda kulembela kwa ajili ya mwanangu Matatizo. Ahena mbali kudaresalama. Hambu nangu ngutenda kuyuwa kwa wazee wohewohe mulongolele mbele. Akina nzee Ntongwechu, Nandoka, Chindengu, Chikandema na vanji vohe. Munnole mdukulu wenu kwahena kwa vanu. Anapate matatizo lohelohe. Kwangu nangu hambu nanga malove chondechonde, ndimalila. (uk. 20)

**Bi. Somoe:** (*Anachukua kata ya maji anakunywa, kisha anamrushia Mata yale maji ya kinywani utosini*). Nangu chingutenda kulembela kwa mwanangu Matatizo kuhena aneko mbali. Hambu mwanangu vikale na vazee mmohemohe mulongolele nangu ngutenda kuyuwa munnole mwana aneyo anapate matata chonde chonde chonde, nangu nimalila. (uk. 21)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Safari ya Chinga*, 2009)

Nukuu hii inaonesha matumizi ya lugha za asili katika kupeleka dua mbele ya muumba. Mantiki hapa ni imani inayojengwa katika matumizi ya lugha ya asili katika matambiko na kuomba dua ili kuwaunganisha wanadamu husika na Mungu (mungu) wao. Jambo hili linatokana na imani kwamba kwa dini na imani nyingi, lugha inayoonekana kuaminika kuwa na nguvu ya kupokeleka na kupata majibu

yanayohitajika kwa wakati sahihi na haraka ni lugha asili iliyumba dini husika (Mbiti, 1969; p'Bitek, 1975; Alabi, 2015). Kitendo cha mwandishi kutokutumia Kiswahili katika dua, kunaonesha uwezo wake katika kung'amua falsafa iliyomo katika miviga, visasili na theolojia ya dini na wafuasi wake. Kwani tunaona katika maeneo mengine ya unenaji wa Che Mundu na Bi Somoe, lugha iliyotumika ni Kiswahili cha kilahaja. Lakini ilipofika hatua ya wao kufanya dua, wakatumia lugha ya Kimakonde badala ya hicho Kiswahili au lahaja ya Kiswahili. Hili ni jambo la kifalsafa na kiimani zaidi. Halikutokea kwa bahati mbaya. Kwa hiyo, hapa mwandishi hajaitenga tamthilia kutoka jamii halisi badala yake ameifungamanisha kwa namna inayomfanya msomaji kujiona kuwa katikati ya tukio halisi la kijamii.

Tukiondoa matumizi ya dua kwa lugha ya asili - Kimakonde, utafiti umebaini kuwa robo tatu ya lugha iliyotumika katika tamthilia hii imebeba athari ya matamshi na lafudhi ya Kimakonde au lahaja ya Kimgao. Utafiti umebaini kuwapo kwa uchanganyaji ndimi wa Kiswahili na Kiingereza kwa kiwango kisichokikubwa. Uchanganyaji ndimi kati ya Kiswahili na Kiingereza (na maneno yaliyotoholewa na mwandishi) inawasilishwa kupitia Jedwali 5.17 lifuatalo: -

**Jedwali 5.16** Matumizi ya Uchanganyaji Ndimi katika *Safari ya Chinga*

<b>Kauli</b>	<b>Kurasa</b>	<b>Kiwango cha Kujitokeza</b>	<b>Maana ya kama Neno kama Lilivyotumika Kitabuni</b>	<b>Lugha Chanzi</b>
Fegi	7	1	Sigara	Kiingereza
Jinzi	8	1	Vazi lenye nembo au kitambaa kigumu kama kile cha “Jeans”	Kiingereza
Nayamaindi	8	1	Nayapenda	Kiingereza
Kisojasoja	8	1	Kijeshijeshi	Kiingereza
Town	8, 9, 10	4	Mjini	Kiingereza
Yes yes	14	2	Ndiyo ndiyo, sawa sawa	Kiingereza
Original	25	2	Halisi, isiyo bandia	Kiingereza
Fotokopi	25	1	Nakala / kivuli cha nakala halisi	Kiingereza
Diet	28	1	Utaratibu maalumu wa chakula	Kiingereza
Fasheni	32, 34	2	Mtindo	Kiingereza
Saizi	33	1	Kipimo, ukubwa	Kiingereza
Tulichosevu	51	1	Tulichookoa	Kiingereza
Solusheni	53	1	Suluhisho, ufumbuzi, jawabu	Kiingereza

**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Safari ya Chinga*, 2018

Jedwali 5.17 linaonesha utajiri wa matumizi ya ndimi zaidi ya moja katika uteuzi na ujenzi wa lugha iliyotumika kubeba maudhui. Mwandishi anaonekana kutumia lugha ya Kiswahili na Kiingereza kukamilisha wasifu wa wahusika ambao ni vijana wa zama hizi za soko huria. Githiora (2002) anatupatia ufafanuzi mrefu kuhusu hali hii ya vijana wa sasa kuchanganya ndimi ya Kiswahili na lugha za kigeni katika mawasiliano yao ya kila siku. Githiora anasema, tafiti zinaonesha vijana wa zama hizi, hata wasiojua kusoma na kuandika, hujitahidi sana kutumia lugha za kimataifa

hata kama hawazimudu vema. Tabia hii huchangia sana kuzaliwa kwa lugha ama sentensi au maneno yasiyorasmi yenye mofolojia ya lugha zaidi ya moja. Maneno au sentensi za namna hii huzalishwa kutoka katika lugha zinazotawala usemi ndani ya jamii husika.

Githiora anaendelea kufafanua kuwa, itakuwa ni ajabu kukuta jamii ambayo haina wazungumzaji wa lugha fulani na lugha hiyo haijawahi kuwa sehemu ya historia ya maingiliano ya watu, maneno ya lugha hiyo mpya yakasikika au kutumika katika jamii isiyokuwa sehemu rasmi ya historia ya lugha hii mpya. Kawaida, lugha zinazochanganywa ni zile zenye wasemaji ndani ya jamii, kihistoria na kisosholojia. Haijalishi wasemaji hao ni wengi au wachache au jamii lugha mpya imekuwapo katika jamii asili kwa muda gani. Kikubwa ni lugha husika kuzalisha wasemaji wapya kwa wasemaji hao kubeba maneno mapya kutoka lugha mpya na kuanza kuyatumia.

Ndiyo maana pamoja na akina Mata kutokujua kusoma na kuandika bado wana misamiati kadhaa ya Kiingereza wanayoitumia katika mazungumzo yao. Huu ni ushahidi mwingine kwamba utandawazi unazidi kuiteka dunia kwa kuifanya kuwa kijiji kidogo (Thuranira, 2017; Wibowo na wenzake, 2017). Kwa hiyo, kizazi cha sasa, hasa vijana wanaonekana kuwa wafuatiliaji na waigaji wazuri wa mambo yanayotokea katika mataifa makubwa. Maingiliano ya watu yasiyokuwa na mipaka nayo yamechangia tamaduni na mila zikiwemo lugha, tabia na matendo fulani fulani kuzaliwa au kufa (International Organization for Migration, 2019). Hii inaonesha namna ukoloni mamboleo ulivyokita mizizi katika ulimwengu uliotawaliwa na wageni.

Kwa ufafanuzi huu, tunabaini ya kwamba, kumbe uteuzi wa wahusika vijana wa kizazi cha utandawazi wa leo umechochea uchanganyaji ndimi kama alivyofanya mwandishi. Kwa maana kwamba, mwandishi hakuwa na namna mbadala ya kuwaumba wahusika vijana wanaoishi katika jamii zinazopokea wageni kila siku, kubaki na lugha yao ya asili pasipo kuchota maneno mapya kutoka wageni hao (rejea mazungumzo ya vijana katika *Safari ya Chinga*, uk. 7 - 10). Kwa mantiki hii, matumizi haya yanabeba ushahidi unaohibitisha ubunifu uliomo ndani ya tamthilia hii ya *Safari ya Chinga* katika kulisuka wazo lililokusudiwa na mwandishi.

Kwa upande wa tamthilia ya *Changamoto*, utafiti umebaini kwamba, mwandishi hakutoa kipaumbele kikubwa kwa matumizi ya uchanganyaji ndimi. Utafiti umebaini kuwapo kwa maneno manne (4) pekee ya Kiingereza. Maneno mawili (2) kati ya hayo manne (4) yanatokana na muundo wa ufupishaji maneno (“MC”, uk. vi; 1, 3 & 20; na “RB”, uk. 30). Neno moja (1) limetokana na utohoaji usiorasmi (“bakigraundi”, uk. 7). Neno jingine - la nne (4); limetumika kama linavyotumika katika lugha ya Kiingereza (“zebra,” uk. 6). Kwa upande wa lugha za Kibantu, limetumika neno “uhule” (uk. 16) ambalo mwandishi amelifasiri kuwa ni “mahindi yaliyokwisha pukuchuliwa.” Uchanganyaji ndimi mwingine unaonekana katika matumizi ya maneno ya Kibantu kupitia salamu ambayo mwandishi hakuipa tafsiri kama alivyofanya kwa neno “uhule.” Maneno hayo yanapatikana katika dailojia ifuatayo:

**Maimatha:** (*Akimsalimia kwa lugha ya Kabila la Kihehe*). Weuli!

**Godwin:** (*Akijibu kwa Kihehe*). Weuli, makasi.

**Maimatha:** (*Akijibu kwa Kihehe*). Ale. (uk. 12)



(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Changamoto*, 2010)

Nukuu hii inaonesha matumizi ya lugha ya Kihehe katika kusalimiana. Ingawa maneno yanayobeba salamu hayakupewa tafsiri, baadhi ya jamii lugha zinazosikilizana na Kihehe zinaweza kuelewa maana ya maneno husika. Kwamba, neno “weuli” linamaanisha “habari ya saa hii / hizi,” wakati neno “makasi” linamaanisha “za kazi” au “za huko utokako” na neno “Ale” linamaanisha “nzuri” au “njema.” Matumizi ya lugha asili miongoni mwa watu wenye kuhusiana kinasaba, kunatajwa na wanataaluma wa lugha na mawasiliano kuwa kitu cha kawaida. Wibowo na wenzake (2017) wanaeleza kuwa, watu wanaojua lugha zaidi ya moja, huwa na tabia ya kusalimiana kwa lugha inayowagusa na kuwapa hisia za ukaribiano. Baada ya hapo, watu hawa huweza kuendelea na mazungumzo kwa lugha tofauti na ile waliyotumia awali kuwasiliana. Kwa hiyo, kitendo cha Maimatha na Godwin kusalimiana kwa lugha ya asili, kisha kuendelea na lugha ya Kiswahili (rejea mazungumzo yao baada ya salamu), ni sehemu ya utamaduni wa kisaikolojia na kisosholojia wa binadamu anayemudu lugha zaidi ya moja – ama kwa kiasi kidogo au kwa kiasi kikubwa.

Hata hivyo, kwa wanajamii wengi, kisaikolojia huwa hawahangaiki na maana zilizomo katika salamu. Badala yake hukisia kwa kuzipa tafsiri yenye kubeba maana na mantiki ya salamu kati ya wazungumzaji kwa kuzingatia mahusiano ya wazungumzaji, rika na jinsi husika. Hivyo kuwafanya wasikilizaji kutokupata kiu wala shauku ya kutafuta undani wa kauli husika. Labda msikilizaji awe na hamu ya kutaka kujifunza lugha anayoisikia au kutokupenda kupitwa na kauli anayoisikia.

Caponecchia (2012) na Farnsworth (2019) wanakubaliana na tulichokisema. Caponecchia pamoja na Farnsworth wanatukumbusha kwamba, binadamu kwa asili humakinikia kile anachokihitaji. Kinyume na hapo hawezi kujihangaisha na jambo au tukio lisilomnyima amani. Kama jambo hilo siyo hitaji lake la msingi kwa wakati huo, kamwe binadamu hana muda wa kulihangaikia.

Aidha, tuna maneno “MC,” (*Master of Ceremony*, lenye kumaanisha Mshereheshaji), “RB” (lenye kumaanisha “namba ya shitaka” kama tulivyozea. Kirefu cha RB ni Report Book ikiwa na maana ya Kitabu cha Ripoti ya Matukio/ Kitabu cha Kurekodi Matukio), “bakigraundi,” na “zebra.” Matumizi ya maneno haya kunaonesha nafasi ya ubunifu katika kutambua na kuzingatia maneno ya kigeni ambayo kimatumizi yamekuwa ya kawaida kusikika masikioni mwa Waswahili. Matumizi ya neno “uhule” na salamu ya Kihehe kunaonesha umaizi wa mwandishi katika kumudu na kutumia lugha zaidi ya moja kimawasiliano na athari yake katika utunzi na uandishi wa kazi bunilizi.

Matumizi ya salamu ya Kihehe kunawasogeza karibu zaidi wahusika kama ilivyo kwa Maimatha (mtoto) na Godwin (baba mwenye kumthamini na kumpenda sana binti yake bila kujali hali). Kiutendaji, lugha hii huwakanisha na kuwafungamanisha wahusika watendaji mchezoni na hadhira - asili ya lugha husika. Vivyo hivyo, kwa watumiaji lugha wenye tabia ya kuchanganya ndimi, pindi wanapokutana na maneno ya lugha ya kigeni ambayo siyo mageni masikioni mwao hujikuta wakivutiwa na kufurahia mawasiliano husika (Low, 2011), kama mwandishi alivyotumia maneno haya. Bila shaka, hii ndiyo sababu iliyomsukuma mwandishi kutumia lugha za kibantu japo kwa uchache.

Tumbaini pia, mwandishi amefanya tafsiri ya maneno “MC” na “Zebra.” Hivyo kuwafanya wasomaji wasiojua Kiingereza, kupata maana inayofungamana na muktadha wa matumizi ya maneno husika. Mwandishi amefasiri “MC” kuwa ni “Mshehereshaji katika dhifa ya Malkia na Walemavu” (uk. vi) ijapokuwa tukitazama matumizi ya neno “MC” katika ukurasa wa 20 hadi 21 tunaona fasili aliyoitoa mwandishi katika ukurasa wa vi inakinzana na dhana nzima ya “MC” kama “mshehereshaji katika dhifa” kwani katika ukurasa wa 20 hadi 21 tunaona shughuli ni ya majonzi – msiba, siyo dhifa!<sup>12</sup> Hapa tunagundua kuteleza kwa mwandishi katika fasili yake.

Kwa muktadha wa tamthilia hii, mwandishi angeweza kufasili “MC” kama “mtu maalumu mwenye jukumu kwa niaba ya waandaaji wa shughuli kutoa utaratibu na mambo mbalimbali yanayotakiwa kutendwa katika shughuli husika. Pia, huwa sehemu ya watia hamasa, ari, faraja na maelekezo jumuishi.” Hii inasadifu maana ya “MC” kama tunavyoona katika shughuli ya dhifa ya Malkia na watu wenye ulemavu (uk. 1 - 3), pia katika shughuli ya maombolezo na ibada ya mazishi ya Kauye (uk. 20 - 21). Pamoja na dosari hii, wasomaji bila shaka hawatahangaika sana na fasili na fasiri ya mwandishi kwani wengi wao wanalijua neno hili.

Aidha, neno “Zebra” limewekwa katika mabano lakini limetanguliwa na maneno “...sehemu ya wavuka kwa miguu pamechorwa pundamilia.” Hapa msomaji atagundua maana iliyokusudiwa siyo ya picha ya mnyama – Pundamilia. Bali mistari inayochorwa kwa rangi nyeupe na nyeusi (katika sakafu za barabara) mfano wa muonekano wa ngozi ya mnyama Pundamilia. Michoro hii hujulikana kama “zebra

---

<sup>12</sup> Dhifa ni chakula ambacho wanapewa waalikwa katika shughuli (TUKI, 2004).

crossing” kwa lugha ya Kiingereza. Lakini, watumiaji wa barabara hufupisha kwa kutamka “zebra” na wanaelewana katika mawasiliano. Hivyo, kwa watumiaji wa barabara au wenye maarifa kuhusiana na alama za barabarani hawawezi kupata shida kuelewa alichokikusudia mwandishi.

Kitendo cha mwandishi kutumia lugha inayotumiwa na wazungumzaji walio wengi kunaonesha ubunifu wa kimkakati katika kujenga daraja la mawasiliano lililosahihi, rahisi na halisi kati yake na wasomaji wake kuelewana. Hata hivyo, mwandishi hajatoa ufafanuzi wala tafsiri yoyote ya maneno “RB” (zaidi ya kusema “Tumechukua maelezo yenu na hii hapa ni RB kwa ajili ya kumkamata mtuhumiwa. (*Anamkabidhi Chuni kikaratasi*) ...”). Pia, hajatoa ufafanuzi au tafsiri ya neno “bakigraundi.” Jambo linaloweza kuleta shida ya maelewano kidogo sana endapo msomaji hatazingatia kanuni ya kutafuta maana ya jumla badala ya maana inayotokana na neno moja moja.

Kwa jumla, tunachokibaini katika tamthilia ya *Changamoto* ni kutokuwapo kwa matumizi makubwa ya uchanganyaji ndimi, pamoja na ukweli kwamba mwandishi ni msomi. Wahusika wake ni wasomi wa viwango tofauti tofauti na kipindi kilichoizaa kazi yake ni cha soko huria ambacho hata matumizi ya lugha yana uholela wa uchanganyaji ndimi miongoni mwa wazungumzaji. Tofauti na ukweli huu, bila shaka, mwandishi alizingatia zaidi ujenzi wa lugha isiyoonesha ubaguzi kama alivyokusudia kufikisha wazo la ujenzi wa jamii mpya na endelevu isiyo na ubaguzi wa namna yoyote ile. Lengo likiwa ni kuleta usawa kimawasiliano kwa faida ya kila mwanajamii kuyafurahia maisha yake kwa kusudi la Muumba aliyemleta duniani kwa hali na namna aliyonayo.

Kutokuwapo kwa utumiaji mkubwa wa uchanganyaji ndimi hakujaifanya tamthilia hii kuwa chapwa bali kumeifanya iendane na lengo kuu la mwandishi katika mazingira ya kibaguzi kutokana na maumbile ya watu katika jamii. Kazi ingekuwa na ubaguzi wa rangi kati ya wasomi na wasiosoma tungenema mwandishi amepwaya katika kuumba wahusika, mandhari na matukio. Kinyume chake, tunaona mandhari, muktadha, mazingira, wahusika na matukio teule kwa kila ploti vinaonesha wakubwa kutokujinua katika kuonesha usomi na ubaguzi wao kupitia lugha za kikabila au kigeni. Aidha, mandhari, muktadha na mazingira yaliyotumika ni ya kawaida yanayowakutanisha watu wengi, hasa watu wa hali ya chini au kati kiasi.

Uchanganyaji ndimi wa kiwango cha chini au kati kiasi unaoonekana pia katika *Kijiji Chetu*, *Harakati za Ukombozi* na *Safari ya Chinga*. Pamoja na kiwango cha chini cha uchanganyaji ndimi, bado kazi hizi zimesheheni ubunifu wa kumfanya msomaji kutokuchoka pindi azisomapo. Hivyo, kigezo cha uchanganyaji ndimi kuwa wa hali ya chini au kati kiasi hakiwezi kuishusha hadhi kiubunifu tamthilia hii ya *Changamoto*. Kwani tumeona kila jambo hufanyika kwa sababu maalumu yaani ili kufikisha kile alichokikusudia mwandishi (Senyamanza, h. m).

Nayo tamthilia ya *Nje – Ndani* imebainika kuwa na matumizi ya uchanganyaji ndimi ya kiwango cha chini, pia. Matumizi hayo yamehusisha lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Kuna neno moja (1) (“Ok” - uk. 33) na kikundi cha maneno kimoja (1) (“English Speaking Zone” – uk. 63) kutoka lugha ya Kiingereza. Maneno mengine yenye asili ya lugha ya Kiingereza yanaonekana kufanyiwa utohoaji usiokuwa rasmi. Maneno hayo ni “rababendi” (uk. 16) kutoka neno “rubberband”, “netiweki” (uk. 32)

kutoka neno “network”, “pulatebo” (uk. 40) kutoka neno “pooltable”, “ubize” (uk. 64) kutoka neno “busy” na “kubeti” (uk. 87) kutoka neno “bet.”

Uteuzi wa maneno haya unaonesha uhusiano uliopo kati ya utunzi na umilisi wa lugha walionao waandishi husika. Hata hivyo, pamoja na waandishi kuwa vijana, wakiwatumia wahusika wanaonekana kuwa wasomi na wang’amuzi wa mambo, bado waandishi wanaonekana kukwepa matumizi makubwa ya uchanganyaji ndimi. Taarifa zinaonesha kuwa waandishi wote wawili (2) ni wadau wakubwa katika jopo la wanaharakati wanaopigania matumizi rasmi ya Kiswahili sanifu. Bila shaka, uamuzi wa kutokujaza maneno ya lugha za kigeni umefanywa kwa makusudi ili kukwepa mkururo na unafiki wa kupinga kwa maneno ukoloni mamboleo ilhali matendo yao yakithibitisha pasipo shaka kwamba wanauunga mkono. Uthibitisho wa mtazamo huu unajipambanua kupitia mazungumzo baina ya Akili na Moyo kama tunavyoyanukuu: -

**Akili:** [*Sura imesawajika kwa hasira*]. Mimi nimechoka maigizo haya, ninaona kama hayana maana yoyote na yanaidhalilisha. Nimezoea kusema ung’eng’e lakini hapana. Ukitaka tufanye maigizo kwa Kimombo.

**Moyo:** Siwezi kuwa mtumwa katika ardhi yangu huru, shida ya kujiumauma ya nini? Kimombo kina maana gani ikiwa bado tuna shombo? Ninajua tunakipenda na ni muhimu lakini sifikiri kuwa ni busara kutusemea au kutuwakilisha. Ni bora tutamatishe maigizo haya kama sharti lako ndilo hilo. [*Anajifanya kunyanyuka kisha anakaa kitako tena*] Umekuja huku kwetu bado unanichagulia namna ya kusema? Ebo! [*Anakasirika*] (uk. 24).

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Nje-Ndani*, 2016)

Tunachokiona katika nukuu hii ya mjadala kati ya Akili na Moyo ni hali ya mtu kujitambua na kuamua kujitenga na maigizo ya maisha kwa kudhamiria kujitenga kabisa na maisha yaliyojaa unafiki. Bila shaka, jambo hili ndilo lililofanya waandishi hawa vijana kutokutumia kwa wingi uchanganyaji ndimi. Vilevile, tunabaini wazo kuu la waandishi ni kujenga jamii mpya yenye uzalendo wa Kiafrika kwa maslahi mapana ya Waafrika. Kwa hiyo isingekuwa rahisi kwao kujaza matumizi makubwa ya lugha za kigeni ndani ya vita yao dhidi ya ukoloni mamboleo na unafiki wa viongozi na wasomi wa Kiafrika. Huu ni umakini mkubwa unaothibitisha uwezo wa waandishi katika kufuma wazo na lugha bunifu pindi waisanapo tamthilia ya awamu ya soko huria iliyojaa unyang'anyi wa kutisha wa raslimali za wanyonge.

Kwa jumla, utafiti umechunguza matumizi ya uchanganyaji ndimi kutoka tamthilia sita (6) teule. Utafiti umebaini kuwapo kwa tamthilia mbili (2) kutoka kila awamu zenye matumizi makubwa kiasi ya lugha za kigeni. Tamthilia hizo ni *Mashetani* na *Safari ya Chinga*. Tamthilia ya *Kijiji Chetu* haina matumizi ya uchanganyaji ndimi. Tamthilia tatu (3) zilizobakia zimetumia kwa kiasi kidogo sana uchanganyaji ndimi. Tamthilia zilizotumia na ambazo hazikutumia uchanganyaji ndimi zinaonekana kuathiriwa na malengo na ujenzi wa dhamira zilizolenga mwandishi – kiwakati na kisanaa. Kipengele kinachofuata ni kuchunguza uwepesi na ugumu wa lugha katika tamthilia sita (6) teule. Tumeanza na tamthilia teule za awamu ya Azimio la Arusha na kumalizia na zile za awamu ya soko huria.

#### **5.2.4 Uwepesi na Ugumu wa Lugha**

Uwepesi na ugumu wa lugha ni suala la kiuajumi zaidi ambalo haliwezi kujadilika kwa urahisi. Kwa sababu, kile unachokiona kuwa ni chepesi; bila shaka, mwingine

atasema kwake ni kigumu! (Eagleton, 2008). Changamoto hii katika kubaini mipaka ya wepesi na ugumu wa jambo ni suala la kihisia tu sawa na kutafuta mpaka dhahiri kati ya uzuri na ubaya kama alivyowahi kubainisha Leibniz (Broad, 1975). Kumbeni basi, wepesi na ugumu katika kulitazama jambo huamuriwa na tajriba na mapokeo ya msomaji au ya jamii husika na si vinginevyo. Hata hivyo, baadhi ya wanataaluma wanakubaliana kuwa, mara nyingi, ugumu wa lugha ya kisanaa unajitokeza pale mwandishi anapotumia maneno mengi ya lugha ambayo ni mageni kwa wasomaji au wasikilizaji. Pia, ugumu wa lugha hujitokeza pale mwandishi anapotumia kwa wingi mafumbo, ishara na misimu isiyozagaa kwa kiwango kikubwa sana (Low, 2011; Jilala, 2012).

Kwa muhtasari huu kutoka kwa Low pamoja na Jilala, kwa mujibu wa utafiti huu, wepesi wa lugha ya kifasihi ulihesabika kuwapo katika tamthilia teule pale tu tamthilia teule zilipothibitika kuwa hazijatumia ama zimetumia kwa uchache lugha ya sitiara, tashihisi, tafsida, mafumbo, ishara, uchanganyaji ndimi (kwa wasioijua lugha ya pili) na misimu isiyokuwa ya kitaifa. Pili, kama tamthilia zilitumia aina tajwa za semi (hata kama ni kwa kiwango kikubwa) lakini kauli zilizotumika kuwakilisha semi hizi zilionekana siyo ngeni masikioni mwa wasomaji wa tamthilia za Kiswahili. Basi, tamthilia husika zilihesabika kuwa na matumizi ya lugha yaliyomepesi kiubunifu. Kinyume chake, endapo tamthilia teule zilithibitika kuwa na utajiri mkubwa wa lugha ya mafumbo, ishara, misimu na uchanganyaji ndimi wa kiwango cha juu bila tafsiri zake ilhali ni ngeni masikioni mwa wasomaji wengi basi tamthilia husika ilihesabika kutumia lugha ngumu. Utafiti wetu uliongozwa na nadharia ya Fasihi Linganishi ili kujibu maswali: Kwa vipi? Ya nini? Kwa nini?



Lini? na wapi? Jilala (2016) anatumainisha kuwa, lengo la Fasihi Linganishi kama mbinu ya kisanaa, ni kuibua vipengele vinavyofananisha, kutofautisha na kuhusianisha kazi za fasihi za ulimwengu na Fasihi Linganishi za jamii mahususi.

Matokeo na mjadala wa data za utafiti unaonesha kwamba, tamthilia ya *Mashetani* imetumia lugha ya kijazanda na kisitiari kwa kiwango cha hali ya juu. Hali hii inatokana na matumizi makubwa ya lugha ya taswira. Hivyo, kuifanya ionekane kuwa ngumu kwa mtu mwenye uwezo wa chini wa kupasua sitiari. Pia, tamthilia ya *Mashetani* inaonekana kutumia lugha ngumu kwa mwenye uwezo wa chini katika kuhusianisha matukio ya kihistoria na matini halisi. Mfano wa lugha iliyotawala tamthilia hii ni kama inavyojidhihirisha katika nukuu ifuatayo: -

SHETANI: Unanijua mimi nani?  
 Mimi Shetani.  
 Siyo jini wala kuhani.  
 Mimi Shetani.  
 Uwezo wangu hauhifadhiki.  
 Wema wangu hauhisabiki.  
 Ubaya wangu hausemiki.  
 Ninajenga.  
 Ninabomoa.  
 Ninatukuza.  
 Ninadhalilisha nitakavyo.  
 Mimi ni nguvu na nguvu ni mimi.  
 Mimi ni uwezo na uwezo ni mimi.  
 Tazama muujiza. (*Anajibadilisha.*) Sasa mimi nani?

BINADAMU: Kama ndege... vile... ndege.

SHETANI: Sawa. Nimejigeuza ndege. Ninaweza kadhalika kuwa upepo, nikiwa kila mahali. Naweza kuwa

nafsi, nikaingia katika roho yako au ya wenzako. Sasa tazama. Unaona nini?

BINADAMU: Unarukia tawi.

SHETANI: Na sasa, unaona tawi?

BINADAMU: Tawi limegeuka kiti!

SHETANI: Umeshuhudia miujiza. Nimekuonesha miujiza ili uamini uwezo wangu... (uk 1 - 2)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Mashetani*, 1971)

Data katika nukuu hii inaonesha lugha ya kitaswira iliyojaa mafumbo yanayomfanya msomaji kutokuielewa kwa haraka kazi hii. Matumizi ya “Binadamu,” “Shetani,” “ndege,” na “tawi” ni baadhi ya misimbo ya kitaswira inayobeba lugha ya picha na ishara yenye kumfanya msomaji kulazimika kutumia Uhalisia mazingaombwe<sup>13</sup> kupasua sitiari ili kupata maana iliyokusudiwa. Kwa namna maneno haya yalivyotumika ndani ya tamthilia ya *Mashetani*, yanatoa uwakilishi ufuatao: - (i) Binadamu ni mwananchi mnyonge, (ii) Shetani ni mamlaka au kiongozi katili. (iii) Ndege inaashiria uwezo wa hali ya juu wa kufanya jambo kwa namna isiyokuwa ya kawaida. Na, (iv) tawi linaweza kuashiria kitu au mfumo anaotegemea mtawala kuhodhi mamlaka. Maana hizi siyo rasmi.

Kwa hiyo kila msomaji anaweza kuzifasili dhana-picha husika kwa kadri ya uelewa wake. Kwa jumla, tamthilia hii ina utajiri mkubwa wa lugha ya picha na ishara. Utafiti wa S. M. A. Massoud (2013) ulibaini ya kwamba, tamthilia hii ya *Mashetani* ina jumla ya tamathali za usemi zipatazo 160. Tamathali hizo na kiasi chake katika

<sup>13</sup> Kiutunzi, nadharia hii hutumika kulifumba wazo au tukio la kawaida ili lionekane kuwa siyo la kawaida. Kiuhakiki, nadharia hii hutumika kulifichua fumbo au jambo linaloonekana kuwa siyo la kawaida (mfano: sihiri, ulozi, uchawi, ushirikina, miungu, nk) ili lionekane kuwa la kawaida kimaana na kiuhalisi. Mfano, ulozi unaweza kufichuliwa kama mfumo, mali, sera, fursa, rushwa, sheria, nk zinazowadhibititi watu ili wasiweze kwenda kinyume na matakwa ya watawala au kundi maslahi husika (Senkoro, 2007).

mabano ni kwa mchanganuo ufuatao: - sitiari (35), tashibiha (30), takriri (28), taswira (25), ishara (17), tashihisi (10), majazi (8), na mbaalagha (7). Idadi hii ni mbali na matumizi ya nidaa, uchanganyaji ndimi, mdokezo, methali, nahau, misemo, chuku na tabaini.

Matumizi haya ya lugha ya kisanaa yaliyobainishwa na S. M. A. Massoud (2013), yanathibitisha ugumu uliopo katika kuifasili tamthilia hii ya *Mashetani* endapo msomaji hana stadi, maarifa wala upeo wa kuzipasua sitiara zilizotumika. Ugumu wa lugha katika tamthilia hii ulishawahi kuelezwa na wanataaluma wengine, wakiwemo Sengo (1975) na Chiraghdin (rej. utangulizi wa *Jogoo Kijijini na Ngao ya Jadi*, 1976). Mathalani, Sengo anasema “Ebrahim Hussein anaonekana amekua zaidi kwa upande wa uandishi – *Mashetani*<sup>14</sup> ndio mchezo uliopunguza zaidi idadi ya wasomaji wake na kwamba ni watu wachache mno, hata miongoni mwa wasomaji wa kiwango cha juu, wawezao kuusoma na kuuelewa kwa mara ya kwanza [...]” (uk. 80). Huu ni uthibitisho mwingine juu ya matumizi ya lugha ngumu zaidi yaliyotumika katika tamthilia hii.

Pia, tamthilia hii imetumia baadhi ya mandhari za kitaswira kama vile mbuyuni na pangoni. Lynch na Roberts (2010) wanatueleza ya kuwa, kwa asili ya Mwafrika, maeneo haya ni miongoni mwa maeneo yanayoogopwa na, au kuheshimika mno. Kwani huaminika kuwa ni maeneo hatari ambako hukaa viumbe dhahania hasa miungu, mashetani, mizimu na kila aina ya roho chafu. Watu wengine huhusisha maeneo tajwa na utakatifu kutokana na unyeti wake katika ibada za asili (Mulokozi, 2017). Hapa tunapata mantiki ya kwa nini mwandishi akateua maeneo haya mawili

---

<sup>14</sup> Italiki ni ya mtafiti. Katika matini husika tulikonukuu, jina husika halina italiki.

na kuyatumia kuumba mandhari, wahusika, muktadha na matuko. Ndiyo maana tunaona hata baadhi ya wahusika mfano Binadamu, Jini, na Shetani wakiwa ni sehemu muhimu ya mchezo huu. Wahusika hawa watatu ni wa kitaswira zaidi. Kuwapo kwao kunaufanya mchezo kubeba maana iliyofichika ambayo ni ngumu kuelezeka kwa kutumia lugha nyepesi endapo msomaji siyo mahiri wa kupasua sitiara. Vilevile, mwandishi ametumia uchanganyaji ndimi wa kiwango kikubwa bila kuweka faharasa. Jambo hili limechangia kuongezeka kwa ugumu katika kuielewa kazi hii. Kwani, kwa asiyejua Kiingereza mathalani, hawezi kupata maana kamili au kwa urahisi wa kilichosemwa mchezoni.

Tunapochunguza kwa kina msingi wa matumizi ya sitiara katika matumizi ya lugha, uumbaji wazo, wahusika na mandhari, kwa kiwango cha juu tunabaini kwamba, dhamira zilizomo katika tamthilia hii zinafungamana moja kwa moja na mapambano ya dola iliyopindua dola ya awali huko Zanzibar. Mwandishi ametathmini namna tabaka jipya la “wanamapinduzi” lilivyokengeuka na kuanza kutenda na kuishi katika mfumo wa maisha ya kikoloni, kisultani na kibepari. Mfumo huo unaonekana siyo rafiki kwa wanyonge waliowategemea wanamapinduzi kuleta haki, amani, upendo, usawa na ustawi endelevu wa jamii nzima.

Usaliti huu umeelezwa na wanazuoni mbalimbali wakiwemo Okello (1967), Hettiger (h. m.), Lukumbo (2008), Msekwa (2013) na Mbogo (2015). Wanazuoni wanafanana sana katika kuiangazia historia ya mapinduzi na maisha mapya baada ya kile kinachoitwa mapinduzi matukufu ya Zanzibar. Kila mmoja wao anakiri kuwapo kwausaliti na kuibuka kwa makundi yanayosigana. Huku wale walioshiriki mapinduzi hayo kwa kuwa mstari wa mbele katika uwanja wa mapambano, wakiishia kutupwa

nje ya ulingo wa wanufaikaji – sawasawa na wale waliopinduliwa. Taarifa hii haiwezi kuwavutia wale wanaojiita wanamapinduzi. Kwa sababu, baadhi yao hawakuwa mstari wa mbele vitani wala hawakuwahi kushiriki kupanga mikakati ya mapinduzi. Lakini wanatajwa katika machapisho kadhaa kama wazalendo walioongoza mapinduzi husika.

Kwa hiyo, bila shaka mwandishi alifanya haya ili kukwepa mkono wa dola ya wasaliti wa mapinduzi na wananchi waliojenga tumaini kubwa juu yao. Kitendo cha mwandishi kutumia sitiara kwa kiwango cha juu, huonesha kiwango cha juu cha weledi wa mwandishi katika ujenzi wa kazi yake. Pia, huashiria urahisi anaoupata mwandishi kusana wazo ambalo analiona kuwa ni ngumu kulieleza kwa lugha isiyo ya kitaswira zaidi. Hasa kama jambo hilo linagusa na kuathiri mfumo na maisha ya tabaka tawala na vibaraka wao (Mukobwa, 1985; Jilala, 2012; Simon, 2014).

Hata hivyo, pamoja na kuwapo kwa uwezekano wa msomaji kusoma lakini asiweze kuelewa kusudio la mwandishi, bado kuwapo kwa lugha ya ucheshi, misimu na uchanganyaji ndimi kunaweza kumpa ari ya kufurahia na kupenda tamthilia za Kiswahili. Hali hii ipo katika upokevu wa mlaji (Education Standards Research Team, 2012). Kwa mfano, mtu anaweza kusikiliza au kutazama wimbo ambao umetumia lugha asiyoijua lakini akatokea kuupenda wimbo huo kutokana na mapigo ya ala za muziki zilizotumika. Pia, anaweza kuupenda wimbo huo kutokana na utulivu wa sauti za vyombo na mwimbaji, pamoja na maleba na uchezaji wa wasanii. Vilevile, kwa wimbo wenye picha za vitendo anaweza kuona vitendo (uigizaji) ambavyo humsaidia kupata uelewa na kuvutiwa nao (Saarikallio na Erkkilä, 2007). Kwa hiyo, mtu anaweza asielewe maudhui yaani dhamira, lakini akavutiwa na

namna kazi ilivyowasilishwa. Tunapoitazama tamthilia ya *Mashetani*, kwa jicho la ziada, tunaona ina sifa ya kumvutia msomaji kupitia ucheshi na misimu iliyotumika.

Katika tamthilia ya *Kijiji Chetu*, utafiti umebaini kuwapo kwa matumizi ya lugha nyepesi na rahisi kueleweka miongoni mwa wasomaji wanaojua vizuri lugha ya Kiswahili. Hali hii imetokana na uamuzi wa mwandishi kutokutumia kwa wingi taswira na lugha za kigeni. Hata pale alipotumia kauli yenye kubeba maana zaidi ya moja, hakusita kuipa maana aliyoikusudia kupitia mhusika mwingine punde changamoto hiyo ya kimawasiliano ilipoibuka. Mfano ufuatao unathibitisha madai haya:

**MWANAMKE I:** Basi mwana wa watu akajifunga kibwebwe, mwiko mkononi! Akamnyima chakula cha usiku mumewe!!

**MWANAMKE 3:** Chakula cha usiku (*Anakauka kucheka kiasi cha kuwashangaza wenzake*).

**MWANAMKE 2:** Ala babu wee – kitu gani cha kukuchekesha namna hiyo?

**MWANAMKE 3:** Aibu hiyo. Anamchukia kiasi cha kumnyima... (*Anapasuka tena*).

**MWANAMKE I:** Waswahili bwana, wanataka kulipindua kila neno. Husemi neno likabaki na maana ile ile uliyokusudia.

**MWANAMKE 2:** Ai babu we!! Ndiyo cha kukufanya upasuke mbavu, hicho tu! Kumbe ulitaka asemeje?

**MWANAMKE 3:** Ugali.

**MWANAMKE I:** Na kama hali ugali? (uk. 35)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Kijiji Chetu*, 1975)

Kupitia nukuu hii, utafiti umebaini mazungumzo ambayo yana kauli ya ukakasi “...akamnyima chakula cha usiku mumewe!” Kauli hii ina utata kimaana unaoibuliwa na Mwanamke 3 lakini Mwanamke I na Mwanamke 2 wanamrejesha kwenye maana waliyoikusudia. Utata huu inatokana na maana ya msingi (chakula cha usiku au chakula cha jioni) kukutana na maana ya ziada inayobebwa na msembo / tafsida ya “chakula cha usiku” inayomaanisha tendo la ndoa. Kuwapo kwa Mwanamke I na Mwanamke 2 kumesaidia kutambua maana ya ziada iliyofikiriwa na Mwanamke 3. Palepale, wanawake hawa wakabeba jukumu la kutoa ufafanuzi uliosaidia kutoa picha kamili kwa usahihi na haraka pasipo kuacha chembe ya shaka kumea.

Kitendo cha mwandishi kumpa nafasi mhusika wake kutoa ufafanuzi kwa kauli yenye utata, kimesaidia kuifanya tamthilia hii kubeba lugha nyepesi na rahisi kueleweka miongoni mwa wasomaji wanaokitumia Kiswahili katika mawasiliano yao kwa weledi. Pia, urahisi wa lugha unabebwa na historia ya Azimio la Arusha kufahamika kwa wengi. Hivyo, yeyote anayeifahamu historia ya azimio hili hata kwa kiwango cha chini, basi hatapata shida katika kuelewa kwa haraka na wepesi tamthilia hii.

Utafiti katika tamthilia ya *Harakati za Ukombozi* umebaini kuwapo kwa matumizi ya lugha ya Kiswahili kwa asilimia tisini na tisa na pointi kadhaa. Lugha iliyotumika inaonekana kuwa nyepesi na rahisi kueleweka miongoni mwa wasomaji wanaokimudu Kiswahili na kuitambua historia ya Tanzania wakati wa awamu ya Azimio la Arusha. Ushahidi wa kauli yetu umezingatia mifano mbalimbali inayopatikana ndani ya tamthilia husika. Mmoja wa mifano hiyo ni nukuu ifuatayo:

**MZEE:** Waliketi kuliunda Azimio. Sasa wanaketi tena kulisaliti. Ni mahodari kulihubiri majukwaani, lakini kumbe wao wenyewe ndio wasaliti wakubwa wa Azimio. Vijana mtaletaje mapinduzi nyie kweli?

**KIJANA 1:** Hao ni baadhi tu ya viongozi. Wapo viongozi ambao wako katika mkondo mzuri. Wao pamoja na wazalendo wenye moyo safi wameshirikiana kwa pamoja na kuanzisha Chama chetu cha Mapinduzi.

**KIJANA 2:** Tumeanzisha CCM ili kuwapiga vita wapinga mapinduzi hao wachache, wanaotumia mbinu haramu ili kunyonya, kulimbikiza mali na kuhujumu uchumi wetu....

**KIJANA 3:** Twaingia watoboa mashua, kizazi kipya cha Tanzania.

Ni sisi waleta tufani mpya kuuponda ubeberu,

ghasia

dhiki

na unyonyaji.

Sisi ni makaburi,

Wazika uhuru wa bendera,

Wazika walaji asali wa inda,

Wapiga domo kaya juu ya mapinduzi,

Watafuta uhuru wa kweli.

Uhuru wa uchumi,

Uhuru wa siasa,

Uhuru wa utamaduni. (uk. 21 - 22)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Harakati za Ukombozi*, 1982)

Kupitia nukuu hii, utafiti umebaini kutumika kwa lugha ya Kiswahili inayoeleweka kwa urahisi na wepesi. Msomaji anayejua vizuri lugha ya Kiswahili, na kuitambua historia ya Tanzania wakati wa awamu ya Azimio la Arusha, hawezi kupata shida kubaini kinachoelezwa katika nukuu hii. Nukuu hii inazungumzia kwa kifupi historia



ya Azimio la Arusha na kuzaliwa kwa Chama cha Mapinduzi (CCM). Inaangazia pia tathmini fupi itokanayo na kizazi cha Azimio la Arusha dhidi ya utekelezwaji wa azimio hilo na matarajio hafifu waliyonayo kwa kuzaliwa kwa CCM. Tena inagusa namna kizazi kipya cha Chama cha Mapinduzi (CCM) kilivyoweka matumaini makubwa na ari kubwa kwa CCM kama suluhisho la changamoto zinazokwamisha ukombozi wa kweli na endelevu wa Mtanzania mzalendo. Mtanzania huyo si mwingine bali ni yule anayeugulia mateso ya usaliti na unyang'anyi wa ukoloni mamboleo na wakoloni weusi.

Kumbe basi, lugha iliyotumika ni ya kisanaa lakini isiyo na mafumbo wala taswira nyingi zinazoweza kuleta utata na uvuli fikrani mwa msomaji wa tamthilia hii. Hivyo, uteuzi wa lugha ya namna hii unaonesha ubunifu uliomo ndani ya tamthilia husika katika kuteua na kuumba wazo lake kwa kulenga kundi maslahi linalotakiwa kutambua sababu ya kushindwa kwa Azimio la Arusha na kuzaliwa kwa CCM. Mbise (1996) anafafanua hoja hii kwa kusema kuwa, kazi yoyote ile ya kisanaa huwa na lengo fulani kwa jamii. Lengo hilo humsukuma mwandishi kuamua namna, aina na kiasi cha ubunifu atakachotumia kuiumba sanaa yake.

Kwa hiyo, matumizi ya lugha ngumu au nyepesi siyo kipimo pekee cha ubora na udhaifu wa sanaa husika. Kwa sababu, kwa baadhi ya wanafasihi hususani wanaoamini katika mkabala wa kimaudhui, kama sanaa haimgusi msomaji na kumsaidia kutatua changamoto zake za kila siku; basi sanaa hiyo haina msaada wowote kwa jamii (Wamitila, 2002). Baada ya kuchunguza matumizi ya lugha (uwepesi na ugumu) katika tamthilia teule tatu za Azimio la Arusha, sehemu

inayofuata inaangazia matumizi ya lugha (uwepesi na ugumu) katika tamthilia teule tatu za awamu ya soko huria.

Utafiti umebaini tamthilia ya *Safari ya Chinga*, pamoja na matumizi makubwa ya matamshi na lafudhi ya Kimakonde, lugha iliyotumika inaeleweka kwa wepesi miongoni mwa wasomaji wenye weledi wa lugha ya Kiswahili, Kiingereza (kwa maneno ya Kiingereza yaliyotumika) na utamaduni wa Kibantu. Aidha, katika kuhakikisha mawasiliano kati ya msomaji na mwandishi hayakutani na kizingiti, mwandishi amefanya tafsiri kwa kauli na maneno yanayotokana na lugha ya asili au misimu inayopatikana katika ukanda wa Kusini mwa nchi ya Tanzania. Sehemu ya kwanza ya tafsiri inaonekana katika dua zilizofanywa na mzee Che Mundu na mkewe - Bi. Somoe. Data ifuatayo inathibitisha kile kilichobainika katika utafiti wetu:-

**Che Mundu:** *(Anachukua kata ya maji anakunywa, kisha anamrushia Mata yale maji ya kinywani utosini). Phwaa! (Anachukua mtama katika mkungu na kumwaga chini kidogokidogo). Nangu Che Mundu chingutenda kulembela kwa ajili ya mwanangu Matatizo. Ahena mbali kudaresalama. Hambu nangu ngutenda kuyuwa kwa wazee wohewohe mulongolele mbele. Akina nzee Ntongwechu, Nandoka, Chindengu, Chikandema na vanji vohe. Munnole mdukulu wenu kwahena kwa vanu. Anapate matatizo lohelohe. Kwangu nangu hambu nanga malove chondechonde, ndimalila.*

*(Mi Che Mundu ninaomba kwa ajili ya mwanangu, Matatizo. Anaenda mbali Dar es Salaam. Mimi ninachofanya ni kuomba kwa wazee wote mliotangulia mbele za haki. Akina Ntongwechu, Nandoka,*

Chindengu, Chikandema na wengine wote. Mumlinde huyu mjukuu wenu anaenda kwa watu. Mumuepushe na matatizo yoyote. Mimi sina maneno mengi ila nakuombeni chonde chonde. Nimemaliza). (uk. 20)

**Bi. Somoe:** (*Anachukua kata ya maji anakunywa, kisha anamrushia Mata yale maji ya kinywani utosini*). Nangu chingutenda kulembela kwa mwanangu Matatizo kuhena aneko mbali. Hambu mwanangu vikale na vazee mmohemohe mulongolele nangu ngutenda kuyuwa munole mwana aneyo anapate matata chonde chonde chonde, nangu nimalila.

(Mimi naomba mwanangu Matatizo anaenda mbali. Mwanangu usiwe na tabia tofauti ukae vizuri na wenyeji wako. Wazee wote mliotangulia nawaombeni mumuangalie huyu mtoto asipate matatizo. Chonde chonde, nimemaliza). (uk. 21)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Safari ya Chinga*, 2009)

Kuwapo kwa tafsiri za dua zilizofanywa na Che Mundu na Bi. Somoe kunawafanya wasomaji kutambua na kuelewa kila kitu kilichosemwa na wazazi hawa kwa kijana wao, Mata. Endapo mwandishi asingeweka tafsiri, basi wasomaji wasioifahamu lugha iliyotumika wasingeweza kufahamu kilichosemwa. Hivyo wangeona kipande hiki cha dua kuwa ni sehemu ngumu kwao. Kitendo cha mwandishi kuweka tafsiri ya dua husika, ni dhahiri wasomaji wake watasema tamthilia imetumia lugha nyepesi kwa wao kuelewa dhamira na kuifurahia fani ya kazi hii. Pia, katika kuhakikisha lugha haiwi kikwazo kwa msomaji katika kuvuna dhamira na kuifurahia fani iliyotumika, mwandishi ameweka sherehe. Baadhi ya vitabu hutumia neno “Faharasa” badala ya “Sherehe” (Mdee, 2006). Mdee (2006) anafasili sherehe kama

orodha ya msamiati na maana zake katika andiko mahususi ili kumpa urahisi msomaji kulielewa andiko husika bila kupata ugumu wowote. Sherehe ya mwandishi wa *Safari ya Chinga* imesheheni sehemu kubwa ya msamiati unaotokana na misimu, maneno ya Kiingereza na kikabila. Sherehe hiyo ya *Safari ya Chinga* tunainukuu hapa:

<b>Buku tano</b>	Elfu tano
<b>Changu</b>	Changudoa
<b>Chikandanga</b>	Mchanganyiko wa unga wa nafaka pamoja na ming'oko iliyochemshwa na kupondwa
<b>Demu</b>	Msichana, rafiki wa kike
<b>Fasta</b>	Haraka
<b>Funda</b>	Twanga vitu vikavu mpaka vilainike viwe unga
<b>Kikupwa</b>	Kipande kikuu kuu cha mkeka au jamvi
<b>Kindende</b>	Kisigino
<b>Mamwera</b>	Polisi
<b>Mbilini</b>	Katika ndoa
<b>Ming'oko</b>	Aina ya mizizi kama mihogo inayoota porini
<b>Njini</b>	Mjini
<b>Pamba</b>	Nguo
<b>Shingi</b>	Shilingi
<b>Tendegu</b>	Mguu wa kitanda (uk. 57)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Safari ya Chinga*, 2009)

Orodha iliyonukuliwa ni jumla ya msamiati na maana zake zinazopatikana katika tamthilia teule. Kitendo cha mwandishi kuweka kipengele cha sherehe mwishoni mwa tamthilia yake kumewasaidia kwa kiwango kikubwa wasomaji waliokuwa hawajui maana ya maneno tuliyoyanukuu, kuyafahamu. Kwa wao kufahamu maana, kutawawezesha kujenga uelewa kamili wa wazo lililoumbwa katika muktadha wa

sentensi zilizobeba misamiati husika. Kwa mantiki hii, tunaweza kusema ya kwamba tamthilia ya *Safari ya Chinga* kwa kiasi kikubwa imetumia lugha nyepesi, na yenye kueleweka kirahisi kwa mjuzi wa lugha ya Kiswahili. Pia, tamthilia hii imetumia ubunifu wenye kumuongezea msamiati mpya mtumiaji wa lugha ya Kiswahili ambaye hana utajiri wa mawanda ya msamiati wa Kiswahili sanifu na Kiswahili cha kisanaa.

Si hivyo tu, mwandishi amejitahidi kuyaandika maneno mengi ya kigeni aliyoyatumia kwa namna ambayo hata anayejua kusoma Kiswahili lakini hajui Kiingereza asishindwe kusoma wala kulielewa neno husika. Maneno ya Kiingereza mengi yameandikwa kwa kutumia tahajia ya Kiswahili badala ya tahajia ya Kiingereza. Maneno yaliyoandikwa kwa kutumia tahajia ya Kiswahili ni *fegi, jinzi, nayamaindi, kisoja soja, asikirimu, fotokopi, fasheni, chenji, tulichosevu, na solusheni*. Ilhali, maneno ya Kiingereza yaliyoandikwa kwa tahajia ya Kiingereza ni manne (4) pekee ambayo ni *town, yes, original, na diet*. Kwa sehemu kubwa maneno haya manne (4) yanaonekana kutokuwa mageni masikioni mwa jamii ya watu wanaotumia au kuishi miongoni mwa watumiaji wa Kiingereza.

Kuwapo kwa maneno haya manne (4), kunabeba maana fulani kisanaa - kwa mwandishi na wasomaji wake. Kama mwandishi angekuwa amefanya kwa bahati mbaya, basi hata yale maneno mengine kumi (10) ya Kiingereza yaliyoandikwa kwa tahajia ya Kiswahili yangeandikwa kwa Kiingereza kama ilivyo kwa haya manne (4). Kitendo cha mwandishi kutumia tahajia ya Kiswahili kwa maneno ya Kiingereza kunatoa ushahidi mwingine wa weledi wa mwandishi katika kuumba mtandao wa mawasiliano chanya kati yake na wasomaji wake kupitia kazi yake. Hii inatufanya

tubaini ya kuwa, Shani Omari amecheza na lugha hizi sawa na watumiaji wa Sheng kule nchini Kenya. Sheng ni aina ya uzungumzaji au lugha isiyorasmi iliyozaliwa na wazungumzaji wanaojua lugha ya Kiingereza (kwa kiasi kikubwa) na Kiswahili (kwa kiasi). Hivyo kujikuta wakiunda misamiati inayotokana na uunganishaji wa maneno au sehemu ya maneno ya lugha hizi mbili.

Kwa sasa, aina hii ya uzungumzaji ina watumiaji wengi sana nchini Kenya, hasa katika Jiji la Nairobi na viunga vyake. Wengi wa watumiaji wa Sheng ni vijana kuliko rika nyingine nchini Kenya (Githiora, 2002). Penelope (2000) anatumiaji kuwa, tofauti ya uzungumzaji na uzaliwaji wa lugha mpya hutokana na mambo mengi yenye kufungamanisha hisia, uchumi, sosholojia, utamaduni, teknolojia, uhamaji watu, elimu, maendeleo na mabadiliko ya kijamii. Na kwamba, hali hii huwezi kuidhibiti kwa namna yoyote ile. Kwa sababu, jamii hasa vijana huzalisha msamiati na namna ya uzungumzaji kwa haraka zaidi kuliko wafanyavyo taasisi za ukuzaji na ustawishaji lugha.

Naye Momanyi (2009) anatumiaji kwamba, kwa zama hizi, watu wengi wanaendelea kuathiriwa na utamaduni wa kuchanganya ndimi au kuunda maneno mapya kusikorasmi – kupitia udondoshaji na uambatishaji. Na kwamba, haya yote yanatokea kama sehemu ya matokeo ya kuishi katika ulimwengu huru wa utandawazi. Watu wanaonekana kuwa mbele zaidi ya ulimwengu rasmi wa wadhibiti na wathibiti lugha. Aina hii ya uzungumzaji ipo pia hata nchini Tanzania japo siyo kwa kiwango sawa na Kenya. Kwa hiyo basi, tunahitimisha hoja ya uwepesi na ugumu wa lugha katika tamthilia ya *Safari ya Chinga* kwa kusema ya kwamba, lugha iliyotumika inaeleweka kwa urahisi na haraka miongoni mwa wasomaji

wanaokimudu Kiswahili na kile kinachoitwa “Kiswangilishi.” Msanjila (2011) anatumia lugha ya kwamba, lugha ina uhusiano mkubwa na sosholojia ya jamii yenye kutumia lugha. Kwa hiyo jamii lugha inayotumika kwa sana miongoni mwa kundi maslahi huonesha ukubalikaji na umaslahi wake kwa jamii husika.

Kwa upande wa tamthilia ya *Changamoto*, utafiti ulichunguza na kubaini ya kwamba, pamoja na kuwapo kwa salamu ya Kihehe ambayo haijatafsiriwa, bado kazi hii kwa sehemu kubwa inaonekana kutumia lugha ya kawaida inayoeleweka kwa wepesi na urahisi miongoni mwa wasomaji wa kazi bunilizi za Kiswahili. Ufuatayo ni mfano wa lugha inayoeleweka kwa wepesi na urahisi: -

**Malkia:** Ni furaha yangu kuwapo mahali hapa na kukutana nanyi. Leo ni siku ya mwaka mpya na nimeonelea ni jambo jema tuwe na utaratibu wa kukutana kila mwaka. Lengo la siku hii ni kutiana moyo na kutakiana heri katika mwaka mpya unaoanza na siku ya leo. (*Hadhira ambayo ni walemavu na wasio na ulemavu inapiga makofi na kushangilia*). Jambo la msingi ni kuwaomba msitumie upungufu wenu wa viungo kama kikwazo, hapana. Upungufu huo uwe ni changamoto ya kukuleteeni maendeleo. Hakuna haja ya kulilia mkono au mguu uliopotea. Bali ni kutumia viungo vilivyobakia katika kuchakarika ili kujitafutia riziki. (*Walemavu wanapiga makofi*). Kwa hayo machache, nawakaribisha sana kwenye hafla hii niliyowaandalieni ili tule, tunywe, na tufurahi. Asanteni. (*Anaondoka na kurudi mahali pake na anakaa. Watu wanapiga makofi sana na kushangilia*). (uk. 2 – 3)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Changamoto*, 2010)

Kauli ya Malkia kama kiongozi mkuu wa nchi inaonesha matumizi ya lugha ya kawaida, nyepesi na inayoeleweka vizuri miongoni mwa watu wanaojua na kuitumia

lugha ya Kiswahili katika matumizi mbalimbali. Kwa nafasi ya Malkia, kama angekuwa mtu mwenye majivuno, bila shaka angetumia uchanganyaji ndimi mwingi. Hata Kiswahili kingebeba msamiati unaobeba taaluma tofauti tofauti mfano za utabibu, siasa, sheria, uchumi, teknolojia na theolojia kueleza haya tunayoyaona katika nukuu. Lakini kwa kutambua changamoto za watu wenye ulemavu, aina ya hadhira, lengo kuu la lugha katika jamii, saikolojia na heshima aliyopewa na jamii inayomzunguka ambayo ni tofauti na ile ya Umofia katika riwaya ya *Shujaa Okonkwo* (Achebe, 1973), Malkia anaamua kutumia lugha nyepesi na rahisi kueleweka.

Uteuzi huu wa lugha unaonesha mapinduzi na hamasa kwa watunzi na wasomaji. Kwamba, mabadiliko ya kijamii dhidi ya watu wenye ulemavu hayaepukiki bali yanapaswa kupewa msukumo, thamani na nafasi chanya katika jamii. Kumbe basi, ubunifu wa utunzi huu siyo wa bahati mbaya bali umezingatia lengo la mwandishi, muktadha wa tukio na wahusika teule. Tunagundua haya yametokea ili kujenga ulimwengu wa kitamthilia unaofungamana na mahitaji halisi ya watu (Culpeper na wenzake, 1998). Hata kwa aina ya salamu iliyotumia maneno matatu (3) pekee ya kikabila, kisaikolojia watumia lugha wasiojua maana huwa hawapati taabu kwa imani kwamba hiyo ni salamu ambayo haina athari kwao. Kwa sababu nao hutenda vivyo hivyo (Muysken, 2000). Changamoto huwa kwa wale wasioenzi lugha za asili yao. Hawa wataona huu ni mwendelezo wa kuendekeza ukale na ukabila. Lakini kwa wabantu wengi, wataona ni fahari kukumbuka asili yako hata kwa salamu ya asili ya jamii yako. Tena, si ajabu maneno katika salamu hii yanafanana au kukaribiana na maneno yanayopatikana katika salamu za makabila mengine ya Kibantu. Kwa



mujibu wa Massamba (2002), upo ushahidi usio na shaka kihistoria na kiisimu unaoonesha jamii nyingi za Kibantu zinafanana sana katika msamiati, miundo ya tungo, maana, miundo ya vitenzi na ujifunzaji wake.

Hata hivyo, Muysken (2000) anaeleza kuwa, pale inapotokea mazungumzo yakaendelea kwa muda mrefu, hata kama ni sehemu ya salamu, msikilizaji asiyejua lugha husika huanza kuhisi mazungumzo hayo yana jambo la mficho ambayo yanambagua. Hivyo, kuanza kutamani kujua kiini cha mazungumzo husika. Asipopata msaada wa maana ya kilichokuwa kinasemwa, msikilizaji huyu huona kuwapo kwa ugumu wa kimawasiliano na kimahusiano. Bila shaka, kwa kuutambua ukweli huu, mwandishi Elizabeth Mahenge akaona si vema kuibua ugumu usio na sababu ilhali walengwa wake ni jamii pana yenye lugha tofauti tofauti – mbali na Kihehe.

Hata uteuzi na utumiaji wa maneno ya Kiingereza “MC” na “RB” hakuoneshi kuleta ugumu kimawasiliano hata kama watu wengi wanaweza wasiwe wanajua virefu vyake. Lakini kwa maana za kimuktadha na kiutumizi si shaka kwamba jamii za watumia lugha ya Kiswahili na wale waliowahi kuhudhuria au kusikiliza masimulizi yahasuyo sherehe zenye washehereshaji au mashitaka yaliyofikishwa kituo cha Polisi, watakuwa wanayafahamu maneno haya na maana zake – hata kama siyo kwa usahihi.

Kwa upande wa tamthilia ya *Nje – Ndani*, utafiti umebaini kuwapo kwa lugha yenye mafumbo inayohitaji msomaji kufikiria kwa makini. La sivyoy, mtu huyo kuwa mfuatiliaji mzuri wa mazungumzo na matukio mbalimbali yanayotokea katika jamii ya Mtanzania ili kuweza kuielewa lugha na dhamira zilizoumbwa na waandishi.

Tofauti na hapo, msomaji ataishia kusema tamthilia hii ni ngumu kuelewa kwani imetumia lugha ngumu. Mfano wa umbo linalopatikana katika tamthilia hii likibeba lugha ya picha ni hili tunalolinukuu hapa chini:-

**Macho:** [*Kwa upole na ufukunyuzi*], Vipi mmeanza kuchimba?

**Moyo:** Kuchimba kitu gani?

**Macho:** Mali ya ardhini.

**Moyo:** Aaaaah! Viazi, mbona kitambo?

**Macho:** Hongereni sana.

**Moyo:** Kwa lipi tuhongere? Hatupiki wala hatuli zaidi ya kupakua.

**Moyo:** Hata hivyo, viazi vyenyewe si vingi kwa wote. Sisi wengine faida tuipatayo ni mashimo kwa ajili ya kujengea vyoo vyetu baada ya viazi kuchimbwa.

**Macho:** Hata kule nilikotoka hakuna tofauti kubwa na hapa.

**Akili:** Kama twiga na faru.

**Akili:** Haya ndovu na pembe zao

**Moyo:** Wamefanyaje?

**Akili:** Wanapaa.

**Akili:** Afadhali mashimo, hawa si mkia, si ngozi, si kwato.

**Moyo:** Ubeberu.

**Akili:** Ubeberu wa mbuzi au kondoo?

**Moyo:** Si mbuzi wala kondoo. Ni makuwadi wa soko holela. Hula njama na wanyonyaji. Sasa ili uwalinde basi wahitajika kuwa watu.

**Moyo:** Haya baada ya hapo faida gani kubwa yaja?

**Akili:** Kujipendekeza tu. (uk. 72 - 75)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Nje-Ndani*, 2016)

Ukichunguza katika mifano iliyotolewa kwenye nukuu hii, utaona kuwa mazungumzo kati ya Akili, Macho na Moyo yanathibitisha ubunifu wa lugha ya kitaswira na kimapumbo iliyojengwa katika tamthilia hii. Kwa mtu mwenye upeo wa

chini katika kupembua mambo, au asiyekuwa na utamaduni wa kufuatilia matukio halisi yanayotokea katika jamii yake – ndogo na pana, bila shaka nukuu hii itaonekana ni ngumu ijapokuwa imetumia lugha ya Kiswahili. Kwa hiyo, ili msomaji aweze kuielewa kwa urahisi kazi hii, sharti aweze kufikiria kwa makini na kuwa mfuatiliaji mzuri wa matukio mbalimbali yanayotokea katika jamii hasa ya Mtanzania. Zaidi ya hapo, lazima awe mweledi na mtumiaji mzuri wa nadharia ya Uhalisia mazingaombwe.

Uhalisia mazingaombwe ni nadharia ya kisanaa na kihakiki ambayo Senkoro (2007:03) anaitazama kama “mtindo au aina ya fasihi ambamo mazingaombwe / uchawi au mambo ambayo hayafanani na ya kawaida yaliyozoeleka kwa hadhira hutokea sambamba na yale ambayo ni ya kawaida. Yote haya hutokea katika mandhari au mazingira ambayo kwa kiasi kikubwa sana yana uhalisi tunaoujua [...]. Ukiondoa maajabuajabu yanayojitokeza, unabaki na visa ambavyo ni vya kawaida tulivyovizoea.” Kwa maelezo ya Senkoro, tunaweza kufananisha uhalisia mazingaombwe na mawingu mazito, moshi mzito au uvulivuli unaofunika anga. Ama, tunaweza kufananisha na eneo fulani lenye kuleta hali ya taharuki yenye usiri mzito ndani yake. Kwa namna ambayo hali isiyo ya kawaida hutawala fikra na uoni wa mtu.

Lakini punde hali hiyo ikiondoka, basi mambo hujionesha katika uhalisi wake na kumfanya msomaji au mtazamaji kung’amua ya kwamba mawingu mazito ama moshi mzito au uvulivuli uliotanda fikrani au machoni mwake ulikuwa ni uwakilishi wa dhana au jambo mahususi kwa njia fiche. Hali hii hutokea pia ndani ya matini ya kisanaa kutokana na uteuzi na ujenzi makini wa vijenzi kadha wa kadha vya kifani

na kimaudhui. Baadhi ya vijenzi hivyo ni: lugha ya kitaswira, wahusika wa kitaswira, wazo la kitaswira, mandhari ya kitaswira, itikadi kupitia taswira, falsafa kupitia taswira, muktanda wa kitaswira, na mambo mengine yoyote ambayo yasingewezekana kuelezwa kwa uwazi pasipo kuleta dhoruba miongoni mwa wanajamii - hasa wanajamii wasio na kiasi. Ndiyo maana Senkoro anaona uhalisia mazingaombwe ni ujabuajabu ama uchawi katika kuuzuga ukawaida machoni na fikrani mwa watu.

Kwa jumla, tunaweza kusema ya kwamba, tamthilia ya *Nje-Ndani* imetumia lugha ngumu kiasi ambayo inamuwia vigumu msomaji asiyesoma matini haya kwa utulivu na umakini mkubwa. Ama, kwa yeyote asiyefuatilia matukio yanayotukia katika jamii au asiye na weledi katika uhakiki wa matini ya kimazingaombwe. Kwa Wanauhalisia mazingaombwe, ugumu katika kazi bunilizi ni matokeo ya mhakiki na, au msomaji kushindwa kufahamu kusudi hasa la maandishi. Hivyo, kuishia kuiona kazi husika kama zao lisilokuwa na mvuto wala ushawishi kwa msomaji (Warnes, 2006). Matumizi ya lugha ngumu waliyotumia maandishi wa tamthilia ya *Nje-Ndani* yanatokana na dhamira walizotathmini na kuyawasilisha mbele ya kaumu. Tunapochunguza dhamira zao, tunabaini ya kwamba, maandishi wanawakejeli watawala huku wakifumua na kuanika hadharani uozo na uvundo unaofichwa na watawala na vibaraka wao - kwa kila hali.

Katika hali ya kawaida, dhamira za namna hii haziwezi kufurahiwa na watawala manyang'au. Hivyo, mwandishi anayeamua kujivika bomu na kujilipua machoni pa watawala hawa, hujikuta akipata vitisho na, au hata kuuu. Hapa tunakutana na tabaka la mfumo wa maisha ya kikoloni, kidikteta, kisultani na kibepari. Mfumo huu

haujawahi kuwa rafiki kwa wanyonge waliowategemea wanamapinduzi kuleta haki, amani, upendo, usawa na ustawi endelevu wa jamii nzima. Aidha, mfumo huu huwa siyo rafiki kwa waandishi wa namna hii. Ndiyo maana katika kukwepa mkono wa dola, waandishi hawa kwa makusudu wakaamua kutumia sitiara kwa kiwango cha juu. Walifanya hivi ili kulifumba wazo husika na hatimaye kuwaachia wasomaji kusoma na kutafsiri kwa kadri ya upeo wao katika kupasua sitiara. Mbinu hii ya kisanaa huonesha kiwango cha juu cha mwandishi katika ujenzi wa kazi yake (Mukobwa, 1985). Pia, humpa mwandishi urahisi wa kulisuka wazo ambalo analiona kuwa ni ngumu kuelezeka kwa lugha isiyo ya kitaswira zaidi. Hasa kama jambo hilo linagusa na kuathiri mfumo na maisha ya tabaka tawala na vibaraka wao (Jilala, 2012; Simon, 2014).

Pamoja na kuwapo kwa uwezekano wa msomaji kusoma lakini asiweze kuelewa kusudi la mwandishi, bado matumizi ya lugha ya ucheshi, misimu na uchanganyaji ndimi humpa msomaji husika ari ya kufurahia na kupenda tamthilia za Kiswahili. Hali hii ipo katika upokevu wa mlaji (Education Standards Research Team, 2012). Kwa mfano, Saarikallio na Erkkilä (2007) wanatueleza kuwa, mtu anaweza kusikiliza au kutazama wimbo ambao umetumia lugha asiyojua lakini akatokea kuupenda wimbo huo. Ataupenda wimbo huo si kwa sababu anaelewa kinachoimbwa; bali kwa sababu kadhaa. Sababu hizo ni pamoja na: (i) kuupenda wimbo husika kutokana na mapigo na ala za muziki zilizotumika. (ii) kuupenda wimbo husika kutokana na utulivu wa sauti za vyombo na mwimbaji. (iii) kuupenda wimbo husika kutokana na uchezaji wa wasanii. Na, (iv) kwa wimbo wenye picha zinazoakisi matendo fulani fulani, anaweza kuona vitendo (uigizaji) ambavyo

humsaidia kuelewa kile kinachoimbwa na hatimaye kuvutiwa. Kwa hiyo, mtu anaweza asielewe dhamira lakini akavutiwa na namna kazi ilivyowasilishwa. Tunapoitazama tamthilia ya *Nje-Ndani*, kwa jicho la ziada, tunaona ina sifa ya kumvutia msomaji kupitia ucheshi uliojengwa.

Kwa jumla, utafiti umebaini kuwa tamthilia ya *Mashetani* ni ya kwanza kwa matumizi ya lugha ngumu ikifuatiwa kwa mbali kiasi na tamthilia ya *Nje-Ndani*. Lakini, tamthilia za *Kijiji Chetu*, *Harakati za Ukombozi*, *Safari ya Chinga* na *Changamoto* zinaonekana kutumia lugha nyepesi inayoeleweka kwa urahisi miongoni mwa wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili.

Muhtasari wa matokeo ya utafiti juu ya matumizi ya lugha unaonesha kuwa: - (i) tamthilia zote sita (6) teule zina lugha ya ucheshi kwa viwango na aina tofauti tofauti. (ii) Tamthilia zote sita (6) teule zina lugha ya misimu kwa viwango na aina tofauti tofauti. (iii) Tamthilia tano (5) teule kati ya sita (6) zina uchanganyaji ndimi kwa viwango na aina tofauti tofauti. Tamthilia ya *Kijiji Chetu* ndiyo tamthilia pekee iliyothibitika kutokutumia lugha ya uchanganyaji ndimi. (iv) Tamthilia mbili (2) teule kati ya sita (6) zinaonekana kutumia lugha ngumu huku tamthilia nne (4) zilizobaki zinaonekana kutumia lugha nyepesi - kwa viwango na aina tofauti tofauti.

Msingi mkuu wa utofauti na mfanano wa matumizi ya lugha ndani ya tamthilia hizi sita (6) teule unatokana na uhusiano kati ya ubunifu wa waandishi husika na matukio yanayojitokeza na kutawala nyanja na nyakati mahususi za maisha ya watu nchini Tanzania. Pia, utafiti umebaini kuwapo kwa utofauti na mfanano wa matumizi ya lugha unaotokana na msisitizo maalumu kutokana na matukio yanayoathiri maisha ya watu katika nyanja na nyakati mahususi za maisha nchini Tanzania. Kwa mfano,

matumizi ya lugha katika tamthilia tatu (3) teule za awamu ya Azimio la Arusha yamekita zaidi katika athari za siasa na ukoloni kwa taifa katika kipindi husika. Huku, matumizi ya lugha katika tamthilia tatu (3) teule za awamu ya soko huria yamejikita zaidi katika kuchochea mjadala unaogusa ukoloni mamboleo na athari yake kwa jamii ya leo.

Hii yote ni kwa sababu, wakati na mazingira yaliyomlea mwandishi huchangia sana mwandishi mmoja au tofauti tofauti kuandika jambo lile lile kwa namna ama ile ile au tofauti (Soyinka, 1979; Culpeper na wenzake, 1998; Maake, 2006; Ruhumbika, 2006; Adeseke, 2016; Senyamanza, h. m.). Soyinka (1979), Ruhumbika (2006) na Jilala (2012) wanaongeza kuwa, mifumo ya kiutawala ina mchango mkubwa katika kumfanya mwandishi kuwa huru au mtumwa katika kubuni na kuwasilisha wazo lake kwa namna anayoona inafaa. Kwa muktadha huu, njia ya uteuzi na uwasilishaji wa matumizi ya lugha kati ya mwandishi mmoja na mwingine, au mwandishi yuleyule mmoja katika kazi zake kadhaa ndiyo huleta utofauti kiubunifu. Kwani wakati, mazingira na mifumo ya kiutawala ndani ya jamii anamoishi mwandishi huamua hatima ya mwandishi kisanaa.

Mjadala huu unaungwa mkono na Wanafasihi Linganishi wa mlengo wa Kifaransa na zaidi sana wale wa Kimarekani. Kwa Guyard (katika Cao, 2013), ulinganishaji wa fasihi za jamii moja au tofauti tofauti unapofungamanishwa na historia ya jamii kupitia mahusiano ya fasihi kitaifa na kimataifa huibua kufanana na kutofautiana. Kwa sababu jamii zinazohusiana huwa na tabia ya kuathiriana moja kwa moja au kwa kiasi katika nyanja mbalimbali za maisha. Kuathiriana huko kunaweza kuwa kwa kufanana au kutofautiana (Cao, 2013). Hali hii hutokana na tofauti au mfanano

wa mawasiliano ya dhati yanayohusisha pande mbili za sanaa au zaidi. Mawasiliano hayo ni kati ya kazi na kazi, pia misukumo na maisha ya waandishi wa fasihi kadhaa ndani na nje ya mipaka ya fasihi hizo ndani ya wakati na mazingira mahususi (Carrer, katika Cao, 2013). Mambo haya yote yanapomsonga mwandishi, humfanya mwandishi husika achague mwelekeo wa mwono wa sanaa yake kiubunifu – ama kwa kujua au kwa kutokujua. Hatimaye, mwandishi huyo hutoa kazi inayofanana au kutofautiana na waandishi wengine au kazi zake nyingine - ama kwa karibu au kwa mbali (Cao, 2013).

Kwa jumla, matumizi ya nadharia ya Fasihi Linganishi yametusaidia sana katika kubaini kwa vipi, ya nini, kwa nini, lini na wapi matumizi ya lugha ya tamthilia zote sita (6) teule yanafanana, kutofautiana na kuhusiana. Tamthilia zote sita (6) teule zimebainika kujadili matumizi ya lugha yanayofanana na kutofautiana katika kubeba dhamira. Kupitia lugha teule, dhamira za msingi kwa mnyonge zimejengwa kiubunifu na kiweledi. Dhamira zote ni mwendelezo wa kilio cha watu wanyonge katika jamii.

### **5.3 Hitimisho**

Sura hii imewasilisha matokeo ya utafiti juu ya lengo la pili la utafiti huu ambalo ni kulinganisha ubunifu katika matumizi ya lugha yanayojitokeza katika tamthilia teule za Kiswahili za awamu ya Azimio la Arusha na zile za soko huria ili kubaini kama kuna ubunifu endelevu. Matokeo yamethibitisha kuwapo kwa ubunifu endelevu miongoni mwa tamthilia zote sita katika matumizi ya lugha ya ucheshi, lugha ya misimu, uchanganyaji ndimi, na wepesi na ugumu wa lugha kwa wasomaji. Kila tamthilia ina mkito wake katika kutumia lugha ya kisanaa. Lugha iliyotumika katika



kila tamthilia teule ina athari kubwa katika uumbaji na uwasilishaji wa maudhui. Sura inayofuata inawasilisha tathmini ya athari ya ubunifu wa dhamira na matumizi ya lugha katika kuchochea maendeleo endelevu ya Tamthilia ya Kiswahili.

## **SURA YA SITA**

### **ATHARI YA UBUNIFU WA DHAMIRA NA MATUMIZI YA LUGHA KATIKA KUCHOHEA MAENDELEO ENDELEU YA TAMTHILIA YA KISWAHILI**

#### **6.1 Utangulizi**

Sura hii inabeba mjadala wa kina unaoangazia namna ubunifu katika tamthilia teule unavyosaidia msomaji wake kujikomboa kifikra hata kumwezesha kuyamudu maisha yake katika nyanja anuai za maisha. Ukombozi huo ndio unaoweza kumfanya mtunzi na msomaji kupenda na kuendelea kutunga, kununua na kusoma tamthilia za Kiswahili zenye ubora kifani na kidhamira kwa faida binafsi ya binadamu na sanaa husika. Sura hii inajibu swali la tatu la utafiti wetu ambalo ni “kwa vipi athari ya ubunifu katika dhamira na matumizi ya lugha yanayojitokeza katika tamthilia teule za Kiswahili za awamu ya Azimio la Arusha na zile za soko huria yanaweza kuchochea maendeleo endelevu ya Tamthilia ya Kiswahili kisanaa?”

#### **6.2 Athari ya Ubunifu Endelevu katika Tamthilia ya Kiswahili**

Tathmini ni mfumo sanifu wa kisayansi wa kuchunguza ufaafu na utofaafu wa jambo ili kupendekeza nini kifanyike kwa tija ya leo na siku zijazo (Unterhalter, 2019). Matokeo ya utafiti chini ya tathmini hii hayawezi kuwa jumuishi bali yatajengwa katika tamthilia teule tulizozichunguza. Matokeo haya yanajibu lengo mahususi la tatu lilikusudia kujibu maswali madogo matatu (3) yatokanayo na swali mama moja (1). Maswali hayo madogo ni:- (i) Je, kuna ongezeko la dhamira ama la? (ii) Je, kuna ongezeko la matumizi ya lugha ama la? (iii) Je, ubunifu katika tamthilia teule unasaidiaje kutoa suluhisho la changamoto za maisha ya jamii kiasi cha jamii

kutamani kuwa sehemu endelevu ya ukuaji na ustawi wa Tamthilia ya Kiswahili nchini Tanzania? Maswali haya yaliongozwa na nadharia ya fasihi linganishi na mkabala wa kiufafanuzi kuchakata data za msingi.

### **6.2.1 Athari ya Ubunifu wa Dhamira katika Tamthilia ya Kiswahili**

Utafiti ulikusanya data za msingi kwa njia ya kusoma kwa makini kila tamthilia teule. Baada ya uchambuzi wa data tumebaini kuwa, tamthilia zote sita (6) teule zimebeba ubunifu endelevu wa dhamira faafu kwa ustawi endelevu wa jamii na Tamthilia ya Kiswahili. Kila tamthilia ina usemezano na upekee wa ubunifu wa dhamira. Pia, ukiondoa tamthilia ya *Changamoto* (2010) ya Elizabeth Mahenge, tamthilia tano (5) teule zilizobakia hazionekani kutoa suluhisho la moja kwa moja la nini kifanyike juu ya changamoto zinazowakabili wananchi. Badala yake, wamewaachia wasomaji wafanye uamuzi sahihi kulingana na mazingira yao kwa wakati wao.

Haya yanadhihirika kupitia muhtasari wa matokeo ya kina ya utafiti huu juu ya ubunifu wa dhamira uliopo katika Jedwali 6.1 (Kiambatisho B). Muhtasari wa dhamira umewekwa kama kiambatisho kutokana na ukubwa wa data unaofikia kurasa mbili na zaidi kwa vipimo vya ukubwa wa maneno kuwa 11 katika muundo wa Times New Roman unaokubalika na chuo kwa jedwali lenye data zinazozidi ukurasa mmoja (1) (rej. OUT, 2022; uk. 4).

Kutoka katika Jedwali 6.1, data zinaonesha ya kwamba, mwandishi wa tamthiya ya *Mashetani* ameonesha kuwapo kwa matabaka yasiyo na usawa miongoni mwa wanajamii kiasi cha kuzalisha ubaguzi wa rangi, mali na mamlaka. Matabaka yanayozungumzwa katika tamthiya hii yanatokana na utofauti wa kiuchumi na

kihistoria ambao umesababisha mafarakano baina ya wale waliojiita “wazalendo – wanamapinduzi” na “wazalendo – wapinduliwa.” Ubaguzi wa kitabaka unawasilishwa na Ebrahim N. Hussein kupitia mhusika Shetani na Binadamu pia vijana waliokuwa marafiki ambao ni Juma na Kitaru. Mhusika mwingine anayelisadifu hili ni Baba Kitaru. Mahusiano haya yanabeba urafiki feki wenye kujaa chuki, visasi, wivu, masimango, hasira, matambo, majivuno pia unyonge kutokana na kutokuwapo kwa muafaka wa kitaifa na kijamii kati ya wananchi, watawala wa jana na watawala wa leo. Hali hii inathibitishwa na majibizano baina ya Juma mbele ya Kitaru. Data ifuatayo inalisawili jambo hili:-

JUMA: Hatuwezi kusahau. Kila siku tunafunguliwa vifua na kujazwa sumu ya mambo ya jana.

*(Kitaru anaitikia. Kimya.)*

JUMA: Kwa heri.

KITARU: Hatuonani tena?

JUMA: Hatuonani tena.

KITARU: Kwa nini?

JUMA: Sababu nyingi.

KITARU: Mojawapo?

JUMA: Mpanda ngazi na mshuka ngazi hawewezi kushikana mikono.

KITARU: Pili?

JUMA: Wewe unaishi leo mimi naishi jana. Tutakuwaje marafiki? Na kila leo yako ni kidato cha kesho yako. Mimi, kila leo yangu ni kidato cha jana zangu. Na kila nikienda huko, nikirudi ninarudi na hadithi... hadithi za mashetani. (uk 56)

**(Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Mashetani*, 1971)

Kupitia nukuu hii, utafiti umebaini kuwapo kwa tofauti ya kimamlaka, kiuchumi, kimaisha na kihistoria kati ya tabaka tawala na tabaka tawaliwa. Badala ya kujenga umoja wa kitaifa baada ya mapinduzi, “wanamapinduzi” wanazidisha visasi na ubaguzi kwa wale wote ambao walikuwa wanatawala au kuunga mkono utawala uliokuwapo awali. Mjadala huu ni hai tangu awamu ya Azimio la Arusha kwani kinachojadiliwa kinaishi hadi hii leo (rej. Okello, 1967; Amory, 1994; Chachage, 2000; Lukumbo, 2008; Hettiger, h. m.; Mbogo, 2015). Nukuu hii inalieleza jambo hili kwa lugha yenye ubunifu iliyojaa tafakuri na kejeli kwa wanamapinduzi. Mwandishi anaendeleza mjadala wa madai ya haki sawa kwa wote katika nyanja zote za maisha kwa kutumia lugha ya kisanaa iliyojaa staha lakini yenye majeraha ndani yake. Hata hivyo, mwandishi anaonesha kukata tamaa kwa mnyonge badala ya kumpa ari ya kupigania haki yake mpaka tone la mwisho. Bila shaka, hali hii inaakisi hulka ya mnyonge kukata tamaa pindi juhudi zake zinapoonekana kutokuzaa matunda aliyoyatarajia. Hali hii ni kinyume cha wahenga waliotuasa kwa kusema, “atafutaye hachoki; akichoka, kishapata.”

Naye mwandishi Ngalimecha Ngahyoma kupitia tamthilia yake ya *Kijiji Chetu* (1975) anaonekana kuonesha kiubunifu namna baadhi ya viongozi wanavyotumia umaamuma wa wananchi wengi kutokujua kwa usahihi sera, sheria na taratibu kuwaibia, kuwanyanyasa na hatimaye kuvuruga umoja na ustawi wa jamii na taifa. Mwandishi anaonesha namna watu wengi walivyogeuka makasuku wa kila kinachosemwa na viongozi. Hata pale, wanapojitokeza wenye kuujua ukweli, viongozi na makasuku hukimbilia kuwaziba midomo, kuibua taharuki, kuwadharau na kutokuwasikiliza kama inavyojidhihirisha kwenye daolojia ifuatayo: -

- MZEE I:** Ujamaa mpya mwingi ni wa kwenye kitabu. Na hatari yake ni kama hii. (*Akionyesha mdomo*). Maneno mengi na mikutano kila siku bila vitendo. Kufika hapa na kujirundika pamoja twadhani tunaishi kijamaa. Ingawa babu zetu hawakujirundika kama sisi walikuwa wakiishi kijamaa kuliko sisi. Ujamaa ulikuwa ni maisha yao. Kulikuwa hakuna shamba la ushirika kama yetu hapa. Kila mtu alikuwa na lake lakini lilikuwa likilimwa na kijiji, siyo mtu mmoja. Ushirikiano uliendelea mpaka kwenye ulinzi. Mtu mmoja akipiga mbinja ya kutaka msaada wote hutoka kusaidia...
- MTU 3:** Tunajadili kuwafukuza wavivu mzee na siyo ujamaa...
- MTU I:** Mara ya mwisho sasa, unajifanya mwamba sana!
- MZEE I:** Ni mambo kama haya yanayoleta tofauti ya ujamaa wa kitabu na wetu wa asili. Turudi basi kwenye suala letu. Ni wazi kuwa watu wote hawawezi kuwa sawa...
- MTU 3:** (*Anakurupuka*). Unapinga usawa!
- MZEE:** Usinielewe vibaya mwanangu. Usirukie kitu kabla hujasikia mwisho wake. Ndiyo maana nawaambieni mna kitabu tu mbele yenu, lakini mawazo yenu si ya kijamaa. Watu wote siyo sawa ingawa binadamu wote ni sawa...
- MTU 3:** Ala! Ndiyo unasema nini. Kama umechoka mzee si kuacha.
- MZEE I:** Viongozi wetu wanatufanya tuishi maisha ya kijamaa na wanaona upande mmoja zaidi nao ni wa siasa... (uk. 16 – 18, 46)
- PINDUO:** Ndugu siyo kweli kuwa nimekata tamaa. Moyo wangu ni ule ule....
- SAUTI:** Mwongo... (*na wengine wanamguna*).

**PINDUO:** Kabisa ndugu. Na bado nina imani ileile kamili kwa ujamaa. Lakini, je, unaoendeshwa hapa na Mwenyekiti, wewe hapo Makamu na wachache wetu, wa kuendelea kumiliki biashara ni ujamaa? Kama wote tunataka kuendelea vipi basi tuwaache watu wachache wanufaike na watupe hata sisi tamaa ya kutaka mali!

**MTU 2:** (*Huku akicheka*). Hakika unadhihirisha jinsi ulivyokosa akili. Hilo ni jambo la kusema hapa kweli! Hasa wewe wamekusifia kuwa ulikuwa mwanamapinduzi! Kumbe wako ni wivu na kuona wengine wanafaidi nawe tamaa imekushika. Ndugu wananchi mwamueni mwanamapinduzi huyu.

**SAUTI:** Aondoke. – wote hao ni sawa, wanatupotezea wakati.... (*Wanakijiji wengine wanacheka wengine wanamkabili kwa ghadhabu wakiongozwa na Mtu 3.*) Mwisho sasa. – Mwondoeni. – mwondoeni. – Na Pinduo. – Wote, na Mwenyekiti na Makamu wake. (*katika vurumai hiyo vikundi mbalimbali vya wanakijiji vinawakusanya wanaohusika na kijana mmoja anaanzisha aina ya wimbo jukwaani*). Kizito aondoke, Pinduo. – aondoke. – Mwenyekiti. – aondoke. - wavivu. – Waondoke. – (uk. 54 - 55)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Kijiji Chetu*, 1975)

Kupitia data za nukuu hii, utafiti umebaini namna wazalendo wa kweli pamoja na kuwaonesha wananchi wenzao chanzo cha uozo, na nia ya kuendelea kuujenga ujamaa, bado wananchi wasio na uelewa wanafanya maamuzi ya kuwaadhibu kwa kuwatimua pamoja na wanyonyaji. Tunachojifunza hapa ni kwamba, unafiki na tofauti ya uelewa wa mambo ni miongoni mwa mambo yanayochangia kukosekana kwa shabaha katika kupambana na adui yeyote katika maisha. Tena, si kila mtu ana

sifa ya kushiriki au kufanya maamuzi sahihi yenye tija kwa jamii kwa kisingizio cha demokrasia. Kitendo cha kila mtu kuonekana kuwa sehemu ya maamuzi ilipingwa na Socrates (rej. Schlosser, 2009). Kwa mantiki kwamba, katika kundi wapo maamuma wengi na wengine wananunulika kirahisi, hivyo wanaweza kufanya maamuzi ya hovyoy kwa sababu hawaongozwi na mantiki wala sayansi kupima yale wanayotakiwa kuyafanyia uamuzi. Badala yake, wengi huongozwa na utashi, hisia, tamaa, rushwa na nguvu ya ushawishi katika kuamua hatima yao na vizazi vyao.

Kwa nukuu teule tulizozinukuu hivi punde kutoka tamthilia ya *Kijiji Chetu* na mjadala huu ni dhahiri ya kwamba mwandishi alitumia ubunifu unaorejelea historia ya Tanzania katika kuteua na kujenga mjadala kuhusu matokeo hasi ya utekelezwaji wa Azimio la Arusha. Na kwamba maendeleo ya Tamthilia ya Kiswahili hayakujitenga kiubunifu na maendeleo ya kijamii, kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni ya Mtanzania katika awamu husika, kihistoria. Changamoto pekee tunayoibaini katika tamthilia hii ni mwandishi kutokutoa suluhisho la wazi kabisa la kimkakati lenye kubeba dira ya mapinduzi endelevu ya kumkomboa mnyonge. Namna alivyomaliza mchezo ni dhahiri kwamba anawaambia kiucheshiucheshi wasomaji wake kuwa, kwa aina ya jamii iliyopo hata wafanyeje hawawezi kufikia ukombozi wa kweli mpaka wajikomboe kifikra kwanza. Funzo hili linapatikana kwa msomaji makini pekee. Lakini kwa msomaji asiye makini hawezi kuupata ujumbe huu.

Hali hii ndiyo tuliyoiona hata katika tamthilia ya *Mashetani* ambapo mwandishi anatuonesha kuwa mnyonge si lolote wala chochote machoni pa tabaka tawala. Uandishi wa namna hii ni kinyume na mtazamo wa wanaharakati wa haki za binadamu wenye kujitua muhanga kumpigania mnyonge. Kwa wao, mnyonge hana



cha kupoteza ila minyororo inayompa unyonge wenyewe (Rodney, 1972). Tena ni heri kufa umesimama kuliko kufa ukiwa umelala au kukaa. Kwa sababu, hakuna siku itakayokuja, kwa utashi binafsi, tajiri na mtawala dhalimu kuishi maisha ya hadhi sawa na mnyonywaji (Settles, 1996; Sharma, 2015). Hii ndiyo imani ya Wanaumaksi ambao hutamani daima ajenda ya kumkomboa mnyonge na namna ya kumkomboa vidhihirishwe kwa uwazi katika majukwaa yote ya kumtetea mnyonge – fasihi ikiwemo (Mushengyezi, 2003).

Kwa upande wa tamthilia ya tamthilia ya *Harakati za Ukombozi* (1982), waandishi wameonesha kwamba mapinduzi ya kweli siyo lelemama kwani hukumbana na vikwazo vingi kutoka kwa watu wa ndani na nje. Waandishi wanaonesha ya kwamba, vijana ni jamii inayoweza kusukuma mbele ajenda yoyote lakini hawawezi kuleta mapinduzi ya kweli kwa sababu wamejaa mihemuko pasipo akili na maarifa. Na kwamba, vijana wanatumika kama dodoki mradi tu uweze kuwakamata ufahamu kwa kugusa yale wanayotamani kuyasikia. Hawana muda wa kutathmini kwa kina ili wabaini kiini cha changamoto zinazoikabili jamii. Hili linatambulishwa kupitia malumbano kati ya Mzee na vijana, kama inavyoonekana katika nukuu ifuatayo: -

**KIJANA 4:** Ndiyo tumeifutilia mbali, tumeitupilia mbali. Sasa tutaleta mapinduzi.

**MZEE:** Nafasi mnaweza pewa, lakini je mtaweza?

**KIJANA 2:** Kuweza tutaweza kwa vile tumeazimia.

**MZEE:** Hata sisi babu zenu tuliiazimia lakini tulishindwa.

**KIJANA 3:** Mlishindwa kwa sababu mlikuwa na kasumba ya ukoloni.

**MZEE:** Je ninyi mmeshaifuta hiyo kasumba?

**KIJANA 4:** Ndiyo tumeifutilia mbali, tumeitupilia mbali. Sasa tutaleta mapinduzi.

- MZEE:** Haya vijana ukumbi ni wenu, kazi kwenu, jaribuni!
- KIJANA 1:** Siyo tujaribu, bali tutaleta mapinduzi kwa kutekeleza kwa vitendo maazimio na maamuzi yote ya Chama.
- WOTE:** Tumechachamaa
- KIJANA 8:** Tatalima sana
- WOTE:** Tumechachamaa
- KIJANA 8:** Tutafanya kazi
- WOTE:** Tumechachamaa
- KIJANA 8:** Hatutaki rushwa
- WOTE:** Tumechachamaa
- KIJANA 8:** Tutajenga nchi
- WOTE:** Tumechachamaa
- KIJANA 8:** Tutasonga mbele
- WOTE:** Tumechachamaa
- KIJANA 8:** Tutasoma sana
- WOTE:** Tumechachamaa
- Tumechachamaa. (uk. 24 - 25)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Harakati za Ukombozi*, 1982)

Ujumbe tunaopewa na vijana ni kwamba mwanamapinduzi hapaswi kusikiliza maneno wala kutazama matendo ya “wahujumu” mapinduzi wanaoweza kusababisha kukata tamaa. Hata hivyo, kupitia Mzee, waandishi wanaonekana kutoa tahadhari kwa yeyote anayekusudia kusonga mbele pasipo kukata tamaa. Kwamba, mapambano ya kutokukata tamaa ni sharti yaendane na kuheshimu tathmini inayotolewa na waliokutangulia katika mapambano ili kuepuka kurudia matokeo yale yale yaliyowafanya watangulizi kushindwa kufikia malengo yao.

Picha hii inajitokeza vema katika awamu ya Azimio la Arusha (rej. *Kijiji Chetu*) hadi hivi sasa. Kwani, vijana wameendelea kutumika kwa juhudi kubwa kulinda masilahi

ya makundi tawala pasipo kuchoka ili azimio liweze kutekelezeka. Vijana hawako tayari kurudi nyuma japo wengi wao huonekana kutokuwa na maarifa na mbinu sahihi za kumshinda adui aliyewashinda viongozi na jamii ya awali. Hili ndilo somo wanalotupatia waandishi. Kwamba, mtoto akililia wembe, mpeni; ukimkata shauri yake. Hivi ndivyo walivyohitimisha mjadala wa mapambano dhidi ya watawala dhalimu. Tafsiri yake ni kwamba, “wanamapinduzi” hawa tayari wameshashindwa vita hata kabla ya kuanza kupambana. Hii yote ni kwa sababu iliyo wazi kuwa, bado hawajamjua adui yao halisi wala mbinu anazozitumia kuwasambaratisha (Kezilahabi, 1998; Jain, 2016).

Naye mwandishi Shani Omari katika tamthilia yake ya *Safari ya Chinga* (2009) anatufundisha kwamba, changamoto zinazowakabili wanyonge hususani vijana wajasiriamali haziwezi kutatuliwa kwa kutumia sheria ikatayo upande wa wanyonge, vyombo vya ulinzi, mahakama na magereza. Badala yake, viongozi na watendaji hawana budi kuja na sera na mipango rafiki inayochochea maendeleo rafiki kwa jamii yote ili kila mmoja katika mazingira yake asitamani kukimbilia eneo dogo linalofanywa kuwa kitovu cha maendeleo. Nukuu ifuatayo inaliangazia jambo hili: -

**Hakimu:** Kama riziki ni popote kwa nini usiuzie nyumbani kwako.

**Mata:** Njini nilikuwa nafata wateja.

**Hakimu:** Huoni kwamba ulikuwa unavunja sheria za jiji kifungu namba 005 cha mwaka 2008.

**Mata:** Sikubahatika kuzisoma. Kama sheria ningepewa nikazisoma, wala nisingezivunja mweshimiwa hakimu.

**Hakimu:** Kwa kuvunja sheria za usafi miji, unatakiwa kulipa faini ya shilingi laki moja. Au kifungo cha miezi mitatu jela na kazi ngumu.

[...]

**Hakimu:** Kesi kama hii si ya kusikilizwa mara mbili. Umeshindwa leo kutoa faini unaenda ndani miezi mitatu. Ili iwe fundisho kwa vijana wengine wanaokimbilia mijini bila shughuli maalumu za kufanya.

**Mata:** (*Akilia na kupenga kamasi*). Mweshimiwa hakimu, naomba huruma yako. Kukaa kijijini kulima pia tumechoka. Nilikuja njini kutafuta kazi. Wazazi wangu kijijini wananitegemea. Sasa kibanda changu cha biashara kimevunjwa. Mali zangu zote zimepotea. Mweshimiwa hakimu, nyie wa juu tusaidieni. Sisi vijana wenu tunataabika. Hatuna kazi. (uk. 47-48)

**Mata:** Eh! Ndio nakumbuka. Ulitaka kuniambia nini vile?

**Ntumusha:** Nilitaka kukwambia katika biashara kuna mambo mengi. Unaweza kuibiwa, vichochoroni vibaka wanaweza kukupora. Sasa ingetokea ukaporwa mali ungesema urudi kijijini? Hapana, tugangamale tu. Tutafanikiwa. Hata tukirudi *home* matatizo ni yale yale. Mbona vijana wengi tu kama sisi wamefanikiwa? Kinachotakiwa ni uvumilivu. Mchumia juani hulia kivulini. (uk. 54)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Safari ya Chinga*, 2009)

Kupitia data za nukuu hizi mbili, utafiti umebaini namna sheria, mahakama na magereva yasivyoweza kutatua changamoto zinazowagusa wanyonge. Kwa sababu, baada ya mtu kumaliza kifungo hurudi mtaani kuyaanza maisha akiwa amepoteza

hata kile alichokuwa nacho awali. Kwa wamachinga, mwandishi ameonesha kwamba, wanaokamatwa ni wachache kuliko waliobaki uraiani wakiendelea kukimbizana na serikali. Ni kana kwamba mwandishi anatuuliza haya maisha ya paka na panya kati ya serikali na vijana wajasiriamali yataendelea hivi mpaka lini? Na, hali hii ni kwa faida ya nani? Wakati mwandishi akiungana na wadau wengi (mathalani, International Labour Organisation, 2022; Makinda katika Ismail, 2022; Satpayeva, na wenzake, 2022) kupigania mazingira rafiki ya vijana kujiajiri, bado serikali kama mdau mkuu wa maendeleo ameendelea kuwa chanzo kikuu cha kuua ajira binafsi za vijana wengi (Ministry of Finance and Planning, 2021; Mwananchi, 2021).

Si tamthilia hizi pekee ndizo zimejadili changamoto na kukwepa kutoa suluhisho la moja kwa moja lenye mashiko, hata mwandishi Elizabeth Mahenge kupitia tamthilia yake ya *Changamoto* (2010) anaonekana kufanya vivyo hivyo. Kila mmoja anaonesha matatizo lakini linapokuja suala la nini kifanyike, wanakuwa tuli ili msomaji atafute majibu mwenyewe kupitia mjadala aliuousoma kitabuni. Mathalani, Mahenge anaonesha namna viongozi wa serikali, jamii na watendaji wasivyokuwa tayari kuvikabili vigingi vinavyowakwamisha watu wenye ulemavu kupata haki sawa – sawasawa na watu wengine katika jamii. Mahenge anawapitisha wahusika wake (watu wenye ulemavu) katika maeneo mbalimbali ili kusaka haki, pasipo mafanikio. Mwishoni, mwandishi anawapeleka wahusika wake polisi kisha mahakamani kama eneo linalotazamiwa kubeba suluhisho la upatikanaji wa haki. Data ifuatayo inathibitisha hili tulilolibaini katika utafiti wetu: -

**Peti:** Mwongo huyu! Tena tummwagie petrol kabisa, tumwue!

- Godwin:** Hapana! Sheria itamhukumu akikutwa na hatia. Sio vizuri kulipiza kisasi – tunaamini mahakimu wetu huko mahakamani wanahukumu kwa haki!
- Rajab:** (*Akimsihi Godwin*) Niache tafadhali nitakupa kitu kidogo!
- Godwin:** Maisha yangu hadi leo hii sijawahi kuhongwa kitu chochote. Huwezi kunishawishi. Twende! (*Akimburuta Rajab na kuiacha baiskeli yake pale pale*). Twende mbele ya sheria. Lazima unyanyaswaji na uonevu dhidi ya watu wenye ulemavu ukomeshwe.
- Rajabu:** (*Akimwamrisha*) Niachie mzee! Nasema niachieeee! (*Rajabu anafurukuta kujitoa mikononi mwa Godwin na anampiga teke la tumboni. Godwin anagugumia kwa maumivu na anaanguka chini. Rajabu anakimbia kuelekea walikokaa hadhira. Wakati huo huo Kimweri anapurukushana na Chaazye na anajitoa mikononi mwake na anakimbia. Walemavu waliokuwapo jukwaani wanapiga kelele za kuomba msaada. Wanasikika wakisema: **KAMATA! KAMATA! KAMATA!** Lakini hakuna mtu anayejitokeza kumkamata mhalifu yeyote anayekimbia. Pazia linafungwa*). (uk. 27 - 28)
- [...]
- Megno:** Nafikiri tunahitaji kuripoti Polisi vitendo viovu tulivyofanyiwa ili wahalifu wakabiliwe na mkondo wa sheria. Unaonaje?
- Peti:** Usemayo ni kweli Megno. Lakini kumbuka kuna mambo ya rushwa... baada ya siku mbili unamwona mhalifu anazurura mtaani.

**Megno:** Usemayo ni kweli. Lakini hatutasimama wenyewe kama walemavu... tutatafuta mawakili wa utetezi ambao watalisimamia shauri letu hadi haki itendeke.

**Peti:** (*Akicheka kwa kejeli*) Hivi wewe kaka yangu Megno bado tu una ndoto za Abunuwasi?

**Megno:** Una maana gani?

**Peti:** Hivi hao mawakili wa utetezi unaowataja utawapa nini? Au utauza baiskeli yako ili uwalipe... halafu uanze kutambaa kwa kukosa kitimwendo?

**Megno:** Peti mbona unafika mbali hivyo?

**Peti:** Sio kwamba nafika mbali, huo ni ukweli halisi. Hivi wewe mlemavu (*Akimpapasapapasa kichwani*) una hela gani ya kuweka mawakili wa utetezi?

**Megno:** Wapo wanaotoa msaada wa kisheria bure. Na sisi tutakwenda huko huko kwa hao wanaotoa huduma hiyo. Hawa wameamua kuitumikia jamii. Na jamii yenyewe ndio sisi.

**Peti:** Ahaa! Labda hivyo. Maana najua walemavu wengi ni masikini kwa sababu mbalimbali....  
(uk. 32 - 33)

[...]

**Abuu:** (*Akibubujikwa na machozi*) Usinifunge Mheshimiwa.

**Hakimu:** Haifai kabisa kwa uhalifu namna hii kukutoza faini badala ya kukupeleka jela. Kwa vile nimekugundua na hatia ya kuua kwa kukusudia basi umehukumiwa kunyongwa mpaka kufa ili liwe fundisho na kwa wengine. (uk. 37)

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Changamoto*, 2010)

Data kupitia nukuu hii zinaonesha kwamba jamii haina umoja wala ushirikiano katika kumkomboa mtu mwenye ulemavu. Kila mmoja anajiona kutokuwa sehemu muhimu katika kumtetea na kumpigania mnyonge huyu. Wazazi wengi waliozaa watoto wenye ulemavu nao wameingia kwenye mkumbo huu wa kuwatelekeza na kuwaacha watoto hawa wakinyanyasika na kudhulumiwa kwa kila hali na nia. Kwa hakika mtiririko huu wa visa na mikasa inayowakumba watu wenye ulemavu, unathibitisha ya kuwa mwandishi hakukurupuka katika kufuma na kusana dhamira zake. Hata hivyo, mtazamo wa mwandishi kuona polisi na mahakama kama vyanzo vikuu vya kumkomboa mnyonge, unatofautiana kwa kiasi na jamii inayomzunguka. Kwani watu wengi hawana imani na polisi pia mahakama katika kutoa haki bila upendeleo (Masabo, 2014). Mpaka leo hii, si mahakama wala mawakili ama polisi walioiadhibu serikali kama mdau mkuu wa kujenga thamani ya mtu mwenye ulemavu. Miundombinu mingi si rafiki kwa watu wenye ulemavu.

Ripoti ya Shirikisho la Vyama vya Watu wenye Ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA, h.m.) inaonesha kuwa, sheria (ikiwemo sheria ya watu wenye ulemavu namba 9 ya 2010) na sera anuai bado hazionekani kuwa mwarobaini wa shuruti kwa wadau kuboresha mazingira ya kuwahudumia watu wenye ulemavu katika nyanja mbalimbali za maisha. Kwamba, mambo mengi yanatendeka kwa sura ya hisani badala ya haki ya msingi ya watu wenye ulemavu. Utashi wa kisiasa ungali duni kumsaidia mtu mwenye ulemavu. Hivyo basi, kimantiki; hata pendekezo la kukimbilia polisi na mahakamani – kwa mazingira ya Tanzania hii ni pendekezo



lisilo na msaada sana. Kwa sababu uhitaji wa haki miongoni mwa watu wenye ulemavu ni zaidi ya hukumu ya kumnyonga mtu hadi kufa. Kwani hukumu ya namna hii hutolewa kwa yeyote aliyewa mtu kwa kukusudia, hata kama aliyeuawa siyo mtu mwenye ulemavu. Suluhisho la dhati ni watu kujikomboa kifikra kwa faida jumuishi za jamii nzima.

Katika tamthilia ya *Nje – Ndani* (2016), waandishi wameonesha chanzo cha maisha duni ni sababu za nje na ndani ya nchi. Miongoni mwa sababu hizo ni udhalimu wa watawala na watendaji, ukoloni mamboleo na unafiki wa viongozi na wananchi kutoona umuhimu wa wao kuwa sehemu ya tatizo katika kutatua changamoto zinazowakabili. Badala yake, kila mmoja amebaki kutoa shutuma kwa mataifa makubwa kuwa kichocheo cha mapito machungu ya Waafrika. Hali hii inasababisha madhara yenye kuambatana na unyonge na uonevu mkubwa miongoni mwa nchi duni - kijeshi, kitaaluma, kiteknolojia; ijapokuwa zimejaa raslimali nyingi zinatohitajiwa na mabeberu, kama wanavyobainisha Akili, Utashi-Nafsi na Moyo: -

**Akili:** Maana yangu ni hii, ni nani katika sisi anayehoji thamani yake, usawa, haki na anakumbuka wajibu wake? [...] Eeeh? Doto anapigwa kule, Kulwa hapa kimyaa. Ukiona hivyo ujue mambo msegemnege.

**Moyo:** Kuhusu Afrika?

**Akili:** Si Afrika tu, bali dunia nzima. [...] Tunajitia ububu kwa uziwi wao wa makusudi. Sijui ni kwa nini hata wenye macho hawaoni wakati wanatazama kabisa? (uk. 28)

**Utashi-Nafsi:** Akina mama, wafanyabiashara wadogowadogo, vijana, misukule na manamba wa miamala.

**Akili:** Ahaaaa! Nimemuelewa sasa.

**Moyo:** Hata mimi, yaani mtumwa kwa mtumwa mwingine. Yaani dunia hii, kila mtumwa ana mtumwa wake. Ama kweli, dunia mti mkavu.

**Akili:** Utumwa unakujaje sasa? Mbona ulishaisha?

**Moyo:** Chukua moja rudisha mbili, yaani mara mbili!!

**Macho:** Tena ulete mbili kabla hiyo moja haujaipata vizuri.

**Moyo:** Duuuuh! Ni ukatili, unyama na ufedhuli mkuu. (uk. 69 – 70)

**Utashi-Nafsi:** [...] Mama yangu Afrika,

Lengo nisije badili,

Vina vinavyotumika,

Vyanipatia shughuli,

Machozi yananitoka,

Na maumivu makali,

We! Mamangu Afrika,

Nakupenda kwelikweli.

*[Utashi Analia, machozi yanatiririka mashavuni, anaanguka analala kimya. Akili na Moyo wanamkimbilia kumsaidia. Anastuka anasimama kama hawaamini vile na anaonyesha hataki msaada wa yeyote. Anawaacha anaondoka taratibu kama mzee wa miaka mia moja mpaka anatokomea]. (uk. 93 – 95)*

(**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Nje-Ndani*, 2016)

Nukuu hii inadhihirisha kuwapo kwa usaliti, ukibaraka, ubinafsi, dhuluma, unyonyaji, matabaka, kutokujiamini. Changamoto nyingine ni udhaifu katika miundo ya kiutawala, kiulinzi, kiusalama, kiuchumi, kijamii, kisiasa na kadhalika. Hali hii imesababisha viongozi wengi wa mataifa yasiyo na nguvu kuwa vibaraka na wenye kujipendekeza kwa viongozi wa mataifa makubwa. Matokeo yake, mataifa dhaifu na wananchi wanyonge wamejikuta wakitumikia maslahi ya wakoloni badala ya jamii zao. Pamoja na waandishi hawa kuonesha changamoto zote hizi, bado wameishia

kumwonesha mnyonge kuwa hawezi kujinasua zaidi ya kulia, kugaragara chini na hatimaye kuzeeka na kungoja kifo.

Suluhisho la namna hii haliungwi mkono na wanaumajumui wa Kiafrika wakiwemo Rodney (1972), Nyerere (1973, 1994), Shivji (1976, 1985, 2013), Independent Commission of the South on Development Issues (1992), Mwiru (2013), Sitta (2013), Chachage (2000, 2014) na Masabo (2014), kutaja kwa uchache. Kwa wao, viongozi wazalendo ni lazima watoe majawabu ya changamoto zinazowatesa wananchi. Viongozi ni nguzo muhimu sana katika kumsaidia mnyonge kujitambua na kutafuta ukombozi wa kweli. Pamoja na mwono huu wa wanamajumui, wanafasihi wengi hasa wa Kiafrika mathalani Ebrahim N. Hussein, Edwin Semzaba, Emmanuel Mbogo, Euphrase Kezilahabi, Kyaro W. Wamitila, Ngugi wa Thiong'o, Okot p'Bitek, Penina Mhando, Said A. Mohamed, Shafi A. Shafi, Wole Soyinka, miongoni mwa wengi; kazi zao nyingi zinaonekana kukwepa kutoa suluhisho la moja kwa moja la kumkomboa mnyonge.

Tunaporejelea nadharia ya Fasihi Linganishi, tunapata cha kusema juu ya kutokuwapo suluhisho la moja kwa moja. Kwamba, ukwepaji huu bila shaka unatokana na kile walichokijadili Sanchez (1973), Nazareth (1978), Kezilahabi (1993), Maake (2006), Ruhumbika (2006) na Adeseke (2016) juu ya uhuru wa mwandishi. Wataalamu hawa wanasema, mazingira ya nchi nyingi zinazoendelea si rafiki kwa waandishi kutokana na kuwapo kwa changamoto nyingi zinazotokana na vichocheo vya ndani na nje ya mataifa husika. Kwa hiyo, mwandishi hawezi kuwa huru kutoa suluhisho zito au moja faafu kutokana na kiwango na vyanzo vya changamoto hizo kutofautiani.

Kwa mfano, watawala wengi hasa wa Kiafrika hawapendi kukosolewa hivyo kumwona mwandishi mwenye mapendekezo yasiyowapendeza kama tishio la usalama na ulinzi wa tabaka tawala. Kwa muktadha huu, mwandishi akithubutu kutoa mapendekezo yasiyowapendeza tabaka tawala, atakuwa amehatarisha uhai na usalama wake na wa watu wake wa karibu au kazi yake kupigwa marufuku isionekane sokoni. Hali hii imewahi kuwakuta waandishi kadhaa. Kwa mfano Abdilatif Abdalla alitupwa gerezani sawasawa na Katama Mkangi na Alamin Mazrui. Mwandishi mwingine aliyetupwa gerezani ni Shafi A. Shafi aliyehusishwa na makosa ya uhaini baada ya mauaji ya Rais mzawa wa Zanzibar Abeid A. Karume.

Wengine walilazimika kukimbia nchi zao, kwa mfano Chinua Achebe. Mwingine ni Ismail Mbise aliyelazimika kukimbilia Namibia baada ya kuandamwa kwamba anachochea umwagaji damu katika eneo la Meru na Arumeru kupitia kupitia kitabu chake cha *Blood on Our Land*. Mbali ya mwandishi huyu kukimbia nchi, kitabu tajwa nacho kilipigwa marufuku kutumika wala kuonekana mahali popote ndani ya mipaka ya Tanzania. Mwandishi mwingine ni Ngugi wa Thiong'o aliyepelekwa kizuizini nyakati za utawala wa Jomo Kenyatta na Daniel A. Moi. Alipotoka kizuizini akakimbilia uhamishoni Marekani huku kazi yake *Matigari ma Njiruungi* ikipigwa marufuku.

Katika mazingira yenye changamoto za kuhatarisha uhai na vipaji vya waandishi, Mwenda Mbatiah anapolinganisha roho ya uzalendo ya waandishi bunilizi wa zamani na hawa wa sasa, anaishia kusema “sidhani ikiwa kuna mwandishi nchini [...] ambaye amewahi kujipata matatanikwa sababu ya maandishi yake jinsi Ngugi wa Thiong'o alivyojipata mashakani kwa kuandika kazi kama vile *Matiagari ma*

*Njiruungi*” (rej. Matundura na Mugambi, 2022, uk. 176). Mwenda Mbatiah anairejelea kazi hii kwa sababu ni kazi iliyosababisha vitisho vingi kwa mwandishi na kampuni za uchapishaji zilizotaka kuufadhili mswada huu. Kampuni ya East African Educational Publishers ilipojitia kiburi na kuchapisha nakala 700 za kazi hii mnamo mwaka 1987, ilijikuta ikipata hasara kubwa baada ya maafisa wa serikali ya Daniel A. Moi kuvamia ofisi na kuchukua nakala zote 700 na kwenda kuziteketeza huku mchapishaji akielekezwa kwenda ikulu kudai fedha yake. Jambo ambalo mchapishaji alishindwa kulifanya kwa kukosa ujasiri kwani tayari alikuwa amepokea vitisho vingi kutoka kwa watu asiowajua (Matundura na Mugambi, 2022).

Mbali ya changamoto hii, katika hali ya kushitua, Ngugi wa Thiong’o aliporejea nchini Kenya baada ya kukaa ughaibuni kwa miongo kadhaa, nyumba yake ilivamiwa na watu wasiojulikana. Watu hao hawakupora mali yoyote ndani ya nyumba ile. Bali walimbaka Njeeri (mke wa Ngugi wa Thiong’o) huku Ngugi wa Thiong’o akiambulia kipigo na kuchomwa kwa moto wa sigara (rej. BBC News, Jumatatu, 16 Agosti 2004 kwa anwani ya *Kenyan writer’s wife was raped*). Wapo waandishi walishuhudia kazi zao zikipigwa marufuku kusomwa, kuuzwa wala kusambazwa sokoni. Hao ni Euphrase Kezilahabi ambaye riwaya yake ya *Rosa Mistika* iliondolewa sokoni. Huku mchezo wa kuigiza uliotokana na shairi la *Dhifa* nao ukipigwa marufuku. Waandishi wengine ambao kazi zao zilipigwa marufuku (nchini Kenya) ni Zimkitha Mlanzeli kutoka Afrika Kusini (*Blood Ties*). Mwingine ni Smith Hempstone (*Rogue Ambassador: An African Memoir*).

Yupo pia, Salman Rushdie kupitia riwaya yake ya *The Satanic Verses*. Kazi hii ilimfanya mwandishi huyu atorokee kusikojulikana huku ikiwagharimu uhai wafasiri

wawili (2) - wa Kijapani na wa Kiitaliano pamoja na mchapishaji wa kitabu hiki. Na, kazi husika kupigwa marufuku nchini Iran na mwandishi husika kutangaziwa hukumu ya kuuu na yeyote - mahali popote atakapokutwa almaarufu kwa jina la fatwa. Matundura na Mugambi (2022) wamefafanua kwa kirefu masaibu yaliyowapata baadhi ya watunzi walioonekana kuligusa tabaka tawala.

Waandishi waliouawa ama kutupwa gerezani au kukimbia nchi zao au kazi zao kupigwa marufuku walihusishwa na harakati za kisiasa kupitia kazi au kauli zao kuhusishwa na kile kilichotajwa na watawala kama harakati za uhaini au uchochezi wenye nia ovu dhidi ya serikali na wadau wa maendeleo (Kezilahabi, 1993 & 1995; Matundura na Mugambi, 2022). Katika mapito ya namna hii, si ajabu waandishi wengi wamejikuta wakikimbiza mbawa zao kwa kujikita katika kuonesha changamoto kwa njia ya ubunifu tete kwa kuiachia jamii iamue yenyewe nini cha kufanya au kutumia lugha ya mficho kuwasilisha wazo.

Aidha, mifumo ya maisha na uongozi haifanani kati ya kiongozi na kiongozi, wakati na wakati, sera na sera, jamii na jamii, kutaja kwa uchache. Kwa hiyo, mwandishi akipendekeza suluhisho ambalo ni faafu kwa mazingira yake ya leo kiutunzi ni dhahiri kuwa suluhisho hilo litakuwa au halitakuwa faafu kwa mazingira ya jamii yake ya leo na, ama jamii nyingine au nyakati za siku za usoni. Historia inatueleza, wanamapinduzi (aghalabu wafanyakazi) wa Urusi hawakuwahi kuamini kwamba wakulima wa mashambani wanaweza kushiriki kikamilifu katika mapinduzi ya kuwang'oa watawala dhalimu. Wanamapinduzi hao waliwadharau wakulima hata kufikia hatua ya kuwafananisha wakulima hao na viazi ndani ya magunia yaliyofungwa (Smith, 2012).

Lakini historia ya mapinduzi matukufu ya China, chini ya Mao ze Dong (au ze Tung) inawatambua wakulima wa mashambani kama kitovu cha mafanikio ya mapinduzi hayo. Historia ya kuwatumia wakulima wa mashambani kutetea kesho ya mnyonge ndiyo iliyojitokeza hata nchini Cuba, Korea Kaskazini na Vietnam dhidi ya uvamizi wa Marekani na vibaraka wao (Smith, 2012). Kwa hiyo; wakati, msukumo, aina ya watu na mipango ya mapinduzi katika jamii moja imethibitika kuwa tofauti kati ya jamii na jamii. Vivyo hivyo, mwandishi hawezi kusema njia hii ni sahihi zaidi kuliko ile wakati anatambua wasomaji wa kazi yake si wa jamii yake pekee.

Mfano mwingine, Marekani haijawahi kukubali fomula ya ukuaji na ustawi wa uchumi wa Japani. Kwa sababu kihistoria baada ya vita ya pili ya dunia, uchumi wa Japani unatajwa kukua na kustawi kwa namna ya mruko sawa na ule wa helikopta (mruko wima). Wakati kwa falsafa ya Marekani, ukuaji na ustawi endelevu wa uchumi ni sharti uwe wa muundo wa mruko wa ndege ya abiria au mizigo inayopaa kutoka ardhini kwa kuinuka juu kwa hatua moja kwenda nyingine kuelekea mbele kiasi cha kuzalisha nyuzi 45. Historia hiyohiyo, inatufundisha kwamba, upatikanaji wa uhuru wa mataifa yaliyotawaliwa haukuwa kwa namna moja. Kuna mataifa mathalani Kenya, Zimbabwe, Afrika Kusini, Angola, Namibia na mengine yalilazimika kumwaga damu kama hatua ya kujikomboa kutoka katika mikono ya wakoloni. Ilhali, mataifa kama Ghana na Tanzania hayakumwaga damu ili kupata uhuru kutoka kwa wakoloni (Settles, 1996; Sharma, 2015).

Kwa jumla, utafiti umebaini kwamba, kila tamthilia imesawili maisha ya wakati wake na na nyakati za usoni. Kila tamthilia inajadili mambo ambayo yanaonekana kisayansi yalikuwapo na mengine yameibuka kwa namna tofauti kama nyoka

aliyejivua gamba. Mambo mengine yanaonekana kujadiliwa katika tamthilia za awamu ya soko huria kwa sababu ya matokeo ya utashi wa kisiasa kuvunja “miiko” ya jamii. Mambo hayo ni ubakaji, UKIMWI / VVU, rushwa, uufisadi na haki za watu wenye ulemavu, kutaja kwa uchache. Mambo haya yalikuwapo hata wakati wa awamu ya Azimio la Arusha lakini hayakujadiliwa kwa uzito kama yanavyojadiliwa sasa. Bila shaka hali hii inatokana na uhuru wenye baraka za tabaka tawala (Kezilahabi, 1993). Kwa vile dhamira zimekita kiubunifu katika nyakati, mazingira na nyanja tofauti tofauti za maisha ya mwanadamu, kunatupatia picha ya kwamba tamthilia hizi teule ni chachu ya ukuaji na ustawi endelevu wa Tamthilia ya Kiswahili na wasomaji wake hususani Watanzania – pindi zikitumika kwa dhati.

### **6.2.2 Athari ya Ubunifu wa Matumizi ya Lugha katika Tamthilia ya Kiswahili**

Matumizi bunifu ya lugha ni nyenzo muhimu sana katika kuchochea na kusukuma mbele gurudumu la maendeleo endelevu ya maisha ya jamii na sanaa (Mnyampala, 1990; Senyamanza, h. m.). Matokeo yanaonesha kuwa kila tamthilia ina matumizi ya lugha yenye kuchochea ubunifu endelevu wenye kuleta matumaini kwa ustawi endelevu wa Tamthilia ya Kiswahili. Matokeo ya matumizi ya lugha yamewekwa kwa muhtasari katika Jedwali 6.2. Katika jedwali tajwa, kuna matumizi ya tarakimu zilizofungiwa na ambazo hazijafungiwa mabano. Tarakimu zilizofungiwa mabano zinaonesha nafasi iliyoshikwa na tamthilia husika wakati tarakimu ambazo hazijafungiwa mabano zinabeba kiwango cha utokeaji wa matumizi ya lugha katika tamthilia husika.



**Jedwali 6.1** Mdafao wa Ubunifu wa Matumizi ya Lugha katika Tamthilia Teule

Tamthilia	Ucheshi	Misimu	Uchanganyaji ndimi <sup>15</sup>	Wepesi na ugumu wa lugha
<i>Mashetani</i>	52 (2)	07 (3)	50 (1)	Ngumu – (1)
<i>Kijiji Chetu</i>	15 (5)	05 (5)	00 (6)	Nyepesi – (1)
<i>Harakati za Ukombozi</i>	08 (6)	05 (5)	01 (5)	Nyepesi – (2)
<i>Safari ya Chinga</i>	63 (1)	18 (2)	15 (2)	Nyepesi – (4)
<i>Changamoto</i>	38 (4)	6 (4)	08 (3)	Nyepesi – (3)
<i>Nje – Ndani</i>	42 (3)	21 (1)	07 (4)	Ngumu – (2)

*Chanzo:* Data za Utafiti Kutoka Tamthilia za *Mashetani, Kijiji Chetu, Harakati za Ukombozi, Safari ya Chinga, Changamoto, Nje – Ndani, 2018*

Matokeo ya utafiti yanayobebwa na Jedwali 6.2 yanathibitisha upekee wa kila tamthilia kiubunifu. Hapa tunaona hakuna tamthilia yenye sifa sawa kwa viwango sawa na tamthilia nyingine katika ubunifu wa matumizi ya lugha. Uchunguzi tulioufanya katika kila tamthilia umebaini ya kwamba, tofauti hizi zimetokana na aina ya ubunifu katika kuteua wazo, wakati, walengwa (walaji), wahusika, mandhari, miktadha, mazingira na falsafa iliyokusudiwa na mwandishi. Kwa mfano, tamthilia ya *Mashetani* inajadili usaliti wa viongozi watawala kwa wananchi wao. Wahusika

<sup>15</sup> Hesabu ya uchanganyaji ndimi imepatikana kwa kujumlisha utokeaji wa maneno katika umbo kamilifu la usemi. Yaani kama mhusika alitamka neno moja, sehemu ya sentensi moja, ama sentensi moja au kifungu cha sentensi kimoja (aya) kwa lugha ya kigeni halafu akarudi katika Kiswahili, basi tuliheسابu neno husika ama sentensi husika au kifungu cha sentensi husika kama uchanganyaji ndimi wa kwanza, wa pili, wa tatu na kuendelea. Pia, maneno yote ya kigeni yaliyoandikwa kwa tahajia za Kiswahili lakini uandishi huo siyo utohoaji rasmi, nayo yaliheسابika kuwa sehemu ya uchanganyaji ndimi – endapo tu utokeaji wake ulisimama peke yake kama neno ama sentensi katikati ya kauli ya Kiswahili.

teule wengi wao ni wasomi na watumishi wa umma ambao Mnenuka (2010) na Mwiru (2013) wanawatambulisha kama wazungu weusi au wakoloni weusi.

Tamthilia hii ya *Mashetani* ilichapishwa mnamo mwaka 1971, ikiwa ni miaka minne (4) tangu kuanzishwa kwa Azimio la Arusha, miaka saba (7) tangu kutokea kwa mapinduzi ya kisiasa nchi Zanzibar na miaka sita (6) kabla ya kuzaliwa kwa CCM. Kwa aina hii ya historia, malengo ya kisiasa, watawala wanafiki, wakati wa utunzi, mazingira ya utunzi na lengo la mwandishi, lazima mwandishi makini atawaambia wahusika matumizi changamani ya lugha ikiwemo lugha ya kigeni inayosawili historia ya mkoloni aliyetawala jamii husika. Pia, kutokana na kuogopa mkono wa mtawala asiyependa kukosolewa, lazima mwandishi atalazimika kutumia lugha ya taswira zaidi. Kumbe basi, aina na kiwango cha matumizi ya lugha tuliyoyashuhudia siyo jambo la bahati mbaya bali ni zao la ubunifu wa mwandishi katika kuyasawili mazingira yaliyomlea na kumkuza kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni.

Tamthilia za *Kijiji Chetu* na *Harakati za Ukombozi* hazionekani kutumia sana matumizi ya lugha teule tuliyoyashughulikia kutokana na kile kile tulichokisema. Yaani, aina ya wazo, wakati, walengwa (walaji), wahusika, mandhari, miktadha, mazingira na falsafa. Hivi vyote vimebainika kuwaathiri waandishi husika kutokujaza matumizi ya lugha tuliyoyashuhudia katika tamthilia ya *Mashetani*.

Tamthilia ya *Kijiji Chetu* ilichapishwa mnamo mwaka 1975, ikiwa ni miaka minane (8) toka kuzaliwa kwa Azimio la Arusha, 1967 na miaka miwili kabla ya kuzaliwa kwa CCM. Nayo tamthilia ya *Harakati za Ukombozi* ilichapishwa mnamo mwaka 1982 hivyo kufanya kuwapo kwa tofauti ya miaka mitano (5) tangu kuzaliwa kwa CCM, na miaka kumi na mitano tangu kuzaliwa kwa Azimio la Arusha

lililotangazwa rasmi na Mwalimu Julius K. Nyerere mnamo tarehe 5. 2. 1967. Tena, utunzi wa tamthilia ya *Harakati za Ukombozi* ukitokana na ombi la vijana wa CCM mkoa wa Dar es salaam kwa ajili ya kusheherekea kile kilichotajwa kama mafanikio ya kuzaliwa kwa CCM.

Katika mazingira ya namna hii kwa haraka, tunabaini tamthilia hii ilizaliwa katikati ya kilele cha utekelezwaji wa Azimio la Arusha na mapinduzi ya Zanzibar huku viongozi wa kisiasa wakijinasibu kwa wananchi kwamba maamuzi ya kisera na kisheria ni suluhisho la maisha duni ya mnyonge. Aidha, baadhi ya wanahistoria wanatujaza kwamba, katika kipindi hiki hakukuwa na uhuru wa kidemokrasia kama ilivyo sasa kwa wakosoaji wa utekelezaji wa wanamapinduzi na wanaazimio. Kila aliyewakosoa watendaji na wanasiasa “wazalendo” alihesabika kuwa ni mhaini na kibaraka wa wakoloni na ukoloni mamboleo (Matundura na Mugambi, 2022). Mbali ya hayo wananchi wengi walijengwa katika msingi wa imani ya kuwaamini viongozi, kupokea na kuimba kama kasuku yale yote yaliyotamkwa na viongozi pasipo kujipa wasaa wa kutafakari (Hyden, 1980; Lukumbo, 2008; Chachage, 2014; Fouéré, 2014).

Ndiyo maana katika kazi zote mbili waandishi wamewatumia wazee (wasio na nafasi ya maamuzi katika jamii, chama na serikali) kufanya tafakuri ya mambo kwa kina. Lakini mawazo yao yanatupiliwa mbali kwa sababu wananchi wengi ni maamuma aliokamatwa ufahamu na viongozi wasaliti wenye sauti katika jamii, chama na serikali. Vilevile kwa Tanzania, hiki ni kipindi ambacho matumizi ya lugha ya Kiswahili yalisisitizwa sana na ikawa ni moja ya viashiria vya uzalendo wa kweli miongoni mwa wale wanaoendelea kung’oa mizizi na machipukizi ya ukoloni

mkongwe. Kwa hiyo matumizi ya lugha ya Kiswahili yalikuwa ni mwitiko wa wasomi na watu wote kukienzi Kiswahili na utamaduni wa Mtanzania (rej. Wizara ya Elimu na Utamaduni, h. m).

Katika hili, Mbiti (1969) pamoja na Lynch na Roberts (2010) wanaturejesha katika Falsafa ya Kiafrika. Kwamba mkubwa hata akikosea; basi anayesimangwa na kuzodolewa ni msaidizi au mshauri wake – hata kama chanzo cha kosa ni mkubwa mwenyewe kutokusikiliza ushauri. Kwa hiyo, badala ya wakosoaji kumlenga moja kwa moja mkubwa, wao humwambia mkubwa ‘wasaidizi / washauri wako wamekupotosha.’ Na kwamba, wasaidizi wametumia fursa ya mkubwa kuwaamini na kuwasikiliza, kumgombanisha na wananchi.

Vilevile, kwa busara ya Kiafrika, siku ya jambo la furaha siyo sahihi hata kidogo kutenda au kusema jambo hasi machoni na masikioni mwa waliopo shereheni. Kwa sababu nia ya kila mmoja ni kunywa, kula na kuburudika huku wakisindikizwa na usemi wa kupongezana tu - hata kama mambo hayako sawa. Kawaida, changamoto au mambo ya kuumiza hungojea siku yake maalumu. Kama italazimika kusema, basi msemaji huhitajika kutumia busara na weledi wa hali ya juu sana kunena ili asijeharibu lengo kuu cha shughuli (Mbiti, 1969).

Kwa mantiki hii, tunapozichunguza tamthilia hizi mbili, tunagundua kuwapo kwa athari ya Falsafa ya Kiafrika katika ukosoaji wa tabaka tawala. Kwa hoja hizi, tunabaini ya kuwa aina na kiwango cha matumizi ya lugha teule yaliyosanwa katika tamthilia hizi mbili yamezingatia ubunifu wenye kuakisi mazingira yaliyotawala utunzi wa kazi husika kama wanavyosisitiza wanataaluma wa uandishi bunilizi (rej.

Mohamed, 1990; Kezilahabi, 1993; Senkoro, 1995; Mlama, 2003; Ruhumbika, 2006).

Nayo tamthilia ya *Safari ya Chinga* inaonekana ina utajiri wa kutosha wa matumizi ya lugha kutokana na kile kilichobainika kupitia utafiti wetu. Kwamba, wakati wa uandishi wa tamthilia hii ni kipindi cha utandawazi wa soko huria ambapo mambo mengi yanawafikia watu kwa haraka na wepesi kuliko awamu ya Azimio la Arusha. Tayari kuna uhuru mkubwa wa watu kupashana habari hasa kwa njia ya simu za rununu na kusafiri kwa urahisi kupitia barabara zenye vyombo vingi vya usafiri huku miundombinu yake ikiwa bora kuliko ile ya awamu ya Azimio la Arusha. Wigo wa kuwakutanisha vijana kupitia vyombo vya habari na ajira rasmi na zisizorasmi umepanuka zaidi. Mfumo wa kidemokrasia wenye mawazo mbadala katika siasa umeimarika sana, kutaja kwa uchache tu. Mambo haya yote pamoja na mengine mengi yanapatikana hata katika ripoti ya Economic and Social Research Foundation (2018).

Kwa hiyo, aina ya wahusika, mandhari, mazingira na wazo kuu la mwandishi halikuwa na namna nyingine ya kuumbwa kupitia namna na viwango tulivyovibaini. Sehemu kubwa ya wahusika wa mwandishi ni vijana wanaoukataa ukale. Wanafuatilia taarifa mbalimbali zikiwemo za kiuchumi, kisiasa na kijamii. Tena, baadhi ya vijana wanaonekana kuwavuta wenzao kutoka vijijini ili wakashirikiane kutengeneza kesho yao kupitia biashara ya ujasiriamali. Kila mandhari imepewa muktadha unaotambulisha wasifu wa maisha na tabia ya wahusika kwa uzito stahiki. Ndiyo maana kwa kuteua mazingira ya mikoa ya mwishoni mwa kusini mwa Tanzania, tumekutana na lahaja ya Mgao na mazungumzo ya kinyonge na mengine

yenye taarifa sahihi na zisizo sahihi kuhusu maisha ya dunia ya leo. Lakini tulipofika jijini Dar es salaama, tunawaona wahusika wengi hawazungumzi lahaja ya Mgao. Na, kauli zao zinabeba lugha ya maisha halisi ya dunia ya leo.

Kwa mujibu wa Penelope (2000), tofauti ya uzungumzaji na uzaliwaji wa lugha mpya hutokana na mambo mengi yenye kufungamanisha hisia, uchumi, sosholojia, utamaduni, teknolojia, uhamaji watu, elimu, maendeleo na mabadiliko ya kijamii. Na kwamba, hali hii huwezi kuidhibiti kwa namna yoyote ile. Kwa sababu, jamii hasa vijana huzalisha msamiati na namna ya uzungumzaji mpya kwa haraka zaidi kuliko wafanyavyo taasisi za ukuzaji na ustawishaji lugha. Kumbe basi, hata Shani Omari alilitambua hili na kulifinyanga vizuri ili lengo lake lishikamane vema na vipengele vingine vya kifani na kimaudhui. Mazingira ya jamii inayolengwa yanapozingatiwa kwa ukamilifu huifanya hadhira kujihisi kama mlengwa halisi wa kazi husika. Kinyume chake, kazi husika hukosa walaji (Senkoro, 1995). Huu ni ubunifu usio na shaka katika kuteua na kuumba wazo la kisanaa ili kuchochea maendeleo endelevu kwa jamii na Tamthilia ya Kiswahili.

Kwa upande wa tamthilia ya *Changamoto* haonekani kuwa na utajiri mkubwa wa matumzi ya lugha teule. Bila shaka hali hii inatokana na uteuzi wa wahusika ambao kwa miaka mingi wamekuwa wakinyanyapaliwa katika kupata haki sawa za kiuchumi, kijamii, kisiasa na kiutamaduni. Wahusika wengi katika tamthilia hii ni vijana wenye changamoto ya ulemavu wa viungo ambao wengi wao wameishi maisha ya kutengwa na jamii kwa kufichwa ndani – kwa sehemu kubwa ya umri wa uhai wa maisha yao. Hivyo kukosa fursa ya kujifunza lugha inayotawala mazingira ya jamii yao. Watu wengi wenye ulemavu kwa miaka mingi wamenyimwa fursa ya

kupata haki ya: elimu, kumiliki uchumi, kuishi kwa furaha, matibabu, uongozi, ulinzi na usalama, kuishi bila unyanyapaa, kutaja kwa uchache (SHIVYAWATA, h.m.).

Kwa mazingira ya namna hii, watu hawa hawawezi kuwa na utajiri wa lugha kama walionao watoto au vijana wenzao ambao sehemu kubwa ya malezi na makuzi yao imekuwa huru katikati ya jamii kwa kuishi kama jumua moja katika kila hatua ya makuzi (Clark, 2009). Bila shaka, mwandishi Elizabeth Mahenge alizingatia zaidi ukweli huu katika kuteua na kuumba lugha inayosadifu maisha ya wahusika wake. Hata hivyo kwa upande mwingine, tunaweza kujiuliza sababu ipi hasa iliyomfanya mwandishi kumpa hadhi sawa na wahusika wengine, mhusika Maimatha katika matumizi ya lugha teule. Katika tamthilia ya *Changamoto*, Maimatha ndiye mhusika pekee mwenye ulemavu wa viungo anayetambulishwa kama msomi (uk. vi) aliyefaulu usaili kwa njia ya simu – nafasi ya usekretari kisha kunyimwa ajira hiyo baada ya kugundulika kuwa ni mlemavu (rej. uk. 10 – 14).

Katika kurasa zote tajwa pamoja na kurasa zilizofuatia - alizozungumza Maimatha (uk. 34 - 35), mwandishi hakumpatia Maimatha utajiri wa lugha tunaoshughulika nao isipokuwa maneno mawili ya Kihehe – “weuli” na “ale” akimsalimia baba yake mzazi (uk. 12). Lakini hata pale alipokutana na katibu muhtasi pia mkuu wa shule, Maimatha hakuzalisha msimu wala uchanganyaji ndimi. Hata alipokutana na watu wenye ulemavu wenzake, Maimatha hakuzungumza chochote badala yake aliendelea kuzungumza na baba yake – ijapokuwa aliwatambua watu wenye ulemavu wenzake. Kitendo cha mwandishi kumtenga Maimatha na watu wenye ulemavu kama yeye na kumweka karibu na baba yake kila mara tunaona ndiyo sababu ya Maimatha kama kijana msomi kutokuzalisha misimu na lugha ya kigeni hata moja isipokuwa ile ya

asili ya baba yake. Tunasema hivi kwa sababu, Kiafrika mtoto mwenye adabu aliyefundwa akafundika hawezi kuzungumza kitu kisichokubalika kwa wazee (Lynch na Roberts, 2010). Kwa mantiki hii, kama Maimatha angezungumza misimu au lugha aliyojifunza shuleni na, au vyuoni – lugha ambayo haijulikani kwa baba yake, ni dhahiri Godwin (baba wa Maimatha) angemwona kama kijana mhuni aliyeharibika baada ya kupata elimu au kuchangamana na watoto wengine huko shuleni na vyuoni.

Kwa hiyo, eneo pekee ambalo Maimatha angeweza kuzalisha misimu na lugha za kigeni - mbali na Kihehe, ni pale mahakamani alipokutana na watu wenye ulemavu wenzake pia shuleni. Hata hivyo, katika mazingira yote mawili, bado Maimatha alikuwa ameongozana na baba yake. Jambo lililomfanya kwa mwono wetu kushindwa kwa mara nyingine kuzalisha lugha mbadala. Ingawa shuleni Maimatha angeweza kuchanganya lugha, bado tunabaini mazingira hayakuwa rafiki kuchanganya ndimi kwa sababu walipokelewa shuleni kishari. Pia, kwa mujibu wa Roy-Campbell na Qorro (1997) shule nyingi zinakabiliwa na changamoto ya walimu, wanafunzi na wafanyakazi kushindwa kumudu lugha za kigeni. Hivyo, wengi huishia kuzungumza ama Kiswahili au kuchanganya lugha au kuongea lugha ya kigeni iliyo mbovu.

Pamoja na mwono huu, bado tunasisitiza kuwa katika mazingira ya zama hizi, siyo rahisi kijana msomi kuzungumza mwanzo mwisho bila kuchanganya ndimi (Muysken, 2000). Hasa katika mazingira yanayomkutanisha na watumia lugha anayoimudu – hata kama mzazi wake haelewi au anaofikiria kuzungumza nao hawaimudu vizuri lugha husika. Tena, hapo ndipo angetaka kumwonesha mzazi



kwamba, gharama aliyoitumia kumpa elimu haikwenda bure. Kwa hali hii, katika kumuumba Maimatha kisaikolojia, kishosholojia na kiweledi, ubunifu wa mwandishi uliminywa kwa kiasi hivyo kudunisha matumizi ya lugha - ama kwa kujua au kutokujua.

Nayo tamthilia ya *Nje - Ndani*, utafiti umegundua kuwa na misimu mingi zaidi kushinda tamthilia teule nyingine. Uchunguzi wetu umebaini kwamba, waandishi wote wawili ni vijana wa miaka ya 1980s hivyo kwa wao misimu ni sehemu ya maisha ya kila siku. Reuster-Jahn na Kiebling (2006) wanatueleza kuwa, misimu hujitokeza sana katika lugha za mitaani kwa sababu kundi kubwa kwa uzalishaji na utumiaji misimu ni vijana huko mtaani kuliko ofisini ambako matumizi ya lugha sanifu husisitizwa sana. Nao Timothy (2016) na Malima (2018) wanaongeza kwamba, kwa zama hizi; mitandao ya kijamii ndiyo inayoonekana kuwa kitovu cha kuzalisha misimu.

Malima (2018) anafafanua zaidi kwa kusema, misimu huweza kuhudumu kama misemo, mafumbo na ishara miongoni mwa wahusika wake kama njia ya kutunza siri. Na kwamba, matumizi na maana ya neno ambalo ni msimu haitegemei uwezo au kiwango cha elimu ya darasani bali mazingira na mahusiano ya watumia lugha ya misimu husika. Misimu huweza kutokana na matumizi ya neno jipya, matamshi mapya, utanuzi usiorasmi wa maana au matumizi ya maneno ya mkopo ama utohoaji usiorasmi wa maneno. Hii ndiyo sababu tamthilia zote zenye matumizi ya juu ya misimu (rej. *Mashetani* na *Safari ya Chinga*), zimebainika kuwa na uchanganyaji ndimi wa juu, ucheshi pia lugha ngumu au nyepesi kiasi kinyume na *Kijiji Chetu*, *Harakati za Ukombozi* na *Changamoto* zenye matumizi ya chini ya misimu.

Pia, utafiti umebaini mambo mazito yamejadiliwa katika tamthilia hii. Baadhi ya mambo hayo ni kashfa za ufisadi kupitia utoroshaji wa nyara za serikali na maliasili nyingine za taifa, mikopo chechefu kwa wanyonge, mfumo wa elimu uliosambaratika, mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi pasipo kiini cha tatizo kushughulikiwa, kutaja kwa uchache. Mambo haya pamoja na mengine yanaligusa tabaka tawala moja kwa moja. Kwa vile wahusika hawako tayari kukutana na mkono wa dola, wamelazimika kutumia lugha ya ucheshi na misimu ili kujenga tafakuri huku wakileta umbo la nafsi kujisuta yenyewe. Yaani wametumia ubunifu wa mtu mmoja kuzungumza mwenyewe (intrapersonal communication) kama kichaa anavyozungumza ilhali akifikisha ujumbe kwa jamii inayomsikiliza.

Ubunifu wa kutokulikabili tabaka tawala moja kwa moja, badala yake mwandishi anatumia lugha ya mficho yenye hinda umetumiwa na watunzi kadhaa wakiwemo Ebrahim N. Hussein (katika *Mashetani*), J. Ngomoi (katika *Ndoto ya Ndaria*), Shaaban Robert (katika *Kusadikika* na *Kufikirika*) na Said Ahmed Mohamed (katika *Kivuli Kinaishi*). Aidha, hekima hii inajidhihirisha kwa nabii Nathani alipotumwa na Mungu kwenda kumtangazia Mfalme Daudi hukumu ya kuzini na mke wa Uria, mmoja wa wanajeshi wake. Nabii huyu hakufika na kutangaza hukumu moja kwa moja, badala yake alitumia hadithi fumbo yenye kufanana na kile alichokitenda Mfalme Daudi. Baada ya hapo, nabii alimuuliza mfalme, kama ungekuwa wewe mfalme ungemtenda nini mtu huyu? Mfalme alitoa jibu lenye kiapo ndani yake. Ndipo nabii akamwambia mtu huyo ni yeye Mfalme Daudi. Mfalme Daudi hakuweza kumwadhibu nabii kwa vile tayari ameshaapa ambapo kwa mila zao, huwezi kutengua kiapo chako – sharti ukitimize; labda iamriwe vinginevyo kwa

taratibu maalum. Simulizi hii inapatikana katika 2 Samweli, sura ya 11 hadi sura ya 12 katika Bible Society of Tanzania (1997).

Kwa jumla, tamthilia ya *Nje–Ndani* kama ilivyo kwa tamthilia ya *Mashetani* imetumia lugha yenye ubunifu inayowafundisha watunzi chipukizi, wahakiki na wasomaji kutambua nafasi ya busara katika kuteua cha kuongea na namna ya kukiongea. Kwa sababu, ingawa siyo kila mara kitaeleweka miongoni mwa wasikilizaji na wasomaji kwa namna iliyokusudiwa, bado maisha yako kama mzungumzaji yana thamani kwako binafsi na jamii inayokutegemea. Ubunifu usiozingatia hali halisi ya mazingira nao una uwalakini kisanaa (Mohamed, 1990). Hii ni kwa sababu nyakati hazigandi na dunia siyo tuli (Senkoro, 1987) kwa vile lisilowezekana leo, kesho linaweza kubadilika na kuwa heri au ole zaidi.

### **6.3 Hitimisho**

Ubunifu ni jambo muhimu sana kisanaa ili kufanya walaji wa bidhaa husika kutokuikifu na kuipa kisogo. Utafiti wetu umethibitisha kwamba, kila tamthilia teule ina athari mahususi kwa wasomaji, wahakiki, walimu, wanafunzi na watunzi wa leo na siku zijazo. Kila mwandishi ana upekee unaojenga upya wenye kuchochea maendeleo endelevu ya jamii na Tamthilia ya Kiswahili. Kila tamthilia inabeba wajibu wa kumkomboa mnyonge kwa kumchochea kuchukia uovu ili atafakari mwenyewe namna bora na sahihi ya kuzitatua changamoto zake na za jamii inayomzunguka katika wakati husika, mazingira husika na jamii husika pasipo kuwategemea wengine kumkomboa. Sura ni mwisho wa kuwasilisha matokeo na mjadala wa matokeo ya utafiti. Sura ya mwisho ni sura ya saba inayobeba muhtasari wa utafiti, mahitimisho ya utafiti na mapendekezo ya utafiti.

## **SURA YA SABA**

### **MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO**

#### **7.1 Utangulizi**

Sura hii inabeba majumuisho ya taarifa zilizomo katika sura sita (6) za awali za andiko hili. Maudhui ya sura hii ni mengi lakini yanawasilishwa kwa ufupi sana tofauti na sura zilizotangulia. Lengo la ufupisho huu ni kutoa picha kamili ya nini kilichotarajiwa, kwa sababu gani, kwa vipi, kwa faida ya nani, nini kilichobainika, na nini kifanyike. Sura hii imefumbata taarifa zote muhimu juu ya utafiti wetu. Taarifa hizo zimewekwa chini ya mada ndogo nne (4) kuu. Mada hizo ni muhtasari wa utafiti, ufaafu wa utafiti, mahitimisho ya utafiti na mapendekezo ya utafiti. Taarifa hizi ni kwa faida ya wasomaji wa andiko hili na taaluma yenyewe ya Tamthilia ya Kiswahili na Fasihi ya Kiswahili.

#### **7.2 Muhtasari**

Sehemu hii inawasilisha kwa ufupi maudhui yanayopatikana katika sura ya kwanza, sura ya pili, sura ya tatu, sura ya nne, sura ya tano na sura ya sita. Maudhui ya sura hizi sita (5) yamegawanywa katika vipengele vikuu viwili. Kipengele cha kwanza ni muhtasari wa tatizo, mapitio ya maandiko na mbinu za utafiti. Kipengele cha pili kinahusu muhtasari wa matokeo ya utafiti.

##### **7.2.1 Muhtasari wa Jumla**

Utafiti ulilenga kuchunguza maendeleo ya ubunifu katika Tamthilia ya Kiswahili ya awamu ya Azimio la Arusha na soko huria kwa kutumia utafiti linganishi. Uchunguzi ilifanyika kwa njia ya usomaji makini katika kubainisha, kulinganisha na kulinganua dhamira na matumizi ya lugha ili kubaini kufanana na kutofautiana kwa ubunifu

katika tamthilia (6) sita teule za Kiswahili za awamu ya Azimio la Arusha na zile za awamu ya soko huria. Vipindi hivi viwili viliteuliwa makusudi kwa sababu vimekuwa vikitajwa kuwa na utofauti mkubwa wa kisera na kimfumo. Hivyo kuathiri mfumo wa maisha ya watu katika nyanja zote za maisha kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni, kijamii, kisanaa na kidini kwa namna na viwango tofauti tofauti.

Msukumo wa kufanyika kwa utafiti huu ulitokana na ombwe la taarifa rasmi zinazohusiana na maendeleo ya Tamthilia ya Kiswahili katika awamu ya soko huria nchini Tanzania. Aidha, kulikuwapo na madai ya kuwa Tamthilia ya Kiswahili imedumaa nchini Tanzania huku ikionekana kukua na kustawi nchini Kenya. Miongoni mwa sababu zilizotolewa ni pamoja na changamoto ya ubunifu, mabadiliko ya kisera na uholela wa soko la vitu, fasihi ikiwemo. Kwa hiyo, mtafiti alitaka kuthibitisha ukweli na kiwango cha madai haya yaliyotoka kwa Gromov (2014) na Olali (2015). Lengo kuu lilikuwa ni kulinganisha kazi za awamu ya Azimio la Arusha na zile za soko huria ili kubaini kufanana na kutofautiana katika ubunifu wa ujenzi wa dhamira na matumizi ya lugha.

Lengo hili liligawanyika katika malengo mahususi matatu (3). Lengo la kwanza lilikuwa ni kulinganisha ubunifu katika dhamira zinazojitokeza katika tamthilia teule za Kiswahili za awamu ya Azimio la Arusha na zile za soko huria ili kubaini kama kuna ubunifu endelevu. Lengo la pili lilikuwa ni kulinganisha ubunifu katika matumizi ya lugha yanayojitokeza katika tamthilia teule za Kiswahili za awamu ya Azimio la Arusha na zile za soko huria ili kubaini kama kuna ubunifu endelevu. Na, lengo la tatu lilikuwa ni kutathmini athari ya ubunifu katika dhamira na matumizi ya lugha yanayojitokeza katika tamthilia teule za Kiswahili za awamu ya Azimio la

Arusha na zile za soko huria ili kubaini namna zinavyochochea maendeleo endelevu ya Tamthilia ya Kiswahili kisanaa.

Utafiti uliongozwa na maswali makuu matatu (3) ambayo ni: (i) Je, ubunifu katika dhamira zinazojitokeza katika tamthilia teule za Kiswahili za awamu ya Azimio la Arusha unafanana na kutofautiana vipi na ule wa tamthilia teule za Kiswahili za awamu ya soko huria? (ii) Je, ubunifu katika matumizi ya lugha yanayojitokeza katika tamthilia teule za awamu ya Azimio la Arusha unafanana na kutofautiana vipi na ule wa tamthilia teule za Kiswahili za awamu ya soko huria? (iii) Kwa vipi athari ya ubunifu katika dhamira na matumizi ya lugha yanayojitokeza katika tamthilia teule za Kiswahili za awamu ya Azimio la Arusha na zile za soko huria yanaweza kuchochea maendeleo endelevu ya Tamthilia ya Kiswahili kisanaa?

Matokeo ya utafiti huu yanatarajiwa kuwa ya faida kwa wadau tofauti tofauti wa taaluma na Fasihi ya Kiswahili, hususani tamthilia kwa kuchangia taarifa sahihi ambazo hazijapata kuwapo awali juu ya maendeleo ya Tamthilia ya Kiswahili kiubunifu. Baadhi ya wanufaika wa utafiti huu ni pamoja na wanafunzi, walimu, watunzi, watafiti na wahakiki wa kazi za kitamthilia. Utafiti ulishughulikia ubunifu katika ujenzi wa dhamira, lugha ya ucheshi, misimu, matumizi ya uchanganyaji ndimi pia uwepesi na ugumu wa lugha katika tamthilia sita (6) teule. Zaidi ya hayo, mtafiti alihakikisha haendi kinyume na masuala yote ya kiitikeli ili kutokuathiri mchakato mzima wa utafiti na matokeo ya utafiti huu.

Mtafiti alitalii maandiko yakiwemo yale ya tafiti tangulizi juu ya utunzi, historia na maendeleo ya Tamthilia ya Kiswahili. Utafiti wetu umeonesha kuwapo kwa tafiti kadha wa kadha zenye kuhusiana na tamthilia teule za awamu ya Azimio la Arusha.

Tulibaini kuwa hakuna utafiti linganishi ambao umefanyika kwa lengo la kuchunguza na kulinganisha maendeleo ya ubunifu ya tamthilia za awamu ya Azimio la Arusha na soko huria kwa kumakinikia tamthilia sita (6) teule tulizozichunguza. Hivyo, utafiti huu uliona kuna haja ya kufanya utafiti wa kina ili kuziba pengo hili. Katika kuziba pengo hili, utafiti huu ulichunguza maendeleo ya ubunifu wa dhamira na matumizi ya lugha katika Tamthilia ya Kiswahili katika awamu ya Azimio la Arusha na awamu ya soko huria kwa kutumia utafiti linganishi. Lengo lilikuwa ni kubaini kama kuna ubunifu endelevu ama la. Kiunzi cha utafiti huu kilikuwa ni nadharia ya Fasihi Linganishi kwa ajili ya kuchambua kisha kulinganisha na kulinganua tamthilia za awamu ya Azimio la Arusha na zile za awamu ya soko huria.

Utafiti ulikuwa ni wa maktabani kutokana na mahitaji ya msingi ya asili ya utafiti wenyewe. Tamthilia teule ziliteuliwa kwa kutumia usampulishaji nasibu tabakishi. Data zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji makini iliyoongozwa na maswali kadhaa yenye kuhusiana na malengo mahususi ya utafiti huu. Uwasilishaji wa matokeo ya utafiti umeongozwa na mkabala wa kiufafanuzi. Tamthilia sita (6) teule zilikuwa ni *Mashetani* (1971) ya Ebrahim N. Hussein, *Kijiji Chetu* (1975) ya Ngalimecha Ngahyoma na *Harakati za Ukombozi* (1982) ya Amandina Lihamba, Ndyanao Balisidya na Penina Mhando zilizowakilisha awamu ya Azimio la Arusha. Nyingine ni *Safari ya Chinga* (2009) ya Shani Omari, *Changamoto* (2010) ya E. Mahenge na *Nje–Ndani* (2016) ya A. A. Majid Mswahili na M. S. Njonjolo zilizowakilisha awamu ya soko huria.

### **7.2.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti**

Sehemu hii inaelezea kwa ufupi yaliyojili katika kila lengo mahususi la utafiti wetu. Matokeo ya jumla ya utafiti yanaonesha ya kwamba, kuna ubunifu endelevu katika uteuzi na ujenzi wa dhamira na matumizi ya lugha katika kila awamu. Maendeleo endelevu ya dhamira na matumizi ya lugha katika kila tamthilia yanafungamana kiubunifu na wakati na aina ya jamii ya ndani na nje ya Tanzania. Mafungamano hayo yanaonekana kuwa ya faida kwa jamii nzima - kimfanano na kiutofauti.

Lengo mahususi la kwanza lilikuwa ni kulinganisha ubunifu katika dhamira zinazojitokeza katika tamthilia teule za Kiswahili za awamu ya Azimio la Arusha na zile za soko huria ili kubaini kama kuna ubunifu endelevu. Matokeo yanaonesha ya kuwa, kila tamthilia ina ubunifu endelevu wa dhamira za kijamii, kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni. Lengo la pili lilikuwa ni kulinganisha ubunifu katika matumizi ya lugha yanayojitokeza katika tamthilia teule za Kiswahili za awamu ya Azimio la Arusha na zile za soko huria ili kubaini kama kuna ubunifu endelevu. Matokeo ya jumla yanaonesha ya kwamba, kila tamthilia imetumia ubunifu katika kuumba lugha kwa sababu, namna na viwango tofauti tofauti vinavyofungamana na wazo, wakati na historia ya jamii lengwa.

Lengo la tatu lilikuwa ni kutathmini athari ya ubunifu katika dhamira na matumizi ya lugha yanayojitokeza katika tamthilia teule za Kiswahili za awamu ya Azimio la Arusha na zile za soko huria ili kubaini namna zinavyochochea maendeleo endelevu ya Tamthilia ya Kiswahili kisanaa. Matokeo yanaonesha, kila tamthilia ina ubunifu unaochochea athari chanya kwa ukuaji na ustawi endelevu wa jamii na Tamthilia ya Kiswahili ya sasa na ya nyakati zijazo. Hali hii imetokana na umakini wa kila



mwandishi kuteua na kufinyanga vema kiubunifu wazo na vijenzi vingine mfano mandhari, wahusika, miktadha, mazingira, ploti, huku wakizingatia wakati unaosadifu historia ya jamii lengwa kiutunzi na kimaisha.

### **7.3 Ufaafu wa Utafiti Huu**

Mchango mkuu wa utafiti wetu ni kudhihirika kwa maarifa mapya ya kiuchunguzi na taarifa sahihi juu ya ubunifu endelevu katika Tamthilia ya Kiswahili nchini Tanzania. Ambapo, kupitia utafiti linganishi matokeo ya jumla yamedhihirisha kuwapo kwa ubunifu endelevu katika Tamthilia ya Kiswahili nchini Tanzania kwa awamu zote mbili tulizozishughulikia. Matokeo haya ni kinyume na madai yaliyochochea kufanyika kwa utafiti huu. Hivyo, utafiti huu umekuwa daraja muhimu kwa watunzi, wahakiki, watafiti, walimu, wanafunzi na wengineo watakaobahatika kusoma tasnifu hii. Kwa sababu, utafiti umechunguza tamthilia kongwe na chipukizi. Kupitia tasnifu hii, maarifa haya mapya yanakwenda kufahamika duniani kote.

### **7.4 Mahitimisho**

Utafiti ulijikita katika kuchunguza maendeleo ya ubunifu katika Tamthilia ya Kiswahili ya awamu ya Azimio la Arusha na soko huria nchini Tanzania, kwa kutumia mbinu ya utafiti linganishi. Utafiti umebaini kuwapo kwa ubunifu endelevu katika tamthilia za Kiswahili za awamu ya Azimio la Arusha na zile za soko huria. Kwani kila mwandishi ameteua na kusana dhamira zake kwa namna yake na kwa mkazo wake. Kila mwandishi anaonekana kuathiriwa na jamii na wakati unaomzunguka katika kuteua na kuyasana maudhui. Hali ya maisha katika vipindi husika vya kihistoria nchini Tanzania imeathiri maendeleo ya ubunifu katika Tamthilia ya Kiswahili kwa namna na viwango tofauti. Kila tamthilia imejikita

katika mjadala wa kina juu ya hali duni ya maisha miongoni mwa wanyonge, ufa mkubwa kati ya miji na vijiji, na ufa mkubwa kati ya wenye nacho na wasiokuwa nacho. Mambo haya yote yanagusa na kuathiri hatima ya jamii katika kila nyanja ya maisha. Hivyo, kiubunifu, waandishi wamefanikiwa kuonesha kwamba ukombozi wa dhata na endelevu ni ajenda hai na endelevu.

Kwa upande wa matumizi ya lugha, tumegundua ya kwamba, kila mwandishi ana namna yake ya kutambaa na lugha. Na kwamba, siyo rahisi kukutana na waandishi (hata wa awamu moja) wakifanana na kutofautiana kwa asilimia 100. Pia, tamthilia zote sita (6) zimebainika kuwa na makutano na mwachano huru ndani na nje ya awamu husika. Hii inatoa picha ya kwamba, kila tamthilia na kila awamu ina vionjo vya pekee na jumishi kiubunifu. Makutano na mwachano huu huru unatokana na ukweli kuwa, kila tamthilia ina athari ya historia ya malezi, makuzi, wakati na utamaduni wa jamii iliyotawala mazingira ya uandishi wa mwandishi husika. Hali inayoonesha kuwapo kwa matumaini ya athari chanya kwa ustawi endelevu wa watunzi, jamii na Tamthilia ya Kiswahili.

### **7.5 Mapendekezo**

Utafiti huu ulijikita katika kuchunguza maendeleo ya ubunifu katika Tamthilia ya Kiswahili ya awamu ya Azimio la Arusha na soko huria nchini Tanzania, kwa kutumia mbinu ya utafiti linganishi. Mapendekezo yanarejelea walengwa waliobainishwa katika sura ya kwanza - kipengele cha umuhimu wa utafiti (1.6). Kwa hiyo mapendekezo yetu yatakuwa mahususi kwa watunzi, wahakiki, watafiti, walimu na wanafunzi.

### **7.5.1 Mapendekezo kwa Watunzi**

Utafiti wetu umebaini kwamba, watunzi wamejitahidi sana kiubunifu kuteua na kusana dhamira zinazoigusa jamii moja kwa moja. Pia, dhamira hizi zinakwenda na wakati. Hata hivyo, kwa upande wa matumizi teule ya lugha inaelekea watunzi hawatilii sana uzito vipengele vya uchanganyaji ndimi na misimu. Hivyo, mtafiti anapendekeza pasipo kuathiri lengo la mwandishi katika maudhui; matumizi ya uchanganyaji ndimi na misimu yapewe uzito wakati wa utunzi. Vilevile, matumizi ya lugha ngumu yanaonekana kuwa siyo njia mwafaka sana ya kuwasiliana na jamii kwa wepesi na rahisi. Hivyo, tunashauri pasipo kuathiri usalama wa watunzi, matumizi ya lugha ngumu yasiwe ya kiwango cha juu sana kama ilivyodhihirika katika tamthilia ya *Mashetani*. Angalau, tamthilia ya *Nje-Ndani* ina matumizi ya lugha ngumu kiasi inayoweza kumfanya msomaji kupata wazo kusudiwa. Lengo ni kuifanya tamthilia izidi kuwa jirani zaidi na wasomaji huku ikitunza na kustawisha historia ya jamii, lugha ya Kiswahili na Tamthilia yenyewe ya Kiswahili.

### **7.5.2 Mapendekezo kwa Wahakiki na Watafiti**

Utafiti wetu umebaini kwamba wahakiki na watafiti wengi wanawekeza zaidi katika uchambuzi na utafiti wa tamthilia za watunzi nguli, wakongwe na maarufu. Watunzi hawa, wengi ni zao la awamu ya Azimio la Arusha. Wahakiki na watafiti wachache wanaonekana kuwachunguza wale “wasio maarufu” ambao wengi ni zao la awamu ya soko huria. Athari ya utamaduni huu ni kwa jamii ya wasomaji kushindwa kuzibaini kazi mpya huku wengine wakidhani watunzi chipukizi hawana uwezo kiubunifu. Hali hii inaathiri hata tathmini ya historia na maendeleo ya Tamthilia ya Kiswahili.

Hivyo, tunapendekeza tamthilia za watunzi ambao ni zao la awamu ya soko huria kutafitiwa na matokeo kuchapishwa kwa wingi. Pia, utafiti linganishi utumike zaidi kuchunguza utunzi wa kazi za awamu ya soko huria zenyewe kwa zenyewe; na kati ya tamthilia za ndani dhidi ya zile za nje ya awamu ya soko huria za nchini Tanzania na za nje ya nchi. Hata hizi tulizozitalii (*Safari ya Chinga, Changamoto na Nje-Ndani*) bado zinahitaji kutafitiwa katika vipengele vingine vya fani na maudhui.

### **7.5.3 Mapendekezo kwa Walimu na Wanafunzi**

Kiini cha utafiti huu mbali ya hoja ya Gromov (2014) na Olali (2015) ni Tamthilia ya Kiswahili nchini Tanzania kushuka kiubunifu ikilinganishwa na zile za nchini Kenya. Kwa kurejelea matokeo huu, utafiti umebaini kwamba, madai haya siyo ya kweli. Hivyo tunapendekeza, walimu na wanafunzi wajenge utamaduni wa kutafuta, kusoma na kuzichunguza tamthilia nyingi za Kiswahili za kila awamu inayobeba historia na maendeleo ya Tamthilia ya Kiswahili - nchini Tanzania na nje ya Tanzania. Kusoma vyanzo vichache vya taarifa kunaweza kuathiri mawanda ya usahihi wa taarifa katika mapana yake. Utamaduni wa kutafiti na kusoma matini kutoka vyanzo sahihi vingi kadri ya uwezo wa msomaji, kutaondoa kauli jumuishi na ukasuku miongoni mwa wanafunzi na walimu. Aidha, kwa kusoma ripoti za utafiti na kazi bunilizi za Tamthilia ya Kiswahili kwa wingi na kwa kina zaidi, wapo watakojifunza mbinu anuai za kiutunzi zitakazowawezesha kunoa uwezo wao kiutunzi na kihoja.

### MAREJELEO

- Abdulla, M. S. (1974). *Kuandika hadithi za kubuni: uandishi wa Tanzania*. Dar es salaam: East African Literature Bureau.
- Achebe, C. (1973). *Shujaa Okonkwo*. Nairobi: East African Publishing House.
- Adeseke, A. E. (2016). African literature (drama) and the language issue. Katika *Social Science Review*, 2 (1) (49-59). <https://pingpdf.com/pdf-african-literature-drama-and-the-language-issue-social-science-.html>.
- Alabi, D. O. (2015). 2 Kings 18:26-28 and the role of indigenes language in the growth of African independent churches in Nigeria. Katika *Journal of Philosophy, Culture and Religion*, 4 (16 – 21). <https://iiste.org/Journals/index.php/JPCR/article/view/19280/19703>.
- Ally, B., Yahya-Othman, S., & Shivji, I. (Wahariri). (2013). *Miongozo miwili kupaa na kutunguliwa kwa Azimio la Arusha*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: Kigoda cha Taaluma cha Mwalimu Nyerere.
- Arkadie, B. V. (1995). Economic strategy and structural adjustment in Tanzania. Katika *PSD Occasional Paper No. 18*. The World Bank: Private Sector Development Department. [documents.worldbank.org/curated/en/649601468765032908/pdf/multi0page.pdf](https://documents.worldbank.org/curated/en/649601468765032908/pdf/multi0page.pdf).
- Arowolo, D. (2010). Effects of western civilisation and culture on Africa. Katika *Afro-Asian Journal of Social Sciences*, 1 (1, Quarter IV) (hakuna kurasa). [https://www.researchgate.net/publication/266252078\\_The\\_effects\\_of\\_western\\_civilisation\\_and\\_culture\\_on\\_Africa](https://www.researchgate.net/publication/266252078_The_effects_of_western_civilisation_and_culture_on_Africa).
- Bandura, A. (1977). *Social learning theory*. Englewood Cliffs, NJ: Prentice-Hall.
- Baraza la Kiswahili la Zanzibar. (2010). *Kamusi la Kiswahili fasaha*. Nairobi: Oxford University Press, East Africa Ltd.
- Barnett, M. A. (1988a). Reading through context: how real and perceived strategy use affects 12 comprehension. Katika *The Modern Language Journal*, 72 (2)

(150–162).<https://onlinelibrary.wiley.com/doi/abs/10.1111/j.1540-4781.1988.tb04177.x>.

- Barnett, M. A. (1988b). *Sociology and development*. London: Routledge
- Berg, L. B. (2001). *Qualitative research methods for the social sciences* (4th ed.). Boston and London: Allyn & Bacon.
- Bertoncini, E. Z. (1989). *Outline of swahili literature*. Leiden: E. J. Brill.
- Bible Society of Tanzania. (1997). *Maandiko matakatifu ya Mungu yaitwayo BIBLIA*. Nairobi: Africa Area Typesetting Unit.
- Broad, C. D. (1975). *Leibniz: An introduction*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Cao, S. (2013). *The variation theory of comparative literature*. NY & London: Springer – Verlag Berlin Heidelberg.
- Caponecchia, C. (2012). *The human: basic psychological principles*. Victoria: The Safety Institute of Australia Ltd.
- Chachage, C. S. L. (2000). *Environment, aid and politics in Zanzibar*. Dar es Salaam: DUP
- Chachage, S. C. (2002). *Makuadi wa Soko Huria*. Dar es salaam: E & D Vision Publishing Limited.
- Chachage, S. L. C. (2014). *Uchambuzi wa sera, uongozi na maslahi ya Watanzania*. Dar es salaam: E & D Vision Publishing Limited.
- Chiraghdin, S. (1976). Utangulizi. Katika Hussein, E. N, *Jogoo Kijijini na Ngao ya Jadi*. Nairobi: Oxford University Press.
- Chomsky, N. (2004). Knowledge of language as a focus of inquiry. Katika Lust, B., na Foley, C (Wahariri). *First language acquisition: The essential readings*. Malden: MA: Blackwell Pub.
- Clark, E. V. (2009). *First language acquisition* (second edition). Cambridge: Cambridge University Press.

- Culpeper, J., Short, M., & Verdonk, P. (Wahariri). (1998). *Exploring the language of drama from text to context*. London: NY: Routledge.
- Davidson, B. (1978). *African in modern history: The search for a new society*. London: Allan Lane.
- de Saussure, F. (1966). *Course in general linguistics*, 117. Trans, Wade Baskin, New York: McGraw-Hill
- Duerden, D., & Pieterse, C. (Wahariri). (1988). *African writers talking*. Oxford: Heinmann International Publishing.
- Eagleton, T. (2008). *Literary theory: An introduction* (anniversary edit.). UK: Blackwell Publishing.
- Economic and Social Research Foundation. (2018). *Muhtasari Tanzania ripoti ya maendeleo ya binadamu 2017: Sera ya kijamii katika muktadha wa mageuzi ya kiuchumi*. <http://www.esrf.or.tz/docs/thdr2017swsummary.pdf>.
- Education Standards Research Team. (2012). *Research evidence on reading for pleasure*. Department of Education. [https://assets.publishing.service.gov.uk/government/uploads/system/uploads/attachment\\_data/file/284286/reading\\_for\\_pleasure.pdf](https://assets.publishing.service.gov.uk/government/uploads/system/uploads/attachment_data/file/284286/reading_for_pleasure.pdf).
- Farnsworth, B. (2019). Human behavior: The complete pocket guide. <https://imotions.com>.
- Fouéré, M. (2014). Julius Nyerere, ujamaa, and political morality in contemporary Tanzania. *Katika African Studies Review*, 57 (1) (1–24). doi:10.1017/asr.2014.3. [http://journals.cambridge.org/abstract\\_S0002020614000031](http://journals.cambridge.org/abstract_S0002020614000031).
- Frank, C. (1951). *Imekwisha*. Nairobi: The Highway Press.
- Githiora, C. (2002). Sheng: peer language, Swahili dialect or emerging creole? *Katika Journal of African Cultural Studies*, 15 (2) (159-181). <http://www.jstor.org/stable/3181415>.

- Grenville, K. (2001). *Writing from start to finish: A six – step guide*. Crows Nest: Allen & Unwin.
- Gromov, M. D. (2014). The present state of Swahili literature as an artistic and social phenomenon. *Katika Journal of Language, Technology and Entrepreneurship in Africa*, 5 (1) (30-41).
- Hancock, G. (1991). *Lords of poverty: The power, prestige and corruption of the international aid business*. London: Atlantic Monthly Press.
- Hanson, B. J. (1997). *Takadini*. Dar es salaam: Mathew Bookstore and Stationers.
- Helge, K. (1996). *Ecology control and economic development in East African history*. London: James Currey.
- Hettiger, M. (h. m). *The racialization of politics in revolutionary Zanzibar*. [https://www.usna.edu/History/files/documents/Honors-Program/2010/Hettiger\\_Zanzibar.pdf](https://www.usna.edu/History/files/documents/Honors-Program/2010/Hettiger_Zanzibar.pdf).
- Hoffman, C. (1991). *An introduction of bilingualism*. London: Longman Publisher.
- Hotuba ya Mwalimu Nyerere Hoteli ya Kilimanjaro, Dar es salaam. (Juni 14, 1995). <https://www.youtube.com/watch?v=kP9-yViUa9w>.
- Hussein, E. N. (1967/1973/1980). *Wakati Ukuta*. Nairobi: East African Educational Publishers.
- Hussein, E. N. (1971). *Mashetani*. Peramiho: Ndada Press.
- Hussein, E. N. (1976). *Jogoo Kijijini na Ngao ya Jadi*. Dar es salaam: Oxford University Press.
- Hussein, E. N. (1988). *Kwenye Ukingo wa Thim*. Dar es salaam: Oxford University Press.
- Hussein, E. N. (2003). Hatua mbalimbali za kubuni na kutunga tamthilia kufuatana na misingi ya Ki – Aristotle. Katika TUKI, *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III: Fasihi* (197-205). Dar es salaam: Idara ya Kiswahili.



- Hyden, G. (1980). *Beyond ujamaa in Tanzania: Underdevelopment and an uncaptured peasantry*. Berkeley: University of California Press.
- Hyslop, G. (1957). *Afadhali Mchawi*. Nairobi: EALB.
- Independent Commission of the South on Development Issues. (1992). *The challenge to the south: the report of the south commission*. Oxford University Press.
- International Labour Organisation. (2016). *World employment and social outlook: trends 2016*. [https://www.ilo.org/wcmsp5/groups/public/---dgreports/---dcomm/---publ/documents/publication/wcms\\_443480.pdf](https://www.ilo.org/wcmsp5/groups/public/---dgreports/---dcomm/---publ/documents/publication/wcms_443480.pdf).
- International Labour Organisation. (2022). *World employment and social outlook: Trends 2022*. Geneva: International Labour Office.
- International Organization for Migration. (2019). *World migration report 2020*. [https://publications.iom.int/system/files/pdf/wmr\\_2020.pdf](https://publications.iom.int/system/files/pdf/wmr_2020.pdf).
- Ismail, B. (Jumatano, 12 Oktoba 2022). Makinda awataka vijana kujitafutia ajira wenyewe. Katika *Mwananchi*. Mwananchi Communications Limited.
- Jilala, H. (2012). Conceptualisation of metaphors in bongo flava music. Katika *Online International Journal of Arts and Humanities*, 1 (4) (59-67). <http://www.onlineresearchjournals.org/IJAH>.
- Jilala, H. (2016). *Misingi ya fasihi linganishi: nadharia, mbinu na matumizi*. Dar es salaam: Daud Publishing Company.
- John, J., & Mduda, F. (2014). *Kiswahili: Kidato cha tano na sita* (chapa ya pili). Dar es Salaam: Oxford University Press (T) Ltd.
- Juhani, K. (1988). *People and production in late pre-colonial Tanzania: History and structures*. Uppsala: Scandinavian Institute of International Studies.
- Kezilahabi, E. (1993). Uhuru wa mwandishi. Katika Mulokozi, M. M. & Mung'ong'o, C. G. (Wahariri), *Fasihi II, Uandishi Na Uchapishaji: Makala ya Semina ya Umoja wa Waandishi wa Vitabu Tanzania*. Dar es salaam: Dar es salaam University Press.

- Kezilahabi, E. (1995). Siasa, teknolojia na ukuaji wa fasihi ya Kiswahili. Katika *Kioo cha Lugha*, 1 (1–17). Dar es salaam: TUKI.
- Khatib, M. S. (1988). *Fungate ya Uhuru*. Dar es salaam: Aidan Publishers.
- Kiango, S. D. (1988). Kijiji Chetu. Katika *Mulika*, 20 (56-75).  
<https://journals.udsm.ac.tz/index.php/mj/article/view/1680/1569>.
- King'ei, K. (2010). *Misingi ya isimu jamii*. Dar es Salaam: TUKI.
- Kioko, E. M. (2017). Regional varieties and 'ethnic' registers of sheng.  
<https://www.researchgate.net/publication/278688615>.
- Kothari, C. R., & Gaurav, G. (2019). *Research methodology: Methods and techniques* (4<sup>th</sup> Edition). New Delhi: New Age International Publishers.
- Kuria, H. (1957). *Nakupenda, Lakini....* Nairobi: EALB.
- Langa, N. (2013). Challenges facing women entrepreneurs in accessing loans from microfinance institutions: The case of Dar es Salaam. (Tasnifu ya Shahada ya Uzamili Haijchapishwa), Chuo Kikuu cha Mzumbe.  
<http://scholar.mzumbe.ac.tz/bitstream/handle/11192/2295/MBA-CM-Langa-Neema-2013.pdf?sequence=1>.
- Lihamba, A., Balisidya, N., & Mhando, P. (1982). *Harakati za Ukombozi*. Dar es salaam: Tanzania Publishing House.
- Low, N. R. (2011). Athari ya lugha katika kuibua dhamira: Mifano kutoka nyimbo za kizazi kipya zihusuzo UKIMWI. (Tasnifu ya Shahada ya Uzamili Haijchapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es salaam.
- Lukumbo, L. (2008). Zanzibar revolution saluted, but the poor seek better deal. Katika *Sunday Observer* (January 13, 2008). <http://kurayangu.com/cgi-bin/ipp/print.pl?id=106184>.
- Luoga, E. J., Witkowski, E. T. F., & Balkwill, K. (2000). Economics of charcoal production in miombo woodlands of Eastern Tanzania: Some hidden costs associated with commercialization of the resources. Katika *Ecological*

*Economics*, 35 (2) (243-257).

<https://www.sciencedirect.com/science/article/abs/pii/S0921800900001968>.

Lynch, P. A., & Roberts, J. (2010). *African mythology A to Z*, (second edition). New York: Chelsea House Publishers.

<https://img.fireden.net/tg/image/1454/78/1454787608049.pdf>.

Maake, N. (2006). Between freedom and self – subjection: the dilemma of writing in an African language. *Katika Literator*, 27 (1) (127-140).

[https://www.researchgate.net/publication/266412242\\_Between\\_freedom\\_and\\_self-subjection\\_the\\_dilemma\\_of\\_writing\\_in\\_an\\_African\\_language/link/54aff2b90cf220c63ccdc9da/download](https://www.researchgate.net/publication/266412242_Between_freedom_and_self-subjection_the_dilemma_of_writing_in_an_African_language/link/54aff2b90cf220c63ccdc9da/download).

Madumulla, J. S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili: nadharia, historia na misingi ya uchambuzi*. Dar es salaam: Mture Educational Publishers Ltd; Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Mahenge, E. (2010). *Changamoto*. Dar es salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.

Malima, C. C. (2018). Kuchunguza matumizi ya misimu ya wanavyuo inavyotumika katika mitandao ya kijamii mjini Morogoro. (Tasnifu ya Shahada ya Uzamili Haijchapishwa), Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Masabo, C. J. (2014). Corruption and fraudulent culture: The case of Tanzania. Katika Nduku, E. & Tenamwenye, J. (Wahariri), *Corruption in Africa: A Threat to Justice and Sustainable Peace* (145-165).

[https://www.globethics.net/documents/4289936/13403252/GE\\_Focus\\_14\\_web.pdf](https://www.globethics.net/documents/4289936/13403252/GE_Focus_14_web.pdf)

Masatu, F. J., Hyera, V. F., Ndunguru, O. R., & Ponera, A. K. (2020). Mwingilianomatini katika tamthilia ya *Utangamano Wetu Ushindi Wetu* (2017) ya Anitha E. Mgimba. Katika *East African Journal of Swahili Studies*, 2 (2), (128-143). <https://doi.org/10.37284/eajss.2.2.217>.

Masebo, J. A., & Nyangwine, N. (2008). *Tahakiki: vitabu teule vya fasihi kidato cha 5 na 6*. Dar es salaam: Nyambari Nyamwine Publishers.

- Masebo, J. A., & Nyangwine, N. (2016). *Nadharia ya lugha Kiswahili 1: kidato cha 5 na 6* (toleo jipya). Dar es salaam: Nyambari Nyamwine Publishers.
- Massamba, D. P. (2002). *Historia ya Kiswahili: 50 BK hadi 1500 BK*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.
- Massoud, S. M. A. (2013). Maudhui na fani katika tamthilia za Kiswahili: Utafiti linganishi wa tamthilia za *Mashetani* na *Kivuli Kinaishi*. (Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu Haijachapishwa), Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Massoud, S. S. (2018). Kutathmini matumizi ya mtindo na dhamira katika tamthiliya za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi*: Utafiti linganishi. (Tasnifu ya Shahada ya Uzamili Haijachapishwa), Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Matteru, M. L. (1974). *Hadithi na riwaya*. Dar es salaam: Chama cha Kiswahili cha Chuo Kikuu cha Dar es salaam.
- Matundura, E. & Mugambi, A. (2022). Udhhibiti wa fasihi Afrika Mashariki na athari zake kwa waandishi na utunzi. Katika *Mulika*, 41 (2) (175 – 191). <https://doi.org/10.56279/mulika.na41t2.4>.
- Mazigwa, S. A. (1991). *Fasihi ya Kiswahili*. Peramiho: Benedictine Publication Ndanda.
- Mbise, I. R. (1996). *Creative writing I: literature in English*. Dar es salaam: OUT.
- Mbiti, J. S. (1969). *African religion and philosophy*. London: Morrison and Gbb Ltd.
- Mbogo, E. (2015). *Nyerere na Safari ya Kanaani*. Dar es salaam: Karljamer Print Technology.
- Mbogo, E. (2015). *Sadaka ya John Okello*. Dar es salaam: Karljamer Print Technology.
- Mdee, J. S. (2006). *Nadharia na historia ya leksikografia*. Dar es salaam: TUKI.
- Mhando, P. (1982). *Nguzo Mama*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press
- Mhilu, G., Nyangwine, N., & Kanyuma, Y. (2008). *Tahakiki: vitabu teule vya fasihi kidato cha 3 na 4*. Dar es salaam: Nyambari Nyamwine Publishers.

- Ministry of Finance and Planning. (2021). *National five-year development plan 2021/22-2025/26: Realising competitiveness and industrialisation for human development.*\_
- Mirikau, S. A. (2011). Taswira ya mwanamke katika tamthilia za Wamitila K. W. (Tasnifu ya Shahada ya Uzamili Haijchapishwa), Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Mkapa, B. W. (2019). *My life, my purpose: A Tanzanian president remembers*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.
- Mlama, P. O. (2003). Utunzi wa tamthiliya katika mazingira ya Tanzania. Katika TUKI, *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III: Fasihi* (206-225). DSM: Idara ya Kiswahili.
- Mnenuka, A. (2010). Fomula ya tamthiliya ndani ya tamthiliya katika tamthiliya teule za Kiswahili. Katika *Kioo cha Lugha*, 8 (93-106).
- Mnyampala, M. E. (1990). *Diwani ya Mnyampala*. Dar es Salaam: East African Literature Bureau.
- Mochiwa, Z. (1978). Dhamira za *Kijiji Chetu*. Katika *Mulika*, 13 & 14 (38-44). <https://journals.udsm.ac.tz/index.php/mj/article/view/1615/1510>.
- Mohamed, A. N. (2013). *Matumizi ya lugha tandawazi katika simu za kiganjani*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Mohamed, A. S. (1990). *Mbinu na Mazoezi ya Ushairi*. Nairobi: Evans.
- Mohamed, S. A. (1995). *Kunga za nathari ya Kiswahili: Riwaya, tamthiliya, na hadithi fupi*. Nairobi: East African Educational Publishers.
- Momanyi, C. (2009). The effects of ‘sheng’ in the teaching of Kiswahili in Kenyan schools. Katika *The Pan African Studies*, 2 (8) (127–138). <https://citeseerx.ist.psu.edu/viewdoc/download?doi=10.1.1.569.6993&rep=rep1&type=pdf>.
- Mrikaria, S. E. (2010). Kejeli na fasihi ya Kiswahili – Tanzania. Katika *Swahili Forum* (17). [www.qucosa.de/fileadmin/data/qucosa/documents/9089/17\\_09\\_Mrikaria.pdf](http://www.qucosa.de/fileadmin/data/qucosa/documents/9089/17_09_Mrikaria.pdf).

- Msanjila, Y. P. (2011). *Isimu jamii: Sekondari na vyuo*. Dar es Salaam: TUKI.
- Msekwa, P. (2013). *50 Years of independence: A concise political history of Tanzania*. Dar es salaam: Nyambari Nyangwine Publishers.
- Msokile, M. (1992). *Misingi ya hadithi fupi*. Dar es salaam University Press.
- Mswahili, A. A. M., & Njonjolo, M. S. (2016). *Nje – Ndani*. Dar es salaam: Culture Link Africa Ltd.
- Mtoi, M. (2012). Hotuba ya Mwalimu Nyerere siku ya Mei mosi 1995 Mbeya. <https://tangamano.wordpress.com/2012/10/14/hotuba-ya-mwalimu-nyerere-siku-ya-mei-mosi-1995-mbeya/>.
- Mukandala, R. S., & Gasarasi, C. (Wahariri). (2000). *Governance and development at the grassroots in Tanzania*. Dar es Salaam: University of Dar es Salaam Press.
- Mukobwa, M. J. N. (1985). Maendeleo ya kimaudhui katika tamthiliya tano za Ebrahim N. Hussein. (Tasnifu ya Shahada ya Uzamili Haijachapishwa), Chuo Kikuu Cha Nairobi. <https://ir-library.ku.ac.ke/bitstream/handle/123456789/17576/Maendeleo%20ya%20kimaudhui%20katika%20tamthilia.pdf?sequence=1&isAllowed=y>.
- Mulokozi, M. M. (2017). *Taaluma ya lugha na fasihi - 2: Utangulizi wa fasihi ya Kiswahili kozi za fasihi vyuoni na vyuo vikuu*. Dar es salaam: KAUTTU.
- Murungi, G. K. (2013). Mtindo unavyoendeleza maudhui katika *Natala*. (Tasnifu ya Shahada ya Uzamili Haijachapishwa), Chuo Kikuu Cha Nairobi, Kenya. [erepository.uonbi.ac.ke/8080/handle/11295/8018/discover?field=author&filtertype=author&filter\\_relational\\_operator>equals&filter=Kanyua%2C+Murungi+G](https://erepository.uonbi.ac.ke/8080/handle/11295/8018/discover?field=author&filtertype=author&filter_relational_operator>equals&filter=Kanyua%2C+Murungi+G).
- Mushengyezi, A. (2003). *Twentieth century literary theory*. Makerere University: Department of Distance Education, Institute of Adult and Continuing Education.
- Mutembei, A. K. (2009). *Ukimwi katika fasihi ya Kiswahili, 1982 - 2006*. Dar es salaam: Chuo Kikuu cha Dar es salaam.

- Muysken, P. (2000). *Bilingual speech: A typology of code mixing*. Cambridge University Press.
- Mwananchi. (Jumamosi, 25 Septemba 2021). Machinga waanza kuhamishwa. Dar es salaam: Mwananchi Communications Limited.
- Mwiru, K. N. (17 Aprili 2013). Unafiki umeua Azimio la Arusha. Katika Elias Msuya, *Mwananchi*. <http://www.mwananchi.co.tz/makala/1597592-1750698-1528kmg/index.html>.
- Nauta, D. (1972). *The meaning of information*. The Hague: Mouton & CO., Printers. <https://archive.org/details/TheMeaningOfInformation>.
- Nazareth, P. (1978). *The third world writer: His social responsibility*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Nell, V. (1988). The psychology of reading for pleasure: Needs and gratifications. Katika *Reading Research Quarterly*, 23 (6-50). <https://msu.edu/~dwong/CEP991/CEP991Resources/Nell-RdngPleasure.pdf>.
- Ngahyoma, N. (1975). *Kijiji Chetu*. Dar es salaam: Tanzania Publishing House.
- Ngomoi, J. (1976). *Ndoto ya Ndaria*. Dar es salaam: Tanzania Publishing House.
- Nguti, M. (2013). Ulinganishi wa matumizi ya tafsida za muktadha wa nyumbani katika lugha ya Kikamba na Kiswahili. (Tasnifu ya Shahada ya Uzamili Haijachapishwa), Chuo Kikuu Cha Nairobi, Kenya.
- Ngwale, S., & Kironde, J. M. (2000). *Urbanizing Tanzania: issues, initiatives and priorities*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Nicolini, C. (2016). Uhakiki wa tamthilia za Kiswahili zihusuzo VVU/UKIMWI. Katika *Swahili Forum*, 23 (98-121). <http://ul.qucosa.de/api/qucosa%3A15400/attachment/ATT-0/>.
- Njogu, K., & Chimera, R. (1999). *Ufundishaji wa fasihi: nadharia na mbinu*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.
- Ntarangwi, M. (2004). *Uhakiki wa kazi za fasihi*. Rock Island: Augustina College.
- Nyerere, J. K. (1970). *Ujamaa*. Dar es salaam: DUP.

- Nyerere, J. K. (1973). *Uhuru na maendeleo*. Oxford: Oxford University Press.
- Nyerere, J. K. (1994). *Uongozi wetu na hatima ya Tanzania*. Dar es salaam: Mkuki na Nyota Publishers
- Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. (2018). Ripoti kuu ya mwaka ya mdhibiti na mkaguzi mkuu wa hesabu za serikali: Ukaguzi wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2017. Katika <http://changetanzania.org/wp-content/uploads/2018/04/RIPOTI-KUU-YA-MIRADI-YA-MAENDELEO.pdf>.
- Ofisi ya Waziri Mkuu. (2018). *Mkakati wa nne wa taifa wa kudhibiti ukimwi Tanzania (2018/19-2022/23)*.  
<http://library.tacaids.go.tz/bitstream/handle/123456789/126/Mkakati%20wa%20Onne%20wa%20Kudhibiti%20UKIMWI.SWAHILI.pdf?sequence=1&isAllowed=y>.
- Okello, J. (1967). *Revolution in Zanzibar*. Nairobi: East African Publishing House.
- Olali, T. (2015). Trends and development of the Swahili drama since 1957 to 2014. Katika *International Journal of Humanities Social Sciences and Education*, 2 (10) (1–7). <https://www.arcjournals.org/pdfs/ijhsse/v2-i10/1.pdf>.
- Omari, S. (2009). *Safari ya Chinga*. Dar es salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.
- Oso, W. Y., & Onen, D. (2009). *A general guide to writing research proposal and report: A handbook for beginning researchers* (revised edition). Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.
- OUT. (2022/2023). Appendix X: General Regulation and Guidelines for Theses/Dissertations. <http://www.out.ac.tz>.
- Oxford. (2020). *Oxford advanced learner's dictionary* (12<sup>th</sup> edition). Nairobi: Oxford University Press, East Africa Ltd.
- p'Bitek, O. (1975). *Wimbo wa Lawino: Ombolezo*. Dar es salaam: EAPH
- Pamba, S. E. (2012). An analysis of the impacts of structural adjustment programmes on education in Sub – Sahara Africa: A case study of Kenya (1980 - 2010).



(Tasnifu ya Shahada ya Uzamili Haijchapishwa), Chuo Kikuu cha Nairobi, Kenya.

[http://erepository.uonbi.ac.ke/bitstream/handle/11295/8564/pamba\\_An%20Analysis%20of%20the%20Impact%20of%20Structural%20Adjustment%20Programmes%20on%20Education%2c%20in%20Sub-saharan%20Africa%20a%20Case%20Study%20of.pdf?sequence=1&isAllowed=y](http://erepository.uonbi.ac.ke/bitstream/handle/11295/8564/pamba_An%20Analysis%20of%20the%20Impact%20of%20Structural%20Adjustment%20Programmes%20on%20Education%2c%20in%20Sub-saharan%20Africa%20a%20Case%20Study%20of.pdf?sequence=1&isAllowed=y)

Pearson, R. (2000). Rethinking gender matters in development. Katika Allen, T & Thomas, A. (Wahariri), *Poverty and development into the 21<sup>st</sup> century*. Oxford: Oxford University Press.

Penelope, E. (2000). *Linguistic variation as social practice*. Oxford: Blackwell.

Poncian, J. & George, C. (2015). Mining extraction for socio-economic transformation of Tanzania: The need to move from papers to implementation of mining policy and law. Katika *Journal of Social Science Studies and Macrothink Institute*, 2 (2) (160 – 175). <http://jsss.macrothink.org>.

Provine, R. R. (1996). Laughter: The study of laughter provides a novel approach to the mechanisms and evolution of vocal production, perception and social behavior. Katika *American Scientists*, 84 (38 – 45).

[https://www.researchgate.net/publication/232489851\\_Laughter\\_A\\_Scientific\\_Investigation?enrichId=rgreq-5641a36062d2c24cca7b49ee33a9cde7-XXX&enrichSource=Y292ZXJQYWdlOzIzMjQ0OTg1MTtBUzo2NDA2NTE3MTY2OTQwNjRAMTQ1ODIyOTEwNjk2NQ%3D%3D&el=1\\_x\\_2&\\_esc=publicationCoverPdf](https://www.researchgate.net/publication/232489851_Laughter_A_Scientific_Investigation?enrichId=rgreq-5641a36062d2c24cca7b49ee33a9cde7-XXX&enrichSource=Y292ZXJQYWdlOzIzMjQ0OTg1MTtBUzo2NDA2NTE3MTY2OTQwNjRAMTQ1ODIyOTEwNjk2NQ%3D%3D&el=1_x_2&_esc=publicationCoverPdf).

Raiamwema. (Juni 01, 2012). Ufisadi maliasili. [www.raiamwema.co.tz/ufisadi-maliasili/](http://www.raiamwema.co.tz/ufisadi-maliasili/).

Reuster-Jahn, U., & Kiebling, R. (2006). Luga ya mitaani in Tanzania: The poetics and sociology of a young urban style of speaking with a dictionary comprising 1100 words and phrases. Katika *Swahili forum 13: Special Issue*. [https://www.researchgate.net/publication/315912602\\_Luga\\_ya\\_Mitaani\\_in\\_Tanzania\\_The\\_poetics\\_and\\_sociology\\_of\\_a\\_young\\_urban\\_style\\_of\\_speaking\\_w](https://www.researchgate.net/publication/315912602_Luga_ya_Mitaani_in_Tanzania_The_poetics_and_sociology_of_a_young_urban_style_of_speaking_w)

[ith a dictionary comprising 1100 words and phrases/link/58ece8b1458515316aac16de/download.](#)

Richards, R. J. (1992). *The meaning of evolution: the morphological construction and ideological reconstruction of Darwin's theory*. Chicago: University of Chicago Press.

Riemer, N. (2010). *Introducing semantics*. New York: Cambridge University Press.  
<http://f.javier.io/rep/books/Introducing.Semantics.pdf>.

Rodney, W. (1972). *How Europe underdeveloped Africa*. London: Bogle-L'Ouverture Publications.

Romaine, S. (1995). *Bilingualism*. Oxford: Blackwell.

Roy-Campbell, Z., & Qorro, M. A. S. (1997). *Language crisis in Tanzania: The myth of English versus education*. Dar es salaam: Mkuki na Nyota Publishers.

Ruhumbika, G. (2006). Mwandishi wa Kiswahili na lugha yake katika Tanzania huru. Katika S. S. Sewangi & J. S. Madumulla (wahariri), *Makala ya Kongamano la Kimataifa la Jubilei ya TUKI-2005*. University of Dar es salaam: TUKI.

Saarikallio, S., & Erkkilä, J. (2007). The role of music in adolescents' mood regulation. Katika *Psychology of Music*, 35 (1) (88–109).  
<https://sonictonic.io/wp-content/uploads/2016/10/The-role-of-music-2.pdf>.

Samwel, M. (2013). *Tamthiliya ya Kiswahili: kutoka miviga ya kidini hadi filamu*. Dar es salaam: Meveli Publishers.

Sanchez, V. A. (1973). *Art and society*. London: Monthly Review Press.

Satpayeva, Z. T., Kangalakova, D., Ibraimova, S. & Utemissova, G. (2022). The science impact on country's socio-economic development. Katika *Eurasian Journal of Economic and Business Studies*, 65 (3), (27-46).  
<https://doi.org/10.47703/ejeb.v3i65.142>.

Schlosser, J. A. (2009). Engaging Socrates. (Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Duke.

- Seers, D. (1972/2012). Economic growth: What are we trying to measure? Katika Jolly, R. (Mhariri). (2012), *Milestones and turning points in development thinking*. Hampshire; New York: Palgrave Macmillan.
- Selden, R. (1985). *An introduction to literary criticism*. New York: Harvester Wheatsheaf.
- Senzaba, E. (2003). *Tamthiliya ya Kiswahili*. Dar es salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Sengo, S. D. (1973). *Misemo ya mitaani*. Dar es Salaam: DUP.
- Sengo, S. D. (1975). Ebrahim N. Hussein, mwandishi wa michezo ya kuigiza. Katika Sengo, S. D., & Kiango, T. S. Y., *Hisi zetu 2*. Dar es salaam: TUKI.
- Sengo, S. D., & Kiango, T. S. Y. (1973). *Hisi zetu*. Dar es salaam: TUKI.
- Senkoro, F. E. M. K. (1982). *Fasihi*. Dar es Salaam: DUP.
- Senkoro, F. E. M. K. (1987). *Fasihi na jamii*. Dar es salaam: Kauttu Ltd.
- Senkoro, F. E. M. K. (1995). Sanaa, ubunifu na jamii katika nadharia za fasihi. Katika *Kioo cha Lugha*, 1 (2) (81-92).
- Senkoro, F. E. M. K. (2007). Uhalisiamazingaombwe katika fasihi ya Kiswahili: istilahi mpya, mtindo mkongwe. Katika F. E. M. K. Senkoro & K. K. Kahigi (Wahariri), *Kioo cha Lugha*, 5 (1-12). Dar es Salaam: TUKI. <https://journals.udsm.ac.tz/index.php/kcl/article/view/1504/1402>.
- Senkoro, F. E. M. K. (2011). *Fasihi: Mfululizo wa lugha na fasihi*. (kitabu cha kwanza). Dar es Salaam: Press and Publicity Center.
- Senyamanza, C. A. (2015). Tathmini ya mabadiliko ya rara mintarafu maendeleo ya kijamii: Uchunguzi katika mikoa ya Mbeya na Dar es salaam. (Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu Haijachapishwa), Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Senyamanza, C. A. (h. m). *Misingi ya kazi za kubuni: nadharia, mbinu na mifano ya kazi bunilizi*. Dar es salaam: Karljamer Print Technology.
- Settles, J. D. (1996). The impact of colonialism on African economic development. Katika *University of Tennessee honors thesis projects*.

[https://trace.tennessee.edu/cgi/viewcontent.cgi?article=1182&context=utk\\_cha\\_nhonoproj](https://trace.tennessee.edu/cgi/viewcontent.cgi?article=1182&context=utk_cha_nhonoproj).

Sharma, A. (2015). The making of the third world: The impact of colonialism. *Katika Research Journal of English Language and Literature*, 3 (2) (141–144).  
<https://www.researchgate.net/publication/281497487> THE MAKING OF THE THIRD WORLD THE IMPACT OF COLONIZATION.

Shivji, I. (2013). Dibaji. Katika Ally, B., Yahya-Othman, S., & Shivji, I. (Wahariri). *Miongozo miwili kupaa na kutunguliwa kwa Azimio la Arusha*. Chuo Kikuu cha Dar salaam: Kigoda cha Taaluma cha Mwalimu Nyerere.

Shivji, I. G. (1976). *Class struggles in Tanzania*. Heinemann and Tanzania Publishing House.

Shivji, I. G. (1985). *The state and the working people in Tanzania*. Dakar: CODESRIA.

SHIVYAWATA. (h.m.). Taarifa: Hali ya haki za watu wenye ulemavu Tanzania.  
<http://shivyawata.ort.tz/survey/download>.

Shklovsky, V. (1966). *Theory of prose*. Champaign & London: Dalkey Archive Press.

Short, T. L. (2007). *Peirce's theory of signs*. Cambridge: Cambridge University Press

SID. (2009). *The extractive resource industry in Tanzania: status and challenges of the mining sector*. Nairobi: Society for International Development.

Siegler, R. & Schlosser, D. B. (1990). *Political stability and development*. London: Lynne Rienner.

SIKIKA. (2013a). *Kamati za kudhibiti UKIMWI nchini Tanzania*.  
<http://www.sikika.or.tz/sw/wp-content/uploads/2013/12/MACs-SWAHILI-REPORT-2013.pdf>.

SIKIKA. (2013b). *Maoni ya wananchi juu ya huduma za VVU na UKIMWI nchini Tanzania*. [www.sikika.or.tz/sw/wp-content/uploads/2014/03/Ripoti-ya-Maoni-ya-Wananchi-B5-mail.pdf](http://www.sikika.or.tz/sw/wp-content/uploads/2014/03/Ripoti-ya-Maoni-ya-Wananchi-B5-mail.pdf).

- Silverman, D. (2005). *Interpreting qualitative data: methods for analysing talk, text and interaction* (2<sup>nd</sup> Edition). London: SAGE publishers.
- Simala, K. I. (mwandishi wa makala, na Mhariri wa chapisho). (2002). Miradi ya utafiti katika vyuo vikuu mnamo karne ya ishirini na moja. Katika *Utafiti wa Kiswahili*. Moi University: Moi University Press.
- Simon, K. B. (2014). Ishara katika *Kaptula la Marx na Kijiba cha Moyo*: mtazamo wa kisemiotiki. (Tasnifu ya Shahada ya Uzamili Haijchapishwa), Chuo Kikuu cha Nairobi, Kenya. [www.researchkenya.or.ke/thesis/.../ishara-katika-Kaptula-la-Marx-na-Kijiba-cha-Moyo-mtazamo-wa-kisemiotiki](http://www.researchkenya.or.ke/thesis/.../ishara-katika-Kaptula-la-Marx-na-Kijiba-cha-Moyo-mtazamo-wa-kisemiotiki).
- Sitta, S. (Machi 18, 2013). Mwanasiasa mwadilifu hawezi kuwa tajiri. [www.ibn-tv.com/sw/2013/03/arusha-textile-mill-pledges-to-employ-10000-youth-by-2015/](http://www.ibn-tv.com/sw/2013/03/arusha-textile-mill-pledges-to-employ-10000-youth-by-2015/).
- Skinner, B. (1957). *Verbal behavior*. New York: Appleton Century Crofts, Inc.
- Soyinka, W. (1979). The influence of colonialism on the artist, his milieu and his public in developing countries. Speech addressing UNESCO conference at Dar es salaam. <https://books.google.com.tr/books?id=The%20Influence%20of%20Colonialism%20on%20the%20Artist%20His%20Milieu%20and%20his%20Public%20in%20Developing%20Countries%20by%20Soyinka&f=false>.
- Stephano, R. (2015). Uzingatizi wa viakifishi katika uandishi wa kitaaluma: Mifano kutoka shule za msingi Tanzania. (Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu Haijchapishwa), Chuo Kikuu Cha Dodoma. <http://hdl.handle.net/20.500.12661/1543>.
- Stewart, N. (1951). *Divide and rule: British policy in Indian history*. London: Guilford Press.
- Taasisi ya Elimu Tanzania. (2005 / 2013). *Mtaala wa elimu ya msingi Tanzania*.  
 \_\_\_\_\_
- TANU. (1967). *Chama cha Mapinduzi: Azimio la Arusha na siasa ya TANU ya ujamaa na kujitegemea*. Dar es salaam: Idara ya Habari, TANU.

- Tanzania Commission for AIDS. (2018). *Tanzania HIV impact survey (THIS) 2016-2017*. [https://www.tacaids.go.tz/phocadownload/THIS\\_2016\\_17.pdf](https://www.tacaids.go.tz/phocadownload/THIS_2016_17.pdf).
- Tanzania HIV Impact Survey. (Disemba, 2017). Matokeo ya awali: Utafiti wa viashiria na matokeo ya UKIMWI Tanzania (THIS) wa mwaka 2016 – 17. [www.nbs.go.tz/nbs/takwimu/this2016-17/Tanzania\\_SummarySheet\\_Swahili.pdf](http://www.nbs.go.tz/nbs/takwimu/this2016-17/Tanzania_SummarySheet_Swahili.pdf).
- Thiong'o, N. (1986). *Decolonizing the mind: The politics of language in African literature*. London: Heinemann Educational Books Ltd.
- Thuranira, I. S. (2017). Maudhui ya ukoloni mamboleo katika tamthilia teule za Kiswahili. (Tasnifu ya Shahada ya Uzamili Haijchapishwa), Chuo Kikuu Cha Nairobi, Kenya. <http://erepository.uonbi.ac.ke/bitstream/handle/11295/101772/IKUATHU%20SILAS%20THURANIRA.pdf?sequence=1&isAllowed=y>.
- Timothy, K. (2016). Maana ya usemi na mazungumzo katika mitandao ya kijamii hususani facebook na twitter. Chuo Kikuu cha Nairobi. [http://erepository.uonbi.ac.ke/bitstream/handle/11295/98232/kiunga\\_Maana%20Ya%20Usemi%20Na%20Mazungumzo%20Katika%20Mitandao%20Ya%20Kijamii%20Hususani%20Facebook%20Na%20Twitter.pdf?sequence=1&isAllowed=y](http://erepository.uonbi.ac.ke/bitstream/handle/11295/98232/kiunga_Maana%20Ya%20Usemi%20Na%20Mazungumzo%20Katika%20Mitandao%20Ya%20Kijamii%20Hususani%20Facebook%20Na%20Twitter.pdf?sequence=1&isAllowed=y).
- TUKI. (1981). *Kamusi ya Kiswahili sanifu*. Nairobi: Oxford University Press East Africa Limited.
- TUKI. (2000). *English-Swahili dictionary* (2<sup>nd</sup> Edition). Dar es Salaam: TUKI.
- TUKI. (2014). *Kamusi ya Kiswahili sanifu* (toleo la tatu). Nairobi: Oxford University Press East Africa Limited.
- United Nations Economic Commission for Africa. (2016). *Measuring corruption in Africa: The international dimension matters*. [https://www.uneca.org/sites/default/files/PublicationFiles/agr4\\_eng\\_fin\\_web\\_1\\_1april.pdf](https://www.uneca.org/sites/default/files/PublicationFiles/agr4_eng_fin_web_1_1april.pdf).

- United Nations. (2014). Economic development in Africa report 2014. [https://unctad.org/en/PublicationsLibrary/aldcafrica2014\\_en.pdf](https://unctad.org/en/PublicationsLibrary/aldcafrica2014_en.pdf).
- Unterhalter, E. (2019). *Measuring the unmeasurable*. London: Routledge.
- Villanueva, D. (2011). Possibilities and limits of comparative literature today. Katika CLCWeb: *Comparative Literature and Culture*, 13 (5) (1-10). <https://doi.org/10.7771/1481-4374.1915>.
- Wafula, R. M. (1999). *Uhakiki wa tamthiliya: historia na maendeleo yake*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Wakota, J. (2018). Ujamaa's villagization and gender dynamics in selected Tanzanian fiction. Katika *Journal of African Cultural Studies*, 30 (1) (49-64). [10.1080/13696815.2016.1207158](https://doi.org/10.1080/13696815.2016.1207158).
- Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa fasihi: Misingi na vipengele vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- Wamitila, K. W. (2003). *Kichocheo cha fasihi: Simulizi na andishi*. Nairobi: Focus Publications Ltd.
- Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya fasihi 1: Misingi ya uchanganuzi wa fasihi*. Nairobi: Vide~Muwa Publishers Ltd.
- Warnes, C. (2006). Magical realism and german idealism. Katika *Modern Language Review* 101/2. [https://www.jstor.org/stable/20466796?seq=1#page\\_scan\\_tab\\_contents](https://www.jstor.org/stable/20466796?seq=1#page_scan_tab_contents).
- Wazambi, F., & Mikongoti, P. (2018). Muhtasari wa ripoti ya haki za binadamu Tanzania 2017: Tanzania bara. Dares salaam: Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu. [https://humanrights.or.tz/assets/images/upload/files/THRR%202017%20Swahili%20Booklet%20\(1\).pdf](https://humanrights.or.tz/assets/images/upload/files/THRR%202017%20Swahili%20Booklet%20(1).pdf).
- Wibowo, A. I., Yuniasih, I., & Nelfianti, F. (2017). Analysis of types code switching and code mixing by the sixth president of Republic Indonesia's speech at the national of independence day. Katika *Progressive*, XII (2) (13-22).

<https://media.neliti.com/media/publications/227310-analysis-of-types-code-switching-and-cod-1287515d.pdf>.

Wizara ya Elimu na Utamaduni. (h. m). *Sera ya utamaduni*. \_\_\_\_\_

Wollaeger, M. (2006). *Modernism, media, and propaganda: British narrative from 1900 – 1945*. Princeton na Oxford: Princeton University Press.

Yussuf, M. A. (2017). Kuchunguza matumizi ya tafsida katika lahaja ya Kipemba: Uchunguzi wa mazungumzo. (Tasnifu ya Shahada ya Uzamili Haijachapishwa), Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Zepetnek, S. T. (1998). *Comparative literature: Theory, method, application*. Amsterdam – Atlanta, GA: Rodopi B. V.

Zúbková, E. B., Gromov, M. D., Khamis, S. A. M., & Wamitila, K. W. (2009). *Outline of Swahili literature: Prose, fiction and drama* (Second Edition, Extensively Revised and Enlarged). Leiden and Boston: Brill.  
[http://eprints.soas.ac.uk/14038/1/outline\\_of\\_swahili\\_literature.pdf](http://eprints.soas.ac.uk/14038/1/outline_of_swahili_literature.pdf).



## VIAMBATISHO

**Kiambatisho A: Jedwali 5.16 Uchanganyaji Ndimi katika Tamthilia ya  
Mashetani**

<b>Kauli</b>	<b>Kurasa</b>	<b>Kiwango cha Kujitokeza</b>	<b>Maana ya Neno kama Lilivyotumika Kitabuni</b>	<b>Lugha Chanzi</b>
Waltz	8	1	Aina ya uchezaji muziki ambapo wachezaji (aghalabu huwa ni mwanaume na mwanamke) hushikana mikono ama kiunoni au mgongoni kwa kutumia mkono mmoja huku mkono wa pili ukinyooshwa kwa nyuma. Mchezaji hukaza miguu na kusimamia kidole / vidole vya miguu. Hucheza kwa kuruka hapa na pale huku wakijizungusha na kuachana kisha kushikana tena	Kiingereza asili ni Kijerumani (walzen yaani kujizungusha kwenye mhimili. Kiingereza inaitwa <i>to revolve</i> )
Setting	13	1	Mandhari	Kiingereza
Slides	13	1	Vioo, Matini zinazonyiririka	Kiingereza
Projector	13	1	Chombo kitupacho picha mbele	Kiingereza
Chief	15	1	Mkuu / Kiongozi	Kiingereza
Holiday	15	1	Likizo, mapumziko, sikukuu	Kiingereza
Time	15	1	Muda / wasaa	Kiingereza
I say	15, 17	17	Nasema / husema	Kiingereza
Party	15	1	Karamu/ sherehe	Kiingereza
Outline of African History	15	1	Muhtasari wa Historia ya Afrika	Kiingereza
University	15, 16, 17	7	Chuo Kikuu	Kiingereza
You must read it	15	1	Lazima ukisome (kitabu)	Kiingereza
The Essence of Colonial Heritage	16	1	Msingi / Kitovu cha Urithi wa Ukoloni	Kiingereza
Of course, anytime	16	1	Sawa / Ndivyo / Naam, wasaa / muda wowote	Kiingereza
Law	16	1	Sheria	Kiingereza
Faculty	16	1	Kitivo	Kiingereza
Grandmother	16	1	Bibi	Kiingereza

Shell	16	1	Kampuni inayojishughulisha na mambo ya mafuta	Kiingereza
Factory	17	1	Kiwanda	Kiingereza
Degree	17	1	Shahada ya kwanza, digrii	Kiingereza
No	17, 20	1	Hapana, sivyo	Kiingereza
Serious, seriously	18, 20	3	Siyo utani, maanisha, kwa dhati; maanisha kabisa, kwa dhati kabisa, kwa uzito kabisa	Kiingereza
Cowboy	18	2	Mchungu ng'ombe (katika tambarare za Amerika), mfanyabiashara asiye mwaminifu; mhuni, mdanganyifu (TUKI, 2014)	Kiingereza
I see	18	2	Naona, naelewa	Kiingereza
Cowboy films	18	1	Filamu za mchungu ng'ombe (katika tambarare za Amerika)	Kiingereza
Red Indians	18	1	Wahindi Wekendu (huko Amerika)	Kiingereza
Okey	20	1	Sawa	Kiingereza
Feelings	21	1	Hisia	Kiingereza
I like some money	21	1	Napenda fedha / napenda vizuri	Kiingereza
I like some honey	22	1	Napenda asali / napenda vizuri / navutiwa na warembo	Kiingereza
A very good life	22	2	Maisha mazuri sana	Kiingereza
A very beautiful wife	22	1	Mke mrembo / mzuri sana	Kiingereza
A very good wife	22	1	Mke mzuri / mwema sana	Kiingereza
Yes memsahp	27, 29, 32	3	Ndiyo / naam mpenzi	Kiingereza, Kiarabu
What nonsense	27	1	Upuuzi gani / Upuuzi!	Kiingereza
That's very normal	27	1	Hiyo ni kawaida kabisa	Kiingereza
God	30	1	Mungu	Kiingereza
Sitting room	33	1	Sebule (ni)	Kiingereza
Neurosis	33, 34	4	fadhaa, kuchanganyikiwa, jakamoyo	Kiingereza
Tip	40	2	Kidokezi, bahshishi	Kiingereza

Yes Sir	40, 43	2	Naam / ndiyo bwana	Kiingereza
Aam (I'm).. yes. Can you fetch one beer and one whisky?	40	1	Aah.. Ndiyo. Unaweza kuniletea bia moja na wiski (aina ya pombe kali) moja?	Kiingereza
Whisky, double or single?	40	1	Wiski, mbili (jozi / maradufu) au moja?	Kiingereza
No. One beer for him, and one whisky for me	40	1	Hapana. Bia moja kwake, na wiski moja kwangu.	Kiingereza
Whisky, double au single?	40	1	Wiski, mbili au moja?	Kiingereza
Double na single...? Whisky...	41	2	Mbili na moja...? Wiski...	Kiingereza
Double?	41	2	Mbili?	Kiingereza
Two beers and double whiskies	43	1	Bia mbili na wiski mbili (maradufu / jozi)	Kiingereza
Fetch here two beers quick	43	2	Lete bia mbili haraka	Kiingereza
Of course,	50	1	Ndivyo, naam	Kiingereza
Yah!	52	1	Ndiyo	Kiingereza

**Chanzo:** Data za Utafiti Kutoka Tamthilia ya *Mashetani*, 2018

**Kiambatisho B: Jedwali 6.1 Mdafao wa Dhamira Zilizotawala Tamthilia Teule**

N/M	Tamthilia	Dhamira Tawala	Mdafao wa Dhamira
1.	<i>Mashetani</i>	i. Ukombozi wa kifikra ii. Mithiolojia za kijadi iii. Nafasi ya mapinduzi kwa jamii iv. Ukoloni mamboleo v. Umuhimu wa elimu rasmi na isiyorasmi vi. Changamoto ya madaraka na mamlaka vii. Matabaka na ubaguzi viii. Ujinsia katika Sanaa ix. Dhuluma, usaliti na uonevu	9
2.	<i>Kijiji Chetu</i>	i. Ukombozi wa kifikra ii. Mithiolojia za kijadi iii. Ujinsia katika Sanaa iv. Azimio la Arusha v. Nafasi ya vijana, wanawake na wazee vi. Ndoa na mapenzi vii. Umuhimu wa elimu na utamaduni wa kujisomea viii. Unyonyaji, dhuluma na fitina,	13

---

	ix. Usaliti na uzalendo	
	x. Wizi na rushwa	
	xi. Changamoto ya madaraka na mamlaka	
	xii. Matabaka na ubaguzi	
	xiii. Nafasi ya demokrasia kwa jamii	
3. <i>Harakati za Ukombozi</i>	i. Ukombozi wa kifikra	13
	ii. Falsafa na itikadi	
	iii. Nafasi ya vijana na wazee	
	iv. Mikataba ya kazi na umuhimu wa bima	
	v. Utumwa, ukoloni na ukoloni mamboleo	
	vi. Umuhimu wa elimu na utamaduni wa kujisomea	
	vii. Unafiki, dhuluma, unyonyaji,	
	viii. Usaliti, fitina na undumilakuwili	
	ix. Wizi, ufidadi na rushwa	
	x. Changamoto ya madaraka na mamlaka	
	xi. Matabaka na ubaguzi	
	xii. Athari ya kukata tamaa	
	xiii. Hali ngumu ya maisha	
	xiv. Mapinduzi na uzalendo	
4. <i>Safari ya Chinga</i>	i. Ukombozi wa kifikra	19
	ii. Ujasiramali na changamoto zake	
	iii. Mikumbo na upotofu wa taarifa	
	iv. Nafasi ya elimu rasmi na isiyorasmi	
	v. Hali ngumu ya maisha	
	vi. Ukoloni mamboleo	
	vii. Sheria na utekelezwaji wake	

---

	viii. Matabaka na ubaguzi	
	ix. Uzalendo na utu	
	x. Mithiolojia za kijadi	
	xi. Athari ya mfumodume, ndoa na mimba za utotoni	
	xii. Unyonyaji na dhuluma	
	xiii. Usaliti, wizi na rushwa	
	xiv. Vijana na ajira	
	xv. Mila na desturi potofu	
	xvi. Nidhamu ya fedha na matumizi	
	xvii. Utapeli na wizi	
	xviii. Kukata tamaa na Ujuaji	
	xix. UKIMWI / VVU na jamii	
5. <i>Changamoto</i>	i. Ukombozi wa kifikra	13
	ii. Mithiolojia za kijadi	
	iii. Changamoto za Ulemavu katika jamii	
	iv. Dhuluma, chuki na usaliti	
	v. Wizi, rushwa na unyonyaji	
	vi. Unyanyapaa, matabaka na ubaguzi	
	vii. Nafasi ya elimu rasmi na isiyorasmi	
	viii. Hali ngumu ya maisha	
	ix. Siasa, ulinzi, usalama na sheria	
	x. Changamoto ya madaraka na mamlaka	
	xi. Umuhimu wa umoja na mshikamano	
	xii. UKIMWI / VVU na jamii	
	xiii. Ubakaji	
6. <i>Nje – Ndani</i>	i. Ukombozi wa kifikra	16
	ii. Nafasi ya busara, hekima, subira na maarifa	

		iii. Ukoloni na ukoloni mamboleo iv. Unafiki na usaliti wa viongozi v. Hali ngumu ya maisha vi. Tamaa na usaliti katika ndoa na mapenzi vii. Ulinzi na usalama kwa watu wa makundi maalumu viii. Nafasi ya elimu na wasomi katika ukombozi ix. Uhujumu uchumi, unyonyaji x. Ufisadi na rushwa xi. Athari ya umoja na ushirikiano katika jamii xii. Umuhimu wa elimu na utamaduni wa kujisomea xiii. Matabaka na ubaguzi xiv. Ujasiriamali na changamoto zake xv. Ujinsia na jamii xvi. Changamoto ya mikopo kwa wananchi na taifa	
--	--	--	--

*Chanzo:* Data za Utafiti Kutoka Tamthilia za *Mashetani, Kijiji Chetu, Harakati za Ukombozi, Safari ya Chinga, Changamoto, Nje – Ndani, 2018*

**Kiambatisho C: Maswali ya Kuongoza Uchunguzi wa Matini Teule kwa Ajili ya Data za Msingi**

**1. Kubainisha Dhamira zinazojitokeza katika Tamthilia Teule**

- i. Dhamira zipi zinajitokeza katika tamthilia ya *Mashetani*?
- ii. Dhamira zipi zinajitokeza katika tamthilia ya *Kijiji Chetu*?
- iii. Dhamira zipi zinajitokeza katika tamthilia ya *Harakati za Ukombozi*?
- iv. Dhamira zipi zinajitokeza katika tamthilia ya *Safari ya Chinga*?
- v. Dhamira zipi zinajitokeza katika tamthilia ya *Changamoto*?

vi. Dhamira zipi zinajitokeza katika tamthilia ya *Nje – Ndani*?

## **2. Kuchambua Matumizi ya Lugha Yanayojitokeza katika Tamthilia Teule**

### **(a) Ucheshi**

- i. Ucheshi upi unajitokeza katika tamthilia ya *Mashetani*?
- ii. Ucheshi upi unajitokeza katika tamthilia ya *Kijiji Chetu*?
- iii. Ucheshi upi unajitokeza katika tamthilia ya *Harakati za Ukombozi*?
- iv. Ucheshi upi unajitokeza katika tamthilia ya *Safari ya Chinga*?
- v. Ucheshi upi unajitokeza katika tamthilia ya *Changamoto*?
- vi. Ucheshi upi unajitokeza katika tamthilia ya *Nje – Ndani*?

### **(b) Misimu**

- i. Misimu ipi inajitokeza katika tamthilia ya *Mashetani*?
- ii. Misimu ipi inajitokeza katika tamthilia ya *Kijiji Chetu*?
- iii. Misimu ipi inajitokeza katika tamthilia ya *Harakati za Ukombozi*?
- iv. Misimu ipi inajitokeza katika tamthilia ya *Safari ya Chinga*?
- v. Misimu ipi inajitokeza katika tamthilia ya *Changamoto*?
- vi. Misimu ipi inajitokeza katika tamthilia ya *Nje – Ndani*?



**(c) Matumizi ya Uchanganyaji Ndimi**

- i. Ndimi zipi zinajitokeza katika tamthilia ya *Mashetani*?
- ii. Ndimi zipi zinajitokeza katika tamthilia ya *Kijiji Chetu*?
- iii. Ndimi zipi zinajitokeza katika tamthilia ya *Harakati za Ukombozi*?
- iv. Ndimi zipi zinajitokeza katika tamthilia ya *Safari ya Chinga*?
- v. Ndimi zipi zinajitokeza katika tamthilia ya *Changamoto*?
- vi. Ndimi zipi zinajitokeza katika tamthilia ya *Nje – Ndani*?

**(d) Uwepesi au Ugumu wa Lugha Iliyotumika katika Kuwasilisha Dhamira za Tamthilia Teule**

- i. Uwepesi au ugumu upi wa lugha unajitokeza katika tamthilia ya *Mashetani*?
- ii. Uwepesi au ugumu upi wa lugha unajitokeza katika tamthilia ya *Kijiji Chetu*?
- iii. Uwepesi au ugumu upi wa lugha unajitokeza katika tamthilia ya *Harakati za Ukombozi*?
- iv. Uwepesi au ugumu upi wa lugha unajitokeza katika tamthilia ya *Safari ya Chinga*?
- v. Uwepesi au ugumu upi wa lugha unajitokeza katika tamthilia ya *Changamoto*?
- vi. Uwepesi au ugumu upi wa lugha unajitokeza katika tamthilia ya *Nje – Ndani*?

**3. Kulinganisha na Kulinganua Dhamira Zinazojitokeza katika Tamthilia Teule za Awamu ya Azimio la Arusha na Zile za Awamu ya Soko Huria**

- i. Kwa vipi dhamira zinazojitokeza katika *Mashetani*, *Kijiji Chetu* na *Harakati za Ukombozi* zinafanana na zile zinazojitokeza katika *Safari ya Chinga*, *Changamoto* na *Nje – Ndani*, kiubunifu?
- ii. Kwa vipi dhamira zinazojitokeza katika *Mashetani*, *Kijiji Chetu* na *Harakati za Ukombozi* zinatofautiana na zile zinazojitokeza katika *Safari ya Chinga*, *Changamoto* na *Nje – Ndani*, kiubunifu?

**4. Kulinganisha na Kulinganua Matumizi ya Lugha Yanayojitokeza katika Tamthilia Teule za Awamu ya Azimio la Arusha na Zile za Awamu ya Soko Huria**

- i. Kwa vipi matumizi ya lugha yanayojitokeza katika *Mashetani, Kijiji Chetu* na *Harakati za Ukombozi* yanafanana na yale yanayojitokeza katika *Safari ya Chinga, Changamoto na Nje – Ndani*, kiubunifu?
- ii. Kwa vipi matumizi ya lugha yanayojitokeza katika *Mashetani, Kijiji Chetu* na *Harakati za Ukombozi* yanatofautiana na yale yanayojitokeza katika *Safari ya Chinga, Changamoto na Nje – Ndani*, kiubunifu?

**5. Kutathmini Athari ya Ubunifu katika Dhamira na Matumizi ya Lugha Yanayojitokeza katika Tamthilia Teule za Kiswahili za Awamu ya Azimio la Arusha na Zile za Soko Huria ili Kubaini Namna Zinavyochochea Maendeleo Endelevu ya Tamthilia ya Kiswahili Kisanaa.**

- i. Kwa vipi ubunifu wa dhamira na matumizi ya lugha yanayojitokeza katika *Mashetani, Kijiji Chetu, Harakati za Ukombozi, Safari ya Chinga, Changamoto na Nje – Ndani*, yanachochea maendeleo endelevu ya Tamthilia ya Kiswahili nchini Tanzania?
- ii. Je, kuna ongezeko la dhamira? Kama ni ndiyo, kwa kiwango gani, zipi, kiviipi?
- iii. Je, kuna ongezeko la matumizi ya lugha? Kama ni ndiyo, kwa kiwango gani, zipi na kiviipi?
- iv. Je, nini kifanyike ili kuboresha utunzi bunilizi na endelevu kwa ustawi wa Tamthilia ya Kiswahili na wasomaji wake hasa wa Tanzania?

**Kiambatisho D: Orodha ya Tamthilia ya Kiswahili Zilizotumika katika Hatua  
za Usampulishaji**

**I. Tamthilia za Kiswahili katika Awamu ya Azimio la Arusha**

1. *Wakati Ukuta na Alikiona* (1967) za Ebrahim N. Hussein
2. *Dunia Iliyofarakana* (1967) ya Crispin Hauli
3. *Johari Ndogo* (1968) ya Felician Nkwera
4. *Kinjekitile* (1969) ya Ebrahim N. Hussein
5. *Makbethi* (1968) ya S. S. Mushi
6. *Tufani* (1969) ya S. S. Mushi
7. *Juliasi Kaizari* (1969) ya Julius K. Nyerere
8. *Mabepari wa Venisi* (1969) ya Julius K. Nyerere.
9. *Mashetani* (1971) ya Ebrahim N. Hussein
10. *Mfalme Juha* (1971) ya Farouk Topan
11. *Hatia* (1972) ya Penina Mhando
12. *Ndoto ya Mwendawazimu* (1972) ya E. Ganzel
13. *Tambueni Haki Zetu* (1973) ya Penina Mhando
14. *Heshima Yangu* (1974) ya Penina Mhando
15. *Wala Mbivu* (1974) ya Angelina Chogo
16. *Pambo* (1975) ya Penina Mhando
17. *Kijiji Chetu* (1975) ya Ngalimecha Ngahyoma
18. *Huka* (1976) ya Ngalimecha Ngahyoma
19. *Jogoo Kijijini na Ngao ya Jadi* (1976) za Ebrahim N. Hussein
20. *Thamani Yangu* (1976) ya Johnson Mwangudza
21. *Mbio za Sakafuni* (1976) ya Abel Ndumbu
22. *Machози ya Mwanamke* (1977) ya Ibrahim Ngozi
23. *Taraka Si Mke Wangu* (1977) ya Penina Mhando
24. *Mtumwa* (1978) ya Tigiti S. Y. Sengo
25. *Mukwava wa Uhehe* (1979) ya Mugyabuso M. Mulokozi

26. *Hatari kwa Usalama* (1979) ya Felix Osodo
27. *Hukoo Darisalama* (1980) ya M. L. Muba
28. *Arusi* (1980) ya Ebrahim N. Hussein
29. *Tendehogo* (1980) ya Edwin Semzaba
30. *Hawala ya Fedha* (1980) ya Amandina Lihamba
31. *Dhamana na Mabatini* (1980) ya G. Z. Kaduma
32. *Giza Limeingia* (1980) ya Emmanuel Mbogo
33. *Uasi na Tazama Mbele* (1980) za Jay Kitsao
34. *Tone la Mwisho na Watoto Wetu* (1981) za Emmanuel Mbogo
35. *Njia Panda* (1981) ya Henry Muhanika
36. *Nguzo Mama* (1982) ya Penina Mhando
37. *Buriani* (1983) ya David Mulwa na A. S. Yahya
38. *Uchafu* (1983) ya V. A. Malima
39. *Lina Ubani* (1984) ya Penina Mhando
40. *Ukame* (1984) ya David Mulwa na A. S. Yahya
41. *Sofia wa Gongolamboto* (1984) ya Edwin Semzaba
42. *Ayubu* (1984) ya Paukwa Theater Group
43. *Maisha Subira* (1985) ya Said A. Omar
44. *Zabibu Chungu* (1985) ya Amana Boukheit
45. *Duka la Kaya* (1985) ya Tegamwage Ndimara
46. *Kwenye Ukingo wa Thim* (1988) ya Ebrahim N. Hussein
47. *Pungwa* (1988) ya Said A. Mohamed
48. *Ngoswe Penzi Kitovu Cha Uzembe* (1988) ya Edwin Semzaba
49. *Kivuli Kinaishi* (1990) ya Said A. Mohamed
50. *Ushuhuda wa Mifupa* (1990) ya Ibrahim Ngozi
51. *Msomi* (1990) ya V. Rukambelya
52. *Zimwi la Mrima* (1991) ya F. Fawah

## II. Tamthilia za Kiswahili katika Awamu ya Soko Huria nchini Tamthilia

1. *Mkutano wa Pili wa Ndege* (1992) ya Amandina Lihamba
2. *Kinyamkera* (1992) ya Edwin Semzaba
3. *Morani* (1993) ya Emmanuel Mbogo
4. *Jinyama Madevu* (1993) ya Edwin Semzaba
5. *Amezidi* (1995) ya Said A. Mohamed
6. *Kilio Chetu* (1995) ya Medical Aid Foundation
7. *Chuano* (1995) ya Paukwa Theater Group
8. *Sundiata* (1995) ya Emmanuel Mbogo
9. *Kila Siyesikia* (1997) ya Mathias E. Mnyampala
10. *Kaptula la Marx* (1998) ya Euphrase Kezilahabi
11. *Kitumbua Kimeingia Mchanga* (2000) ya Said A. Mohamed
12. *Adila* (2002) ya Fikirini E. M. K. Senkoro
13. *Giza* (2004) ya Hadija Jilala
14. *Mpaka lini?* (2004) ya Mariam S. Mwiru
15. *Mazonge* (2004) ya Ali M. Rashid
16. *Kilio cha Jesca* (2004) ya Ambrose F. Mghanga
17. *Orodha* (2004) ya Steve Reynolds (Mfasiri: Saif D. Kiango)
18. *Kija: Chungu cha Mwana Mwari wa Giningi* (2005) ya Shani Kitogo.
19. *Mabepari wa Bongo: kumbukizi* (2007) ya Frowin P. Nyoni
20. *Utando* (2007) ya Tatu M. Ngelangelala
21. *Mwalimu Rose* (2007) ya Ambrose F. Mghanga
22. *Ngoma ya Ng'wanamalundi* (2008) ya Emmanuel Mbogo
23. *Posa ya Bikisiwa* (2008) ya Said A. Mohamed na Kitula King'ei
24. *Safari ya Chinga* (2009) ya Shani Omari
25. *Amri ya Wakati* (2009) ya Said A. Mohamed
26. *Fumo Liongo* (2009) ya Emmanuel Mbogo
27. *Ningekuwa na Uwezo* (2009) ya Katama Mkangi

28. *Changamoto* (2010) ya Elizabeth Mahenge
29. *Janga la Werevu* (2011) ya Said A. Mohamed
30. *Damu ya Kibena Mzimuni* (2015) ya Subira S. Kabelwa
31. *Nyerere na Safari ya Kanaani* (2015) ya Emmanuel Mbogo
32. *Wangari Maathai* (2015) ya Emmanuel Mbogo
33. *Sadaka ya John Okello* (2015) ya Emmanuel Mbogo
34. *Nje – Ndani* (2016) ya A. A. Majid Mswahili na M. S. Njonjolo